BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

FEBRUARI, 2023

## YALIYOMO


SEHEMU YA KWANZA 6

**1.0 UTANGULIZI** 6

1.1 WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI YA PAC 6

1.1.1 Waheshimiwa Wajumbe: 7

1.1.2 Sekretarieti: 7

SEHEMU YA PILI 9

2.0 MAUDHUI: 9

2.1 OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI 9

6.2.1: FUNGU C 01 - OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS, SERA URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI 9

6.2.2 MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (ZEMA) 12

6.2.3: FUNGU C 03 - TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR 21

2.2 FUNGU D 01 WIZARA YA NCHI (OR) TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ 29

MRADI WA MJI SALAMA 34

FUNGU D 02 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) 39

JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) - PEMBA 57

6.3.3: WAKALA WA ULINZI WA JESHI LA KUJENGA UCHUMI (SGA) 68

FUNGU D 03 - CHUO CHA MAFUNZO ZANZIBAR 77

CHUO CHA MAFUNZO PEMBA 92

6.3.5 - FUNGU D04: KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) - UNGUJA 95

FUNGU D09 - MKOA WA KASKAZINI UNGUJA 152

MKOA WA KASKAZINI - PEMBA 167

FUNGU D12 - WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII 168

WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO 173

6.4.1 FUNGU F 01 - OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO 173

TUME YA MIPANGO - PEMBA 202

WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA WA SERIKALI – PEMBA 225

WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI - UNGUJA 228

6.10: WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI 250
6.10.1 - FUNGU K 01 - WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI 250
6.10.2: BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU 262
BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU- PEMBA 267
6.10.5: BARAZA LA MITIHANI ZANZIBAR 270
OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU 275
6.10.4: AFISI YA MRAJIS WA BARAZA LA ELIMU ZANZIBAR 277
6.11.1: FUNGU L01 - WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO 279
IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO ZANZIBAR 298
IDARA YA MISITU ZANZIBAR 300
IDARA YA KILIMO 319
TAASISI YA UTAFITI WA MIFUGO ZANZIBAR (ZALIRI) 325
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO ZANZIBAR (ZARI) 328
WAKALA WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO - UNGUJA 331
WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO - PEMBA 336
RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM KUHUSU MALIPO YA WAZEE YA PENCHENI JAMII KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2020 340
UKAGUZI WA MFUMO WA USIMAMIZI WA PENCHENI JAMII (ZANZIBAR UNIVERSAL PENSION SYSTEM - ZUPS) 346
RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM KUHUSU UFANISI WA UTEKELEZAJI WA MRADI WA KILIMO CHA PILIPILI HOHO KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2020. 349
UTEKELEZAJI WA MRADI WA PILIPILI HOHO KATIKA ENEO LA BAMBI 358
MRADI WA PILIPILI HOHO PANGATUPU 360
UTEKELEZAJI WA MRADI WA PILIPILI HOHO KATIKA MAENEO YA PUJINI NA FINYA KISIWANI PEMBA 360
KIKAO MAALUM CHA WIZARA ZILIZOHUSIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI WA PILIPILI HOHO 361
RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM KUHUSU UNUNUZI WA MCHELE NA MBOLEA KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2020. 362
5.2: IDARA YA UHAKIKI WA CHAKULA NA LISHE 362
5.3: UNUNUZI WA TANI 740 ZA MBOLEA (UREA) U$D 279,720 365
RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM KUHUSU UKODISHWAJI WA MASHAMBA YA MIKARAFUU. 371
MAMBO YALIYOBAINIKA WAKATI KAMATI ILIPOKUTANA NA BAADHI YA WAKODISHWAJI WA

MASHAMBA YA MIKARAFUU 382
UCHUNGUZI WA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KUHUSU RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO (CDF) KUANZIA MWAKA 2019 HADI 2020 384
MAELEZO YA JUMLA YA KAMATI YA PAC 384
UTEKELEZAJI WA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KATIKA WILAYA YA WETE - PEMBA KWA MWAKA 2019 HADI 2020 385
UTEKELEZAJI WA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KATIKA WILAYA YA CHAKE CHAKE - PEMBA KWA MWAKA 2019 HADI 2020 387
UTEKELEZAJI WA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KATIKA WILAYA YA KUSINI - PEMBA KWA MWAKA 2019 HADI 2020 390
UTEKELEZAJI WA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KATIKA WILAYA YA MJINI KWA MWAKA 2019 HADI 2020 393
MIRADI ILIYOTEKELEZEZWA NA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KATIKA MANISPAA YA MAGHARIBI - "A" KUANZIA MWAKA 2019/2020 405
MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA MANISPAA YA MAGHARIBI – 'B' KWA MWAKA 2019-2020 412
SEHEMU YA TATU 420
HITIMISHO 420

SEHEMU YA KWANZA

RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI
HESABU ZA SERIKALI (PAC) YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR,
KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## 1.0 UTANGULIZI

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ya PAC imefanikiwa kufanya uchunguzi wa Vitabu Vitatu kati ya Sita vya Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufuatia uwasilishwaji wake uliofanywa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman mbele ya Baraza la Kumi Mkutano wa Nane wa Baraza katika kikao cha tarehe 13 Septemba, 2022.

Katika uchunguzi wa Vitabu vilivyowasilishwa, jumla ya Ripoti Tatu zilifuatiliwa na kuchunguzwa. Ripoti zenyewe ni:

1. Ripoti ya Ukaguzi Maalum Unaohusu Utekelezaji wa Maagizo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi wakati wa kuwaapisha Viongozi Wakuu unaohusu:

    a) Ripoti ya Ukaguzi Maalum Kuhusu Malipo ya Wazee ya Pencheni Jamii kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.
    b) Ripoti ya Ukaguzi Maalum kuhusu ufanisi wa utekelezaji wa Mradi wa Kilimo cha Pilipili Hoho kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.
    c) Ripoti ya Ukaguzi Maalum kuhusu ununuzi wa mchele na mbolea kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.
    d) Ripoti ya Ukaguzi Maalum kuhusu ukodishwaji wa Mashamba ya Mikarafuu.

2. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021;
3. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019 hadi 2020.

## 1.1 WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI YA PAC

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati hii imeundwa na Wajumbe Sita (6) na Sekretarieti ya Watendaji 7 kama ifuatavyo:

### 1.1.1 Waheshimiwa Wajumbe:

| Na. | Jina Kamili | Cheo/Wadhifa |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Juma Ali Khatib | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Salha Moh'd Mwinjuma | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mihayo Juma N'hunga | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Maryam Thani | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |

Sekretarieti ya Kamati hii ilikuwa na Maofisa Watatu (3) ambao ni Makatibu wa Kamati na Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama wafuatao:

### 1.1.2 Sekretarieti:

| Na. | Jina Kamili | - | Cheo/Wadhifa |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Maryam Haji Ali | - | Katibu |
| 2. | Ndg. Said Khamis Ramadhan | - | Katibu |
| 3. | Ndg.Nassor Mdachi Mwinyi | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti - (Unguja) |
| 4. | Ndg. Aley Mohamed Abeid | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti - (Unguja) |
| 5. | Ndg. Mussa Kadir Mussa | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti - (Unguja) |
| 6. | Ndg. Muhamad Saleh Juma | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti - (Pemba) |
| 7. | Moh'd Suleiman Amour | - | Mkaguzi - Ofisi ya Mdhibiti - (Pemba) |

## 1.2 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya PAC imezingatia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo hutumika kuwa ni Hadudi Rejea, matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Sheria ya Kinga, Uwezo na Fursa za Wajumbe pamoja na Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020).

Sambamba na hilo, Kamati ilikutana na Watendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali zilizohusika na hoja zilizoibuliwa katika Ripoti ya Mdhibiti kwa kufanya mahojiano, kupitia vielelezo na hatimae kufanya ziara katika maeneo mbali mbali kushuhudia uhalisia wa majibu yaliyotolewa na Wizara au Taasisi husika pamoja na Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Aidha, Kamati kwa kuzingatia haja iliyokuwepo, ilifanya ziara katika maeneo husika na baadae ilifanya mijadala ya hoja mbali mbali.

Shughuli hizi zilifanyika ndani ya mizunguko mitano kama ifuatavyo:

Mzunguko wa Kwanza: Ulianzia tarehe 28/3/2022 hadi 01/4/2022 - Pemba na kumalizia tarehe 4/4/2021 hadi 14/4/2022 - Unguja

Mzunguko wa Pili: Ulianzia tarehe 2/8/2022 hadi 5/8/2022 - Pemba na kumalizia tarehe 9/08/2022 hadi 19/08/2022

a; naMzunguko wa Tatu: Ulianzia tarehe 24/10/2022 hadi tarehe 28/10/2022  Pemba na kumalizia tarehe 31/1/2023 hadi tarehe 03/2/2022 - Unguj

Mzunguko wa Nne: Ulianzia tarehe 16/1/2023 hadi 20/1/2023 - Pemba na kumalizia tarehe 23/1/2023 hadi 03/2/2023 - Unguja;

## SEHEMU YA PILI

## UCHUNGUZI WA RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2020

### 2.0 MAUDHUI:

### 2.1 OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

### 6.2.1: FUNGU C 01 - OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS, SERA URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 45,263,608,741. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu Baraza la Wawakilishi iliweza kukusanya jumla ya shilingi 13,689,862,866 sawa na asilimia 30 ya makadirio.

**Majibu ya Wizara**

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 45,263,608,741. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu Baraza la Wawakilishi iliweza kukusanya jumla ya shilingi 13,689,862,866 sawa na asilimia 30 ya makadirio.

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi 175,000,000 na kuziwasilisha Hazina ikiwa ni sehemu ya vyanzo vya mapato ya Serikali. Hadi kufikia Juni 2021 jumla ya fedha zilizokusanywa ni Shilingi 123,231,900 ambazo ni sawa na asilimia 70.

Kiasi cha fedha kilichokadiriwa na kukusanywa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Fungu C01) kilitokana na huduma kutoka katika Idara/Taasisi nne za Ofisi ya Makamu

wa Pili wa Rais kwa mchanganuo ufuatao:

| Na | Idara | Kilichopangwa (TSH) | Kilichokusanywa (TSH) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 62,800,000 | 24,297,800 | 39 |
| 2. | Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira | 98,000,000 | 90,874,100 | 93 |
| 3. | Ofisi Kuu Pemba | 14,200,000 | 8,060,000 | 57 |
| | **Jumla** | **175,000,000** | **123,231,900** | **70** |

Kiasi cha fedha zilizokusanywa kupitia Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa kinatokana na ukodishaji wa vifaa vya sherehe ikiwemo mashamiana na viti pamoja na kodi ya milango ya maduka iliyopo Mwanakwerekwe; kwa upande wa Ofisi Kuu Pemba makusanyo yake yalitokana na huduma za ukodishaji wa mashamiana, ada ya uhifadhi wa mazingira na ada ya ukaguzi wa mazingira.

Aidha, mapato ya makusanyo ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira yanatokana na ada ya uhifadhi wa mazingira na ukaguzi wa mazingira.

Upatikanaji wa asilimia kidogo ya mapato ya makusanyo kwa upande wa Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa (39%) na Ofisi Kuu - Pemba (57%) unatokana na uhaba na uchakavu wa vifaa vinavyokodishwa hasa mashamiana pamoja na kujitokeza kwa wakodishaji binafsi wengi wenye mashamiana ya mapya na ya kisasa pamoja na kukodisha kwa bei nafuu zaidi. Hivyo, wateja wa huduma hiyo hukimbilia zaidi kwa watoa huduma binafsi.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kuchunguza hoja hii ya mapato, Kamati ya PAC imebaini kwamba kulikuwa na utofauti wa makadirio na mapato yaliyopatikana yaliyoelezwa katika Ripoti ya Mdhibiti na makadirio na mapato yaliyowasilishwa na Wizara. Hata hivyo, baada ya kupitia kwa makini hesabu za mapato zilizowasilishwa, Kamati yetu iligundua hakukuwa na tofauti kwa sababu taarifa ya Mdhibiti ilijumuisha pamoja na makadirio ya mapato ya Wizara na Washirika wa Maendeleo lakini Wizara ilichanganua moja baada ya nyengine (hazikujumuishwa pamoja). Hivyo, baada ya kuweka sawa hesabu, Kamati iliridhika kwamba hesabu zote mbili zinafanana na Kamati yetu haikuwa na hoja zaidi.

## Taarifa ya Matumizi

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,034,800,306 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 50,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 6,580,382,083 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ambapo ni sawa na asilimia 82 ya makadirio na shilingi 50,000,000 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 100 ya makadirio.

### Majibu ya Wizara

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,034,800,306 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 50,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 6,580,382,083 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ambapo ni sawa na asilimia 82 ya makadirio na shilingi 50,000,000 ziliingizwa na kutumikakwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 100 ya makadirio.

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Fungu C01) katika mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia Shilingi 23,247,454,741 kwa kazi za kawaida ambapo Shilingi 4,538,696,642 ni kwa ajili ya mishahara, posho zinazoendana na mishahara na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na Shilingi 3,496,103,664 kwa matumizi mengineyo (OC). Aidha, ruzuku (Subvention) zilizokadiriwa ni Shilingi 14,742,126,000 kwa ajili ya Idara ya Uhamiaji, Zanzibar na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa na Shilingi 470,528,435 kwa ajili ya mishahara ya Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa.

Hadi tarehe 30 Juni, 2021 Ofisi ilitumia Shilingi 12,043,081,162 (51.8%) ya kiasi kilichopangwa ambapo Shilingi 4,386,532,059 ni mishahara na malipo mengine yanayoendana nayo ikiwa ni asilimia 96.6 ya kiasi kilichopangwa; Shilingi 2,193,850,054 ni kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 62.8 ya kiasi kilichokadiriwa; Shilingi 4,993,370,614 (33.9%) kwa ajili ya ruzuku ya matumizi mengineyo na Shilingi 469,328,435 (99.7%) ni ruzuku ya mishahara ya Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa.

Kwa upande wa kazi za maendeleo, Ofisi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia Shilingi 21,841,154,000 ambazo miongoni mwao Shilingi 50,000,000 ni mchango wa Serikali na Shilingi 21,791,154,000 ni mchango wa Wahisani. Hadi kufikia Juni 30, 2021 Ofisi iliingiziwa Shilingi 1,523,549,804 sawa na asilimia 7 ya fedha zilizopangwa. Kati ya fedha zilizopatikana, Shilingi 50,000,000 sawa na asilimia 100 ni mchango wa SMZ na Shilingi 1,473,549,804 sawa na asilimia 6.8 ni mchango wa Wahisani (Kiambatisho Nam. 2 kinahusika).

Baadhi ya matumizi yalikuwa ni kwa asilimia kidogo kutokana na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ikiwemo matumizi mengineyo (62.8%) na ruzuku ya matumizi mengineyo (33.9%). Kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha, Ofisi iliamua kutokufanya matumizi kwa baadhi ya shughuli na huduma ikiwemo ununuzi wa gari pamoja na vifaa vipya vya sherehe na kuendelea na utafiti mmoja badala ya kufanya tafiti nyengine mpya. Kwa upande wa ruzuku ya matumizi mengineyo, asilimia iliyopatikana ilikuwa ni ndogo kutokana na kutokuingizwa fedha katika Akaunti za Idara ya Uhamiaji kwa mujibu wa makubaliano yaliyopo awali.

Halkadhalika, Ofisi ilipata asilimia kidogo kwa upande wa kazi za maendeleo ambapo

iliingiziwa asIlimia 7 tu ya fedha iliyokadiriwa. Hali hiyo imetokana na fedha zilizokusudiwa kwa Mradi wa Kupunguza Kaya Maskini kutokuingizwa kama ilivyokusudiwa ambapo badala ya Shilingi Bilioni 21.8 Ofisi iliingiziwa Shilingi Bilioni 1.5. Hali hiyo ilipelekea Ofisi kutekeleza baadhi ya shughuli za mpango huo na shughuli nyengine kuzitekeleza mwaka uliofuata.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Maelezo ya uchunguzi wa hoja hii ya taarifa za matumizi unalingana na maelezo ya uchunguzi wa taarifa ya mapato.

6.2.2 MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (ZEMA)

**Hoja ya nambari 6.2.2.1: Kutokuwepo kwa uthibitisho wa uhalali wa utoaji wa fedha za mapato shilingi 40,098,000.**

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 40,098,000 ni fedha ambazo zimetolewa katika daftari la ujumla la Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa uthibitisho wa barua iliyoidhinisha utolewaji wa fedha hizo kwa ajili ya ukaguzi, hivyo kupelekea kushindwa kujua uhalisia unaotokana na utolewaji wa fedha hizo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Mamlaka ya Mazingira kuhakikisha unasimamia kikamilifu Taasisi zake ili kuhakikisha kwamba sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya fedha inafuatwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika upatikanaji wa idhini ili kuepusha uwezekano wa kuweza kujitokeza kwa viashiria vya ubadhirifu katika matumizi ya fedha za Umma.

Majibu ya Mamlaka

Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais inakusanya mapato kutoka vyanzo vyake mbali mbali na kuingiziwa na wadau moja kwa moja katika Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kama taratibu zilivyo na baadae fedha hizo huhamishwa na kupelekwa Benki ya Tanzania (BOT). ZEMA na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais haina idhini ya kutoa fedha hizo.

Kwa hivyo utokaji wa fedha za mapato kwenye general ledger ulisababishwa na uingizwaji wa taarifa za mapato mara mbili kimakosa. Hivyo Maafisa wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais walishirikiana katika kurekebisha tatizo la mapato hayo ili kuweka sawa taarifa za Mapato. Hali hiyo inaonesha kuwa hakuna fedha zilizopotea kwa sababu ripoti zote za Mapato kutoka PBZ na Wizara ya Fedha ziko Sawa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imegundua kwamba kujitokeza kwa hoja hii kumetokana na muhusika ambae atumia mfumo kuingiza taarifa za mapato zaidi ya mara moja alikuwa masomoni kipindi ambacho Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ambapo kulihitajika uthibitisho wa kuwepo kwake masomoni haukupatikana.

Hata hivyo, Kamati yetu ilijiridhisha kwamba kweli kulitokea kasoro ya kuingiza mapato mara mbili lakini hakukuwa na fedha ambayo ilipotea. Hali hiyo lilitokea kutokana na muingizaji kuona kwamba alipoingiza fedha katika mfumo kwa mara ya kwanza, mfumo haukupokea fedha hizo na kuingiza tena kwa mara ya pili na kusomeka kwamba fedha zimeingizwa mara mbili.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wizara wanaohusika na uingizaji wa fedha za mapato katika mfumo wa IFIMS wanatakiwa kuwa makini wanapotekeleza majukumu yao ili kuepusha kuonekana kasoro zinazoweza kupelekea upotevu wa fedha za Umma.

**Hoja ya nambari 6.2.2.2: Kukosekana kwa tozo la adhabu kwa Wawekezaji wanaopatiwa huduma za kimazingira.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla wawekezaji 59 wameshindwa kukatwa tozo ya adhabu na Mamlaka ya Mazingira - ZEMA kutokana na kumaliza kwa muda wa matumizi ya vibali vya ukaguzi wa mazingira ambao ni miaka mitano ya matumizi. Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na tozo hizo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamamizi wa Mazingira ya Zanzibar.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhakikisha unasimamia kikamilifu Taasisi zake ili kuhakikisha kwamba sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya fedha inafuatwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika upatikanaji wa idhini ili kuepusha uwezekano wa kuweza kujitokeza kwa viashiria vya ubadhirifu katika matumizi ya fedha za Umma.

**Majibu ya Mamlaka**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 46(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2015, Ukaguzi wa Kimazingira, utafanywa kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:-

(a) Shughuli ambayo inafanyika bila ya kuwa na Cheti cha Tathmini ya Athari za Kimazingira na inaelekea kuwa na athari kubwa kwa mazingira na jamii; au

(b) Shughuli ambayo itakuwa na Cheti cha Tathmini ya Athari za Kimazingira na utekelezaji wake umefikia miaka mitano tokea tarehe ya kuanza shughuli za

uzalishaji (an activity which is operating with Environmental Impact Assessment Certificate for a period of five years from the date of commencement of the operation phase);

(c) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1)(b) cha kifungu hiki, ukaguzi wa kimazingira unaweza kufanywa kwa shughuli yeyote itakayoamuliwa na Mamlaka kupitia ufuatiliaji wa mara kwa mara.

Kwa mujibu wa kifungu hicho cha 46(1)(b) ni kuwa Ukaguzi wa Kimazingira utafanyika baada ya miaka mitano (5) tokea tarehe ya kuanza shughuli za utekelezaji wa mradi na sio tarehe ambayo Cheti cha Tathmini za Kimazingira kilipotolewa. Maelezo ya Miradi iliyohusika ni kama ifuatavyo:

### Maelezo ya Miradi

| Nam. | Jina la Mradi | Maelezo |
|---|---|---|
| 1. | Construction of Jetty for Fruit and Spice Farm | Miradi ya aina hii haifanyiwi Ukaguzi wa Kimazingira kutokana na kuwa haibadiliki na Ukaguzi wake wa kimazingira kuchanganywa na ukaguzi wa hoteli ambao ulitakiwa ufanyike mwaka 2022 na mchakato wake umeshaanza. |
| 2. | Construction of 9 Holes Golf Course | Mradi huu ulianza kazi rasmi mwaka 2017 na hivyo, unahitaji kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022 ambao mchakato wake umeshaanza. Hata hivyo, mradi huu haufanyi kazi vizuri kwa kukosa watenda na mashindano makubwa kama ilivyotarajiwa. |
| 3. | Zenj Petrogas Deport for Zenj Petrogas Company Ltd | Mradi huu haukufanyika kutokana na eneo la la Mradi liliopo Mtoni lilifutiwa Land lease kwa kuwa Depot zote zinatakiwa kuhama eneo la Mtoni na kuhamia Mangapwani. |
| 4. | The Liquefied Petroleum Gas Filling Station | Mradi huu haujafanya Ripoti ya Ukaguzi kwa sababu Mradi huu unatakiwa kuhamia Mwangapwani ambapo atafanya Ripoti mpya ya Tathmini za Kimazingira. |
| 5. | Uroa Paradise Beach Resort | Mradi huu ulipewa Cheti cha Tathmini ya Athari za Kimazingira mwaka 2019 na hivyo, utahitaji kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2024. |
| 6. | Amber Golf and Beach Resort | Mradi huu haujamaliza ujenzi na Audit kwa mujibu wa Sheria hufanywa baada ya miaka mitano kuanzia tarehe ya kuanza kazi (in operation). |
| 7. | Island Paradise Inn Hotel | Hoteli hii ilianza kufanya kazi mwaka 2017 na hivyo ilihitaji kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022 na taratibu zimeshaanza. |
| 8. | Tulia Resort (Nature Safari Lodge) | Hoteli hii ilipewa Cheti mwaka 2015, na ilianza kazi mwaka 2017 na hivyo, inatakiwa kufanya |

| | | |
|---|---|---|
| | | Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. Taratibu za kufanya Ukaguzi zimeshaanza. |
| 9. | Beach Resort Project (Fard Company) | Mradi huu ulitakiwa kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022 na tayari umeshaanza kufanyiwa. |
| 10. | Uzuri Zanzibar Resort Project | Mradi huu ulitakiwa kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022 na tayari umeshaanza kufanyiwa. |
| 11. | Zas Villa Luxury and Resort | Mradi huu ulitakiwa kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022 na tayari umeshaanza kufanyiwa. |
| 12. | The proposed Kizimkazi Petrol Service Station | Kituo hiki kilipewa Cheti mwaka 2015, na kilianza kazi mwaka 2018 na hivyo, kinatakiwa kufanya Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2023. |
| 13. | The proposed Land Reclamation and Marina Development Project at Mtoni Marine Hotel | Hoteli hii ilipewa Cheti mwaka 2015, na ilianza kazi mwaka 2017 na hivyo, inatakiwa kufanya Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022 na hatua zimeshachukuliwa. |
| 14. | Parklane Holdings Best Western Hotel Place | Hoteli hii ilipewa Cheti mwaka 2015, na ilianza kazi mwaka 2017 na hivyo, inatakiwa kufanya Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. Hatua tayari zimeshaanza kuchukuliwa. |
| 15. | Fundo Eco-lodge | Hoteli hii ilipewa Cheti mwaka 2015, na ilianza kazi mwaka 2017 na hivyo, inatakiwa kufanya Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. Hatua tayari zimeshaanza kuchukuliwa. |
| 16. | Construction of expansion of jetty at Wesha | Mradi huu ulipewa Cheti mwaka 2015, lakini haustahiki kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira. Kimaumbile haustahiki kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira hadi hapo itakapotaka kujengwa upya. |
| 17. | Renovation and Redigning of Mtoni Marine Hotel (Hotel Verde) | Hoteli hii imepewa Cheti mwaka 2015, na ilianza kazi mwaka 2017 na hivyo, inatakiwa kufanya Ukaguzi wa Kimazingira 2022. Hatua tayari za kufanya ukaguzi zimechukuliwa. |
| 18. | Pemba Lala lodge | Hoteli hii imepewa Cheti mwaka 2015, na ilianza kazi mwaka 2017 na hivyo, unatakiwa kufanya Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. Hatua tayari zimeshachukuliwa. |
| 19. | Mass Services Petrol Station | Kituo hiki kilipewa Cheti mwaka 2015 na kilianza Operesheni mwaka 2017 na hivyo, kitakiwa kufanya Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. |
| 20. | Proposed Construction of Beach Resort and Spa At Michamvi Kae | Umepewa Cheti cha Tathmini za Kimazingira mwaka 2015 lakini haukuendelezwa na ulifanyiwa tena Tathimini ya Kimazingira na kupewa Cheti mwaka 2021 na hivyo, unahitaji kufanyiwa ukaguzi mwaka 2026. |
| 21. | Kisauni CCM Petrol Station | Kituo hiki kilipewa Cheti mwaka 2015 na hadi hivi sasa hakijajengwa. |

| | | |
|---|---|---|
| 22. | Natural Kendwa Hotel | Mradi huu umefanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira na kupewa Cheti cha Ukaguzi wa Kimazingira tarehe 03/03/2020 na hivyo, unahitaji kufanyiwa mwaka 2025. |
| 23. | Seaside Villa Limited | Hoteli hii ipewa Cheti mwaka 2015, na ilianza kazi mwaka 2017 na hivyo, inatakiwa kufanya Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. Hatua za kufanya Ukaguzi huo zimeshaanza kuchukuliwa. |
| | TLapnet White Paradise (White Paradise) - Pongwe Ndudu | Hoteli hii imepewa Cheti mwaka 2015, na ilianza kazi mwaka 2016 na hivyo, ilitakiwa kufanya Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2021. Hivyo, Hoteli hii imefanya Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2021 na Ripoti yake imewasilishwa ZEMA mwishoni mwa mwaka 2021 na kupewa Cheti cha Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. Hivyo, Ukaguzi mwengine wa Kimazingira utafanyika mwaka 2027. |
| 24. | Communication Tower - Airtel (Stone Town) | Miradi hii ilipewa vyeti tarehe 01/11/2016 na ulianza operesheni mwaka 2017 na hivyo inatakiwa kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. Taratibu za kufanya Ukaguzi huu zimeshachukuliwa. |
| 25. | Proposed Communication tower - Airtel Blue Bay | |
| 26. | Proposed Communication tower - Airtel, Amani Magogoni | |
| 27. | Proposed Communication tower -Airtel, Unguja Ukuu | |
| 28. | Proposed Communication tower - Airtel, - Mwera | |
| 29. | Proposed Communication tower - Airtel, Fuoni | |
| 30. | Kibuteni Petrol Station | Ulipewa Cheti tarehe 04/02/2016. Hata hivyo, ujenzi wake upo katika hatua za mwisho za kumalizika na hivyo mradi huu haujaanza operesheni. |
| 31. | Construction of Airstrip Kigunda | EIA ya mwanzo ilifanywa mwaka 2016 na kupewa Cheti mwaka huu. Hata hivyo, mradi huu ulichukuliwa na Serikali ambapo ulifanyiwa Tathmini ya Athari za Kimazingira mwaka 2020 na kuanza operesheni mwaka 2021. Hivyo, utahitaji kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2026. |
| 32. | Expansion of Sugar Factory Limited | Kiwanda hiki kilipewa Cheti mwaka 2016 na kuanza kazi mwaka 2017 na hivyo, kinahitaji kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. Hatua za kufanya ukaguzi huu zimeshachukuliwa. |
| 33. | Makunduchi Petrol Station | Ulipewa Cheti mwaka tarehe 01/11/2016 na ulianza operesheni mwaka 2018 na hivyo inatakiwa kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira |

| | | |
|---|---|---|
| | | mwaka 2023. |
| 34. | Zanzibar/Africa Queen hotel | Hoteli hii imepewa Cheti mwaka 2016 na ilianza operesheni mwaka 2017 na hivyo inahitaji kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. Hatua za kufanya ukaguzi huu zimeshachukuliwa. |
| 35. | Cinnamon Hotel | Hoteli hii imepewa Cheti mwaka 2016 na ilianza operesheni mwaka 2017 na hivyo inahitaji kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. Hatua za kufanya ukaguzi huu zimeshachukuliwa. |
| 36. | The Development of Amber Marina Resort - Penny Royal Hotel. | Ujenzi wa sehemu ya bahari ya Mradi huu haujaanza na operesheni na kwa hivyo, ukaguzi wa kimazingira wa hoteli hii haujafikiwa na muda wake. |
| 37. | Fumba Uptown Living Project | Mradi huu ulipewa Cheti mwaka 2016 na operesheni ya mradi ulianza mwaka 2017. Ukaguzi wa Kimazingira unahitaji kufanyika mwaka 2022 ambapo hatua za kufanya zimeshachukuliwa. |
| 38. | Petrol Pump Station – Fuoni-Meli Tano | Kituo hiki kilipewa Cheti mwaka 2016 na hadi sasa hakijafunguliwa na hivyo, hakijaanza kazi. |
| 39. | The proposed Construction of jetty platform and Bay Pavilion Villa Konokono | Cheti cha Mradi huu kilitolewa mwaka 2016 na ilianza kazi mwaka 2019 na hivyo, inahitaji kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2024. |
| 40. | Zamani Villa and Spa | Hoteli hii ilipewa Cheti mwaka 2016 na ilianza kazi mwaka 2018 na hivyo inatakiwa kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2023. |
| 41. | Indoor Residual, Spraying Against Malaria Vector | Hii ni project ya Msimu ya kunyunyunyiza dawa ya malaria majumbani. Na inapotokezea kufanywa shughuli hiyo ni Tathmini ya Kimazingira hufanywa. |
| 42. | ZSSF Real Estate | Mradi huu ulipewa Cheti mwaka 2016 na ulizinduliwa mwaka 2020 na hivyo utahitaji kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2025. |
| 43. | Baladin Zanzibar Beach Hotel | Mradi huu ulipewa Cheti mwaka 2016 na ulianza kazi mwaka 2017 na hivyo, utahitaji kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. Hatua za kufanya Ukaguzi wa Kimazingira tayari zimeshachukuliwa. |
| 44. | Proposed Communication Tower at Kiwengwa | Minara hii ilipewa Cheti mwaka 2016 na ulianza operesheni mwaka 2017 na hivyo inatakiwa kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2022. Hatua za kufanya Ukaguzi wa Kimazingira tayari zimeshachukuliwa. |
| 45. | Proposed Communication Tower at Mwera | |
| 46. | Proposed Communication Tower at Tunguu | |
| 47. | Proposed Communication Tower at Micheweni Pemba | |

| | | |
|---|---|---|
| 48. | Proposed Communication Tower at Jambiani | |
| 49. | Proposed Communication Tower at Kitogani | |
| 50. | Proposed Communication Tower at Chaani Kikobweni | |
| 51. | Proposed Communication Tower at Makunduchi | |
| 52. | Proposed Communication Tower at Mbweni | |
| 53. | Proposed Communication Tower at Chwaka Bay | |
| 54. | Proposed Communication Tower at chwaka Bay TTCL | |
| 55. | Premier Laundry Services | Mradi huu ulipewa Cheti mwaka 2016 na ulianza kazi mwaka 2018 na hivyo, unahitaji kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2023. |
| 56. | Opulent Silver Sand Beach - PONGWE | Ulipewa Cheti mwaka 2016 na hadi sasa haujaanza ujenzi. |
| 57. | Milele Resort - UROA | Mradi huu ulipewa Cheti mwaka 2016 na ulianza kazi mwaka 2018, na hivyo unahitaji kufanyiwa Ukaguzi wa Kimazingira mwaka 2023. |
| 58. | Al - Jasara Petroleum, Micheweni | Kituo hiki kilipewa Cheti mwaka 2016 na kilianza Ujenzi mwaka 2018 na hivyo unahitaji kufanyiwa Audit mwaka 2023. |
| 59. | Imania Petrol Station, Micheweni | Kituo hiki kilipewa Cheti mwaka 2016 na kilianza Ujenzi mwaka 2018 na hivyo unahitaji kufanyiwa Audit mwaka 2023. |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC baada ya kuelezwa kwamba ili Mamlaka ya Mazingira iweze kuanza kutonza ada za ukaguzi, ni lazima Mradi husika uwe umeshatimiza miaka mitano tokea uanze kufanya kazi. Kamati iliipitia Miradi iliyoainishwa katika Ripoti ya Mkaguzi na kugundua kwamba mingi yao ilikuwa haijatimiza masharti hayo na kuridhika na majibu ya Mamlaka baada ya kujiridhisha kupitia Kifungu cha 46(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2015 na haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.2.2.3: Kutokuwepo kwa uwiano wa taarifa baina ya hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na uhalisia wa matumizi ya fedha Shilingi 75,148,676.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 75,148,676 zinatokana na tofauti iliyobainika kupitia katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na mlinganisho wa taaarifa halisi ya matumizi ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petrol na Diesel ambapo katika hesabu za mwisho wa mwaka matumizi hayo yanaonekana ni shilingi 161,148,710 lakini katika uhalisia wa taarifa kupitia katika hati za malipo ni shilingi 86,000,034 na kupelekea tofauti iliyobainishwa hapo juu. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya

mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhakikisha unasimamia kikamilifu Taasisi zake ili kuhakikisha kwamba sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya fedha inafuatwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika utayarishaji wa taarifa za fedha ili kuepusha uwezekano wa kuweza kujitokeza kwa utofauti wa taarifa zinazowasilishwa katika mamlaka husika pamoja na taarifa zinazotumika katika taasisi.

**Majibu ya Wizara**

Fedha zilizoripotiwa ndani ya kitabu cha hesabu za mwaka 2020/2021 ni jumuishi ambazo zinahusisha Idara zote za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Matumizi ya vifungu vya mafuta vilivyoripotiwa katika kitabu cha hesabu ni vya Idara zote za Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Ukaguzi wa vifungu vya mafuta uliofanyika ni wa Idara za ndani tu.

Matumizi ya Mafuta ya Idara ambazo zipo nje ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kama vile Idara ya Uratibu Dar-es-Salaam, Idara ya Watu wenye Ulemavu, Idara ya Mazingira, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira pamoja na Ofisi kuu Pemba hazikujumuishwa. Kiambatisho Namba 3 kinatoa ufafanuzi wa matumizi halisi ya mafuta ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba tofauti ya fedha shilingi 75,148,676 ilitokana uzembe wa Watendaji wa Wizara kutozijumuisha fedha za Taasisi zinazojitegemea (zenye ‘vote’) ikiwemo Afisi Kuu Pemba na hesabu za mwisho wa mwaka za Wizara kushindwa kutoa taswira halisi ya mapato na matumizi yaliyofanyika.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inasisitiza kwamba pamoja na kwamba Taasisi nyengine za Serikali zinajitegemea lakini Wizara ndio Mama Mkuu wa Taasisi hizo, hivyo, hesabu zao zinatakiwa kuonekana katika hesabu za mwisho wa mwaka za Wizara husika.

**Hoja nambari 6.2.2.4: Matumizi ambayo hayakuainishwa katika Mpango wa Manunuzi Shilingi 127,500,000**

Jumla ya shilingi 127,500,000 zimelipwa kupitia hati namba 13/2/2021 ya tarehe 22/2/2021 ambazo amelipwa Tononoka Fireworks Ltd. kwa ajili ya malipo yanayohusu upigaji wa fash fash kwa mwezi wa Januari 2021, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa matumizi hayo hayakuainishwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka wa Ofisi wa Makamo wa Pili wa Rais ili kuepusha kufanyika kwa mtumizi ambayo hayaendani na makadirio halisi na kupelekea kutokupatikana kwa uthibitisho wa matumizi katika kipindi cha mwaka husika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya

Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhakikisha unasimamia kikamilifu Taasisi zake ili kuhakikisha kwamba Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma inafuatwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika utayarishaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka ili kuepusha uwezekano wa kutokuingizwa kwa baadhi ya taarifa zitokanazo na ununuzi wa huduma au bidhaa.

**Majibu ya Wizara**

Fedha za Maadhimisho ya Sherehe za Mapinduzi kikawaida hupangwa katika bajeti ya Serikali ya kila mwaka ikiwa ni sehemu ya bajeti ya Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Fedha hizo hupitishwa na BLW kwa ujumla kutokana na kiasi cha ukomo wa bajeti iliyopewa Idara hiyo na baadae hupangiwa matumizi kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali juu ya namna ya kuadhimisha sherehe hizo kwa mwaka husika. Fedha hizo baadae hugawiwa kwa kila Kamati kulingana na maelekezo yaliyotolewa kupitia vikao vya Halmashauri ya Sherehe vinavyoanza mwezi Oktoba.

Kutokana na mazingira hayo, suala la ununuzi wa vifaa vya sherehe za Mapinduzi kwa miaka iliopita vilikuwa haviingizwi katika Mpango wa Ununuzi wa Ofisi kwa vile wakati yanaandaliwa mahitaji ya vifaa na shughuli nyengine za Sherehe na namna ya Sherehe zitakavyokuwa inakuwa bado haijaamuliwa kwa kuwa Mpango wa manunuzi huandaliwa mwezi wa Juni baada tu ya bajeti kupitishwa. Hata hivyo, mara maamuzi na maelekezo ya vikao vya Halmashauri ya Sherehe yanapotoka juu ya ufanikishaji wa sherehe Ofisi hufuata taratibu zote za ununuzi wa vifaa na huduma zilizoelekezwa kufanikisha sherehe husika ikiwemo fash fash kwa kiasi cha fedha kilichopatikana.

Aidha, kutokana na ushauri uliotolewa juu ya haja ya kuweka ununuzi wa huduma na vifaa vinavyohusika na Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar katika Mpango wa Ununuzi, Ofisi imezingatia na kufanyia kazi suala hilo na tayari imeweka katika Mpango wa Ununuzi wa Mwaka wa fedha unaofuata na inayofuata.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika WIzara hii, ni kweli kwamba Wizara ilikuwa ilikuwa na kasoro hizo. Hata hivyo, hivi sasa tayari WIzara imeshairekebisha ksoro hiyo na tayari wameshaandaa Mpango wa Manunuzi wa Wizara. Hivyo, Kamati yetu haikuwa na hoja zaidi.

**6.2.3: FUNGU C 03 - TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR**

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya Uchaguzi  Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 57,500,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliweza kukusanya jumla ya shilingi 167,772,000 sawa na asilimia 292 ya makadirio.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haikupokea majibu ya kuhusu Taarifa za Mapato za Tume ya Uchaguzi Kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) linalotaka taarifa za Wizara ziwasilishwe siku mbili kabla ya Kamati kufika eneo husika. Hata hivyo, Kamati yetu iliuliza kuhusiana na vyanzo vya mapato vya Tume na kuelezwa kwamba Tume inacho chanzo kimoja tu cha mapato yake kinachotokana na rufaa zinazoambatana na shughuli za uchaguzi.

Kwa mnasaba huo, Kamati yetu inaisisitiza Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ihakikishe inawasilisha majibu ya Taarifa zake za Mapato mbele ya Kamati siku mbili kabla kukutana na Kamati kama matakwa ya Kanuni za Baraza zinavyoelekeza.

**Taarifa ya Matumizi**

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 7,093,181,245 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufi kia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 6,208,523,660 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 87 ya makadirio.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa upande wa majibu ya Taarifa za Matumizi, Kamati pia haikupatiwa majibu na kuelekeza kwamba Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ihakikishe inawasilisha majibu ya Taarifa zake za Matumizi mbele ya Kamati siku mbili kabla kukutana na Kamati kama matakwa ya Kanuni za Baraza zinavyoelekeza.

**Hoja nambari 6.2.3.1: Kutokuingizwa kwa taarifa za mali za kudumu katika hesabu za mwisho wa mwaka (Financial Statements).**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliandaa na kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka katika Ofi si ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuainishwa kwa baadhi ya mali za kudumu za Tume katika hesabu za mwisho wa mwaka (Financial Statements) zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kufanya Hivyo kunaweza kupelekea kutokupatikana kwa usahihi wa hesabu

zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Orodha ya mali za kudumu ambazo hazikuainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka ni kama zinavyoonekana hapo chini:-

### Majibu ya Tume

Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inakubaliana na pendekezo la Mkaguzi la kuingiza taarifa za Mali za Kudumu katika Hesabu za mwaka. Hii imetokana na kutokukamilika kwa Buku la kuweka Hesabu za Mali za Afisi ambalo linaendelea kutayarishwa na Kitengo husika. Hata hivyo, kwa Mwaka wa Fedha unaofuata, Afisi itahakikisha taarifa za mali za kudumu zitapatikana na kuingizwa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

- Kukosekana kwa taarifa za majengo matatu yaliopo Maisara.
- Kukosekana kwa taarifa za ghala kuu liliopo Kikwajuni.
- Kukosekana kwa taarifa za jengo liliopo Wilaya ya Magharibi A.
- Kukosekana kwa taarifa za jengo liliopo Wilaya ya Kati Unguja.
- Kukosekana kwa taarifa za jengo liliopo Wilaya ya Kusini.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar uhakikishe unafanya usahihi wa taarifa zinazotayarishwa na kuwasilishwa katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikiwa ni pamoja na kujumuisha kikamilifu taarifa zote zinazohusu mali za kudumu katika kipindi cha mwaka husika.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Pamoja na Watendaji wa Tume kukubali kwamba wakati Mkaguzi anafika Ofisini kwao, Tume haikuingiza taarifa za mali za kudumu katika hesabu zake za mwisho wa mwaka. Kamati yetu imebaini kwamba changamoto hiyo ilijitokeza kutokana na kutokuwa na umiliki halisi wa baadhi ya majengo wanayoyatumia isipokuwa yalikuwa yanamilikiwa na Taasisi nyengine. Hata hivyo, hivi sasa kuna baadhi ya Majengo yakiwemo jengo la Ofisi ya Tume Wilaya ya Magharibi 'A' Mwera kwa hati nambari CRO/Z.110/2022/0771937 na jengo liliopo Koani - Wilaya ya Kusini kwa hati nambari CRO/Z.109/2022/0771937.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Tume ihakikishe inaziingiza taarifa zote za Mali zake za kudumu ili hesabu yao ya mwisho wa mwaka iweze kutoa taswira halisi na sahihi ya mali zake inazomiliki na isizomiliki.
2. Serikali ifanye utaratibu wa kuipatia Tume ya Uchanguzi Zanzibar majengo yake ya kudumu ili iondokane na hoja za Ukaguzi zinazoweza kuepukika.

**Hoja nambari 6.2.3.2: Kukosekana kwa hatimiliki za majengo**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar inamiliki majengo mbali mbali, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa hati miliki za majengo hayo ili kuweza kuthibitisha uhalali wake ambapo kunaweza kupelekea upotevu wa majengo hayo pasipo na kujuwa. Majengo hayo ni kama ifuatavyo:-

- Majengo Matatu ya Ofi si ya Tume Maisara.
- Ghala kuu la Kikwajuni.
- Jengo Wilaya ya Magharibi A.
- Jengo Wilaya ya Kati Unguja.
- Jengo la Wilaya ya Kusini.

**Majibu ya Tume**

Majengo mengi yanayotumika kwa shughuli za Uchaguzi ni majengo yaliyopatikana kwa njia ya kuazimwa au kupewa na Serikali kwa njia ya barua. Afisi inaendelea na taratibu za kufuatilia upatikanaji wa hatimiliki za majengo yake. Hadi kufikia sasa, Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Mamlaka inayohusika na upimaji wa Ardhi imeshafanya upimaji na kuingiza katika ramani ya nchi, maeneo yote yanayomilikiwa na Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Hivi sasa tumeshapata Hatimiliki za majengo ya Afisi ya Wilaya ya Kati pamoja na Wilaya ya Magharibi A. Tunaendelea kukamilisha hatua za kupatiwa Hatimiliki na majengo matatu yaliyopo Maisara kwa kushirikiana na Msajili wa Ardhi Zanzibar.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uchunguzi na mapendekezo kuhusiana na hoja hii yanalingana na uchunguzi na mapendekezo yalitoelezwa katika hoja nambari 6.2.3.1 ya Ripoti hii.

**Hoja nambari 6.2.3.3: Kutokatiwa bima vyombo vya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.**

Ukaguzi umebaini kuwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar inamiliki vyombo mbali mbali vya usafiri ikiwemo gari na vespa, dosari iliobainika ni kwa baadhi ya vyombo kutokukatiwa bima. Kutokukatiwa bima kwa vyombo vya moto kunaweza kukapelekea kudumaza shughuli za taasisi pale majanga yanapotokezea na kupelekea kutumia gharama kubwa ya matengenezo jambo ambalo linaweza likapelekea kupangua mipango ya utekelezaji wa shughuli nyengine walizojipangia.

Ukaguzi unashauri ni vyema taasisi za umma kuvikatia bima vyombo vyake ili kuepkua

usumbufu utakao jitokeza pindipo majanga yanapotokezea. Mchanganuo wa vyombo ambavyo havijakatika bima ni kama inavyooekana katika jadweli nambari 26 la Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021 katika ukurasa nambari 43.

**Majibu ya Tume**

Magari kumi ya Nissan patroli yaliyotajwa katika Ripoti hiyo, yamesharudishwa Serikalini na yanaendelea kutoa Huduma katika Afisi ya Rais Ikulu. Magari manne ya Prado yameshaanza utaratibu wa kukatiwa Bima, kuanzia mwaka wa fedha 2022/2023. Afisi haikuweza kuyakatia Bima kwa mwaka uliofanyika Ukaguzi kutokana na upungufu wa Fedha zinazopatikana katikafungu la OC. Aidha, TUKTUK zote ambazo zimeorodheshwa zitakatiwa Bima kwa Awamu, kulingana na upatikanaji wa Fedha katikafungu la OC.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Tume kukubaliana na hoja hii lakini Kamati yetu ilitaka kujua kwasasa hatua imefikia wapi na kuelezwa kwamba kuna baadhi ya gari tayari zimeshakatiwa bima katika Shirika la Biama Zanzibar zikiwemo gari nambari SMZ 847A iliyokatiwa bima kwa shilingi 2,616,250 na gari nambari SMZ 1016 imetumia shilingi 3,220,000.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Tume iandae Mpango bora utakaohakikisha vyombo vyake vinakatiwa bima ili kuepusha kutumia gharama kubwa pindipo itatokezea kupata ajali na muda mwingi kukaa bila kufanyiwa matengenezo.

**Hoja nambari 6.2.3.4: Malipo kwa Mtoa Huduma ambaye hakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 8,461,754**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi. Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, Kampuni au Chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar imefanya manunuzi kwa mujibu wa hati namba 2/10 ya tarehe 16/10/20 yenye thamani ya shilingi 8,461,754 ambazo amelipwa kampuni ya Hiffah General Trading Co Ltd ikiwa ni Sehemu ya malipo ya Ujenzi wa Ukuta wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa kampuni hiyo haikusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato, aidha ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. DEPOSIT ACCOUNT - Hesabu Namba 0404346000.

**Majibu ya Tume**

Afisi ilifanya Biashara na Kampuni ya Hiffah General Traders kwa kutambua kuwa Taasisi hiyo imesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi. Mhusika alivyolipwa awamu ya kwanza ya malipo yake alikuwa yumo katika orodha ya Taasisi zilizosajiliwa na Mamlaka. Kwa kuwa alibakisha deni, Afisi ililazimika kutayarisha malipo ya awamu ya Pili ambapo Ukaguzi umebaini kuwa hakusajiliwa na Mamlaka. Suala ni kuwa hakuhalalisha (renew) Usajili wake wakati alipolipwa awamu ya pili. Afisi imepokea ushauri wa Mkaguzi na italifanyia kazi suala hilo ili lisitokee kwa mara ya pili.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Baada ya kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba kweli Tume ilimtumia Mtoa Huduma ambae hakusajiliwa na Mamlaka husika kinyume na kifungu cha 23(1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Hili limetokana na unyeti wa vifaa vilivyopangwa kununuliwa kwa matumizi ya muhimu ya Ofisi kwa wakati huo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauri Tume kwamba inapotokezea manunuzi muhimu na dharura, Tume ihakikishe inaiandikia barua Mamlaka husika ili kuwepo na kielelezo kinachotoa idhini ya utekelezaji wa shughuli husika.

**Hoja nambari 6.2.3.5: vifaa ambavyo havikuingizwa katika daftari la ghalani shilingi 67,533,238**

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shingi 67,533,238 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta na vifaa mbali mbali lakini mafuta na vifaa hivyo havikuingizwa katika daftari kutunzia vifaa ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake.

Kutokuingizwa mafuta na vifaa hivyo katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 27: Mafuta na vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Hati Namba | HundiNamba | Kiasi Kilichotumika (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 60/11/20<br><br>(17/11/20) | TT | 45,779,232 | Machochoki Telecommunication &<br><br>General Services | Ununuzi wa vifaa vya<br><br>kuandikia |
| 59/11/20<br><br>(13/11/20) | TT | 21,754,006 | | Ununuzi wa vifaa vya<br><br>Kutengenezea magari. |
| **Jumla** | | **67,533,238** | | |

**Majibu ya Tume**

Afisi ya Tume ya Uchaguzi imekamilisha kuviingiza vifaa vyote kwenye daftari la ghalani na viko tayari kwa Ukaguzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC baada ya kuvipitia vifaa vilivyokuwa havijarikodiwa katika daftari la ghalani ilitaka kujua sababu iliyoifanya Tume ishindwe kulitekeleza hilo na kuelezwa kwamba vifaa hivyo vilinunuliwa katika kipindi cha uchaguzi muda ambao ulikuwa na shughuli nyingi za matayarisho ya uchaguzi Mkuu. Hata hivyo, vifaa hivyo tayari kasoro hiyo imesharekebishwa.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Tume ihakikishe inafuata taratibu zilizoelezwa na Sheria ya Ununuzi hususan katika uinigizaji wa vifaa walivyonunua ili kuepusha kujitokeza hoja zinazoweza kuepukika.

**Hoja nambari 6.2.3.6: Malipo kwa watoa huduma wasiosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji mali za Umma shilingi 236,798,419.**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi. Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato, aidha ni kwenda kinyume na

Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 28: Malipo yaliyofanyika kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| **Hati Namba** | **Kiasi kilicholipwa (TShs)** | **Aliyelipwa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| 5/7 ya 30/6/20 | 20,117,500 | Galfe Tech Engineering | Uwekaji wa mitambo ya video conference katika ofi si ya Tume Unguja & Pemba Fedha kwa ajili ya ufungaji wa annares katika hema la kuchukulia fomu za wagombea. |
| 22/9 ya 9/8/20 | 2,042,500 | Planet Printing & Decoration | Fedha kwa ajili ya ufungaji wa Bannares katika hema la kuchukulia fomu za wagombea. |
| 4/8 ya 3/8/20 | 208,493,779 | GS Agents Limited | Ununuzi wa wino usiofutika pamoja na lakiri za masanduku ya vifaa vyakupigia kura. |
| 23/11/20 (3/11/20) | 4,721,640 | F.A Glass Works | Malipo kwa ajili ya ujenzi wa mnara wa tangi la maji. |
| 24/11/20 (10/11/20) | 850,00 | | Malipo kwa ajili ya matengenezo ya Ofisi ya Tume. |
| 29/12/20 (22/12/20) | 573,000 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji. |
| **Jumla** | **236,798,419** | | |

**Majibu ya Tume**

Ununuzi wa wino usiofutika ni moja kati ya bidhaa nyeti ambazo upatikanaji wake unategemea uamuzi wa Tume ya Uchaguzi. Kutokana na hali hiyo uamuzi wa Tume juu ya mkandarasi aliyepewa kazi na Tume umezingatia mambo mengi ikiwemo usalama na unyeti wa upatikanaji wake kwa maslahi mapana ya Taifa. Kwa upande mwengine, Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imelipokea pendekezo lililotolewa na Mkaguzi kuhusu kununua huduma kwa watoa huduma waliosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji mali za Umma na tayari imeshalifanyia kazi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Uchunguzi na mapendekezo kuhusiana na hoja hii yanalingana na uchunguzi na mapendekezo yalitoelezwa katika hoja nambari 6.2.3.1 ya Ripoti hii.

## 2.2 FUNGU D 01 WIZARA YA NCHI (OR) TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Katika kuchunguza Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ya PAC ilifanikiwa kupitia, kufanya mahojiano na kuchunguza vielelezo vilivyohusika na

hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti katika Wizara na Taasisi zote za fungu D 01 zinazosimamiwa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, zikiwemo Afisi Kuu Unguja na Pemba, Wakala wa Matukio ya Kijamii, VIkosi vyote Vitano (KMKM, Chuo cha Mafunzo, JKU, KZU na Kikosi cha Valantia.

Ufafanuzi wa Uchunguzi, Matokeo na Mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo:

### 6.3.1 - FUNGU D0I: AFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum ilipangiwa kukusanya mapato ya shilingi 832,800,000.00 na kukadiria kutumia kiasi ya shilingi 28,451,630,000.00. Kati ya hizo shilingi 14,055,400,000.00 ni kwa kazi za kawaida na shilingi 14,396,230,000.00 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwisho wa mwaka 2020/2021 Wizara imepokea shilingi 14,745,376,197.00 sawa na asilimia 52 ya makadirio.

### Taarifa za Mapato

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ilipangiwa kukusanya Tsh. 832,800,000.00 za adayaulinzi (Wakalawa Ulinzi JKU) hadi kumalizika mwaka wa fedha 2020/2021 ilifanikiwakukusanyaTsh 275,000,000.00 sawanaasilimia 33 yamakadirio.

| Kasma | Maelezo | Makadirio kwa mwaka 2020/2021 | Halisi 2020/2021 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1422086 | Ada ya Ulinzi (Wakala wa Ulinzi JKU) | 832,800,000 | 275,000,000 | 33 |

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati haikupatiwa majibu kuhusu taarifa za Mapato lakini Kamati ya PAC imegundua kwamba makadirio ya mapato yaliyoainishwa na Wizara ambayo ni 832,800,000 ni kidogo na tofauti na makadirio yaliyoainishwa na Mkaguzi (30,627,192,391). Hali hiyo ilitokana na Wizara kutoingiza makadirio ya mapato yanatokana na vyanzo vyengine vikiwemo misaada kutoka UNICEF na Wakala wa Barabara. Kwa mazingira hayo, hata mapato halisi yaliyokusanywa nayo yametofautiana. Kamati imebaini kwamba Watendaji wa Wizara hawakuwa na mapato yaliyokadiriwa na kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi tu.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara inapoainisha makadirio na makusanyo ya mapato yake ijumuishe mapato yote

inayokadiria na kuyakusanya kutoka katika vyanzo vyake vyote na sio kuonesha baadhi na baadhi kuviacha.

## Taarifa za Matumizi

Taarifa za Matumizi za (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ni kama yanavyojionesha katika Majadweli la hapa chini:-

### 1.1. Matumizi ya Kawaida

| Na. | Maelezo | Makadirio | Halisi | % |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mishahara | 1,740,900,000 | 1,782,674,360 | 102 |
| 2. | Matumizi Mengineo OC | 11,025,800,000 | 3,567,382,639 | 35 |
| 3. | Ruzuku ya OC kwa Wakala wa Ulinzi JKU na Tume ya Utumishi Idara Maalum za SMZ | 1,288,700,000 | 242,701,000 | 19 |
| **Jumla** | | **14,055,400,000** | **5,592,757,999** | **42** |

### 1.2. Matumizi ya Fedha na Miradi ya Maendeleo

| Na. | Maelezo | Makadirio | Halisi | % |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mradi wa Ugatuzi wa Madaraka Serikali za Mitaa | 3,896,230,000 | 350,000,000 | 9 |
| | | (SMZ-1,000,000,000; Mhisani -2,896,230,000) | 0 | 0 |
| 2. | Mradi wa Kiwanda cha nguo cha Idara Maalum (ZQTL) | 2,500,000,000 | 974,291,288 | 39 |
| 3. | Mradi wa Mji Salama (CCTV) | 8,000,000,000 | 7,828,326,910 | 98 |
| **Jumla** | | **14,396,230,000** | **9,152,618,198** | **64** |

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati yetu haikupatiwa majibu ya Taarifa za Matumizi ila imebaini kwamba hoja ya Taarifa ya Matumizi inalingana na hoja ya Taarifa ya Mapato (kulikuwa na tofauti ya matumizi baina ya Mkaguzi na Wizara). Hivyo, Kamati yetu imeisisitiza Wizara inapoelezea kuhusu taarifa za matumizi zijumuishe matumizi yote ya Wizara na Taasisi zake zikiwemo matumizi ya fedha za Washirika wa Maendeleo ili taswira kamili ya fedha za Wizara ziweze kufahamika na kueleweka.

**Hoja nambari 6.3.1.1: Malipo nje ya Mapango wa Manunuzi shilingi 1,065,448,560.**

Kwa kuzingatia kifungu namba 42(1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "kitengo cha ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kitaandaa na kuwasilisha kwa mlipaji mkuu wa Serikali mpango wake wa mwaka wa ununuzi na uondoshaji kwa mwaka unaofata".

Kifungu namba 42(7) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "ununuzi hautofanyika kinyume na mpango wa manunuzi na uondoshaji wa mali za umma isipokuwa kwa hali ya haraka na dharura.

Ukaguzi umebaini kwamba kwa mwaka wa fedha unaoishishia Juni 30, 2021 Ofisi ya Raisi, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ilikadiria jumla ya shilingi 1,158,130,000 kupitia kasma ya "SECURITY SERVICES" yenye utambulisho wa nambari 2200112 na kufanya malipo yenye thamani ya shilingi 1,065,448,560 kwa kumlipa Umawa na Smart Secutities kwa ajili ya kupatiwa huduma ya ulinzi dosari iliyobainika ni kufanyika kwa malipo hayo nje ya mpango wa manunuzi.

Kufanya hivyo kunapelekea kuathiri matumizi yaliyopangwa kwa mujibu wa mapango wa manunuzi wa mwaka ambapo ni kwenda kinyume na vifungu vya sheria vilivyonakiliwa hapo juu.

**Majibu ya Wizara**

Kufuatia mabadiliko ya Sheria za Mamlaka za Serikali za Mitaa (ugatuzi) sekta ya Elimu ya Msingi na Maandalizi zilikua chini ya Serikali za Mitaa, hivyo bajeti zote zinazohusiana na elimu ya msingi na Maandalizi zilikuwa chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wizara ilikabidhiwa mkataba wa kampuni za ulinzi za Umawa na Smart Security, kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kama watoa huduma za ulinzi katika maskuli yote ya Msingi na Maandalizi. Tuliendelea kuwalipa kwa mujibu wa mkataba husika, watoa huduma za ulinzi hao. Wakati wa uandaaji wa mpango wa manunuzi haikuzingatiwa kuingizwa katika mpango wa manunuzi kwa vile mkataba wake unaendelea, iliwekewa bajeti tu kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hata hivyo, mwezi wa Julai, 2021/2022 sekta za ugatuzi zimerejeshwa kwenye Wizara husika ambazo ni Elimu, Afya na Kilimo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haikuridhishwa na majibu ya Wizara kwani Kamati yetu imebaini Mpango wa Manunuzi haukufanyiwa marekebisho pamoja na kwamba kulikuwa na Mkataba wa utoaji huduma za ulinzi ulikuwa ukiendelea.

Hali hiyo inaweza kutoa mwanya kwa Watendaji wasiokuwa na uadilifu na uaminifu kuweza kutumia fedha za Serikali vibaya. Lakushangaza Watendaji wa Wizara walilifanya hilo wakijua kwamba kabla ya matumizi yoyote kufanywa ni matakwa ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kuwepo kwa Mpango utakaokuwa ukiongoza jinsi gani matumizi ya Serikali yafanyike na sio kufanya matumizi kiholela.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe inapotekeleza shughuli zake ilizojipangia ni lazima kuwepo kwa Mpango wa Manunuzi ili kuondosha hoja kama za Mkaguzi kujitokeza.

**Hoja nambari 6.3.1.2: Kutorikodiwa kwa mafuta katika daftari la mafuta ghalani shilingi 150,758,377.00.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ imetumia jumla ya shilingi 150,758,377 kwa ununuzi wa mafuta kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za ofi si lakini mafuta hayo hayakurikodiwa katika daftari la kutunzia mafuta ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake.

Aidha Wizara imeshindwa kuwasilisha vitabu vilivyotumika katika mgao wa mafuta (issuer vocher) kwa ajili ya ukaguzi. Hali ambayo imepelekea wakaguzi kushindwa kujiridhisha na mtiririko mzima wa mgao wa mafuta ya ofisi hiyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 220(1) (2) cha kanuni za fedha za mwaka 2005.

**Jadweli Nambari 31: Kutorikodiwa kwa mafuta katika daftari la kutunzia mafuta ghalani**

| Hati Namba | Alielipwa | Thamani (Tshs) | Risiti/Ankara | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 12/8 ya 18/8/2020 | United Group Limited | 4,998,544 | Risiti namba 04971/Ankara namba 3073 | Malipo kwa ajili ya Ununuzi wa mafuta ya shughuli za Ofisi |
| 39/8 ya 25/8/2020 | Zanzibar Petroleum | 1,275,925 | Risiti namba 35687/Ankara namba 5891 | |
| 18/9 ya 3/9/2020 | Zanzibar Petroleum | 1,153,620 | Risiti namba 08463/Ankara namba 3215 | |
| 16/10 ya 20/10/2020 | | 2,499,154 | Risiti namba 06476/Ankara namba 3318 | |
| 18/10 ya 20/10/2020 | Gulioni Filling Station | 1,020,000 | Risiti 1336 | |
| 17/1 ya 13/1/2021 | United Group Limited | 2,999,928 | Risiti namba 327/Ankara namba 3459 | |
| 9/9 ya 3/9/2020 | | 787,500 | Risiti namba 08461/Ankara namba 3200 | |
| 10/9 ya 3/9/2020 | | 1,935,500 | Risiti namba 08462/Ankara namba 3199 | |
| 63/9 ya | Kijangwani | 11,200,000 | Risiti namba 0198/Ankara | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 22/9/2020 | Petrol Station | | namba 0901 | |
| 74/9 ya 23/9/2020 | United Group Limited | 1,919,414 | Risiti namba 08473/Ankara namba 3258 | |
| 16/10 ya 20/10/2020 | | 2,499,815 | Risiti 06476 Ankara namba 3318 | |
| 4/2 ya 4/2/2021 | | 2,712,407 | Risiti namba 938/Ankara namba 3491 | |
| 27/2 ya 22/2/2021 | | 7,905,762 | Risiti namba 1268 | |
| 61/2 ya 26/2/2021 | | 16,740,000 | - | |
| 5/8 ya 4/8/2020 | Kijangwani Petrol Station | 48,791,000 | Risiti namba 3421/Ankara namba 0287 | |
| 12/8 ya 18/8/2020 | United Group Limited | 4,999,808 | Risiti namba 04971/Ankara namba 3073 | |
| 49/8 ya 26/8/2020 | Kijangwani Petrol Station | 6,120,000 | Risiti3175/ Ankara namba 0160 | |
| 80/4 ya 28/4/2021 | | 1,200,000 | - | |
| 2/1 ya 6/1/2021 | Kijangwani Petrol Station | 30,000,000 | Risiti namba 0922/Ankara namba 0055 | |
| **Jumla** | | **150,758,377** | | |

**Majibu ya Wizara**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ilinunua mafuta kwa shughuli mbali mbali za Wizara yenye thamani ya shilingi 150,758,377.00 kama yalivyoainishwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2021. Aidha mafuta hayo yamerikodiwa kwa mujibu wa sheria na kanuni katika daftari la kurikodia bidhaa na kutolewa kwa mujibu wa taratibu. Kumbukumbu za mafuta hayo zipo kwa ajili ya kukaguliwa. Mchanganuo wa mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haikufurahishwa na utaratibu uliokuwa ukitumiwa na Wizara katika uhifadhi wa kumbukumbu zake kwani Kamati yetu imebaini kuwa Mkaguzi hakupatiwa vielelezo kwa vile Wizara ilikuwa imehama kutoka Vunga kwenda Chuo cha Mafunzo kwa muda. Hata hivyo, hiyo sio sababu ya kukosekana vielelezo iwapo kungekuwa na umakini katika uhifadhi wa vielelezo vya matumizi ya mafuta ya Wizara.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara iwe makini katika uhifadhi wa kumbukumbu zake hususan nyaraka zinazohusiana na matumizi ya mafuta kwani hizo ni fadha zinazotokana na jasho la wananchi.

## MRADI WA MJI SALAMA

**Hoja nambari 6.3.1.3: Mapungufu yaliyomo kwenye mkataba wa awamu ya pili wa Mradi wa Mji Salama**

Mradi wa Mji Salama ni moja wa mradi uliochini ya ofi si ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za mitaa na Idara Maalum za SMZ wenye dhima ya kulinda usalama wa mji wa Zanzibar. Mradi huu kwa Unguja upo Mkoa wa Mjini Magharibi na kwa Pemba unajumuisha Pemba nzima. Mradi huu upo kwenye awamu ya pili (phase 2) na unahusiana na miundo mbinu ya uwekaji wa kamera na kufanya matengenezo ya kamera hizo pale zinapokabiliwa na changamoto za aina mbalimbali. Mradi huu wa Zanzibar Salama kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021, ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,000,000,000.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 mradi ulitumia jumla ya shilingi 7,828,326,910, aidha malipo ya mradi huu hulipwa kutoka kwenye mradi wa miundo mbinu ulioko chini ya usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Hazina kwa kuingiza fedha moja kwa moja kwenye hesabu ya mtoa huduma aitwae “ROM Solution Ltd”. Aidha ukaguzi umebaini kuwepo wa dosari mbali mbali zinazotokana na mkataba, vifaa na utekelezajiwa mradi husika. Dosari zenyewe ni kama zifuatazo:

**(i) Mapungufu yaliomo kwenye Mkataba wa Phase II**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imeingia mkataba siku ya tarehe 4/12/2019 baina ya ROM Solution Ltd na ofi si hiyo kwa ajili ya uwekaji wa miundo mbinu ya kamera pamoja na kamera katika Mkoa wa Mjini Magharibi na Pemba kwa thamani ya USD 10,655,166 kwa muda wa miaka mitatu. Aidha ukaguzi umebaini kuwepo kwa “addendum” inayohuisiana na malipo iliyotiwa saini siku ya tarehe 1/7/2020 ambayo imeeleza kwamba malipo yote yatakuwa na thamani ya USD 3,701,148 sawa na asilimia 34.74.

Ukaguzi umebaini uwepo wa dosari zifuatazo zinazotokana na mkataba huo:-

- Kutofanyiwa matengenezo kwa mali za kudumu za Mradi wa Mji Salama.
- Uwepo wa pikipiki 20 zilizonunuliwa kwa ajili ya mradi huo, kati ya hizo pikipiki 14 zinaendelea kufanya kazi kama ilivyokusudiwa na zilizobaki 6 zimeharibika kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo.
- Uwepo wa gari 12 zilizokuwa zinatumika kwenye mradi ambazo zimeharibika bila ya kufanyiwa matengenezo na Mtoa huduma wa mradi yaani Rom Solution ltd na Ofi si ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 33(1) cha mkataba ulioainishwa hapo juu kinachoeleza kwamba "The supplier shall with no additional cost from the client make maintenance of the goods for the period of five years". Jadweli lifuatalo linaonyesha mchanganuo wa vyombo hivyo:-

**Jadweli Nambari 32: Dosari katika vyombo vya Moto**

| Aina ya Chombo | Nambari ya Chombo | Nambari ya Umiliki wa Chombo | Mtumiaji wa Chombo/Mahali Kilipo Chombo | Dosari na Chombo Husika |
|---|---|---|---|---|
| Honda – KTM | SMZ 1270 C | Z-047369542 | CCTV | Battery na fuel pump) |
| Honda – KTM | SMZ 1275 C | Z-047369641 | CCTV | (Battery na fuel pump) |
| Honda – KTM | S<br>SMZ 1273 C | Z-047369608 | CCTV | (Fuel pump na valve) |
| Honda – KTM | SMZ 1280 C | Z-047369740 | CCTV | (Battery na brake liver) |
| Honda – KTM | SMZ 1280 C | Z-047369784 | CCTV | (Fuel pump) |
| Honda – KTM | SMZ 1282 C | Z-047369828 | CCTV | (Battery na fuel pump) |
| Trailer ZBV inspection | SMZ 1283 C | Z-048353602 | CCTV-Bandarini | - |
| vehicle | SMZ 959 A | Z – 047008544 | AR-TMIM za SMZ | Nosel |
| Amaroc | SMZ 632 A | Z- 047008665 | AR-TMIM za SMZ | Clutch |
| Amaruc | SMZ 636 A | Z- 046730453 | KMKM | Nosel |
| Amaruc | SMZ 583 A | Z- 046730156 | KMKM | Nosel |
| Amaruc | SMZ 577 A | Z- 046730354 | Mafunzo | Clutch, gear box na bearing |
| Amaruc | SMZ 581 A | Z-046730398 | Mafunzo | Nosel na mipira |
| Amaruc | SMZ 582 A | Z- 046730134 | Mafunzo | Nosel |
| Amaruc | SMZ 576 A | Z-0467301910 | KZU | Nosel |
| Amaruc | SMZ 578 A | Z- 046730277 | KZU | Nosel |
| Amaruc | SMZ 579 A | Z- 047008588 | KVZ Kazi Maalum | - |
| Amaruc | SMZ 634 A | Z- 046729573 | KVZ | Nosel |

Ukaguzi unashauri uongozi wa ofisi uhakikishe kwamba vyombo vyote vinavyohitaji matengenezo vifanyiwe matengenezo ili viweze kusaidia katika kutekeleza majukumu yaliowekwa na mradi.

**Majibu ya Wizara**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, iliingia Mkataba na Kampuni ya ROM Solution LTD. kwa ajili ya kazi ya uwekaji wa miundombinu ya Kamera za kiulinzi (CCTV), Mkataba ambao ulifungwa tarehe 4 Disemba, 2019. Utekelezaji wa Mkataba huu ni wa muda wa miezi thelathini na sita (36) ambao unagharimu Dola za Kimarekani (USD$10,655,166).

Katika kutekeleza Mkataba huu ilifanyika nyongeza ya Mkataba (Addendum) inayohusu mabadiliko ya Jadweli la malipo yanayotokana na utekelezaji wa Mkataba wa awali wenye jumla ya thamani ya Dola za Kimarekani (US$10,655,166). Nyongeza ya Mkataba ilisainiwa tarehe 1 Julai, 2020 mabadiliko hayo ya Jadweli la malipo hayajaathiri bei ya mkataba wa awali bali yalihusu namna au mabadiliko ya malipo kwa mwezi ambapo awali mkandarasi alitakiwa kulipwa Dola 250,000 kwa miezi minne ya kwanza (Julai hadi Oktoba 2020) na badala yake kufuatia mabadiliko ya Jadweli la malipo alilipwa Dola 425,287 ambazo zilihamishwa kutoka mwezi Septemba hadi Disemba 2022 na badala yake kwa sasa miezi hii inalipwa Dola 250,000.

Hivyo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, haijafanya mkataba mwingine na Kampuni ya ROM Solution LTD. wa nyongeza kuhusiana na Dola za Kimarekani (US $ 3,701,148) sawa na asilimia 34.74 kama ilivyoainishwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka wa fedha 2020/2021.

Aidha, Ofisi ilifunga mkataba wa matengenezo (contract for services) na Kampuni ya ROM Solutions wenye thamani ya Dola za Kimarekani 443,550 USD. ambapo malipo yake yalilipwa kwa kila mwezi Dola za Kimarekani 36,962. Mkataba huu ulisainiwa tarehe 01/07/2020 na kuishia tarehe 30/06/2021. Matengenezo hayo yalihusu miundombinu ya mradi wa Mji Salama 'Phase I' ambapo mkataba wake uliisha tarehe 30/06/2020.

Matengenezo ya mali za kudumu za mradi yanaendelea kufanyika na kwasasa vyombo vya usafiri vimeshafanyiwa marekebisho na vinaendelea kufanyakazi za mradi kama ilivyokusudiwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilifuatilia kwa undani hoja hii na kubaini kwamba ni kweli wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Ofisi ya Tawala za Mikoa, vifaa vya Mradi wa Mji Salama vilikuwa havijafanyiwa matengenezo kwa wakati huo lakini hivi sasa tayari kasoro hiyo imesharekebishwa.

Utata ulijitokeza ni nani aliyekuwa na wajibu wa kufanya matengenezo hayo ambapo Mkaguzi alisema Wizara husika na Watendaji walieleza ROM Solution. Kutokana na utata uliojitokeza, Kamati yangu ililazimika kupitia Mkataba husika na kukutana na Kampuni ya ROM Solution, iliyoeleza kwamba jukumu lao la kuvifanyia matengenezo (service) vifaa vya Mradi lilimalizika katika awamu ya mwanzo (Juni, 2020 na sio kwenye

awamu ya pili ila bado Kampuni inaendelea kuisaidia Serikali.

Hata hivyo, wakati Kamati yetu inamaliza kutekeleza majukumu yake, tayari baadhi ya vifaa hivyo vilikuwa vimeshafanyiwa matengenezo hayo ikiwemo pikipiki.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Ni vyema kwa Wizara kuwa na mpango maalum ulioandaliwa wa kuvifanyiwa matengenezo vifaa vya mradi hasa ukizingatia vifaa hivyo vimetumia fedha nyingi za Serikali.

**(ii) Kutotumika na kutofanya kazi kwa baadhi ya vifaa vilivyomo kwenye mradi**

Ukaguzi ulifanya mahojiano na baadhi ya watendaji wanaohusiana na mradi wa CCTV kamera siku ya tarehe 20/10/2020 na kubaini kuwepo kwa baadhi ya vifaa ambavyo havijaanza kutumika katika mradi huo toka kupokelewa kwake. Kwa mfano ndege mbili zisizo na rubani (Drones) zinazotumika kwa ajili ya kupiga picha ambazo zimehifadhiwa kwenye maboksi badala ya kutumika kwenye shughuli mbalimbali za utekelezaji wa mradi.

Aidha ukaguzi umebaini uwepo wa gari aina ya trailer ZBV yenye namba SMZ 959 A iliyoletwa kwa ajili ya ukaguzi wa mizigo hapo bandarini ambayo toka kupokelewa kwake miaka miwili haijafanya kazi. Hii imetokana na kutofanya kazi kwa mtambo uliomo kwenye gari hilo, kwa sasa gari hii ipo Makao Makuu ya mradi hapo Maisara. Aidha ukaguzi umebaini kutofanya kazi kwa baadhi ya kamera zilizowekwa katika maeneo tofauti yaliomo kwenye mradi.

**Majibu ya Wizara**

Kwa vifaa ambavyo havijafanya kazi vya mradi wa Mji Salama (drone na gari la scanner) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ipo katika mazungumzo na kampuni ya ROM Solution juu ya kutokufanya kazi kwa vifaa hivyo ili waweze kurekebisha kasoro zilizojitokeza. Hata hivyo Mradi bado haujakabidhiwa kwa Wizara na Serikali kiujumla. Wizara itahakikisha vifaa vyote vinafanya kazi kabla ya kukabidhiwa mradi huo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kupitia hoja hii, Kamati yetu imebaini kwamba vifaa vya Mradi vikiwemo ‘drones’ na ‘scanner’ ni vizima na vinakuwa vinatumika pale inapohitajika kwa maslahi ya usalama wa nchi yetu.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe inaendelea kuvifanyia matengenezo 'service' vifaa vya mradi kwa wakati ili kuvifanya kufanyakazi kwa muda mrefu.

**FUNGU D 02 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU)**

**Taarifa ya Mapato**

Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 34,328,698,851 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 JKU ilikusanya jumla ya shilingi 31,228,409,512 sawa na asilimia 91 ya makadirio.

**Majibu ya JKU**

Kwa mwaka 2020/2021 JKU haikuvuka lengo la makusanyo kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo hali ya hewa namlipuko wa ugonjwa wa Corona. Ni jambo linalofahamika kuwa sehemu kubwa ya vyanzo vya mapato ya JKU yanategemea mvua za msimu ambazo mara nyingi hupekelea kukosekana kwa mavuno ya uhakika hasa mpunga. Lifuatalo ni jeduweli linaloonyesha makadirio na makusanyo pamoja na asilimia ya makusanyo kwa kila fungu.

**Mpango wa ukusanyaji mapato ya JKU kwa mwaka 20020/2021**

| Gfs code | Chanzo cha mapato | Makadirio ya mapato kwa 2020/2021 | Makusanyo halisi 2020/2021 | Asilimia ya makusanyo kwa mwaka |
|---|---|---|---|---|
| 1415004 | Kodi ya Maduka | 2,224,000 | 2,306,500 | 103 |
| 1415010 | Karafuu | 5,000,000 | 2,000,000 | 40 |
| 1421004 | Mapato ya Mpunga | 10,000,000 | 4,000,000 | 40 |
| 1421006 | Mapato ya mazao ya Bustani | 15,000,000 | 9,525,500 | 63.5 |
| 1422027 | Mazao ya Baharani | 2,000,000 | 0 | 0 |
| 1422052 | Mapato ya Viwanda Vidogo vidogo | 15,000,000 | 9,500,000 | 63.3 |
| 1422088 | Ada ya Mafunzo/Wanafunzi | 36,000,000 | 38,000,000 | 105.5 |
| 1421011 | Mapato ya mifugo | 2,000,000 | 2,100,000 | 105 |
| **Jumla** | | **87,224,000** | **66,632,000** | **76.4** |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa kuna tofauti ya makadirio ya mapato yalioainishwa na JKU na Mkaguzi. Hili limetokana na Mkaguzi kujumuisha fedha zote walizopatiwa JKU zikiwemo zilizotoka Serikalini na mapato yao ya ndani (Tzs. 34,328,698,851/-) wakati JKU imeonesha makadirio kama yalivyopitishwa na Baraza la Wawakilishi (Tzs. 66,632,000/-). Kamati ya PAC imeridhika na majibu na haikuwa na hoja zaidi.

**Taarifa ya Matumizi**

Jeshi la Kujenga Uchumi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 34,328,098,851 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 31,228,409,512 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 91 ya makadirio.

**Majibu ya JKU**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 JKU iliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi Tzs. 27,057,600,000.00 kati ya fedha hizo Tzs. 24,066,000,000.00 kwa mshahara na Tzs. 2,991,600,000.00kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Juni, 2021 JKU ilishaingiziwa na kutumia jumla ya Shilingi Tzs. 28,290,226,845.00, kati ya fedha hizo Tzs. 26,518,520,845.00 kwa ajili ya mshahara ambayo ni sawa na asilimia mia moja na kumi (110%) ambapo ongezeko hili limetokana na nyongeza ya pungufu ya mshahara iliyojitokeza kwenye bajeti na Tzs. 1,771,706,000.00 kwa ajili ya kazi za kawaida (OC) ambayo ni sawa na asilimia hamsini na tisa.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 JKU iliidhinishiwa kutumia jumla ya Tzs. 4,500,000,000.00 kwa kazi za maenedeleo. Hadi kufikia mwezi Juni, JKU imeshaingiziwa jumla ya Tzs. 2,871,550,667.00 kwa miradi ya Skuli ya Ufundi JKU Mtoni na Ujenzi wa mahanga na nyumba za askari Msaani Pemba ambayo ni sawa na asilimia sitini na nne (64%) ya makadirio. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kuchimba na kujenga mashimo ya maji machafu, kukamilisha mfumo wa umeme, kukamilisha kazi za rangi, kutia tarazzo ya chini katika mahanga na bwalo la chakula, kufunga milango na madirisha pamoja na vyuma vya kingo za varanda na njia, kutia visaruji (interlocks) katika eneo la nje linalozunguka majengo hayo unaendelea kwa hatua ya kazi za umaliziaji.

**Jedweli la makadirio na matumizi halisi ya mshahara, matumizi mengineyo (OC) na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021**

| Nam. | Maelezo | Makadirio | Matumizi halisi |
|---|---|---|---|
| 1 | Mishahara | 24,066,000,000 | 26,518,520,845 |
| 2 | Matumizi mengineyo | 2,991,600,000 | 1,771,706,000 |
| 3 | Maendeleo | 4,500,000,000 | 2,871,550,667 |
| **Jumla** | | **27,057,600,000** | **28,290,226,845** |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa kuna ongezeko la fedha za matumizi Tzs. 2,683,274,851 lililosababishwa na ongezeko la Mshahara linalotokana na upandishwaji wa vyeo vya Maaskari. Kamati ilitaka kujua kama fedha hizo ziliombwa kwa mujibu wa utaratibu na kuelezwa kwamba Jeshi liliandika barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango tarehe 12 Aprili, 2021 yenye kumbukumbu nambari MMJKU/U.10/2/13/JD15/61. Kamati baada ya kuipitia iliridhika na idhini iliyotolewa ya kutumia fedha iliyotajwa hapo juu.

**Hoja nambari 6.3.2.1: Hati za malipo zilizokosekana kwa Ukaguzi shilingi 647,863,625**

Ukaguzi umepitia taarifa ya utoaji wa fedha kwa njia ya IFMS (Exchequer releases) na kubaini jumla ya shilingi 1,329,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Hanga mbili na Bwalo moja la Askari Msaani Pemba (JKU) .

Aidha, ukaguzi umepitia hati za malipo yenye jumla ya shilingi 681,136,375 na kubaini amelipwa Mzabuni SABAH STORE kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Hanga Msaani Pemba. Aidha, hati za malipo pamoja na vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa malipo yenye thamani ya shilingi 647,863,625 hazikupatikana kwa ukaguzi.

Kutokupatikana kwa ukaguzi kwa hati za malipo pamoja na vielelezo vinavyothibitisha malipo hayo kunapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma jambo ambalo linaweza kupelekea kuisababishia hasara Serikali.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 pamoja na kanuni na kanuni namba 95(4) ya mwaka 2005.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha hati za malipo zinapatikana pamoja na vielelezo vyake kwa ukaguzi ili kuthibitisha uhalali wa malipo husika. Hati za malipo zilikosekana ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 33: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi**

<table>
<tr><th>Hati namba</th><th>Aliyelipwa</th><th>Kiasi (Tshs)</th><th>Maelezo</th></tr>
<tr><td>Pv namba 5/5/2021</td><td rowspan="4">Sabah Store</td><td>204,814,500</td><td rowspan="4">Malipo kwa ajili ya gharama za vifaa vya ujenziKambi ya Jku Msaani</td></tr>
<tr><td>Pv namba 18/6/2021</td><td>299,940,375</td></tr>
<tr><td>Trh 17/6/2021</td><td>96,040,000</td></tr>
<tr><td>Trh 17/6/2021</td><td>49,100,000</td></tr>
</table>

| | | | |
|---|---|---|---|
| Trh 17/6/2021 | | 31,241,500 | |
| **Jumla** | | **681,136,375** | |

### Majibu ya JKU

Hati za malipo zilizoainishwa kwenye kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa hazikuonekana zipo na zimeambatanishwa katika ripoti hii.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati yetu ilibaini kwamba majibu yaliyotolewa yanatofautiana na majibu yaliyojibiwa awali na JKU kupitia 'management letter' yao ya tarehe 1 Aprili, 2021 inayoeleza kwamba Nanukuu 'Taasisi haina maelezo kuhusu suala hili ila jitihada za kupata taarifa za kina zinaendelea kuchukuliwa'.

Kamati baada ya kudadisi kwa ndani iligundua kwamba kipindi hicho kilikuwa ni Wakuu wengi wa JKU walikuwa na madai ya ubadhirifu wa fedha na ZAECA katika kutafuta ukweli ilivichukua vielelezo hivyo. Hivyo wakati Mkaguzi anafika JKU vielelezo hakupatiwa lakini Kamati imebahati kuviona, kuvikagua na kuvikubali. Miongoni mwa vielelezo ambavyo Kamati imeweza kuviona ni vocha ya malipo ya tarehe 5/5/2021 inayohusiana na malipo ya gharama za vifaa vya ujenzi wa kambi ya JKU Msaani. Vile vile kulikuwa na vocha ya tarehe 17/6/2021 inayohusiana na malipo ya ujenzi wa Mahanga ya Vijana wa JKU - Msaani.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Makamanda wa JKU wawe wepesi kutoa mashirikiano ya karibu anapofika Mkaguzi kutekeleza majukumu yake ikiwemo kumpatia majibu yaliyokuwa sahihi pamoja na nyaraka anazohitaji.
2. Jeshi la Kujenga Uchumi liwe na utaratibu mzuri wa kuhifadhi nyaraka zake ili ikihitajika iweze kupatikana kwa urahisi nyaraka hiyo ikiwemo kuzitoa nakala vielelezo hivyo ili 'nyaraka halisi ikichukuliwa nakala itakuwepo.

### Hoja nambari 6.3.2.2: Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi shilingi 61,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya malipo ya shilingi 61,000,000 kwa ndugu RASHID MOHAMMED SOUD kwa ajili ya ununuzi wa gari mbili (2) aina ya PRADO kwa mujibu wa ankara namba 128 ya mwezi wa Disemba 2020. Katika ufuatiliaji wa ukaguzi wa ndugu Rashid Mohamed Soud imebainika amejisajili kutoa huduma za uuzaji wa Vipuri (Spare Parts) na sio uuzaji wa magari kama ilivyonunuliwa na Jeshi la Kujenga Uchumi.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa gari hizo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Hata hivyo ukaguzi umebaini Jeshi la Kujenga Uchumi limekiuka muongozo wa Baraza la Mapinduzi wenye kumbukumbu namba BLM/97/M/C.5/VOL.V/27 wa tarehe 27 Septemba 2021 kutoka Serikalini uliotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kuwaagiza Wakuu wote wa Taasisi kuwasilisha maombi ya ununuzi wa gari kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na kuacha kununua magari yaliyotumika (Used Car) pamoja na kuacha kununua magari kwa wazabuni binafsi kwa lengo la kununua gari kwa thamani kubwa kuliko bei ya sokoni ambapo Jeshi la Kujenga Uchumi limenunua gari mbili zilizotumika (Used Car) bila ya kupata ridhaa ya kibali kutoka kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, hata hivyo ukaguzi haukuweza kupatiwa ripoti ya ukaguzi wa gari hizo (Inspection Report) kutoka kwa fundi mkuu wa Karakana ya Serikali kwa vile gari hizo hazikufanyiwa uchunguzi wa kina kujua umadhubuti na uzima wa gari hizo, ukaguzi haukuweza kupatiwa hatiya mapokezi ya gari hizo (Delivery Note).

Kufanya manunuzi kinyume na matoleo ya Serikali kunapelekea taasisi ya umma kutumia gharama kubwa ya ununuzi unaotokana na wazabuni kuwauzia Serikali magari kwa gharama kubwa ukilinganisha na bei ya soko ilivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ili kuepusha kutumia fedha za umma kinyume na utaratibu.

**Majibu ya JKU**

JKU ililazimika kukununua magari haya katika kipindi cha mwezi Septemba 2020 ili kuweza kukabiliana na shughuli mbali mbali za Kitaifa. Ikumbukwe ya kwamba kwa kipindi hicho nchi yetu ilikua inakabiliwa na uchaguzi mkuu ambapo JKU ilipangiwa majukumu mbali mbali ambayo kwa aina ya gari zilizokuwepo isingewezekana kuyatimiza.

**Uchunguzi wa kamati ya PAC**

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati ya PAC iligundua kwamba mwaka 2020/2021, ulikuwa ni mwaka wa harakati za uchaguzi. Hivyo, gari zilizonunuliwa zilikuwa kwa lengo la kutekeleza agizo la kitaifa kwa maslahi ya Taifa letu hususan kusimamia uslama wa watu na mali zao. Hata hivyo, Kamati yetu ilihoji kuhusiana na gari hizo na kuelezwa zilikuwa mbili (2) ambazo zilinunuliwa kwa shilingi 61,000,000 ambapo moja tayari imeshalipwa lakini moja gari ya pili bado haijalipwa kwa vile madeni yote ya Serikali kwa

kipindi hicho yaliwaslishwa hazina. Kamati baada ya kupata majibu hayo haikuwa na hoja zaidi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ya Fedha na Mipango kwa vile tayari gari moja imeshalipwa, ni busara deni la gari moja iliyobakia (Tzs. 31,000,000) zilipwe ili Mfanya biashara huyo aache kufika Ofisini kudai malipo yake.

**Hoja nambari 6.3.2.3: Kukosekana kwa uhalali wa Deni la ununuzi wa Gari lenye jumla ya shilingi 31,000,000**

Ukaguzi umepitia taarifa mbalimbali za Jeshi la kujenga uchumi pamoja na baadhi ya taarifa za manunuzi na kubaini kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya manunuzi wa Gari aina ya Toyota Prado yenye chassis nambari TRT 120-5022-585 yenye usajili wa Z 128 HK iliyonunuliwa kutoka kwa Nd. Rashid Mohammed Soud, kupitia Ankara nambari 128 ya tarehe 21/12/2020 yenye thamani ya shilingi 31,000,000. Ukaguzi umebaini kuwa fedha hizo hazijalipwa hadi kumalizika kwa Ukaguzi. Ithibati za vielelezo vya kuthibitisha deni haikupatikana kwa ukaguzi miongoni mwao ni kama hizi zifuatazo:-

- Kukosekana kwa Kibali cha ruhusa ya ununuzi wa gari Used kutoka kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.
- Kukosekana kwa kumbukumbu za bodi ya manunuzi za ufunguzi wa document za Wazabuni.
- Kutotangazwa kwa zabuni ya Ununuzi wa Gari.
- Kukosekana kwa Zuio la kodi (VAT NA ZRB).
- Kukosekana kwa ripoti ya tathmini (Evaluation report).
- Kukosekana kwa fomu za viapo za wajumbe wa tathmini (Code of Ethics).
- Kukosekana kwa mkataba wa makubaliano ya mauziano ya gari 2 baina ya Rashid Mohammed Soud na Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar nk.

Kufanya manunuzi kinyume na matoleo ya Serikali kunapelekea taasisi ya umma kutumia gharama kubwa ya ununuzi unaotokana na wazabuni kuwauzia Serikali magari kwa gharama kubwa ukilinganisha na bei ya soko ilivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ili kuepusha kutumia fedha za umma kinyume na utaratibu.

**Majibu ya Wizara, Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa majibu ya Wizara, uchunguzi na mapendekezo ya hoja hii

yanafanana na majibu ya Wizara, uchunguzi na mapendekezo ya Hoja nambari 6.3.2.2.

**Hoja nambari 6.3.2.4: Tofauti ya matumizi ya fedha baina ya Exchequer na Hati za Malipo shilingi 506,551,018**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kujitokeza kwa tofauti ya malipo baina ya hati za malipo na fedha iliyoingizwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Kwa mujibu wa fedha iliyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina (Exchequer Release) ilikuwa na thamani ya shilingi 2,871,550,667 ambapo JKU lilitumika jumla ya shilingi 2,364,999,649 kwa ajili ya kumlipa mzabuni Sabah Store kwa ajili ya kutoa huduma mbali mbali katika Jeshi la Kujenga Uchumi.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa taarifa za tofauti ya matumizi ya shilingi 506,551,018 zilizobainika pamoja na vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa uwepo wa matumzi hayo jambo ambalo limepelelekea kuashiria upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unasimamia miongozo na sheria za usimamizi wa fedha ili kuepuka kujitokeza kwa vitendo vya uhujumu wa uchumi.

**Majibu ya JKU**

Kwa mujibu wa Exchaquer release, JKU imeingiziwa TZS 2,871,550,667 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi TZS 1,329,000,000 zililipwa k-patika Account ya JKU kupitia mfumo wa Wizara ya Fedha na TZS 1,542,550,667 zimesomeka kama dami kupitia mfumpo [wa malipo wa Wiozara ya Fedha Zanzibar na kulipwa Mzabuni moja kwa moja. Vielelezo vya matumizi ya TZS 1,329,000,000 vipo na vimeambatanishwa katika taarifa hii. Aidha ushahidi wa malipo ya dami ya TZS 1,542,550,667 yaliyolipwa moja kwa moja kwa mzabuni na Wizara ya Fedha yameambatanishwa katika ripoti hii. Hivyo, madai ya tofauti ya matumizi ya fedha baina ya Exchequer na Hati za Malipo shilingi 506,551,018 hayapo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imegundua kwamba fedha zilizoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti (Tzs. 506,551,018) zililipwa kwa njia ya Dammy kupitia barua ya tarehe 30/6/2021 yenye kumbukumbu nambari DC.184/199/01/04/58. Kamati yetu ilibahatika kuiona barua hiyo na kuzipitia vocha kadhaa za malipo hayo na kuridhika navyo. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilibaini kwamba malipo hayo yalifanyika pasi na JKU kufuatilia vielelezo vyao Wizara ya Fedha na Mipango wakati aina hiyo ya malipo huathiri bajeti yao.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

JKU inapofanya malipo kwa njia ya Dummy, ihakikishe inafuatilia vielelezo vinavyohalalisha matumizi ya fedha hizo Wizara ya Fedha na Mipango.

**Hoja nambari 6.3.2.5: Kukiukwa kwa taratibu za manunuzi kwa ununuzi wa chakula cha askari wanaopangiwa lindo yenye thamani ya shilingi 1,613,055,435**

Ukaguzi umebaini kuwa Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya ununuzi wa chakula kwa ajili ya huduma kwa askari wanaopangiwa kutoa huduma ya kulinda katika vituo vyao vya malindo kupitia mtoa huduma SH TRADER AND FURMIGATION na YESS BOSS SHOP. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa utoaji wa huduma na mzabuni huyo ambapo kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Aidha, katika ufuatiliaji wa mapokezi ya vyakula vilivyonunuliwa ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa mapokezi ya vyakula hivyo kutokana na kukosekana kwa ukaguzi hati inayothibitisha mapokezi ya chakula hicho (delivery note). Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kupatiwa taratibu walizokubaliana na mzabuni huyo katika ulipwaji wa fedha zinazotumika katika ununuzi wa chakula hicho (Mode of payment) jambo ambalo limetia shaka juu ya matumizi ya fedha za umma na kupelekea uwepo wa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi JKU kuhakikisha unatekeleza matakwa ya kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 34: Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi**

| Hati yaMalipo | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 45/6/2021 | T.T | 75,130,435 | YESS BOSS | alipo ya Chakula cha watumishiwa Jeshi la Kujenga Uchumi |
| 35/3/2021 | T.T | 82,080,000 | | |
| 1/11/2020 | T.T | 74,788,750 | H Trader and Furmigation | |
| 27/12/2020 | T.T | 74,788,750 | | |
| 24/10/2020 | T.T | 74,788,750 | | |
| 13/8/2020 | T.T | 74,788,750 | | |
| 1/7/2020 | T.T | 74,788,750 | | |
| 1/9/2020 | T.T | 74,788,750 | | |
| 17/6/2021 | TT | 120,753,300 | Yess Boss Shop | |
| 21/5/2021 | TT | 120,753,300 | | |
| 38/4/2021 | T.T | 120,753,300 | | |
| 33/3/2021 | TISS | 120,753,300 | | |
| 6/3/2021 | TISS | 120,753,300 | | |
| 27/7/2020 | TISS | 24,660,000 | Juma Mohd Pweka | |
| 26/7/2020 | TISS | 62,113,200 | Sabaha Store | |
| 26/11/2020 | TISS | 34,060,000 | Juma Mohd Pweka | |
| 25/11/2020 | TISS | 62,113,200 | Sabaha Store | |
| 24/9/2020 | TISS | 62,113,200 | | |
| 25/12/2020 | TISS | 96,173,200 | Juma mohd pweka | |
| 20/10/2020 | TISS | 62,113,200 | Sabah Store | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jumla | 1,613,055,435 | | |

**Majibu ya JKU**

Vocha za malipona delivery note za malipo ya TZS 1,613,055,435 kwa ununuzi wa chakula cha askari wanaopangiwa lindo pamoja na barua inayothibitisha ruhusa ya manunuzi ya chakula kwa njia ya single sourcezimeambatanishwa katika taarifa hii.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilipofuatilia hoja hii imegundua kwamba katka ufanyaji wa zabuni, JKU kweli hawakufuata taratibu zake. Hilo lilisababishwa na kutumia njia ya ununuzi wa kwenda kununua moja kwa moja kwa Mfanyabiashara maalum (Direct Procurement Method). Kuthibitisha hilo, Kamati ya PAC imebahatika kuiona barua hiyo iliyotoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya tarehe 17/3/2021 yenye kumbukumbu nambari MUUMU.BA.370/383/04/18.

Sambamba na hilo, Kamati yetu imebaini kwamba JKU ilionekana imetumia zaidi ya Kampuni moja kwa wakati huo kutokana na huduma zilizokuwa zikitolewa na Kampuni husika hazikuwa za kuridhisha na ndipo wakaja na maamuzi ya kuvunja nao Mkataba mpaka walipompata Mtoa Huduma walieridhika nae.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

JKU inapotaka kupata Mtoa Huduma katika eneo lililokuwa nyeti (Sensitive area) iiandikie Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ili wapate ridhaa yao kwa vile Sheria ya Ununuzi inaruhusu kufanya hivyo.

**Hoja nambari 6.3.2.6: Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi kwa ujenzi wa Mahanga shilingi 681,136,375**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya malipo kwa msambazaji SABAH STORE yenye thamani ya shilingi 681,136,375 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Mahanga mawili ya Askari na Bwalo Moja - Msaani Pemba.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi, kukosekana kwa makisio ya ujenzi (B.O.Q), kukosekana kwa taarifa za vikao (minutes),kukosekana kwa ripoti ya tathmini, kukosekana kwa taratibu za malipo (TOR) zinazoonesha namna za ulipwaji wa malipo hayo (Mode of Payment).

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unatekeleza

miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufanya malipo kwa mujibu wa mpango wa manunuzi ili kuepusha kutumia fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Ujenzi wa Mahanga na Bwalo - Msaani Pemba) kinyume na utaratibu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 35 : Kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi**

| Hati namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Kiasi (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Pvnamba5/5/2021 | T.T | Sabah Store | 204,814,500 | Malipo kwa ajili ya gharama za vifaa vya ujenzi Kambi ya Jku Msaani |
| Pv namba 18/6/2021 | T.T | | 299,940,375 | |
| Trh 17/6/2021 | T.T | | 96,040,000 | |
| Trh 17/6/2021 | T.T | | 49,100,000 | |
| Trh 17/6/2021 | T.T | | 31,241,500 | |
| **Jumla** | | | **681,136,375** | |

**Majibu ya JKU**

Katika ripoti ya CAG imeeleza ukiukwaji wa taratibu za manunuzi ikiwemo kutokuitishwa kwa zabuni na kutokuwepo kwa mkataba. Kumbukumbu zinaonesha JKU iliitisha zabuni na baada ya mchakato huo kuisha ilifunga mkataba na kampuni ya Sabah Store wenye thamani ya TZS 1,791,844,467 kwa usambazaji wa vifaa vya ujenzi. Mkataba na barua ya kukubalika kwa zabuni hii zimeambatanishwa katika taarifa hii.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati yetu ilipofuatilia hoja hii, ilibaini kwamba nyaraka zilizohitajika zilikuwepo isipokuwa zilikuwa zimechukuliwa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) kufuatia tuhuma za uhujumu wa uchumi na ubadhirifu wa mali ya umma uliokuwa ukiwakabili baadhi ya Makamanda wa JKU. Kwa bahati nzuri, Kamati yetu ilibahatika kupatiwa vielelezo hivyo na kukubaliana navyo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

JKU ihakikishe inakuwa na utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu zake ikiwemo kutoa nakala kutoka kwenye kila nyaraka halisi (original) ili muda wowote zitakapohitajika ziweze kupatikana bila ya usumbufu wowote.

**Hoja nambari 6.3.2.7: Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi kwa ujenzi wa Skuli ya Ufundi JKU Mtoni shilingi 1,683,863,274**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya malipo kwa msambazaji SABAH STORE yenye thamani ya shilingi 1,683,863,274 kwa ajili ya ununuzi

wa vifaa vya ujenzi wa Skuli ya Ufundi JKU Mtoni.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi, kukosekana kwa makisio ya ujenzi (B.O.Q), kukosekana kwa taarifa za vikao (minutes), kukosekana kwa ripoti ya tathmini, kukosekana kwa taratibu za malipo (TOR) zinazoonesha namna za ulipwaji wa malipo hayo (Mode of Payment), kukosekana kwa nyaraka za mzabuni (Tender Document), kukosekana kwa ripoti ya Upembuzi yakinifu (Feasibility Study Report) pamoja na kukosekana kwa cheti cha Mshauri Elekezi (Consultance Certificate) kabla ya malipo.

Aidha ukaguzi haukuweza kuthibitisha mapokezi ya vifaa hivyo kutokana na kutokupatikana kwa daftari la kupokelea mali ghalani (Site Ledger Visit) pamoja na hati ya kupokelea vifaa (Delivery Note).

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufanya malipo kwa mujibu wa mpango wa manunuzi ili kuepusha kutumia fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Ujenzi wa Skuli ya Ufundi JKU Mtoni) kinyume na utaratibu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 36: Kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi**

| Hati ya malipo | Hundinamba | Thamani (shs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| --ya tarehe 28/8/2020 | TISS | 232,791,165 | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa skuli ya Ufund Jku Mtoni, pamoja na vifaa vya Funiture Res House Gombani Pemba. |
| 2/4/2021 ya 30/3/2021 | TISS | 414,829,036 | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa shule na Jku Mtoni |
| --ya 13/4/2021 | TISS | 508,907,630 | |
| 5/7/2020 ya 9/7/2020 | TISS | 527,335,443 | |
| **Jumla** | | **1,683,863,274** | |

### Majibu ya JKU

Katika ripoti ya CAG imeeleza ukiukwaji wa taratibu za manunuzi ikiwemo kutokuitishwa kwa zabuni na kutokuwepo kwa mkataba. Kumbukumbu zinaonesha JKU iliitisha zabuni na baada ya mchakato huo kumalizika ilifunga mkataba na kampuni ya Sabah Store wenye thamani ya TZS 2,500,000,000 kwa usambazaji wa vifaa vya ujenzi. Mkataba huu

umeambatanishwa katika taarifa hii.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

1. Katika uchunguzi wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa Mkataba ulikuwepo wa tarehe 1/7/2020 baina ya Sabah Store na Jeshi la Kujenga Uchumi. Hata hivyo, Kamati yetu ilitaka kujua kwanini alipopita Mkaguzi hakupatiwa Mkataba huo na kuelezwa kwamba hilo lilitokana na kutowepo kwa nyaraka hiyo kulikosababishwa na kuchukuliwa na ZAECA.
2. Kamati yatu imebaini kuwa jengo hilo limejengwa kwa fedha zao wenyewe na haikutumia fedha za mradi wa maendeleo ambapo Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) walilikagua na kuridhika na ujenzi uliofanyika. Kaamti yetu imefarijika kuone ushauri wake uliotoa katika ukaguzi wa mwaka 2019/2020 umetekelezwa kwa vitendo ambapo jengo hilo limekemilika na linaendelea kutumika.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

JKU ihakikishe inatoa ushirikiano wa karibu kwa Mkaguzi hususan anapokuja kufanya ukaguzi katika maeneo yao ili aweze kupata majibu yanayomtosheleza.

**Hoja nambari 6.3.2.8: Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi ya vifaa vya ujenzi shilingi 221,492,500**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya malipo yenye thamani ya shilingi 221,492,500 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi pamoja na samani za nyumba ya Rest House Gombani.

Katika malipo hayo jumla ya shilingi 98,730,000 zililipwa kwa msambazaji RASHID MOHAMMED SOUD kwa ajili ya ununuzi wa samani kwa ajili ya nyumba ya Rest House Gombani Pemba na jumla ya shilingi 122,762,500 zililipwa kwa msambazaji SABAH STORE kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa samani na vifaa vya ujenzi, kukosekana kwa makisio ya ujenzi (B.O.Q), kukosekana kwa taarifa za vikao (minutes),kukosekana kwa ripoti ya tathmini, kukosekana kwa taratibu za malipo (TOR) zinazoonesha namna za ulipwaji wa malipo hayo (Mode of Payment), kukosekana kwa nyaraka za mzabuni (Tender Document), kukosekana kwa ripoti ya Upembuzi yakinifu (Feasibility Study Report) pamoja na kukosekana kwa cheti cha Mshauri Elekezi (Consultance Certificate) kabla ya malipo.

Aidha tarehe 17/01/2022 ukaguzi ulitembelea jengo hilo la Rest House Gombani Pemba kwa lengo la kufanya uhakiki juu ya uwepo wa vifaa hivyo na kubaini kwamba hakuna kumbukumbu yoyote inayoonesha mapokezi ya vifaa hivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya

Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufanya malipo kwa mujibu wa mpango wa manunuzi ili kuepusha kutumia fedha kinyume na utaratibu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 37: Kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi**

| Hati namba | Ankara namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fed- ha kilicholipwa(shs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| –ya tarehe 28/8/2020 | 0276 ya 24/7/2020, 0285 ya tarehe 12/6/2020, 0277 ya tarehe 27/7/2020, 0278 ya 25/7/2020, 0279 ya 23/7/2020, 0286 ya tarehe 12/6/2020. | Rashid Mohammed Soud | 98,730,000 | Ununuzi wa vifaa vya Rest house Gombani Pemba |
| –-ya 28/8/2020 | 0438 ya 10/8/2020 0439 ya 10/8/2020 | Sabah Store | 122,762,500 | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi. |
| **Jumla** | | | **221,492,500** | |

**Majibu ya JKU**

Ujenzi huu ulikua unajengwa kwa fedha za OC. Hivyo, malipo yake yalilipwa kidogo kidogo kuanzia mwaka 2018. Hadi sasa bado JKU inadaiwa na mzabuni wa usambazaji wa vifaa. Katika ujenzi huu JKU ilitumia Single source ili jengo liweze kutumiwa na wapiganaji kwa uharaka. Mkataba huu wa ujenzi wa Rest House Gombani umeambatanishwa katika taarifa hii.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika uchunguzi wa hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa jengo hilo limejengwa kwa kutumia fedha za OC na taratibu za ujenzi zilifuatwa ambapo vielelezo vilikuwepo na vimepitiwa na Kamati na kuridhika navyo kwasababu alipopita Mkaguzi vielelezo hivyo vilikuwa vimechukuliwa na ZAECA.

**Hoja nambari 6.3.2.9: Kutokuwasilishwa kwa baadhi ya vifaa vyenye thamani ya shilingi 62,630,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Jeshi la kujenga Uchumi Zanzibar limefanya malipo yenye thamani ya shilingi 243,617,500 tarehe 28/08/2020 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vilivyokusudiwa kutumika katika jengo la Rest House Gombani kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ukaguzi umepitia hati za malipo hayo sambamba na

Ankara husika pamoja na kufanya uhakiki wa uhalisia juu ya uwepo wa vifaa hiyo, na kubaini kwamba hadi kufikia tarehe 19/01/2022 wakati wa kufanyika ukaguzi wa mwisho na kubaini baadhi ya vifaa vyenye thamani ya shilingi 62,630,000 havikuwasilishwa kabisa katika jengo hilo kwa ajili ya matumizi husika licha ya kufanyika kwa malipo ya ununuzi wa vifaa hivyo.

Aidha hakuna taarifa yeyote iliyoripotiwa na JKU kutokana na kutowasilishwa kwa vifaa hivyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni ya 190 na 193 ya sheria namba 12 usimamizi wa fedha za umma ya 2005.

Ukaguzi unashauri uongozi wa JKU kuhakikisha kwamba unasimamia vizuri utekelezaji wa Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 38: Gharama za Vifaa ambavyo vimenunuliwa na havikuwasilishwa kwa ujenzi**

| Nambari ya Ankara | Msambazaji | Vifaa husika | Idadi ya Ankara | Idadi iliyopo | Thamani ya vifaa visivyo wasilishwa (shs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 0278 ya 25/7/2020 | Rashid Mohammed Soud | Fire Extinguisher | Seti 3 | 0 | 2,550,000.00 |
| | | Vitasa vya Mlango Mkubwa | 2 | 0 | 360,000.00 |
| 0279 ya 23/7/2020t | | Air Condition 1.5tone | 12 | 0 | 19,200,000.00 |
| | | Air Condition 2 tone | 3 | 0 | 5,400,000.00 |
| | | Heater | 11 | 9 | 900,000.00 |
| | | CCTV Camera | Seti 3 | 0 | 3,600,000.00 |
| | | TV inch 32 | 13 | 0 | 6,500,000.00 |
| | | TV inch 48 | 2 | 0 | 2,600,000.00 |
| 0286 ya 12/6/2020 | | Water Pump 1.5 | 1 | 0 | 1,200,000.00 |
| 0438 of 10/8/2020 | Sabah Store General traders | Book shelf 5 door | 1 set | 0 | 4,000,000.00 |
| | | TV inch 32 | 1 | 0 | 600,000.00 |
| | | Shoes cabin | 1 | 0 | 500,000.00 |
| | | Excutive chair | 1 | 0 | 1,500,000.00 |
| | | Excutive table | 1 | 0 | 3,200,000.00 |
| 0439 of 10/8/2020 | | Conference chairs | 50 | 41 | 3,420,000.00 |
| | | Reception Table | 2 | 0 | 3,000,000.00 |
| | | TV inch 52 | 1 | 0 | 2,500,000.00 |
| | | TV inch 32 | 8 | 6 | 1,200,000.00 |
| | | TV inch 21 | 1 | 0 | 400,000.00 |
| | | **Jumla** | | | **62,630,000** |

**Majibu ya JKU**

Ripoti ya CAG inaeleza ya kwamba kuna vifaa havikuwasilishwa na mzabuni katika ujenzi wa Rest House Gombani. Kumbukumbu ya Delivery note inaonesha vifaa hivyo vimepokelewa. Hadi sasa vifaa hivyo vimeshawekwa kwenye nyumba na vinatumika. Nakala ya Delivery note ya vifaa hivyo imeambatanishwa katika ripoti hii.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati yetu imegundua ni kweli kulikuwa na tofauti ya fedha za matumizi halisi ukilinganisha na fedha zilizoainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka (Financial Statement). Kamati yetu ilielezwa kwamba hilo lilisababishwa na uhaulishaji uliofanywa na JKU katika baadhi ya vifungu.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

JKU ifuate nidhamu ya matumizi ya fedha za umma ili kuepuka kujitokeza tofauti ya fedha jambo ambalo kupelekea kutokuwepo taswira nzuri na halisi.

**Hoja nambari 6.3.2.10: Tofauti ya taarifa ya fedha zilizoripotiwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka na matumizi halisi shilingi 733,564,213**

Katika kupitia taarifa mbali mbali zikiwemo taarifa za Hesabu ya mwaka, daftari la kurikodia kumbukumbu za fedha pamoja na taarifa za matumizi (hati za malipo). Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya vifungu vilivyoripotiwa katika taarifa ya Hesabu ya Mwaka vinatofautiana na taarifa za hati za malipo.

Kuwepo kwa tofauti hiyo, kunapelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha usahihi wa taarifa zilizoripotiwa katika ripoti ya fedha ya mwaka. Hali hiyo inapelekea taarifa ya hesabu kutotoa sura (Taswira) halisi na sahihi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha kwamba wanazifanyia marekebisho taarifa zenye tofauti katika ripoti ya fedha ya mwaka ili kupata ripoti yenye kuakisi uhalisia na iliyosahihi.

**Jadweli Nambari 39: Tofauti za taarifa za Fedha.**

| Kifungu | Makario(Tshs) | Taarifa ya fedha upitia hati za malipo (Tshs) | Thamani iliyoripotiwa katika taarifa za fedha (Tshs) | Tofauti (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Mafuta (Petrol na Diesel) | 400,000,000 | 191,745,000 | 203,500,000 | 11,755,000. |
| Chakula cha Askari | 867,600,000 | 1,103,319,835 | 766,740,000 | 336,579,835 |
| Ujenzi wa Majengo (Msaanina Mtoni) | 4,548,203,050 | 2,522,470,813 | 2,907,700,192 | 385,229,378 |
| **Jumla** | **5,815,803,050** | **3,817,535,648** | **3,877,940,192** | **733,564,213** |

**Majibu ya JKU**

Baada ya kupitia vocha za malipo, JKU imebaini hakuna tofauti ya malipo ya TZS 733,564,213 kama ilivyoripotiwa katika kitabu cha CAG. Hati hizi za malipo ya mafuta, chakula na ujenzi wa majengo zinaonesha ya kwamba fedha iliyolipwa JKU na Wizara ya Fedha ndio iliyotumika. Hati za malipo hayo zimeambatanishwa katika taarifa hii.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba kulikuwepo na tofauti ya fedha kama ilivyoainishwa na Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati yetu imegundua tofauti hiyo imetokana na kuhaulishwa kwa baadhi ya vifungu vya matumizi. Kamati yetu ilifanikiwa kupitia vocha tofauti na kugundua kufanyika kwa jambo hilo, kwa mfano vocha ya matunda hawakununua isipokuwa walinunua vifaa vya kuandikia. Hali hiyo ilipelekea kifungu cha matunda, fedha zake zimepungua na fedha za vifaa vya kuandikia (stationeries) fedha zake zimepanda. Kamati ilipouliza kuhusiana na kielelezo cha uhaulishaji wa fedha hizo lakini haikupatiwa. Kamati yetu iliangalia vocha hizo na imeridhika na majibu kwa vile hakukuwa na upotevu wowote wa fedha.

**Mapedekezo ya Kamati ya PAC**

1. Makamanda wa JKU wanapofanya matumizi wafuate nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali kama zinavyoelekezwa na Sheria za usimamizi wa fedha.
2. Mkuu wa JKU ajenge uwezo wa watendaji wake wa kitengo cha fedha ili wanapoandaa taarifa ya hesabu yao ya mwisho anapokuja Mkaguzi aweze kupatiwa majibu yaliyosahihi.

**Hoja nambari 6.3.2.11: Kuwepo kwa tofauti baina ya taarifa za mapato zilizoainishwa katika taarifa ya fedha ya mwaka (Annual Financial Statement) na taarifa za mapato zilizorikodiwa katika daftari la fedha taslim (cash book) shilingi 96,085,000**

Katika kupitia taarifa ya fedha ya mwaka 2020/2021, ukaguzi umebaini kuwa taarifa za mapato zilizoainishwa katika taarifa ya fedha ya mwaka hazilingani na makusanyo halisi ya mapato yaliyorikodiwa katika daftari la fedha taslim.

Kuwepo kwa tofauti ya mapato halisi yaliyokusanywa na taarifa za mapato zilizoripotiwa katika taarifa ya fedha ya mwaka kunapelekea kutoa taarifa zisizo sahihi.

Uongozi wa JKU unashauriwa kuhakikisha kwamba taarifa zote za hesabu zinafungwa kwa usahihi na kwa ukamilifu. Mchanganuo wa tofauti hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 40: Tofauti ya mapato baina ya taarifa ya fedha ya mwaka na taarifa zilizorikodiwa katika daftari la fedha taslim.**

| Chanzo Cha Mapato | Makadirio | Daftari la Pesa Taslim (Cash Book) (A) (shs) | Taarifa ya Fedha ya Mwaka (B) (shs) | uti (B-A)(shs) |
|---|---|---|---|---|
| Rental of cloves plantation | 5,000,000.00 | 7,179,000.00 | 200,000.00 | (6,489,000) |
| Earning from sales of horticulture | 15,000,000.00 | 67,030,000.00 | 9,525,500.00 | (55,804500) |
| Earning from livestock | 2,000,000.00 | 8,193,500.00 | 2,100,000.00 | (6,093,500) |
| Earning from sale of rice | 10,000,000.00 | 21,800,000.00 | 4,000,000.00 | (17,800,000) |
| Tution fee | 36,000,000.00 | 37,500,000.00 | 38,000,000.00 | (500,000) |
| Rent of commercial cite | 2,224,000.00 | 6,000,000.00 | 1,406,500.00 | (4,593,500) |
| Small scale industries | 15,000,000.00 | 45,159,500.00 | 9,500,000.00 | (4,804,500) |
| **Jumla** | **85,224,000** | **192,862,000** | **64,732,000** | **(96,085,000)** |

### Majibu ya JKU

JKU huandaa mpango wa makusanyo ya mapato vikosini kila mwaka kwa ajili ya makusanyo ya fedha zinazokwenda katika mfuko mkuu wa Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 JKU ilipangiwa kukusanya TZS 87,224,000 na kukusanya TZS 66,632,000 kama inavyosomeka katika taarifa yake ya matumizi ya mwisho wa mwaka (Final Account) ukurasa namba 20.

Kwa msingi huo hakuna tofauti ya taarifa za mapato kama ilivyolalamikiwa katika ripoti ya CAG. Mpango wa makusanyo hayo kutoka katika vikosi mbali mbali, makusanyo halisi pamoja na cashbook ya mapato ya mfumo zimeambatanishwa katika taarifa hii.

### Uchunguzi wa Kamati

Kamati ya PAC imebaini majibu na mapendekezo ya hoja hii yanafanana na hoja nambari 6.3.2.10.

### JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) - PEMBA

***Hoja Nambari 6.3.2.12: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 12,000,000.***

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 12,000,000 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba lakini baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa na hati za malipo ilikuwezakuthibitisha uhalali wamalipo hayo.

Kutokuabatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 41: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 20/10 ya 20/10/2020 | 678053 | 3,000,000 | Kamanda wa JKU Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma mbali mbali za chakula |
| 16/12 ya 16/12/2020 | 678094 | 3,000,000 | | |
| 12/12 ya 12/12/2020 | 678090 | 6,000,000 | | |
| | | **12,000,000** | | |

**Majibu ya JKU**

VR No 20/10/2020 na 16/12/2020 zenye hundi nambari 678053 na 678094 zenye thamani ya shilingi 3,000,000/- kwa kila moja, Yakiwa ni malipo ya huduma ya chakula pamoja na viungo kwa askari wapya ambao wanakaa Kambini (single) kwa mwezi wa Oktoba na Dis, 2022 ambapo risiti na subvoucher zilitumika kwa huduma hizo.

VR No 12/12/2022 yenye hundi nambari 678090 yenye thamani ya shilingi 6,000,000/-, yakiwa ni malipo ya chakula na huduma kwa vijana wa kujitolea waliopo katika Zoni ya JKU Pemba kwa mwezi Dis, 2020 ambapo risiti na subvoucher zilitumika katika huduma hiyo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa wakati Mkaguzi anafanya ukaguzi, risiti zilikuwa bado hazijapatikana. Kamati yetu ilitaka kujua kwanini hivi sasa vielelezo viwepo na kuelezwa kwamba kipindi alichopita Mkaguzi hawakujua wapi vielelezo hivyo.

Hata hivyo, Kamati yetu imepata fursa ya kuvikagua hivyo vielelezo vilivyokosekana ikiwemo kielelezo cha ombi la kutoa fedha ya shilingi 3,000,000 aliyelipwa Mkuu wa Zone JKU, risti namba 2312 tarehe 29/12/2020. Kamati iliridhika na majibu yaliyotolewa hasa ukizingatia kipindi cha uchaguzi wahusika wengi walikuwa hawakai Ofisini.

**Mapendekezo ya kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaushauri Uongozi wa JKU kuweka kumbukumbu vizuri ili anapokuja Mkaguzi wapatiwe kwa wakati.

**Hoja Nabari 6.3.2.13: Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 4,343,100**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 4,343,100 zimetumika kwa ununuzi wa bidhaa mbali mbali dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokurikodiwa kwa manunuzi hayo katika daftari la kumbukumbu la ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 42: Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 2/9 ya 25/9/2020 | 01101 | 193,100 | Kamanda JKU Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diese lita100 |
| 01/07 ya 01/07/2020 | 077989 | 650,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petrol lita 170.9 pamoja na ununuz wa chakula. |
| 4/12 ya 4/12/2020 | 678085 | 2,500,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa mafuta ya Diese Lita 600 |
| 9/10 ya 9/10/2020 | 678046 | 1,000,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa mafuta ya Petro Lita 300 |
| **Jumla** | | **4,343,100** | | |

**Majibu ya JKU**

Bidhaa ya hizo tayari zimeshaingizwa katika daftari la ghalani kama inavyoonekana katika Jadweli hapa chini:-

**Jadweli (i) Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi kilicholipwa | Aliyelipwa | Idadi ya lita | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 2/9 ya 25/9/2020 | 001101 | 193,100 | Chake Chake | 100 | Ipo uk 1 ladger No 2 |
| 1/7 ya 1/7/2020 | 677989 | 370,000 | | 170.9 | Ipo uk 5 ladger No 3 |
| 4/12 ya 4/12/2020 | 678095 | 550,000 | | 294.7 | Ipo uk 1 ladger No 3 |
| 9/10 ya 9/10/2020 | 678046 | 400,000<br><br>320,000 | Kamanda wa JKU | 208.5<br><br>168.8 | Ipo uk 3 ladger No 3<br><br>Ipo uk 6 ladger No 3 |
| **Jumla** | | **1,833,100** | | | |

**Majibu ya JKU**

NB: Katika hali hiyo kiasi cha fedha shilingi 2,510,000/- kimeongezeka.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Makamanda wa JKU kukubaliana na kuwepo kwa hoja ya Mkaguzi. Kamati ya PAC ilitaka kujua kwanini awali bidhaa hizo hazikuingizwa katika daftari la ghalani na kuelezwa kwamba wakati ukaguzi unafanyika, kulikuwa na mabadiliko makubwa ya Maaskari wenye utaalamu wa Manunuzi na Utunzaji ghala na baadhi ya vielelezo vilichukuliwa na ZAECA kwa ajili ya uchunguzi. Kamati baada ya kuvipitia vielelezo hivyo iliridhika na majibu hayo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

JKU iandae utaratibu mzuri wa kuhifadhi na kutumia kumbukumbu zake ili zitakapohitajika ziweze kupatikana kwa wakati ikiwemo pia na kutoa nakala ya kumbukumbu hizo ili nyaraka moja ikichukuliwa moja inabakia.

**Hoja Nambari 6.3.2.14: Uhamisho wa kikazi kwa Wapiganaji wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) Pemba**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 89(1)(2)(3) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 kinatoa maelekezo kwa mtumishi yoyote atakaepewa uhamisho kutoka Unguja kwenda Pemba, Tanzania Bara au kinyume chake atapaswa kulipwa Posho la Usumbufu litakalokuwa sawa naposho la siku saba pamoja na usafiri wa ndani wa kufidia usumbufu atakao upata katika kutekeleza amri hiyo ya uhamisho. Aidha, kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha kwanza na cha pili ya kanuni hii mtumishi huyo atastahiki kugharamiwa uhamishaji wa familia na mizigo yake.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 60(g) cha Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ kinaeleza "Posho la usumbufu ambalo lita fungamana na uhamisho wa kutoka Unguja kwenda Pemba au kinyume chake la asilimia 25 ya mshahara".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha JKU Pemba kimefanya uhamisho wa kikazi kwenda Unguja kwa wapiganaji wake mbali mbali, dosari ya kiutumishi iliyobainika ni kutokutekelezeka kwa vifungu nilivyoviainisha hapo juu kutokana na kukosekana kwa vielelezo mbali mbali vilivyothibitisha upokeaji wa stahiki za malipo yatokanayo na shughuli ya uhamishaji wa familia na mizigo kwa mujibu wa utaratibu.

Kuwakosesha stahiki za uhamisho kwa wapiganaji hao kunaweza kupelekea kupunguza hamasa ya ufanyaji wa kazi na hatimae kujitokeza kwa malalamiko ya chini kwa chini ambayo hupelekea kuondoa imani kwa Wakuu wa Vikosi vya ulinzi na Usalama.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama kuhakikisha unatekeleza kikamilifu maagizo ya Kanuni za Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni za Idara Maalum za Vikosi vya SMZ kwa lengo la kuondosha igongano na migogoro kwa wapiganaji

makazini. Mchanganuo wa wapiganaji hao ni kama unavyoonekana katika Jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 43: Orodha ya wapiganaji waliohamishwa kikazi bila ya kufanyiwa malipo**

| Namba | Jina la Mpiganaji | Namba | Jina la Mpiganaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Zainab Omar Haji | 17 | Haji Bakar Yussuf |
| 2 | Hada Diwa ni Juma | 18 | Jadidi Rehani Hassan |
| 3 | Mwajuma Machano Juma | 19 | Khamis Moh'd Abdalla |
| 4 | Ngwali Khamis Ngwali | 20 | Machano Shangama Khamis |
| 5 | Haji Makame Haji | 21 | Mbaraka Kombo Saleh |
| 6 | Moh'd Juma Ali | 22 | Mtumwa Saleh Amour |
| 7 | Nasra Abdu Kassim | 23 | Ngwali Machano Ngwali |
| 8 | Jaffar Khamis Juma | 24 | Moh'd Juma Mussa |
| 9 | Juma Mussa Usi | 25 | Murid Soud Khamis |
| 10 | Hasnuu Hassan Juma | 26 | Moh'd Abdulla Moh'd |
| 11 | Nassra Kassim Moh'd | 27 | Moh'd Mussa Machano |
| 12 | Husna Yakoub Khamis | 28 | Sebastin James Maziku |
| 13 | Khamis Rajab Khamis | 29 | Ibrahim Mora Ali |
| 14 | AliMsaji Ali | 30 | Mshenga Haji Makame |
| 15 | Muhamad Juma Hussein | 31 | Omar Haji Abass |
| 16 | Ame Khamis Juma | | |

**Majibu ya JKU**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 JKU Zoni ya Pemba ilishindwa kulipa stahiki za uhamisho kutoka Pemba kwenda Unguja kutokana na kukosekana kwa bajeti ya fedha hizo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba suala la uhamisho wa Wapiganaji linakuwa linatokea mara kwa mara na kusababisha upungufu wa bajeti ya fedha za uhamisho hasa ukizingatia fedha zinazoombwa sio zinazopatikana. Kamati ya PAC iliridhika na majibu iliyopatiwa na kusisitizza kwamba JKU itoe kipaumbele kwa kujali haki za watu.

**Mapendekezo ya kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inaushauri Uongozi wa JKU kwamba licha ya kuwa na bajeti ndogo wanayoingiziwa wahakikishe Wapiganaji wakati wa kupata uhamisho wanawapatia stahiki zao ili kuondoa migogoro na migongano isiyo ya lazima.
2. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuwapatia bajeti ya kutosha JKU

ili waweze kukamilisha malengo yao vizuri na kuimarisha ulinzi wa nchi yetu.

3. Wizara ya Tawala za Mikoa kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikalini iifanyie marekebisho Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ili kanuni hizo ziweze kuendana.

**Hoja Nmbari 6.3.2.15: Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 15,487,640**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii, Mtu, Kampuni au Taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa Mtu, Kampuni au Chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na Taasisi ya Ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba limefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipohayoni kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 44: Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 02/10<br>05/10/2020 | 001106 | 458,759 | Abdalla Anas Ali | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula. |
| 02/11<br>04/11/2020 | 001122 | 227,000 | Rashid Mohammed Soud | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme |
| 03/11<br>04/11/2020 | 001123 | 455,337 | | |
| 11/11<br>27/11/2020 | 001131 | 158,000 | | |
| 01/12<br>08/12/2020 | 001134 | 876,453 | | |
| 04/01 | 001147 | 347,919 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 05/01/2021 | | | | |
| **Jumla** | | **2,523,468** | | |

**Majibu ya JKU**

- Abdalla Anasi Ali ni mfanya biashara maarufu wa bidhaa za chakula ambae tunamtumia katika kupata huduma mbali mbali za chakula, baada ya kugundua kwamba hajakamilisha utaratibu wa usajili katika mamlaka husika, tulimshauri na baadae kuweza kupata usajili.
- Rashid Mohammed Soud ni mfanya biashara ambaye amesajiliwa katika mamlaka husika mwenye nambari ya usajili REG No 451/G/2020.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa ni kweli JKU wametoa huduma kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi. Hali hiyo ilitokana na kuwepo na mazingira maalum ya dharura kwa maslahi ya Taifa kwa Wapiganaji wetu. Kwa muhtadha huo, Kamati yetu iliridhika na maelezo yaliyotolewa na haikuwa na hoja zaidi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

JKU inapokuwa inahitaji huduma wa Watoa huduma maalum, ihakikishe inaiandikia barua Mamlaka ya Manunuzi ili kupata ridhaa kama inavyoelekeza Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

**Hoja Nambari 6.3.2.16: Kukosekana kwa taarifa za mapato yatokanayo na uzalishaji wa mazao mbali mbali**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba linamiliki maeneo mbali mbali ya uzalishaji yenye ukubwa wa ekari zipatazo 913 ambapo maendeleo hayo hutumiwa kwa ajili ya kilimo cha mazao ikiwemo mpunga, muhogo, mahindi, minazi, mboga mboga na kunde.

Ukaguzi umebaini Jeshi la Kujenga Uchumi mara baada ya mavuno hufanya uuzaji wa mazao hayo kwa taasisi mbali mbali pamoja na watu binafsi kwa lengo la kujipatia kipato kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa kikosi hicho.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa taarifa na kumbukumbu zinazobainisha mapato halisi yaliyopatikana yanayotokana na mauzo ya bidhaa hizo jambo ambalo linapelekea kutia shakajuu ya uhalali wa matumizi ya fedha ya mapato hayo ambapo haijulikani kima halisi cha fedha kilichopatikana pamoja na kile kilichotumika na shughuli iliyopelekea kutumika kwa mapato hayo jambo ambalo hupelekea viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 45: Kukosekana kwa taarifa za mapato yatokanayo na uzalishaji wa mazao mbali mbali**

| Nam. | Jina la Kambi | Miradi uliofanyika |
|---|---|---|
| 1 | Chokocho | Ufugaji wa kuku wa kisasa |
| | | Ufugaji wa kuku wa kienyeji |
| 2 | Mwambe | Ufugaji wa samaki |
| 3 | Chambani | Ufugaji wa ngombe |
| | | Kilimo cha mboga mboga |
| 4 | Pujini | Kilimo cha mboga mboga |
| 5 | Kwapweza | Kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua |
| | | Kilimo cha mboga mboga |
| | | Ufugaji wa kuku wa kisasa |
| 6 | Ngezi | Uatikaji wa miche ya minazi |
| | | Kilimo cha mboga mboga |
| | | Kilimo cha viazi vitamu |
| | | Kilimo cha njugunyasa |
| | | Ufugaji wa kuku wa kienyeji |
| 7 | Msaani | Kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua |
| | | Kilimo cha muhogo |
| | | Kilimo cha kunde |
| | | Kilimo cha mboga mboga |

**Majibu ya JKU**

Katika ripoti ya CAG imeeleza kuwepo kwa shughuli za uzalishaji wa mazao mbali mbali kutoka katika Kambi na Vituo vya JKU Zoni ya Pemba kiasi ambacho hakuonekani mapato yoyote kutoka katika Kambi hizo. Katika kipindi hicho, vipo Vituo ambavyo vilifanya shughuli za kilimo na kuweza kuzalisha na kupata mapato ambayo yaliingizwa katika akaunti ya Miradi ya JKU Pemba kama inavyoonekana katika jadweli linalofuata:-

| Tarehe | Kambi | Kiasi cha Fedha | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 03/11/2020 | Kituo cha JKU Kwapweza | 1,000,000 | Mauzo ya matikiti |
| 12/11/2020 | Kituo cha JKU Kwapweza | 225,000 | Mauzo ya kuku |
| 19/11/2020 | Ofisi ya Uzalishaji Mali | 100,000 | Mauzo ya asali |
| 07/12/2020 | Kituo cha Pujini | 180,000 | Mauzo ya tungule |
| 07/12/2020 | Kituo cha JKU | 300,000 | Mauzo ya kuku |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Kwapweza | | |
| 11/01/2021 | Kituo cha JKU Kwapweza | 600,000 | Mauzo ya matikiti |
| **Jumla** | | **2,405,000** | |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ya kikatiba, ndio muda ambao harakati za uchaguzi zilikuwepo na kusababisha ugumu wa upatikanaji wa Watendaji masuul wa kuweza kutoa majibu yanayotakiwa.

Aidha, kulikuwa na hali mbaya (changamoto ya tabia nchi) isiyoridhisha ya uzalishaji iliyosababishwa na ukosefu wa mvua hali ya kwamba kilimo chao kilikuwa kikitegemea maji ya mvua kwa asilimia kubwa. Kamati imeelezwa kwamba kwasasa tayari JKU imeanza utaratibu wa kilimo cha umwagiliaji kitakachokuwa na ongezeko kubwa la uzalishaji.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inaishauri Wizara ya Fedha iwababakishie JKU asilimia 40 ya mapato yanayotokana na mazao wanayoyazalisha ili fedha zitakazopatikana ziweze kutumika kama gharama za uendeshaji.
2. Kamati ya PAC inashauri uongozi wa JKU kuwa makini wakati wa kupanda mazao na kuzingatia msimu sahihi wa kupanda mazao.
3. Uongozi wa JKU uharakishe kuingia katika kilimo cha umwagiliaji kwani ndio kilimo cha uhakika hasa kipindi hiki chenye changamoto ya tabianchi.

**Hoja Nambari 6.3.2.17: Bidhaa ambazo hazikuingizwa kwenye daftari la ghalani shilingi 4,772,000**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 4,772,000 zimetumika kwa ununuzi wa bidhaa mbalimbali dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuingizawa bidhaa hizo kwenye daftari la ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake.

Kutokuingizwa bidhaa katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na kifungu cha 123(i)(ii) cha Kanuni ya Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 ya zanzibar pamoja na sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo huo wa bidhaa hizo ni kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 46: Bidhaa ambazo hazikuingizwa kwenye daftari la ghalani**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 08/10 16/10/2020 | 001113 | 2,000,000 | Mkuu wa Miradi ya JKU Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petroli lita 52 |
| 09/10 20/10/2020 | 001114 | 959,000 | Chake Petrol Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Diesel lita 500 |
| 11/10 23/10/2020 | 001116 | 740,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya magari |
| 05/11 18/11/2020 | 001125 | 200,000 | Mkuu wa Miradi ya JKU Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kuku |
| 07/1119/11/2020 | 001127 | 873,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo. |
| **Jumla** | | **4,772,000** | | |

**Majibu ya JKU**

Bidhaa hizo tayari zimeshaingizwa katika daftari la ghalani kama inavyoonekana hapo chini:-

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi kilicholipwa | Aliyelipwa | Idadi ya lita | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 8/10 ya 16/10/2020 | 001101 | 600,000 | Miradi ya JKU | 313 | Ipo uk 3 ladger No 2 |
| 09/10 ya 20/10/2020 | 001114 | 959,000 | Chake Chake | 500 | Ipo uk 1 ladger No 2 |
| 11/10 ya 23/10/2020 | 001116 | 740,000 | | Bearing pc 1<br>Tire pc 1<br>Boll joint pcs 2<br>Propaler pc 1<br>Rejeta pc 1 | Ipo uk 67 ladger B<br>Ipo uk 35 ladger B<br>Ipo uk 7 ladger B<br>Ipo uk 20 ladger B<br>Ipo uk 20 ladger B |
| 05/11 ya 18/11/2020 | 001125 | 200,000 | Miradi ya JKU | Box 1 | Risiti Nambari |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 7/11 ya 19/11/2020 | 001127 | 300,000 | | Spray 16Ltrs pc1<br><br>Spray 2Ltrs pc 1<br><br>Urea 50kgs<br><br>Kani 50kgs<br><br>NPK 50kgs<br><br>Bamic 100m pc 2 | Risiti Nambari 637<br><br>ya tarehe 21/11/20 |
| **Jumla** | | **2,799,000** | | | |

NB: Katika hali hiyo kiasi cha fedha shilingi 1,973,000/- kimeongezeka.

VR No 05/11/2020 yenye thamani ya shilingi 200,000/-, VR No 07/11/2020 yenye thamani ya shilingi 300,000/- yakiwa ni malipo ya fedha kwa ununuzi wa kuku na vifaa vya pembejeo ambazo hazikuingizwa katika daftari la ghalani kwa sababu wahusika walipokabidhiwa fedha hawakuziwasilisha risiti kwa ajili ya kurekodiwa katika daftari la ghalani.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Baada ya Kamati kupata maelezo hayo, haikuwa na maelezo zaidi.

**Mapendekezo ya kamati ya PAC**

Kamati ya inashauri uongozi wa JKU kufuatilia vielelezo mara baada ya mauziano kukamilika na kuweka kumbukumbu kwa wakati ili kuepusha kujitokeza kwa hoja wakati wa ukaguzi.

### 6.3.3: WAKALA WA ULINZI WA JESHI LA KUJENGA UCHUMI (SGA)

**Taarifa ya Mapato**

Wakala wa Ulinzi wa JKU ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,157,700,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wakala ilikusanya jumla ya shilingi 1,869,650,110 sawa na asilimia 59.2 ya makadirio.

**Majibu ya Wakala, Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haikupokea majibu ya Wakala kuhusiana na Taarifa za Mapato yao siku mbili kabla ya kikao kufanyika kama zinavyoelekeza Kanuni zetu za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020). Hata hivyo, Kamati yetu ilihoji na imebaini sababu kuu iliyopelekea Wakala kutofikia lengo la makusanyo ni kuwepo kwa maradhi ya COVID 19 yaliyosababisha baadhi ya hoteli kufungwa na kukatisha Mikataba yao.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa Ulinzi wa JKU kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,316,050,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,876,584,907.95 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 81 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa Wakala ulishindwa kutumia fedha zake kwa asilimia 100 kutokana na kuingia Mkataba Kampuni kwa lengo la kuwaletea sare za Maaskari lakini Kampuni hiyo ilishindwa kutekeleza wajibu kama walivyokubaliana na hatimae kukatisha Mkataba husika. Hali hiyo ilisababisha fedha zilizokuwa zimepangwa kutumika hazikutumika.

**Hoja nambari 6.3.3.1: Kutumika kwa stakabadhi za malipo zisizokuwa za Serikali**

Katika kupitia stakabadhi za malipo zinazotolewa na wakala kwa wateja wake waliopatiwa huduma za ulinzi. Ukaguzi umebaini kuwepo kwa makusanyo yenye jumla ya shilingi 1,719,265,110.28 ambayo yamekusanywa kupitia stakabadhi zilizotengenezwa na kutolewa na Wakala wa Ulinzi kwa ajili ya huduma ya ukusanyaji wa mapato.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa idhini ya matumizi ya stakabadhi hizo kutoka kwa mlipaji Mkuu wa Serikali. Kutumia stakabadhi ambazo hazikuthibitishwa na Serikali inapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na uuzwaji wa stakabadhi hizo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 (1) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Kamati ya PAC imebaini kwamba Wakala walifanya makosa kutokana na kutojua taratibu za uandaaji na matumizi ya risiti kwa Taasisi za Serikali. Hilo lilisababishwa na Wakala kukosa mtendaji mwenye weledi wa kazi za uhasibu (Muhasibu) kwa vile hadi sasa Wakala bado haijafanikiwa kuwa na Muhasibu. Sambamba na hilo, hadi Kamati inaondoka Wakala, hakuna Mtendaji mweledi wa masuala ya Manunuzi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi kuhakikisha matumizi yote ya stakabadhi yanayotumika yanapata ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa lengo la kuipatia mapato Serikali.Mchanganuo wa stakabadhi na mapato hayo ni kama

inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 47: Malipo yanayotokana na Stakabadhi za Wakala wa Ulinzi**

| Namba | Stakabadhi | Thamani (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | 00817-00850 | 120,526,000.00 |
| 2. | 00851-00900 | 164,251,690.29 |
| 3. | 00901-00950 | 156,100,000.00 |
| 4. | 00951-01000 | 147,228,200.00 |
| 5. | 01001-01050 | 146,140,557.14 |
| 6. | 01051-01100 | 175,760,000.00 |
| 7. | 01101-01150 | 181,785,771.43 |
| 8. | 01151-01200 | 147,156,457.14 |
| 9. | 01201-01250 | 183,746,857.14 |
| 10. | 01251-01300 | 138,062,857.14 |
| 11. | 01301-01326 | 158,506,720.00 |
| **Jumla** | | **1,719,265,110.28** |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na kukiri kwao, Kamati yetu ilitaka kujua ni aina gani za risiti ambazo Wakala ulikuwa ukitumia na kuelezwa kwamba walitumia risiti zilizokuwa zimechapwa na Wakala wa Uchapaji Zanzibar kwa kuweka nembo yao ili waweze kujitangana.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wakala uhakikishe unaiandikia barua Wizara ya Fedha na Mipango kuomba Muhasibu wa kutekeleza majukumu yao.
2. Mkurugenzi wa Wakala achukue juhudi za makusudi kuhakikisha anaipatia Wakala Afisa Ununuzi ili kuondosha changamoto zinazoweza kujitokeza.

**Hoja nambari 6.3.3.2: Matumizi ya ziada na makadirio shilingi 299,965,434**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wakala wa Ulinzi imefanya manunuzi yenye thamani ya shilingi kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya uendeshaji wa kazi za ofisi.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 32(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 Taasisi za umma zinatakiwa kupanga makadirio ya mapato na matumizi na kupata uthibitisho wa matumizi ya mapato hayo kutoka katika vikao vya Bodi au kuidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kwamba kutokuwepo kwa Bodi inayosimamia shughuli za wakala imepelekea kutumika kwa fedha za ziada kinyume na makadirio ya mapato hayo jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi JKU kufanya mawasiliano ya karibu na Waziri mwenye dhamana kwa lengo la kumpendekeza Mwenyekiti wa Bodi ambae atateuliwa na Mheshimiwa Rais kwa lengo la kusimamia mapato na matumizi yatokanayo na taasisi hiyo. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 48: Matumizi ya ziada na Makadirio**

| Mahitaji | Makadirio (Tshs.) | Matumizi halisi (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| Ununuzi wa mafuta (ulinzi) | 162,000,000 | 341,645,934 | -179,645,934 |
| Ununuzi wa chakula | 98,900,000 | 204,502,500 | -105,602,500 |
| Service za magari | 42,700,000 | 57,417,000 | -14,717,000 |
| **Jumla** | **303,600,000** | **603,565,434** | **-299,965,434** |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC ilitaka kujua kwa mwaka 2020/2021 Bodi ya Wakala ilikuwa tayari imeshaundwa au bado na kuelezwa kwamba Bodi ya Wakala huo iliundwa tangu mwaka Desemba, 2018 na ilipofika mwaka 2021 ilimaliza muda ambapo miezi mitatu kabla ya kumaliza muda, Mwenyekiti wa Bodi hiyo alifariki. Kutokana na mazingira hayo, kwa vile shughuli za kiutendaji zilikuwa zikifanyika, Wajumbe wa Bodi hiyo walimchagua Mkurugenzi wa Wakala kutekeleza kwa muda majukumu ya Mwenyekiti kupitia maamuzi ya kikao cha Bodi cha tarehe 25/2/2021. Kamati ya PAC baada ya kupatiwa maelezo hayo haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.3.3.3: Kukosekana kwa barua za uhaulishaji wa vifungu (Realocation)**

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Ulinzi imefanya matumizi mbalimbali ambayo yamevuka kiwango halisi cha makadirio yaliyopangwa na kutumia, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanyika kwa uhaulishaji wa fedha kutoka katika vifungu mbali mbali vya matumizi bila ya kuwepo kwa vielelezo vya ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 20(1)(2)(3) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi JKU kuhakikisha unafuata na kuzingatia misingi ya uhalishaji kwa lengo la kuweka wazi matumizi na hatimae kuleta tija iliyokusudiwa. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 49: Kukosekana kwa taratibu za uhaulishaji**

| Mahitaji | Makadirio (Tshs.) | Matumizi halisi (Tshs.) | Tofauti(Tshs.) |
|---|---|---|---|
| Chakula cha Walinzi | 98,900,000 | 204,502,500 | -105,602,500 |
| Ununuzi wa Mafuta | 162,000,000 | 341,645,934 | -179,645,934 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Service za Magari | 42,700,000 | 57,417,000 | -14,717,000 |
| Ujenzi wa Mahanga | - | 16,549,000 | 16,549,000 |
| **Jumla** | | | **316,514,434** |

Kamati imebaini kuwa majibu ya hoja hii yanafanana na majibu ya Hoja nambari 6.3.3.2. Hivyo, Kamati iliridhika na majibu hayo.

**Hoja nambari 6.3.3.4: Kukosekana kwa muongozo wa ulipaji wa posho kwa wakuu wa maidara yenye jumla ya shilingi 27,330,000**

Katika kupitia hati mbali mbali za malipo pamoja na daftari la fedha, ukaguzi umebaini kwamba wakala wa ulinzi amekuwa akifanya malipo kwa wakuu wa maidara na watendaji kupitia hesabu 0400001000. Ukaguzi umebaini kwamba hakuna toleo au kibali kilichoruhusu ulipwaji wa Posho hizo kwa mujibu wa miongozo ya utumishi wa umma. Kukosekana kwa miongozo ya ulipwaji wa posho kunaweza kupelekea wakala kutumia fedha za umma kinyume na utaratibu. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi JKU kufanya ufuatiliaji wa upatikanaji wa ruhusa ya malipo au kumuandikia Waziri mwenye dhamana kuweza kuliwasilisha suala hilo katika kikao cha Baraza la Mapinduzi kwa lengo la kuomba idhini ya Matumizi hayo. Baadhi ya hati hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 50: Hati za malipo zilozotumika kuwalipa Wakuu wa Idara na Walinzi Posho mbali mbali**

| Tarehe | Hati ya malipo | Jumla ya fedha kwa mujibu wa hati ya malipo (Tshs.) | Thamani ya posho inayolipwa kwa walinzi, vijana na Wakuu wa Idara (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 23/06/2021 | PV. 33 | 57,390,000 | 1,500,000 | Malipo kwa ajili ya posho la walinzi, vijana pamoja na posho la wakuu wa maidara |
| 01/12/2020 | PV. 02 | 40,000,000 | 3,450,000 | |
| 02/10/2020 | PV. 02 | 42,950,000 | 3,350,000 | |
| 29/12/2020 | PV. 29 | 41,100,000 | 3,850,000 | |
| 02/09/2020 | PV. 01 | 44,950,000 | 3,200,000 | |
| 29/04/2021 | PV. 36 | 56,750,000 | 4,090,000 | |
| 28/05/2021 | PV. 28 | 58,960,000 | 4,140,000 | |
| 24/10/2020 | PV. 21 | 10,000,000 | 3,750,000 | |
| **Jumla** | | **352,100,000** | **27,330,000** | |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati ya PAC ilipitia Sheria ya Wakala wa Ulinzi na kugundua kwamba kifungu cha 12(4) kinatoa uwezo kwa Wakala kufanya malipo ya mishahara na posho kwa wafanyakazi wake kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

Aidha, Kamati ilitaka kujua ni utaratibu gani ambao Bodi inatumia kuidhinisha Mishahara na posho za Walinzi wao na kuelezwa kuwa mishahara yao hutoka JKU isipokuwa posho huidhinishwa na Bodi kupitia matoleo kutoka Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma. Kamati baada ya kupata majibu hayo haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.3.3.5: Kukosekana kwa mikataba ya ununuzi wa mafuta wenye jumla ya shilingi 341,645,934**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wakala wa Ulinzi imefanya matumizi mbali mbali kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya uendeshaji wa shughuli za wakala kutoka kampuni ya IJITIMAI PETROL STATION na MAP OIL, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuwepo kwa makubaliano ya mikataba midogo midogo inayotoa uhalali wa matumizi hayo.

Kutokuwepo kwa makubaliano ya mikataba midogo midogo kunaweza kukatia dosari upande wowote wa makubaliano pale ambapo itakapobainika dosari za kiutendaji na mmoja kati ya wawili atakapoamua kuvunja makubaliano hayo jambo ambalo linaweza likapelekea kupelekana katika vyombo vya Sheria na kutoa haki isiyostahiki kwa upande mmoja.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi JKU kuhakikisha matumizi yoyote yatakayovuka shilingi 15,000,000 ni vyema kuandikishiana mikataba ya makubaliano kwa mujibu wa matakwa ya kifungu nambari 29(m) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 51: Kukosekana kwa mikataba ya ununuzi wa mafuta**

| Hati namba | Hundi namba | Aliyelipwa | Thamani(Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1/4/2021 | T.T | Ijitimai Petrol Statior | 15,000,000 | |
| 4/5/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 2/9/2020 | 000041 | Map Oil | 7,000,000 | |
| 1/9/2020 | 000040 | | 10,000,000 | |
| 1/8/2020 | 000037 | | 25,000,000 | |
| 4/10/2020 | 00046 | | 14,000,000 | |
| 1/10/2020 | 000042 | | 17,500,000 | |
| 1/3/2021 | T.T | | 12,000,000 | |
| 1/2/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 12/6/2021 | T.T | | 2,148,000 | |
| 15/6/2021 | T.T | | 15,000,000 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 19/6/2021 | T.T | jitimai petrol statement | 15,000,000 | |
| 39/6/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 14/5/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 18/4/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 28/3/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 20/3/2021 | T.T | | 14,000,000 | |
| 13/12/2020 | T.T | | 6,000,000 | |
| 27/1/2021 | T.T | | 13,000,000 | |
| 14/1/2021 | T.T | | 13,000,000 | |
| 27/12/2020 | 000730 | | 8,000,000 | |
| 26/12/2020 | 000731 | | 5,000,000 | |
| 14/12/2020 | 000717 | | 5,997,934 | Ununuzi wa mafuta kwa matumizi ya Ofisi ya wakala wa ulinzi Jku |
| 18/11/2020 | 000694 | Map Oil | 15,000,000 | |
| 21/9/2020 | 000653 | | 10,000,000 | |
| 9/9/2020 | 000641 | | 5,000,000 | |
| 10/8/2020 | 000623 | | 12,500,000 | |
| 23/7/2020 | 000606 | | 11,500,000 | |
| **Jumla** | | | **341,645,934** | |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika uchunguzi wake, Kamati ya PAC ilibaini kwamba Mkataba upo wa tarehe 1/12/2020 hadi 30/6/2021 na baada ya kuupitia iligundua unatosheleza kutekeleza lengo lililokusudiwa. Hivyo, Kamati haikuwa na maelezo ya ziada.

**Hoja nambari 6.3.3.6: Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi kwa ununuzi wa chakula cha Askari shilingi 214,377,500**

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa ulinzi umefanya ununuzi wa chakula kwa ajili ya huduma kwa askari wanaopangiwa kutoa huduma ya kulinda katika vituo vyao vya malindo kupitia mtoa huduma YES BOSS SHOP. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa utoaji wa huduma na mzabuni huyo ambapo kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Aidha, katika ufuatiliaji wa mapokezi ya vyakula vilivyonunuliwa ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa mapokezi ya vyakula hivyo kutokana na kukosekana kwa ukaguzi hati inayothibitisha mapokezi ya chakula hicho (delivery note). Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kupatiwa taratibu walizokubaliana na mzabuni huyo katika ulipwaji wa fedha zinazotumika katika ununuzi wa chakula hicho (Mode of payment) jambo ambalo limetia shaka juu ya matumizi ya fedha za umma na kupelekea uwepo wa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi JKU kuhakikisha unatekeleza matakwa ya kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za

Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 52: Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi**

| Hati ya malipo | Hundi Namba | amani(Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 2/3/2021 | 000793 | 7,500,000 | Yess Boss Shop | Ununuzi wa chakula kwa walinzi wa wakala |
| 4/2/2021 | 000050 | 5,000,000 | | |
| 2/6/2021 | T.T | 7,700,000 | | |
| 20/6/2021 | T.T | 7,700,000 | | |
| 40/6/2021 | T.T | 11,500,000 | | |
| 24/5/2021 | 000861 | 8,000,000 | | |
| 16/4/2021 | T.T | 7,500,000 | | |
| 23/4/2021 | T.T | 1,857,500 | | |
| 34/4/2021 | T.T | 10,487,000 | | |
| 25/3/2021 | T.T | 7,500,000 | | |
| 18/3/2021 | T.T | 7,500,000 | | |
| 15/2/2021 | T.T | 7,500,000 | | |
| 8/2/2021 | 000773 | 7,500,000 | | |
| 15/1/2021 | 000753 | 7,500,000 | | |
| 2/1/2021 | 000740 | 7,500,000 | | |
| 19/12/2020 | 000721 | 7,500,000 | | |
| 19/11/2020 | 000693 | 7,000,000 | | |
| 5/11/2020 | 000680 | 5,229,000 | | |
| 4/11/2020 | 000679 | 5,000,000 | | |
| 19/10/2020 | 000675 | 6,500,000 | | |
| 10/10/2020 | 000660 | 5,500,000 | | |
| 17/9/2020 | 000648 | 7,600,000 | | |
| 4/9/2020 | 000637 | 7,600,000 | | |
| 17/8/2020 | 000651 | 5,000,000 | | |
| 5/8/2020 | 000618 | 8,000,000 | | |
| 6/7/2020 | 000587 | 7,000,000 | | |
| **Jumla Ndogo** | | **204,502,500** | | |
| 27/6/ 2021 | 000886 | 1,061,600 | Khamis Othman khamis | Ununuzi wa mikate ya walinzi |
| 6/5/2021 | 000848 | 692,200 | | |
| 6/4/2021 | 000818 | 1,000,000 | | |
| 3/3/2021 | 000796 | 915,200 | | |
| 1/2/2021 | 000769 | 984,000 | | |
| 9/12/2020 | 000710 | 940,000 | | |
| 28/12/2020 | 000733 | 831,000 | | |
| 1/10/2020 | 000656 | 928,000 | | |
| 7/9/2020 | 000640 | 853,000 | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3/8/2020 | 000619 | 835,000 | | |
| 4/7/2020 | 000588 | 835,000 | | |
| **Jumla Ndogo** | | **9,875,000** | | |
| **Jumla Kuu** | | **214,377,500** | | |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya hoja hii na baada ya kupitia majibu na kufanya rejea majibu ya hoja kama hiyo yaliyojibiwa na Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU). Hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.3.3.7: Matumizi yenye vielelezo pungufu shilingi 27,500,000**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 27,500,000 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Wakala wa ulinzi JKU, dosri iliyobainika ni kwamba baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 53: Matumizi yenye vielelezo pungufu**

| **Hati nam-ba** | **Hundi namba** | **Kiasi cha fedha kili-cholipwa (Tshs.)** | **Aliyelipwa** | **Maelezo** | **Mapungufu** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1/5/2021 | 000055 | 7,500,000 | Visiwani generalsupplier | Ununuzi wa makoti ya mvua. | Kukosekana kwa Delivery note |
| 1/5/2021 | 000053 | 5,000,000 | | | Kukosekana kwa invoice na deliverynote |
| 2/5/2021 | 000054 | 5,000,000 | | | Kukosekana kwa Delivery note |
| 26/6/2021 | 000890 | 5,000,000 | Central trading Co. | Ununuzi wa kitambaa vya uniform | |
| 25/6/2021 | 000889 | 5,000,000 | | | |
| **Jumla** | | **27,500,000** | | | |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya kuwepo kwa hati ya kuwasilisha bidhaa (delivery note) ya tarehe 17/4/2021 kutoka ‘Visiwani Genaral Supplier’. Hata hivyo, Kamati yetu ilitaka kujua kwamba kwanini alipopita Mkaguzi hakupatiwa nyaraka hizo hadi leo ndio zipatikane na kuelezwa kuwa walikuwa hawajui wameziweka eneo gani lakini baada ya kuzitafuta wameziona.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wakala uwe na utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu zake ili zitakapohitajika ziweze kupatikana kwa wakati.
2. Wakala utoe ushirikiano wa karibu anapokuja Mkaguzi ikiwemo kumpatia majibu yaliyo sahihi ili kuondosha hoja zisizokuwa za msingi kujitokeza katika katika Ripoti yake.

Aidha, Kamati pia imepitia Mkataba wa chakula wa tarehe 1/7/2020.

FUNGU D 03 - CHUO CHA MAFUNZO ZANZIBAR

Taarifa ya Mapato

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Chuo cha Mafunzo kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 75,720,000 kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Chuo cha Mafunzo kilikusanya jumla ya shilingi 41,704,000 sawa na asilimia 55 ya makadirio.

Majibu ya Chuo na Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati haijapokea majibu ya Taarifa ya Matumizi siku mbili kabla ya kikao kama ilivyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020). Hata hivyo, Wajumbe walihoji kuhusiana na vyanzo vyao vya mapato na kupatiwa maelezo machache. Kamati haikuwa na Maelezo zaidi.

Taarifa ya Matumizi

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Chuo cha Mafunzo kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 21,833,600. Kati ya hizo shilingi 20,333,600,000 zilipangwa kutumika kwa ajili ya kazi na shilingi 1,500,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Kikosi cha Mafunzo kiliingiziwa jumla ya shilingi 18,303,767,139sawa na asilimia 83.83 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 18,053,767,139 zilitumika kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 88.79 ya makadirio na shilingi 250,000,000 zilitumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 16.67.

Majibu ya Chuo na Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati haijapokea majibu ya Taarifa ya Mapato siku mbili kabla ya kikao kama ilivyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020). Hata hivyo, Kamati haikufurahishwa kuwasilisha majibu bila kuainisha majibu ya taarifa za Matumizi kwani barua iliyowasilishwa kwao pamoja na utaratibu mzima wa Kamati za kusimamia masuala ya fedha siku zote huwa zinaelekeza hivyo.

**Hoja nambari 6.3.4.1: Matumizi ya Masurufu (imprest) ambayo hayana marejesho shilingi 10,000,000**

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 10,000,000 za mapato amelipwa Kamishna Chuo cha Mafunzo kupitia hati nambari 7/4/2021 ya tarehe 12/4/2021, ikiwa ni masurufu kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya Chuo, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokupatikana kwa marejesho ya matumizi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanisha vielelezo vya malipo husika ni kwenda kinyume na kanuni ya fedha kifungu namba 95 ya 2005 na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha marejesho ya matumizi yaliyokosekana pamoja na vielelezo vyake vinaambatanishwa na hati za malipo kwa ajili ya ukaguzi.

**Majibu ya Chuo cha Mafunzo**

Ni kweli ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi milioni kumi 10,000,000/- za mapato zimetumika kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya Chuo Cha Mafunzo bila ya kukuwepo kwa marejesho ya matumizi hayo, ila kwa sasa marejesho ya matumizi hayo yapo na tuko tayari kwa ajili ya ukaguzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Makamanda wa Chuo cha Mafunzo kukubaliana na hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilitaka kujua sababu ya kutopatiwa Mkaguzi vielelezo na kuelezwa kuwa wakati huo Chuo cha Mafunzo kilikuwa na harakati nyingi zenye maslahi na maendeleo ya Zanzibar na Wananchi wake. Hivyo hawakuwa na muda mzuri wa kuvitafuta na kuviwasilisha kwa Mkaguzi, Kamati yetu ilipata fursa ya kuvikagua vielelezo hivyo na kuridhika navyo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kikosi cha Chuo cha Mafunzo kihakikishe kinatoa mashirikiano stahiki kwa Mkaguzi anapokwenda katika Ofisi zao kutekeleza majukumu yao.

Kikosi cha Chuo cha Mafunzo kiandae utaratibu mzuri wa kuhifadhi vielelezo vya matumizi wanayoyafanya ili kuepusha kukosekana wakati vianapohitajika.

**Hoja nambari 6.3.4.2: Malipo yasiyozingatia ushindani wa bei shilingi 32,140,500**

Ukaguzi umebaini Chuo cha Mafunzo kimetumia jumla ya shilingi 32,140,500 za mapato kwa ajili ya kupata huduma pamoja na manunuzi ya vifaa mbalimbali, dosari iliyobainika ni kutokuwepo kwa ushindani wa bei jambo ambalo linaweza kupelekea kufanyika kwa

malipo ya bei ya juu ukilinganisha na uhalisia wa mahitaji yanavyopatikana kwa bei ya sokoni.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha unafanya matumizi kwa kuzingatia matakwa ya kanuni na sheria za fedha ili kuepuka kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 54: Malipo yasiyozingatia ushindani wa bei**

| Hati namba | Tarehe | Aliyelipwa | hamani(Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1/11/2020 | 13/11/2020 | Duka Chuo Cha Mafunzo | 2,558,000 | Ikiwa ni ununuzi wa vifaa vya ushoni. |
| 1/8/2020 | 3/8/2020 | | 1,750,000 | Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa computer. |
| 2/12/2020 | 3/12/2020 | | 4,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya vifaa vya ujenzi. |
| 6/12/2020 | 10/12/2020 | | 1,000,000 | |
| 8/12/2020 | 14/12/2020 | | 2,100,000 | |
| 9/12/2020 | 15/12/2020 | | 1,250,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya uunuzi wa vifaa vya usafi. |
| 2/3/2021 | 8/3/2021 | | 1,030,000 | Ikiwa ni manunuzi ya vifaa vya kufekea majani uwanja wa ndege |
| 4/3/2021 | 8/3/2021 | | 1,150,000 | Ikiwa ni manunuzi ya mipira ya gari. |
| 5/3/2021 | 11/3/2021 | | 1,452,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ujenzi kujenga mitaro na makaro gerezani |
| 6/4/2021 | 12/4/2021 | | 6,000,000 | Ikiwa ni ununuzi wa saruji. |
| 10/4/2021 | 16/4/2021 | | 7,950,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya vifaa vya matumizi ya Ramadhani |
| 9/4/2021 | 14/4/2021 | | 1,900,500 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mbao na miti. |
| **Jumla** | | | **32,140,500** | |

## Majibu ya Chuo cha Mafunzo

Taarifa ya ukaguzi imesema kwamba baadhi ya malipo yamekosa ushindani wa bei ila katika kila matumizi ambayo yamefanywa ushindani wa bei, yaani Ankara tatu zimetumika na tupo tayari kwa ajili ya ukaguzi.

## Uhunguzi wa Kamati ya PAC

Kwa vile Makamanda wa Chuo cha Mafunzo hawajakubaliana na hoja ya Mkaguzi, Kamati ya PAC ilifuatilia kwa undani hoja za pande zote mbili pamoja na kupitia vielelezo vilivyowasilishwa na kubaini kwamba ni kweli utaratibu haukufuatwa ipasavyo lakini hilo lilifanyika kwa maslahi ya Zanzibar na Wapiganaji wa Chuo. Hivyo Kamati yetu imeridhika na majibu yaliyowasilishwa na haikuwa na maelezo zaidi.

**Mmapendekezo ya Kamati ya PAC**

Makamanda wa Chuo cha Mafunzo wanapokuwa wanahitaji kutekeleza kazi nyeti wahakikishe wanapeleka maombi kwa Watoa huduma, wapeleke maombi yao katika Mamlaka husika ili wapate ridhaa zao.

**Hoja nambari 6.3.4.3: Kutokatwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) inayotokana na ununuzi na utoaji wa huduma shilingi 373,193,601**

Ukaguzi ulipitia hati mbalimbali zinazohusiana na malipo na kubaini kuwepo kwa hati za malipo zinazohusiana na manunuzi na utoaji wa huduma zenye thamani ya shilingi 373,193,601 ambazo zilistahiki kukatwa kodi ya ongezeko la thamani ya shilingi 58,918,643.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokukatwa kodi ya ongezeko la thamani na kuziwasilisha katika ofisi inayohusiana na mapato kwa mujibu wa sheria. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 55: Kutokatwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani**

| Hati namba | Ankara namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | VAT (15%) |
|---|---|---|---:|---:|
| 1/7/2020 | 0423 | Sabah Store | 48,821,450 | 7,704,150 |
| 6/8/2020 | 0435 | | 56,502,500 | 8,919,281.25 |
| 3/9/2020 | 0444 | | 53,454,960 | 8,440,260 |
| 19/10/2020 | 0604 | | 71,542,291 | 11,296,151 |
| 1/11/2020 | 0615 | | 79,049,500 | 12,481,500 |
| 21/12/2020 | 0623 | | 63,822,900 | 10,077,300 |
| **Jumla** | | | **373,193,601** | **58,918,642.25** |

Chuo cha Mafunzo kushindwa kukata kodi ya ongezeko la thamani kunapelekea kuikosesha Serikali mapato hali inayosababisha kutofikiwa kwa malengo yaliopangwa katika mpango mkakati wa Taasisi zinazosimamia kodi na Serikali ambapo kufanya hivyo ni ukiukwaji wa sheria, kanuni na miongozo ya kodi iliyowekwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha unasimamia suala zima la ukataji wa kodi ya ongezeko la thamani kwa kila manunuzi au huduma zinazotolewa ili kwenda sambamba na sheria ya kodi.

**Majibu ya Chuo cha Mafunzo**

Ni kweli Wakaguzi walipokuja waliona kuwa katika manunuzi ya chakula hatujakata VAT 15% lakini kutokana na maelekezo ya Maafisa wa ZRB na TRA walituwekea semina na walitutaka tunapofanya malipo ya bidhaa za chakula tukate asilimia tano (5%) kati ya

hizo asilimia tatu (3%) iende ZRB na asilimia mbili (2%) iende TRA na makato hayo yamefanyika kama walivyotutaka tufanye.

**Uhunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Makamanda kukiri kwamba kodiya zuio haikukatwa ipasavyo. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilitaka kujua kwanini hilo likatokezea na kuelezwa kwamba Chuo cha Mafunzo walipatiwa Semina iliyowaelekeza kodi ya zuio ikatwe kwa jumla ya asilimia 5 (3 kwa ZRB na 2 kwa TRA). Kamati ilienda ndani zaidi kutaka kufahamu kama kuna kielelezo chochote kilichoelekeza wafanye hivyo na kuelezwa hayo yalifanywa pasi na kuwepo kielelezo chochote.

Sambamba na hilo, Kamati yetu imebaini kwamba kulijitokeza ufahamu usio sahihi wa mafunzo waliyopatiwa na hatimae kupelekea utekelezaji usio sahihi. Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC, haikuridhishwa na majibu na sababu zilizotolewa. Kwasasa Chuo cha Mafunzo kimerekebisha kasoro hiyo ambapo wanazuia kodi ipasavyo kwa Watoa huduma wanaofanya nao biashara.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Makamanda wa Chuo cha Mafunzo watekeleze majukumu yao kwa kufuata ipasavyo Sheria za kodi na iwache kufuata maelekezo yasiyokuwa na uthibitisho ili waweze kuipatia mapato Serikali.

**Hoja nambari 6.3.4.4: Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu shilingi 130,844,030**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 130,844,030 amelipwa Kamishna Chuo cha Mafunzo kwa ajili ya malipo ya watoa huduma mbalimbali badala ya kufanya malipo ya moja kwa moja kwa wahusika kama taratibu za fedha zinavyoelekeza. Kutokufanya malipo moja kwa moja kwa mtoa huduma kupitia hesabu yake (bank account) kunaweza kupelekea upotevu wa fedha za umma na kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi. Aidha ukaguzi umeshindwa kuthibitisha kuwa malipo hayo yamelipwa kwa njia ya hundi au fedha taslim kutokana na kutorikodiwa kumbukumbu za malipo zilizonakikiliwa katika vishina vya hundi au kuoneshwa katika hati za malipo jambo ambalo ukaguzi umetia shaka juu ya kufanyika kwa malipo hayo kwa watoa huduma hao.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo uhakikishe kwamba malipo yote yanalipwa moja kwa moja kwa watoa huduma kupitia katika bank account zao kama sheria za fedha zinavyoelekeza ili kuepuka upotevu wa fedha za umma. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 56: Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu**

| Hati namba | Alielipwa | Mtoa huduma | Stakabadhi Nam | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 5/7/2020 | | | 1116 | 15,109,000 | Malipo kwa ajili ya chakula na vifaavya usafi |
| 22/10/2020 | Kamishna Chuo Cha Mafunzo | Duka la Chuo Cha Mafunzo | 1507<br>1508<br>1509 | 60,000,000 | Malipo ya chakula kwa ajili ya uchaguzi |
| 21/10/2020 | | | - | 14,375,000 | Magodoro na vifaa vya ujenzi |
| 7/7/2020 | | | 1115 | 15,000,000 | Malipo kwa ajili ununuzi wa dawa nambolea |
| 21/10/2020 | | FA Glass Works | 751 | 2,259,230 | Matengenezo ya madirisha |
| 6/7/2020 | | Naima Amar Shebe | 0001 | 12,500,000 | Malipo kwa ajili vifaa mbali mbali |
| 22/10/2020 | | | 003 | 11,600,800 | Malipo ya ununuzi wa Mashine zakusagia mpunga. |

**Majibu ya Chuo cha Mafunzo**

Ni kweli ukaguzi umebaini kwamba shiligi 130,844,030/- amelipwa Kamishna Chuo Cha Mafunzo kwa ajili ya malipo ya Watoa huduma mbali mbali badala ya kufanya malipo moja kwa moja kwa wahusika kama taratibu za fedha zinavyo elekeza. Hii ni kwasababu ya kupata uharaka wa kupata mahitaji kwa kipindi husika kwa mfano ununuzi wa chakula cha stendibai na ununuzi wa madawa ya kuulia wadudu na mbolea za kutia mashambani.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imegundua kwamba ni kweli wakati Mkaguzi inatekeleza majukumu yake Chuo cha Mafunzo hakupatiwa vielelezo vya malipo kutoka kwa Watoa Huduma. Hata hivyo, Kamati yetu ilitaka kujua huduma hiyo ilihusiana na utoaji huduma ya chakula katika duka la Chuo cha Mafunzo ambapo fedha zilikuwa zinalipwa kwa Mkuu wa Chuo hicho na kwenda dukani lakini hali hiyo ilisitishwa tarehe 30 Disemba, 2022 na hivi sasa fedha zinazolipwa zote zikitoka Serikalini wanalipwa Watoa Huduma husika.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Chuo cha Mafunzo ihakikishe kinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti na maelekezo ya Sheria zinazosimamia matumizi ya fedha za Umma ikiwemo Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

**Hoja nambari 6.3.4.5: Kukosekana kwa hatimiliki za vyombo vya Chuo cha mafunzo 847,241,905**

Ukaguzi umebaini kuwa Chuo Cha Mafunzo kinamiliki vyombo mbalimbali vya usafiri

zikiwemo gari 45 na pikipiki 2, ambapo gari 36 na pikipiki 2 zipo Unguja na gari 9 zipo Pemba. Ukaguzi umepitia kumbukumbu na nyaraka zinazohusika na vyombo hivyo na kubaini kuwa vyombo hivyo vinamilikiwa na Chuo, taasisi nyengine za Serikali baadhi ya vyombo umiliki wake ni watu binafsi kinyume na utaratibu, Kiambatisho Nambari 4 Kinahusikakiliomo katika RIpoti ya Mdhibiti husika kinahusika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na miongozo ya fedha taslim (IPSAS CASH) nambari 17. Aidha, ukaguzi umebaini kwamba vyombo vyote hivyo havijakatiwa Bima. Kufanya hivyo ni kinyume na Sheria namba 7 ya mwaka 2003 ya usalama barabarani pamoja na miongozo ya Serikali.

Kukosekana kwa hati miliki kunaplekea kushindwa kumiliki mali hizo kisheria, aidha kunasabisha upotevu wa mali hizo na kupelekea hasara chuo na Serikali kwa ujumla

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kwamba mali zote za Chuo zina tambuliwa na kusajiliwa kisheria kwa ajili ya kupata umiliki halali, ili kuepusha upotevu wa mali hizo.

**Majibu ya Chuo cha Mafunzo**

Ni kweli Ukanguzi umebaini kuwa Chuo Cha Mafunzo kinamiliki vyombo mbali mbali vya usafiri na baadhi ya vyombo hivyo umiliki wake ni watu binafsi kinyume na utaratibu. Hata hivyo Chuo Cha Mafunzo kimeanza kufanya marekebisho ya vyombo hivyo na kwasasa tayari vyombo tisa tumebadilisha usajili na tayari umiliki wake ni Chuo cha Mafunzo na taratibu zinaendelea kwa kumalizia vyombo vyote vilivyobakia.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Makamanda wa Chuo cha Mafunzo kukubali kwamba wakati Mkaguzi anamaliza kazi yake, hatimiliki za vyombo vya moto zilikuwa hazipo na bima havijakatikatiwa. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kwamba usajili wa vyombo hivyo umeanza kufanyika.

Hilo limethibitishwa na Kamati baada ya kuchunguza risiti tofauti za usajili huo ulifanyika tarehe 21/10/2022 zikijumuisha gari aina ya Toyota Hilux MF5530, Fuso Mitsubishi MF1023, Toyota Dyna MF1015, Town ace MF1020 na Suzuki Vitara MF1003 isipokuwa bado vyombo hivyo havijakatiwa bima kutokana na upungufu wa fedha. Hata hivyo, Chuo hicho kimepanga kuvikatia bima vyao kidogo kidogo. Kamati yetu imeridhika na majibu yaliyowasilishwa.

**Hoja nambari 6.3.4.6: Madeni ya Chuo cha Mafunzo yanayodaiwa kutokana na huduma waliyopatiwa na Watoa Huduma mbali mbali**

Ukaguzi umebaini kuwa Chuo cha Mafunzo kina daiwa jumla ya shilingi 847,241,905 kutoka kwa watoa huduma mbalimbali lakini baadhi ya vielelezo vinavyohusiana na madeni hayo havikupatikana kwa ukaguzi, aidha madeni ambayo vielelezo vyake

vimepatikana vinatofautiana na rikodi iliyoainishwa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kuthibitisha na kujiridhisha usahihi wa madeni hayo kutokana na Chuo kutoweka kumbukumbu na rikodi sahihi za madeni hayo. Kutokuwepo kwa kumbukumbu sahihi na usimamizi imara wa madeni kunaweza kusababisha upotevu wa fedha za Serikali na ni kwenda kinyume na sheria na miongozo ya fedha iliyopo. Aidha kutasababisha athari kwa bajeti ya mwaka unaofuata na kupelekea mipango iliyopangwa kutotekelezeka kwa wakati.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha unasimamia na kufuatilia kwa kina madeni yake pamoja na kuyathibitisha ili kuepuka kurejea kulipa madeni hayo jambo ambalo linapelekea upotevu wa fedha za Serikali.Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 57: Madeni ya Chuo cha Mafunzo wanayodaiwa kutokana na huduma walizopatiwa**

| **Mdai** | **Muda wa deni** | **Deni katika hesabu ya mwisho wa mwaka** | **Vielelezo vya deni vilivyo patikana kwaukaguzi** | **Tofauti** |
|---|---|---|---|---|
| Visiwani General Traders | Haujulikani | 120,790,100 | 40,081,020 | 80,709,080 |
| Russan Store | | 34,160,000 | Hana vielelezo | |
| Sabah Store | | 36,142,300 | 183,621,292 | 147,478,992 |
| Issa Ali Sefu | | 8,000,000 | Hana vielelezo | |
| Abdallah Iddi Abdallah | | 7,090,000 | Hana vielelezo | |
| Afisi ya Mapato (Farm-Earning) | | 127,012,505 | Hana vielelezo | |
| JKU | | 21,500,000 | Hana vielelezo | |
| Bi Naima Amour Shebe | | 387,267,000 | 341,734,000 | 45,533,000 |
| Amo Stationary Services | | 4,700,000 | Hana vielelezo | |
| Safiana Traders | | 65,500,000 | 65,507,000 | 7,000 |
| Juma Faki Salim | | 23,580,000 | 23,580,000 | Vimepatikana |
| M4 Hard Ware | | 11,500,000 | Hana vielelezo | |
| **Jumla** | | **847,241,905** | | |

**Majibu ya Chuo cha Mafunzo**

Ni kweli Chuo Cha mafunzo kilikuwa na madeni yapatayo 847,241,905/- ambayo vielelezo vyake baadhi havikuonekana wakati wa ukaguzi kutokana na muda mrefu wa madeni hayo, hata hivyo baadhi ya vielelezo hivyo vimeonekanwa na baadhi ya wahusika wamesha lipwa nakwasasa madeni hayo hatuna.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Makamanda wa Chuo cha mafunzo kukiri kuwepo kwa kasoro hiyo wakati Mkaguzi amefika Chuoni hapo. Hata hivyo, Kamati imebaini madeni hayo yalikuwa ni ya zamani ambayo Serikali iliyafanyia uhakiki na kulipwa madeni hayo yote, isipokuwa kuna madeni ambayo kweli yalikuwa yakidaiwa lakini hayakuthibitishwa (hayakuwa na vielelezo) hayajalipwa.

Baadhi ya madeni yaliyolipwa baada ya kuthibitishwa ni shilingi 573,640,142 kwa utaratibu ufuatao:-

| Nam. | Mzabuni/Mdai | Kiasi cha deni kilichothibitishwa |
|---|---|---|
| 1. | Naima Amar Shebbe | 341,734,000 |
| 2. | Visiwani General Traders | 150,009,810 |
| 3. | Safina Traders | 65,507,000 |
| 4. | Sabah Store | 16,389,332 |
| **Jumla** | | **573,640,142** |

Baadhi ya madeni ambayo hayajathibitishwa na kulipwa ni shilingi milioni 273,475,566. Aidha, Kamati yetu imebaini kuwa kuna baadhi ya madeni ambayo hayakupelekwa kwa Mkaguzi ili yaweze kuthibitishwa likiwemo deni la mkopo wa mabati lenye thamani ya shilingi 70,000,000 linalotokana na Mkataba wa miaka mitano kuanzia tarehe 2/9/2020 kati ya Chuo cha Mafunzo na Mfanyabiashara Moh'd Shaali Abeid unaohusu Ukopeshaji wa Mabati.

Kamati ilitaka kujua kwanini deni hilo halikulipwa na kuelezwa kwamba wakati Wahasibu walipokuwa wakiendelea kufanya marejesho kupitia kukata fedha kutoka katika mishahara ya Wafanyakazi, mikato hiyo ilisitishwa na kushindwa kupatikana fedha za kuwasilisha kwa Mtoa Huduma.

Kadhilika, Kamati imebaini kwamba kuna deni la SACCOS ambalo taarifa zake zimepelekwa ZAECA kwa uchunguzi zaidi ili iweze kubainika wadai halisi wanaohusika na kurejeshewa fedha zao.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Chuo cha Mafunzo kiangalie uwezekano wa kuwatafuta wote wenye vielelezo ikiwemo kuwaita Watoa Huduma hao (wenye mikataba) na kuyawasilisha madeni hayo Wizara ya Fedha na Mipango.
2. Chuo cha Mafunzo iwaite askari wote waliokopa na waliokopesha na kuwasiliza ili ikibainika wawasilishe madeni hayo Wizara ya Fedha na Mipango ili yaweze kulipwa kwani kuwepo kwa madeni hayo kunachafua utendaji mzuri unaofanywa na Serikali yetu.

### Hoja nambari 6.3.4.7: Ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali ya Umma shilingi 87,212,400

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Chuo cha Mafunzo kimefunga mikataba minne katika kutekeleza shughuli mbalimbali za uwendeshaji wa Chuo yenye thamani ya shilingi 1,371,916,000 kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 58: Ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Namba | Mtoa huduma | Namba ya Mkataba | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Karibu Phamarcy | SMZ/DO3/G/ RNCB/2020/ – 2021/01 | 52,349,500 | Kupatiwa madawa ya wanafunzi kwamwaka mmoja, Agosti 2020-2021 |
| 2. | Dundo | SMZ/DO3/G/ RNCB/2020 – 2021/02 | 154,525,000 | Kupatiwa sare za wanafunzi, mwaka Mmoja, Agosti 2020-2021 |
| 3. | Visiwani G. Supplier | SMZ/DO3/G/ RNCB/2020– 2021/03 | 603,626,500 | Kupatiwa vifaa vya ujenzi kwa kwa mradi Pemba, mwaka mmoja, Jan 2021- Feb2021 |
| 4. | RM2 | SMZ/DO3/G/ RNCB/2020– 2021/04 | 561,415,000 | Kupatiwa chakula cha wanafunzi kwamwaka mmoja, Agosti 2020-2021 |
| **Jumla** | | | **1,371,916,000** | |

Katika utekelezaji wa makubaliano ya mikataba hiyo ukaguzi umebaini Chuo cha Mafunzo kimefanya malipo yenye thamani ya shilingi 87,212,400 kinyume na makubaliano ya mkataba kwani imebainika kwa mujibu wa mkataba alipaswa anunue dawa kwa Karibu Pharmacy na badala yake alifanya manunuzi ya dawa kwa Magogoni Pharmacy yenye thamani ya shilingi 7,212,400 jambo ambalo halipo katika makubaliano ya mkataba wake wa awali.

Aidha, imebainika kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa chakula alipaswa kumlipa msambazaji RM2 Food Stuff na badala yake amelipwa Duka la Chuo cha Mafunzo malipo yenye thamani ya shilingi 20,000,000 jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya mkataba wa awali.

Vile vile imebainika kwa mujibu wa makubalino ya mkataba wa ununuzi wa chakula alipaswa kumlipa msambazaji RM2 Food Stuff na badala yake amelipwa Duka la Chuo cha Mafunzo malipo yenye thamani ya shilingi 60,000,000 jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya mkataba wa awali.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutekeleza makubaliano ya mkataba aliyofunga na watoa huduma mbali mbali jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma kwa kufanya malipo kwa duka la Chuo cha Mafunzo jambo ambalo litapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi mbali mbali kwa watoa huduma. Aidha, kufanya malipo yenye thamani ya shilingi 80,000,000 kwa Chuo cha Mafunzo ni kwenda kinyume na miongozo ya Baraza la Mapinduzi inayowataka

Wakuu wa Taasisi kuwacha kufanya malipo kwa njia ya fedha taslim (Cash Payment).

Kufanya malipo kinyume na makubaliano ya mikataba kunaweza kukapelekea kuingiza Serikali kwenye matatizo yasiyo ya lazima pale ambapo mtoa huduma atakapoamua kuishtaki Serikali na kupelekea Serikali kulipa fidia kubwa zaidi ya makubaliano ya kwenye mkataba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kufuata misingi na miongozo ya fedha ili kuepuka kuitia hasara Serikali inayotokana na uzembe wa kufanya maamuzi bora.

Mchanganuo wa malipo yaliyolipwa kinyume na makubaliano ya mikataba na watoa huduma mbali mbali ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 59: Malipo yaliyolipwa kinyume na makubaliano ya mikataba**

| Nam | Hati namba | Hundi namba | Alielipwa | Thamani(Shs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1/1/2021 | TISS | Magogoni Phamarcy | 7,212,400 | Malipo kwa ajili ununuzi wa madawa kwa mwezi wa Jan 2021.Kwa mujibu wa mkataba alipaswa kulipwa Karibu Pharmacy |
| 5 | 22/10/2020 | CASH | Duka chuo cha mafunzo | 60,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya chakula kwa uchaguzi Oct, 2020 Kwa mujibu wa mkataba alipaswa kulipwa RM2 FOOD STUFF |
| 6 | 20/12/2020 | Cash | Duka la Chuo Cha Mafunzo | 20,000,000 | Ikiwa ni malipo ya chakula kwa maafisa na wapiganaji. kwa mujibu wa mkata- ba alipaswa kulipwa RM2 FOOD STUFF |
| **Jumla** | | | | **87,212,400** | |

**Majibu ya Chuo cha Mafunzo**

Ni kweli Wakaguzi walipokuja waligundua kuna matumizi yaliyo fanyika pasi na makubaliano ya Mkataba na tukamlipa Magogoni Phamarcy na tulitakiwa tumlipe Karibu Phamarcy. Hii ni kwa sababu mwaka wa fedha 2019/2020, tulifunga Mkataba na karibu Phamarcy lakini kwa bahati mbaya ulipoingia mwaka wa fedha 2020/2021 tulikua na madeni hivyo tukaona ni busara kuondosha deni la nyuma tupate kuendelea na Mzabuni mpya.

Aidha tulimlipa Duka la Chuo cha Mafunzo 60,000,000/- na 20,000,000/- kwa ajili ya chakula wakati tuliofunga nao mkataba ni RM2 food staff. Hii ni kwa sababu fedha hizi tuliingiziwa kwa ajili ya matumizi ya 'standby' ya uchaguzi na hii haikuwemo katika bajeti ya chakula tulichofunga Mkataba na RM2 Food Staff.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Makamanda kukubaliana na kasoro alizozieleza Mkaguzi katika Ripoti yake. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kwamba ununuzi huo ulifanyika kwa maslahi ya Taifa letu na Maaskari wake. Hivyo, Kamati iliridhika na majibu hayo na haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.3.4.8: Malipo yasiyozingatia ushindani wa bei shilingi 95,908,055**

Ukaguzi umebaini Chuo cha Mafunzo kimetumia jumla ya shilingi 95,908,055 za mapato kwa ajili ya kupata huduma pamoja na manunuzi ya vifaa mbalimbali, dosari iliyobainika ni kutokuwepo kwa ushindani wa bei jambo ambalo linaweza kupelekea kufanyika kwa malipo ya bei ya juu ukilinganisha na uhalisia wa mahitaji yanavyopatikana kwa bei ya sokoni.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha unafanya matumizi kwa kuzingatia matakwa ya kanuni na sheria za fedha ili kuepuka kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 60: Malipo yasiyozingatia ushindani wa bei**

| Namba | Hati namba | Tarehe | Alielipwa | Thamani(Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 5/7/2020 | 9/7/2020 | Duka la ChuoCha Mafunzo | 15,109,000 | Malipo kwa ajili ya chakula navifaa vya usafi |
| 2 | 6/7/2020 | 10/7/2020 | Naima Amar Shebe | 12,500,000 | Malipo kwa ajili vifaa mbali mbali |
| 3 | 7/7/2020 | 16/7/2020 | Duka la ChuoCha Mafunzo | 15,000,000 | Malipo kwa ajili ununuzi wa dawa na mbolea |
| 4 | 7/8/2020 | 8/8/2020 | | 32,347,500 | |
| 5 | 21/10/2020 | 20/10/2020 | | 18,692,325 | Malipo kwa ajili matumizi mbali mbali |
| 6 | 22/10/2020 | 20/10/2020 | Kamishna Chuo ChaMafunzo<br><br>FN GLASSWORK | 2,259,230 | Matengenezo ya madirisha |
| **Jumla** | | | | **95,908,055** | |

**Majibu ya Chuo cha Mafunzo**

Wakanguzi walisema hakuna ushindani wa bei lakini ukiangalia stakabadhi zote utagundua vielelezo vyote vipo (Ankara tatu), vikiwemo profoma invoice, tax invoice, LPO, ambavyo vinaonesha ushindani wa Wazabuni, na vyote hivyo vimeambatanishwa

katika stakabadhi husika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Ilivyokuwa Makamanda wa Chuo cha Mafunzo walikubaliana na hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati yetu imebaini kwamba Chuo cha Mafunzo hawakuitisha zabuni badala yake walitafuta 'quotation' tatu na kumchagua Mtoa huduma. Kulingana na kiasi cha fedha kilichotumika, kwa mnasaba huo, Chuo cha Mafunzo kilitakiwa kuitisha zabuni kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi.

Kamati yetu ilichunguza zaidi hoja hiyo na kubaini kwamba kutokana na mazingira waliyokabiliana nayo yenye maslahi na Taifa letu Chuo cha Mafunzo hakikuweza kuviwasilisha vielelezo hivyo kwa Mkaguzi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati inakishauri kikosi cha Chuo cha Mafunzo kufuata kikamilifu Sheria na Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ili kuepuka hoja kama hizi kujitokeza na kutia dora utendaji wa Taasisi hiyo.
2. Kikosi cha Chuo cha Mafunzo kihakikishe kinampatia ushirikiano Mkaguzi anapokuja kutekeleza majukumu yake katika Ofisi zao ili waweze kumpatia vielelezo na kuepuka hoja zinazoweza kuepukika.

**Hoja nambari 6.3.4.9: Malipo yasiyo na Mkataba pamoja na vielelezo vinavyothibitisha huduma iliyotolewa shilingi 43,000,000**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 43,000,000 zimelipwa kwa ajili ya shughuli mbali mbali za utekelezaji wa mradi wa ujenzi Pemba, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa makubaliano ya mkataba pamoja na vielelezo vinavyothibitisha gharama halisi ya kazi iliyofanyika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi yaliyofanyika jambo ambalo limepelekea kushindwa kuthibitisha thamani halisi ya fedha na kiwango cha ujenzi kilichofanyika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuingia mkataba kwa ajili ya shughuli mbali mbali za utekelezaji wa mradi wa ujenzi ili kuweza kujiweka mahali salama pale zinapotokezea sintofahamu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 61: Malipo yaliyofanyika bila ya kuwepo kwa mkataba na vielelezo husika**

| Nam. | Hati Namba | Alielipwa | Kiasi cha fedha (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 1/8/2020 | Mahmoud Abdallah Ramadhan | 18,000,000 | Malipo ya Posho. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2. | 1/8/2020 | Said Ali Faki | 6,000,000 | Malipo ya Posho la mhandisi. |
| 3. | 1/9/2020 | Juma Faki Ali (Kubwa lijalo) | 19,000,000 | Malipo kwa utengenezaji wa milango. |
| **Jumla** | | | **43,000,000** | |

**Majibu ya Chuo cha Mafunzo**

Wakaguzi walipokuja waliona kuna baadhi ya malipo hayana mkataba lakini suala hilo liko hivi;-

a) Said Ali Faki kalipwa 6,000,000/- huyu ni Injinia ambae amefunga mkataba tokea ujenzi wa majengo ya Chuo cha Mafunzo unaanza.
b) Moh'd Abdallah Ramadhan kalipwa 18,000,000/- huyu ni Mkandarasi tulimpa kazi ya muda mfupi ya kusuka nondo na umwagaji wa zege na tumefunga nae mkataba.
c) Juma Faki Salim kalipwa 19,000,000/- huyu nimtoa huduma na amefunga mkataba na Chuo cha Mafunzo wa kututengenezea milango na madirisha.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba hoja ilitakiwa kuainishwa kama ni hoja ya kukosekana kwa Mkataba wa ujenzi na Wahandisi kutoka nje ya Chuo cha Mfunzo. Hili limeelezwa na Kamati baada ya kuambiwa kwamba Serikali inawapa Chuo cha Mafunzo fedha kwa ajili ya ujenzi ambapo wao wenyewe wanao mafundi wa kujenga, isipokuwa wanahitaji kuingia mkataba na wataalamu (technical person) kwa baadhi ya mambo ambayo yapo nje na uwezo (utaalamu) nayo. Kufuatia tathmini hiyo, Kamati ya PAC imeridhika na majibu hayo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Chuo cha Mafunzo kinapotaka kufanya ujenzi, kihakikishe kinautumia Wakala wa Ujenzi Zanzibar (ZBA) kwa wale wataalamu waliokuwa hawana ili iweze kuepuka kasoro kama hizi.

**Hoja nambari 6.3.4.10: Kutokatwa kwa kodi ya thamani (VAT) inayotokana na ununuzi na utoaji wa huduma shilingi 17,718,150**

Ukaguzi ulipitia hati mbalimbali zinazohusiana na malipo na kubaini kuwepo kwa hati za malipo zinazohusiana na manunuzi na utoaji wa huduma zenye thamani ya shilingi 118,121,200 ambazo zilistahiki kukatwa kodi ya ongezeko la thamani ya shilingi 17,718,150.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokukatwa kodi ya ongezeko la thamani na kuziwasilisha katika Ofisi inayohusiana na Mapato kwa mujibu wa sheria. Mchanganuo

wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 62: Kutokatwa kwa Kodi ya Ongezeko la thamani**

| Hati namba | Ankara namba | Aliyelipwa | Thamani(Tshs) | VAT (15%) |
|---|---|---|---|---|
| 1/8/2020 | 3689 | Visiwani General Supplies | 6,600,000 | 990,000 |
| 1/10/2020 | 3676 | | 72,461,200 | 10,869150 |
| 1/11/2020 | 3690 na 3691 | | 39,060,000 | 5,859,000 |
| **Jumla** | | | **118,121,200** | **17,718,150** |

Chuo cha Mafunzo kushindwa kukata kodi ya ongezeko la thamani kunapelekea kuikosesha Serikali mapato hali inayosababisha kutofikiwa kwa malengo yaliopangwa katika mpango mkakati wa Taasisi zinazosimamia kodi na Serikali ambapo kufanya hivyo ni ukiukwaji wa sheria, kanuni na miongozo ya kodi iliyowekwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha unasimamia suala zima la ukataji wa kodi ya ongezeko la thamani kwa kila manunuzi au huduma zinazotolewa ili kwenda sambamba na sheria ya kodi.

**Majibu ya Chuo cha Mafunzo**

Ni kweli Wakaguzi walipokuja waliona kuwa katika manunuzi ya bidhaa hizo hatujakata VAT 15% lakini kutokana na maelekezo ya Maafisa wa ZRB na TRA walituwekea semina na walitutaka tunapo fanya malipo ya bidhaa tukate asilimia tano (5%) kati ya hizo asilimia tatu (3%) iende ZRB na asilimia mbili ( 2%) iende TRA na makato hayo yamefanyika kama walivyotutaka tufanye.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini majibu ya hoja hii yanalingana na majibu ya hoja nambari 6.3.4.3.

**CHUO CHA MAFUNZO PEMBA**

Hoja **nambari 6.3.4.11: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 54,616,000**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 54,616,000 zimetumika kwa matumizi mbali mbali ya Chuo cha Mafunzo, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwepo kwa baadhi ya vielelezo pungufu vilivyoambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 63: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati namba | Hundinamba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tsh.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 06/07 20/07/2020 | 002100 ya 21/07/2020 | 5,868,000 | Kamanda Mkuu Chuo cha Mafunzo Pemba. | Malipo ya fedha kwa ajili ya mikato mbali mbali ya dharura wanayokatwa Maofisa na Wapiganaji |
| 18/08 21/08/2020 | 002122 ya 21/08/2020 | 8,360,400 | | |
| 08/09 21/09/2020 | 002134ya 21/09/2020 | 7,013,100 | | |
| 12/10 19/10/2020 | 002152ya 19/10/2020 | 13,615,500 | | |
| 23/11 25/11/2020 | | 10,717,600 | | |
| 14/12 23/12/2020 | 002196 ya 23/12/2020 | 9,041,400 | | |
| **Jumla** | | **54,616,000** | | |

**Majibu ya Chuo cha Mafunzo**

Ni kweli ukaguzi umebaini kwamba kuna mikato ya dharura ambayo walikua wakikatwa wapiganaji wa Chuo Cha Mafunzo ila mikato hii ni mikato kwa ajili ya madeni ambayo Wapiganaji walikua wakikopa ndani ya Idara kwa ajili ya kujikimu mambo mbali mbali pale wanapokutwa na shida. Vile vile, kuna baadhi ya Wapiganaji huletewa kesi za madeni kutoka nje (Uraiani), hivyo kwa kudhibiti kesi hizi zisiende Polisi, Idara ya Chuo Cha Mafunzo huchukua jukumu la kumkata Mpiganaji husika katika mshahara wake pale itakapothibitika na kukiri kwa kuwepo kwa deni hilo ila kuanzia mwezi wa kwanza mwaka 2021 mikato hii ilisitishwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Ilivyokuwa Makamanda wa Chuo cha Mafunzo wamekiri kuwepo kwa hoja hiyo awali. Na kwa kuwa tayari mikato hiyo imesitishwa tangu Januari, 2021. Kamati ya PAC haikuwa na maelezo zaidi.

**Hoja nambari 6.3.4.12: Utumiaji wa fedha za mapato bila ya kupelekwa benki shilingi 3,602,000/-**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Chuo Cha Mafunzo Pemba kinakusanya mapato kupitia vyanzo tofauti. Dosari iliyo bainika na ukaguzi ni kuwepo kwa ya baadhi kumbukumbu za makusanyo hayo katika vituo husika bila ya kupeleka banki ambapo baadhi ya kumbukumbu za makusanyo hayo zimekosekana kwa ukaguzi

Kufanya hivyo kunapelekea kuwepo kwa upotevu wa mapato hayo. Aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 30 cha usimamizi wa fedha za umma ya Zanzibar ya mwaka 2016 pamoja na kifungu nambari 23(1) na (4) cha kanuni ya usimamizi wa fedhaza umma ya mwaka 2021. Mchaganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini:-

**Jadweli nambari 54: Utumiaji wa fedha za malipo bila ya kupelekwa Benki**

| **Kituo** | **Fedha zilizo kusanywa** | **Fedha zilizo pelekwa banki** | **Fedha zilizotumika Bila ya kupelekwa benki (Tzs)** |
|---|---|---|---|
| Kituo cha Kengeja Mafunzo | 2,587,000/- | 375,000/- | 2,212,000/- |
| Kituo cha Kangagani Mafunzo | 1,114,000/- | 0 | 1,114,000/- |
| Kituo cha Tungamaa Mafunzo | 476,000/- | 200,000 | 276,000/- |
| **Jumla** | | | **3,602,000/-** |

**Majibu ya Chuo cha Mafunzo**

Ni kweli Wakaguzi walipokuja ilibainika kwamba Chuo Cha Mafunzo Pemba kimekusanya mapato kutoka katika vyanzo tofauti na katika baadhi ya vituo kama vile Kengeja, Kangagani na Tungamaa wametumia pesa za mapato bila ya kupelekwa benki kama utaratibu unavyoeleza, ila kwasasa tatizo hili tayari tumeshalipatia utatuzi wake na hakuna pesa itakayotumika vituoni kwani kila pesa inayokusanywa hupitia benki kwa kutumia 'control number' husika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Ilivyokuwa Makamanda wa Chuo cha Mafunzo wamekiri kwa hoja hiyo awali ilikuwepo. Na kwa kuwa tayari mikato hiyo imesitishwa tangu Januari, 2021. Kamati ya PAC haikuwa na maelezo zaidi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati kuendelea kufata utaratibu na miongozo na taratibu za malipo kulipa benk ili kuepusha upotevu wa mapoato Serikalini.

### 6.3.5 - FUNGU D04: KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) - UNGUJA

Ukaguzi wa hesabu za Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

#### Taarifa ya Mapato

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 30,384,688,766 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufi kia tarehe 30 Juni, 2021 Kikosi kilikusanya jumla ya shilingi 30,384,688,766 sawa na asilimia 100 ya makadirio.

#### Majibu ya KMKM na Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikupatiwa majibu ya Taarifa ya Mapato kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020. Hata hivyo, Kamati yetu ilitaka kujua kwamba KMKM wanavyanzo vingapi vya mapato na kujibiwa kuwa KMKM inacho chanzo kimoja tu cha mapato kinachuhusiana na ujenzi ndicho kinachochangia katika Serikali. Kadhalika, Kamati ilielezwa kwamba Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ndio inayowapangia kiasi gani cha fedha wanatakiwa wakusanye kutokana na chanzo hicho bila ya kufanyiwa tathmini halisi ya makusanyo kulingana na uwezo wa KMKM.

Kamati pia ilitaka kujua kwamba KMKM hawana vyanzo vyengine vya mapato na kujibiwa kuwa kwasasa wanavyo vyanzo vyao vya ndani vikiwemo utoaji wa huduma za afya, uvuvi wa samaki na ufugaji majongoo ya pwani.

Kamati yetu ilizipitia hesabu za mwisho wa mwaka na kugundua kwamba ‘Note 6’ inayotoa ufafanuzi wa ‘other receipts’ haikuwa na ufafanuzi wake kama zinavyotaka taratibu za kitaifa na kimataifa ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka. Kutokana na hilo, Kamati yetu ililazimika kuomba kupatiwa mchanganuo wa mapato na matumizi ya KMKM lakini kwa bahati mbaya hadi Kamati inakamilisha kazi zake za uchunguzi hakukuwa na mchanganuo uliowasilishwa.

#### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wizara ya Fedha na Mipango inapopanga makadirio yake ya mapato kwa KMKM inatakiwa ifanye tathmini juu wa uwezo wake wa kuweza kukusanya mapato hayo.
2. KMKM ihakikishe inakuwa makini inapofunga hesabu zake za mwisho wa mwaka ikiwemo kuweka ufafanuzi taarifa zote zilizoelezwa kwenye ‘Note’ husika pamoja na kuainishwa kwa vyanzo vyake vyote vya mapato.

#### Taarifa ya Matumizi

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 37,462,820,260 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufi kia

tarehe 30 Juni 2021 jumla ya shilingi 30,359,568,766 zimetumika sawa na asilimia 81 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati yetu imegundua kwamba kuna tofauti ya jumla ya matumizi yaliyotumiwa ambapo Mkaguzi alionesha (30,359,568,766) na KMKM ilionesha jumla ya shilingi 30,384,688 sawa na tofauti ya shilingi 25,120,000. Katika kulitafutia ufumbuzi suala hilo, Kamati imebaini kuwa tofauti hiyo ilitokana na Watumishi wa fedha kujumlisha jumla ndogo na kupelekea jumla ya fedha kuwa nyingi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa KMKM hususan Wahasibu wanatakiwa kuwa makini sana wakati kuandaa hesabu za mwisho wa mwaka ili tofati ya jumla ya miaka iweze kulingana.

**Hoja namba 6.3.5.1: Kukosekana kwa Mshika Fedha Mkuu**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kikosi cha Kuzuia Magendo kina wajibu wa kusimamia na kutekeleza shughuli mbali mbali zinazohusiana na usimamizi wa fedha za Serikali katika uendeshaji wa shughuli za kikosi dosari iliyobainika ni kukosekana kwa mshika fedha mkuu katika kitengo cha uhasibu ambaye ndiye mwenye jukumu la kulipa na kuweka kumbu kumbu mzuri za mapato na matumizi.

Kufanya hivyo kunapelekea kupunguwa kwa ufanisi juu ya suala zima la ulipaji na uwekaji wa kumbu kumbu za fedha ambapo ni kwenda kinyume na Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo.

**Majibu ya KMKM**

Mshika fedha Mkuu alikuwepo hapo kabla, ila kutokana na tatizo lililojitokeza la kusimamishwa kazi kwa mshika fedha aliyekuwepo na kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili, na haikujulikana lini mshika fedha huyo atarudi Uongozi kwa kutambua hilo ukachukua jitihada ya kumteua mshika fedha mwengine wa kikosi na tayari anaendelea na majukumu yake.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imeridhishwa na majibu ya KMKM kwa vile tayari Mshika Fedha huyo ameshakuwepo na anaendelea na majukumu yake pamoja na kwamba Maguzi alipokuwa akifanya kazi zake ni kweli Mshika Fedha huyo hakuwepo. Hivyo, Kamati yetu haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja namba 6.3.5.2: Kutokuainishwa kwa mapato ya shilingi 1,057,505,085.02 na matumizi ya shilingi 918,253,383 katika hesabu ya mwisho wa mwaka**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) kiliandaa na kuwasilisha mahesabu ya mwisho wa mwaka katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuainishwa kwa jumla ya shilingi 1,057,505,085.02 za mapato na shilingi 918,253,383 za matumizi katika hesabu ya mwisho wa mwaka yaliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kufanya hivyo kunapelekea kutokuonesha kwa sura halisi na sahihi ya hesabu za mwisho wa mwaka ya Kikosi cha Kuzuia Magendo. Mchanganuo wa mapato na matumizi ambayo hayakuainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 65: Mapato na Matumizi ambayo hayakuainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka**

| Maelezo | Mapato | Matumizi |
|---|---|---|
| Ujenzi wa Afi si ya Shirika la Bandari **(mapato yatokanayo na ujenzi)** | 572,031,260.02 | - |
| Kutoka katika vyanzo vya Afya KMKM na Pharmacy KMKM | 485,473,825.00 | - |
| Matumizi mbali mbali ya huduma za afya | - | 474,253,383.00 |
| Ununuzi wa vifaa kwa ujenzi wa Hanga 1, Hanga 2, Staff House, Mess, Hospital, Quorter guard (wete) | - | 350,000,000 |
| **Jumla** | **1,057,505,085.02** | **918,253,383** |

## Majibu ya KMKM

Taarifa za mapato na matumizi yatokanayo na miradi ya ndani ya kikosi hazikuwa zikiripotiwa katika hesabu ya fedha ya mwaka kwa miaka yote iliyopita, hivyo baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutushauri, shauri lao tumelichukua na kwa mwaka wa fedha uliofuata 2021-2022 taarifa za mapato na matumizi ya miradi ya ndani tayari zimeripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

## Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Pamoja na kwamba Makamanda wa KMKM kukiri kwamba kweli walikuwa hawakiingizi shilingi 1,057,505,085.02 za mapato na shilingi 918,253,383 za matumizi katika hesabu ya mwisho wa mwaka lakini Kamati ilitaka kujua sababu iliyopelekea hivyo na kuelezwa kwamba kwamba walikuwa hawana uelewa wa suala hilo. Kamati yetu ilienda ndani zaidi kwa kuhoji ni mapato gani ambayo hayakuwekwa wazi katika 'financial statement' na kujibi wa kwaba ni chanzo kinachotokana na utoaji wa huduma za afya zinazotolewa katika hospitali yao Kibweni.

Kamati haikufurahishwa na uzembe uliofanyika kwani hicho ni chanzo kinachoeleweka ambapo kutokionesha kunaweza kutumika kama mwanya wa kuchota mapato hayo na kuyatumia kinyume na mwelekeo wa taratibu za nchi yetu. Hivyo, Kamati imeungana na hoja ya Mkaguzi pamoja na kwamba kwa mwaka huu tayari kasoro hiyo imesharekebishwa.

**Hoja namba 6.3.5.3: Kutokulingana kwa fedha halisi iliyotumika na iliyowasilishwa kwenye hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 182,418,839**

Katika kupitia taarifa mbali mbali zikiwemo taarifa za Hesabu ya mwaka, daftari la kurikodia kumbukumbu za fedha pamoja na taarifa za matumizi. Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya taarifa zilizoripotiwa katika Hesabu za Mwisho wa Mwaka zinatofautiana na taarifa za hati za malipo.

Kutokulingana kwa fedha halisi iliyotumika pamoja na iliyowasilishwa katika hesabu za mwisho wa mwaka kunapelekea kutokuonyesha kwa uhalisia wa hesabu zilizowasilishwa ambapo ni kwenda kinyume na viwango vya ufungaji wa hesabu vya kitaifa na kimataifa. Mchanganuo wa taarifa hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 66: Fedha halisi iliyotumika na iliyowasilishwa kwenye hesabu za mwisho wa mwaka**

| Kifungu | Makadirio (Tshs.) | Thamani iliyoripotiwa katika taarifa za fedha (Tshs.) (A) | Kupitia hati za malipo (Tshs.) (B) | Thamani ya mkataba (Tshs.) | Tofauti Ya shilingi (Tshs.) (A-B) |
|---|---|---|---|---|---|
| Militaring Cataring | 1,267,800,000 | 1,244,827,289 | 1,062,408,450 | 626,964,000 | 182,418,839 |

## Majibu ya KMKM

Ni kweli ukaguzi umebaini kwamba kifungu cha Military Catering (fungu la chakula) kilivyoripotiwa katika taarifa ya Hesabu ya Mwaka kinatofautiana na taarifa za hati za malipo. Hii inatokana na kuwepo kwa ufinyu wa fedha za matumizi mengineyo (OC) tulizoingiziwa na kuna matumizi ya umuhimu yanajitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya kikosi ya kila siku na inatupasa kupunguza fedha katika kifungu cha Military Catering na kutumia kwenye matumizi mengine. Hii ndio iliyopelekea kuwepo kwa utofauti kati ya hati za malipo na thamani iliyoripotiwa katika taarifa ya fedha ya mwisho wa mwaka.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Pamoja na Makamanda wa KMKM kukubali kwamba kulijitokeza kasoro hiyo. Hata hivyo, Kamati imekemea vikali matumizi holela ya fedha za Serikali bila ya kuwepo nidhamu halisi ya matumizi husika, hasa ukizingatia kutolingana kwa fedha iliyotumiwa ya shilingi 182,418,839 ukilinganisha na taarifa iliyowasilishwa kwa Mkaguzi. Hizo ni fedha nyingi ambapo kimsingi Kamati ya PAC inaungana na hoja ya Mkaguzi na kueleza kwamba kiukaguzi fedha hizo zimeibwa.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Makamanda wa KMKM wanatakiwa kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma hususan kwa kuwasilisha taarifa zao za kifedha zinazoendana na uhalisia wa matumizi yaliyofanyika.
2. KMKM inapotaka kufanya uhaulishaji wa fedha kutoka kifungu kimoja na chengine, taratibu za uhaulishaji wa matumizi ya fedha hizo ufuatwe.

**Hoja nambari 6.3.5.4: Kukosekana kwa taarifa za fedha zilizohaulishwa shilingi 1,667,182,238**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Kuzuia Magendo KMKM kilipokea jumla ya shilingi 1,667,182,238 zilizohaulishwa kutoka (OR), Fedha na Mipango kupitia mfumo wa IFMIS kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwenda Canteen ya KMKM Zanzibar kwa vipindi tofauti, dosari iliyobainika ni kukosekana kwa taarifa za mapokezi na matumizi ya fedha hizo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa upokeaji pamoja na utumiaji wa fedha zilizohaulishwa kutoka Hazina.

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji wa kumbu kumbu za taarifa za fedha ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Kuzuia Magendo kuhakikisha kwamba unasimamia ipasavyo uwekaji wa taarifa za mapokezi na matumizi ya fedha za umma ili kuepusha kujitokeza kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za umma. Mchanganuo wa uhaulishwaji wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 67: Kukosekana kwa taarifa za fedha zilizohaulishwa**

| Tarehe | Hati namba R/Db | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilichohaulishwa (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 22-Jul-2020 | D04PV2000000021 | Canteen ya KMKM Zanzibar | 281,527,300.00 |
| 20-Aug-2020 | D04PV2000000063 | | 270,058,300.00 |
| 21-Sep-2020 | D04PV2000000094 | | 281,362,833.00 |
| 22-Oct-2020 | D04PV2000000129 | | 274,778,000.00 |
| 26-Nov-2020 | D04PV2000000164 | | 279,850,150.00 |
| 21-Dec-2020 | D04PV2000000187 | | 279,605,655.00 |

**Majibu ya KMKM**

Taarifa za mapokezi na matumizi ya jumla ya shilingi 1,667,182,238 zilikuwepo, mapungufu yaliyojitokeza ni kuwa wakati wa ukaguzi wakaguzi waliangalia daftari la mapato na matumizi lililoishia mwaka wa fedha 2019/2020 ambalo lilikuwa limeshajaa. Hivyo baada ya kutupa taarifa kupitia first draft report tukawapatia daftari la mwaka wa fedha husika 2020/2021 kwa ajili ya kulikagua na kupata taarifa sahihi za mapato na matumizi ya fedha hizo na kutuahidi kuwa wataiondoa hoja hiyo lakini kwa bahati mbaya hoja hiyo imerudi katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilizisikiliza hoja zote mbili za Makamanda wa KMKM na Mkaguzi na kugundua kwamba pamoja na Makamanda kuwasilisha daftari husika kwa Mkaguzi lakini muda waliowasilisha daftari hilo ulikuwa umepita muda wa ukaguzi uliowekwa kisheria (mwezi mmoja) na ndio maana hoja hii ikaingia ndani ya kitabu cha Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati yetu imelipitia daftari hilo na kugundua kwamba kweli taarifa hizo zilikuwemo ndani yake. Hivyo, Kamati ya PAC haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja namba 6.3.5.5: Malipo kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 2,246,867,100**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi. Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi kwa mujibu wa Sheria ambapo ukaguzi ulishindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa malipo hayo.

Kuwatumia watoa huduma ambao hawakusajiliwa hupelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na vifungu vya Sheria vilivyonakiliwa hapo juu. Mchanganuo wa malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na ZPPDA ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 68: Watoa huduma ambao Hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| **Na.** | **Mtoa Huduma** | **Hati namba** | **Fedha iliyolipwa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|

| | | | (Tshs) | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kemisy | T.T | 486,539,300 | Ununuzi wa Gari |
| 2 | Haroub Ali Suleiman | 1/4/2020 yenye Ununuzi wa Gari<br><br>hundi namba<br><br>000448 | 31,000,000 | |
| 3 | Mosal Trading Enterprises | T.T | 33,977,800 | Msambazaji wa Chakula |
| 4 | Ihsan | T.T | 62,540,000 | Ununuzi wa Gari |
| 5 | Rjr Group Srl | T.T | 1,632,810,000 | Malipo kwa ajili ya ushauri elekezi |
| **Jumla** | | | **2,246,867,100** | |

**Majibu ya KMKM**

Kuhusu mzabuni Kemisy, aidha Ununuzi wa gari kutoka Kemisy shilingi 486,539,300 kikosi cha KMKM kimemtumia mzabuni Kemisy kwasababu ni mzabuni alietumiwa na Serikali kwa malipo kupitia Wizara ya Fedha na Mipango katika ununuzi wa gari za Toyota Landcruiser Brand New 2020 kwa vikosi vyote vya ulinzi na usalama pamoja na Mradi wa Mji salama.

Kuhusu ununuzi wa gari kutoka kwa Haroub Ali Suleiman kwanza fedha iliyotumika kwa ununuzi wa gari hii ni faida ya kikosi iliyopatikana kutoka meli ya wachina iliyokuwa katika utafiti wa mafuta na sio fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serekali pia Ununuzi wake haukufanywa katika mwaka huu wa ukaguzi ulioripotiwa na ilikua ni 2019/2020.

Kuhusu Mzabuni Ihsan General Trader ni msajiliwa wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma na Certificate yake ya usajili ipo.

Kuhusu Mzabuni MOSAL ni msajiliwa wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma na Certificate yake ya usajili ipo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuifuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imegundua kwamba Mtoa huduma Ihsan General Traders kweli alisajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi isipokuwa usajili wake ulikuwa tayari umemaliza muda kwani alisajiliwa 2019/2020 na sio mwaka 2020/2021 ambao Mkaguzi aliufanyia kazi. Kwa mantiki hiyo, Kamati yetu inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kwamba kulikuwa na uzembe uliofanywa na Makamanda wetu.

Kwa upande wa Mosal Trading Enterprises, Kamati yetu imebaini alisajiliwa na Mamlaka mwezi Juni, 2021 wakati Watoa huduma Kemisy, Haroub Ali Suleiman pamoja na Rjr Group Srl Kamati iligundua kwamba kweli walikuwa hawakusajiliwa na Mamlaka

isipokuwa makamanda wa KMKM kwa kipindi hicho walipokea agizo kutoka Baraza la Mapinduzi kuhusu kuwapatia kazi hiyo kwa nia njema kwa vile kazi iliyokuwa ikihitajika kutekelezwa ilihitaji Watoa huduma maalum. Hivyo, Kamati imesisitiza kwamba pakitokezea mazingira kama iliyoelezwa, ni busara Makamanda wakatumia njia nyengine sahihi ambazo zimeelezwa katika Sheria zetu.

Kufuatia ukaguzi uliofanywa na Kamati yetu, tumebaini pamoja na kuwepo kwa kasoro katika manunuzi lakini hakukuwa na fedha ya Serikali iliyopotea.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kikosi cha KMKM kinapotaka kufanya kazi na Watoa Huduma watumie Watoa Huduma waliosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

### Hoja namba 6.3.5.6: Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu shilingi 33,977,800

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 33,977,800 kwa ajili ya ujenzi wa Bekar pamoja na ununuzi wa vifaa mbali mbali vya Bekar kwa lengo la uanzishwaji wa mradi wa kutengeneza mikate kwa matumizi ya Kambi na kutoa huduma hiyo kwa wananchi watakaohitaji, dosari iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za ujenzi na ununuzi wa vifaa kwa mujibu wa Sheria kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa bajeti ya ujenzi wa bekar pamoja na mchoro.
- Kukosekana kwa nukuu tatu kwa watoa huduma tofauti.
- Kukosekana kwa taarifa ya upembuzi yakinifu ya ujenzi wa bekari.
- Kukosekana kwa tathmini ndogo ya ujenzi.

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji taarifa zinazohitajika kwa matumizi ya baadae ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

### Majibu ya KMKM

Kuhusu ununuzi wa vifaa vya bekari shilingi 33,977,800 ufafanuzi ni kama ifuatavyo;-

Kikosi cha KMKM kilikubaliana na Kampuni ya Mosal Trading Enterprises kwamba kikosi kitakarabati jengo na ununuzi wa vifaa utafanywa na Mosal kama ni ubia na hayo yote yalifanyika lakini kufikia kwenye utekelezaji wa mkataba kwa maandishi tulishindwa kufikia makubaliano ya mgawanyo wa faida ndipo KMKM ikaamua kumlipa gharama za ununuzi wa mashine ya kutengenezea mikate ya bekari ili kikosi kibaki na mradi wa

bekari kwa kujitegemea wenyewe. Hii ndio sababu iliopelekea kutofanyika kwa taratibu za manunuzi kwasababu ununuzi ulifanywa na kampuni ya Mosal kama Mosal na sio kikosi cha KMKM.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imegundua kwamba malipo yaliyofanyika ya milioni 33,977,800 yalikuwa sahihi kwa vile malipo hayo yalitumiwa na Kampuni ya Mosal. Hata hivyo, Kamati imebaini kulikuwa na changamoto katika kifungu cha 5 cha Makubaliano ya awali (MoU) uliosainiwa tarehe 1/5/2021.

Katika kifungu hicho kilieleza kwamba iwapo kutatokea mgogoro baina ya Washirika, utatatuliwa kwa majadiliano na iwapo itashindikana basi pande iliyovunja makubaliano italazimika kununua vifaa vya Mshirika mwengine. Kamati imeenda ndani zaidi kwa kufikiria ingekuwaje iwapo KMKM ndio ingelivunja Makubaliano hayo, ingemlazimu kutumia gharama kubwa na kungekuwa na upotevu wa fedha za umma.

Kamati iliuliza kuhusu ufanisi wa bekari hivi sasa na kuelezwa kwamba Bekari hiyo inafanyakazi ipasavyo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

KMKM iwe makini inapoandaa makubaliano na Watoa Huduma ili kuepuka kuweka masharti yatakayokuwa magumu katika utekelezaji wake.

**Hoja namba 6.3.5.7: Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu shilingi 699,999,500**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo kwa msambazaji Mzalendo Hardware General kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa hanga namba 1, Hanga namba 2, Quorter guard, Hospital, Staff House, Messi na Msikiti. Dosari iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za ununuzi wa vifaa kwa mujibu wa Sheria kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa dondoo (minutes) za kikao cha Bodi ya Zabuni kilizopitisha maamuzi ya ujenzi.
- Kukosekana kwa Tangazo la zabuni ya ununuzi wa vifaa vya Ujenzi katika Gazeti.
- Kukosekana kwa taratibu za utayarishaji wa B.O.Q pamoja na uwasilishaji wa michoro.
- Kukosekana kwa ripoti ya tathmini.
- Kukosekana kwa ushiriki wa mshauri elekezi wa fedha katika timu ya tathmini.
- kukosekana kwa ushiriki wa Enginear katika timu ya tathmini.

- kukosekana kwa Afisa Manunuzi kutoka katika Taasisi nyingine.
- Kukosekana kwa kitabu cha zabuni kwa wazabuni.
- Kukosekana kwa viapo vya wajumbe wa timu ya tathmini.
- Kukosekana kwa Idhini ya Mwanasheria Mkuu ya kuendelea na taratibu za kufunga Mkataba.
- Kukosekana kwa Mkataba baina Mzabuni Mzalendo na KMKM.
- Kukosekana kwa ruhusa kutoka Mamlaka ya Manunuzi ya kuendelea na taratibu za Mkataba (Comment za Mamlaka).
- Kukosekana kwa ripoti ya Mshauri Elekezi.
- Kukosekana kwa report ya technical supporting.
- Kukosekana kwa Cheti cha malipo cha Mshauri Elekezi kabla ya kufanyika kwa Malipo.
- Kukosekana kwa ripoti ya kitaalamu (technical support report) baada ya kukabidhiwa vifaa.

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji wa taarifa zinazohitajika kwa matumizi ya baadae ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa manunuzi kinyume na taratibu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 69: Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu**

| Hati namba | Hundi namba | Fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 0001 na 0002 ya 8/9/2020 | T.T | 339,805,555 | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 28/6/2021 | | 10,193,945 | Malipo ya kodi ya zuio (ZRB) |
| … tarehe ya hati 29/4/2021 | CASH | 350,000,000 | Fedha kwa ajili ya ujenzi wa mahanga ya kulalia wapiganaji kikosi cha KMKM - Wete Pemba. |
| **Jumla** | | **699,999,500** | |

## Majibu ya KMKM

Kimsingi vielelezo vyote vipo vinavyohusiana na manunuzi na matumizi ya fedha shilingi 349,999,500 za ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa hanga namba 1, Hanga namba 2, Quorter guard, Hospital, Staff House, Messi na Msikiti katika kambi ya KMKM Kiuyu Pemba kwa Vote DO4 ya mwezi Septemba, 2020. Barua yenye kumbukumbu nambari KM/HQ/01E/01/2021 ya tarehe 18/01/2021 ambayo imewasilishwa kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar nayo pia imefafanua kuhusiana na ujenzi wa kambi KMKM Kiuyu Pemba.

Kimsingi vielelezo vyote vipo vinavyohusiana na manunuzi na matumizi ya fedha shilingi

za kitanzania milioni mia tatu hamsini (Tsh. 350,000,000/-) za ujenzi wa hanga la askari wa KMKM Wete Pemba kwa Vote DO4 ya mwezi Mei, 2021.

Fedha hizo kwa vile ziliingizwa karibu ya mwisho wa mwaka wa fedha 2020/2021, Kikosi kiliomba kwa Mamlaka ya Manunuzi kuzitumia fedha hizo za ujenzi kwa kutumia njia ya *force account* kwa barua ya tarehe 5/5/2021 iliyokwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Manunuzi Zanzibar yenye kumbukumbu namba KM/HQ/01C/41C/2021 ambayo imejibiwa kwa barua ya tarehe 18/5/2021 yenye kumbukumbu namba MUUMU.BA.370/383/04/31 barua ambayo ilizuia kutumika kwa njia ya *force account* na kusisitizwa kufuatwa kwa taratibu za manunuzi suala ambalo lilitekelezwa na Kikosi.

Kikosi baada ya kupata muongozo huo kutoka Mamlaka ya Manunuzi kilichukua hatua ya kufanya tenda kwa njia isiyo ya wazi (restricted tender) kupitia vikao vitatu (3) vya tarehe 10/6/2021, 9/7/2022 na 23/7/2021. Hatua hiyo iliendelea hadi kufikia kufanya *evaluation* na kupeleka Mamlaka ya Manunuzi kwa barua ya tarehe 12/07/2021 yenye kumbukumbu namba KM/HQ/01C/79B/2021.

Aidha Kikosi kilipokea majibu ya barua hiyo kwa barua ya tarehe 20/07/2021 yenye kumbukumbu namba MUUMU.CBA.164/406/10/16 ambapo Mamlaka ya Manunuzi ilielekeza kurejewa kwa mchakato huo kutokana na mapungufu waliyoainisha.

Pamoja na maelekezo hayo ya Mamlaka ya Manunuzi lakini kutokana na kuwa muda ulikuwa hautoshi kufanya upya mchakato wa tenda kulingana na mahitaji ya haraka ya uwepo wa hanga ili kuwahi kuwaweka Askari watakaokwenda Pemba kwenye Operesheni Karafuu, Kikosi kiliomba rasmi Wizara ya Fedha na Mipango kununua vifaa vya Ujenzi huo kwa njia ya dharura (Emargence Procurement) kwa barua ya tarehe 9/8/2021 yenye kumbukumbu namba KM/HQ/01C/92/2021 ambapo kufuatia maombi hayo ujenzi huo ulianza na kuendelea mpaka umefikia hatua ya kumaliza kuezekwa.

Baada ya kufikia hatua hiyo ujenzi huo ulilazimika kusita ili kuweza kutumika kwa matumizi ya ghafla na dharura ya makaazi ya askari kwa ajili ya kufanikisha mradi wa ujenzi wa madarasa na masoko ya Ahuweni ya Uviko 19 ambapo mafundi wengi walilazimika kuhamia Pemba ili kufanikisha ujenzi wa madarasa hayo.

Maombi hayo yaliwasilishwa kwa maandishi Wizara ya Fedha na Mipango kwa barua ya tarehe 29/04/2022 na yenye kumbukumbu namba KM/HQ/01C/66/2022 ambapo hadi ujenzi huo unasitishwa jumla ya fedha zilizotumika ni Shilingi za kitanzania 289,747,492 na kufanya fedha zilizosalia kuwa ni shilingi za kitanzania 60,252,508 na kufanya jumla ya fedha zote kuwa ni shilingi za kitanzania milioni mia tatu hamsini (Tsh. 350,000,000).

Kwa kuwa ujenzi huo umefanyika kwa matumizi ya njia ya dharura (Emargence Procurement) na kwa vile ujenzi huo matumizi yake hayajakamilika na ujenzi unaendelea ni kwamba utaratibu wa kisheria unaeleza kuwa vielelezo vyote kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango baada ya kukamilika ujenzi na matumizi ya fedha husika suala ambalo litafanywa na Kikosi.

Suala kama hilo limejitokeza kwa barua ya tarehe 26/08/2021 yenye kumbukumbu namba CAB.93/293/01/6 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambayo ilikuwa inatoa muongozo na maelekezo ya kuwasilisha taarifa za ununuzi uliofanyika chini ya kanuni ya 51 ya Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nam.11 ya 2016.

Aidha vielelezo vyote sahihi vinavyohusiana na ujenzi huo vipo na vimehifadhiwa vizuri ambapo muda wake ukifika vitawasilishwa kunakohusika kama ambavyo sheria inavyoelekeza. Hata hivyo CAG baada ya kutoviona vielelezo vya hanga la Wete alishindwa kuwasiliana na muhusika sahihi ili kupata majibu na ufafanuzi sahihi juu ya nyaraka za ujenzi huo.

Kwa upande wa pili ni kwamba nyaraka na vielelezo hivyo vya matumizi havikuonekana kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa sababu matumizi ya fedha hizo yamefanyika mwazoni mwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Aidha kwa vile suala la ujenzi wa madarasa limekamilika na fedha za kukamilisha ujenzi huo zipo, Kikosi kimeandika barua kwenda Wizara ya Fedha na Mipango kutoa taarifa ya kuendelea na umaliziaji wa hanga hilo kwa barua ya tarehe 31/08/2022 yenye kumbukumbu namba KM/HQ/01C/142/2022.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Baada ya kuchunguza kwa undani hoja hii, Kamati ya PAC haikuridhika na majibu ya Makamanda wa KMKM kwani inakubaliana na Mkaguzi kwamba matumizi ya fedha (shilingi 699,999,500) hayakufuata taratibu kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma. Kamati imefikia maamuzi haya kwa vile matumizi ya njia za ununuzi ambayo KMKM imeitumia yaan Forced Account au Restricted Procurement, ilitumiwa bila ya kupata ruhusa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Lakini kama hiyo haitoshi, ni utaratibu wa kisheria kwamba ruhusa ya matumizi ya njia ya 'forced account' ni lazima ipatikane ruhusa kutoka kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kitu ambacho hakijafanyika.

Kwa upande wa matumizi ya shilingi milioni 350,000,000 zilizotumika kwa ajili ya ujenzi wa mahanga ya kulalia wapiganaji kikosi cha KMKM - Wete Pemba kwa njia ya 'Restricted Procurement', ilitumika pasi na kupata ruhusa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambapo kiutaratibu ni lazima ruhusa itoke ya kuendelea na matumizi ya fedha na ndio matumizi yafanyike.

Kwa mantiki hiyo, Kamati inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kwamba katika utekelezaji wa Miradi hii, KMKM haukufuta taratibu za manunuzi kama inavyoelekezwa na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Hivyo, hoja hiyo imebakia na haikupata majibu ya kuridhisha.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kikosi cha KMKM kihakikishe kinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma hususan inapofanya matumizi ya fedha za Umma kwa maslahi ya Umma.

**Hoja namba 6.3.5.8: Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu Shilingi 575,499,205.56**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 575,499,205.56 kwa wasambazaji Kemisy Investment Co. LTD, Haroub Ali Suleiman pamoja na Ihsan General Traders kwa ajili ya ununuzi wa gari sita (6) zishazotumika (used car).

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa gari hizo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Hata hivyo ukaguzi umebaini KMKM imekiuka muongozo wa Baraza la Mapinduzi wenye kumbukumbu namba BLM/97/M/C.5/VOL.V/27 wa tarehe 27 Septemba 2021 kutoka Serikalini uliotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kuwaagiza Wakuu wote wa Taasisi kuwasilisha maombi ya ununuzi wa gari kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na kuacha kununua magari yaliyotumika (Used Car) pamoja na kuacha kununua magari kwa Wazabuni binafsi kwa lengo la kununua gari kwa thamani kubwa kuliko bei ya sokoni ambapo KMKM imenunua gari sita zilizotumika (Used Car) bila ya kupata ridhaa ya kibali kutoka kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Hata hivyo, ukaguzi haukuweza kupatiwa Ripoti ya Ukaguzi wa gari hizo (Inspection Report) kutoka kwa Fundi Mkuu wa Karakana ya Serikali kwa vile gari hizo hazikufanyiwa uchunguzi wa kina kujua umadhubuti na uzima wa gari hizo, ukaguzi haukuweza kupatiwa hati ya mapokezi ya gari hizo (Delivery Note).

Kufanya manunuzi kinyume na matoleo ya Serikali kunapelekea taasisi ya umma kutumia gharama kubwa ya ununuzi unaotokana na wazabuni kuwauzia Serikali magari kwa gharama kubwa ukilinganisha na bei ya soko ilivyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa manunuzi kinyume na taratibu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 70: Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu**

| Hati namba | Hundi namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| PV 13/7/2020 | T.T | Ihsan General Traders | 62,540,000.00 | Ununuzi wa gari ya Fuso kwa ajili ya kikosi cha Kmkm |
| Pv 1/4/2020 ya 3/4/2020 | | HAROUB ALI SULEIMAN | 31,000,000.00 | Ununuzi wa gari ya Center Dyna kwa matumizi ya Kikosi. |
| | Dummy | Kemisy Investment Co Ltd. | 289,534,775.56 | Malipo ya 60%(124,222.80). Kwa ununuzi wa gari tatu mpya USD 207,038 kwa matumizi wa kikosi. |
| | | | 192,424,430.00 | Malipo ya 40%(82,815). Kwa ununuzi wa gari tatu mpya USD 207,038 kwa matumizi wa kikosi. |
| **Jumla** | | | **575,499,205.56** | |

## Majibu ya KMKM

Gari used yenye PV 1/4/2020 ya tarehe 3/4/2020 imetokana na mradi wa meli ya utafiti wa mafuta na gesi baharini uliofanywa na Kampuni ya RAK GAS pamoja na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Shirika la Bandari Zanzibar. Maombi ya ununuzi wa gari hizo yamefanyika kwa kupitia barua ya tarehe 3/7/2019 na vocha Namba 12/2/2020.

Msingi mkuu wa ununuzi wa gari hizo ni mahitaji ya dharura ya gari za doria za ulinzi katika kipindi cha matayarisho ya Uchaguzi Mkuu wa Dola wa 2020 ambapo kikosi kilikuwa na uhaba wa gari kwa ajili ya kufanikisha shughuli za ulinzi na usalama katika kipindi cha uchaguzi.

Ununuzi wa gari hizo ulilenga zaidi maslahi ya taifa na uliwezesha kupunguza changamoto ya ukosefu wa gari upande wa Unguja na Pemba na kupelekea Kikosi kufanikisha majukumu yake ya doria na usafirishaji wa askari kipindi cha uchaguzi kwa ufanisi mkubwa.

Kuhusu ununuzi wa gari kwa mzabuni Kemisy Investment Co. Ltd, gari hizo zimenunuliwa mpya na hazikua zimeshatumika (used) na malipo yamefanywa na Wizara ya fedha na Mipango kupitia dummy.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba ununuzi wa gari zilizotajwa ulifanyika kwa maagizo ya Serikali kwa lengo la kufanikisha kazi maalum. Hata hivyo, KMKM ilitakiwa kuandaa RIpoti itakayokuwa ikieleza kwa undani chanzo chake na maamuzi yaliyofikiwa ili iwe kielelezo kitakachotumika wakati Mkaguzi atakapokuwa anatekeleza kazi zake.

Kadhalika, Kamati imebaini kwamba gari tatu kati ya sita zilikuwa ni gari mpya wala sio gari zilizokuwa zimetumika kama ilivyoelezwa katika Ripoti ya Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati iliridhika na maelezo ya majibu iliyopatiwa kwani ni kweli kwamba kwa kipindi husika kulikuwa na dharura ya ununuzi wa gari kwa matumizi maalum.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kikosi cha KMKM kihakikishe kinatekeleza Sheria za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwani Sheria hiyo inaruhusu na kutambua ununuzi wa dharura iwapo kutatokea maagizo ya namna hiyo.
2. Pamoja na kwamba kulikuwa na agizo lililohitaji utekelezaji, Kikosi cha KMKM kihakikishe maagizo kama hayo yakitolewa wanayaandalia Ripoti maalum itakayojumuisha sababu za ununuzi, Mnunuzi na Maamuzi yatakayoamuliwa pamoja na saini za Waziri, Mkuu wa KMKM na wahusika wengine.

**Hoja namba 6.3.5.9: Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu shilingi 634,901,500**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 634,901,500 kwa wasambazaji Baba Three Store (Julai hadi Disemba) na MR2 FOOD STUFF (Febuari hadi Aprili) kwa ajili ya ununuzi wa chakula kwa askari waliopo kambini, dosari iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za ununuzi wa chakula kwa mujibu wa Sheria kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama ifuatavyo:-

- Kutokutangazwa kwa zabuni ya Wazi.
- Kukosekana kwa barua kutoka Mamlaka ya ununuzi iliyowaruhusu kutumia njia ya (Restricted).
- Kukosekana kwa fomu za wajumbe za viapo kwa timu ya tathmini (Code of Ethic).
- Kukosekana kwa barua za kuwajulisha walioshiriki mchakato wa zabuni kupitia kanuni namba 141 (1).
- Kukosekana kwa idhini ya Mwanasheria Mkuu inayoruhusu kuendelea na mkataba.
- Kukosekana kwa taarifa ya mapokezi ya bidhaa (Delivery Order).
- Kukosekana kwa hadidu rejea (TOR) inayoonyesha malipo yatalipwa kwa awamu ngapi.

- Kukosekana kwa Usajili wa Mtoa huduma kutoka Mamlaka ya Manunuzi.
- Kukosekana barua ya kuzawadiwa ushindi (Awarded latter). Taarifa ya tathmini ya mchakato wa kumpata BABA THREE ya 22/10/2018 mpaka 31/10/2018 ripoti ya tathmini inaeleza kuwa, alipitishwa kwa shilingi 626,964,000
- Kukosekana kwa mkataba baina ya mtoa huduma MR2 na Kikosi. (mkataba ulioambatanishwa kutoka kwa mtoa huduma BABA umefungwa 5/12/2019)
- Kukosekana kwa idhini kutoka Mamlaka ya Manunuzi baada ya report ya tathmini kukamilika.
- Kukosekana kwa hati ya makubaliano ya punguzo la bei kwa ukaguzi (Negotiation report)

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji wa taarifa zinazohitajika kwa matumizi ya baadae ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

### Majibu ya KMKM

Kuhusu taratibu za manunuzi juu ya ununuzi wa chakula zimefuatwa, aidha baadhi ya document ambazo zimeripotiwa kuwa hazipo na wakaguzi document hizo zipo kama vile;-

- Barua za kuwajulisha walioshiriki mchakato wa zabuni kupitia kanuni ya 141(1).
- Taarifa ya mapokezi ya bidhaa (Delivery Order).
- Usajili wa Mtoa huduma kutoka Mamlaka ya Manunuzi.
- Barua ya kuzawadiwa ushindi (Awarded latter).
- Mkataba baina ya mtoa huduma MR2 FOOD STUFF na Kikosi.

Aidha kutokutangazwa kwa zabuni ya wazi kwa ununuzi wa chakula cha wapiganaji, kawaida zabuni hiyo kwa Idara Maalum za SMZ huwa hazitangazwi na hufanywa kwa zabuni isiyo ya wazi (Restricted).

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kwamba Kikosi cha KMKM kwa kiasi kikubwa ilishindwa kufuata taratibu za ununuzi wa chakula kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kwani pamoja na Kikosi kutumia njia ya zabuni ya 'Restricted' lakini ilitakiwa kuwepo kuwajulisha wote waliopatiwa zabuni hata kama hajashinda na kuwajulisha sababu za kushindwa kwao na sio kumjulisha mshindi pekee, Mkaguzi hakupatiwa vielelezo stahiki pamoja na mkataba haukupata idhini ya mwanasheria Mkuu.

Vile vile, Kamati haikupatiwa usajili wa Mtoa huduma kutoka Mamlaka ya Manunuzi, barua za kuwajulisha walioshiriki mchakato wa zabuni kupitia kanuni namba 141 (1) pamoja na kukosekana kwa barua kutoka Mamlaka ya ununuzi iliyowaruhusu kutumia njia ya (Restricted). Kutokana na kuwepo kasoro nyingi, Kamati yetu imepata mashaka kuhusu matumizi ya shilingi 634,901,500 kwamba hayakufuata utaratibu. Hivyo, Kamati ya PAC haikuridhika na majibu ya Kikosi na hoja imebakia.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kikosi cha KMKM kihakikishe kinafuata taratibu zilizoelezwa na Sheria ya Manunuzi hususan kabla, wakati na baada ya kufanya ununuzi wowote.
2. Kutokana na fedha za umma zilizopotea, Vyombo husika vifuatilie kwa karibu manunuzi yaliyofanyika ili waweze kubaini uhalisia wa matumizi ya shilingi 634,901,500 na kama kuna wahusika wowote walishiriki katika upotevu huo basi Sheria za nchi zichuue nafasi yake.

**Hoja namba 6.3.5.10: Malipo ya ujenzi yaliyofanyika kinyume na taratibu Shilingi 1,861,710,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 1,861,710,000 kwa wajenzi na wasambazaji Mzalendo Hardware General Supplies, Ihsan Supplier General Traders pamoja na Mkuu wa KMKM kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo tofauti, dosari iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za ujenzi na ukarabati wa majengo tofauti kwa mujibu wa Sheria kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa Minutes za vikao vya Bodi ya Zabuni zilizopitisha maamuzi ya ujenzi.
- Kukosekana kwa Tangazo la zabuni ya ununuzi wa vifaa vya Ujenzi katika Gazeti.
- B.O.Q imefanyiwa marekebisho ya thamani bila ya kusainiwa na Engineer.
- Ripoti ya Enginear haikupatikana kwa ukaguzi kupitia kanuni ya manunuzi 118.
- Kukosekana kwa ushiriki wa mtaalam wa fedha katika timu ya tathmini.
- Kukosekana kwa ushiriki wa Enginear katika timu ya tathmini.
- Kukosekana kwa Afi sa Manunuzi kutoka katika Taasisi nyingine.
- Kukosekana kwa Tender Document za wazabuni wasiopungua watatu (3).
- Kukosekana kwa viapo vya wajumbe wa evaluation team.
- Kukosekana kwa Idhini ya Mwanasheria Mkuu ya kuendelea na taratibu za kufunga Mkataba.
- Kukosekana kwa saini kwa upande wa anaepokea huduma (Purchaser).
- Kukosekana kwa sahihi za awali katika mkataba uliofungwa 22/6/2021.
- Kukosekana kwa ruhusa kutoka Mamlaka ya manunuzi baada ya taarifa ya

tathmini. kwa ajili ya kuendelea na taratibu za Mkataba.
- Kukosekana kwa ripoti ya Mshauri Elekezi (Consultance).
- Kukosekana kwa TOR inayoonyesha malipo yatalipwa kwa awamu ngapi.
- Kukosekana kwa “Certificate” ya Mshauri Elekezi kabla ya kufanyika kwa Malipo.

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji wa taarifa zinazohitajika kwa matumizi ya baadae ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa Mchanganuo wa malipo ya ujenzi kinyume na taratibu yanaonekana katika Jadweli Nambari 71 ya Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021.

**Majibu ya KMKM**

Kwa kawaida KMKM hutumika kama mzabuni kwa zabuni zote tunazopokea kutoka taasisi za Serikali ambapo taratibu zote za manunuzi hufanywa na taasisi husika, hivyo KMKM hupokea malipo kwa ajili ya kukamilisha ujenzi husika ambapo KMKM hutegemea faida, hivyo hatuwezi kutangaza zabuni ndani ya zabuni kwani itapelekea kupanda kwa gharama na kutokumalizika kwa kazi husika kwa muda uliopangwa, aidha kazi hizo kwa Idara Maalum hufanywa kwa uzalendo na gharama nafuu kwa maslahi ya Taifa na wakati mwengine huwa ni maagizo maalum kutoka Serikalini.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati haikuridhishwa na majibu ya kikosi cha KMKM ambapo Kamati imefanikiwa kuoneshwa baadhi ya vielelezo vikiwemo mikataba ya ujenzi lakini lakushangaza vielelezo hivyo havikuwa na alama ya kuonesha Mkaguzi alipatiwa, amevipitia na kukubaliana navyo.

Hivyo, Kamati ya PAC inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kwamba Makamanda wa Kikosi hawakuw makini walipokuwa wakifanya malipo ya ujenzi kwa yaliyofanyika kinyume na taratibu na kupelekea upotevu wa shilingi 1,861,710,000

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kikosi cha KMKM kifuate Sheria za Ununuzi inapotekeleza shughuli zake ili kuepusha hoja nyingi za Mkaguzi kujitokeza.
2. Kwa vile kuna fedha nyingi za ujenzi zilizotumika kinyume na utaratibu, Sheria ichukue mkondo wake kwa wale wote watakaochunguzwa na vyombo vya uchunguzi au usimamizi wa sheria na kuthibitika kwamba wanahusika na upotevu wa fedha hizo.

**Hoja namba 6.3.5.11: Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu Shilingi 344,146,772.9**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 344,146,772.90 kwa ajili ya ununuzi wa Dawa za binaadamu na vifaa tiba kwa wasambazaji tofauti kama wanavyoonekana katika jadweli hapo chini, dosari iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa mujibu wa Sheria kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama ifuatavyo: -

- Kutokuingizwa katika mpango wa manunuzi wa taasisi

- Kutokuwepo kwa ushindani wa zabuni
- Kutokuwepo kwa mkataba wa ununuzi wa dawa hizo
- Kukosekana kwa taarifa za upokeaji wa dawa hizi (delivery note)
- Kutokuwepo kwa utaratibu wa stock taking katika duka la Madawa hayo
- Kutokuwepo kwa bajeti ya matumizi hayo

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji wa taarifa zinazohitajika kwa matumizi ya baadae ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu yanaonekana katika Jadweli Nambari 72 ya Kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021.

#### Majibu ya KMKM

Ununuzi wa dawa za Hospital ni sehemu ya mradi wa ndani wa kikosi cha KMKM, hivyo haukuwahi kuingizwa kwenye mpango wa manunuzi wa taasisi kwa miaka yote iliyopita na wala hatukuwahi kupata muongozo unaotuongoza juu ya suala hili, kwasababu mradi huu unajitegemea na wala haupati fungu kutoka Serikali Kuu (bajeti).

#### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Pamoja na kwamba mradi w ununuzi wa dawa na vifaa tiba sio mradi ulioanzishwa na Serikali lakini Kikosi cha KMKM kinafanyakazi ikiwa ni Taasisi ya Serikali, hivyo mambo inayoyaanzisha yanatakiwa yafanyika wa mujibu wa Sheria za Zanzibar. Kwa matiki hiyo, Kamati inakubaliana na hoja ya Mkaguzi na kusisitiza kwamba ununuzi wa dawa na vifaa tiba uandaliwe mpango wake wa manunuzi kama zinavyoelekeza Sheria.

#### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kikosi cha KMKM ihakikishe inaviainisha vyanzo vyake vyote katika bajeti yake na kuvitekeleza kwa mujibu wa sheria za nchi.

#### Hoja nambari 6.3.5.12: Malipo kwa Mshauri Elekezi wa Upembuzi Yakinifu wa Ujenzi wa Chelezo cha KMKM kinyume na taratibu shilingi 1,632,810,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 1,632,810,000 kwa Mshauri RJR GROUP SRL kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Chelezo cha KMKM, dosari iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za kumpata Mshauri Elekezi huyo kwa mujibu wa Sheria kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa tangazo la kumtafuta Mshauri Elekezi.
- Kukosekana kwa Kibali cha ruhusa kutoka Wizara ya Fedha.
- Kutotangazwa kwa zabuni.
- Kukosekana kwa Ripoti ya tathmini (Evaluation Report).
- Kukosekana kwa mkataba.
- Kukosekana kwa barua kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ya kuendelea na kufunga mkataba.
- Kukosekana kwa barua kutoka Mamlaka ya Manunuzi inayotoa ruhusa ya kuendelea na taratibu za kuendelea na kufunga mkataba.
- Kukosekana kwa Bid Security ya mtoa huduma (bank guarantee).
- Kukosekana kwa document za Wazabuni.
- Kukosekana kwa report kabla ya kuanza kazi na baada ya kumaliza kazi.
- Kukosekana kwa 'Certifckete' kabla ya muendelezo wa malipo inayoruhusu kumlipa.

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji wa taarifa zinazohitajika kwa matumizi ya baadae ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa Malipo kwa Mshauri Elekezikinyume na taratibui kinyume na taratibu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 73 : Malipo kwa Mshauri Elekezi wa upembuzi yakinifu wa Ujenzi wa Chelezo cha KMKM kinyume na taratibu**

| Hati ya malipo | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| (Dummy) | RJR GROUP SRL | 584,220,000 | Asilimia 30% ya mshauri Elekezi wa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa chelezo cha Kmkm yenye thamani ya Euro 210,000 ( ex tzs 2,782 (malipo yote ni Euro 700,000) |
| | | 1,048,590,000 | Ikiwa ni asilimia 30% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ya mwisho ya Mshauri elekezi wa upembuzi yakinifu wa Ujenzi wa Chelezo yenye thamani<br><br>ya Euro 210,000 na Malipo ya **Chuo cha Mafunzo** ya Uzamiaji yenye jumla ya Euro 156,000 (**exchenge rate**<br><br>**2,865**) |
| **Jumla** | | **1,632,810,000** | |

**Majibu ya KMKM**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kiliingia mkataba na kampuni ya RJR GROUP SRL kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Chelezo cha KMKM ikiwa ni muendelezo wa mradi wa vituo vya uzamiaji na uokozi, aidha mradi huu kuanzishwa kwake ni kupitia Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kutokana na barua yenye kumbukumbu nambari KM/HQ/01C/118/2019 pamoja na mazungumzo yaliyofanyika Wizara ya Fedha na Mipango na kikao cha tarehe 17/01/2020 kilichofanyika Ofisini kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhusiana na mada ya kazi ya upembuzi yakinifu kwa ujenzi wa chelezo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba kutokana na unyeti wa kazi ya ujenzi wa Chelezo hicho, kulikuwa na agizo maalum lililotolewa na Baraza la Mapinduzi ambalo lilielekeza jinsi gani kazi hiyo ifanyike ikiwemo uteuzi wa Mshauri Elekezi wa kufanya upembuzi yakinifu. Hata hivyo, kutolewa agizo ni jambo moja lakini utekelezaji wa agizo hilo ni jambo jengine.

Kikosi cha KMKM baada ya kupokea agizo husika ilitakiwa ilitekeleze kwa kufuata sheria zilizopo ikiwemo kuwepo kwa barua kutoka Mamlaka ya Manunuzi inayotoa ruhusa ya kuendelea na taratibu za kufunga mkataba pamoja na kuwepo kwa mkataba husika. Hivyo, Kamati imekubaliana na hoja ya Mkaguzi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kikosi cha KMKM pamoja na kupokea maagizo ihakikishe inayatekeleza kwa mujibu wa Sheria za nchi.

**Hoja nambari 6.3.5.13: Kutumika kwa fedha za Klabu ya michezo kinyume na taratibu shilingi 55,080,000**

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefungua hesabu ya benki nambari 0405792000 (Michezo KMKM) kwa lengo la kuhifadhi mikato (michango) kutoka kwa wafanyakazi ambayo itatumika kwa ajili ya kugharamikia shughuli zote za klabu ya michezo KMKM. Mkuu wa Utawala na Mhasibu Mkuu wa KMKM ndio wenye dhamana ya hesabu hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 55,080,000 kutoka katika hesabu nambari 0405792000 (Michezo KMKM) zilitumika kwa ajili ya matumizi ya huduma za kiutawala na uendeshaji.

Aidha, taarifa za matumizi hayo hazikuainishwa katika ripoti za utekelezaji wa mpango wa manunuzi, ripoti za utekelezaji mpango kazi wala kuainishwa katika taarifa ya fedha ya mwaka, Matumizi hayo yapo nje ya mipaka iliyowekwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 46(6) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Jadweli Nambari 74: Fedha za Klabu zinazotumika kinyume na utaratibu**

| **Tarehe** | **Maelezo** | **Kiasi (Tshs)** | **Aliyelipwa** |
|---|---|---|---|
| 08/09/2020 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa kofia za BOTSWANA kwa Afisa Wanafunzi - aliyelipwa ni (IHSANI GENERAL TRADERs) | 27,960,000 | Michezo KMKM |
| 23/09/2020 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa Fiber, machine 2 na Bettry 38. (AL -NABHANY AUTO MOBILE) | 27,120,000 | Michezo KMKM |
| **Jumla** | | **55,080,000** | |

**Majibu ya KMKM**

Ni kweli wakati wa ukaguzi wakaguzi walibaini kwamba jumla ya shilingi 55,080,000 kutoka katika hesabu nambari 0405792000 (Michezo KMKM) zilitumika kwa ajili ya matumizi ya huduma za kiutawala na uendeshaji wa kikosi, hii ni kutokana na kutopatikana kwa wakati fedha za matumizi ya kazi za kawaida kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na wakati mwengine kutokupata kabisa jambo ambalo lilipelekea kikosi kuangalia ni eneo gani lenye fedha ili kuweza kuhami hali ya matayarisho ya matumizi kwa ajili ya kufanyia services vyombo vya KM Bawe na KM Misali kwa dharura, ununuzi wa faiba boat na mashine mbili  pamoja na ununuzi wa kofia za Botswana kwa sherehe ya kuwatoa maafisa wapya wa KMKM kwenye chuo chake huko Kama.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Makamanda wa KMKM wamekiri kuwepo kwa kasoro hiyo, Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Makamanda wa KMKM kutokana na dharura maalum ya ulinzi na usalama wa Taifa letu iliyokuwepo kwa wakati huo. Hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile fedha hizo zinatokana na michango ya wafanyakazi kwa lengo la kuendeleza michezo, Kikosi cha KMKM kihakikishe fedha hizo zinarudishwa katika hesabu (account) yake.

**Hoja nambari 6.3.5.14: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 1,170,874,800**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 1,170,874,800 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Kikosi cha kuzuia Magendo, dosari iliyobaini ni kukosekana kwa hati za malipo na vielelezo vinavyothibitisha matumizi ya fedha hizo.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali rejea Jadweli Nambari 75 lililoelezwa katika Ripoti ya Ukaguzi wa Taarifa ya Fedha za Serikali Kuu kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021 linalohusiana na hati za malipo zilikosekana kwa ukaguzi

**Majibu ya Hoja**

Mapendekezo ya wakaguzi ya kututaka kufuata sheria kwa kutumia hati za malipo pasi na kutumia TT kama ni vocha au hati ya malipo, huko awali tulikua tunafanya malipo kupitia TT kama ni hati za malipo zinazojitosheleza ili kutofautisha hati za malipo za

bank na hati za malipo ya mkononi na wakaguzi walikua wanakagua kama wanavyokagua hati za malipo nyengine, ila kwasasa shauri lao tumelipokea na tayari limeshafanyiwa kazi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile ushauri wa Mkaguzi umepokelewa na kufanyiwa kazi ipasavyo, Kamati yetu haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.3.5.14: Hati za malipo zilizokosa idhini ya malipo ya Mkuu wa KMKM shilingi 291,710,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 291,710,000 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Kikosi cha Kuzuia Magendo KMKM kupitia hati za malipo mbali mbali, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuidhinishwa kwa malipo hayo katika hati za malipo husika na Mkuu wa KMKM ambapo kunapelekea kutokuthibitika kwa malipo yaliyofanyika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo ya hati hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 76: Hati za malipo zilizokosa idhini ya malipo ya mkuu wa KMKM**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Pv 3/7/2020 | Ihsan General Traders | 27,380,000 | Mkuu wa KMKM | Muendelezo wa ukarabati wa nyumba za maendeleo Michenzani block no 1 |
| Pv 19/8/2020 | | 97,515,000 | | Ununuzi wa vifaa kwa muendelezo wa Ofisi ya Shirika la Bandari Zanzibar |
| Pv 20/8/2020 | | 50,600,000 | | Ununuzi wa vifaa kwa kufanya land scaping kwenye Nyumba za makamo wa pili wa Rais Pagali |
| Pv 5/8/2020 | | 71,665,000 | | Malipo ya muendelezo wa kazi za ujenzi wa nyumba Makamo wa pili wa Rais Chake chake |
| Pv 11/9/2020 | | 44,550,000 | | Fedha kwa ajili ya gharama za vifaa kwa ukarabati sehemu ya Baraza la Wawakilishi<br><br>la zamani na sehemu ya ofi si ya makamo<br><br>wa pili |
| **Jumla** | | **291,710,000** | | |

**Majibu ya Hoja**

Hakuna malipo yaliyofanyika bila ya kupata idhini ya Mkuu wa KMKM.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba Kikosi cha KMKM kilipojibu 'management letter' iliyowasilishwa na Mkaguzi kwa barua yenye kumbukumbu nambari KM/HO/OIG/05/2022 ya tarehe 22 Aprili, 2022 imeeleza kwamba Kikosi cha KMKM kimekiri kwamba kuna baadhi ya nyaraka zilikosa baraka za Mkuu wa Kikosi ambapo Mkuu wa Kikosi alikuwa na taarifa na malipo hayo. Kutokana na majibu yaliyowasilishwa kwa Mkaguzi na Kikosi chenyewe kuwa hayana utata wowote, Kamati yetu haikuwa na maelezo zaidi isipokuwa ilikubaliana na hoja ya Mkaguzi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Kikosi wanatakiwa wawe makini wanapojibu 'Management letter' kwani ushahidi wa maandishi unadumu na unakuwa sahihi zaidi.

**KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) – PEMBA**

**Hoja nambari 6.3.5.16: Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 9,722,480**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 9,722,480 zimetumika kwa ununuzi wa bidhaa mbali mbali lakini bidhaa hizo hazikurikodiwa katika madaftari ya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 77: Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 04/05<br><br>30/04/2021 | 01534 | 760,480 | Malinge<br><br>Enterprises | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi<br><br>wa vifaa vya kuandikia. |
| 7/10 | 289 | 6,022,000 | KMKM Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 20/10/2020 | | | | wa Petrol lita 672.7 |
| 12/10<br><br>23/10/2020 | 291 | 1,800,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi<br><br>wa chakula. |
| 14/10<br><br>26/10/2020 | 293 | 1,140,000 | | |
| **Jumla** | | **9,722,480** | | |

**Majibu ya KMKM**

Ni kweli katika ukaguzi uliofanyika Wakaguzi walibaini baadhi ya matumizi katika ununuzi wa bidhaa mbali mbali hazikurikodiwa katika daftari la ghalani. Uongozi umefanya jitihada za kuwataka wahusika wa ghala kuzipitia kumbukumbu za matumizi hayo na kuzirikodi kama inavyotakiwa ili kuepusha upotevu wa mali za umma. Kwa sasa matumizi hayo yamesharikodiwa na yapo tayari kwa ukaguzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Watendaji wa KMKM Pemba walitambua kasoro zao na kuzifanyia marekebisho, Kamati ya PAC imesisitiza pendekezo moja na haikuwa na maelezo ya ziada kuhusiana na hoja hii.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Makamanda wa KMKM wahakikishe wanafuata maelekezo yaliyoainishwa katika sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma hususan wanaponunua vifaa viwe vinaingizwa katika daftari la ghalani.

**Hoja nambari 6.3.5.17.1: Malipo Kwa Watoa Huduma Ambao Hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi n Uondoshaji wa Mali za Umma Shilingi 15,487,640**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Pemba (KMKM) limefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 78: Malipo kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi ilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 10/06<br><br>18/06/2021 | 01541 | 10,487,640 | Mbarouk Juma Ali | Malipo ya fedha kwa ajili ya chakula |
| 11/06<br><br>23/06/2021 | 0519 | 5,000,000 | Salim Ali Humoud na<br><br>Khamis Hardware | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi na ukarabati wa vituo vya afya |
| **Jumla** | | **15,487,640** | | |

**Majibu ya KMKM**

Ni kweli katika ukaguzi uliofanyika ilibainika kuna baadhi ya watoa huduma wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo bado walikuwa hawajasajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar. Kwa sasa watoa huduma hao tayari wameshasajiliwa katika Mamlaka hiyo na vielelezo vyao vipo tayari kuonekana.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Watendaji wa KMKM Pemba walitambua kasoro zao na kuzifanyia marekebisho, Kamati ya PAC haikuwa na maelezo ya ziada kuhusiana na hoja hii.

**Hoja nambari 6.3.5.18: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 136,393,270**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 136,393,270 zimetumika kwa matumizi mbali mbali ya Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo lakini baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli nambari 79: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi | Kiasi ilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|

| | Namba | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2/11 ya 3/11/2020 | 295 | 500,000 | KMKM Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi mbali mbali |
| 01/05 ya 30/04/2021 | 0510 | 3,000,000 | | |
| 05/05 ya 12/05/2021 | 0513 | 11,782,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya vitoweo kwa mabaharia. |
| 17/06 ya 7/6/2021 | 0518 | 11,332,000 | | |
| 05/09 ya 22/09/2020 | 0285 | 20,166,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya mikato ya wapiganaji |
| 24/08 ya 24/08/2020 | 0282 | 18,706,500 | | |
| 04/07 ya 27/07/2020 | 0279 | 19,344,900 | | |
| 13/10 ya 26/10/2020 | 0294 | 17,594,870 | | |
| 23/12 ya 23/12/2020 | 01602 | 17,482,720 | | |
| 01/11 ya 30/11/2020 | 0299 | 16,484,280 | | |
| **Jumla** | | **136,393,270** | | |

### Majibu ya KMKM

Ni kweli ukaguzi uliofanyika umebaini kuwepo kwa vielelezo pungufu vya jumla ya Tzs. 136,393,270 katika matumizi yaliyofanyika, tulifanya jitihada za kuvitafuta vielelezo vilivyokuwa pungufu na tumefanikiwa kuviona, vielelezo hivyo vimekamilika na vipo tayari kwa ukaguzi.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Pamoja na Watendaji wa KMKM Pemba kukiri juu ya kuwepo kwa vielelezo pungufu lakini Kamati yetu ilitaka kujua kwa kwanini vielelezo hivyo hakupatiwa Mkaguzi na kugundua kwamba hilo lilitokana na uzembe katika uwekaji vizuri wa kumbukumbu za Serikali na kupelekea kutoa taswira mbaya juu ya upotevu wa fedha nyingi za Serikali. Hatimae, Kamati ilipivipitia vielelezo hivyo na kuridhika navyo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Kikosi cha KMKM Pemba waweke utaratibu mzuri wa kukutana na Mkaguzi na kumpatia vielelezo anavyovihitaji.

**KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU) - UNGUJA**

**Taarifa ya Mapato**

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 16,841,600,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Kikosi kilikusanya jumla ya shilingi 13,037,715,609 sawa na asilimia 77 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC ilitaka kujua sababu za kutofikia lengo la makusanyo na kuelezwa kwamba hali hiyo ilitokana na kuondolewa kwa kifungu cha ulinzi na kutanuka kwa biashara ya uuzaji wa mitungi ya gesi ambapo hivi sasa kuna wafanya biashara binafsi wengi wanauza mitungi hiyo tena kwa bei nafuu zaidi uklinganisha na bei zao. Kamati yetu haikuwa na hoja zaidi na iliridhika na majibu hayo.

**Taarifa ya Matumizi**

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 16,841,600,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 13,037,715,609 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 77 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC baada ya kupatiwa majibu ya Taarifa ya Matumizi haikuwa na hoja zaidi

**Hoja nambari 6.3.6.1: Kutofuatwa kwa taratibu za ununuzi wa gari shilingi 232,996,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanya muendelezo wa malipo kwa Ndugu OMAR MOH'D OMAR yenye thamani ya shilingi 71,996,000 kwa ajili ya ununuzi wa gari mbili (2) aina ya Mabasi zinazotumiwa kwa shughuli za Kikosi ambapo malipo ya awamu tatu yalilipwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kupelekea uwepo wa bakaa la fedha la shilingi 71,996,000 ambazo zinaendelea kulipwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Aidha ukaguzi umebaini Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanya ununuzi mwengine wa magari mawili (2) ambayo ni aina ya ISUZU kwa ajili ya matumizi ya kubebea maji ya kuzimia moto na aina ya CANTER kwa ajili ya kubebea Askari kwa thamani ya shilingi 161,000,000 ambapo hadi ukaguzi unakamilika imebainika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimemlipa Ndugu OMAR MOH'D OMAR jumla ya shilingi 16,150,000 na kubakia

bakaa ya shilingi 144,850,000 anazozidai.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa gari hizo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kupatiwa taratibu walizokubaliana na mzabuni huyo katika ulipwaji wa fedha zinazotumika katika ununuzi wa gari hizo (Mode of payment) ambapo ukaguzi umebaini malipo hayo yanafanyika kwa kila mwezi kwa kutumia fedha za matumizi mengineyo (OC) jambo ambalo limetia shaka juu ya matumizi ya fedha hizo kutokana na kukiukwa matakwa ya muongozo nambari BLM/97/M/C.5/VOL.V/27 wa tarehe 27 Septemba 2021 kutoka Serikali uliotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kuwaagiza Wakuu wote wa Taasisi kuwasilisha maombi ya ununuzi wa gari kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na kuacha kununua magari yaliyotumika (Used Car) pamoja na kuacha kununua magari kwa wazabuni binafsi kwa lengo la kununua gari kwa thamani kubwa kuliko bei ya sokoni.

Hata hivyo alieleza kwa vile Serikali ina mpango wa kununua magari yatakayotumiwa na taasisi za umma kwa wingi ili kuepusha kutumia fedha za (OC) kutekeleza majukumu ya manunuzi ya magari na kupelekea kushindwa kutekeleza malengo waliyojipangia kwa mujibu wa makadirio ya bajeti.

Kufanya manunuzi kinyume na matoleo ya Serikali kunapelekea taasisi ya umma kutumia gharama kubwa ya ununuzi unaotokana na wazabuni kuwauzia Serikali magari kwa gharama kubwa ukilinganisha na bei ya soko ilivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ili kuepusha kutumia fedha za umma kinyume na utaratibu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 80: Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi ya gari**

| Hati Namba | Kiasi (Tshs) | Maelezo | Vielelezo vilivyothibitisha malipo kufanyika |
|---|---|---|---|
| **Malipo kwa ajili ya ununuzi wa Mabasi mawili** | | | |
| R8/8/2020 ya 08/01/2020 | 24,600,000 | Malipo ya nne ya ununuzi wa gari zakusafirishia maafisa na askari agost 2020. | Risiti namba 705 ya 5/8/2020 |
| R21/9/2020 ya | 19,680,000 | Malipo ya tano ya ununuzi wa gari za kusafirishia maafisa na | Risiti namba 707 ya 7/9/2020 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 30/9/2020 | | askari wakzu kwa mwezi sept 2020 | |
| R23/10/2020 ya 26/10/2020 | 9,840,000 | Malipo ya sita ya ununuzi wa gari zakusafirishia maafisa na askari kwa mwezi oct. 2020. | Risiti namba 715 ya 29/10/2020 |
| R6/11/2020 ya 18/11/2020 | 12,300,000 | Malipo ya saba ya ununuzi wa gari | Risiti namba 729 ya 23/11/2020 |
| R19/12/2020 ya 19/12/2020 | 5,576,000 | Malipo ya nane ya ununuzi wa gari. | Risiti ya 726 ya 22/12/2020 |
| **Jumla Ndogo (A)** | **71,996,000** | | |
| Malipo kwa ajili ya ununuzi wa ISUZU na CANTER | | | |
| 5/1/2021 | 16,150,000 | Malipo ya awali ya ununuzi wa gariaina ya Isuzu na Canter. | - |
| Jumla Ndogo (B) | 16,150,000 | | |
| Bakaa la Deni (C) | 144,850,000 | | |
| **Jumla Kuu (A+B+C)** | **232,996,000** | | |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuifuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli Mkaguzi aligundua kasoro za kuwepo kwa ununuzi wa gari pasi na kufuata utaratibu. Hata hivyo, Kamati imeelezwa wale wote waliohusika na kadhia hiyo walisimamishwa kazi na wameshapelekwa ZAECA kwa hatua za uchumguzi zaidi.

Aidha, Kamati ilipohoji kuhusu kwanini KZU walishindwa kupeleka taarifa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ya ununuzi wa gari hizo, ilielezwa kwamba siku tatu baada ya kununuliwa gari hizo ndio kukatokea kusimamishwa kazi kwa Wahusika.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

KZU wahakikishe wanafuata sheria na taratibu ziliopo katika ununuzi wanaoufanya ili kuepusha kujitokeza hoja kama hizo kwa wakati mwengine.

**Hoja nambari 6.3.6.2: Kukosekana kwa mkataba wa ununuzi wa mafuta (Framework Contract) wenye jumla ya shilingi 205,524,671**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanya malipo kwa HIFFAH GENERAL TRADING CO. yenye thamani ya shilingi 236,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa Compressor kwa matumizi ya shughuli za Kikosi ambapo malipo ya awamu mbili zilizopita yalilipwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kubainika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimeendelea kulipa kupitia hati namba 27/10/2020 kupitia hundi namba TISS yenye thamani ya shilingi 14,250,000 ikiwa

ni malipo ya awamu ya tatu kwa ajili ya ununuzi wa compressor.

Aidha ukaguzi umebaini Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanya ununuzi mwengine wa vifaa vya ujenzi kwa thamani ya shilingi 700,000,000 kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba ambapo hadi ukaguzi unakamilika imebainika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimemlipa Ndugu JUMA FOUM MCHA jumla ya shilingi 71,583,272.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi pamoja na compressor, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kupatiwa taratibu walizokubaliana na mzabuni huyo katika ulipwaji wa fedha zinazotumika katika ununuzi wa vifaa pamoja na compressor (Mode of payment) ambapo ukaguzi umebaini malipo hayo yanafanyika kwa kila awamu kwa kutumia fedha za matumizi mengineyo (OC) jambo ambalo limetia shaka juu ya matumizi ya fedha hizo kutokana mtiririko wa malipo yanayofanyika kwa awamu.

Kufanya malipo kwa awamu pasi na kujulikana makubaliano ya mikataba yanayopelekea kufanyika malipo kwa awamu na kutokujulikana malipo hayo yatalipwa kwa awamu ngapi (Mode of Payment) kunapelekea taasisi ya umma kutumia gharama kubwa ya ununuzi unaotokana na wazabuni kuwauzia Serikali vifaa kwa gharama kubwa ukilinganisha na bei ya soko ilivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufanya malipo kwa mujibu wa mpango wa manunuzi ili kuepusha kutumia fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Ujenzi wa Mahanga ya Chanjaani - Pemba) kinyume na utaratibu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 81: Malipo kwa ajili ya Ununuzi wa Mafuta**

| Hati namba | Ankara namba | Aliyelipwa | Kiasi (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| **Ununuzi wa Mafuta ya Petroli** | | | |
| 16/07/2020 | 0281 ya 27/07/2020 | Kijangwani Petr.Station | 1,000,000 |
| 2//08/2020 | 3129 ya 30/07/2020 | | 3,115,878 |
| 16/09/2020 | 3246 ya 15/09/2020 | | 2,703,000 |
| 28/10/2020 | 3338 ya 26/10 | | 1,454,400 |
| 2/11/2020 | 3366 ya 18/11 | | 1,478,400 |
| 20/12/2020 | 3411 ya 14/12 | | 2,174,400 |
| 3/01/2021 | 3468 ya 11/01/2021 | | 2,138,400 |
| 5/02/2021 | 3517 ya 3/02/2021 | | 4,455,000 |
| 3/04/2021 | 3604 ya 15/03/2021 | | 4,815,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1/5/2021 | 3741 ya 3/05/2021 | United Group Ltd | 5,162,500 |
| 34/6/2021 | 3865 ya 29/06/2021 | | 4,999,944 |
| **Jumla ndogo** | | | **33,496,922** |
| **Ununuzi wa Mafuta ya Diesel** | | | |
| 20/12/2020 | 3411 ya 14/12/2020 | | 10,823,960 |
| 28/10/2020 | 3338 ya 26/10/2020 | | 8,543,944 |
| 2/11/2020 | 3366 ya 18/11/2020 | | 706,400 |
| 34/06/2021 | 3865 ya 29/06/2021 | | 4,998,882 |
| 2/08/2020 | 3129 ya 30/07/2020 | United Group Ltd Diesel | 14,883,500 |
| 16/07/2020 | 0281 ya 27/07/2020 | Kijangwani Pet.Station | 3,000,000 |
| 5/02/2021 | 3517 ya 3/02/2021 | | 14,696,500 |
| 28/10/2020 | 3338 ya 26/20/2021 | | 8,543,944 |
| 3/04/2021 | 3604 ya 15/03/2021 | | 15,528,000 |
| 1/5/2021 | 3741 ya 3/05/2021 | | 854,128 |
| | 3740 ya 3/05/2021 | | 16,192,000 |
| 34/6/2021 | 3865 ya 29/06/2021 | | 4,998,882 |
| 5/2/2021 | 3517 ya 3/02/2021 | | 14,696,500 |
| 3/01/2021 | 3468 ya 11/01/2021 | | 9,860,487 |
| 5/09/2020 | 3221 ya 4/09/2020 | | 13,873,860 |
| 16/09/2020 | 3246 ya 15/09/2020 | | 15,296,402 |
| 16/07/2020 | 0281 ya 27/07/2020 | United Group Ltd Diesel | 3,000,000 |
| 02/11/2020 | 3366 ya 18/11/2020 | | 706,400 |
| 20/12/2020 | 3411 ya 14/12/2020 | | 10,823,960 |
| **Jumla Ndogo** | | | **172,027,749** |
| **Jumla Kuu** | | | **205,524,671** |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli wakati Mkaguzi anakamilisha majukumu yake, KZU haikuwa na Mkataba. Hata hivyo, hivi sasa wanakubaliana na Watoa huduma na kuwalipa kila mwezi.

**Hoja nambari 6.3.6.1: Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi ya compressor shilingi 236,000,000 na ujenzi wa mahanga shilingi 700,000,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanya malipo kwa HIFFAH GENERAL TRADING CO. yenye thamani ya shilingi 236,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa Compressor kwa matumizi ya shughuli za Kikosi ambapo malipo ya awamu mbili zilizopita yalilipwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kubainika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimeendelea kulipa kupitia hati namba 27/10/2020 kupitia hundi namba TISS yenye thamani ya shilingi 14,250,000 ikiwa ni malipo ya awamu ya tatu kwa ajili ya ununuzi wa compressor.

Aidha ukaguzi umebaini Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanya ununuzi mwengine wa vifaa vya ujenzi kwa thamani ya shilingi 700,000,000 kwa mujibu wa makubaliano ya

mkataba ambapo hadi ukaguzi unakamilika imebainika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimemlipa Ndugu JUMA FOUM MCHA jumla ya shilingi 71,583,272.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi pamoja na compressor, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kupatiwa taratibu walizokubaliana na mzabuni huyo katika ulipwaji wa fedha zinazotumika katika ununuzi wa vifaa pamoja na compressor (Mode of payment) ambapo ukaguzi umebaini malipo hayo yanafanyika kwa kila awamu kwa kutumia fedha za matumizi mengineyo (OC) jambo ambalo limetia shaka juu ya matumizi ya fedha hizo kutokana mtiririko wa malipo yanayofanyika kwa awamu.

Kufanya malipo kwa awamu pasi na kujulikana makubaliano ya mikataba yanayopelekea kufanyika malipo kwa awamu na kutokujulikana malipo hayo yatalipwa kwa awamu ngapi (Mode of Payment) kunapelekea taasisi ya umma kutumia gharama kubwa ya ununuzi unaotokana na wazabuni kuwauzia Serikali vifaa kwa gharama kubwa ukilinganisha na bei ya soko ilivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufanya malipo kwa mujibu wa mpango wa manunuzi ili kuepusha kutumia fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Ujenzi wa Mahanga ya Chanjaani – Pemba) kinyume na utaratibu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 82: Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi ya vifaa vya ujenzi wa Mahanga Chanjaani - Pemba na ununuzi wa Compressor**

| Hati Namba | Kiasi (Shs) | Alielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| **Malipo kwa ajili ya ununuzi wa Compressor** | | | |
| 27/10/2020 | 14,250,000 | Hiffah General Trading Co. | Malipo ya awamu ya tatu yaununuzi wa Compressor. |
| **Jumla** | **14,250,000** | | |
| **Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Ujenzi wa Mahanga** | | | |
| Pv 13/03/2021 | 16,150,000 | | |
| Pv 06/04/2021 | 2,233,272 | | |
| Pv 17/12/2020 | 7,125,000 | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Pv 18/10/2020 | 8,550,000 | Juma Foum Mcha | Malipo ya ununuzi wa vifaa vyaUjenzi wa Mahanga |
| Pv 15/09/2020 | 14,250,000 | | |
| Pv 22/08/2020 | 12,825,000 | | |
| Pv 03/07/2020 | 12,350,000 | | |
| **Jumla** | **71,583,272** | | |

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati yetu imegundua kwamba ujenzi uliokuwa unaozungumziwa katika hoja hii ulikuwa unaendelea na tayari Mkaguzi aliwahi kuukagua na kuutolea ripoti mwaka 2019/2020. Hivyo, Makamanda wa KZU walidai kuwa kwa vile tayari waliwasilisha vielelezo hawastahiki tena kuwasilisha vielelezo vyengine vya uendelezaji wa ujenzi huo jambo ambalo sio sahihi.

Kuhusiana na ununuzi wa gari 2, Kamati imethibitisha kwamba gari hizo kweli zipo na zinaendelea kutumiwa na Kikosi cha Zimamoto lakini gari moja bado haijalipwa kwa vile ilikosa vielelezo vya ununuzi wake baada ya kufanywa tathmini na Serikali.

Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inalitafutia ufumbuzi suala la kulipwa Mnunuzi wa gari kwa kumtafuta na kukaa nae ili kutafuta ushahidi na ikijithibitisha impatie haki yake.

**Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 90,302,514**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 90,302,514 zimetumika kwa malipo mbali mbali ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuambatanishwa hati za malipo na vielelezo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuhakikisha unafanya manunuzi na kuambatanisha vielelezo vyote katika hati za malipo kwa mujibu wa taratibu na sheria za fedha. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 83: Malipo yenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Kiasi (shs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 25/03/2021 | 3,340,000 | | Malipo ya uzalishaji poshombali mbali. |
| 30/04/2021 | 28,048,500 | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 02/07/2020 | 1,100,000 | Kamishna Zimamoto na Uokozi | |
| 02/07/2020 | 2,000,000 | | Malipo ya makusanyo yamapato |
| 14/12/2020 | 6,162,807 | | Malipo ya wanachama wa Askari wanachama wa ZSSF. |
| 31/10/2020 | 6,162,807 | | |
| 23/09/2020 | 18,488,400 | | |
| 26/08/2020 | 3,000,000 | Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha za Mipango | malipo ya makusanyo yamapato |
| 12/10/2020 | 2,000,000 | | |
| 14/09/2020 | 1,000,000 | | |
| 13/11/2020 | 1,000,000 | | |
| 14/08/2020 | 7,000,000 | Kamishna Zimamoto na Uokozi | |
| 14/08/2020 | 1,000,000 | Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha za Mipango | |
| 14/12/2020 | 5,000,000 | Kamishna Zimamoto na Uokozi | Matumizi ya fedha kwa shughuli mbali mbali za Kikosi |
| 04/09/2020 | 2,500,000 | | |
| 04/09/2020 | 2,500,000 | | |
| **Jumla** | **90,302,514** | | |

**Majibu ya KZU**

Naomba kuwasilisha vielelezo vya hati hizo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba awali vielelezo vilikuwa havipo lakini wakati Kamati inafika KZU vielelezo vilikuwepo na kuelezwa kwamba vilikosekana kwasababu ya kutokuwepo kwa baadhi ya watendaji waliosimamishwa kazi. Hivyo, Kamati haikuwa na maelezo zaidi.

**KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ) - UNGUJA**

**Taarifa ya Mapato**

Kikosi cha Valantia Zanzibar kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 20,135,000,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Kikosi kilikusanya jumla ya shilingi 17,965,270,061 sawa na asilimia 89 ya makadirio.

**Majibu ya Kikosi**

Kikosi cha Valanta Zanzibar, hakina chanzo chochote cha mapato ya ndani na badala yake kinategemea kupata fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya mshahara, matumizi mengineo (OC) na fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha kikosi kinaendelea na jitihada za kuanzisha miadi mbali mbali ya uzalishaji mali ili kiweze kujipatia kipato cha ndani na kuweza kuchangia Serkalni.

Kwa mnasaba huo ilikuweza kujipata vyanzo vya mapato kikosi kimepanga kuanzisha kiuo cha kuuzia mafuta (petrol staton) katika kambi ya Muyuni, Ufugaji wa kuku wa nyama na mayai, utengenezaji wa mbolea sambamba na utotoleshaji wa viaranga katika kambi ya Muyuni na ujenzi wa Bekari ya kisasa katika kambi ya Makao makuu Mtoni KVZ, kufanikiwa kwa utekelezaji wa miradi hii, kutapelekea kujipata kipato cha ndani na hatimae kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imegundua kwamba kikosi cha Valantia hakina mapato ya kuaminika yanayochangia katika Serikali isipkuwa wanategemea fedha kutoka Serikali Kuu. Hata hivyo, Kikosi kinachukua juhudi ya kuanzisha shughuli tofauti ili kupata fedha za kujiendesha hasa ukizingatia fedha wanazopata kutoka Serikali huwa hazipatikani zote.

Kwasasa Kikosi hicho kina mpango wa kuanzisha kituo cha kuuzia mafuta (Petrol Station), Ufugaji wa Kuku huko Muyuni, ununuzi wa ndege ya abiria pamoja na kiwanda cha uzalishaji wa mabati Pangatupu.

**Taarifa ya Matumizi**

Kikosi cha Valantia Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 21,073,690,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 17,965,270,061 zilitumika kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo sawa na asilimia 85 ya makadirio.

**Majibu ya Kikosi**

Ikosi kimefanya manunuzi kwa mtoa huduma aitwae Magomeni jitini, aliyesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na uondoshaji wamali za Umma kwa usajili wa manunuzi na usambazaji wa vitu tofauti (general suppler). Hivyo kikosi kimeona kimtumie msambazaji huyo kutokana na kukidhi vigezo vy amanunuzi. Aidha vielelezo vyote vya mtoa huduma vipo na uongozi upo tayari kuwasilisha vielelezo hivyo katika uongozi wa Kamati.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba sababu kuu ya Kikosi kutofikia lengo la matumizi ni kutokupata kwa fedha za matumizi kwa mujibu wa makadirio kulikotokana na kuwepo kwa maradhi ya 'Covid 19' ambapo makusanyo ya Serikali yetu yalipungua. Kukosekana kwa fedha hizo kumepelekea miradi yao ya maendeleo ya ujenzi wa Kambi katika maeneo tofauti likiwemo la Kikungwi ilishindwa kutekelezeka ipasavyo. Kamati yetu imegundua kwamba Kikosi cha Valantia pamoja na kuwasilisha majibu yao lakini hayakuainisha mchanganuo wa jinsi gani matumizi hayo yamefanyika.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kikosi cha Valantia Zanzibar kinapoandaa ripoti zake za mapato na matumizi kihakikishe kinaweka mchanganuo wake ili uweze kutoka uhalisia wa kilichofanyika.

**Hoja nambari 6.3.7.1: Malipo kwa Watoa Huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma shilingi 538,813,156**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Kikosi cha Valantia (KVZ) kimefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Aidha, ukaguzi umebaini Kikosi cha Valantia kimefanya manunuzi kwa Mtoa huduma aitwae Magomeni Jitini aliyesajiliwa kwa ajili ya usambazaji na uuzaji wa Vipuri vya vyombo vya moto (Spare Parts).

Dosari iliyobainika na kutia shaka ukaguzi ni kwamba Kikosi cha Valantia kimenunua chakula kwenye duka la uuzwaji wa vipuri jambo ambalo limetia shaka juu ya uhalali wa matumizi hayo.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 86: Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Hati Namba | Hundi namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Pv 3/7/2020 | T.T | | 43,350,168 | Ununuzi wa chakula cha Askari |
| Pv 11/10/2020 | T.T | | 12,782,608 | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi. |
| PV 9/8/2020 | T.T | | 42,241,110 | Ununuzi wa Chakula cha Askari. |
| Pv 2/9/2020 | T.T | | 42,836,835 | |
| Pv 52/10/2020 | T.T | | 41,230,305 | |
| Pv 10/10/2020 | T.T | | 35,172,200 | |
| Pv 45/10/2020 | T.T | | 39,547,768 | |
| Pv 12/10/2020 | T.T | | 4,285,000 | Ununuzi wa vifaa vya mazoezi. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Pv 9/11/2020 | T.T | Magomeni Jitini | 35,452,952 | Ununuzi wa chakula cha Askari. |
| Pv 3/1/2021 | T.T | | 1,563,080 | |
| Pv 11/2/2021 | T.T | | 56,213,228 | |
| Pv 3/3/2021 | T.T | | 56,213,228 | |
| Pv 8/10/2020 | CASH | | 315,000 | |
| Pv 1/4/2021 | T.T | | 63,804,837 | |
| Pv 1/5/2021 | T.T | | 63,804,837 | |
| Pv 1/6/2021 | T.T | | 64,078,273 | |
| Pv 24/4/2021 | T.T | | 6,817,391 | Ununuzi wa vifaa vya jikoni. |
| Pv 3/11/2020 | T.T | | 2,000,000 | Ununuzi wa vifaa vya michezo. |
| Pv 24/6/2021 | CASH | | 12,303,000 | Ununuzi wa vifaa vya michezo. |
| Pv 7/5/2021 | Kamanda Mkuu | | 3,191,000 | Ununuzi wa vifaa vya jikoni. |
| **Jumla** | | | **538,813,156** | |

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Valantia kufuata Sheria kikamilifu katika kutekeleza majukumu yake.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Kikosi cha Valantia kukiri kwamba kulikuwa na kasoro kwa wakati huo. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kwamba kulikuwa na mpango maalum wenye maslahi na Taifa letu. Kutokana na hali hiyo, ilisababisha Kikosi kutafuta Mtoa Huduma mwenye uzalendo, uwezo na umahiri zaidi katika utekelezaji wa kazi zake.

Hata hivyo, Kamati yetu imebaini Kikosi kimejuchukua juhudi ya kurekebisha kasoro hiyo ili isije kutokezea tena kwani Kamati ilifanikiwa kuoneshwa usajili wa Mtoa Huduma huyo kupitia cheti cha tarehe 10/2/2022 hadi tarehe 10/2/2023 chenye nambari ya usajili G000474.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kikosi cha Valantia kihakikishe kinawatumia Waroa Huduma ambao wamesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma.
2. Kamati ya PAC inakishauri Kikosi iwapo kitahitaji Watoa Huduma maalum kwa kazi maalum (very sensitive task) waombe ruhusa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ili kiweze kuruhusiwa kutumianjia muafaka ya ununuzi kwa mujibu wa sheria.

**KIKOSI CHA VALANTIA (KVZ) - PEMBA**

**Hoja nambari 6.3.7.2: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 34,996,000**

Kwa mujibu wa kumbukumbu ya hati za malipo namba 4/10 ya tarehe 05/10/2020 kupitia hundi namba 000489 yenye thamani ya shilingi 34,996,000 aliyolipwa Kikosi cha Valantia kwa ajili ya malipo ya fidia ya vijana waliojenga nyumba za kuishi katika eneo la Kambi Micheweni.

Ukaguzi umebaini malipo hayo yamefanyika bila ya kuambatanisha vilelezo husika kwenye hati ya malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya KVZ**

Kikosi cha Valantia Zanzibar, kilifanya malipo ya fidia kwa waliojenga nyumba za kuishi, katika eneo la kambi ya Micheweni mnamo tarehe 05/10/2020 ambapo vijana hao walijenga nyumba moja ya kuishi na boma ambalo lipo katika hatua ya kuezekwa kwenye eneo la kambi ya Kikosi cha Valantia zoni ya Pemba Micheweni bila kufata taratibu za kisheria.

Kwa kuzingatia hilo, Kikosi kilichukua hatua ya kufanya mazungumzo na wahusika sambamba na kuunda kamati ndogo kutoka Zoni ya Pemba ili kufuatilia taratibu zote kwa mujibu wa sheria zinavoeleza katika mauziano hayo, vile vile vielelezo vyote vimehifadhiwa katika file maalum na vinapatikana muda wowote kwa ajili ya ukaguzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

1. Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC ilibaini mambo yafuatayo:
2. Ni kweli kulikuwepo na nyumba mbili karibu na kamabi ya KVZ iliopo Micheweni ambazo moja ilikuwa inamilikiwa na Bwana Juma Hamad Mbwana na Bwana Hamad Khamis Omar;
3. Kutokana na ziara ya Waziri wa Vikosi aliyoifanya katika Kambi ya KVZ Wete, Mheshimiwa Haji Omar Kheir na kuona kwamba kwa mazingira ya Kikambi ni vyema nyumba hizo zikachukuliwa na KVZ kwa kufidiwa fedha wamiliki wa nyumba husika;
4. Nyumba hizo hazikuwa na umiliki ulio rasmi kutoka katika Taasisi ya Serikali;
5. Mauziano hayo yalithibitishwa na Sheha wa Shehia ya Maziwang'ombe (Micheweni) kwani kulikuwa na barua yake iliyothibitisha hana pingamizi na ulipwaji huo wa fidia;
6. Fidia ya nyumba hizo ilifanyika mwaka 2020 kwa jumla ya shilingi 34,996,000 kwa nyumba zote mbili.
7. Kutokana na mazingira ya mauziano yaliyofanyika, Kamati imegundua hakukuwa na biashara iliyofanyika inayohitaji kupatiwa mikataba na vielelezo;
8. Malipo kweli yalifanyika kwa njia ya fedha taslim ambapo Kamati ilibahatika kuona nyaraka ya malipo yenye saini za walipwaji;
9. Malipo yaliyofanywa hayakupitia benki, hivyo hayakukatwa kodi kokote yoyote

kwa vile wamiliki walikuwa hawana hesabu ya benki na hawakuwa tayari kufungua.

Kwa mnasaba huo, Kamati imejiridhisha kwamba mauziano hayo hayakuwa ni biashara isipokuwa ni kufidia gharama ambazo Wamiliki hao walizitumia katika ujenzi huo. Kamati imeridhika na majibu na haikuwa na maelezo zaidi.

**Mapendekezo ya kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri kuwa kuwe na maelewano mazuri kwa pande zote mbili baina ya Mkaguzi na Mkaguliwa ili kuepusha mgongano na migogoro.

**Hoja Nambari 6.3 7.3: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 4,000,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 4,000,000 zimelipwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Kikosi Cha Valantia Pemba ambapo malipo hayo yamefanyika kwa mujibu wa hati namba 09/10 ya tarehe 23/10/2020 yenye thamani ya shilingi 3,000,000 iliyolipwa kwa hundi namba 000493 pamoja na hati namba 11/10 ya taehe 29/10/2020 yenye thamani ya shilingi 1,000,000 ambayo imelipwa kwa hundi namba 000495.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanyika kwa malipo hayo kwa fedha taslimu jambo ambalo linapelekea kuikosesha Serikali mapato. Kufanya hivyo kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya KVZ**

Uongozi wa Kikosi Cha Valantia Zoni ya Pemba umefanya matumizi kwa njia ya fedha taslim kutokana na hali halisi ilokuwepo kwa wakati ule, ikumbukwe kua kipindi hiki ilikua ni kipindi kigumu cha zoezi la uchaguzi mkuu wa kugombea udiwani, uwakilishi, ubunge na uraisi wa Zanzibar, hivyo Kikosi kiliishiwa mafuta kwa ajili ya harakati za uchaguzi na kulazimika kufanya matumizi ya dharura kwa kutumia fedha taslim kwa wazabuni wa chakula na mafuta ili kufanya uharaka wa upatikanaji wa huduma hizo.

Kwa kipindi hicho kwa upande wa Pemba ilikuwa ni vigumu kupatiwa mafuta pamoja na chakula kwa njia ya mkopo kutokana na hali ya kisiasa iliyopo na mahusiano yaliyopo yasiyo Madhubuti baina ya vikosi vya Idara Maalum na wazabuni kwa Pemba. Hivyo Kikosi kinathibitisha kua kimefanya matumizi haya kwa dharura maalum na sio katika hali ya kawaida na vielelezo vya ununuzi huo vipo tayari kwa ukaguzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Baada ya maeelezo kutoka Kikosi cha Valanti, Kamati imebaini hoja hii imetoka na maagizo maalum kutoka Serikali Kuu kama ilivyoelezwa kwa urefu katika hoja nambari 6.3.7.2. Hivyo, Kamati yetu haikuwa na hoja zaidi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

KVZ inapofanya malipo ya huduma mbali mbali ihakikishe inalipa kupitia Benki na izuie kodi ambayo Serikali itanufaika nayo kupitia mauziano hayo.

**Haja Nambari 6.3.7.4: Uhamisho wa kikazi kwa Wapiganaji wa Kikosi cha Valantia Pemba**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 89(1)(2)(3) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 kinatoa maelekezo kwa mtumishi yoyote atakaepewa uhamisho kutoka Unguja kwenda Pemba, Tanzania Bara au kinyume chake atapaswa kulipwa Posho la Usumbufu litakalokuwa sawa na posho la siku saba pamoja na usafiri wa ndani wa kufidia usumbufu atakao upata katika kutekeleza amrihiyo ya uhamisho. Aidha, kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha kwanza na cha pili ya kanuni hii mtumishi huyo atastahiki kugharamiwa uhamishaji wa familia na mizigo yake.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 60(g) cha Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ kinaeleza "Posho la usumbufu ambalo litafungamana na uhamisho wa kutoka Unguja kwenda Pemba au kinyume chake la asilimia 25 ya mshahara".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Valantia Pemba kimefanya uhamisho wa kikazi kwenda Unguja kwa wapiganaji wake mbali mbali, dosari ya kiutumishi iliyobainika ni kutokutekelezeka kwa vifungu nilivyoviainisha hapo juu kutokana na kukosekana kwa vielelezo mbali mbali vilivyothibitisha upokeaji wa stahiki za malipo yatokanayo na shughuli ya uhamishaji wa familia na mizigo kwa mujibu wa utaratibu.

Kuwakosesha stahiki za uhamisho kwa wapiganaji hao kunaweza kupelekea kupunguza hamasa ya ufanyaji wa kazi na hatimae kujitokeza kwa malalamiko ya chini kwa chini ambayo hupelekea kuondoa imani kwa wakuu wa Vikosi vya ulinzi na Usalama.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama kuhakikisha unatekeleza kikamilifu maagizo ya kanuni za Utumishi wa Umma pamoja na kanuni za Idara Maalum za Vikosi vya SMZ kwa lengo la kuondosha migongano na migogoro kwa wapiganaji makazini. Mchanganuo wa wapiganaji hao ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 87: Orodha ya wapiganaji waliohamishwa kikazi bila ya kufanyiwa malipo**

| Namba | Jina la Mpiganaji | Namba | Jina la Mpiganaji |
|---|---|---|---|
| 1 | AV 0016 CAPT V A Abass | 24 | MV 1466 PTE Yussuf M. Silima |
| 2 | AV 0022 CAPT J A Makwaya | 25 | MV 1501 PTE Abdul-Kadir Malik |
| 3 | AV 0026 CAPT H Kh Ali | 26 | MV 1504 PTE Abdulla Ali Haji |
| 4 | AV 0033 CAPT J Ch Masanja | 27 | MV 1511 PTE Abdul-Malik Juma |
| 5 | AV 0035 CAPT M F Hamad | 28 | MV 1515 PTE Abdul-Rahim Moh'd |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6 | AV 0038 CAPT H R Makame | 29 | MV 1517 PTE Juma Moh'd Juma |
| 7 | MV 0228 WOI Shoka Khatib Juma | 30 | MV 1546 PTE Ali Hamad Ali |
| 8 | MV 0162 WOI Sadi Ussi Khamiss | 31 | MV 1649 PTE Ali Hassan Pandu |
| 9 | MV 0146 S/SGT Amour Ali Amour | 32 | MV 1733 PTE Juma Maziku Ngula |
| 10 | MV 0194 SGT Khamis A. Hassan | 33 | MV 1826 PTE Maulid Husein |
| 11 | MV 0182 SGT Ibrahim Moh'd | 34 | MV 1818 PTE Makame Mussa Ali |
| 12 | MV 0537 SGT Akida Masoud Akida | 35 | MV 1879 PTE Nicolaus Peter |
| 12 | MV 0493 CPL Haji Ali Haji | 36 | MV 1899 PTE Othman Ali Amour |
| 14 | MV 1139 CPL Othman Iddi Khamis | 37 | MV 1920 PTE Rashid Juma Omar |
| 15 | MV 0584 CPL Himid Makame Vuai | 38 | MV 1937 PTE Shauri Ali Shauri |
| 16 | MV 0780 CPL Shaib Mtumwa Haji | 39 | MV 1974 PTE Talib Mbaraka |
| 17 | MV 1020 PTE Thobias Yohana | 40 | MV 2017 PTE Zubeir Juma Rashid |
| 18 | MV 1333 PTE Ali Choum Juma | 41 | MV 0203 PTE Yussuf Haji Juma |
| 19 | MV 1386 PTE Juma Said Maalim | 42 | MV 1616 PTE Fuom Haji Foum |
| 20 | MV 1389 PTE Juma Zaid Juma | 43 | MV 0308 PTE Mahmoud Gharib |
| 21 | MV 1416 PTE Makame Haji Khamis | 44 | MV 1713 PTE Juma Makame S |
| 22 | MV 0980 PTE Ibrahim Makame | 45 | MV 1605 PTE Faki Hassan Issa |
| 23 | MV 1500 PTE Abdul-Hamid Haji | | |

Majibu ya KVZ

Kikosi Cha Valantia Zanzibar (KVZ) Zoni ya Pemba, kinaheshimu na kutekeleza kikamilifu maagizo ya Kanuni za Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni za Idara Maalum za Serkali ya Mapinduzi ya Zanzimbar (SMZ), kwa kuhakikisha Maafisa na Wapiganaji wake wanapata stahiki zao zote za uhamisho kutoka Unguja Kwenda Pemba na Pemba Kwenda Unguja, kwa kuzingatia hilo Kikosi kimetenga bajeti kwenye mpango kazi wake kwenye kifungu cha "masilahi ya uhamisho" kwa lengo la kuondoa migongano na migogoro kwa Maafisa na Wapiganaji makazini.

Aidha kama tunavojua kwenye taasisi zetu za Kijeshi suala la uhamisho ni jambo la lazima kwa mujibu wa kiapo tunachoapa baada ya kuajiriwa kwamba utakuwa tayari kufanya kazi mahali popote.

Changamoto kubwa katika hili ni uhaba wa fedha za OC tunazo ingiziwa kutoka serkali kuu na hivyo inapelekea kupewa fedha za nauli na posho kidogo pamoja na usafiri wa gari, kutoka nyumbani kuelekea bandarini au airport, endapo fedha ingetoka kama tulivopanga kusingekuwepo malalamiko hayo, kwani wanao hamishwa wangepata stahiki zao zote kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo, hivyo kikosi kina ahidi kuwapatia malipo ya posho pamoja na uhamishaji wa familia na mizigo kwa wanaopata uhamisho kwa kadiri fedha itakavyo patikana.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC imeridhika na majibu yaliyotolewa na kusisitiza kuwa KVZ ihakikishe inawapatia stahiki zao Maofisa na Wapiganaji wote wanaopatiwa uhamisho kwani kutawajenga zaidi imani na majeshi yao pamoja na kuongeza ufanisi katika kazi zao.
2. Wizara ya Tawala za Mikoa kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikalini iifanyie marekebisho Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ili kanuni hizo ziweze kuendana.

**Hoja nambari 6.3.7.5 Vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 3,500,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 3,500,000 zimelipwa kwa bwana Salum Hamdan kupitia hati namba 01/04 ya tarehe 27/04/2021 kwa hundi namba 00076 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi, hata hivyo imebainika kuwa vifaa hivyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya KVZ**

Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ) Zoni ya Pemba, kinakiri kufanya malipo ya jumla ya Tsh 2,882,000/- kwa Bw. Salum Hamdani na Tsh 618,000/- kwa Bw. Asaa Kher Asaa, jumla ya pesa zote ni Tsh 3,500,000/= tarehe 27/04/2021 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi, ambapo kwa lengo la kuthibitisha uhalali wa mapokezi na matumizi ya vifaa hivyo kikosi kimeweza kurekodi kwenye daftari maalum vifaa vyote vilivyo nunuliwa na vilivyo tumika kwa ajili ya ujenzi ulio kusudiwa na daftari husika linapatikana mda wowote kwa ajili ya ukaguzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya kikosi cha Valantia kukiri kuwepo kwa hoja hii, hata hivyo, Kamati ya PAC ilitaka kuja kulikuwa na changamoto gani iliyosababisha kutorikodiwa kwa vifaa katika daftari la ghalani na kuelezwa kwamba Watoa huduma walichelewa kuleta vielelezo mapema ili virikodiwe katika daftari la ghalani lakini hivi sasa tayari vifaa hivyo vimesharikodiwa. Kamati yetu ilibahatika kulikagua daftari hilo na kubaini kuwa ni kweli vimesharikodiwa na Kamati imeridhika.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri kikosi cha Valantia kuhakikisha vifaa vinaponunuliwa viingizwe katika daftari la ghalani ili kuepusha hoja kama hizo kuripotiwa katika RIpoti ya Mdhibiti.

**Hoja nambari 6.3.7.6 Malipo kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 6,500,000**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii Mtu, Kampuni au Taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Kikosi cha Valantia kimefanya manunuzi na Watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 88: Malipo kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati Namba | Hundi Namba | Fedha zilizolipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 61/07<br><br>7/10/2020 | 00067 | 3,000,000 | Khamis Khalfan | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 01/01<br><br>18/01/2021 | 00072 | 3,500,000 | RSM Korea Timber & Hardware | |
| **Jumla** | | **6,500,000** | | |

## Majibu ya KVZ

Kikosi Cha Valantia (KVZ) Zoni ya Pemba kinakiri kutumia wazabuni ambao hawakusajiliwa na malaka ya Ununuzi na uondoaji wa mali za Umma ambao ni Ndugu, Khamis Khalfani Tsh. 3,000,000. Tarehe 07/10/2020 na RSM Korea Timber & Hardware Tsh. 3,500,000/- tarehe 18/01/2021 ambapo tatizo hili lilitokea baada ya wazabuni hawa kushindwa kurekebisha upya (renew) usajili wao na kutoa taarifa za uongo kwa Uongozi wa kikosi cha Valantia Zoni ya Pemba, siku ya kikao cha kujadili juu ya uwezekano wa upatikanaji wa vifaa tulivyovihitaji kwa ajili ya kikosi na kukiri kwamba wapo kihalali, wamesajiliwa na waliahidi kutuwasilishia vielelezo vya usajili huo baada ya kikao hicho na wakati tunasubiri kuwasilishwa vielelezo hivyo kikosi kiliamua kuanza nao biashara kwa sababu mahitaji yetu yalikuwa ni ya haraka na bidhaa tulizohitaji kwa wakati huo zilikuwa zinapatikana kwa Wazabuni hao tu. Baada ya Wazabuni hao kushindwa kutuwasilishia vielelezo vya usajili vinavyostahiki, bila kusita na bila kuchelewa kikosi

kilichukua hatua ya kutafuta Wazabuni wengine ambao wamekamilisha taratibu zote za kisheria.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Kikosi cha Valantia kumekiri kukosea na tayari kimechukua juhudi za kurekebisha kasoro hizo. Kamati ya PAC haikuwa na hoja zaidi.

**Mapendekezo ya kamati ya PAC**

Kamati inakishauri Kikosi cha Valantia kutumia Watoa huduma ambao wamesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi ili kuepusha migongano na kuipatia Serikali mapato stahiki.

**FUNGU D08 - MKOA WA KUSINI UNGUJA**

**Taarifa ya Mapato**

Mkoa wa Kusini Unguja kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 15,748,952,435. Kati ya hizo jumla ya shilingi 50,750,000 zilikadiriwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Mkoa, jumla ya shilingi 15,698,202,435 zilikadiriwa kupatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ikiwa ni ruzuku.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 13,646,908,014 zilipokelewa ikiwa sawa na asilimia 86.65 ya makadirio, kati ya hizo jumla ya shilingi 34,458,500 zilipokelewa kutoka vyanzo vya ndani vya Mkoa sawa na asilimia 68 ya makadirio, jumla ya shilingi 13,612,449,514 zilipatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 86.7 ya makadirio.

**Majibu ya Mkoa**

Mkoa wa Kusini Unguja Kupitia vote yake ya D08 uliweza kukusanya fedha kutoka katika vyazo vyake vya mapato kutoka Mfuko Mkuu wa hazina na mapato yake ya ndani ya uhalishaji Ardhi na kuweza kupokea jumla ya shilingi 13,646,908,014 sawa na asilimia 86.7 ikiwa ni upungufu ukulinganisha na makadirio ya shilingi 15,748,952,435.

Mkoa wa Kusini Unguja Umekubwa na changamoto kadha za upatikanaji wa makusanyo yake kupitia fedha Mfuko Mkuu wa Hazina kwa aliji ya matumizi ya kawaida na makusanyo yake ya ndani na kusabaisha kutofikia malengo yaliopangwa, changamoto zenyewe ni kama ifuatavyo:-

Kutofikiwa kwa malengo katika chanzo cha mapato ya ndani ya Mkoa kumetokana na sababu zifuatazo:-

1. Uelewa mdogo wa Wananchi katika umuhimu wa uhaulishaji wa Ardhi.
2. Urasimu wa Mfumo wa Uhaulishaji.
3. Ugumu wa chanzo cha mapato kutokuwa na shinikizo kwa Wananchi la kufanya

uhaulishaji.
4. Uhalisia wa chanzo cha mapato kutegemea na Mwananchi kufanya au kutofanya uhaulishaji.
5. Kuwepo kwa mfumo wa zamani wa ukusanyaji mapato.
6. Kutopatikana Fedha za kutosha hasa za Matumizi ya kawaida (OC) kutika Mfuko Mkuu wa Hazina.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Baada ya kupokea majibu hayo, Kamati ya PAC haikuwa na hoja zaidi.

**Taarifa ya Matumizi**

Mkoa wa Kusini Unguja kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 15,748,952,435 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na mapato yao ya ndani, kati ya hizo shilingi 15,542,252,435 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 206,700,000 kwa matumizi ya maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mkoa wa Kusini Unguja uliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 13,646,908,014 sawa na asilimia 86.65 ya makadirio. Kati ya hizo shilingi 13,608,187,006 zilitumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 87.56 ya makadirio na shilingi 4,262,508 zilitumika kwa matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 2 ya makadirio.

**Majibu ya Mkoa**

Mkoa wa Kusini Unguja kupitia vote yake ya D08 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 15,748,952,435 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na mapato ya ndani, kati ya fedha hizo shilingi 1,633,864,457 kwa matumizi ya mishahara shilingi 758,630,000 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 13,305,707,978 kwa matumizi ya ruzuku .

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mkoa wa Kusini Unguja uliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 13,646,908,014 sawa na asilimia 86.65 ya makadirio, Kati ya fedha hizo shilingi 1,507,635,095 zilitumika kwa matumizi ya mishahara, shilingi 210,253,379 kazi za kawaida na shilingi 11,874,561.014 zillitumika kwa ruzuku kwa Baraza la Mji Kati na Halmashauri ya Kusini sawa na asilimia 87.56 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati yetu iliridhika na majibu ya yaliyowasilishwa.

**Hoja nambari 6.3.9.1: Mapungufu yaliojitokeza kwenye Daftari la Fedha Taslim (Cashbook)**

Ukaguzi ulikagua daftari la fedha taslim la kuwekea kumbukumbu zinazohusiana na mapato linalotumiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja na kubaini kuwepo kwa changamoto ya kurikodiwa mapato kwa kutumia “bank statement” badala ya kutumia vitabu vya risiti. Hali hii imepelekea kutokuwepo kwa risiti namba katika kumbukumbu za mapato zilizoainishwa katika daftari hilo.

Aidha ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa mchanganuo wa mapato halisi yaliokusanywa ya kila Wilaya yanayotokana na uhaulishaji wa ardhi na ucheleweshaji wa usajili wa vyeti vya vizazi kwenye daftari hilo. Kuwepo kwa mapungufu yalioainishwa hapo juu kunapelekea kutopatikana kwa uhalisia wa taarifa za mapato na pia kuwepo ugumu wakati wa kuzifatilia na kuzifanyia kazi taarifa hizo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mkoa wa Kusini kufuata taratibu za kurikodi kumbukumbu za taarifa za fedha katika daftari la kurikodia fedha taslimu (Cash Book) kwa kutumia stakabadhi za kukusanyia mapato na kuacha kurikodi kwa kutumia taarifa za kibenki “bank statements” jambo ambalo linaweza kupelekea kupokea taarifa isiyo sahihi inayotokana na kusahauliwa kwa baadhi ya stakabadhi za malipo kurikodiwa kwa usahihi au kutokurikodiwa kwa kusahauliwa.

**Majibu ya Mkoa**

Uongozi unakubaliana na hoja ya kuwepo kwa changamoto ya kurikodiwa mapato kwa kutumia “Banki statement” badala ya kutumia vitabu vya risiti. Hali hii imetokana na kuwepo mfumo wa kupeleka fomu za uhaulishaji ardhi na maombi ya usajili wa vizazi Wilayani na kurikodi mapato kwa kutumia risiti Wilayani ambako washika fedha wa Wilaya ndio wanaopokea risiti pamoja kurikodi mapato hayo katika madaftari yao “Cash Book” za Wilaya. Aidha statement za Benki hufanyiwa kazi Mkoa na kurikodi mapato halisi yanayowasilishwa benki na Wananchi kwa sababu wapo wanaolipa benki na wasiwasilishe slip zao Wilayani kwa kupatiwa risiti. Hata hivyo, Uongozi umechukua hatua ya kurekebisha kasoro hiyo kwa kutoa mafunzo ya vitendo kwa kujifunza kwa wezetu wa Mkoa wa Mjini kwa kumpeleka Msaidizi Mhasibu Mapato na kuanza kurekebisha kasoro hizi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi ambapo kasoro hiyo tayari imesharekebishwa.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Baada ya kupokea majibu yaliyowasilishwa, Kamati ya PAC haikuwa na maelezo zaidi.

**Hoja nambari 6.3.9.2: Kutofautiana kwa fedha za vifungu zilizorikodiwa kwenye Daftari Kuu na Hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 9,207,157.**

Ukaguzi umefanya uwiano baina ya daftari kuu (general ledger) na hesabu za mwisho wa mwaka zinazowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na

kubaini kutowiana kwa baadhi ya fedha za vifungu vilivyoiainishwa kwenye ripoti hizo.Hali halisi ya tofauti hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 89: Tofauti ya fedha iliyobainika katika daftari kuu na Hesabu za Mwisho wa mwaka**

| Jina la Kifungu | Makadirio ya Fedha kwa Mwaka 2020/2021 (Tshs) | Fedha Halisi Zilizoripotiwa Kwenye "General Ledger" kwa Mwaka 2020/2021 (Tshs) | Fedha Halisi Zilizoripotiwa Kwenye Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2020/2021 (Tshs) | Tofauti ya fedha Iliyojitokeza (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Ada ya uhaulishaji waardhi | 56,760,000 | 42,185,500 | 34,458,500 | 7,727,000 |
| Usafiri wa ndani | 6,000,000 | 900,000 | 2,020,000 | (1,120,000) |
| Vifaa vya kuandikia | 30,015,000 | 20,730,745 | 13,585,745 | 7,145,000 |
| "General Social welfare" | 36,180,000 | 23,911,457 | 22,510,000 | 1,401,457 |
| **Jumla** | | | | **9,207,157** |

Kutofautiana kwa fedha za vifungu vilizorikodiwa kwenye daftari kuu na hesabu za mwisho wa mwaka kunapelekea kutopatikana kwa uhalisia na usahihi wa fedha hizo na hatimae hesabu ya mapato na matumizi kutokuonesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unashauri uongozi kuhakikisha kwamba taarifa za fedha zilizorikodiwa katika daftari kuu (General Ledger) zinawiana na taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka.

**Majibu ya Mkoa**

Uongozi hakuona mapungufu yoyote ya kutowiyana kwa fedha za vifungu zilizoripotiwa kwenye daftari kuu na hesabu za Mwisho wa Mwaka katika vifungu ilivyoripotia ambavyo vimeanishwa katika jadueli. Uongozi ulilinganisha kumbukumbu hizo kutoka katika vifungu husika vya Ada ya Uhalishaji Ardhi (land transfer fees) Usafiri wa ndani (Domestic Travel), Vifaa vya Kuandikia (Stationary and Supplies) na General Social Welfare kutoka katika Notes za Financial Statements na Daftari Kuu (General Ledger) kwa mwaka wa fedha 2020-2021 ambazo kutoka katika mfumo wa Wizara ya Fedha na Mipango. Uongozi umeambatanisha na kopi ya Dafari Kuu kwa maelezo zaidi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba kuna baadhi ya wakati watendaji hupatiwa nakala ya matumizi ya Taasisi isiyokuwa ya mwisho na kupelekea kujitokeza tofauti iwapo Mfumo utahuishwa (updated). Kamati ya PAC imelichukua wazo hilo na kupanga kuliwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango ili kujua usahihi wake.

**Hoja nambari 6.3.9.3: Malipo ya Mafuta yaliyolipwa kwa fedha taslim (Cash) shilingi 2,750,000**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja ilifanya malipo yenye thamani ya shilingi 2,750,000 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa kazi za uendeshaji, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kufanya matumizi kwa njia ya mfumo wa fedha taslim wa malipo (cash) badala ya kulipa kwa kutumia njia ya benki (uhaulishaji yaani TISS) kwa kupitia watoa huduma mbali mbali.

Kufanya malipo kwa mfumo wa fedha taslim ni kwenda kinyume na sheria, kanuni na miongozo ya fedha na pia ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 90: Malipo ya Mafuta yaliolipwa kwa Fedha Taslim**

| Hati Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 2/3 ya 3/3/2021 | Zanzibar Petrolem. (Jumbi Services Station) | 500,000 | fedha kwa ajili ya ununuzi wamafuta ya Petrol |
| 1/6 ya 1/6/2021 | | 650,000 | |
| 2/3 ya 3/3/2021 | | 1,600,000 | |
| **Jumla** | | **2,750,000** | |

### Majibu ya Mkoa

Uongozi haukuwa na nia ya kukiuka sheria, kanuni na miongozo ya Serikali kwa kufanya malipo ya mafuta kwa Mfumo wa Malipo wa Fedha Taslim (Cash). Hata hivyo, Uongozi kwa sasa unahakikisha kwamba hakutokuwa na dosari nyingine inayoweza kujitokeza kwa hilo, kwa vile inaendelea kuimarisha na kusimamia vyema sheria, kanuni na miongozo ya Serikali kwa nia njema.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba Watendaji wa Mkoa walilazimika kusababisha kasoro zilizojitokeza kwa vile kulitokea shughuli za kitaifa za kufanyika kwa kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama cha ghafla na kupelekea kutumia fedha bila kwa njia ya 'cash'. Kamati haikuridhika na majibu hayo kwani Mkoa ulikuwa unaelewa kwamba kufanya hivyo ni kosa.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Mkoa uhakikishe unafanya matumizi kwa kuzingatia sheria ya Usimamizi wa Fedha za

Umma pamoja na Sheria ya Manunuzi.

**Hoja nambari 6.3.9.4: Kutorikodiwa kwa vifaa na Mafuta katika Daftari la Kumbukumbu la Ghalani shilingi 51,091,220**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 198(1) cha Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005 kinaeleza kuwa "Vifaa vyote vitakavyopokelewa ghalani haraka iwezekanavyo lazima viwekwe katika madaftari husika pamoja na vielelezo vya upokeaji wa vifaa hivyo kama inavyoelekeza katika kanuni hii".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 51,091,220 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta na vifaa mbalimbali vya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja bila ya kurikodiwa kwenye daftari la ghalani liliopo katika ngazi ya Mkoa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 198 (1) na kifungu nambari 203 (1) cha Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 91: Vifaa na Mafuta ambavyo havijarikodiwa katika Daftari la Ghalani**

| Hati Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 4/8 ya 19/08/2020 | Zanzibar Petroleum | 1,000,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petrol. |
| 28/8 ya 21/08/2020 | | 781,993 | |
| 31/8 ya 25/08/2020 | | 1,926,068 | |
| 4/10 ya 15/10/2020 | | 3,000,000 | |
| 37/10 ya 22/10/2020 | | 2,000,000 | |
| 31/10 ya 23/10/2020 | | 5,000,000 | |
| 30/8 ya 25/08/2020 | | 1,102,410 | |
| 3/11 ya 03/11/2020 | | 1,000,000 | |
| 4/11 ya 03/11/2020 | | 1,000,000 | |
| 8/2 ya 12/02/2021 | | 1,000,000 | |
| 15/2 ya 17/02/2021 | | 1,000,000 | |
| 22/2 ya 22/02/2021 | | 500,000 | |
| 11/4 ya 20/04/2021 | | 850,000 | |
| 10/5 ya 07/05/2021 | | 10,389,439 | |
| 11/5 ya 07/05/2021 | | 641,597 | |
| 12/5 ya 07/05/2021 | | 2,230,561 | |
| 36/5 ya 28/05/2021 | | 621,500 | |
| 15/6 ya 08/06/2021 | | 823,093 | |
| 9/6 ya 02/06/2021 | | 1,120,000 | |
| 9/1 ya 18/01/2021 | | 700,000 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 36/5 ya 28/05/2021 | | 10,118,500 | |
| 35/1 ya 27/01/2021 | | 500,000 | |
| 36/8 ya 25/08/2020 | Mji Mpya Bureau | 513,324 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 2/5 ya 29/04/2021 | Amo Computer Serices | 527,583 | |
| 35/8 ya 25/08/2020 | | 475,300 | |
| 21/6 ya 09/06/2021 | One to One | 907,284 | |
| 11/1 ya 18/01/2021 | Mji Mpya Secretarial Bureuau | 662,568 | |
| 4/1 ya 07/01/2021 | RJ Refrigiration and Electric | 700,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Air Condition |
| | | **51,091,220** | |

Kutoingizwa vifaa katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani kunapelekea kukosekana kwa uthibitisho wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Ukaguzi unapendekeza kwamba vifaa vyote ambavyo vinanunuliwa viingizwe katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani pamoja na vielelezo vinavyohusika na vifaa hivyo ili kuweza kuthibitisha mapokezi na matumizi ya vifaa hivyo.

## Majibu ya Mkoa

Uongozi umekwishasimamia hilo na kuhakikisha mafuta na vifaa vyote tayari vimerikodiwa katika madaftari ya ghalani baada ya kupata maelekezo muhimu kutoka kwa watendaji waliopita na watendaji wa Wilaya za Kati na Kusini ambayo yalihitajika kwa kupata ufafanuzi wa mafuta na vifaa hivyo.

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Licha ya Watendaji wa Mkoa kukubaliana na kasoro aliyoionesha Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua kwamba suala hilo lilisababishwa na nini na kuelezwa kwamba Mkoa ulikuwa ukitoa fedha kwa ajili ya matumizi ya Wilaya ambapo baada ya Wilaya kununua vifaa huwa havipitishwi katika ghala la Mkoa. Kamati imesisitiza kuwa kwa vile hizo ni fedha zilizotoka katika Mkoa, vifaa vilihitajika kupitishwa katika ghala la Mkoa na kurikodiwa kama alivyoeleza Mkaguzi.

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Mkoa uandae utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu zake hususan vifaa vinavyonunuliwa view vinarikodiwa katika daftari la ghalani.
2. Mkoa uhakikishe unampatia Mkaguzi vielelezo anavyohitaji ili aweze kujiridhisha na usahihi wa taarifa za utekelezaji za Mkoa.

## FUNGU D09 - MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

## Taarifa ya Mapato

Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulikadiriwa kukusanya

jumla ya shilingi 17,372,646,710. Kati ya hizo jumla ya shilingi 27,500,000 zilikadiriwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Mkoa, jumla ya shilingi 17,115,146,710 zilikadiriwa kupatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ikiwa ni ruzuku na jumla ya shilingi 230,000,000 zilikadiriwa kupatikana ikiwa ni msaada.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 15,223,044,277 zilipokelewa ikiwa sawa na asilimia 87.6 ya makadirio, kati ya hizo jumla ya shilingi 12,645,000 zilipokelewa kutoka vyanzo vya ndani vya Mkoa sawa na asilimia 45.9 ya makadirio, jumla ya shilingi 15,000,761,277 zilipatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 87.6 ya makadirio na jumla ya shilingi 206,638,000 zilipatikana ikiwa ni msaada kutoka kwa washirika wa maendeleo na wananchi sawa na asilimia 89.8 ya makadirio.

### Majibu ya Mkoa

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Mkoa wa Kaskazini Unguja ulikisia kupata jumla ya TZS. 17,372,646,710.00 lakini fedha iliyopatikana ilikuwa ni TZS. 15,223,044,270.00 kutoka katika vyanzo mbali mbali vya upatikanaji wa fedha hizo.

Mkoa wa Kaskazini Unguja unakusanya mapato yake kutokana na chanzo cha uhaulishaji wa ardhi, lakini mapato hayo si ya kutegemea ni chanzo chenye ugumu wa kutabirika.

**Jadweli Nam. 1: Ufafanuzi wa makisio na makusanyo kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.**

| Maelezo | Makisio yamwaka 2020/2021 | Mapatohalisi(Zilizopatikana) | Tofauti | Asilimiaya mapato. |
|---|---|---|---|---|
| Mishahara | 1,504,200,000 | 1,466,952,855 | 37,247,145 | 97.62 % |
| Fedha za kuendeshea Ofisi (OC) | 526,700,000 | 247,503,972 | 279,196,028 | 46.99 % |
| RuzukuyamatumiziyakuendesheaOfisikwaMabarazayaMji(Subvention for Other Charge) | 1,822,900,000 | 454,403,675 | 1,368,496,325 | 24.93 % |
| RuzukuyamishaharayaMabarazayaMji (Subvention forSalary) | 13,262,846,710 | 12,834,900,775 | 427,945,935 | 96.77 % |
| **Jumlandogo** | **17,115,146,710** | **15,003,761,277** | **2,111,385,433** | **87.66%** |
| WashirikawaMaendeleo–(UNICEF) | 230,000,000 | 206,638,000 | 23,362,000 | 89.84% |
| Uhaulishajiwa Ardhi | 27,500,000 | 12,645,000 | 14,855,000 | 45.98% |
| **Jumlakubwa** | **17,372,646,710** | **15,223,044,270** | **2,149,602,440** | **87.63%** |

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC ilipotaka kujua vyanzo vya mapato ya Mkoa ilielezwa kwamba awali

Mkoa ulikuwa na chanzo cha usajili wa vizazi na vifo lakini baada ya mabadiliko (ugatuzi), chanzo hicho kiliondolewa na Serikali na kubakia na chanzo cha 'late registration'. Hata hivyo, Kamati yetu imebaini kwamba chanzo hicho hakijaainishwa katika majibu ya Mkoa na kuifanya Kamati kukosa kujua mapato halisi yanayotokana na chanzo hicho. Kamati hatimae iliridhika na majibu ya Mkoa licha ya kuwepo kwa kasoro hiyo.

**Taarifa ya Matumizi**

Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 17,345,146,710 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na mapato yao ya ndani, kati ya hizo shilingi 17,233,766,710 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 111,380,000 kwa matumizi ya maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mkoa wa Kaskazini Unguja uliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 15,203,210,367.8 sawa na asilimia 87.6 ya makadirio. Kati ya hizo shilingi 15,142,149,917.8 zilitumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 87.8 ya makadirio na shilingi 61,060,450 zilitumika kwa matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 54.8 ya makadirio.

**Majibu ya Mkoa**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mkoa wa Kaskazini Unguja ulikisia kutumia jumla ya TZS. 17,345,146,710.00. Hadi kumaliza mwaka, fedha zilizotumika ni TZS. 15,203,210,367.80 sawa na asilimia 87.65. Matumizi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja yameonekana kutokufikia lengo kwa mwaka huu. Hali hii ilitokana na kutotekelezwa kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa kutokana na upungufu wa fedha hasa zile zilizotegemewa kwa ajili ya kuendeshea Ofisi (OC).

**Jadweli Nam. 2: Ufafanuzi wa matumizi kwa mwaka wa Fedha 2020/2021**.

| **Maelezo** | **Makisioyamwaka 2020/2021** | **Matumizi halisi** | **Tofauti** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| Mishahara (Personnel Emoluments) | 1,504,200,000 | 1,466,952,855 | 37,247,145 | 97.52 |
| UpatikanajiwaRuzuku za MabarazayaMji. | 15,085,746,710 | 13,289,304,450 | 1,796,442,260 | 88.90 |
| Vifaanabidhaa za matumizi (Supplies and Consumable Goods) | 324,562,158 | 133,308,574.00 | 191,253,584 | 41.07 |
| Matengenezonaukarabatiwakawaida (Routine Maintenance and Repair) | 25,572,864 | 16,355,000.00 | 9,217,864 | 63.98 |
| Kusaidiawazeenawanan | 38,640,000 | | 9,805,000 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| chikatikashughuli za kijamii (social benefit) | | 28,835,000 | | 74.62 |
| Matumizimengineyo | 25,044,978 | 7,944,948. | 17,100,030 | 31.72 |
| Matumizi yanayohusiana na fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 230,000,000 | 199,449,090.80 | 30,550,909.20 | 83.72 |
| **Jumlandogo** | **17,233,766,710** | **15,142,149,917.8** | **2,091,616,792.2** | **87.86** |
| Ununuzi wa mali (purchase of assets) | 111,380,000 | 61,060,450 | 50,319,550 | 54.82 |
| **Jumla kubwa** | **17,345,146,710** | **15,203,210,367.8** | **2,141,936,342.20** | **87.65** |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilipokea majibu ya Taarifa ya Matumizi na haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.3.10.1: Kukosekana kwa Wasimamizi wa Mapato**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 61(1) cha Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005 kinaeleza kwamba "Afisa utumishi hatoweza kukusanya mapato ya Serikali isipokuwa awe ameruhusiwa kufanya hivyo".

Ukaguzi ulifanya mahojiano na watendaji wanaoshughulika na ukusanyaji wa mapato wa Wilaya ya Kaskazini "A" na "B" na kubaini kwamba watendaji wanakusanya mapato kinyume na nyadhifa walizokuwa nazo katika Ofisi zao. Katika Wilaya ya Kaskazini "B" afisa tarishi hutumika katika zoezi la ukusanyaji wa mapato na katika Wilaya ya Kaskazini "A" kumbukumbu za mapato hurikodiwa na mwangalizi wa Ofisi badala ya mtendaji anaehusiana na masuala ya fedha. Aidha kutokana na dosari iliyobainika hapo juu ukaguzi haukuweza kupatiwa uthibitisho na vielelezo vinavyowataka watendaji hao kufanya shughuli ya ukusanyaji wa mapato kinyume na kada wanazozifanyia kazi.

Uwepo kwa wakusanyaji wa mapato wasiokuwa na taaluma ya kazi wanazozifanya kunaweza kukapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma na hatimae kukosekana kwa taarifa na kumbukumbu za ukusanyaji wa mapato zilizoandaliwa kitaalamu.

**Majibu ya Mkoa**

Tunakiri kuwa Wilaya ya Kaskazini "A" na Wilaya ya Kaskazini "B" kulikuwa hakuna Washika Fedha wakufuatilia ukusanyaji wa mapato. Kwa mnasaba huo, hivi sasa tayari tumeshapatiwa Washika Fedha kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ili kuondosha dosari zilizojitokeza. Hata hivyo, mapato hayo yanayotokana na uhaulishaji wa ardhi si chanzo cha kutegemea kwa vile tozo inayotozwa ni TZS. 50,000/- tu kwa kila uhaulishaji.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Watendaji wa Mkoa wamekubaliana na hoja ya Mkaguzi na kueleza kwamba hilo limejitokeza kwa Mkoa ulikuwa hauna watendaji wa fedha ambapo awali watendaji wa kada nyeingine walikuwa wanatumiwa kushughulikia makusanyo ya mapato. Hata hivyo, hivi sasa changamoto hiyo imesharekebishwa ambapo Mkoa inae Muhasibu na Msaidizi wa fedha.

**Hoja nambari 6.3.10.2: Kutokuwepo ripoti za ukusanyaji wa mapato**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja inakusanya mapato mbali mbali yatokanayo na vyanzo vya mapato, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuwepo kwa ripoti za ukusanyaji wa mapato jambo ambalo linapelekea ugumu wa kuweza kuthibitisha uhalali na uhalisia wa fedha zilzokusanywa na zilizowasilishwa kutoka ngazi za Wilaya kwenda ngazi za Mikoa.

Kutokuwepo kwa ripoti za ukusanyaji wa mapato kunapelekea kutokupatikana kwa kumbu kumbu halisi ya kima cha fedha kilichokusanywa kulingana na makadirio yaliyopangwa jambo ambalo litaikosesha taasisi kuweza kuitathmini juu ya kufikia lengo lililopangwa kukusanywa na hatimae kupelekea uwepo wa makadirio makubwa ambayo hayataweza kufikiwa kwa mwaka unaofuata.

Ukaguzi unashauri Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ihakikishe kwamba inawasimamia vyema watendaji wao katika suala zima la kuweka kumbukumbu za taarifa za mapato ya kila mwezi na za miezi mitatu ili kujua uhalisia wa makusanyo kwa kulinganisha na daftari la kurikodia fedha taslim.

**Majibu ya Mkoa**

Uongozi unakubalina kupokea mapendekezo yaliyotolewa na Ofisi yako na hatua tumeanza kuchukua za uaandaaji wa ripoti hizo kila mwezi, miezi mitatu, miezi sita, miezi tisa pamoja na mwaka. Hata hivyo, ripoti za ukusanyaji wa mapato hutakiwa ziwasilishwe kila mwezi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kutokuwepo Watendaji wa Kada ya Fedha ndio kulikopelekea kasoro hii kijitokeza kama ilivyoelezwa katika hoja iliyopita. Kwa vile Mkoa tayari umeanza kutekeleza ushauri wa Mkaguzi, kamati yetu haikuwa na maelezo zaidi.

**Hoja nambari 6.3.10.3: Kutokuthibitishwa kazi kwa watumishi wa Umma**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 9(1) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 inaeleza kwamba " Bila ya kuathiri kifungu cha 60 cha sheria ya Ajira namba 11 ya 2005, mtumishi yeyote ambae ameajiriwa kwa mara ya kwanza atalazimika kuwemo katika majaribio ya utumishi kwa muda wa miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuajiriwa".

Ukaguzi umebaini uwepo wa watendaji 11 walioajiriwa kwa mara ya kwanza ambao hawajathibitishwa kuwa wafanyakazi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja licha ya kuwa wameshapitiliza miezi kumi na mbili toka kuajiriwa. Mchanganuo wa wafanyakazi hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 92: Wafanyakazi waliokuwa hawajathibitishwa kazi**

| Jina Kamili | Kada Aliyoajiriwa | rehe yaAjira | rehe Aliyopaswa Kuthibitishwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Salha M. Suleiman | Afisa Utumishi | 28/07/2019 | 28/07/2020 | Hakuna hatua zozote zilizochukuliwa |
| Nasra Suleiman Mtumwa | Karani Masjala | 01/09/2019 | 01/09/2020 | |
| Khatib Khamis Ali | Afisa Tehama | 21/10/2019 | 21/10/2020 | |
| Abdulhamid Kh. Haji | Fundi Mchundo | 21/10/2019 | 21/10/2020 | |
| Hassan M. Hassan | Afisa Takwimu | 21/10/2019 | 21/10/2020 | |
| Hadia Muhidini Khamis | Muhudumu | 01/12/2019 | 01/12/2020 | |
| Munira Omar Othmani | Mtunza ghala | 07/03/2020 | 07/03/2021 | |
| Patima J. Haji | Mtunza ghala | 07/03/2020 | 07/03/2021 | |
| Tatu Khamis Moh'd | Karani Masjala | 27/03/2020 | 27/03/2021 | |
| Mwanaisha Manzil Nawaje | Karani Masjala | 27/03/2020 | 27/03/2021 | |
| Saleh Haruob Saleh | Tarishi | 21/03/2020 | 21/03/2021 | |

Kutokuwathibitisha watendaji walioajiriwa kwa wakati kunapelekea kuwakosesha haki zao za msingi ikiwemo fursa za kupata mikopo, fursa ya masomo ya muda mrefu, pamoja na kuwakosesha fursa za uingiaji wa mikataba ya kimaendeleo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini uhakikishe kwamba wanachukua hatua za haraka kuwathibitisha watendaji hao kwa wale waliotimiza masharti kwa lengo la kuwapatia fursa na stahiki zao kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa umma.

## Majibu ya Mkoa

Uongozi unakubalina kupokea mapendekezo yaliyotolewa na Ofisi yako na hatua za haraka zimeshachukuliwa za kuwathibitisha watendaji hao 11. Kwa mnasaba huo, wafanyakazi tayari wote wameshathibitishwa kazi.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Watendaji wa Mkoa wa kaskazini kukubaliana na hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilitaka kujua sababu iliyopelekea Watumishi hao kutokuthibitishwa na kuelezwa kwamba suala hilo lilisababishwa na ukosefu wa fedha za kuwalipia mafunzo ya 'inductive Course' yanayotolewa na Chuo cha Utawala wa Umma kama inavyoelekezwa na matoleo ya Afisi Kuu ya Utumishi.

Kwasasa Watumishi hao wameshathibitishwa kazini kupitia barua ya tarehe 26/5/2022 yenye kumbukumbu nambari TUS/OR/C/KW/14/27/16 ambayo Kamati imeiona na kukubaliana nayo. Kwa mnasaba huo, Kamati yetu iliridhika na majibu hayo na haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.3.10.4: Kutokuwasilishwa kwa fedha za makato ZSSF shilingi 15,636,653**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 17(1-3) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii nambari 2 ya mwaka 2014 kinazitaka "Taasisi za Umma kuwasilisha makato ya mishahara ya wafanyakazi wake kwa kila mwezi kwa mujibu ya kiwango kilichowekwa kwa mujibu wa matakwa ya sheria hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 15,636,653 za makato ya mwezi wa Januari zilikatwa kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba makato hayo hayakuwasilishwa ZSSF kwa wakati kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo badala yake ziliweza kutumika kwa mambo mengineyo na kupelekea kuwasilishwa mwezi wa Februari 2021 jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kuhakikisha unawasilisha fedha za mikato ya watumishi wao kwa wakati ZSSF ili kuepuka gharama ya tozo ya adhabu kwa taasisi itakayobainika kuchelewa kuwasilisha fedha hizo na kupelelekea kuingiza hasara Serikali.

**Majibu ya Mkoa**

Tumepokea ushauri uliotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Uongozi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja inathibitisha kwamba fedha za michango ya ZSSF hazikutumika kwa matumizi mengine. Ufafanuzi juu ya suala hili ni kwamba mshahara wa mwezi wa Januari, 2021 uliingizwa na mapungufu ya asilimia 13% na kupelekea kushindwa kuwasilisha michango hiyo kwa wakati muafaka. Na mara tu baada ya fedha kutoka Ofisi Rais, Fedha na Mipango zilipoingizwa michango hiyo iliwasilishwa ZSSF.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Ilivyokuwa kasoro zilizojitokeza zimerekebishwa na Mkoa, Kamati ya PAC haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.3.10.5: Kukiukwa kwa makubaliano ya mkataba**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja imeingia mkataba wenye nambari No.SMZ/D09/ G/Q/2019/2020/001 uliofungwa tarehe 3/6/2020 baina ya Zenj Motors

Company Ltd na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja wenye thamani ya shilingi 95,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa basi la utoaji wa huduma za usafiri kwa ajili ya wafanyakazi wa Ofisi hiyo.

Kwa mujibu wa makubaliano yaliomo kwenye mkataba "Malipo yatalazimika kulipwa kwa awamu mbili". Awamu ya mwanzo yatalipwa mara tu baada ya kusainiwa kwa mkataba kwa asilimia 70 sawa na shilingi 66,500,000 awamu ya pili italipwa kwa asilimia 30 sawa na shilingi 28,500,000 baada ya kukabidhi basi hilo kwa muajiri na muajiri kuridhika nalo.

Dosari za ukaguzi zilizobainika ni kukosekana kwa makubaliano ya kufanya malipo kinyume na asilimia zilizoainishwa katika mkataba ambapo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja imefanya malipo ya awamu ya kwanza ya asilimia 42.1 na malipo ya awamu ya pili ya asilimia 57.9. Aidha ukaguzi umebaini malipo hayo yamehaulishwa kutoka katika vifungu mbali mbali lakini hatukuweza kupatiwa vielelezo na kumbu kumbu za barua na taratibu zilizopelekea kufanyika kwa uhaulisho huo jambo ambalo linaweza kupelekea kuathiri matumizi ya bajeti ya vifungu husika.

Ukaguzi unashauri watendaji wanaohusiana na ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kuwa makini katika kufuata sheria na kanuni pale wanapotekeleza majukumu yao ya kiutendaji ya kila siku ili kuepuka uvunjaji wa sheria.

**Majibu ya Mkoa**

Tunapenda kukiri kuwa dosari hizi zilizojitokeza kwa kulipa kinyume na mkataba, zilitokana na uhaba wa fedha na kupelekea kushindwa kufuata mkataba. Hata hivyo, Mtoa huduma alikubali tumlipe kutokana na hali ya kifedha ilivyokuwa kwa wakati ule.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini Watendaji wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, hawakufuata masharti ya Mkataba wa ununuzi wa basi la usafiri ambapo mambo kama hayo yanaweza kuisababishia hasara Serikali iwapo Mtoa huduma akiamua kushitaki.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Ofisi ya Mkoa wa kaskazini Unguja wahakikishe wanatekeleza masharti ya Mikataba wanayoingia na Watoa huduma kama zinavyoelekeza Sheria za usimamizi wa fedha.

**Hoja nambari 6.3.10.6: Kutorikodiwa kwa Mafuta Kwenye Daftari la Ghalani shilingi 24,098,386**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 198(1) cha Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005 kinaeleza kuwa "Vifaa vyote vitakavyopokelewa ghalani haraka iwezekanavyo lazima viwekwe katika madaftari husika pamoja na vielelezo vya upokeaji wa vifaa hivyo kama inavyoelekeza katika kanuni hii". Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja imefanya matumizi mbali mbali kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa kazi za uendeshaji, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokurikodiwa kwa manunuzi hayo kwenye daftari la kumbu kumbu za manunuzi jambo ambalo tumeshindwa kuthibitisha uhalali wa matumizi hayo.

Kutokurikodiwa kwa taarifa za manunuzi kunaweza kukapelekea udanganyifu katika manunuzi na hatimae kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kuhakikisha unaimarisha udhibiti wa ndani juu ya usimamizi wa mafuta katika ngazi zote za Mkoa na Wilaya.

Mchanganuo wa manunuzi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 93: Matumizi ya Mafuta ambayo hayajarikodiwa kwenye Daftari la Ghalani**

| Hati Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 6/6 ya 10/6/2021 | Gapco Zanzibar Ltd | 1,060,326 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |
| 4/8 ya 19/8/2020 | | 1,800,000 | |
| 5/8 ya 19/8/2020 | Zanzibar Petroleum Ltd | 2,000,000 | |
| 10/8 ya 13/8/2020 | | 188,500 | |
| 3/8 ya 11/8/2020 | | 1,000,000 | |
| 21/6 ya 14/6/2021 | | 880,000 | |
| 8/10 ya 6/10/2020 | | 2,000,000 | |
| 10/10 ya 14/10/2020 | | 200,000 | |
| 36/10 ya 26/10/2020 | | 498,680 | |
| 28/1 ya 28/1/2021 | | 742,300 | |
| 2/3 ya 25/2/2021 | | 2,500,000 | |
| 17/4 ya 23/4/2021 | United Group Ltd | 4,000,000 | |
| 28/5 ya 24/5/2021 | | 7,228,580 | |
| **Jumla** | | **24,098,386** | |

## Majibu ya Mkoa

| Hati Nam. | Alielipwa | Thamani (Tshs) | Risiti/Ankara Namba | Maelezo | Majibu ya Mkoa |
|---|---|---|---|---|---|
| 3/8 ya 11/8/2020 | Zanzibar Petroleum Ltd | 1,000,000 | Risiti nambari 56592/ Ankara | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa | Mafuta haya yalinunuliwa Wilaya ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | nambari 937 | mafuta kwa matumizi ya Ofisi Mkoa wa Kaskazini Unguja | Kaskazini A na yameingizwa ghalani tarehe 14/08/2020 |
| 4/8 ya 19/8/2020 | Gapco Zanzibar Ltd | 1,800,000 | Ankara nambari 2362 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa matumizi ya Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja. | Mafuta haya yalinunuliwa Wilaya ya Kaskazini B yameingizwa ghalani tarehe 17/8/2020 |
| 5/8 ya 19/8/2020 | Zanzibar Petroleum Ltd | 2,000,000 | Risiti nambari 56745/ Ankara nambari 1005 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa matumizi ya Ofisi ya Wilaya Kaskazini A na Mkoa wa Kaskazini. | Mafuta haya yalinunuliwa Wilaya ya Kaskazini A yameingizwa ghalani tarehe 29/08/2020 |
| 10/8 ya 13/8/2020 | Zanzibar Petroleum Ltd | 188,500 | Risiti nambari 6366/ | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya mafuta kwa kazi za Idara ya Uchumi na Uzalishaji. | Haya ni marejesho ya fedha kwa ununuzi wa mafuta siku mbali mbali alizotumia mfanyakazi kwa kufuatilia kazi za Ofisi. |
| 28/5 ya 24/5/2021 | United Petroleum | 7,228,580 | Risiti nambari 3237/ Ankara nambari 3679 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa ajili ya kuuaga | Mafuta haya yamerikodiwa katika Halmashauri ya Kaskazini B. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mwili wa marehemu JPM Halmashauri ya Kaskazini B | na yameingizwa tarehe 31/3/2021 jumla yalita 5830 za diesel. |
| 8/10 ya<br><br>6/10/2020 | Zanzibar Petroleum Ltd | 2,000,000 | Risiti nambari 57122/ Ankara nambari 1171 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Wilaya ya Kaskazini B | Mafuta haya yalinunuliwa Wilaya ya Kaskazini B na yameingizwa ghalani tarehe 6/10/2020 |
| 10/10 ya<br><br>14/10/2020 | Zanzibar Petroleum Ltd | 200,000 | Risiti nambari 57256/ Ankara nambari 1176 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa Wilaya ndogoTumbatu | Mafuta haya yameingizwa ghalani |
| 36/10 ya<br><br>26/10/2020 | Zanzibar Petroleum Ltd | 498,680 | Risiti nambari 57336/ Ankara nambari 1253 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa ajili ya matumizi ya Ofisi | Mafuta haya yalinunuliwa Wilaya ya Kaskazini B na yameingizwa ghalani tarehe 26/10/2020 |
| 28/1 ya<br><br>28/1/2021 | Zanzibar Petroleum Ltd | 742,300 | Risiti nambari 58282/ Ankara nambari 114 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A | Mafuta haya yameimgizwa ghalani. |
| | | | | | |
| 2/3 ya<br><br>25/2/2021 | Zanzibar Petroleum Ltd | 2,500,000 | Risiti nambari 58712/<br><br>Ankara nambari 229 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B | Mkoa wa Kaskazini – 1,500,000 – yameingizwa katika daftari la ghalani tarehe 11/3/2021<br><br>Wilaya ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Kaskazini A – 500,000 yameingizwa ghalani, Wilaya NdogoTumbatu – 500,000 – yameingizwa ghalani. |
| 17/4 ya<br><br>23/4/2021 | United Group Ltd | 4,000,000 | Risiti nambari 2649/<br><br>Ankara nambari 3679 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa kumuaga Mh. marehemu John Pombe Magufuli | Mafuta haya yamerikodiwa katika Halmashauri ya Kaskazini B. na yameingizwa tarehe 31/3/2021 jumla ya lita 5830 za diesel. |
| 6/6 ya<br><br>10/6/2021 | Gapco Zanzibar Ltd | 1,060,326 | Risiti nambari 3601/<br><br>Ankara nambari 2705 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B | Mafuta haya yalinunuliwa Wilaya ya Kaskazini B na yameingizwa ghalani tarehe 18/6//2021 |
| 21/6 ya<br><br>14/6/2021 | Zanzibar Petroleum Ltd | 880,000 | Risiti nambari 59817/<br><br>Ankara nambari 687 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta Ofisi ya Wilaya ndogo Tumbatu | Yameingizwa ghalani tarehe 11/6/2021. |
| **Jumla** | | **24,098,386** | | | |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati baada ya kupata majibu ya hoja hii iliridhika na haikuwa na hoja.

## MKOA WA KUSINI PEMBA

### Tarifa ya Mapato

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 25,700,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali. Hadi kufikia tarehe juni 2021 jumla ya shilingi 16,248,955 zilikusanywa na ofisi mkoa wa kusini Pemba sawa na asilimia 63.23 ya makadirio.

### Majibu ya Mkoa

Kwa mwaka 2020/2021 Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba ilipanga kukusanya shilingi 25,700,000 ambapo hadi kufikia mwezi Juni 30, 2021, Ofisi ilikusanya katika Mfuko Mkuu wa Serikali shiling 16,248,955 sawa na asilimia 63.23 ya makadirio. Vyanzo vya mapato hayo ni vitatu ambavyo ni ucheleweshaji wa Usajili wa Vizazi (Late registration birth), Ada itokanayo na Uhaulishaji wa Ardhi na Kodi ya Majengo.

### Taarifa za Mapato kwa mwaka 2020/2021

| Chanzo | Makadiro (Tzs) | Halisi (Tzs) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| Uhaulishaji wa ardhi | 5,100,000 | 1,600,000 | 31.37 |
| Kodi ya majengo | 7,200,000 | 7,200,000 | 100.00 |
| Fomu za vyeti vya kuzaliwa | 13,400,000 | 7,448,955 | 55.59 |
| **Jumla ya mapato** | **25,700,000** | **16,248,955** | **63.23** |

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imehoji kuhusiana na vyanzo vya mapato vya Mkoa wa Kusini Pemba na kubaini kuwa katika chanzo cha mapato yatokanayo na fomu za vyeti ya kuzaliwa haikufikia malengo (55.59 asilimia), Kamati imeelezwa kuwa kushuka kwa asilimia ya makusanyo kumetokana na kupangiwa makadirio makubwa kinyume na uwezo wa Mkoa huo. Kwani inaonekana Wizara ya Fedha na Mipango huwapangia makusanyo pasi na kufanya utafiti hususan kwa vyanzo visivyokuwa na uhakika kama vya Fomu za vyeti vya kuzaliwa.

**Mapendekezo ya kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuchukua juhudi za makusudi kufanya utafiti mdogo wa kufuatilia vyanzo vya mapato vya Mkoa wa Kusini ili kupata uhalisia wa mapato wanayotakiwa kukadiriwa kukusanywa na Mkoa huo.

**Tarifa ya Matumizi**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 14,460,900,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 13,818,960,775 zimetumika kwa kazi za kawaida ambapo ni sawa na asilimia 97.82 ya makadirio.

**Majibu ya Mkoa**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mkoa ulitarajia kupata jumla ya shilingi 14,805,151,140. Hadi kufikia Juni 30, 2021, Mkoa ulingiziwa jumla ya shiling 13,818,960,775 sawa na asilimia 93.34 ya Makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 1,361,551,140 sawa na asilimia 96.8 ni Mishahara, Shilingi 262,361,725 sawa na asilimia 34.07 ni Matumizi mengineo (OC). Aidha kwa upande wa Ruzuku Jumla ya shilingi 12,238,603,545 sawa na asilimia 96.6 ni zilipatikana kwa Baraza la Mji Chake Chake na Mkoani.

**Matumizi ya Mkoa wa Kusini Pemba kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

| Fungu | Makadirio (Tzs) | Halisi (Tzs) | Asilimia (% |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 1,361,551,140 | 1,317,995505 | 96.80 |
| Matumizi mengineo | 770,100,000 | 262,361,725 | 34.07 |
| Ruzuku | 12,673,500,000 | 12,673,500,000 | 96.57 |
| **Jumla ya Matumizi** | **14,805,151,140** | **13,818,960,775** | **93.34** |

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imehoji kuhusiana na kushuka kwa mshahara hadi kufikia asilimia 96.80 na imeelezwa kuwa hali hiyo imetokana na ugatuzi wa kuhamishwa kwa Watendaji na kurudishwa katika maeneo walikuwepo awali jambo ambalo lilisababisha kutowalipa baadhi ya mishahara na kupelekea asilimia ya matumizi ya mshahara kufikia 96.80. Kamati ya PAC iliridhika na majibu hayo na haikuwa na hoja zaidi.

### MKOA WA KASKAZINI - PEMBA

### Taarifa ya Mapato

Kwa Mwaka 2020/2021 Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba ilipanga kukusanya Shilingi 25,476,000 hadi kufikia mwezi Juni 2021 Afisi ilikusanya na kuingiza katika Mfuko Mkuu wa Serikali Shiling 13,420,000 sawa na asilimia 52.7 ya makadirio.

### Majibu ya Mkoa

Upungufu katika makusanyo hayo unatokana na vyanzo kidogo vya Mapato ikiwemo; Ada za Usajili wa Vizazi na vifo (Late registration), Uhaulishaji wa Ardhi na Ukodishaji wa Kituo cha Mafuta (Wete Petrol Station) ambapo vyanzo viwili vya Ada ya Usajili wa Vizazi na Vifo na Ada ya Uhaulishaji wa Ardhi ni vyanzo tegemezi.

| Chanzo | Makadirio (Tzs.) | Halisi (Tzs.) | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Uhaulishaji wa Ardhi | 5,000,000 | 600,000 | 12.0 |
| Kodi ya Majengo | 3,000,000 | 3,000,000 | 100.0 |
| Fomu za vyeti vya kuzaliwa | 17,476,000 | 9,820,000 | 56.2 |
| **Jumla** | **25,476,000** | **13,420,000** | **52.7** |

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Uongozi wa Mkoa kuwasilisha majibu yaliyofafanua vyanzo vya mapato yake. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua sababu ya chanzo cha mapato ya Fomu za vyeti vya kuzaliwa (late registration) kutofikia lengo la makusanyo na kuelezwa kwamba kulitokea Mdhamini aliyewalipia fedha maskini moja kwa moja katika Afisi Kuu ya Usajili wa Matukio ya Kijamii. Kamati yetu ilifuatilia suala hilo kwa kukutana na Uongozi wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii katika Makao Makuu yao siku ya tarehe 10/2/2023 na kubaini kwamba maelezo hayo hayakuwa ya ukweli na sahihi kwani Kamati ilielezwa kwamba hakuna mapato yaliyolipwa na Mdhamini yeyote kwa huduma za usajili wa vyeti kwa watu waliokuwa hawakusajiliwa awali (late registration). Kwa mnasaba huo, Watendaji wa Mkoa waliidanganya Kamati kwa kuipatia majibu yasiyokuwa sahihi na yenye uhakika wa kile wanachokijibu jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria ya Fursa, Kinga na Uwezo wa Wajumbe.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Uongozi wa Mkoa uwe makini na majibu rasmi inayoyawasilisha hususan kwa Kamati za Baraza la Wawakilishi kwani kutoa majibu yasiyosahihi ni kuipotosha Kamati na ni kosa la jinai.

### Taarifa ya Matumizi

Kwa upande wa Matumizi, Mkoa ulipanga kutumi shilingi 13,149,224,000 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 2,045,024,000 ni matumizi kwa kazi za kawaida, Shilingi 1,226,400,000 ni Mishahara na shilingi 818,624,000 ni Matumizi Kuendeshea Afisi (OC). Aidha Shilingi 11,104,200,000 ni Ruzuku kwa ajili ya Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

### Majibu ya Mkoa

Kwa Mwaka 2020/2021 upatikanaji wa fedha kwa ujumla ulikuwa wa kuridhisha Shilingi 11,808,930,143 sawa na asilimia 89.8 ya Makadirio zilipatikana, Kati ya fedha hizo shiling 1,521,189,460 ni kwa kazi za kawaida, ambapo shiling 1,278,847,460 sawa na asilimia 104.3 ni Mishahara na Shiling 242,342,000 sawa na asilimia 29.6 ni Fedha za kuendeshea Afisi (OC). Aidha Shilingi 10,287,740,683 sawa na asilimia 92.6 ni Ruzuku kwa ajili ya Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

| Fungu | Makadirio (Tzs.) | Halisi (Tzs.) | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 1,226,400,000 | 1,278,846,460 | 104.3 |
| Matumizi mengineyo | 818,624,000 | 242,342,000 | 29.6 |
| Ruzuku | 11,104,200,000 | 10,287,740,683 | 92.6 |
| **Jumla** | **13,149,224,000** | **11,808,930,143** | **89.8** |

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Baada ya kuwasilishwa majbu hayo, Kamati ya PAC ilitaka kujua kwanini mishahara ya wafanyakazi iliongezeka kufikia asilimia 104.3 na kuelezwa kwamba kulikuwa na ongezeko la mishahara pamoja na kuteuliwa kwa baadhi ya viongozi wapya katika Mkoa huo. Kupitia majibu hayo, Kamati ya PAC haikuwa na hoja zaidi.

## FUNGU D12 - WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

## Taarifa ya Mapato

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imekadiria kukusanya jumla ya shilingi 626,512,000 kutoka katika vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ilikukusanya jumla ya shilingi 636,084,634 sawa asilimia 101.5 ya makadirio.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikupokea majibu ya Taarifa za Mapato siku mbili kabla ya kikao husika kama inavyoelekeza Kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020). Hata hivyo Kamati ya PAC ilitaka kujua sababu ya kuvuka lengo la makusanyo na kuelezwa kwamba wananchi walihamasika kufanya maombi ya vyeti na vitambulisho pamoja na kuwepo kwa uhakiki wa vyeti uliopelekea kugundulika kwamba vyeti vingi ni feki na kuwafanya wananchi kufuatilia. Kwa majibu hayo, Kamati ya PAC haikuwa na maelezo zaidi.

## Taarifa ya Matumizi

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 4,993,414,808 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 kiasi cha shilingi 2,598,752,604 kimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 52 ya makadirio.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kadhalika, Kamati ya PAC haikupokea majibu ya Taarifa za Matumizi siku mbili kabla ya kikao husika kama inavyoelekeza Kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020). Hata hivyo, Wakala uliieleza Kamati kwamba kwa mwaka huo hawakufikia malengo yao waliyoyapanga kwa vile kulikuwa na upungufu wa fedha walizopatiwa.

**Hoja nambari 6.3.13.1: Kuwepo kwa tofauti ya fedha baina ya hesabu ya mwisho wa mwaka na matumizi halisi shilingi 290,425,367**

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia taarifa mbali mbali zikiwemo taarifa za Hesabu ya mwaka, daftari la kurikodia kumbukumbu za fedha pamoja na hati za malipo imebainika kwamba Jumla ya shilingi 290,425,367 ni tofauti ya fedha iliyojitokeza baina ya Hesabu za mwisho wa mwaka ikilinganishwa na matumizi halisi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Viwango vya ufungaji wa hesabu vya kitaifa na kimataifa ambapo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamaizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba hesabu za mwisho wa mwaka zinawiana na matumizi halisi yaliofanyika katika kipindi cha mwaka husika ili kuweza kuonyesha usahihi wa hesabu hizo. Mchanganuo wa baadhi ya vifungu vilivyoonesha tofauti hiyo ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 94: Tofauti baina ya taarifa ya fedha na matumizi halisi**

| Vifungu vya matumizi | Makadirio | Kiasi cha fedha kilichoainishwa katika hesabu (Tshs) | Kiasi cha fedha kilichotumika (Tshs) | Tofauti ya fedha iliyojitikeza (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Petrol | 188,870,000 | 66,898,035 | 45,048,860 | 21,849,175 |
| Sitting Alowance | 46,950,000 | 32,848,830 | 31,788,830 | 1,060,000 |
| Food and refreshment | 34,250,000 | 25,124,000 | 14,650,000 | 10,474,000 |
| Domestic Travel | 49,556,407 | 37,297,306 | 20,303,633 | 16,993,673 |
| Foreign Travel | 58,500,000 | 30,000,000 | 0 | 30,000,000 |
| Government Offices Electricity Bills | 190,000,000 | 108,666,722 | 84,799,130 | 84,799,130 |
| Stationary Supply | 49,000,000 | 49,000,000 | 37,917,000 | 11,083,000 |
| Printing Expenses | 809,700,000 | 265,180,690 | 146,146,726 | 119,033,964 |
| Cleaning Supply | 55,000,000 | 54,581,600 | 37,600,000 | 16,981,600 |
| **Jumla** | **1,292,956,407** | **602,699,148** | **373,205,319** | **290,425,367** |

**Majibu ya Wakala**

Uongozi wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA), ulikubaliana na ukaguzi uliofanyika kwa hesabu za mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 ya kuwepo tofauti baina ya taarifa ya fedha na matumizi halisi.

Uongozi umeeleza kwamba tofauti hiyo ilitokana na kutojumuishwa kwa matumizi yaliyofanyika katika vifungu vya Unguja na Pemba katika Hesabu hiyo kama inavyoainishwa katika Jadweli linaoonesha ufafanuzi wa tofauti baina ya fedha na

matumizi halisi.

| Vifungu vy matumizi | Makadirio | Kiasi cha fedh kilichotumika Unguja | Kiasi cha fedh kilichotumika Pemba | Jumla ya kias cha fedh kilichotumika Unguja n Pemba | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Petrol | 188,870,000 | - | 21,849,175 | 21,849,175 | |
| Sitting Alowance | 46,950,000 | - | 1,060,000 | 1,060,000 | |
| Food and refreshment | 34,250,000 | 7,625,000 | 2,849,000 | 10,474,000 | Hati za malipo za Unguja zinazoonesha matumizi ya kifungu hichi n 22,275,000 na Pemba 2,847,000. Hivyo kufanya jumla n 25,124,000 kama ilivyoainishwa katika Jadweli la hesabu |
| Domestic Travel | 49,556,407 | 1,813,048 | 15,180,625 | 16,993,673 | |
| Foreign Travel | 58,500,000 | 30,000,000 | - | 30,000,000 | Fedha hiz zimetumika Unguja pekee |
| Government Offices Electricity Bills | 190,000,000 | 85,331,826 | 23,334,896 | 108,666,722 | Hati za malipo za Unguja zinaonesha matumizi ya kifungu hichi n 85,331,826 na Pemba 23,334,896. Hivyo kufanya jumla n 108,666,722 kama ilivyoainishwa katika Jadweli la hesabu |
| Stationary Supply | 49,000,000 | 83,000 | 11,000,000 | 11,083,000 | Hati za malipo za Unguja zinaonesha matumizi ya kifungu hichi n |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 83,000 na Pemba 11,000,000. Hivyo kufanya jumla n 11,083,000 kama ilivyoainishwa katika Jadweli la hesabu |
| Printing Expenses | 809,700,000 | 73,317,197 | - | 73,317,197 | Fedha hiz zimetumika Unguja pekee |
| Cleaning Supply | 55,000,000 | 2,400,000 | 14,581,6000 | 16,981,600 | |
| **Jumla** | **1,292,956,407** | **200,570,071** | **89,855,296** | **290,425,367** | |

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Watendaji wa Wakala kukubali kwamba kulikuwepo makosa ya kuwepo kwa tofauti ya fedha baina ya hesabu ya mwisho wa mwaka na matumizi halisi shilingi 290,425,367. Kamati yetu ilitaka kujua kwamba hilo lilisababishwa na nini na kugundua kwamba ulikuwa ni uzembe wa baadhi ya Watendaji wa Wakala kushindwa kujibu ipasavyo mahitaji ya Mkaguzi. Baada ya Kamati kupitia kwa undani majibu hayo, ilibaini mambo ya msingi yafuatayo:

1. Watendaji wa Wakala walishindwa kutoa ushirikiano unaohitajika kwa Mkaguzi. Jambo hilo lilipelekea Mkaguzi kushindwa kutambua kama kuna hesabu za Pemba hazikuingizwa katika hesabu ya mwisho.
2. Kifungu cha 'Foreign Travel' kilichokuwa na jumla ya shilingi 30,000,000 zilihaulishwa bila ya kufuata taratibu na kutumiwa kuwa ni sehemu ya malipo ya deni inalidaiwa Wakala kwa kununulia mabuku ya ndoa na vyeti vya kuzaliwa kwa kupitia vocha nambari D12PV200000041 ya tarehe 17/8/2020.
3. Kuwepo kwa tofauti ya kiasi cha fedha kilichotumika ambacho kimeainishwa na Mkaguzi na zilizooneshwa na Wakala zikiwemo shilingi 108,666,722 ambazo Mkaguzi amezionesha zinatofautiana na shilingi 85,331,826. Hata hivyo, baada ya Kamati kupitia vocha moja baada ya nyengine iligundua kuwa fedha sahihi ni shilingi 108,666,722.
4. Kutoandaliwa kiusahihi taarifa ya hesabu ya mwisho ya mwaka kama inavyoelekeza katika vigezo vya kitaifa na kimataifa kwani hesabu iliyopo ilibainisha mapungufu ya upotevu wa shilingi 290,425,367.

Aidha, Kamati imepata fursa ya kuzipitia na kuzichunguza vocha hizo na hatimae kuridhika nazo. Miongoni mwa vocha hizo ni vocha ya tarehe 30/12/2020 (cheki nambari 16366) yenye shilingi 956,000, vocha ya tarehe 3/10/2020 ya shilingi 660,000, vocha ya tarehe 10/3/2021 (check 019892 yenye shilingi 1,013,000 na vocha ya tarehe

16/3/2021 (check 019953) yenye shilingi 400,000.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Watendaji wa Wakala wahakikishe wanapatiwa ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali wanapotaka kufanya uhaulishaji wa fedha zao.
2. Wakala uhakikishe unafunga hesabu yake ya mwisho wa mwaka kwa kufuata vigezo vinavyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango na vya kimataifa ili kasoro kubwa zisiweze kujitokeza.
3. Wakala uwe makini unapojibu hoja za Mkaguzi ili waweze kuondokana na kutokaa sawa kwa takwimu katika taarifa zao.

**WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO**

**6.4.1 FUNGU F 01 - OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO**

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilitarajiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,549,340,824,000 kutoka katika vyanzo vyake vya Kodi na visivyokuwa vya Kodi.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 891,648,458,176.28 zimekusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya kodi na visivyokuwa vya kodi ambavyo ni sawa na asilimia 58 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC kwa bahati mbaya haikupokea majibu yanayohusiana na taarifa ya mapato siku mbili kabla ya kikao husika kama inavyoelekezwa Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020). Hata hivyo, Kamati kupitia uchunguzi wake, imebaini kwamba Wizara haikufikia malengo yake ya makusanyo kutokana na kuwepo kwa maradhi ya 'Covid 19' ambayo iliendelea kusababisha makusanyo kupungua.

**Taarifa ya Matumizi**

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 129,185,392,882 kwa matumizi ya kawaida, mishahara jumla ya shilingi

8,543,512,000, matumizi mengineyo ni shilingi 15,792,788,000, shilingi 41,920,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali, shilingi 26,250,852,189 kwa kazi za maendeleo kupitia Washirika wa Maendeleo, na shilingi 36,678,240,693 ikiwa ni Ruzuku.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 48,578,035,298 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 38 ya makadirio, ambapo shilingi 8,447,134,942 zimeingizwa na kutumika kwa Mishahara sawa na asilimia 99, matumizi mengineyo 6,132,515,064 sawa na asilimia 39, kazi za maendeleo mchango wa Serikali 8,020,847,568 sawa na asilimia 19 kwa kazi za maendeleo Washirika wa Maendeleo shilingi 3,937,000 sawa na asilimia 0.015 ya makadirio na shilingi 25,973,600,724 ikiwa ni ruzuku sawa na asilimia 71 ya makadirio.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC kwa bahati mbaya haikupokea majibu yanayohusiana na taarifa ya mapato. Hata hivyo, kupitia uchunguzi wake, Kamati yetu imebaini kwamba Wizara haikufikia malengo yake ya makusanyo kutokana na kuwepo kwa maradhi ya 'Covid 19' ambayo iliendelea kusababisha makusanyo kupungua.

### Hoja nambari 6.4.1.1: Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 42,578,400

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imefanya matumizi kwa ajili ya ununzi wa vifaa na huduma mbali mbali za kiofi si zenye thamani ya shilingi 42,578,400. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuambatanishwa kwa vilelezo husika katika hati ya malipo ili kuweza kujiridhisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanishwa kwa vielelezo husika katika hati za malipo kunapelekea kushindwa kujiridhisha kwa matumizi ya fedha yaliyofanyika na kuashiria ukiukwaji wa taratibu, miongozo, kanuni na sheria za usimamizi wa fedha jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

### Jadweli Nambari 96: Malipo yasiyokuwa na vielelezo

| Hati Namba | Kiasi kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| R6/9ya 31/8/2020 | 2,750,000 | Common wealth Institute | Malipo kwa ajili ya ada ya mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| R9/8ya 17/8/2020 | 29,628,400 | Wizara ya Fedha | Malipo kwa ajili ya matumizi mbali mbali. |
| R1/12 ya 1/1/2020 | 10,200,000 | NBAA | Malipo kwa ajili ya ada ya ushiriki wa mkutano Mkuu wa wanachama wa NBAA. |
| **Jumla** | **42,578,400** | | |

**Majibu ya Wizara**

Wakati wa Ukaguzi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameshindwa kwa matumizi ya fedha hizo kwa kutokuambatanishwa vielelezo vya malipo katika hati za malipo zilizo ainishwa katika Jadweli Nambari 96 la taarifa ya Mdhibiti.

Ni kweli kwamba wakati wa ukaguzi baadhi ya vielelezo vya malipo havikuambatanishwa katika voucher husika na kupelekea dosari ndogo kwa Mkaguzi, kwa sasa vilelezo vyote vya malipo vimeambatanishwa na vipo tayari kwa ukaguzi.

Ushauri uliotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tunauchukua na kuufanyia kazi kwa lengo la kuboresha na kuimarisha udhibiti wa Rasilimali za Serikali. Aidha Wizara inachukua juhudi za makusudi kuondowa kasoro hizi ili zisijirudie tena.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Wizara kukiri kwamba kweli kulijitokeza kasoro hizo lakini Kamati ilitaka kujua ni vielelezo gani vilivyokosekana na kwanini hivi sasa vielelezo viwepo na wakati Mdhibiti hakupatiwa vielelezo hivyo na kuelezwa kwamba vilikuwa vielelezo vya safari na ripoti za mafunzo ya wafanyakazi wanaporudi masomoni ambavyo vilikuwa vimehifadhiwa kimakosa sehemu nyengine. Kamati ya PAC haikuridhika na majibu hayo na imevikataa vielelezo hivyo na kuungana na Mkaguzi kwamba fedha ya Serikali ya shilingi 42,578,400 imepotea.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati inaishauri Wizara kusimamia vyema Watendaji wake ili wanaporudi masomoni waweze kuandaa na kuwasilisha vielelezo vya kumaliza kwa mafunzo husika.
2. Wizara ya Fedha na Mipango ikiwa ndio msimamizi mkuu wa Maafisa Masuul wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ikae nao na kuwaelekeza waache kufanyakazi bila ya kuhifadhi vizuri vielelezo na wawe wanatoa mashirikiano kwa Mkaguzi hususan wakati anapofika katika maeneo yao kutekeleza majukumu yake.

### 6.4.2 FUNGU F 02 - HESABU ZA HUDUMA ZA MFUKO MKUU WA SERIKALI

Ukaguzi wa hesabu za Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika mwaka wa Fedha 2020/2021, Hesabu za Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali iliidhinishwa kutumia shilingi 239,230,300,000 kwa ajili ya utoaji wa huduma mbali mbali za Mfuko Mkuu zikiwemo ulipaji wa Viinua Mgongo, Pensheni na malipo ya huduma za hati fungani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 197,071,744,662.50 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya hesabu za huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 82.3 ya makadirio. Aidha, hesabu za Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali ulikuwa na salio la shilingi 1,407,945,086.84 mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2020/2021 katika hesabu yake ya Amana (Public Debt Deposit Account) ambazo zilitumika kwa malipo ya Viinua Mgongo na matumizi mengine maalum ya Serikali. Hadi Kufikia tarehe 30 Juni, 2021 hesabu hii ya Amana ilikuwa na bakaa ya shilingi 835,872,461.31.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC kwa bahati mbaya haikupokea majibu yanayohusiana na taarifa ya mapato siku mbili kabla ya kikao husika kama inavyoelekezwa Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020). Hata hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi kuhusiana na Taarifa ya Matumizi.

**Hoja nambari 6.4.2.1: Kuwepo kwa malipo yaliyofanyika kinyume na Mkataba**

Ukaguzi umepitia Mkataba uliofungwa baina ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Al-Noor Motors FZCO, ambapo mkataba huo uliofungwa tarehe 2 Septemba, 2020 wenye thamani ya USD. 1,424,600. Mkataba huo uliitaka Wizara ya Fedha na Mipango kumlipa Mzabuni Al-Noor Motors FZCO asilimia 50 ya malipo yote ya Mkataba ndani ya siku kumi na nne (14) za kazi baada ya kusainiwa kwa Mkataba pamoja na kuwasilishwa kwa Ankara ya Malipo (Invoice) na asilimia 50 zilizobaki zilipwe baada ya kupokelewa kwa hati ya upokezi wa Mizigo/bidhaa (Bills of Lading) ya gari zote (19) zilizoagiziwa kwa kipindi cha miezi miwili (wiki 8).

Ukaguzi umebaini kufanyika kwa malipo ya awamu ya pili kinyume na Mkataba unavyosema kutokana na kuwepo kwa mapitio ya Mkataba (Addendum No. 2) ambayo yamesainiwa tarehe 02/11/2020 yanayofanya makubaliano baina ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar na Al-Noor Motors FZCO kuongeza muda wa

kuwasilishwa kwa gari 11 ambazo hazikuweza kuwasili katika kipindi cha kwanza cha Mkataba (Miezi miwili) baada ya kupokelewa kwa gari nane (8) ambazo ziliwasili katika kipindi cha Mkataba).

Kutokuwasilishwa kwa gari 11 ambazo zilipaswa ziwasilishwe kwa mujibu wa mkataba wa awali ndani ya miezi miwili na badala yake kuamulika kufanya mkataba mdogo wa makubaliano mapya ya uwasilishwaji wa gari hizo ambapo Kampuni ya Al-Noor Motors FZCO ililipwa malipo yote kabla ya mapokezi ya gari hizo kumepelekea kujitokeza kwa viashiria vya udanganyifu na ukiukwaji wa makubaliano jambo ambalo linaweza kucheleweshwa kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa kwa wakati. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 102: Fedha zilizolipwa kwa ajili ya ununuzi wa magari**

| Nam | Tarehe | Kiasi cha fedha kilicholipwa (USD) | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|
| 1. | 15/09/2020 | 712,300 | AL-NOOR MOTORS FZCO |
| 2. | 24/10/2020 | 472,700 | AL-NOOR MOTORS FZCO |
| **Jumla** | | **1,185,000** | |

**Majibu ya Wizara**

Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa kutofuatwa kwa taratibu pamoja na Makubaliano ya Mkataba wa Ununuzi wa Magari kutoka Mzabuni Al Noors Motors, Hata hivyo hatua zote za utekelezaji wa Mkataba huu umekamilika na gari zote zimeshapokelewa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na tayari wameshapatiwa wahusika kwa ajili ya matumizi.

Aidha, Uongozi wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango inaahidi kufuata utaratibu wa makubaliano yote yaliopo katika kuhakikisha fedha za Serikali hazipotei au kuonesha viashiria vya upotevu wa fedha kwa mujibu wa Sheria za Usimamizi wa Fedha Umma Nam. 12 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nam. 11 ya mwaka 2021. Pamoja na Maelezo hayo naambatanisha nyaraka zifuatazo:-

a) Hati za malipo pamoja na barua ya maombi na Ankara No. 100438 ya tarehe 7/09/2020 ya Al Noor Motors.
b) Mkataba wa makubaliano pamoja na mabadiliko ya mkataba wa awali (Adendum No. 2).
c) Bill of Landing.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Wizara kukubaliana na hoja ya Mkaguzi, Kamati ya PAC imebaini kwamba jambo hilo limetokana na Wizara kushindwa kusimamia ipasavyo

utekelezaji wa Mkataba na kuonesha viashiria vya upotevu wa fedha za umma kwa mujibu wa Sheria za Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya mwaka 2016. Hata hivyo, gari zimenunuliwa kweli na zinaendelea kufanyakazi za Serikali.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe inaandaa na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Mikataba yote hususan inayotumia fedha nyingi za Serikali.

**Hoja nambari 6.4.2.2: Kutokuwasilishwa kwa kidhibiti cha Mkataba (Performance Security)**

Kifungu 18.1 cha SSC ya Mkataba baina ya Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar na Al-Noor Motors FZCO kinamtaka Mzabuni kuwasilisha Kidhibiti cha Mkataba (Performance Security) ndani ya siku 28 baada ya kupokea kwa barua ya kumjuulisha kushinda kwa Zabuni (Clause 18.1 If require as specified in the SCC, the Supplier shall, within twenty-eight (28) days of the notification of contract award, provide a performance security for the performance of the contract in the amount specified in the SCC).

Ukaguzi umebaini kwamba Mzabuni (Al-Noor Motors FZCO) hakuwasilisha kidhibiti cha Mkataba (Performance Security) kama ilivyoelekezwa katika Mkataba. Kutokuwasilishwa kwa kidhibiti cha mkataba na kuendelea kufanya biashara na mzabuni kwa kumlipa fedha zote za malipo aliyodai kunaweza kupelekea hasara kwa Serikali ya kutokupata marejesho ya fedha zake pale ambapo mzabuni atashidwa kuwasilisha vifaa alivyotakiwa kuwasilisha kwa mujibu wa mkataba. Aidha mzabuni atakapovunja uaminifu na kuamua kukimbia Serikali itapoteza fedha kubwa waliomlipa bila ya kuwa na kidhibiti cha kurejesha fedha hizo jambo ambalo ni kinyume na sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mfuko Mkuu wa Serikali kuhakikisha unatekeleza vipengele vyote vya makubaliano ya mkataba ili kuepusha kujitokeza upotevu wa fedha za Serikali kunako sababishwa na kutokufuatwa na makubaliano.

**Majibu ya Wizara**

Ushauri umepokelewa, uongozi wa Mfuko Mkuu wa Serikali utahakikisha unatekeleza vipengele vyote vya makubaliano ya mkataba ili kuepusha kujitokeza upotevu wa fedha za Serikali kunako sababishwa na kutokufuatwa na makubaliano, kwa sasa Ofisi yetu inahikisha malipo yote yanafata utaratibu wa malipo kwa kuzingatia sharia ya Manunuzi na Uondoshaji wa mali za Umma nam 11 mwaka 2016 pamoja na kanuni zake za mwaka 2021. Aidha, hadi kukamilika kwa utekelezaji wa mkataba huu hakukuwa na dosari yoyote ambayo imesababishwa na utekelezaji wa mkataba.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wizara wamekiri kuwepo kwa chanagamoto hiyo, hata hivyo, Kamati yetu imebaini kwamba jambo hilo limetokana na kukosa umakini katika usimamizi wa utekelezaji wa Mikataba.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaitaka Wizara kuisimamia Mkataba ipasavyo wanayoingia na Wafanyabiashara mara tu baada ya kufungwa.

**Hoja nambari 6.4.2.3: Kukosekana kwa Maombi ya Malipo (Payment requisition) kutoka kwa Mzabuni (Al-Noor Motors FCOZ) za madai ya malipo yake ya manunuzi ya magari.**

Mkataba uliofungwa baina ya Wizara ya Fedha na Mipango na Al-Noor Motors FCOZ kupitia kifungu cha 16.2 kinaeleza kwamba Mzabuni atawasilisha maombi yake ya malipo kwa kuambatanisha na Ankara za malipo (16.2 Terms of payment which states that, The Supplier request for payment shall be made to the purchasing in writing, accompanied by invoices). Dosari iliobainika katika ukaguzi ni kutokupatikana kwa vielelezo vinavyothibitisha uwepo wa maombi hayo kwa mujibu wa kifungu 16.2 cha makubaliano ya mkataba.

**Majibu ya Wizara**

Kweli Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa barua ya maombi katika nyaraka za malipo ya ununuzi wa magari kila wakati ambapo Mzabuni anapohitaji kufanyiwa malipo husika, hata hivyo kwa mujibu wa mkataba uliopo baina ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Mzabuni Al-Noor Motors FCOZ katika kifungu cha 16.1 cha “Special Condition” kilimtaka Mzabuni kuwasilishwa Ankara (Invoice) pamoja na ‘bill of landing’ kama nyaraka rasmi ya kuombea malipo. Pamoja na maelezo haya tunaambatanisha na kivuli cha Mkataba wa makubaliano haya.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Wizara kukiri uwepo wa hoja ya kutokuwepo kwa barua ya maombi katika nyaraka za malipo ya ununuzi wa magari. Hata hiyo, Kamati yetu imegundua kwamba hali hiyo ilisababishwa na kuwepo kwa agizo (maelekezo) kutoka Baraza la Mapinduzi lililoitaka Wizara kufanya ununuzi wa gari hizo. Kamati ya PAC inaendelea kuishauri Wizara kwamba kutolewa agizo sio uhalali wa kutekeleza agizo husika pasi na kufuatwa kwa Sheria na Kanuni zilizopo.

**Hoja nambari 6.4.2.4: Kukosekana kwa Makubaliano ya mwisho yanayohusu malipo dhidi ya kesi iliyotokea baina ya Serikali na Kampuni ya Al Ghubra Marine Services LTD.**

Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imefanya malipo dhidi ya Kesi iliyotokea baina ya Kampuni ya Al-Ghubra Marine Services na Serikali ambayo ilisimamiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kesi hiyo ilitokea baada ya Wizara ya Biashara na Viwanda kutoa

barua ya kuvunja Mkataba tarehe 8/4/2016. Baada ya juhudi ya kutafuta ufumbuzi wa shauri hilo nje ya Mahkama kushindikana, Kampuni ya Al-Ghubra ilifungua kesi ya madai katika Mahkama Kuu ya Zanzibar mwezi wa Julai 2016 (Kesi ya madai namba 36 ya 2016).

Ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa makubaliano ya maandishi yatakayoonyesha jinsi ya kufanya malipo hayo (mode of payment) pamoja na muda wa kuanza na kumaliza kulipwa malipo hayo. Aidha ukaguzi haukupatiwa kumbukumbu za maamuzi ya kikao cha mwisho kinachohusiana na majadiliano ya utekelezaji ya maamuzi ya Mahkama ili kuweza kujuwa kama kuna makubaliano mapya ya malipo yatakayofanyika au ni makubaliano yale yale ya awali yaliyotokana na kumbukumbu za kikao cha pili cha majadiliano kati ya pande hizo mbili kilichofanyika tarehe 20/02/2020 kuhusu kesi hiyo, makubaliano ya malipo yalikuwa kama ifuatavyo:-

- Gharama za kodi ya jengo ni shilingi 1,548,000,000.
- Gharama za Mahkama na uwakili ni USD 41,000.

Hadi ukaguzi unakamilika haukuweza kupatiwa makubaliano ya fedha yanayotakiwa kulipwa, muda wa kuanza malipo pamoja na kumalizika kwa malipo hayo dhidi ya kesi iliyotokea baina ya Serikali na kampuni ya Al Ghubra Marine Service Ltd. Aidha kwa mujibu wa majibu tuliopatiwa kutoka Ofi si ya Rais fedha na Mipango yanayosema" Malipo ya Al Ghubra Marine Services Ltd imelipwa kwa mujibu wa maelekezo tulioyapata kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha." Kutokana na majibu hayo ukaguzi umepata shaka ya kwamba malipo hayo yamefanyika kinyume na maamuzi ya Mahkama jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za Umma kwa kufanya malipo makubwa zaidi kuliko maamuzi ya Mahkama au vyenginevyo.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Hesabu za Huduma za Mfuko Mkuu wa Hazina kuhakikisha malipo yoyote yanayofanyika yanakamilika kwa vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa kufanyika malipo hayo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 103: Malipo yaliyofanyika kwa ajili ya kulipa madeni**

| Jina la Hesabu | Hati namba | Kiasi cha fedha (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (DUMMY) | 3 of Feb | 71,000,000 | Alghurba Marine Services LTD. | Malipo ya kumalizia deni la nyuma la Tzs. 21,000,000 zilizobakia na Tzs. 50,000,000 ni<br><br>malipo ya mwanzo ya deni la awamu ya pili la Tzs.<br><br>500,000,000 linalolipwa kwa amri ya Mahkama. Deni awamu ya pili 500,000,000. Kinacholipwa<br><br>sasa 50,000,000, bakaa<br><br>450,000,000. |
| | PD 13/4 | 100,000,000 | Al Ghurba Marine Services Ltd | Malipo ya awamu ya 2 ya hukumu na amri ya mahkama katika kesi ya Al Ghurba. Jumla ya<br><br>madai ni TZ 500,000,000. Kilicholipwa awali ni TZ 50,000,000 na awamu hii TZ 100,000,000. Kilichobaki TZ 350,000,000. Barua no. REF.LW 06/VOL.I/34 ya<br><br>10/12/20 |
| **Jumla** | | **171,000,000** | | |

**Majibu ya Wizara**

Ushauri umepokelewa,Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kubaini kutokuwepo kwa makubaliano ya maandishi yaliooneshа jinsi ya kufanya malipo hayo (mode of payment) pamoja na muda wa kuanza na kumaliza kulipwa malipo hayo baina ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Mzabuni Al Ghurba

Marine Services LTD.

Hata hivyo kwa kuwa malipo haya yalifanyika baada ya maamuzi ya Mahkama Kuu na kuitaka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kumlipa Mzabuni kulingana na maamuzi ya kesi Nam. 36 ya 2016 yaliyotolewa tarehe 30 January 2020, ili kuweza kukamilisha utekelezaji wa agizo la Mahkama. Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ilitumia maamuzi ya Mahkama kufanya malipo kwa kutumia nyaraka za Mahkama. Pamoja na majibu haya tuaambatanisha na vivuli vya nyaraka mbali mbali zilizosaidia kufanyika kwa malipo haya ikiwemo hati ya malipo.

Kwa kuwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ilikuwa ni sehemu ya Taasisi zilizo athirika na maradhi ya UVIKO 19, ambapo ikapelekea Ofisi kushindwa kutekeleza maamuzi ya mahkama kwa awamu moja na kupelekea kufanya malipo kwa awamu mbali mbali, hata hivyo malipo ya mwisho ya madai yalilipwa mnapo tarehe 05/04/2022 ya hati namba 17/04/2022 kwenda kwa mzabuni.

**Uchunguzi na Mapendekezo Kamati ya PAC**

Kwa vile Watendaji wa Idara ya Mhasibu wa Mkuu wa Serikali na kusisitiza kwamba Taasisi au Wizara iwe makini inapotekeleza amri za Mhakama.

**Hoja nambari 6.4.2.5: Kufanyika kwa malipo ya ziada ya mshahara ya shilingi 15,095,379**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika uwepo wa ziada ya malipo ya shilingi 15,095,379 yanayotokana na malipo ya mshahara ya Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege Zanzibar yaliyolipwa na Mfuko Mkuu wa Serikali. Ukaguzi ulifanya ulinganisho wa malipo ya mishahara baina ya mwezi wa Juni 2020 wenye thamani ya shilingi 479,149,648 pamoja na mwezi wa Julai 2020 wenye thamani ya shilingi 494,245,027 kupitia taarifa za kumbukumbu za malipo (cash book report) na kubaini uwepo wa tofauti ya shilingi 15,095,379 kwa ajili ya mshahara kwa mwezi wa Julai 2020.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokupatikana sababu zilizopelekea kujitokeza kwa malipo ya ziada hayo, kutokana na kukosekana kwa mtumishi aliyefanyiwa mabadiliko ya mshahara wake kwa kupata nyongeza ya mshahara au badiliko la posho jambo ambalo ukaguzi ulifanya mahojiano na watendaji wa Mfuko Mkuu kuhusiana na ziada ya fedha iliobainika ambapo wahusika walishindwa kutoa sababu ya utofauti wa uwepo wa ziada hiyo pamoja na kutokupatiwa kwa ukaguzinyaraka ya makubaliano iliothibitishwa na uongozi kati ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege pamoja na Mfuko Mkuu wa Serikali inayohusu maombi ya ulipwaji wa fedha ya ziada kwa mshahara wa mwezi wa Julai 2020.

Kutokana na uhalisia huo ukaguzi unatilia shaka juu ya majibu ya Uongozi wa Mfuko Mkuu yanayoeleza kwamba Mfuko unafanya malipo kutokana na maelekezo yanayoandikwa katika barua ya maombi kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na Mhasibu Mkuu wa Serikali jambo ambalo inabainika kufanyika kwa malipo

kinyume na taratibu na kushindwa kujiridhisha kwa fedha iliyoombwa. Kutokupata vielezo vya uthibitisho wa uhalali wa ziada ya malipo hayo kunaweza kupelekea uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

**Majibu ya Wizara**

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa tofauti ya malipo yaliyojitokeza yatokanayo na maombi ya fedha kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege-Zanzibar kuja Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kulipia mishahara ya mwezi wa Juni na Julai 2020. Baada ya kufuatilia uhalali wa maombi yaliyotoka katika mamlaka ya Viwanja vya ndge Zanzibar Tofauti iliyopo ilisababishwa na ongezekeo la mishahara ambalo limesabishwa na toleo la marekebisho ya mshahara kwa Mashirika ya Serikali la mwaka 2019 ambalo limeanza kutekelezwa Julai 2020. Hadi kufikia June 2020 Mamlaka walikuwa wakitumia muongozo wa malipo wa utumishi uliopita.

Pamoja na maelezo haya naambatanisha na nyaraka zifuatazo:-

a) Kiambatanisho cha Marekebisho ya Mshahara-2019;
b) Hati za malipo na barua za maombi za fedha hizo ya mwezi wa Juni 2020-Barua ya Tarehe 18 Juni 2020 kumbukumbu namba ZAA/WFM/01/01/VOL.1 na stakabadhi namba 32121; pamoja na
c) Hati ya malipo na barua za maombi za fedha hizo ya mwezi wa Julai 2020 - Barua ya Tarehe 18 Juni 2020 kumbukumbu namba ZAA/WFM/01/01/VOL.1 pamoja na stakabadhi namba 32121

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Baada ya kupitia kwa undani nyaraka zilizowasilishwa, Kamati ya PAC haikuridhika na majibu hayo kwani iliiuliza Wizara kuwa kwanini Mkaguzi hakupatiwa vielelezo hivyo, na kubaini kwamba Watendaji wa Wizara na Mkaguzi hawakuwa na mashirikino ya karibu na kusababisha kutokupatikana kwa vielelezo hivyo.

**Hoja nambari 6.4.2.6: Malipo ya fedha yaliyolipwa kwa njia ya Fedha taslim shilingi 500,000,000 na USD 43,000**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi ulipitia hati za malipo pamoja na vielelezo mbalimbali vilivyofanyiwa malipo na kubaini jumla ya shilingi 500,000,000 na Dola za Kimarekani 43,000 zilitumika kwa ajili ya huduma mbali mbali kwa njia ya fedha taslim, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanyika kwa malipo kwa njia ya fedha taslim na kukosekana kwa taarifa za kumbukumbu zilizotiwa saini ya mapokezi ya fedha hizo kama ni kielelezo kinachothibitisha uhalali wa mapokezi ya fedha hizo.

Kufanya malipo kwa njia ya fedha taslim kunaweza kukapelekea kujitokeza kwa matumizi yasio ya lazima ambayo yataambatana na upotevu wa fedha za Umma na kupelekea Serikali kupata hasara jambo ambalo litakwamisha utekelezaji wa malengo

ya taasisi waliyojipangia.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa hesabu za huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali kuhakikisha unatekeleza maagizo ya Serikali ya kutokutumia malipo kwa fedha taslim ili kuepuka vishawishi vinavopelekea upotevu wa fedha za umma. Mchanganuo wa malipo ya fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 104: Malipo yaliyofanyika kwa fedha taslim**

| Hati namba | Kiasi cha Fedha (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 8/10/20 | Tzs 500,000,000 | Ali S. Ali/ Jabir Kipenda Jabir | Malipo kwa ajili ya matumizi mbalimbali |
| 9/10/20 | USD 43,000 | Jabir Kipenda Jabir | Malipo kwa ajili ya matumizi mbalimbaliDUMMY. |

## Majibu ya Wizara

Ushauri umepokelewa, Uongozi wa hesabu za huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali kuhakikisha unatekeleza maagizo ya Serikali ya kutokutumia malipo kwa fedha taslim ili kuepuka vishawishi vinavopelekea upotevu wa fedha za umma. Hata hivyo Mfuko Mkuu wa Serikali ulifanya malipo kupitia hati za malipo nambari 8/10/20 na 9/10/20 ambapo fedha hizo zilihitajika fedha taslim kwa ajili ya mtumizi maalum ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zilivyoagiza.

Pamoja na maelezo haya naambatanisha na nyaraka zifuatazo:-

i. Barua ya maombi Tsh 500,000,000 kumb. namba IKL/TS/SH-54/VOL.11/ ya tarehe 15/10/2020 pamoja na Hati ya malipo.
ii. Barua ya maombi USD 43,000 kumb namba IKL/TS/SH-54/VOL.11/ ya tarehe 21/9/2020 pamoja na Hati ya malipo.

## Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ilipokuwa ikifuatilia hoja hii, ilibaini kwamba utekelezaji uliofanyika ulitokana na kuwepo kwa agizo la Baraza la Mapinduzi. Aidha, Kamati yetu ilibaini kwamba maagizo mengi yakitolewa, hutolewa kwa nia njema isipokuwa Watendaji hushindwa kuyachukua na kuyatekeleza kinyume na Sheria za nchi yetu.

## OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO - PEMBA

Hoja nambari 6.4.1.2: Kukosekana kwa kumbukumbu za mapato ya ukodishwaji wa majengo ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango - Pemba inamiliki majengo mbali mbali katika maeneo ya Pemba kwa ajili ya ukodishwaji na kupelekea upatikanaji wa mapato ya Serikali.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokujulikana kwa mapato halisi yaliyopatikana yanayotokana na ukodishwaji wa majengo kutokana na kukosekana kwa kumbu kumbu za mapato za ukodishwaji wa majengo ya ofisi jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kukamilisha kazi yao kutokana na kukosekana kwa nakala za mikataba ya Ukodishwaji, Hati za kulipia kutoka benki (Pay in slip) pamoja na taarifa za benki (bank statement) ili kuweza kujiridhisha kima halisi cha fedha kwa mujibu wa mkataba na fedha iliyokusanywa kupitia ukodishwaji huo.

Pamoja na uwepo wa dosari hiyo ukaguzi umebaini kwa baadhi ya maeneo fedha zilizolipwa haziendani na thamani halisi ya ukodishwaji wa jengo kutokana na bei ya sokoni ilivyo jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa mambo yafuatayo:-

a) **Jengo lililopo Kilima Tende (Miembeni Chake Chake)**

Ukaguzi umebaini jengo hili lina milango minne (4) pamoja na sehemu ya kuekea bidhaa (store) ambalo limekodishwa kwa thamani ya shilingi laki tatu (Tshs. 300,000) kwa mwezi kwa Bwana Abdalla Hemed Abdalla ambapo bei hii hailingani na bei ya soko kwa kila mlango.

b) **Jengo lililopo MTC mkabala na Hotel ya Chake Chake**

Katika jengo hili imebainika uwepo wa milango tofauti ambapo mlango wa kwanza umekodishwa kwa bwana Salum Alawy ambapo thamani ya bei aliyokodishiwa na Wizara ya Fedha haikuweza kujulikana, hata hivyo mkodishwaji huyo nae amemkodisha Bwana Said Sulum Ahmed kwa thamani ya shilingi 1,500,000 kwa mwaka kinyume na makubaliano ya mkataba wa awali.

Mlango wa pili kakodishwa Bwana Seif Mohd Khamis kwa thamani ya shilingi 10,800,000 kwa kipindi cha miaka mitatu (3).

Kukosekana kwa thamani halisi ya fedha kulingana na eneo pamoja na ukubwa wa duka kutokulingana na bei halisi ya soko kunapelekea kukosesha Serikali mapato.

**Majibu ya Wizara**

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango inasimamia mali za Serikali ambapo baadhi ya mali hizo hukodishwa kwa watu binafsi na Taasisi za Serikali kwa mikataba maalumu. Katika kurahisisha utendaji kazi na kutokana na ukubwa wa mikataba ya ukodishwaji baadhi ya mali za Serikali zilizokodishwa zilizopo Pemba zinasimamiwa na Ofisi Kuu Pemba ambapo kumbukumbu za mapato yatokanayo na ukodishaji wa mali hizo zinapatikana ofisi Kuu Pemba na baadhi ya mali hizo zinakodishwa na ofisi kwa upande wa Unguja ambapo mapato na kumbukumbu nyengine zitahifadhiwa, hivyo mali ambazo wakaguzi hawakuweza kuona kumbukumbu za mapato yake Pemba ni kwamba kumbukumbu za mikataba na malipo yatokanayo na mikataba hiyo ipo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar. Ofisi imechukua hatua za ziada kuhakikisha kwamba mikataba yote inayohusiana na mali zinazokodishwa zilizopo Pemba inashughulikiwa Pemba.

Jengo la Kilimatinde ni jengo ambalo hapo awali lilikua katika hali mbovu sana na kutoweza kutumika na kutoa tija kwa Serikali. Katika kutafuta njia ya kulijenga jengo hilo Wizara ilitafuta mfanyabiashara ili aweze kulijenga kwa gharama yake katika mfumo wa Jenga, Miliki, Rejesha (B.O.T). Aidha Wizara katika kumvutia mfanyabiashara huyo ilipanga mkakati wa kupunguza bei ili iwe ni chachu ya kuweza kujengewa jengo hilo na mara tu mkataba wa awali utakapomalizika jengo hilo litakodihswa kwa mnada wa hadhara ili kuweza

kupata bei halisi ya soko ya ukodishwaji katika eneo hilo;

Kuhusu jengo la Shirika la Magari (MTC), sehemu moja ya jengo hili limekodishwa kwa Bw. Salum Alawi na sehemu nyengine limekodishwa kwa Bw. Said Mohd Said ambapo jengo haliko katika hali nzuri hivyo kupelekea kukosa thamani halisi ya soko wakati wa ukodishaji licha ya hivyo ofisi imeshaanza kufanya utaratibu wa awali utakaowezesha jengo hilo kuiwezesha Serikali kupata mapato Zaidi.

**Uchunguzi wa kamati ya PAC**

Baada ya kuchunguza kwa undani hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa jengo liliopo Kilima Tende lilikodishwa kwa shilingi 300,000 kwa mwezi wakati ambao jengo hilo lilikuwa halijafanyiwa matengenezo. Kutokana na hali ya jengo hilo lilivyokuwa, Kamati iliridhika na bei pamoja na majibu ya Wizara na haikuwa na hoja zaidi.

Kwa upande wa jengo liliopo MTC Mkabala na hoteli ya Chakechake, Kamati imegundua kwamba bei ya kodi ya jengo hilo awali ilikuwa inaridhisha. Hata hivyo, Kamati ye PAC haikufurahishwa na utendaji wa Wizara wa kushindwa kusimamia ipasavyo utendaji wa Watumishi wake. Hili limetokana na Mtu aliyekodishwa kuamua kwenda kinyume na Mkataba wake uliomtaka Mkodishwaji asimkodishe mtu mwengine na kuamua kufanya maamuzi ya makusudi ya kumtafuta na kumkodisha mtu mwengine kwa bei ya juu zaidi bila ya kupata idhini ya Wizara au Mkodishaji.

Kadhalika, Kamati yetu mebaini Ofisi ya Rais, fedha na Mipango Pemba haikuwa na ufuatiliaji mzuri wa kodi za jengo hilo kwani hivi sasa inafika mwaka mmoja yangu Mkataba kumalizia lakini bado Mkodishwaji anadaiwa shilingi milioni mbili baada ya kulipa milioni moja. Kukosekana kulipwa kodi husika kwa wakati, kupelekea kurundikana kwa madeni ya Serikali yasiyolipwa na kushindwa kumudu gharama za uendeshaji wa majengo ya Serikali.

Kamati pia imebaini kuwa kwasasa Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imeshafanya mapitio ya jengo hilo na kusubiri uamuzi wa Serikali kuelekeza kitu cha kufanya ili majengo hayo yaweze kutumika na kuleta tija kwa Serikali na wananchi wake kiujumla.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Pemba ihakikishe inaandaa Mpango madhubuti wa kuyasimamia ipasavyo majengo yake pamoja na wapangaji wanaowakodisha majengo hayo.
2. Watendaji wa Wizara wahakikishe wanalifuatilia deni analodaiwa bwana Said Sulum Ahmed (shilingi milioni mbili) kwa kumpatia miezi mitatu kukamilisha deni hilo baada ya kuwasilishwa hotuba hii na iwapo atashindwa kulipa kwa wakati, Serikali imchukulie hatua za kisheria.

**Hoja nambari 6.4.1.3: Ukodishwaji wa majengo ya Serikali usioendana na thamani ya halisi ya soko**

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba inamiliki majengo ya biashara na kuingia mikataba ya ukodishaji ili kuweza kuingizia Serikali mapato yatokanayo na kodi ya majengo hayo. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa ukodishaji wa majengo ya serikali kwa thamani ndogo ukilinganisha na bei ya soko kwa maeneo husika.

Kufanya hivyo ni kuikosesha Serikali mapato stahiki. Aidha ukaguzi umeshindwa kupatiwa bei elekezi iliyopangwa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ajili ya ukodishaji wa majengo ya Serikali kinyume na miongozo ya fedha.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa thamani halisi ya ukodishwaji wa majengo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 97: Majengo ya Serikali yaliyokodishwa kwa thamani ndogo**

| Tarehe ya mkataba | Aina ya Jengo | Pahala | Muda wa mkataba | Aliyekodishwa | Fedha Zilizolipwa kwa mwezi (Tshs) | Fedha Zilizolipwa kwa mwaka (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1/1/2020 - 31/12/2021 | Bekari | Chake Chake | Mwaka 1 | Mohamed Omar Khamis | 30,000 | 360,000 |
| 1/7/2020 - 30/6/2021 | Mlango wa duka | | | Khatib Omar Khatib | 15,000 | 180,000 |

**Majibu ya Wizara**

Ukodishwaji wa majengo unategemea na hali ya jengo ilivyo, hali halisi ya majengo yaliyotajwa sio nzuri hivyo ukodishwaji kwa mujibu wa thamani ya soko (Market Price) isingekua rahisi, licha ya hivyo Ofisi imeshaanza utaratibu wa kutafuta njia bora ya kuyaboresha majengo hayo na mara tu yatakapokamilika uboreshaji wake mikataba ya ukodishwaji yataendana na bei na thamani ya soko.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Baada ya Kamati ya PAC kupata majibu ya Wizara, Kamati yetu imeridhika na majibu hayo na haikuwa na hoja zaidi hasa ukizingatia kwa sasa tayari majengo hayo yameshafanyiwa matengenezo na matayarisho ya kurekebisha mikataba yameanza ili ilingane na thamani halisi ya majengo hayo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuyatengeneza majengo yake yaliyokuwa yamechakaa kwa muda mrefu ili yaweze kuendana na wakati tulionao.

**Hoja nambari 6.4.1.4: Gharama kubwa ya malipo ya huduma ya usafi shilingi 6,000,000 kwa mwezi**

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba iliingia mkataba na AKB Cleaning Enterprises ya Chake Chake mnamo tarehe 1/1/2021 kwa ajili ya kupatiwa huduma ya usafi wa ndani kwa muda wa miezi sita (6) ambapo malipo ya huduma hiyo kwa mwezi ni shilingi milioni sita (6,000,000) ambapo ni sawa na shilingi 72,000,000 kwa mwaka.

Ukaguzi umebaini kwamba gharama ya malipo ya huduma ya usafi zinazolipwa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango haziendani na uhalisia wa kazi zinazofanywa katika eneo husika ambapo gharama hiyo inajumuisha floo ya chini, ghorofa ya kwanza na ya tatu ya jengo hilo, na kuonekana gharama yake ni mara mbili zaidi ukilinganisha na eneo la jengo hilohilo la ghorofa ya pili ambalo linalipiwa huduma ya usafi kwa gharama za shilingi milioni moja kwa mwezi (1,000,000) ambapo ni sawa na shilingi 12,000,000 kwa mwaka.

Hadi ukaguzi unakamilika imebainika jumla ya shilingi 51,000,000 zimeshalipwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kupelekea uwepo wa bakaa ya shilingi 21,000,000 kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba baina ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Kampuni hiyo.

Ukaguzi unashauri ni vyema kufanyike upembuzi yakinifu wa kuhakikisha kwamba fedha zinazolipwa zinaendana na uhalisia wa upatikanaji wa huduma ili kuepusha viashiria vya upotevu wa fedha. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyooneka katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 98: Gharama za huduma za usafi usiolingana na thamani halisi ya fedha**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha zilizolipwa(Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 5/8 | 16335 | 4,500,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya usafi wa ndani kwa jengo la Ofisi ya RaisFedha na Mipango Pemba. |
| 13/10 | 171068 | 9,000,000 | |
| 42/10 | 18065 | 4,500,000 | |
| 3/1 | 18815 | 4,500,000 | |
| 13/2 | 19350 | 10,500,000 | |
| 15/3 | 19912 | 6,000,000 | |
| 9/4 | 20402 | 6,000,000 | |
| 14/5 | 21072 | 6,000,000 | |
| **Jumla** | | **51,000,000** | |

### Majibu ya Wizara

Ulipaji wa huduma ya usafi unategemea na eneo linalofanyiwa usafi na huduma zinazoambatana na usafi husika. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango-Pemba imeingia mkataba wa usafi na Kampuni ya AKB kwa muda wa mwaka mmoja ambapo mkataba huo unaeleza maeneo ya kufanyia usafi yatakuwa ni ghorofa tatu, ngazi katika ghorofa hizo, vyoo vya ndani katika ghorofa tajwa pamoja na vyoo vya njee katika majengo ya Serikali Gombani na sehemu ya kuhifadhia taka ngumu (Jaa) la majengo ya ofisi za Serikali Gombani ambapo taka zilizomo zinatakiwa kuondoshwa kila siku, huduma nyengine za usafi ni pamoja na kutupatia vifaa vya huduma ya usafi katika sehemu za usafi pamoja na vyoo vilivyopo katika ghorafa tajwa ambapo sehemu na huduma hizo nyengine hazipatikani katika mawizara mengine waliotumika katika kulinganisha gharama. Kwa kuzingatia maelezo ya hapo awali gharama ya usafi kwa Ofisi ya Rais fedha na Mipango haikuwa kubwa.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kuwa gharama za usafi katika majengo ya Ofisi mpya zilizopo Gombani Pemba zinatofautiana kulingana na maeneo ambayo yanahitaji kupatiwa

huduma hiyo. Hivyo, Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Wizara kwa vile Ofisi ya Rais, Fedha na mipango ina maeneo mengi zaidi yakiwemo vyoo vyote vya nje pamoja na eneo la kuhifadhia taka zote. Kimaumbile, maeneo hayo yanatumiwa na takriban Taasisi zote ziliopo katika eneo hilo lakini ni Wizara ya Fedha pekee Pemba ndio inayohusika na malipo ya gharama za usafi wa maeneno hayo.

Kamati ya PAC pia imebaini hoja hii imejitokeza kwa sababu Mkaguzi alilinganisha na mikataba ya Mawizara mengine ambayo maeneo yao sio makubwa ukilinganisha na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Wizara na haikuwa na maelezo zaidi.

**Hoja nambari shilingi 42,032,500/-**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa malipo yenye jumla ya shilingi 42,032,500 kwa ajili ya safari za kikazi lakini malipo hayo yamekosa uthibitisho wa safari kutokana na kutokuonekana kwa majina ya wasafiri hao katika kumbukumbu za kitabu cha wasafiri (manifest) kinachoonesha idadi ya wasafiri, jina la msafiri, tarehe ya safari, muda wa safari pamoja na ndege aliyosafiria.

Kutokana na uwepo wa tiketi za kusafiria tulizowasilishiwa kwa ajili ya ukaguzi tumeshindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa uwepo wa safari hizo kutokana na kukosekana kwa taarifa za majina ya wasafiri hao katika mashirika ya usafiri wa anga kwa siku na tarehe kwa mujibu wa tiketi hizo jambo ambalo linapelekea uwepo wa viashiria vya upotevu wa fedha za umma. Kiambatanisho nambari 5 cha Ripoti ya Mdhibiti kinahusika.

**Majibu ya Wizara**

Ni utaratibu wa kawaida kwa Wizara kuwasafirisha watendaji wake kwenda katika maeneo tofauti kwa ajili ya kutimiza wajibu wao wa kiutendaji ikiwa pia ni kuwaongezea utaalamu. Safari zinazohojiwa uthibitisho wake upo licha ya hilo Wizara itaongeza zaidi udhibiti wa ndani katika kuhakikisha kwamba safari yoyote mtumishi anayokwenda anawasilisha pia ripoti ya safari husika ili kuongeza uthibitisho Zaidi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ilisikiliza maelezo yaliyokuwa yakitofautiana baina ya Mkaguzi (CAG) na Watendaji wa Wizara ambapo upande mmoja ulieleza kwamba kwa vile vielelezo vya malipo ya safari za kikazi (tiketi) vilikuwepo walitaka vichukuliwe kama ni uthibitisho wa kuhalalisha matumizi ya fedha yaliyofanyika wakati CAG alisisitiza

kwamba uhalali wa matumizi ya fedha hizo unathibitishwa na kuwepo kwa majina husika ndani ya 'manifest' ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Pemba.

Kutokana na kuwepo tofauti hiyo, Kamati ya PAC iliamua kulifuatilia zaidi suala hilo kwa kumuandikia barua Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ya tarehe 31 Oktoba, 2022 yenye kumbukumbu namba BLW/K.10/31/40 ili kujiridhisha kwamba orodha ya watumishi ambao wamesafi wamo katika kitabu cha wasafiri (manfest).

Kamati ya PAC imegundua kwamba orodha ya majina ya kitabu cha wasafiri (manfest) iliyopatiwa kupitia majibu ya barua yaliyowasilishwa tarehe 11/11/2022 yenye kumbukumbu nambari ZAA/BLW/01/19/VOL.1 kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege iliyoeleza wazi kwamba hakukuwa na taarifa za majina ya wasafiri kutoka katika Shirika la ndenge la As Salam Air kulingana na muda, siku na tarehe ya safari husika kama inavyoonekana hapa chini:-

**Orodha ya Wafanyakazi waliothibitika kuwa hawakusafiri**

| Na | Jina la aliyesafiri | Tarehe na wakati aliosafiri | Nambari ya tiketi | Ndege aliyosafiria | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Abrahman Abdalla Talib | 9/5/2021 saa 17:15 | 2619168391 | As Salam Air | Kwa mujibu wa kitabu cha Wasafiri (manfest) ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imebainika orodha ya majina ya Watu hao hawakusafiri kama ilivyoelezwa na Mkaguzi. |
| 2. | Mohammed Ali Mohammed | 21/8/2020 saa 17:15 | 2618311358 | As Salam Air | |
| 3. | 1) Salim Hassan Salum | 5/10/2020 saa 7:45 | 2618410874 | As Salam Air | |
| | 2) Bimkubwa Mgeni Rashid | 22/9/2020 saa 17:15 | 2618382735 | As Salam Air | |
| | 3) Firdaus Khatib | 5/10/2020 saa 7:45 | 2618412854 | As Salam Air | |
| | 4) Nachia Suleiman | 4/10/2020 saa 7:45 | 2618413451 | As Salam Air | |
| | 5) Juma Issa Juma | 4/10/2020 saa 7:45 | 2618411153 | As Salam Air | |
| 4. | 1) Hamad Mfaki Rashid | 25/10/2020 saa 16:00 | 2618462331 | As Salam Air | |
| | 2) Haji Sharif | 23/10/2020 saa 18:00 | 2618344071 | | |
| | 3) hashil Fadhil | 19/10/2020 saa | 80017866779 | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Abdullah | 12:00 | | | |
| 5. | Salim Hassan Salim | 1/9/2020 saa 8:10 | 2618333619 | As Salam Air | |

Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC haikuridhika na imesikitishwa kwamba kuna baadhi ya watumishi, wanatumia vibaya fedha za Serikali yetu kwa kufanya udanganyifu wa kuonesha vielelezo visivyo halali ili kuhalalisha malipo ya safari zao za kikazi jambo ambalo linaitia hasara Serikali yetu na kudhoofisha uchumi wa Taifa letu.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inaitaka ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwachukulia hatua kali za kinidhamu Watumishi wote ambao wamefanya udanganyifu wa kughushi vielelezi vya safari bila ya kusafiri ikiwemo kukatwa fedha hizo katika mishahara yao ili ziweze kurudi Serikalini.
2. Wizara ihakikishe inawasimamia kwa karibu Watendaji wake ili kuepusha vitendo vya udanganyifu kufanywa na Watendaji hao.

**Hoja nambari 6.4.1.6: Malipo ya fedha yenye vielelezo pungufu shilingi 79,209,998/-**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo jumla ya shilingi 79,209,998 ambazo zimelipwa kwa mtumizi mbali mbali ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba lakini baadhi ya vielelezo vya matumizi hayo havikuambanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 99: Malipo yenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 06/10 ya 03/10/2020 | 017162 | 4,376,699 | Halim Enterprises | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa UPS na Betri zacomputer. |
| 07/10 ya 03/10/2020 | 017163 | 3,189,519 | Nassor Said Nassor | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitu vidogovidogo. |
| 10/10 ya 03/10/2020 | 34600105 | 1,313,010 | Bin Amour Traders | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vyaCamera. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11/10 ya 03/10/2020 | 01765 | 359,709 | Gombani Garage Co-oparation | Malipo ya fedha kwa ajili yamatengenezo ya Generator. |
| 12/10 ya 03/10/2020 | 017167 | 1,960,000 | Zahran Abdallah Hemed | Malipo ya fedha kwa ajili yaya ununuzi wa Air Condition. |
| 17/10 ya 03/10/2020 | 017171 | 3,092,233 | Misufini Stationary Centre | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa wino wa Printer kwa matumizi ya Ofisi |
| 18/10 ya 03/10/2020 | 017172 | 428,155 | Seif Nassor Salim | Malipo ya fedha kwa ajili yaya ununuzi wa maji. |
| 21/10 ya 3/10/2020 | 346106 | 9,847,573 | Quality Investment Service | Malipo ya fedha kwa ajili yaya ununuzi wa Computer. |
| 25/12 ya 1/1/2021 | 19042 | 3,503,000 | Wizara ya fedha na Mipango Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili yamfuko wa maafa. |
| 36/1 ya 21/1/2021 | 22012171 | 627,000 | Idara ya hazina | Malipo ya fedha kwa ajili yamkato wa Idara ya Hazina. |
| 37/1 ya 21/1/2021 | 22012170 | 1,350,750 | Zanzibar NHIF Collection Account | Malipo ya fedha kwa ajili yamkato wa NHIF. |
| 42/1 ya 25/1/2021 | 19258 | 2,440,485 | Capital Technoloy Center | Malipo ya fedha kwa ajiliya ununuzi wa wino wa Printer. |
| 10/11 ya 5/1/2021 | 18962 | 6,580,000 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili yaposho mbali mbali na likizo. |
| 12/1 ya 18/1/2021 | 18973 | 2,667,408 | Halim Enterprises | Malipo ya fedha kwa ajili yaVifaa vya kuandikia. |
| 09/3 ya 9/03/2021 | 19857 | 585,146 | Seif Moh'd Juma | Malipo ya fedha kwa ajili yaya matengenezo ya Gari. |
| 3/7 ya 20/7/2020 | T.0 | 15,938,643 | TRA Domestic Revenue | Malipo ya fedha kwa ajili yamkato wa Income Tax. |
| 30/8 ya 19/8/2020 | - | 883,320 | Zanzibar NHIF Collection Accounts. | Malipo ya fedha kwa ajili yaNHIF. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 35/8 ya 20/8/2020 | 016661 | 5,223,400 | Tahfif Auto Works | Malipo kwa ajili ya ununuziwa vifaa vya gari SMZ 862A. |
| 3/9 ya 3/9/2020 | 017540 | 1,200,000 | Wizara ya Fedha na Mipango | Malipo kwa ajili ya shughuliza Idara ya IFMS na Ukaguzi. |
| 2/2 ya 5/2/2021 | 19326 | 2,865,000 | Wizara ya fedha na Mipango MtumwaAli Khamis Ali Abdalla Khamis Abeid Mohd Salim. | Malipo ya fedha kwa ajili yasafari ya Unguja kikazi. |
| 33/3 ya 19/3/2021 | 20002 | 3,331,000 | Mfuko wa maafa | Malipo ya fedha kwa ajili yamfuko wa maafa. |
| 43/3 ya 19/3/2021 | 26032152 | 872,948 | TPB Bank PLC | Malipo ya fedha kwa ajili yamkato wa TPB. |
| ¼ ya 1/4/2021 | 20327 | 735,000 | Firdaus Khatib Haji | Malipo ya fedha kwa ajili yasafari kikazi. |
| ¼ ya 1/4/2021 | 20327 | 500,000 | Haski Product And Deliver | Malipo ya fedha kwa ajili yachakula na viburudishaji. |
| ¼ ya 1/4/2021 | 20327 | 1,940,000 | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | Malipo ya fedha kwa ajili yaposho la siku za mapumziko. |
| 7/4 ya 15/4/2021 | 20400 | 2,000,000 | Imprest – Masurufu | Malipo ya fedha kwa ajili yamasurufu (imprest). |
| 16/4 ya 19/4/2021 | 20473 | 1,400,000 | Halim Enterprises | Malipo ya fedha kwa ajili yaununuzi wa Antivirus 14 Pc. |
| **Jumla** | | **79,209,998** | | |

**Majibu ya Wizara**

Vielelezo vyote vinavyotakiwa kuambatanishwa na hati za malipo vipo na hata hivyo, Wizara inachukua jitihada zaidi ya kuboresha mfumo wa udhibiti wa ndani ili kuhakikisha kwamba malipo yanayofanyika vielelezo vyake vinaambatanishwa kwa wakati katika hati za malipo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuna changamoto ya kukosekana ushirikiano baina ya Watendaji wa Wizara na Wakaguzi hususan wakati wa kuhitajika vielelezo. Hili limebainika baada ya kupatiwa vielelezo vyote lakini lakushangaza alipofika Mkaguzi amedai kwamba hakupatiwa vielelezo hivyo. Kwa mantiki hiyo, Kamati yetu haikufurahishwa na Watendaji wa Serikali moja kutofautiana katika utekelezaji wa majukumu yao.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri kuwe na mashirikiano mazuri baina ya Watendaji wa Wizara na Ofisi ya Mdhibiti ili kupatikane ufanisi na katika utekelezaji wa majukumu ya kazi zao.

**Hoja nambari 6.4.1.7: Malipo ambayo hayakuidhinishwa shilingi 34,353,968/-**

Jumla ya shilingi 34,353,968 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango lakini idhini ya kufanyika kwa malipo hayo imekosekana katika hati za malipo.

Kufanya malipo ambayo hayakuidhinishwa kunaweza kunapelekea kushindwa kuthibitika kwa uhalali wa malipo husika, aidha ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 100: Malipo ambayo hayakuidhinishwa**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 5/1<br>03/1/2021 | 6012140 | Zanzibar Revenue Board | 487,849 | Malipo ya fedha ya zuio la kodikwa Watoa huduma . |
| 6/1<br>03/1/2021 | 70011275 | TRA Domestic Revenue Zanzibar | 513,279 | |
| 07/1<br>03/1/2021 | 18818 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 2,770,000 | Malipo ya fedha ya likizo nahuduma nyenginezo |
| 8/1<br>05/1/2021 | 18900 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 1,380,000 | Malipo ya fedha kwa ajili yaSafari kikazi. |
| 9/1<br>11/1/2021 | 18943 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 4,823,687 | Malipo ya fedha kwa ajili yaovertime, Viburudishaji na posho maalumu |
| 10/1<br>15/1/2021 | 18962 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 6,580,000 | Malipo ya fedha kwa ajili yaposho mbali mbali |
| 12/1<br>18/1/2021 | 18973 | Halim Enterprises | 2,667,408 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vyakuandikia. |
| 15/1 | 18984 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 1,470,000 | Malipo ya fedha kwa ajili yasafari kikazi. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 19/1/2021 | | | | |
| 42/1<br><br>25/1/2021 | 19258 | Capital Technology Center | 2,440,485 | Malipo ya fedha kwa ajili yaununuzi wa wino za Printer. |
| 41/1<br><br>21/1<br><br>22/1/2021 | 19016 | People's Bank of Zanzibar | 323,250 | Malipo ya fedha kwa ajili yaPosho la kukaimu. |
| 43/1/2021 | 19074 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 960,000 | Malipo ya fedha kwa ajili yaSafari kikazi. |
| 10/03<br><br>09/03/2021 | 19858 | Hahana restaurant | 547,864 | Malipo ya fedha kwa ajili yaununuzi wa Chakula |
| 9/03<br><br>9/3/2021 | 19857 | Seif Moh'd Juma | 585,146 | Malipo ya fedha kwa ajili yahuduma za gari za Ofisi |
| 13/03<br><br>10/03/2021 | 19893 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba. | 4,410,000 | Malipo ya fedha kwa ajili yaSafari kikazi, Posho la IFMS,Overtime na Likizo. |
| 8/03<br><br>08/03/2021 | 19847 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba. | 4,395,000 | Malipo ya fedha kwa ajili yaSafari kikazi, Overtime na Likizo. |
| **Jumla** | | | **34,353,968** | |

**Majibu ya Wizara**

Malipo ya Serikali yanayolipwa kwa kutumia mfumo wa IFMIS yanaidhinishwa mara tu baada ya malipo husika kuingizwa katika mfumo na kupatikana karatasi inayoitwa vocha list ambapo watendaji wa idara ya Mhasibu Mkuu hawaruhusu uendeleaji wa malipo ikiwemo kuchukua hundi ya malipo endapo vocha list haiwekwa sahihi na afisa masuuli, kwa mantiki hiyo hakuna matumizi ambayo yanaweza kufanywa bila ya idhini kutolewa. Hata hivyo ofisi itaongeza udhibiti wa ndani katika kuidhinisha malipo

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuna changamoto ya kukosekana ushirikiano baina ya Watendaji wa Wizara na Wakaguzi hususan wakati wa kuhitajika vielelezo. Hili limebainika baada ya kupatiwa vielelezo vyote lakini lakushangaza alipofika Mkaguzi amedai kwamba hakupatiwa vielelezo hivyo. Kwa mantiki hiyo, Kamati yetu haikufurahishwa na Watendaji wa Serikali moja kutofautiana katika utekelezaji wa majukumu yao.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhakikisha malipo yote yanayofanyika yanaidhinishwa kama zinavyoelekeza na sheria za usimamizi wa fedha.

Kamati inaishauri Ofisi ya Mdhibiti kutumia alama maalum itakayokuwa vigumu kwa Watendaji wa Serikali kuipata itakayotumika katika kuthibitisha vielelezo alivyovikagua ili kuepusha mgongano wakati inapokuja Kamti ya PAC kwa ajili ya Uchunguzi.

**Hoja nambari 6.4.1.8: Kukosekana kwa muongozo wa malipo ya posho la IFMIS shilingi 17,300,000/-**

Jumla ya shilingi 17,300,000 zimelipwa kwa ajili ya posho la IFMS kwa baadhi ya wafanyakazi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ambapo muongozo wa malipo ya posho hilo umekosekana kwa ukaguzi.

Kukosekana kwa muongozo wa malipo ya posho la IFMS kunaweza kupelekea kutokuthibitika kwa uhalali wa malipo ya posho hilo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchangauo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 101: Kukosekana kwa muongozo wa Malipo ya Posho la IFIMS**

| **Hati Namba** | **Hundi Namba** | **Aliyelipwa** | **Kiasi kilicholipwa (Tshs.)** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|
| 01/10<br><br>01/10/2020 | 017054 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 7,200,000 | Malipo ya fedha za posho. |
| 39/10<br><br>30/10/2020 | 018045 | | 3,700,000 | |
| 10/1<br><br>15/1/2021 | 18962 | | 3,700,000 | |
| 13/03<br><br>10/03/2021 | 19893 | | 2,700,000 | |
| **Jumla** | | | **17,300,000** | |

**Majibu ya Wizara**

Malipo ya posho la IFMIS ni miongoni mwa maposho ambayo yalikua yanalipwa kwa

watendaji waliopo chini ya Ofisi ya Mhasibu Mkuu na malipo haya yalikuwa na lengo la kuongeza ufanisi wa watendaji hao. Hata hivyo posho lilisitishwa kwa watendaji katika kutafuta njia bora ya malipo hayo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa Wizara imefanya malipo bila ya kuwepo muongozo au utaratibu mzuri wa malipo ya posho kwa wafanyakazi jambo ambalo linaleta wasiwasi kuhusiana na upotevu wa fedha za umma. Kwa mnasaba huo, Kamati yetu haikuridhishwa na majibu yaliyoelezwa na Wizara.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaishauri Wizara kuanzisha muongozo maalum wa ulipaji wa posho la IFIMS ili kuondosha wasiwasi wa upotevu wa fedha unaoweza kujitokeza.

### 6.4.3 FUNGU F03 - TUME YA MIPANGO - UNGUJA

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya Mipango kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika mwaka wa Fedha 2020/2021 Tume ya Mipango iliidhinishwa kutumia jumla ya shilingi 23,697,505,582 kwa matumizi ya kawaida, Mishahara 1,536,582,897, Matumizi Mengineyo 5,747,967,625, shilingi 11,618,700,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni Mchango wa Serikali, shilingi 1,190,150,000 kwa kazi za maendeleo kwa Washirika wa Maendeleo, na shilingi 3,604,105,060 ikiwa ni ruzuku.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 5,110,858,910 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 21.57 ya makadirio, shilingi 1,483,214,005 zimeingizwa na kutumika kwa mishahara sawa na asilimia 96.53,matumizi mengineyo 773,017,750 sawa na asilimia 13.45, kazi za maendeleo Mchango wa Serikali 682,000,000 sawa na asilimia 5.87, kwa kazi za maendeleo kwa Washirika wa Maendeleo, shilingi 102,320,000 sawa na asilimia 8.60 ya makadirio, na shilingi 2,070,307,155 ikiwa ni Ruzuku sawa na asilimia 57.44 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haikupokea majibu yanayohusiana na taarifa ya mapato siku mbili kabla ya kikao husika kama inavyoelekezwa Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi

(Toleo la 2020). Hata hivyo, Kamati imeisisitiza Tume ya Mipango kutumia ipasavyo rasilimali fedha inazopatiwa kama zinavyoelekeza SHeria za Fedha za Umma.

**Hoja nambari 6.4.3.1: Kutokukatiwa Bima kwa vyombo vya moto vya Tume ya Mipango**

Ukaguzi umebaini kuwa Tume ya Mipango inamiliki vyombo mbali mbali vya usafiri ikiwemo gari na vespa, dosari iliobainika ni kwa baadhi ya vyombo kutokukatiwa bima. Kutokukatiwa bima kwa vyombo vya moto kunaweza kukapelekea kudumaza shughuli za taasisi pale majanga yanapotokezea na kupelekea kutumia gharama kubwa ya matengenezo jambo ambalo linaweza likapelekea kupangua mipango ya utekelezaji wa shughuli nyengine walizojipangia.

Ukaguzi unashauri ni vyema Taasisi za Umma kuvikatia bima vyombo vyake ili kuepuka usumbufu utakaojitokeza pindipo majanga yanapotokezea. Mchanganuo wa vyombo ambavyo havijakatika bima ni kama inavyooekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 105: Gari ambazo hazina Bima**

| Namba | Namba ya Gari | Aina ya gari | Kabila | Namba ya Chassis | Mwaka | Muundo wa Bodi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SMZ 342 | Mitsubishi 4m 40 | Pajero | V96WLNDDFP | 2011 | Station Wagon |

**Majibu ya Tume**

Tume ya Mipango imeizingatia hoja na Ushauri umepokelewa, kwa sasa gari hiyo tayari imeshakatiwa Bima katika Shirika la Bima la Zanzibar nyenye nambari (sticker No. 22001-11186-87212).

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imegundua ni kweli gari hiyo imekatiwa bima tarehe 21/4/2022. Hivyo, Kamati yetu haikuwa na maelezo zaidi ila imeisisitiza Tume ifuate Sera, Sheria na taratibu zinazoelekezwa na Serikali.

**Hoja nambari 6.4.3.2: Malipo ya safari za kikazi na mafunzo ambayo hayakuambatanishwa na ripoti shilingi 20,945,000**

Ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo mbalimbali ya safari za kikazi na mafunzo yamefanyika lakini ripoti husika zinahusiana na safari hizo hazikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanisha ripoti kwa malipo husika ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya

Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 na kanuni ya 95(4) ya Kanuni ya Fedha ya Zanzibar ya mwaka 2005. Ukaguzi unashauri Tume ya Mipango kusimamia na kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote wanaokwenda safari za kikazi au mafunzo kuwasilisha ripoti ambazo zitaeleza tija itakayopatikana kwao na taasisi kutokana na safari, maonyesho au mafunzo hayo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 106: Malipo ya safari za kazi na mafunzo**

| Hati namba | Tarehe | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 10/4 | 16/4 | 3,000,000 | Tume ya Mipango | Utayarishaji wa ajenda ya utafiti |
| 5/5 | 3/5 | 2,895,000 | | Malipo kugharamia ziara ya uhakiki |
| 15/3 | 24/3 | 15,050,000 | | Malipo kwa ziara ya kimafunzo Ofisi za MkurabitaTanzania Bara (Dodoma) |
| **Jumla** | | **20,945,000** | | |

**Majibu ya Tume**

Malipo ya safari za kikazi na mafunzo ambayo hayakuambatanishwa na ripoti TZS. 20,945,000. Ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo mbali mbali ya safari za kikazi na mafunzo yamefanyika lakini ripoti husika kuhusiana na safari hizo hazikuambatanishwa na hati za malipo ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Majibu ya hoja ni kama ifuatavyo:

**Jadweli nambari 106: Malipo ya safari za kazi na mafunzo**

| Hati namba | Tarehe | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 10/4 | 16/4 | 3,000,000 | Tume ya Mipango | Utayarishaji wa ajenda ya utafiti |
| 5/5 | 3/5 | 2,895,000 | | Malipo kugharamia ziara ya uhakiki |
| 15/3 | 24/3 | 15,050,000 | | Malipo kwa ziara ya kimafunzo Ofisi za Mkurabita Tanzania Bara (Dodoma) |
| **Jumla** | | **20,945,000** | | |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imegundua pamoja na Watendaji wa Wizara kukiri kwamba kweli kulijitokeza kasoro hizo lakini Kamati ilitaka kujua ni vielelezo gani vilivyokosekana na kwanini hivi sasa vielelezo viwepo wakati Mdhibiti hakupatiwa vielelezo hivyo na kuelezwa kwamba vilikuwa vielelezo vya safari na ripoti za mafunzo ya wafanyakazi wanaporudi masomoni ikiwemo Ripoti ya ziara ya Uhakiki wa Programu na Miradi ya Maendeleo ya mwezi Mei, 2021 ambayo ilikuwa imehifadhiwa kimakosa sehemu nyengine. Kamati ya PAC haikuridhika uzembe uliofanyika na Kamati haikukubaliana na vielelezo hivyo. Kwa mnasaba huo, Kamati inaungana na Mkaguzi kwamba fedha ya Serikali ya shilingi 20,945,000 imepotea.

**TUME YA MIPANGO - PEMBA**

**Hoja nambari 6.4.3.3: hati za malipo zenye vielelezo pungufu kifungu jumla ya tzs 10,157,262**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 10,157,262 zimetumika kwa malipo mbali mbali ya Tume ya Mipango lakini baadhi ya vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016.Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 107: Hati za Malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1/5<br><br>6/5/2021 | 020939 | 3,000,000 | Tume ya Mipango Pemba | Malipo ya kwa ajili ya Mafunzo. |
| 3/5<br><br>6/5/2021 | 020940 | 2,116,000 | Sharif Petrol Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Mafuta ya Petrol. |
| 6/4<br><br>15/4/2021 | 020373 | 2,500,000 | Ngoto Auto Accessories | Malipo ya Fedha kwa ajili ya kugawa partition za ofisi. |
| 2/2 | 019294 | 968,447 | AKB Cleaning | Malipo ya Fedha kwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3/2/2021 | | | Enterprises | ajili ya huduma ya Usafi. |
| 7/4<br><br>15/4/2021 | 020374 | 322,815 | AKB Cleaning Enterprises | Malipo ya Fedha kwa ajili ya huduma ya Usafi. |
| 2/8<br><br>7/8/2020 | 016329 | 1,250,000 | Sharif Petrol Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petrol. |
| **Jumla** | | **10,157,262** | | |

**Majibu ya Hoja**

Uhalali wa malipo hayo, Majibu ya hoja ni kama ifuatavyo:

| Hati Namba | Hundi<br><br>Namba | Kiasi<br><br>Kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1/5<br><br>6/5/2021 | 020939 | 3,000,000 | Tume ya Mipango Pemba | Malipo kwa ajili ya Mafunzo | Katika kipindi cha ukaguzi barua za maombi ya ruhusa nambari ZPC/P/W/02 ya tarehe 29.04.2021 ya kutoa mafunzo ilifailiwa katika faili jengine na vilelezo vyake vyote. Hivyo, haikuweza kuonekana katika lililofanyiwa ukaguzi kwa wakati huo. Kwa sasa barua hiyo imeshafailiwa katika faili husika (ZPC/P/V/2021) na vielelezo vyake vyote zikiwemo vaucha. |
| 3/5<br><br>6/5/2021 | 020940 | 2,116,000 | Sharif Petrol Station | Malipo ya Fedha kwa ajili ya ununuzi wa Mafuta ya Petroli | Wakati wa Ukaguzi hati ya mapokezi (Delivery Note) haikuambatanishwa na vielelezo vyengine. Kwa sasa hati ya mapokezi zipo katika faili nambari ZPC/P/V2021pamoja na vielelezo vyote |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ikiwemo vaucha. |
| 6/4<br><br>15/4/2021 | 020373 | 2,500,000 | Ngoto Auto Accessorie | Malipo ya Fedha kwa ajili ya kugawa Partition za Ofisi. | Wakati wa ukaguzi, Mkaguzi aliagiza katika 'Proforma Invoice' kuwe na uchambuzi wa matumizi yaliyochanganuliwa baina ya kazi za ufundi na Vifaa. Kwa sasa matumizi hayo yametenganishwa na yapo pamoja na vielelezo husika ikiwemo vaucha. |
| 2/2<br><br>3/2/2021 | 019294 | 968,447 | AKB Cleaning Enterpries | Malipo ya Fedha kwa ajili ya Huduma za usafi | Katika kipindi cha Ukaguzi risiti ya malipo kwa mtoa huduma za usafi AKB Cleaning haikuwepo katika voucha za malipo na iliwekwa katika faili jengine kwa makosa. Kwa sasa, risiti hiyo ipo katika faili nambari ZPC/P/V/2021 pamoja na vaucha. |
| 7/4<br><br>15/4/2021 | 020374 | 322,815 | AKB Cleaning Enterprises | Malipo ya Fedha kwa ajili ya Huduma za usafi | Katika kipindi cha Ukaguzi risiti ya malipo kwa mtoa huduma za usafi AKB Cleaning haikuwepo katika voucha za malipo na iliwekwa katika faili jengine kwa makosa. Kwa sasa, risiti hiyo ipo katika faili nambari ZPC/P/V/2021 pamoja na vaucha. |
| 2/8<br><br>7/8/2020 | 016329 | 1,250,000 | Sharif Petrol Station | Malipo ya Fedha kwa ajili ya ununzi wa Mafuta ya Petroli | Wakati wa Ukaguzi ukaguzi hati ya mapokezi (Delivery Note) hakikuambatanishwa na vielelezo vyengine. Kwa sasa hati ya mapokezi zipo katika faili nambari |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ZPC/P/V/2021 pamoja na vielelezo vyote ikiwemo vaucha. |
| **Jumla** | | **10,157,262** | | | |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Wakati kamati inafanya uchunguzi wake ilipatiwa hivo vielelezo lakini jambo la kusikitika alipokwenda Mkaguzi kutoka kwa mdhibiti kutokana na maelezo ya mkaguzi hakupatiwa jambo hili imelipa kamati mashaka makubwa. Baada ya Kamati kuhoji, Tume ya Mipango imeleza kuwa baadhi ya vielelezo vilikuwa vimechanganywa na mafaili mengine ndio ikajitokeza hali hii.

Kamati imesikitishwa na majibu Tume ya Mipango ya kutokuweka kumbukumbu vizuri hadi kupelekea baadhi ya vielelezo kutokupatiwa Mkaguzi jambo linaloonesha kwamba Watendaji walikuwa hawana ushirikiano mzuri na Wakaguzi waliofika Ofisini hapo kutekeleza majukumu yao.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaitaka Tume ya Mipango kuweka majalada vizuri na kwa umakini ili kuepusha kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha shughuli walizozitekeleza.

**Hoja nambari 6.4.3.4: Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 4,827,183**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 10,157,262 zimetumika kwa malipo mbali mbali ya Tume ya Mipango lakini baadhi ya vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 4,827,183 zimetumika kwa ununuzi wa bidhaa mbali mbali lakini bidhaa hizo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa bidhaa hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 108: Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 6/4 | 020373 | 2,305,825 | Ngolo Auto Accessories | Matengenezo ya Aluminium Partition. |
| 14/5 | | 713,592 | Malinge Enterprise Wete Pemba | Ununuzi wa:<br><br>Counter Book 4 Q 10 pcs |
| ½ | 019293 | 1,807,766 | Capital Technoloy Centre | Ununuzi wa:<br>i) HP Desk Top Core i5 (HP I TB – RAM 4 GB) 1 set<br>ii) CPU – Desk Top Core i3 |
| **Jumla** | | **4,827,183** | | |

**Majibu ya Wizara**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo | Majibu ya Hoja |
|---|---|---|---|---|---|
| 6/4 | 020373 | 2,305,825 | Ngoto Auto Accessories | Matengenezo ya Aluminium Partition | Matengenezo ya Ofisi Partition hayakuingizwa katika daftari la ghalani. Kwa mujibu wa makubaliano mtoa huduma (Ngoto Auto Accessories) ni kufanya matengenezo na kukabidhi kazi baada ya kukamilika. |
| 14/5 | | 713,592 | Malinge Enterprises | Ununuzi wa:- | Wakati wa Ukaguzi vifaa 'Counter book |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wete Pemba | Counter book 4q 10pcs | 4q 10 pcs' havikurikodiwa ghalani. Kwa sasa mabuku hayo yamerikodiwa katika daftari la ghalani na yapo kwa matumizi ya Ofisi. |
| 1/2 | 019293 | 1,807,766 | Capital Technology | Ununuzi wa:-<br><br>i) HP Desk Top Core i5 (HP TB-RAM 4 GB) 1set<br><br>ii) CPU – Desk Top Core i3 | Ofisi yangu imejiridhisha kwamba vifaa: ((i) HP Desk Top Core i5 (HP TB-RAM 4 GB) 1set<br><br>ii) CPU – Desk Top Core i3) vyote vimerikodiwa katika daftari la ghalani. |
| **Jumla** | | **4,827,183** | | | |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Baada ya Kamati kupata maelezo na Tume ya Mipago kuhusiana na hoja hii, Kamati imeridhika na haikuwa na hoja zaidi.

### 6.4.4: OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya mapato**

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 9,710,000,000 kutoka katika vyanzo vyake vya kodi na visivyokuwa vya kodi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 4,595,269,986 zimekusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya kodi na visivyokuwa vya kodi sawa na asilimia 47 ya makadirio.

**Majibu ya Ofisi**

Kamati ya PAC baada ya kuyapitia majibu ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iligundua kwamba majibu waliyoyawasilisha mbele ya Kamati yalikuwa ya mwaka

2021/2022, mwaka ambao haukulingana na hoja za Ripoti ya Mdhibiti. Kamati ya PAC ilielekeza kwamba majibu hayo yawasilishwe kwa Katibu wa Kamati ili Kamati iweze kuyapitia na kutoa ushauri wake. Lakushangaza, hadi Kamati inawasilisha Ripoti yake leo, lakini hakuna majibu yaliyowasilishwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Hata hivyo, Kamati ya PAC ilitaka kujua ni aina gani ya vyanzo ambavyo Ofisi ya Mtakwimu inavitegemea katika kupata mapato yake na kuelezwa ni utoaji wa huduma za takwimu kwa Washirika wa Maendeleo pamoja na malipo ya kumbi za mikutano. Hivyo, Kamati yetu haikuwa na hoja zaidi.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika mwaka wa Fedha 2020/2021 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iliidhinishwa kutumia jumla ya shilingi 9,710,000,000 kwa matumizi ya kawaida, na jumla ya shilingi 3,602,300,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo pamoja na shilingi 5,922,700,000 kwa kazi za maendeleo kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 4,595,269,986 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 47 ya makadirio, shilingi 1,654,258,070 zimeingizwa na kutumika kwa mishahara na posho sawa na asilimia 57 ya makadirio, matumizi mengineyo shilingi 416,050,065 sawa na asilimia 20 ya makadirio, na shilingi 2,435,807,333 kwa kazi za maendeleo kutoka kwa washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 41 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini majibu ya Taarifa za Matumizi yanatofautina na yale yaliyoainishwa na Mkaguzi, hilo limetokana na kwamba Ofisi ya Mtakwimu imejibu Taarifa za Matumizi za mwaka 2021/2021 badala ya mwaka 2020/2021. Hivyo, Kamati imeitaka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuwasilisha majibu kulingana na mwaka husika. Lakushangaza, hadi Kamati inawasilisha Ripoti yake leo hii, hakuna majibu mengine yaliyowasilishwa.

## 6.7.4: WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA WA SERIKALI - UNGUJA

**Taarifa ya Mapato**

Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,806,950,622 kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,308,295,259.7 zilikusanywa sawa na asilimia 72 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati haikupokea majibu ya Taarifa za Mapato siku mbili kabla ya kikao kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Baraza, Toleo la 2020 isipokuwa ilielekeza majibu hayo yawasilishwe kwa Katibu ili yapate kupitiwa na Kamati lakini kwa bahati mbaya hadi hivi sasa hakuna majibu yaliyowasilishwa mbele ya Kamati.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,806,950,622 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,263,438,297 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 59.2 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati haikupokea majibu ya Taarifa za Mapato siku mbili kabla ya kikao kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Baraza, Toleo la 2020 isipokuwa ilielekeza majibu hayo yawasilishwe kwa Katibu ili yapate kupitiwa na Kamati lakini kwa bahati mbaya hadi hivi sasa hakuna majibu yaliyowasilishwa mbele ya Kamati.

**Hoja nambari 6.7.4.1: Kukosekana kwa mchanganuo wa makusanyo ya mapato ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu Tzs. 253,813,904.00**

Katika kupitia taarifa mbalimbali za fedha Ukaguzi umeshindwa kutofautisha makusanyo halisi ya huduma mbalimbali zinazotolewa na Wakala kwa mujibu wa Sheria ya Wakala kutokana na kushindwa kuweka kumbukumbu za ukusanyaji wa mapato kwa Bandarini na Ofisi kuu kwenye mfumo ambao utaainisha tofauti ya huduma hizo (mchanganuo). kwa kawaida uchunguzi huo unakusanya mapato yanayotokana na uchunguzi wa DNA, Asali, Dawa Asili, Mafuta, Pombe, Maji, Mkojo, Kemikali, vile vile wanatoa huduma ya utoaji Vibali (chemical na chemical product).

Kushindwa kuweka mchanganuo wa makusanyo ya mapato katika mfumo mzuri ambao

utapelekea ufungaji mzuri wa Hesabu za mwaka kutapelekea kushindwa kujua mapato halisi yaliyotokana na vyanzo hivyo, aidha kutojua gharama zinazotumika kwa kufanya huduma ya vifaa vya uchunguzi pamoja na ununuzi wa bidhaa zitakazoleta tija kwa Taasisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kuchukuwa jitihada za kuhakikisha kuwa mapato yote yanayotokana na utoaji wa huduma za Maabara yanarikodiwa kwa utaratibu uliowekwa wa kutofautisha huduma hizo.

**Majibu ya Wakala**

Mfumo wa zamani wa malipo ulikuwa hauwezi kutofautisha vyanzo vya mapato. Uchanganuzi wa malipo mahususi ya huduma hizo za uchunguzi na udhibiti wake mikali unaonekana kwenye Stakabadhi za mapato hayo. Wakala wa Maabara inapokea ushauri wa ukaguzi kwa kuhakikisha kuwa mapato yote yanarikodiwa kwa kutofautisha huduma husika zinazotolewa na Maabara kwa lengo la kujua gharama halisi za uendeshaji kwa kila huduma inayotolewa.

Ingawa kwa sasa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inatumia utaratibu mzuri wa mgawanyo wa malipo kutokana na uwepo wa 'control number' inayoainisha mgawanyo wa malipo ya huduma husika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa ni kweli hesabu za mwisho wa mwaka hazioneshi utofauti wa vyanzo vya mapato vya Wakala wakati alipokamilisha uchunguzi waka Mkaguzi. Hali hiyo imeonekana baada ya Kamati kupitia 'Note' nambari 16 ya Hesabu za mwisho wa mwaka na kugundua hakukuwa na mchanganuo husika. Hata hivyo, kwasasa mchanganuo huo unaonekana katika mfumo wanaotumia wa Zan malipo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali uhakikishe unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na vigezo vya Kitaifa na Kimataifa hususan wakati wa uandaaji wa hesabu za mwisho za Wakala.

**Hoja nambari 6.7.4.2: Kukosekana kwa kibali cha ruhusa ya matumizi ya fedha za mapato Tzs 315,000,000.00**

Ukaguzi umebaini kuwa Taasisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu inafanya matumizi yake kwa kutumia fedha za makusanyo ya ndani kwenye hesabu nambari 0403978000 jumla ya shilingi 315,000,000 zimebainika kutumika kwa matumizi mbali mbali dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa muongozo au ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali inayowataka wakala kutumia fedha za mapato kwa ajili ya uendeshaji wa huduma zinazotolewa na taasisi hiyo.

Kutumia fedha za mapato kwa matumizi mbali mbali bila ya kuwepo kwa ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kuhakikisha unafanya matumizi ya fedha zilizoidhinishwa ili kuepuka kufanya matumizi yasiyo na tija.

**Jadweli Nambari 161: Matumizi ya fedha za mapato zisizoidhinishwa**

| Hati Namba | Hundi namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| R/4/5 ya 20/5/2021 | T.T kutoka A/C 0403978000 ya mapato kwenda 0404060000 PBZya matumizi | Wakala wa Maabaraya Mkemia | 35,000,000 |
| R/19/3 ya 24/3/2021 | T.T | | 30,000,000 |
| R/2/2/2021 ya 12/2/2021 | | | 50,000,000 |
| R/15/01 ya 15/1/2021 | | | 25,000,000 |
| R/17/11 ya 25/11/2020 | | | 20,000,000 |
| R/11/7 ya 27/7/2020 | | | 20,000,000 |
| R/11/6 ya 17/6/2021 | | | 30,000,000 |
| R/28/9 ya 11/9/2020 | | | 30,000,000 |
| R/38/10 ya 21/10/2020 | | | 25,000,000 |
| R/17/11 ya 25/11/2020 | | | 20,000,000 |
| R/11/6 ya 17/6/2021 | | | 30,000,000 |
| **Jumla** | | | **315,000,000** |

Taasisi kufanya matumizi ya fedha za makusanyo ya ndani bila ya kuwa na kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kutapelekea kufanya matumizi yaliyo nje ya bajeti ambayo hayatakuwa na ulazima na kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya ukiukwaji wa matumizi ya fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kuchukuwa jitihada za kuhakikisha Wakala inapata ruhusa ya kutumia fedha za makusanyo kutoka katika taasisi husika.

**Majibu ya Wakala**

Wakala wa Maabara ilikuwa inatumia fedha za makusanyo kwa kutekeleza shughuli iliyojipangia kwa mwaka wa fedha husika. Hii ilitokana na kufuata muongozo wa ndani wa Taasisi ambao ulipata Baraka za Mheshimiwa Waziri wa Afya baada ya kupitishwa na Bodi ya Ushauri.

Hata hivyo, Wakala imepokea ushauri wa ukaguzi wa kutotumia fedha hizo bila ya idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hivyo Wakala ilisitisha mara moja matumizi ya fedha hizo za mapato na kuwasilisha ombi la kutumia fedha hizo kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa matumizi muhimu ya Maabara ikiwemo kufanyiwa 'service machine ya DNA kwa barua yenye kumbukumbu MMS/W.20/F1/71 ya tarehe 13/06/2022. Ruhusa hiyo ilitolewa kwa barua yenye kumbukumbu nambari BC.195/199/01/37/24 ya tarehe 16/6/2022.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba ni kweli malipo ya fedha za mapato yalikuwa yakifanywa kupitia muongozo ambao Bodi yao ya Ushauri iliuridhia, Hata hivyo, Kamati yetu ilitaka kujua Sheria ya kuanzisha Ofisi ya Wakala wa Mkemia Mkuu Zanzibar namba 10 ya mwaka 2011 inasemaje kuhusu mamlaka ya kuidhinisha makusanyo. Kifungu cha 12(1) kinaeleza wazi vyanzo vya mapato ya Wakala lakini haijaainisha mamlaka ya kuidhinisha matumizi ya mapato wanayoyakusanya. Hivyo, uwezo huo unabakia kwa Milipa Mkuu wa Serikali kama inavyoelekeza Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Kamati imebaini kuwa hivi sasa Wakala unatumia makusanyo yake baada ya kupata idhini kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ambapo Kamati imefanikiwa kuona barua ya maombi hayo ya tarehe 13/6/2022 yenye kumbukumbu nambari MMS/W.20/FI/71 na kujibiwa na Mlipaji Mkuu kwa barua ya tarehe 16/6/2022 yenye kumbukumbu nambari BC.195/199/01/37/24.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Ili kuondokana na changamoto ya upungufu wa fedha za uendeshaji, Kamati yetu inaushauri Wakala kufanya marekebisho ya Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ili iweze kutoa uwezo kwa Wakala kubakisha asilimia 20 za makusanyo yake.

**Hoja nambari 6.7.4.3: Kukosekana kwa ulinzi dhamana katika Taasisi ya Wakala wa Mkemia**

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu inajukumu la kutoa huduma za uchunguzi wa madawa ya kulevya, sumu, uchunguzi wa vinasaba pamoja na kuweka kumbukumbu za vinasaba, kudhibiti usajili kemikali na bidhaa zinazotokana na kemikali za majumbani na viwandani, kufanya uchunguzi wa sampuli za chakula pamoja na vinywaji. Ukaguzi umebaini kuwa Taasisi hiyo ina vifaa nyeti (Mashine za kufanyia uchunguzi mbalimbali) kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao bila ya uwepo wa Ulinzi dhamana kwa lengo la kulinda usalama wa vitendea kazi hivyo.

Kutokuwa na usalama wa kutosha katika Taasisi ya wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu kuna uwezekano mkubwa wa kuhujumiwa kwa mashine ambazo Serikali imetumia fedha nyingi kwa kufanya manunuzi hayo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kuchukuwa

jitihada za haraka kuhakikisha kwamba Taasisi hiyo inakuwa na ulinzi dhamana kwa ajili ya usalama wa vitendea kazi

**Majibu ya Wakala**

Ulinzi uliokuwepo awali ulikuwa ni walinzi wa Wizara ya Afya ambao walikuwa hawatoshelezi na kutokuwa na vitendea kazi madhubuti.

Ushauri umefanyiwa kazi na kuanzia Machi 2022, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imepatiwa walinzi kutoka Vikosi vya SMZ (KVZ).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Wakala kukiri kuwepo kwa changamoto ya kutokuwa na ulinzi madhubuti. Hata hivyo, Kamati imegundua kwamba ushauri wa Mkaguzi umefanyiwa kazi ipasavyo ambapo mbali kuwepo kwa ulinzi kutoka Kikosi cha KVZ, pia Wakala umeweka CCTV kamera pamoja na kutumia mfumo wa ulinzi wa 'biometrix' kwa wafanyakazi wanaoingia na kutoka Maabara. Kutokana na majibu hayo, Kamati yetu imeridhika na majibu na kusisitiza kuwa ni vyema kwa Wakala kuweka usalama katika milango ya Maabara yao.

**Hoja nambari 6.7.4.4: Kukosekana kwa Utaratibu wa utoaji mikopo ya ndani kwa wafanyakazi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali**

Katika kupitia taarifa za fedha pamoja na taarifa za benki, Ukaguzi umebaini kuwepo kwa shilingi 13,576,364.35 katika hesabu ya Wakala yenye namba 0406584000 ambazo zinatumika kwa ajili ya Mfuko wa mikopo ya ndani kwa wafanyakazi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu Zanzibar, Mfuko huo ulianzishwa kipindi cha mwaka fedha 2017/2018 kupitia makusanyo ya ndani "Capital" wa jumla ya shilingi 50,000,000.

Aidha, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wameanzisha mfuko huo bila ya kuwa na sera zinazotoa muelekeo wa namna ya kukopa pamoja na kurejesha fedha zilizokopeshwa, jambo ambalo linapelekea kukosekana kwa muongozo na masharti ya kukopa na kulipa mikopo inayotolewa na taasisi hiyo kwa muda muafaka kwa kuzingatia vigezo na masharti ili tija ipatikane kwa watumishi pamoja na taasisi kwa ujumla.

Kukosekana kwa sera ya mikopo kwa mfuko wa mikopo katika Taasisi kutapelekea Taasisi kukosa vigezo vya kumchukulia hatua mtendaji ambae atashindwa kulipa mkopo pindipo atakwenda kinyume na vigezo na masharti yake. Vile vile inapelekea upendeleo wa kupata mikopo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali jitihada za kukaa na watendaji wanaohusika na suala zima la mfuko wa mkopo kwa lengo la kuandaa sheria ya mikopo pamoja na sera za mikopo (Credit Policy)

**Majibu ya Wakala**

Wakala wa Maabara ilipokea ushauri wa ukaguzi na kusimamisha zoezi la utoaji wa mikopo mipya hadi hapo utaratibu utakapokamilika. Kwa wale waliokopa wanaendelea kulipa kupitia mishahara yao.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake ya ukaguzi kwa Wakala wa Mkemia Mkuu, kulikuwepo na fomu maalum ambayo inayo masharti na vigezo vya jinsi gani Mfanyakazi apatiwe mkopo ikiwemo kuandika barua ya maombi, kiwango cha mwisho wa mkopo usiokuwa na riba (3,000,000/-) pamoja na utaratibu wa mkato wa mkopo husika. Kuhusiana na Sera ya Mikopo waliyokuwa wakiitoa na kuelezwa kwamba Wakala unao muongozo wa utoaji mikopo (Staff Regulations) ambapo hadi Kamati inamaliza ukaguzi wake, Wakala ulishindwa kuuwasilisha mbele yake kwa ukaguzi.

Kadhalika, Kamati imegundua kwamba baadhi ya makusanyo waliyokuwa wakiyakusanya, ndio waliyokuwa wakiyatumia kukopeshana. Hata hivyo, utoaji wa mikopo kwa Wafanyakazi kwasasa umesita kwa vile Wakala hautumii makusanyo yake mpaka ipate idhini kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ambapo fedha wanazoingiziwa huwa hazitoshelezi hata matumizi yao ya kawaida.

Kamati ya PAC imeridhika na majibu ya Wakala na kusisitiza kwamba jambo la kukopeshana ni jema, hivyo ni busara kulitafutia mbinu mbadala wa kuliendeleza suala hilo kwa maslahi ya Wafanyakazi kwa vile huongeza mshikamano baina yao.

**Hoja nambari 6.7.4.5: Kutokuwepo kwa msimamizi wa kitengo cha Tehama**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali inatekeleza makujumu yake ya kazi mbali mbali ikiwemo majukumu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, katika ukaguzi uliofanyika timu ya wakaguzi ilifanya mahojiano mbali mbali kwa lengo la kutathmini mwenendo wa kazi za kitengo cha TEHAMA na kubaini kitengo hicho hakina msimamizi dhamana ambae atakuwa na jukumu la kusimamia sera za TEHAMA pamoja na kusamiamia miundombinu na vifaa vyote vya TEHAMA vinayotumika katika taasisi hiyo ikiwemo “hardware, software” pamoja na watumiaji wa miundombinu na vifaa hivyo vya TEHAMA.

Kukosekana kwa msimamizi wa kitengo cha TEHAMA kutapelekea kukosekana kwa udhibiti wa vifaa pamoja na miundombinu ya mifumo ya TEHAMA ya taasisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kuhakikisha unachukuwa jitihada za makusudi ili kumtafuta mtumishi mwenye uwezo na uweledi wa kusimamia masuala ya TEHAMA pamoja na kuwajengea uwezo watumishi waliokuwepo ili kuweza kusaidia changamoto za matumizi ya TEHAMA zinazoweza kujitokeza katika taasisi hiyo.

**Majibu ya Wakala**

Wakala wa Maabara ilipokea ushauri wa ukaguzi na kukiri kuwa tuna mtumishi mmoja (1) tu wa TEHAMA ambaye hajafikia vigezo vya kiutumishi vya kuwa msimamizi wa kitengo hicho.

Tumefanikiwa kupata ruhusa ya kuajiri mtumishi mmoja (1) mwenye fani hiyo husika kwa mwaka huu wa fedha 2022/23. Na mtumishi aliyepo (Afisa Daraja la Kwanza) amefanikiwa kuhudhuria mafunzo mafupi katika chuo cha KIST (Karume Institute of Science and Technology) Zanzibar, mwezi December 2021. Aidha, Afisa huyu amesaidia Afisi yetu kupatikana kwa huduma za E-Office, E-procurement, GMS, Zan-Malipo, E-banking na kadhalika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati yetu imebaini kuwa ni kweli Wakala ulikuwa na kasoro zilizoelezwa na Mkaguzi kwani mfanyakazi aliyekuwepo ana elimu ya shahada ya kwanza ya 'IT' mwenye uzoefu wa miaka mitano ya kazi. Kwa mujibu wa Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014, ili Mtumishi huyo aweze kuwa Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA ni lazima awe na uzoefu wa miaka saba.

Hivyo, Wakala bado utaendelea kuwa na changamoto ya kuweza kujirudia tena hoja hii katika ukaguzi ujao.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kutokana na kuwepo kwa mifumo kadhaa ya utendaji wa kazi za Wakala, ni vyema Wakala huo kufuata taratibu zilizoelekezwa na Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma ili kujaza nafasi ya Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA.

**Hoja nambari 6.7.4.6: Kukosekana kwa ushahidi wa majaribio ya taarifa za nakala**

Katika kupitia taarifa zinazofungamana na mifumo ya mawasiliano, ukaguzi umebaini umebaini kwamba Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali huhifadhi taarifa zake muhimu katika vifaa mbali mbali vya tehama, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba taarifa hizo hazifanyiwi majaribio (Restoration test) ili kuweza kutambua na kuhakikisha kwamba ziko katika hali ya uzima na usalama wa kuweza kufanya kazi kwa ufanisi endapo zikihitajika kufanyiwa kazi.

Kutokuzifanyia majaribio ya utendaji kazi kila mara kwa taarifa zilizokuwa zimehifadhiwa kunaweza kukapelekea athari ya kutozipata taarifa hizo kutokana na kuharibika au kuathirika kwa namna yoyote bila ya kujulikana na hatimae kupelekea kutokezea kwa janga

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu kuanzisha sera za kuhifadhi nakala za taarifa

kutoka katika mifumo yote ya taasisi na kuzifanyia majaribio ya mara kwa mara ili kuweza kuona kama ni sahihi na zinaweza kufanya kazi vzuri na kuzitegemea endapo janga lolote likitokea katika miundombinu ya mikuu ya mawasiliano ya Wakala.

**Majibu ya Wakala**

Ushauri umefanyiwa kazi, na taarifa za nakala zimefanyiwa majaribio, na ushahidi upo tayari kwa ukaguzi. Hata hivyo, Wakala wa Maabara ilipokea ushauri huu.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali kukubaliana na hoja ya Mkaguzi na tayari wameufanyia kazi ushauri wake. Kamati yetu haikuwa na maelezo zaidi.

**Hoja nambari 6.7.4.7: Kutozingatiwa vizuri kwa utengenezaji wa akaunti za watumiaji wa mfumo wa Data Pack**

Ukaguzi umebaini kuwa, kumetengenezwa akaunti nyingi zisizokuwa na ulazima katika mfumo wa (Data Pack) na kubainika akaunti ambazo hazina majina halisi ya watumiaji na nyengine hazitumiwi kabisa na wahusika.

Kutengenezwa kwa akaunti zisizokuwa na majina halisi ya watumiaji au kutengeneza akaunti za matumizi ya mfumo zisizokuwa na ulazima katika mfumo kunaweza kupelekea kutumiwa akaunti hizo kwa kufanya uharibifu bila ya kutambuliwa aliefanya uharibifu huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kuzipitia akaunti zote za mfumo wa data pack na kuhakikisha kuwa kila akaunti inatumika kwa mtumiaji husika wa mfumo na vile vile akaunti hizo ziwekewe ukomo wa matumizi katika mfumo huo (priveledges user access).

**Majibu ya Wakala**

Kutokana kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, bado ni mpya hivyo ilibidi kuwasaidia watumiaji na akaunti hizo zilikuwa tunazijaribia kama mfumo huo umekidhi mahitaji. Hata hivyo, tumeshazifuta baada ya majaribio. Hata hivyo, Wakala wa Maabara ilipokea ushauri huu.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile hoja na majibu ya Wakala kuhusiana na hoja hii yanafanana, ucnhunguzi wa mapendekezo ya Kamati yetu yatakuwa kama yalivyoelezwa katika hoja nambari 6.7.4.6.

**Hoja nambari 6.7.4.8: Kutofanya vizuri kwa mfumo wa (Data Pack)**

Katika kupitia nyaraka mbali mbali zikiwemo hesabu za mwaka, ilibanika kwamba

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu iliununua mfumo wa Data Pack kwa lengo la kurahisisha kazi za taarifa za sampuli na utekelezaji wa kazi ya wachambuzi (Analysts). Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa Data pack ulionunuliwa unahitilafu za muda mrefu ambazo zimepelekea kushindwa kutumika vizuri na kuleta tija na ufanisi kwa ofisi hadi sasa.

Kushindwa kufanyakazi kwa mfumo huo kunapelekea kupunguza ufanisi wa kazi zote zilizokuwa zikifanywa ndani ya mfumo huo. Ukaguzi unashauri kwamba, ofisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu kuchukuwa jitihada za kuimarisha mfumo huo ikiwemo kufanya mazungumzo na walioutengeneza (System Vendor) ili kurudisha ufanisi wa utendaji kazi wa mfumo kulingana na thamani ya fedha iliyotumika kwa kununulia mfumo huo.

**Majibu ya Wakala**

Hitilafu za Mfumo wa Data Pack zimetokana na kuongezeka mahitaji ya Mfumo (System update). Hivyo marekebisho yake yanatakiwa yafanywe na Taasisi ya Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar. Kwa sasa tumeshachukua hatua ya kutenga fedha za kuendeleza mfumo huo kwa kushirikiana na Taasisi ya Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar. Sambamba na hayo, Wakala wa Maabara ilipokea ushauri huu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Wakala umekiri kujitokeza kwa kasoro hiyo na tayari imeshachukua juhudi kurekebisha kasoro hizo. Hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.7.4.9: Kutokuwepo kwa Mkataba wa mfumo wa Data Pack**

Katika kuhakiki taarifa mbali mbali zikiwemo taarifa za Hesabu ya mwaka za Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu ukaguzi umebaini kuwa, Wakala imenunua mfumo wa Data Pack kutoka kwa muuzaji na kuutumia kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za vielelezo vya sampuli (Data Pack), dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba Wakala imenunua mfumo huo na kuutumia bila ya kuingia Mkataba wa aina yoyote na muuzaji wa mfumo kwa lengo la kuweza kupata msaada pamoja na huduma za kiufundi kutoka kwa muuzaji ikiwa mfumo utaleta changamoto au ikibainika dosari yoyote ya kiutendaji katika mfumo huo.

Kutofungwa mkataba wowote baina ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu na wauzaji wa mfumo huo kunaweza kupelekea kushindwa kupata huduma kamili za utendaji kazi katika mfumo ikiwemo kupata msaada wa kiufundi, kuimairishwa kwa mfumo (updates) pamoja na leseni za matumizi ya mfumo huo na kuweza kuwawajibisha wauzaji hao kutokana na dosari na hitilafu kubwa za kiutendaji zitakapotokezea katika mfumo bila ya maelewano yoyote.

Ukaguzi unashauri kwamba, ni vyema kufungwa mikataba madhubuti ya manunuzi

baina ya Taasisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu na Taasisi yoyote itakayonunua mifumo kwao kwani mikataba hiyo itaweza kuilinda taasisi ili kuweza kupata haki ya kulipwa kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

**Majibu ya Wakala**

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu umepokea ushauri na inaahidi kuzifanyia kazi dosari hizi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia majibu ya hoja hizi (6.7.4.7, 6.7.4.8 na 6.7.4.9), Kamati ya PAC imegundua kwamba wakati Wakala ulipokuwa ukifanya maandalizi ya kuingia katika mifumo mipya na matumizi ya vyombo vya kisasa vya uchunguzi, walikuwa hawajiandaa ipasavyo kuendana na mabadiliko hayo na kupelekea utekelezaji wa kazi zao bila kufuata sheria na miongozo mbali mbali au pasi na kuwa na watumishi wenye uweledi na teknolojia mpya. Hili limethibitika baada ya Kamati kuelezwa kwamba Mfumo wa 'dats pack' ulifungwa Wakala bila ya kuwa na Mtaalamu wa masuala ya kompyuta.

Kamati yetu ilitaka kujua mpango uliopo katika kutatua changamoto hiyo na kuelezwa kuwa Wakala umejipanga kuomba ridhaa 'E.govt' ili waweze kupata mfumo unaotumiwa na Wakala wa Mkemia Tanzania Bara.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inaushauri Wakala kuchukua hatua za makusudi za kuajiri wafanyakazi wapya ili waweze kutatua changamoto za uendeshaji wa vifaa vya Teknolojia ya mawano.
2. Wakala uhakikishe unafuata taratibu zote za utoaji huduma kama inavyoelekezwa na sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ikiwemo uandaaji wa Mikataba itakayotumika kusimamia utekelezaji wa mifumo iliyonunuliwa kwa fedha nyingi za Serikali.

**Hoja nambari 6.7.4.10: Mapungufu yaliyojitokeza katika kufanya Service Mashine ya DNA yenye thamani ya USD 21,351.60 (Tsh 49,857,188.40)**

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wameingia mkataba na Company ya M/S. AFRICA BIOSYSTEMS TANZANIA LTD uliofungwa tarehe 15/7/2021 wenye thamani ya USD 21,315.60 sawa na shilingi 49,857,188.40 zilizolipwa kwa hati namba R/33/6 ya tarehe 14/6/2021 kwa ajili ya kutoa huduma ya kuifanyia Service Mashine ya Uchunguzi wa Vinasaba (DNA Machine) kwa lengo la kuhakikisha mashine hiyo inadumu kwa muda mrefu.

Dosari ya ukaguzi iliyobainika ni kukosekana kwa taratibu za kumpata mtoa huduma huyo jambo ambalo linaweza likapelekea kutumia gharama kubwa ya fedha kwa

kukosekana ushindani wa bei.

Kutokana kukiukwa kwa taratibu za kumpata mtoa huduma kumepelekea kujitokeza kwa changamoto mbali mbali ikiwemo kutokuainishwa kwa aina ya kazi na muda ambao utatumika kufanya kazi hiyo, kukosekana kwa mapato ya Serikali yatokanayo na kutokukatwa kodi kwa mtoa huduma huyo na kuiwasilisha kwa mamlaka husika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali kuhakikisha unafuata na kuzingatia matakwa ya kanuni na sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ili kuweza kupatikana kwa mapato yanayokusudiwa.

**Majibu ya Kamati ya PAC**

Utaratibu ulifuatwa wa kumpata mzabuni kwa njia ya "single source" kutokana na mashine iliyotumika ni mahususi kutolewa na Mzabuni huyo, ambae pia anatupatia huduma ya matengenezo ya mashine hiyo (maintenance) na kuzambaza vitendanishi (reagents and consumable).

Aidha matengenezo (maintenance) ya vifaa vikubwa na maalum ni kawaida kufanyiwa matengenezo hayo na kampuni ambayo imesambaza kifaa hicho na ambayo imeonesha utayari wakati wa kufunga mkataba juu ya kuendelea na kukitunza kifaa hicho kwa muda mrefu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa tayari Wakala umeshalifuatilia suala hili E-govt na kupatiwa utaratibu kwamba kwa huduma za 'service', Wakala uingie mikataba na Mnunuzi wa kifaa husika (DNA Mashine) na kwa masuala ya ununuzi wa vifaa vyengine, Kampuni hiyo ijiunge katika Mfumo ili Wakala uweze kuwachagua na kuwanunulia vifaa hivyo. Baada ya kupata maelezo hayo, Kamati ya PAC haikuwa na hoja zaidi isipokuwa imesisitiza kwamba Wakala itekeleze maelekezo hayo kwa umakini wa hali ya juu.

**Hoja nambari 6.7.4.11: Mapungufu yaliyojitokeza katika ununuzi wa DNA Consumable yenye thamani ya USD 60,585.92 (Tsh. 141,710,466.90)**

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wameingia mkataba na Company ya M/S. AFRICA BIOSYSTEMS TANZANIA LTD uliofungwa tarehe 15/7/2021 wenye thamani ya USD 60,585.92 sawa na shilingi 141,710,466.90 zilizolipwa kwa hati namba R/38/6 ya tarehe 30/6/2021 kwa ajili ya ununuzi wa (DNA Machine) kwa lengo la kuhakikisha mashine hiyo inadumu kwa muda mrefu.

Dosari ya ukaguzi iliyobainika ni kukosekana kwa taratibu za kumpata mtoa huduma huyo jambo ambalo linaweza likapelekea kutumia gharama kubwa ya fedha kwa kukosekana ushindani wa bei.

Kutokana kukiukwa kwa taratibu za kumpata mtoa huduma kumepelekea kujitokeza

kwa changamoto mbali mbali ikiwemo kutokuainishwa kwa aina ya kazi na muda ambao utatumika kufanya kazi hiyo, kukosekana kwa mapato ya Serikali yatokanayo na kutokukatwa kodi kwa mtoa huduma huyo na kuiwasilisha kwa mamlaka husika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali kuhakikisha unafuata na kuzingatia matakwa ya kanuni na sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ili kuweza kupatikana kwa mapato yanayokusudiwa.

**Majibu ya Wakala**

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wameingia mkataba na Company ya M/S. AFRICA BIOSYSTEMS TANZANIA LTD kwa ajili ya kununua vitendanishi (consumables) vya machine ya DNA (DNA Machine) kwa lengo la kufanikisha majukumu yake. Kwenye suala la kumpata Mtoa huduma ilitumika utaratibu wa Single source method kutokana uhitaji wa utunzaji wa mashine na muendelezo wa matengezo ya kifaa (DNA Machine) unahitaji muhusika yule yule aliyesambaza mashine. Aidha suala la upatikanaji wa vifaa vya maabara kiutaratibu havikatiwi kodi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati yetu imebaini kuwa ni kweli Wakala ulitumia njia ya ununuzi ya 'Single Source'. Hata hivyo, Wakala ulishindwa kufuata utaratibu wa matumizi ya njia hiyo ikiwemo ruhusa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Manunuzi. Kuhusiana na suala la ukataji wa kodi kwa Mtoa huduma, Kamati imegundua kwamba vifaa vya aina hiyo huwa havikatwi kodi isipokuwa Wizara ya Fedha na Mipango ilifanya makosa kumkata zaidi ya U$D 3,000,000 Mtoa huduma huyo.

Zaidi ya hilo, Kamati yetu imebaini kuwa kwa vile ununuzi wa mashinie ya DNA ulitokana na 'pressure' ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, haikuwa rahisi kwa Wakala kupata nafasi ya kufanikiwa kutekeleza ipasavyo taratibu zote za kisheria. Hivyo, Kamati ya PAC haikuwa na maelezo zaidi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala uhakikishe fedha za kodi alizokatwa kimakosa Mtoa huduma arudishiwe mwenyewe ili apate moyo wa kuitumikia Wakala katika kuipatia huduma usahihi wake.

**Hoja nambari 6.7.4.12: Uwepo wa deni litokanalo na utanuzi wa Maabara Tzs 335,301,404.00**

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wameingia mkataba na M/S SHAMJO COMPANY LTD na CHIEF GOVERNMENT CHEMIST LABOURATORY AGENCY uliofungwa tarehe 31/5/2019 wenye thamani ya USD 767,540,558 zilizolipwa kwa ajili ya utanuzi wa ghorofa moja ambayo imeongezewa katika jengo la zamani na kuongezewa kwa kipande cha nyuma ubavuni mwa jengo hilo.

Dosari ya ukaguzi iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi ikiwemo kutangaza zabuni ya wazi kwa lengo la kumpata msambazaji atakaetoa huduma kwa bei nafuu na kiwango bora cha ujenzi huo, jambo ambalo limekosekana na kupelekea kujitokeza kwa ongezeko la thamani la shilingi 335,301,404 ukilinganisha na bei ya awali.

Kufanya hivyo kwenda kinyume na kifungu nambari cha 49(4)(5) Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinachoeleza kwamba "Iwapo malipo ya mkataba yatazidi asilimia 15 yatalazimika kuwasilishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa lengo la kupata idhini ya matumizi." Jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika hatukuweza kupatiwa idhini ya matumizi iliyopelekea Wakala kulipa malipo ya ziada.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali unashauriwa kuipitia kwa kina mikataba yote wakati wa uandaaji wake, ili kuhakikisha dosari kama hizo zinaepukika.

### Majibu ya Wakala

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilifanya utaratibu wa restricted tender kutokana na uharaka wa matumizi ya fedha kumalizika, fedha ambazo hazikupangwa kama fedha za mradi, Aidha, fedha hizo zilitolewa chini ya idhini ya Wizara ya fedha ambapo zilitakiwa kutumika kabla ya mwaka wa fedha kuisha.

Kwa mujibu wa kikao cha pamoja baina ya Bodi ya ushauri ya Wakala wa Mkemia Mkuu, Wakala wa Majengo (ZBA) na Mkandarasi, ilionekana kuwa deni hilo halina uhalali na hazitolipwa.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC kuna baadhi ya hoja zinaingia katika kitabu cha Mdhibiti kutokana na Watendaji husika aidha kutokuwepo Ofisini au kushindwa kutoa ushirikino kwa Mkaguzi. Hili limetokea baada ya kugundua majibu yaliyojibiwa katika 'management latter' kuwa tofauti na majibu yaliwasilishwa na Wakala.

Majibu aliyopatiwa Mkaguzi yalijibiwa na Mkurugenzi Utawala pasi na kumshirikisha Mkemia Mkuu kwa vile wakati huo alikuwa ameshaondolewa kwenye nafasi. Majibu

hayo yaliyowasilishwa na Wakala tarehe 7/3/2022 yenye kumbukumbu nambari MMS/T.10/B1/42 yalieleza nanukuu “Wakala unakiri kuwa baadhi ya taraibu zilikiukwa kama alivyoeleza Mkaguzi wa nje. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi baadhi ya vielelezo havikuonekana kutokana kutokuwepo mahali husika” mwisho wa kunukuu.

Hali hiyo inabianisha wazi kwamba baadhi ya Watendaji huwa hawapo makini anapokuja Mkaguzi katika maeneo yao au anapoondoka na kuwaachia hoja za awali.

Kamati yetu imeridhika na majibu ya Wakala kwani ukizingatia hukukuwa na upotevu wa fedha za umma uliojitokeza.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Ni vyema uhakikishe unatoa ushirikiano wa karibu Mkaguzi wa Nje anapofika katika maeneo yao kwa ukaguzi ili aweze kupatiwa majibu yaliyokuwa sahihi.

**Hoja nambari 6.7.4.13: Uwepo wa matumizi mabaya ya fedha TZS 18,000,000.00 (VFM)**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za umma yenye thamani ya shilingi 18,000,000 yanayotokana na mshauri elekezi kutokuzingatia matakwa na vigezo vinavyohitajika katika ujenzi wa maabara. Kwa mujibu wa ujenzi wa maabara uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kukabidhiwa 2019/2020 umebainika ya kwamba mshauri elekezi aliwasilisha wazo la kuweka Tiles bila ya kuzingatia unyevu unyevu utakaojitokeza pindipo pakimwagika vimiminika na kusababisha utelezi au kuanguka kwa watumiaji wa eneo hilo.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuzingatiwa kwa thamani ya fedha na aina ya ujenzi uliotumika jambo ambalo baada ya muda mfupi ililazimika kuvunjwa na kuondoshwa kwa taizi zote na kuamuliwa kuwekwa tarazo ambazo zitahimili unyevu unyevu na utelezi jambo ambalo limepelekea upotevu wa fedha za umma kwa kutokuzingatia taaluma na uzoefu wa mshauri elekezi katika ushauri alioutoa.

Pamoja na uwepo wa dosari hizo ukaguzi umeshindwa kujiridhisha uhalali wa matumizi ya fedha hizo kutokana na kukosekana kwa mchanganuo wa matumizi kwa mujibu wa thamani ya vifaa vinavyohitajika kununuliwa na kutumika (BOQ), Quotation document ili kupima ufanisi na tija itakayofikiwa mara baada ya kukamilika kwa ujenzi huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuhakikisha kwamba anafuata na kuzingatia matakwa ya kisheria ili kunusuru matumizi mabaya ya fedha za umma yanayopelekea kuisababishia Serikali hasara.Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 162: Malipo yaliyofanyika kwa ajili ya uwekaji wa tarazo**

| Hati namba | Aliyelipwa | Kiasi (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| R/3/3 ya 5/3/2021 | Iddi Moh'd Nindi a/c **0740631001** | 4,500,000 | Malipo ya awamu ya pili ya uwekaji tarazo katika jengola Maabara |
| R/12/3 ya 18/3/2021 | | 4,500,000 | Uwekaji wa Tarazo katika vyumba saba vya Maabara yaMkemia jumla ya Fedha 5,940,000 |
| R/34/2/2021 Ya 23/2/2021 | | 9,000,000 | Malipo ya awamu ya kwanza ya uwekaji wa Tarazokatika Maabara ya Mkemia |
| **Jumla** | | **18,000,000** | |

**Majibu ya Wakala**

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilitumia fedha hizi kwa ajili ya ukarabati wa jengo kwa kutoa taizi na kuweka tarazo kwa sababu taizi zilikuwa zinabanduka na sio kwamba zilikuwa zinateleza au kusababisha unyevunyevu.

Vilevile, ukarabati huo haukufanyika maeneo yote kama ilivyoainishwa katika ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa hesabu (CAG).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba fundi aliyepewa kazi ya kuweka tiles maabara alitekeleza kazi yake kwa uzembe kwa vile ama alizinyima saruji au hakujua maumbile ya eneo analojenga lipo vipi. Hali hiyo, imepelekea kutumika fedha nyengine kwa ukarabati.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala usimamie kikamilifu kazi za ujenzi inazozitoa kwa Wajenzi mbali mbali ili kasoro au gharama kama hizo zisiweze kujitokeza..

WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA WA SERIKALI – PEMBA

**Hoja nambari 6.7.4.14: Malipo kwa Watoa huduma ambao Hawakujasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 10,345,300**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambapo watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi kwa mujibu wa sheria ambapo kumepelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa malipo hayo.

Kuwatumia wafanya biashara ambao hawajasajiliwa kwa mujibu wa Sheria kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yanayotokana na kodi aidha ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Afisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali- Pemba kufanya manunuzi kwa kuzingatia Kanuni, Sheria pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo. Mchanganuo wa watoa huduma ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 163: Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha kilicholipwa(Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 03/01 25/01/2021 | 001261 | 1,500,000 | Trust Construction Company Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi za ujenzi |
| 01/01 30/12/2021 | T.T | 3,500,000 | Ushirika wa Umawa Cooperative Society | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya ulinzi |
| 12/02 17/02/2021 | 001267 | 1,639,500 | Trust Construction Company Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi za ujenzi |
| 13/02 17/02/2021 | 001268 | 1,000,000 | Asam Electrical Limited | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Air condition |
| 02/05 30/04/2021 | T.T | 205,800 | One 2 One Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Antivirus |
| 10/05 07/05/2021 | T.T | 2,500,000 | Umoja wa Askari Wastaafu (UMAWA) | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya ulinzi |
| **Jumla** | | **10,345,300** | | |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imegundua kwamba ni kweli Watendaji wa Mkemia Mkuu walifanya biashara na Watoa huduma waliokuwa hawajasajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi na uondoaji wa Mali za Umma. Hata hivyo, wafanya biashara hao walikuwa wamesajiliwa ZRA na TRA.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Mkemia Mkuu Pemba wahakikishe wanafanya biashara na Watoa huduma waliokuwa wamesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

**Hoja nambari 6.7.4.15: Hati ya malipo iliyokosenekana kwa ukaguzi (missing voucher) shilingi 2,533,502**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pemba imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 2,533,502 kwa hati ya malipo namba 05/11 ya tarehe 30/11/2020 lakini hati ya malipo hayo haikupatikana kwa ajili ya ukaguzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini ni kweli kulikuwa na kasoro ya kukosekana kwa hati za malipo. Hata hivyo, Kamati yetu imegundua kwamba suala hilo lilitokana na kasoro zilizojitokeza baina ya benki na benki. Hivyo, Kamati iliridhika na majibu.

**Hoja nambari 6.7.4.16: Kukosekana kwa mapato yatokanayo na uchunguzi wa sampuli na DNA shilingi 20,730,000**

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba ofisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pemba inadai Taasisi mbali mbali za Serikali jumla ya shilingi 20,730,000 kwa ajili ya utoaji wa huduma ya uchunguzi sampuli pamoja na utoaji wa huduma katika uchunguzi wa vinasaba. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pemba kuchukuwa juhudi za makusudi ili kuhakikisha kwamba mapato yote kutoka katika vianzio mbali mbali yanakusanywa na kuingizwa katika hesabu husika ya taasisi. Mchanganuo wa mapato yaliokosekana ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 164: Mapato yatokanayo na uchunguzi wa sampuli na DNA.**

| Namba | Jina la Taasisi | Kiasi cha Fedha kinachodaiwa (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Ofisi ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Kusini Pemba | 12,150,000 |
| 2. | Ofisi ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba | 8,580,000 |
| **Jumla** | | **20,730,000** |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha watendaji wa Wakala kukubaliana na hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilitaka kujua ni Taasisi gani ambazo Wakala inazidai na hatua iliyochukua kuhakikisha madeni hayo yanalipwa na kuelezwa kwamba wanalidi Jeshi la Polisi Kusini na Kaskazini Pemba pamoja na Mamlaka ya Dawa za Kulevya Pemba. Sambamba na hilo, Kamati imeziandikia barua Taasisi hizo kuzikumbusha zenye kumbukumbu nambari CA.15/78/01/02 ya tarehe 26/9/2020 na barua CA.15/78/01/01 ya tarehe 23/9/2020. Hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala ufuatilie madeni inayodai kwa kufanya kikao na wahusika ili yaweze kulipwa.

## WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI - UNGUJA

### Taarifa ya Mapato

Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,806,950,622 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,308,295,259.7 zilikusanywa sawa na asilimia 72 ya makadirio.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikupatiwa majibu kuhusiana na Taarifa ya Mapato siku mbili kabla ya kikao na Kamati kama inavyoelekezwa na Kanuni zetu za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020. Hivyo, Kamati ilielekeza majibu hayo yawasilishwe kwa Katibu wa Kamati lakini hadi Kamati yetu inawasilisha taarifa hii, hakuna majiu yaliyowasiishwa.

### Taarifa ya Matumizi

Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,806,950,622 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,263,438,297 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 59.2 ya makadirio.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikupatiwa majibu kuhusiana na Taarifa ya Mapato siku mbili kabla ya kikao na Kamati kama inavyoelekezwa na Kanuni zetu za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020. Hivyo, Kamati ilielekeza majibu hayo yawasilishwe kwa Katibu wa Kamati lakini hadi Kamati yetu inawasilisha taarifa hii, hakuna majiu yaliyowasiishwa.

### Hoja nambari 6.7.5.1: Kutokuainishwa kwa mapato yatokanayo na Ofisi ya Pemba katika taarifa za fedha za mwisho wa mwaka shilingi 129,635,679

Ukaguzi umepitia taarifa za fedha za mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 pamoja na taarifa za benki zinazoonesha mapokezi ya mapato yote ya Wakala wa Dawa na Vipodozi Zanzibar kwa upande wa Unguja na Pemba na kubaini kutokuainishwa kwa mapato ya Ofisi ya Pemba katika taarifa ya fedha ya mwisho wa mwaka iliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kutotoa sura halisi ya mapato yaliyokusanywa na Wakala kwa mwaka husika. Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kujumuisha mapato yote yanayokusanywa na Wakala katika taarifa za fedha za mwisho wa mwaka

**Majibu ya Wakala**

Hii ilitokana na Agizo kutoka Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 bajeti ya Unguja na Pemba ziwe tofauti hivyo kiasi cha shilingi 129,635,679 ziliwekwa tofauti kwa lengo la kuonekana kwa Uwazi Bajeti ya Pemba, Hata hivyo ushauri huo tumeupokea na tumeanza kuufanyia kazi kwenye majumuisho ya hesabu kuu ili kuleta ufanisi

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Watendaji wa Wakala kukubaliana na hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati ya PAC ilitaka kujua kama kuna kielelezo chochote kitakachothibitisha majibu yao na kujibiwa kwamba hawakuwa na kielelezo hicho. Hivyo Kamati ya PAC haikukubaliana na majibu hayo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala unapotekeleza majukumu yake ya maagizo, uhakikishe inakuwa na kielelezo ili atakapokuja Mkaguzi waweze kumuonesha.

**Hoja nambari 6.7.5.2: Kuwepo kwa tofauti ya taarifa za Mapato zilizoainishwa katika taarifa za fedha ya shilingi 74,056,000**

Ukaguzi umepitia taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 iliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar na kubaini kuwepo kwa tofauti ya fedha zilizoripotiwa katika taarifa ya mapato na matumizi (Statement of Receipts and Payments) na taarifa ya Mapato (Statement of Revenue). Kutokukubaliana kwa taarifa hizo hakutoi sura sahihi na halisi juu ya mapato yaliyokusanywa kwa mwaka husika. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 165: Taarifa za ukusanyaji wa Mapato zilizoainishwa katika taarifa za fedha za mwisho wa mwaka**

| Vifungu (Mapato ya Ndani) | Mwaka wa fedha 2020/2021 | |
|---|---|---|
| | Makadirio (Tshs) | Kilichokusanywa (shs) |
| Importation Of Drug/Medical Devices 1422039 (2%) | 199,609,000 | 212,528,750 |
| Importation Of Cosmetics 1422039 (1%) | 30,850,000 | 11,650,000 |
| Importation Of Food 1422039 (0.5%) | 897,513,129 | 624,410,025.27 |
| Registration Of Food (1422025 (Food) | 435,815,500 | 315,825,470 |
| Registration Of Drug/Cosmetics 1422025 (Drug/Cosmetics) | 184,949,000 | 160,973,500 |
| 1422025 GMP | 200,550,000 | 30,290,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **1,355,677,745** |
| Sub Office - Pemba | 174,991,500 | 102,287,779 |
| Jumla Kuu (Statement of Revenue) iliyopo katika Taarifa yahesabu | **2,124,278,129** | **1,457,965,524** |
| Non Tax Revenue (Mapato yaliyoainishwa katika taarifa ya fedha ya mwisho wamwaka (Statement of Receipts and Payments) | **2,124,278,129** | **1,383,906,524.27** |
| **Tofauti** | | **74,059,000** |

Kuwepo kwa tofauti hiyo kumepelekea taarifa ya fedha kutokuwa na usahihi na kutoleta sura halisi ya mapato yaliyoripotiwa. Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar juu ya kuweka umakini wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka ili kutoa taarifa sahihi na zenye kuleta uhalisia wa mapato yaliyokusanywa.

## Majibu ya Wakala

ZFDA iliweza kukusanya kiasi cha fedha shilingi 1,457,965,524 badala yake ilionekana kimakosa ya kiuandishi kama inavyosomeka1,383,906,524.27. Hata hivyo hoja hii pamoja na mapendekezo yake yamepokelewa na tayari tumeyafanyia kazi.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Watendaji wa Wakala kukubaliana na hoja ya Mkaguzi ya kufanya makosa katika taarifa zao za hesabu za mwisho wa mwaka. Hata hivyo, Kamati yetu ilitaka kujua sababu ya kutokea tofauti ya hesabu iliyobainika na kuelezwa kwamba Wakala ulikuwa na watendaji wachache katika kitango cha hesabu ambapo kulipelekea kutopitia vizuri hesabu zao. Kamati imebaini kwamba tofauti ya shilingi 74,000,000 ilisababishwa na Watendaji wa Wakala kugundua kasoro iliyojitokeza lakini walichelewa kurekebisha kasoro hiyo kwani waliwasilisha majibu kwa Mdhibiti tarehe 31/3/2022, wakati ambao ripoti ya Mdhibiti ilikuwa katika hatua ya maandalizi ya mwisho ya kuchapishwa. Kamati haikuridhishwa na majibu na kuungana na hoja ya Mdhibiti.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Watendaji wa Wakala wahakikishe wanawasilisha majibu ya hoja za awali zinazowasilishwa na Mdhibiti mapema ili kasoro zisiweze kujitokeze katika ripoti husika.
2. Watendaji wa Wakala wawe na utaratibu mzuri wa kuandaa na kuhifadhi kumbukumbu zao vizuri hususan muda anaokuja Mdhibiti kufanya ‘verification’ ya majibu yao ili kuthibitisha kama kawakuchelewa kuwasilisha majibu yao.

### Hoja nambari 6.7.5.3: Kukosekana kwa taarifa za “Ledger” za kila kifungu cha Hesabu

Kitengo cha Uhasibu kina jukumu la kuandaa na kuweka kumbukumbu za taarifa zote za fedha zinahusiana na mapato na matumizi kwa usahihi ili kuweza kuandaa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka zinazoendana na taratibu na miongozo inayotolewa na Taasisi za ndani na zile za kimataifa (International Accounting Standard) juu ya usahihi wa uandaaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka.

Katika kupitia taarifa mbali mbali za fedha ukaguzi umebaini kuwa kitengo cha uhasibu hakikuandaa taarifa za kila kifungu “Ledger” ili kurahisisha kuandaliwa kwa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka zilizoendana na taratibu na miongozo inayotolewa na taasisi za ndani na za kimataifa. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na taratibu na miongozo ya uandaaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka inayotolewa na Taasisi za ndani na zile Kimataifa (International Accounting Standard).

Kutoandaa General Ledger kutapelekea kushindwa kulinganisha taarifa za kibenki na matumizi halisi yaliyotumika. Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na

Vipodozi Zanzibar kuchukua juhudi ya kuandaa taarifa zote za kifedha kwa mujibu wa Sheria.

Licha ya Watendaji wa Wakala kukiri hoja ya Mdhibiti. Hata hivyo, Kamati yetu imebaini kuwa hali hiyo ilitokana na upungufu wa watendaji wa kitengo cha fedha kwani wakati huo, kulikuwa na Mhasibu pekee hakuwa na Wasaidizi. Hivi sasa, kasoro hiyo imerekebishwa na tayari Wakala imeshaongeza Mhasibu Msaidizi na Mshika fedha na taarifa husika tayari zimeshaingizwa katika 'general ledger'. Kamati imeridhika na majibu ya Wakala na Kamati haikuwa na hoja zaidi.

**Majibu ya Wakala**

1)Mapungufu hayo yamejitokeza kutokana na sababu zifuatazo 1)Kukosena kwa mfumo wa fedha kwa wakati huo.

2) Uhaba wa watendaji katika kitengo cha Fedha kulikopelekea kushindwa utekelezaji majukumu yote kwa wakati. Hata hivyo Taasisi tayari imeongeza msaidizi mhasibu na mshika fedha pamoja na matumizi ya mfumo wa fedha ambao utasaidia kuweka taarifa vizuri.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wakala wamekubaliana na hoja Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati iliuliza ni sababu gani iliyopelekea jambo hilo kutokea na kuelezwa kwamba wakati Mkaguzi anafanya kazi zake Wakala, kulikuwa na upungufu mkubwa wa Wafanyakazi wa Kitengo cha Uhasibu na kupelekea kuzongwa na majukumu. Hivi sasa kasoro hiyo haitojitokeza tena kwa vile tayari Wakala umeshaajiri Mssaidizi wa Mhasibu na Mshika fedha. Hivyo, Kamati imeridhika na majibu hayo.

**Hoja nambari 6.7.5.4: Dosari katika ukusanyaji wa Mapato**

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari katika ukusanyaji wa mapato pamoja na uwekaji wa kumbukumbu za taarifa ya mapato yaliyokusanywa, dosari hizo ni kutokuwepo kwa uwiano kati ya fedha zilizokusanywa kupitia stakabadhi za mapato na fedha zilizorikodiwa katika daftari la kuweka kumbukumbu za mapato. Mchanganuo wa dosari hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatayo:-

**Jadweli Nambari 166: Tofauti ya taarifa za stakabadhi na daftari la kuhifadhi kumbukumbu za mapato**

| Tarehe | Stakabadhi Namba | Mlipaji | Fedha zilizorikodiwa kwenye Stakabadhi (Tshs.) | Fedha zilizorikodiwa kwenye Daftari la kumbukumbu za mapato (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) |
|---|---|---|---:|---:|---:|
| 14/10/2020 | 12353 | Kigongo | 18,000 | 13,000 | (5,000) |
| 17/10/2020 | 12355 | Rashid Dosa | 44,000 | 40,000 | (4,000) |
| 17/10/2020 | 12356 | Senga | 20,000 | 24,0000 | (4,000) |
| 25/10/2020 | 12363 | Rashid Dosa | 34,000 | 30,000 | (4,000) |
| 26/10/2020 | 12364 | Makame Kasa | 8,000 | 4,000 | (4,000) |
| 16/10/2020 | 12365 | Nahoda Makame | 18,000 | 13,000 | (5,000) |
| 07/12/2020 | 12372 | Makame Kasa | 18,000 | 13,000 | (5,000) |
| 09/11/2020 | 12374 | Denge | 34,000 | 30,000 | (4,000) |
| 10/11/2020 | 12375 | Rashid Dosa | 28,000 | 25,000 | (3,000) |
| 10/11/2020 | 12376 | Hamad Khalfani | 28,000 | 25,000 | (3,000) |
| 27/12/2020 | 13724 | Abuubakar Ali | 18,000 | 14,000 | (4,000) |
| 14/12/2020 | 12430 | Suleiman Nassor | 10,000 | 16,000 | 6,000 |
| 31/05/2021 | 16581 | Mohammed Said | 26,000 | 25,000 | (1,000) |
| 15/12/2020 | 13601 | Mahmoud Juma | 2,000 | 7,000 | 5,000 |
| 13/07/2020 | 08867 | Royal Cosmetics | 400,000 | 44,000 | (356,000) |
| 13/07/2020 | 08868 | Kauthar Sea Food | 558,900 | 585,000 | (26,100) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Limited | | | |
| 16/07/2020 | 08892 | BF Suma Limited | 95,000 | 75,000 | (20,000) |
| 4/8/2020 | 10184 | C.tren | 95,000 | 5,000 | (90,000) |
| 20/8/2020 | 10459 | Jabu Ali Suleiman | 75,000 | 95,000 | 20,000 |
| 26/8/2020 | 10493 | The medi life co.ltd | 95,000 | 15,000 | (80,000) |
| 14/9/2020 | 10427 | Scotch store | 431,517 | 44,343 | (387,174) |
| 19/9/2020 | 10659 | Mahmoud Juma | 4,000 | 8,000 | 4,000 |
| **Jumla** | | | | | **(970,274)** |

Kufanya hivyo kunapelekea upotevu wa Mapato ya Serikali pamoja na kutojua usahihi wa mapato yaliyopokelewa jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu namba 23(4) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuchukuwa jitihada za udhibiti wa mapato katika maeneo ya machinjio kwa kutumia risiti ya kimtandao (EFD) ili kurahisishwa udhibiti wa mapato hayo kwani ukusanyaji wake ni wa muda wa usiku.

**Majibu ya Wakala**

Dosari hii ilitokana na kukosekana kwa mfumo wa utoaji  stakabadhi kwa njia ya ki eletroniki, hata hivyo Ofisi ishatafuta mashine za Mfumo wa malipo kimtandao (PoS) kwa kuondoa tatizo la ukusanyaji mapato katika machinjio, bandarini na Uwanja wa ndege.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Wakala kukiri kwamba kulikuwa na tofauti ya taarifa za stakabadhi na daftari la kuhifadhi kumbukumbu za mapato. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba makusanyo kwenye machinjio yalikuwa hayakusanywi na Watendaji wenye uweledi badala yake Wakaguzi waliopo machinjioni ndio walikuwa wakitumika kufanya

kazi hiyo.

Mbali na hilo, Kamati ya PAC ilikwenda ndani zaidi na kugundua kwamba baadhi ya Watendaji wa Wakala waliokuwa wanajihusisha na Makusanyo ya mapato walikuwa na wakifanya ubadhirifu na mali za umma kwani walikuwa wakikusanya na walichokikusanya kilikuwa hakifiki Serikalini kama kilivyo badala yake kilikuwa kinachotwa na kwenda mfukoni mwa wakusanyaji. Kamati ya PAC haikuridhishwa na upotevu wa fedha hizo kwani hata kama itapotea shilingi kumi ya Serikali basi thamani ya upotevu wake huwezi kuuthainisha na kitu chengine.

Kwasasa kasoro hiyo imesharekebishwa kwa vile Wakala unafanya makusanyo kwa kutumia Mfumo. Kwa vile kasoro imesharekebishwa, Kamati imeridhika na majibu hayo na haikuwa na maelezo zaidi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile kuna upotevu wa fedha za umma zimepotezwa kutokana na uzembe uliofanywa na baadhi ya Wafanyakazi wa Wakala, ni vyema vyombo vya uchunguzi kikiwemo ZAECA kulifuatilia kwa karibu suala hili ili kama kuna Mtendaji au Mtu yeyote anahusika basi hatua za kisheria zichukuliwa dhidi yao.

**Hoja nambari 6.7.5.5: Ucheleweshaji wa upelekaji wa Mapato benki shilingi 18,085,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna ucheleweshaji mkubwa wa uwasilishwaji wa mapato yanayokusanywa na Wakala katika Maeneo ya Machinjio ambapo mapato hayo yanakusanywa na Afisa Afya kutoka Wakala na kuwasilisha kwa Muhasibu kwa ajili ya kupelekwa benki.

Aidha, Ukaguzi umeshindwa kujiridhisha juu ya muda na usahihi wa mapato yanayopokelewa na kupelekwa benki kama yanavyokusanywa kutoka vituoni, hii ni kutokana na kutokuwepo kwa taarifa sahihi za upokeaji na upelekaji wa mapato hayo Benki.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za

Umma ya mwaka 2016. Mapato yenyewe ni kama yanavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 167: Baadhi ya Mapato ambayo yamecheleweshwa kupelekwa benki**

| Tarehe ya Makusanyo | Risiti Namba | Thamani (Shs) |
|---|---|---|
| 05/08/2020 – 17/08/2020 | 10301 – 10321 | 238,000 |
| 18/08/2020 – 31/08/2020 | 10322 – 10341 | 338,000 |
| 01/09/2020 – 13/09/2020 | 10342 – 10350 | 392,000 |
| 15/12/2020 – 31/12/2020 | 13601 – 13614 | 22,000 |
| 31/12/2020 | 13615 | 12,000 |
| 8/1/2021 – 15/1/2021 | 13616 - 13625 | 20,000 |
| 25/1/2021 - 31/1/2020 | 13626 – 13631 | 12,000 |
| 31/1/2021 -31/1/2021 | 13632 - 13637 | 26,000 |
| 9/2/2021 - 14/2/2021 | 13638 - 13646 | 30,000 |
| 19/2/2021 - 28/2/2021 | 13647 - 13650 | 24,0000 |
| 7/2/2021 - 28/2/2021 | 15701 - 15722 | 338,000 |
| 1/3/2021 - 8/3/2021 | 15723 - 15730 | 150,000 |
| 9/3/2021 - 28/3/2021 | 15731 -15750 | 322,000 |
| 13/6/2021 - 24/3/2021 | 16651 -16671 | 403,000 |
| 25/6/2021 - 6/7/2021 | 16672 - 16693 | 434,000 |
| 16/12021 - 29/1/2021 | 15601 - 15618 | 537,000 |
| 30/1/2021 - 12/2/2021 | 15619 - 15642 | 550,000 |
| 13/2/2021 - 19/2/2021 | 15643 15650 | 324,000 |
| 17/12/2020 - 30/12/2020 | 13651 - 13663 | 278,000 |
| 2/1/2021 - 8/1/2021 | 13664 - 13671 | 186,000 |
| 9/1/2021 - 24/1/2021 | 13672 -13687 | 306,000 |
| 28/1/2021 - 31/1/2021 | 13688 - 13694 | 136,000 |
| 31/1/2021 - 6/2 /2021 | 13695 - 13700 | 118,000 |
| 18/8/2020 - 18/8/2020 | 09051 - 09061 | 204,000 |
| 25/8/2020 - 25/8/2020 | 09062 - 09069 | 252,000 |
| 31/8/2020 - 31/8/2020 | 09070 - 09077 | 220,000 |
| 3/9/2020 - 7/9/2020 | 09078 - 09087 | 304,000 |
| 14/9/2020 - 14/9/2020 | 09088 - 09096 | 260,000 |
| 16/9/2020 - 16/9/2020 | 09097 - 09099 | 38,000 |
| 6/1/2021 | 15501 | 70,000 |
| 7/1/2021 - 11/1/2021 | 15502 - 15505 | 140,000 |
| 13/1/2021 - 15/1/2021 | 15506 - 15509 | 120,000 |
| 16/1/2021 - 21/1/2021 | 15510 - 15515 | 195,000 |
| 21/1/2021 - 29/1/2021 | 15516 - 15521 | 224,0000 |
| 30/1/2021 - 31/1/2021 | 15522 - 15523 | 104,000 |
| 2/2/2021 - 3/2/2021 | 15524 – 15525 | 136,000 |
| 4/2/2021 - 10/2/2021 | 15526 -15531 | 242,000 |
| 11/2/2021 - 19/2/2021 | 15532 - 15540 | 356,000 |
| 20/2/2021 - 23/2/2021 | 15541 - 15544 | 98,000 |
| 24/2/2021 - 25/2/2021 | 15545 - 15549 | 228,000 |
| 1/3/2021 | 15550 | 50,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 21/10/2020 - 31/10 /2020 | 12451 - 12457 | 264,000 |
| 2/11/2020 - 3/11/2020 | 12458 - 12461 | 210,000 |
| 13/11/2020 - 13/11/2020 | 12462 -12466 | 156,000 |
| 23/11/2020 - 23/11/2020 | 12467 - 12470 | 256,000 |
| 28/11/2020 - 23/11/2020 | 12471 - 12473 | 264,000 |
| 29/11/2020 - 2/12/2020 | 12474 - 12477 | 110,000 |
| 3/12/2020 - 6/12/2020 | 12478 - 12481 | 222,000 |
| 12/12/ 2020 - 14/12/2020 | 12482 -12485 | 258,000 |
| 16/12/2020 - 24/12/2020 | 12486 - 12490 | 308,000 |
| 23/12/2020 - 29/12/2020 | 12491 - 12495 | 292,000 |
| 30/12/2020 - 5/1/2021 | 12496 - 12500 | 212,000 |
| 24/4/2021 - 29/1/2021 | 16501 - 1604 | 238,000 |
| 30/4/2021 - 10/5/2021 | 1605 - 16515 | 656,000 |
| 11/5/2021 - 12/5/2021 | 16116 - 16517 | 360,000 |
| 13/5/2021 – 17/5/2021 | 16518 - 16522 | 398,000 |
| 18/5/2021 - 23/5/2021 | 16523 - 16529 | 130,000 |
| 24/5/2021 - 1/6/2021 | 16539 - 15638 | 431,000 |
| 2/6/2021 - 8/6/2021 | 16538 - 16544 | 410,000 |
| 9/6/2021 - 10/6/2021 | 16545 - 16546 | 80,000 |
| 11/6/2021 - 14/6/2021 | 16547 - 16550 | 240,000 |
| 15/6/2021 - 18/6/2021 | 16751 - 16755 | 218,000 |
| 12/6/2021 – 28/6/2021 | 16756 - 16766 | 406,000 |
| 29/6/2021 - 30/6/2021 | 16767 - 16768 | 94,000 |
| 3/11/2020 - 16/11/2020 | 12051 - 12520 | 372,000 |
| 17/11/2020 - 3/12/2020 | 12521 - 12537 | 446,000 |
| 4/12/2020 - 17/12/2020 | 12538 - 12550 | 385,000 |
| Jumla | | 18,085,000 |

Ucheleweshwaji wa mapato kupelekwa benki kwa wakati kunapelekea kujitokeza viashiria vya upotevu wa mapato ambapo mapato hayo yanaweza kutumika kinyume na utaratibu na kupelekea kuitia hasara Serikali. Ukaguzi unashauri uongozi ni vyema kwa Idara husika kuhakikisha kwa mapato yote yanakusanywa na kwa wakati na kuwasilishwa benki katika muda muafaka ili kuepusha upotevu wa rasilimali hiyo.

**Majibu ya Wakala**

Tatizo hili limetokana na fedha zilizokusanywa machinjioni zilikuwa zikiletwaOfisini kwa kuandaliwa controll number kwa pamoja kisha zinapelekwa benki, Hata hivyo tatizo hilo limetatuliwa kwamatumizi ya PoS.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa hoja hii inatokana na hoja nambari 6.7.5.4 kwa vile makusanyo katika machinjio yalikuwa yakichelewa kuwasilishwa benki kutokana na Wakusanyaji iliwalazimu wawasilishe makusanyo hayo Ofisini ndio ichukuliwe hatua ya kupatiwa 'control number' na ndio kuwasilishwa Benki. Hivi sasa Wafanyabiashara wanalipa moja kwa moja kupitia mfumo. Kamati ya PAC ilipata muda wa kuupitia mfumo wa malipo na kubaini yafuatayo:-

1. Wafanyabiashara wengi waliopewa 'control number' Pemba hawajafanya malipo.
2. Mfumo una uwezo wa kuonesha wafanyabiashara waliolipa kupitia 'control number' walizopatiwa na Wakala.
3. 'Control number' zinazotolewa zinadumu kwa siku saba na zikimaliza inakuwa haifanyi kazi na iwapo mfanyabiashara halipia, anabakia na deni lake tu atakuwa anadaiwa.
4. Mfumo una changamoto ya kumpata mteja aliyeshindwa kulipa kupitia 'control number' mpaka atakapotaka tena huduma ndio Wakala haumpatii huduma mpaka alipe deni lake linaoonekana katika mtandao

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wakala ifuatilie zaidi kutafuta machinjio yaliyokuwa hayajasajiliwa kwa kukaa na Masheha wa maeneo tofauti kwani Kamati imesisitiza bado yapo machinjio yaliyokuwa hayajasajiliwa yanayofanyika katika maeneo yasiyokuwa rasmi ili iweze kujiongezea mapato.
2. Watendaji wa Wakala ambao wanakusanya mapato, wasikae na fedha za makusanyo kwa muda mrefu.

**Hoja nambari 6.7.5.6: Kukosekana kwa ripoti za mapato za kila mwezi**

Kitengo cha Uhasibu kina jukumu la kuandaa ripoti za kila mwezi za makusanyo ya mapato ili kuweza kulinganisha taarifa za hesabu hizo na makusanyo yanayopelekwa

benki kwa lengo la kuweka kumbukumbu za fedha na kuziwasilisha Hazina ya Serikali kama zitakavyohitajika. Kutofanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 34(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Kutoandaa taarifa za mapato ya kila mwezi kunapelekea kushindwa kulinganisha taarifa za usuluhisho wa kibenki na mapato yaliyorikodiwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha husika.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuchukuwa juhudi za kuandaa ripoti za makusanyo ya kila mwezi kwa lengo la kuweka kumbukumbu za mapato ili kupata ufanisi na uwajibikaji mzuri.

**Majibu ya Wakala**

Uandaaji wa ripoti za mapato unafanyika kila mwezi na ripoti hizo zipo na tayari kwa ukaguzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa ni kweli Wakala haukuandaa ripoti ya mapato ya kila mwezi. Hali hiyo ilisababishwa na kutokuwa na Watendaji wa kutosha wa kitengo cha Uhasibu kwani kulikuwa na Muhasibu pekee ambae alikuwa amezidiwa na majukumu. Hivi sasa kasoro hiyo imesharekebishwa kwa kuongeza Watendaji pamoja na kuwepo kwa mfumo wa kieletroniki. Kwa vile hakukuwa na upotevu wowote wa fedha za umma, Kamati yetu imeridhika na majibu hayo.

**Hoja nambari 6.7.5.7: Kuwepo kwa mapato yaliyopokelewa nje ya Mfumo wa kieletroniki (Control Number) wa Ukusanyaji wa Mapato ya shilingi 110,961,814.27**

Ukaguzi umepitia taarifa za ukusanyaji wa Mapato kwa mwaka 2020/2021 kupitia

Mfumo wa kieletroniki wa upokeaji wa mapato (Control Number) unaotumiwa na Wakala wa Dawa na Vipodozi Zanzibar na kubaini kuwepo kwa jumla ya mapato ya shilingi 1,272,944,710 yaliyokusanywa kupitia mfumo huo.

Aidha ,ukaguzi umepitia taarifa za fedha za mwisho wa mwaka na kubaini kuwepo kwa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani yenye jumla ya shilingi 1,383,906,524.27 ambapo zinafanya kuwepo na tofauti ya shilingi 110,961,814.27 ukilinganisha na kiasi kilichopokelewa kupitia mfumo wa kieletroniki. Hata hivyo ukaguzi umebaini mapato ya shilingi 1,272,944,710 yalipaswa kurikodiwa kwenye vitabu vya kumbukumbu kwa lengo la kurahisisha usuluhisho wa kibenki jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika jambo hilo halikufanyika.

Ukaguzi umeshindwa kujiridhisha juu ya usahihi wa mapato hayo kutokana na kutokuwepo kwa usuluhishi (Reconciliation) baina ya mfumo wa kieletroniki na mfumo wa kawaida ambapo bado unaendelea kutumika licha ya kuwepo kwa mfumo wa kieletroniki. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea upotevu wa mapato kwani Mfumo wa kieletroniki bado haufanyi kazi kama inavyotakiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuchukuwa jitihada za kutoa elimu kwa wafanyabishara na wajasiriamali kufanya malipo kwa kutumia mfumo wa elektroniki (Control Number) ili kuepuka kufanya malipo nje ya mfumo jambo ambalo linapelekea kutokujuulikana kima halisi cha fedha kilichopokewa na kinachoripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

**Majibu ya Wakala**

Hili lilitokana kwa sababu zifuatazo:

1) Ofisi ndogo za ZFDA Pemba kushindwa kwenda sambamba na mfumo wa kielektroniki.

2) Benki kuendelea kupokea fedha kwa kupitisha malipo bila ya Control Number Hata hivyo changamoto zote hizo zishatatuliwa na fedha zote zinapokelewa kwa njia ya control number.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa ni kweli kulikuwepo kwa mapato yaliyopokelewa nje benki ya Mfumo wa kieletroniki jambo ambalo lilisababishwa na Mfumo kuwa katika kipindi cha mpito wa kutumia 'control number' ambapo walikuwa hawaelewi ipasavyo utaratibu wa kulipa mapato ya Wakala kwa vile wateja wengi walikuwa wanakwenda kulipa benki kupitia hesabu ya Wakala bila ya kupatiwa 'control number' na Wakala. Kwa mazingira hayo, fedha haikupotea isipokuwa kulikosekana vielelezo vya malipo. Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC imeridhika na majibu yaliyotolewa na Wakala na haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.7.5.8: Kukosekana kwa utunzaji mzuri wa taarifa za Fedha**

Katika kupitia taarifa mbali mbali za Fedha za Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi ukaguzi umebaini kuwepo na utunzaji usioridhisha wa kumbukumbu ya taarifa za fedha (Bank Slip) ambazo zimekuwa zikiwekwa bila ya utaratibu unaofaa kwa ajili ya utumiaji wa siku za mbele.

Kutokutunza vizuri kumbukumbu za malipo ya fedha kunapelekea kujitokeza kwa upotevu wa taarifa za fedha na hatimae kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi ambazo haziendani na uhalisia wa ukusanyaji wa mapato hayo. Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuchukuwa jitihada za kutosha katika kutunza vizuri taarifa za fedha ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa hizo pale zinapohitajika.

**Majibu ya Wakala**

Dosari hii ilitokana na upungufu wa watendaji katika sehemu ya fedha pamoja a kukosekana kwa mfumo wa kieltoniki wa uwekaji kumbukumbu hizo Hata hivyo taasisi imefanya juhudi za kuongeza watendaji na kurahisisha utunzaji wa kumbukumbu hizo muhimu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Watendaji wa Wakala kukiri kwamba kulikuwepo utunzaji mbaya wa kumbukumbu za Wakala. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua sababu kutokea kasor hiyo na kuelezwa kwamba Watendaji wa Kitengo cha Uhasibu walikuwa wachache. Aidha, sehemu waliyokuwa wanafanyia kazi Wahasibu na kutunza kumbukumbu zao ilikuwa ndogo ila hivi sasa Wakala una mpango wa kuwahamishia katika jengo jipya lenye nafasi ya kutosha. Baada ya kutolewa maelezo hayo, Kamati ya PAC hsikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.7.5.9: Kukosekana kwa mchanganuo wa vyanzo vya makusanyo ya mapato shilingi 1,383,906,524.27**

Katika ukaguzi uliofanyika Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar imewasilisha mapato yenye thamani ya shilingi 1,383,906,524.27 ambayo yamekusanywa kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuoneshwa mchanganuo wa mapato kwa kila chanzo kilichokusanya mapato hayo jambo ambalo limepelekea ugumu kuweza kujua na kutathmini fedha halisi iliyokusanywa kwa kila chanzo kwamba kilifikia lengo lililokusudiwa kwa mujibu wa makadirio ya ukusanyaji wa fedha katika chanzo husika.

Kushindwa kubainisha mchanganuo wa makusanyo ya fedha kwa chanzo husika kunaweza kukapelekea kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya taasisi kwa mujibu wa chanzo husika na hatimae kuwasilisha makadirio ya makusanyo ambayo hayaendani na uhalisia.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuchukuwa jitihada za kuhakikisha kuwa mapato yote yanayotokana na utoaji wa huduma mbali mbali zinazotolewa na Wakala yanarikodiwa kwa utaratibu uliowekwa wa kutofautisha huduma hizo na bei halisi.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Pamoja na Watendaji wa Wakala kukubaliana na hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati iliuliza na kuelezwa kwamba hali hiyo iisababishwa na Mfumo waiokuwa wakiutumia haukkuwa na mchanganuo huo isipokuwa kwasasa tayari Wizara ya Fedha na Mipango imeshawapatia 'GFS CODE' ya kila chanzo ambapo makusanyo yanaonekana kiuwazi. Kamati imegundua hakukuwa na fedha iliyopotea au kuchukuliwa kwani fedha hizo zilikuwa zimejumuishwa katika vyanzo vyengine. Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC haikuwa na maelezo ya ziada.

**Majibu ya Wakala**

ZFDA ilikua ikikusanya mapato yake katika kazi zake kuu bila ya kuwa na GFS Code na kupelekea ugumu wa kutambua vyanzo vya mapato. Hata hivyo Makusanyo hayo yametatuliwa na Ofisi ya Raisi Fedha na Mipango kwa kuandaa GFS Code kwa kila chanzo cha mapato ya ZFDA.

**Hoja nambari 6.7.5.10: Kukosekana kwa Mkataba wa ununuzi wa mafuta (Framework Contract) wenye jumla ya shilingi 65,070,896.**

Katika kupitia hati za malipo pamoja na taarifa mbali mbali za utendaji wa Wakala, Ukaguzi umebaini ya kwamba Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar wananunua mafuta kutoka kwa UNITED GROUP LIMITED kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kila siku za Ofisi bila ya kuwa na makubaliano ya kisheria (Mkataba), kufanya manunuzi katika taasisi za serikali bila ya kuwa na makubaliano ya kisheria ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(m) na kifungu nambari 42(2)(b) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama yanavyoonekena katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 168: Malipo kwa ajili ya Ununuzi wa Mafuta

| Hati Namba | Thamani (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 02/07 ya 14/07/2020 | 3,607,000 | | |
| 28/07 ya 04/07/2020 | 3,607,000 | | |
| 20/08 ya 11/08/2020 | 3,810,000 | | |
| 11/10 ya 09/10/2020 | 1,000,000 | | |
| 40/09 ya 28/09/2020 | 2,686,600 | | |
| 32/09 ya 08/09/2020 | 3,810,000 | | |
| 36/11 ya 12/11/2020 | 2,289,700 | | |
| 60/12 ya 11/12/2020 | 3,424,400 | | |
| 64/12 ya 17/12/2020 | 1,998,596 | | |
| 72/12 ya 07/01/2020 | 3,349,600 | | |
| 45/01 ya 19/01/2021 | 3,334,600 | | |
| 28/02 ya 20/05/2021 | 3,507,200 | | |
| 23/02 ya 11/02/2021 | 3,120,400 | | |
| 47/03 ya 12/03/2021 | 4,071,500 | | |
| 65/03 ya 31/03/2021 | 4,071,500 | | |
| 54/04 ya 23/04/2021 | 4,280,800 | | |
| 50/05 ya 18/05/2021 | 4,343,000 | | |
| 39/06 ya 02/06/2021 | 4,323,000 | United Group Limited | Ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Afisi |
| 53/06 ya 22/06/2021 | 4,436,000 | | |
| **Jumla** | **65,070,896** | | |

Kukosekana kwa mkataba wa ununuzi wa mafuta kunaweza kuapelekea kuathiri shughuli za Wakala endapo kutatokezea kutofautiana baina ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar na watoa huduma hizo muhimu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuandaa mkataba kwa ajili ya kuepuka migogoro endapo ikijitokeza ili kuweka usawa pande zote mbili kati yao.

**Majibu ya Wakala**

ZFDA ilikuwa ikinunua mafuta moja kwa moja (direct procurement) kwa kutumia hati

inayojulikana kama Local Purchasing Order (LPO), inayosimama kama mkataba baina ya mtoa huduma na mnunuaji na kufanya malipo hayo kabla (Pre Paid), Hata hivyo ZFDA imeupokea ushauri na tayari imefunga Mkataba na United Petroleum Limited.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa Wakala ulikuwa na kasoro iliyoelezwa na Mkaguzi kwani walikuwa wanatumia mafuta na mwisho wa mwezi walikuwa wanalipa. Kamati imeisisitiza Wakala kwamba kununua kwa thamani ndogo (Minor value) isiyohitaji zabuni sio kama Mkataba hauhitajiki.

Hata hivyo, Kamati imedhibitisha kwamba kasoro hiyo imefanyiwa kazi na Wakala na kwasasa Mkataba wa ununuzi wa mafuta upo uliofungwa na Wakala na 'United Group Limited' wa tarehe 5/8/2022. Kwa vile hoja hiyo imechukuliwa hatua, Kamati imeridhishwa na majibu.

**Hoja nambari 6.7.5.11: Kugawanywa kwa manunuzi ya vifaa vya Maabara yenye jumla ya shilingi 54,576,240**

Kifungu nambari 42(2)(c) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa mali za Umma kinakataza kugawanywa kwa Manunuzi kwa lengo la kutotumia utaratibu wa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma. Ukaguzi umepitia hati mbali mbali za malipo yaliyofanywa na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar na kubaini kuwepo kwa ununuzi wa vifaa vya maabara ambapo ununuzi wa vifaa hivyo haukutumia utaratibu wa ununuzi uliowekwa kisheria.

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi amekuwa akifanya manunuzi mbali mbali yaliyokiuka kifungu namba 57(1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021 inayokataza kugawanywa kwa manunuzi. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 169: Ununuzi wa Vifaa vya Maabara**

| Hati Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 16/10 ya 09/10/2020 | 5,129,050 | Lab Equip Ltd | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara navitendanishi |
| 14/09 ya 15/09/2020 | 1,050,000 | | |
| 26/11 ya 25/11/2020 | 2,442,450 | | |
| 65/12 ya 17/12/2020 | 5,000,000 | | |
| 26/02 ya 16/02/2021 | 2,151,490 | | |
| 27/02 ya 16/02/2021 | 2,280,000 | | |
| 51/04 ya 12/04/2021 | 5,600,000 | | |
| 61/05 ya 27/05/2021 | 5,923,250 | | |
| 41/03 ya 02/03/2021 | 20,000,000 | Indepth Scientific CompanyLimited | |
| 48/06 ya 28/06/2021 | 5,000,000 | | |
| **Jumla** | **54,576,240** | | |

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 57(1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021. Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kufuata na kutekeleza kikamilifu sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa mali za umma pamoja na kanuni zake.

**Majibu ya Wakala**

Hoja hii ilitokana na sababu zifuatazo:-

1.Maelekezo ya Serikali ya kutaka kuondoa mrundikano wa makontena bandarini hali iliyopelekea taasisikununua media,Kemikali na vitendanishi kwa ajili ya uchunguzi wa bidhaa hizo kabla hazijamfikia mtumiaji.

2. Upatikanaji wa vifaa vya msaada kutoka Global Fund na TANIPAC ililazimu ofisi

kunuua  kemikali  na vitendanishi kwa ajili ya ufungaji na majaribio ya vifaa hivyo.

3. Changamoto yaupatikanaji wa msambazaji mmoja kwakila mahitaji ya vifaa vya aina zote vya Maabara.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile kulikuwa na Agizo kutoka Baraza la Mapinduzi ambapo Kamati imejiridhisha na hilo. Hivyo Kamati haikuwa na maelezo zaidi.

**Hoja nambari 6.7.5.12: Kukosekana kwa Muongozo wa ulipaji wa Posho kwa wanafunzi wanaofanya kazi kwa vitendo shilingi 55,540,000**

Ukaguzi umepitia ripoti na taarifa za utekelezaji, hati za malipo na kubaini jumla ya shilingi 350,000 hutumika kulipa malipo ya posho kwa mwezi kwa kila mwanafunzi anayefanya kazi kwa vitendo (Internship) katika Taasisi ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi bila ya kuwepo kwa muongozo unaoruhusu ulipaji wa posho hilo.

Ulipwaji wa posho bila ya kuwepo kwa muongozo wa malipo hayo kunaweza kukapelekea matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kujitokeza udanganyifu wa malipo hayo kwa kisingizio cha malipo ya wanafunzi wanaofanya kazi za vitendo (Intenship). Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

**Jadweli Nambari 170: Hati za malipo zilizolipwa posho kwa wanafunzi wanaofanya kazi kwa vitendo**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 30/09 ya 30/09/2020 | 0054 | 9,100,000 | | |
| 16/11 ya 18/11/2020 | 0085 | 7,350,000 | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 01/12 ya 02/12/2020 | 0098 | 8,050,000 | Zanzibar Food And Drugs Agency | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho kwa wanafunzi wa intenship. |
| 49/12 ya 30/12/2020 | 0138 | 8,400,000 | | |
| 11/2 ya 11/2/2021 | 0183 | 4,200,000 | | |
| 01/03 ya 01/03/2021 | 0189 | 8,550,000 | | |
| 15/04 ya 12/04/2021 | 0230 | 4,900,000 | | |
| 37/05 ya 31/05/2021 | 0271 | 4,900,000 | | |
| **Jumla** | | **55,450,000** | | |

Kutokuwepo kwa muongozo huo kunapelekea kufanyika kwa matumizi ambayo siyo sahihi. Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kufuata Sheria, Kanuni, Miongozo na taratibu zilizopo katika kutekeleza majukumu yake ili kuleta ufanisi wa utendaji wa kazi.

**Majibu ya Wakala**

Kwa mujibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi 2/06 na marekebisho yake Sheria nambari 3/17 udhibiti wa bidhaa na wataalam wa kada ya Dawa upo chini ya ZFDA, muongozo wamalipo ya wafamasia watarajali (Intenship) tayari umetayarishwa na unatumika. Hata hivyo kuanzia mkupuo wa Januari 2023 malipo ya watarajali wa Pharmacy yatafanywa kupitia Wizara ya Afya

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilitaka kujua wanafunzi hao wanalipwa kiasi gani kila mmoja kwa mwezi na kuelezwa kwamba mpango uliopo unawalipa shilingi 20,400,000 kwa mwezi ambapo jumla yao walikuwepo wanafunzi 13. Kamati imebaini hakukuwa na muongozo wa kiutumishi juu ya ulipwaji huo kama ilivyoelezwa na Mkaguzi. Kamati imeridhika na majibu hayo kwani muongozo wanaoutumia ni miongoni mwa miongozo inayotumika na Taasisi zote ulimwenguni zenye maumbile ya aina moja na Wakala huu.

**WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI - PEMBA**

**Hoja Nambari 6.7.5.13: Kutokuwepo kwa ghala la kuhifadhia bidhaa zilizokamatwa.**

Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Pemba ina jukumu la kufanya ukaguzi wa Chakula, Dawa na Vipodozi na kukamata bidhaa ambazo zimepitiwa na muda, zimeharibika au zilizokua hazifai kwa matumizi ya binaadamu pamoja na bidhaa ambazo hazijasajiliwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa ghala la kuhifadhia bidhaa hizo. Hali hii inapelekea baadhi ya bidhaa za vyakula, vipodozi na dawa zilizokamatwa kuhifadhiwa sehemu ambazo sio sahihi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 61(5)(b)(f) cha Sheria ya uanzishwaji wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi.

**Majibu ya Wakala**

Ofisi ya Wakala wa Chakula na Dawa Pemba inatumia jengo la kukodi katika kuendesha shughuli zake, hata hivyo bado halitoshelezi, hivyo ni kweli Ofisi ya Wakala wa Chakula na Dawa Pemba ina changamoto ya ghala kama ilivyobainika katika ukaguzi, lakini kwa sasa Ofisi imepata eneo katika hospitali ya Wete ambalo lilikuwa likitumiwa na Ofisi ya Bohari kuu ya Dawa Pemba kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa zilizokamatwa ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu.

Aidha kwa mpango wa muda mrefu ZFDA ina mpango wa kujenga Ofisi zake katika maeneo ya Chamanangwe Pemba.

**Uchunguzi wa kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kuwa wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake, ni kweli Wakala ulikuwa ukihifadhi bidhaa zilizokamatwa katika sehemu isiyotosha ba isiyo salama ambayo mtu yeyote anaweza kufika na kuzichukua. Kasoro hiyo kwasasa hiyo imesharekebishwa. Aidha, Kamati imegundua bado Wakala unafakazi katika jengo la kukodi ambapo tayari wameshalipa shilingi 9,360,000 ikiwa ni malipo ya kodi kwa mwaka wote wa 2023.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauri Serikali kwamba kabla ya kufanya maamuzi ya kufanya matengenezo ya jengo linalotumiwa na Taasisi za Serikali, ni vyema ihakikishe Watendaji na vifaa vyao wanapatiwa sehemu yenye eneo la kutosha ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

**Hoja namba 6.7.5.14: Kukosekana kwa kumbukumbu za mapato yatokanayo na usajili wa machinjio.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Pemba haina kumbukumbu sahihi zinazotokana na usajili wa machinjio ambapo imepelekea kushindwa kujua idadi ya machinjio pamoja na kiwango sahihi cha mapato kilichokusanywa,hali ambayo inaweza kujenga taswira ya kutokufahamu uhalisia wa

mapato mbali mbali yatokanayo na usajili wa machinjio. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 40(1),(2) cha sheria nambari 2 ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2006, Aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha zaUmmaya mwaka 2016.

**Majibu ya Wakala**

Hili lilitokana na kusekana kwa Mfumo wa kielektroniki kukusanyia mapato, Hata hivyo, Mfumo huo tayari ushawekwa na mapato yanakusanywa na kupatikana kumbukumbu zake.

**Uchunguzi wa kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa kasoro iliyobainishwa na Mkaguzi ilitokana na kutokuwasilishwa kwa malipo ya machinjio yanayolipwa Serikali za Mitaa kwani wachinjaji hutakiwa kulipa katika Halmashauri au Mabaraza ya Miji. Fedha hutakiwa kuwasilishwa Benki na Watendaji wa Halmashauri au Mabaraza ya Miji na hatimae fedha hizo kuingizwa katika hesabu ya Wakala, jambo ambalo vielelezo vyake vilikuwa haviwasilishwi kwa Wakala.

Sambamba na hilo, Kamati ya PAC imebaini kuwa kulikuwa na uzembe uliofanywa na Watendaji wa Wakala pamoja na Serikali za Mitaa uliosababisha uwezekano mkubwa wa kupotea mapato ya Serikali jambo ambalo tayari Wakala umeshaanzisha Mfumo Maalum wa kielektroniki ambapo malipo yote yatafanywa kupitia mfumo huo ili kuepuka upotevu wa fedha za umma.

**Mapendekezo ya kamati ya PAC**

- Kamati ya PAC inasisitiza Taasisi za Serikali kutocheleweshа marejesho yatokanayo na mapato ili kuepusha upotevu wa fedha za Serikali.
- Kamati ya PAC inashauri wakala wa chakula, Dawa na Vipodozi kuwa na ushirikiano na Ofisi ya Mkaguzi kwa kuwasilisha vielelezo kwa wakati unaohitajika.

**Hoja Nambari 6.7.5.15: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 5,782,900**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 5,782,900 zimetumika kwa malipo mbali mbali ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Pemba lakini vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Unashauri uongozi wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Pemba kuhakikisha kwambamalipo yote yanayofanyika yanatakiwa kufuata utaratibu ikiwemo kuweka rikodi katika vitabu vya kumbukumbu pamoja na uwekaji wa vielelezo sahihi kulingana na malipo yaliyofanyika. Mchanganuo wa malipo yenye vielelezo pungufu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 171: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 2/07 13/07/2020 | 000195 | 120,000 | Wakala wa ChakulaDawa na Vipodozi - Pemba. | Malipo ya Fedha kwa ajili ya Malipo baada ya saa za kazi. |
| 07/09 09/09/2020 | 000210 | 250,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya Gharama za upimaji. |
| 08/09 19/09/2020 | 000210 | 630,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya Uangamizaji wa mchele. |
| 08/01 25/01/2021 | 000242 | 180,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya Kazi maalum. |
| 16/01 28/01/2021 | 000250 | 2,092,900 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya Zoezi la utekelezaji wa bidhaa ya mchele usiofaa kwa binadamu. |
| 02/02 04/02/2021 | 000253 | 600,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya Matumizi madogo madogo ya Ofisi ya ZFDA - Pemba. |
| 09/04 28/04/2021 | 000293 | 250,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya Mafunzo. |
| 15/04 30/04/2021 | 000299 | 1,660,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya uangamizaji wa mchele. |
| **Jumla** | | **5,782,900** | | |

## Majibu ya Wakala

Ulipofanyika ukaguzi, vielelezo hivyo vilikuwa pungufu kutokana na baadhi ya Watendaji kutokuwasilisha vielelezo kwa Mhasibu. Hata hivyo, kwa sasa vielelezo hivyo vipo.

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Licha ya Watendaji wa Wakala kukiri kwamba kuna vielelezo vilikuwa havijakamilika. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua ni vielelezo gani ambavyo vilipelekea hoja hii kuwepo na kuelezwa kwamba kulikosekana barua ya ruhusa inayoruhusu kufanyakazi baada ya muda wa saa za kazi.

Kamati yetu pia imebaini kwamba ZFDA ilikuwa haina muundo wake wa utumishi na kupelekea upungufu mkubwa wa wafanyakazi wanaotakiwa kufanya kazi za ukusanyaji mapato na kuwasilisha marejesho ambapo kwa mwaka huo (2020/2021) walishindwa kufanya majerejesho ya risiti za upimaji wa ardhi Chmanangwe kwani Wakala ulilazimu kuwatumia wafanyakazi wasiokuwa na fani ya uhasibu kukusanya mapato.

Kadhalika, Kamati imegundua kuwa kulijitokeza kasoro ya kuchanganywa kwa stahiki za wafanyakazi kwa vile Wakala ulikuwa ukipanga ratiba ya mwezi mzima na kuchanganya muda wa ziada ndani yake bila ya kuzingatia mtendaji alifika muda wa ziada kutekeleza kazi husika au vyenginevyo. Aidha, Wakala ulikuwa hauandiki barua ya kila mtumshi ili kuomba malipo ya muda wa ziada kufanya.

Kwasasa, Wakala unao wafanyakazi 11 ambao wanatakiwa wapitie katika sehemu zote wanazozifanyia kazi zikiwemo maghala yaliyopo Bandarini na uwanja wa ndege kwa ukaguzi.

**Mapendekezo ya kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inaitaka ZFDA kuweka muongozo maalum kwa ajili ya malipo ya wafanyakazi ambao watakuwa watapatiwa muda wa ziada wa kazi
2. Kutokana na uhaba wa wafanyakazi kamati inasisitiza ZFDA kuongeza wafanyakazi wa kutosha wenye fani mbali mbali ili kuepusha uzorotaji wa kazi

**Hoja Nambari 6.7.5.16: Ucheleweshwaji wa Upelekaji Mapato Benki shilingi 39,339,540**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 39,339,540 zimakusanywa na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi kwa kupitia vianzio vyake mbali mbali lakini mapato hayo yamechelewe shwa kupelekwa benki hali ambayo inaweza kupelekea upotevu wa fedha zilizokusanywana kushindwa kutoa huduma bora zilizokusudiwa kwa wananchi na hivyo kupelekea ukosekanaji wa tija iliyokusudiwa na Serikali Kiambatisho Nambari 8 cha Ripoti ya Mdhibiti husika kinahusika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 56(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Wakala**

Ni kweli mapato hayo yalicheleweshwa kupelekwa Bank kutokana na A/C ya ZFDA Pemba kuzuiliwa kupokea mapato katika A/C yake na mapato yote yalitakiwa kuingizwa kwenye A/C ya ZFDA Unguja kwa njia ya'Control Number'. Hivyo ilipelekea baada ya makusanyo kuomba 'Control Numbe' kutoka Unguja jambo ambalo lilichukua muda kuipata. Lakini kwa sasa Fedha zote zinazokusanywa zinalipiwa kupitia 'Control Number' zinazotolewa na ZFDA Pemba na fedha hizo zinaingia kwenye A/C ya ZFDA.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini wakati Mkaguzi anakamilsha kazi zake za ukaguzi, ni kweli Wakala ulikuwa hauwasilishi mapato benki kwa wakati. Hata hivyo, kwasasa changamoto hiyo imeondoka kutokana na makusanyo hayote yanafanyika kupitia mfumo. Kwa mnasaba huo, Kamati yetu haikuwa na maelezo zaidi.

## 6.10: WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

### 6.10.1 - FUNGU K 01 - WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 215,700,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara ilikusanya jumla ya shilingi 141,108,343 sawa na asilimia 65 ya makadirio.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Elimu imekukusanya kiwango hicho cha fedha kama ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Makusanyo hayo yamepungua kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha bajeti ya makusanyo kwa mwaka 2020-2021ambacho hakiendani na uhalisia wa makusanyo.

| Chanzo cha mapato makadirio | Makadirio Tzs | Makusanyo Tzs | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Leseni za usajili wa skuli binafsi | 15,700,000 | 91,608,840 | 79.2 |
| Leseni za walimu | 100,000,000 | 49,409,503 | 49.4 |
| **Jumla** | **15,700,000** | **141,018,343** | **65.4** |

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haina vyanzo vyake vya moja kwa moja vya makusanyo isipokuwa inategemea vyanzo vya Afisi ya Usajili wa Elimu. Kwa mantiki hiyo, vao vyao vinafanana.

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara ya Elimu ihakikishe inabuni vyanzo vyake vya mapato ili iweze kujitegemea na sio kutegemea vyanzo vya Taasisi zake.

## Taarifa ya Matumizi

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 140,080,860,441. Kati ya fedha hizo shilingi 19,267,400,000 zilikadiriwa kutumika kwa matumizi ya kawaida, shilingi 59,666,476,441 kwa ajili ya mshahara, shilingi 46,180,400,000 kwa ajili ya matumizi ya ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu na mafunzo ya Amali, shilingi 19,116,840,400 zilikadiriwa kutumika katika Taasisi zilizo chini wa Wizara kutokana na vyanzo vyao vya mapato ya ndani. Aidha Jumla ya shilingi 4,500,000,000 zilikadiriwa kutumika kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali na jumla ya shilingi 14,962,084,000 zilikadiriwa kutumika kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 129,891,236,818 zilitumika ikiwa sawa na asilimia 82.60 ya makadirio, kati ya fedha hizo shilingi 4,526,990,407 zilitumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 23.50 ya makadirio, shilingi 58,469,446,248 zilitumika kwa ajili ya mshahara sawa na asilimia 109.83 ya makadirio, shilingi 30,847,082,611 zilitumika ikiwa ni Ruzuku kwa Taasisi zilizo ndani ya Wizara ya Elimu ikiwa sawa na asilimia 66.80 ya makadirio, shilingi 19,186,564,553 zilitumika katika Taasisi zilizo chini wa Wizara kutokana na vyanzo vyao vya mapato ya ndani ikiwa sawa na asilimia 100.36 ya makadirio. Aidha, shilingi 3,509,000,000 zilitumika kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali sawa na asilimia 77.98 ya makadirio na shilingi 13,352,152,999 zilitumika kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa washirika wa maendeleo sawa na asilimia 89.24 ya makadirio.

## Majibu ya Wizara

Wizara yetu imepatiwa kiwango hicho cha fedha kwa matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo. Kiwango hicho cha fedha ni kizuri kiasi ukilinganisha na miaka ya nyuma iliopita kwa upande wa matumizi ya kawaida ilishuka kulinganisha na mwaka jana ambapo kupungua huko kulisababishwa na uwepo wa maradhi ya UVIKO - 19. Kwa kuwa kiwango hicho hakikufikia malengo yaliyopangwa maeneo yafuatayo yaliathirika kiutekelezaji wake

1. Upungufu wa upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika skuli zetu Unguja na Pemba.
2. Malipo ya mitihani ya Kidato cha Nne na Sita kwa Baraza la Mitihani la Taifa
3. Upatikanaji mdogo wa fedha za matumizi ya chakula kwa wanafunzi wanaoshi Dakhalia
4. Malimbikizo ya mishahara , nauli kwa Wafanyakazi hayakulipwa
5. Malipo baadhi ya watowa huduma hatukuweza kulipa.
6. Kutokukamilika kwa ukarabati wa Skuli ya Sekondari Haile, Chwaka Tumbe na Paje Mtule.

Kwa sasa Wizara inaridhika na uingizaji wa fedha za bajeti zilizopangwa, lakini ongezeko la fedha za makadirio ya bajeti kwa kila mwaka wa fedha hayaendani na ukuwaji wa mahitaji halisi ya shughuli za kielimu kwa Nchi yetu. Pia Wizara inaishukuru Serikali kwa kutuingizia fedha za madeni tuliyotokanayo mwaka wa fedha uliopita 2020/2021, ambapo ni TZS4,803,752,243.70 tulipatiwa kwa ajili ya ulipaji wa madeni hayo ambazo zimeingizwa kwa mwaka wa Fedha 22021/2022

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Baada ya Kamati kupokea majibu hayo ya Taarifa za Matumizi haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.10.1.1: Kutokukamilika kwa ujenzi wa Skuli ya Sekondari Kibuteni kwa wakati**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilifunga mkataba wa makubaliano wenye kumbukumbu namba CW/1/SMZ/B/01/210/LOT1 wa tarehe 3 Septemba, 2012 na mzabuni United Distributers Ltd. kwa ajili ya ujenzi wa skuli ya Sekondari Kibuteni, ambapo mkataba huo ulitarajiwa kumalizika tarehe 12 Oktoba, 2013 sawa na wiki 58 wenye thamani ya shilingi 3,945,259,264 ambapo ujenzi huo ulikuwa unafadhiliwa na BADEA I. Dosari iliobainika katika ukaguzi ni kutokukamilika ujenzi kwa wakati na kupelekea shughuli zifuatazo kutokutekelezwa:-

- Ujenzi wa jengo la utawala na madarasa.
- Ujenzi wa jengo la chakula.
- Ujenzi wa jengo la bweni la wanafunzi.
- Ujenzi wa jengo la waalimu.

Kutokana na dosari zilizobainika hapo juu Wizara ilifanya maamuzi ya kusitisha mkataba na mzabuni huyo baada ya kujiridhisha kuwa hana uwezo wa kuendelea na kazi hiyo na kumtaka ailipe Serikali hasara ya shilingi 675,277,138.4. Dosari ziliobainika katika ukaguzi kutokana na kadhia hiyo ni kama zifuatazo:-

- Serikali kupata hasara ya kutokutumia majengo kwa wakati.
- Hasara inayotokana na uchelewaji wa ununuzi wa baadhi ya vifaa vya kutoa

huduma skuli.

- Kutokana na kuongezeka kwa thamani halisi ya bei za bidhaa.
- Hasara ya kuchelewa kwa mradi kukamilika kwa wakati na kupelekea Serikali kubeba gharama za kuumalizia mradi huo kutokana na muda wa mradi kumalizika bila ya mafanikio yaliokusudiwa.
- Kushindwa kujiridhisha na kufanya maamuzi sahihi kwa kamati ya tathmini ya kumtafuta mzabuni mwenye uwezo jambo ambalo limepelekea kuitia Serikali hasara.
- Mzabuni kutokuwa na uwezo wa kifedha jambo ambalo limetia shaka Bodi ya Zabuni kumteuwa.
- Kukosekana kwa taarifa za mzabuni, mahala alipotekeleza mradi wa aina kama hiyo jambo ambalo limeonesha kutokuwa na uzoefu wa utekelezaji wa miradi mikubwa kwa kipindi kifupi.
- Kutokutekelezwa kwa maagizo ya mkataba yanayoitaka Wizara kuchukuwa hatua ndani ya siku 28 pale inapobainika mkandarasi amesimamisha shughuli za utekelezaji wa mradi bila sababu yoyote jambo ambalo Wizara ilichukuwa miaka 8 ndio kuanza kufanya ufuatiliaji.

Pamoja na uwepo wa dosari hizo ukaguzi umebaini Wizara ilishafanya malipo ya shilingi 2,058,486,497 kutoka katika mkataba wake wenye shilingi 3,945,259,264 na kuwepo kwa bakaa ya shilingi 1,886,772,767 ambazo alikuwa hajalipwa. Aidha, pamoja na uwepo wa bakaa hiyo ya fedha ukaguzi umebaini Wizara kuchelewa kufanya maamuzi kumepelekea Mkandarasi kuhamisha vifaa vyake katika eneo la ujenzi bila ya taarifa jambo ambalo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba kama mkandarasi atashindwa kuendelea na hatua ya ujenzi atalazimika vifaa vyote kuviwacha katika eneo la ujenzi.

Katika kuendelea na ujenzi kutokana na hatua iliyofikia Wizara ilifanya Mkataba wa nyongeza na Kampuni ya Rans Company Ltd. kwa thamani ya shilingi 2,054,020,400 kwa ajili ya kazi ya ukamilishaji wa jengo alililoliwacha Mkandarasi wa awali ambapo ujenzi wa dakhalia ya wanaume imegharimu shilingi 1,129,593,900 pamoja na PC SUM shilingi 747,000,000 kwa kazi ya ziada ambazo hazimo katika Mkataba wa mwanzo na jumla ya gharama yote 3,930,614,300 ambapo Wizara imeshafanya malipo ya shilingi 2,361,092,402.

Kutokana na kuendelea kwa ujenzi na Kampuni ya Rans ukaguzi umebaini dosari zifuatazo:-

- Kwa mujibu wa Mkataba wa awali ulieleza iwapo Mzabuni atashindwa kuendelea na ujenzi atapewa Mkandarasi mpya kwa gharama iliyobakia jambo ambalo halikuwezekana kutekelezeka kutokana na kupanda kwa gharama za ujenzi kulikosababishwa na uzembe wa Wizara kuchelewa kuchukuwa maamuzi ya mapema baada ya kubaini Mkandarasi wa mwanzo hana uwezo wa kifedha kuendelea na ujenzi.
- Hadi ujenzi utakapokamilika utagharimu jumla ya shilingi 5,989,100,797 ambapo ni sawa na asilimia 66 ya ziada ya gharama ya awali jambo ambalo

ilipaswa Wizara kufanya maamuzi ya kufunga Mkataba mpya kwa mujibu wa taratibu na sheria za ununuzi na uondoshaji wa mali za Umma.
- Ukiukwaji wa Kanuni ya 49(4)(5) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba iwapo malipo yatazidi bei ya Mkataba zaidi ya asilimia 15 yawasilishwe kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata uthibitisho (Approval).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu kuhakikisha unaongeza umakini katika kufanya tathmini katika kumteuwa Mzabuni ambaye atakuwa na uwezo wa kifedha, pamoja na uzoefu kwa mujibu wa kazi anayotaka kupewa ili kuepusha Serikali kupata hasara zinazotokana na urasimu wa kutokuchukuwa maamuzi haraka.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ilipokea hoja ya Mkaguzi na ufuatao ni ufafanuzi wa hoja hiyo; Kwasasa Skuli tayari imekamilika na Wanafunzi wameshaingia madarasani kwa kuendelea na masomo. Kushindwa kukamilisha kazi za ujenzi Mkandarasi United Bulders Ltd. kwa wakati skuli ya Kibuteni kupitia ufadhili wa BADEA. Kazi zenyewe ni kama ifuatayo:-

- Ujenzi jengo la Utawala na Madarasa
- Ujenzi wa Jengo la Chakula
- Ujenzi wa Jengo la Bweni la Wanafunzi
- Ujenzi wa Nyumba ya Walimu

Kamati ya tathmini ilifanya kazi yake ya kupitia nyaraka za Wazabuni walioomba kazi ya ujenzi wa skuli ya Kibuteni kwa mujibu wa vigezo vilivyoainishwa katika (Bidding Document).

Mkandarasi United Builder ameanza kutekeleza mradi tarehe 3 Septemba, 2012 na ukamilishaji ulikuwa ni tarehe 12 Oktoba, 2013 ambao ni sawa na wiki 58.

Hata hivyo mpaka inafika tarehe 23 Septemba, 2016 ni miaka minne (4) kutoka tarehe ya kusaini Mkataba, Mradi ulikuwa umefikia asilimia 63% ya kazi hiyo, licha ya vikao (site meetings) pamoja na barua nyingi za onyo kumuandikia Mkandarasi huyo lakini kazi bado ikawa inasuasua katika utekelezaji wa ukamilishaji. Kwa muonekano wa Wizara (Client) na Mshauri Elekezi (Consultant) kwamba Mkandarasi hana uwezo wa kifedha (Financial capacity) kukamilisha kazi kwa kipindi alichoongezewa muda.

Wizara ndipo ilipoamua kumuandikia barua ya kuvunja Mkataba (Contract Termination) na Kampuni ya United Builder na kumsimisha asiendelee na kazi eneo la ujenzi Kibuteni, baada ya Mkataba huo kusitishwa, Mshauri Elekezi alitayarisha final Account ambayo aliimbatanisha katika taarifa ya mwisho (Final report) ambayo ilimtaka Mkandarasi kumlipa Muajiri wake (Client) jumla ya shilingi Milioni 675,277,138.4. Kuvunja Mkataba kulitokana na vifuatavyo:-

1. Hasara ya kutokutumia majengo.
2. Hasara ya kucheleweshа ununuzi wa baadhi ya vifaa vya kutoa huduma skulini hapo.
3. Hasara za kuchelewesha mradi kukamilika.

Hadi Mkataba unavunjika Mkandarasi alishalipwa kiasi cha TZS 2,058,486,497.00, kutoka katika Mkataba wake wenye thamani ya TZS 3,945,259,264.00, na bakaa ni TZS 1,886,772,767.00, Mkataba wa awamu ya pili na RANS ulikuwa na thamani TZS 2,054,020,400/- ni kwaajili yakazi yaukamilishaji majengo aliyoyaacha mkandarasi wa awali.

Ujenzi wa Dakhalia ya wanaume imegharimu TZS.1,129,593,900/- pamoja PC SUM 747,000,000/- ni kazi za ziada ambazo hazimo katika Mkataba wa mwanzo kwa kazi ukamilishaji wa ujenzi ni jumla ya TZS.4,112,506,897/-.Hata hivyo, Wizara iliupokea ushauri wa Mkaguzi na kuweza kuufanyia kazi kwa kupata Wakandarasi wenye uwezo.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC haikuridhishwa kabisa na majibu ya Watendaji wa Wizara ambapo kutokana na uzembe uliofanyika uliifanya Serikali kutumia fedha za ziada za umma kurekebisha kasoro zilizojitokeza na kuhakikisha ujenzi unakamilika na wanafunzi wanapata huduma ya kujifunza ipasavyo. Kamati imefikia maamuzi hayo baada ya kuwauliza maswali mengi Watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali bila ya kupata majibu yaliyo sahihi, yaliyo wazi na yenye kuonesha kwamba kuna juhudi za makusudi zimechukuliwa kuondoa changamoto zilizojitokeza.

Miongoni mwa maswali ambayo Kamati iliyauliza ili kupatiwa ufafanuzi ni haya yafuatayo;

- Kwanini Kamati ya tathmini ya awali haikutekeleza wajibu wake ipasavyo kwa kumteua Mkandarasi ambae hakuwa na uwezo wa kifedha uliopelekea kushindwa kukamilisha kazi aliyopatiwa. Watendaji wa Wizara walieleza kwamba Kamati ya Tathmini ilimtathmini Mkandarasi kupitia nyaraka alizowasilisha (documents) na kwenda kuangalia kwenye 'site' bila ya kuchunguza kwa undani uwezo wake wa kifedha kwa kuangalia 'cashflow' yake inavyoenda. Hata hivyo, Kamati yetu imegendua kwamba Kamati ya Tahmini ilifanya uzembe wa kutofuatilia kwa undani uzoefu na uwezo wa Mkandarasi katika ujenzi mkubwa na wenye gharama kubwa.
- Jee Mkataba wa ujenzi huo haukuwa na 'Performance quarantee' na kuelezwa kwamba ilikuwepo ambapo baada ya kukatisha Mkataba, Mjenzi alifungua kesi Mahkama Kuu ya Tanzania Bara (case no. 51/2016) kuomba 'bond' hiyo iondolewe na ikaondolewa. Lakushangaza, bond iliyokuwa imewekwa ilikuwa katika Benki iliyopo Tanzania Bara ambayo kwa wakati huo ilikuwa ishafilisika na kuchukuliwa na benki ya Azania. hivyo Wizara ipo katika mpango wa kudai 'bond' hiyo katika benki hiyo.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ilitaka kujua kwanini wakaingia Mkataba ambao utekelezaji wake haupo rafiki ambao unalazimisha Mahkama Kuu ya Tanzania Bara ndio itumike wakati Zanzibar inazo Mahkama zenye uwezo wa kusimamia ya Mikataba ya ujenzi kama hiyo, Wizara haikuwa na majibu isipokuwa ilieleza ndio Mkataba wenyewe ulivyoelekeza. Hivyo, inaonesha wazi kwamba Watendaji wa Wizara hawakuwa makini katika kuyatathmini masharti yaliyokuwemo ndani ya Mkataba husika.

- Kamati ilitaka kujua kwamba kwanini Wizara ilichelewa kukatisha Mkataba kwa zaidi ya miaka minne kipindi ambacho ni kirefu katika utekelezaji wa Mikataba hususan ya ujenzi na kuelezwa kwamba walichukua juhudi za kumkumbusha kila baada ya muda. Kwani ihali hiyo ilijitokeza wakati Mkataba unalosharti linaloitaka Wizara kuchukuwa hatua ndani ya siku 28 pale inapobainika mkandarasi amesimamisha shughuli za utekelezaji wa mradi bila sababu yoyote jambo ambalo Wizara ilichukuwa miaka 8 ndio kuanza kufanya ufuatiliaji.
- Kadhalika, Kamati ilitaka kujua kwanini Mkandarasi aliondoka ‘site’ wakati anajua kwamba kazi hajaikamilisha na kuelezwa kwamba walizuia baadhi ya vifaa vyake vya kazi vilivyokuwepo ikiwemo dari ya mixture na compressor.
- Vile vile, Kamati ilitaka kujua kwanini wa Watendaji wa Wizara baada ya kukatishwa kwa Mkataba wa awali haikuingia katika Mkataba mwengine badala yake waliingia kwenye nyongeza ya Mkataba na kuvunja Kanuni ya 49(4)(5) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma inayotaka nyongeza ya Mkataba wa Zabuni usizidi asilimia 15 ya Mkataba husika wakati fedha zilizotumika zilizidi na kufikia asilimia 66.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kutokana na wasi wasi wa Kamati juu ya upotevu wa fedha za umma uliosababishwa na uzembe wa Watendaji na Mkandarasi, Kamati inapendekeza kuchunguzwa kwa undani Wahusika wote walioshiriki katika utoaji Zabuni ya Ujenzi wa Skuli ya Kibuteni wakiwemo Bodi ya Zabuni iliyopitisha Zabuni husika, Kamati ya Tathmini pamoja na Mkandarasi wa awali (wakiwemo watendaji wake) ili Serikali ipate majibu kamili ya chanzo cha uzembe, waliochangia uzembe na vipi wataweza kuwajibishwa kwa kuchukuliwa hatua za kisheria.

**Hoja nambari 6.10.1.2: Dosari katika usimamizi wa Dahalia**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umeweza kutembelea maeneo mbali mbali ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendelezo inayotekelezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kutembelea baadhi ya Skuli za ufundi zinazojishughulisha na uzalishaji mali, pamoja na dakhalia mbalimbali kwa lengo la kuweza kubaini baadhi ya changamoto zinazoweza kupelekea kutofaulu vizuri kwa wanafunzi au kutokufi kiwa kwa malengo ya uzalishaji mali unaotokana na uwepo wa changamoto mbali mbali zinazojitokeza katika skuli hizo kama zifuatavyo:-

- Uchache wa upatikanaji wa fedha za chakula kwa mujibu wa bajeti za maskuli ambazo zinazoenda sambamba na wingi wa wanafunzi waliopo na wanaolala katika dakhalia.
- Uchache wa mabweni ya kulala wanafunzi kutokna na idadi kubwa ya wanafunzi wanaolala kutokana na maeneo wanayoishi au skuli wanazotoka.
- Kutokuwepo gari maalum katika dakhalia kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanafunzi pale dharura inapojitokeza.
- Kutokuwepo kwa kituo cha huduma ya Afya kwa ajili ya huduma ndogo ndogo za afya.
- Kukosekana kwa viwanja vya kuchezea watoto ambavyo vitapelekea akili za watoto kukuwa na kuibua vipaji vipya kupitia michezo.
- Kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya kufundishia masomo ya vitendo na nadharia ikiwemo “electronic drawing cards, computer drawing rooms, grinding machines” jambo ambalo linapelekea kuwepo kwa vyumba vya kufanyia mafunzo ya vitendo ambavyo haviendani na uhalisia wa mitaala ya mafunzo ya ufundi stadi.
- Baadhi ya skuli za ufundi kushindwa kufanya uzalishaji mali kutokana na kukosekana kwa ruzuku ya fedha inayopelekea wanafunzi kushindwa kufanya mafunzo ya vitendo na hatimaye Skuli za ufundi kufundisha zaidi kwa nadharia kuliko vitendo.

Kutokana na changamoto zilizobainika, ukaguzi unaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu kuhakikisha inaandaa mazingira bora ya kuboresha skuli za ufundi pamoja na dakhalia mbalimbali ili ziweze kuendana na wakati wa uzalishaji wanafunzi ambao wataweza kujitegemea pindi wanapomaliza mafunzo yao na kuacha kutegemea ajira kutoka Serikalini ambapo lengo la Serikali kuanzisha skuli za ufundi ni kuhakikisha kuwa mwanafunzi anakua mjasiriamali au kuzalisha wahandisi ambao wataendana na dhana ya kuitoa Serikali katika uchumi wa Kati na kuipeleka katika uchumi wa viwanda na kujitegemea.

Aidha, ni vyema Wizara ya Elimu kuhakikisha inaondokana na matumizi ya kutumia umeme mkali katika uzalishaji wa usanifu wa vyuma katika maskuli ya ufundi na kuanza kutumia umeme mwepesi wa usanifu wa aluminium ambapo leo ndipo dunia ilipofikia. Hesabu ya Madawati namba 0404019000

**Majibu ya Wizara**

Kwa upande wa dakhalia, Wizara ya Elimu kupitia Idara ya Elimu Sekondari inahudumia Dakhali 10, 6 zipo Pemba na 4 zipo Unguja ambapo:-

- Idara inatoa fedha TZS. 105,000,000 kila mwezi. Hata hivyo, katokana na fedha zinazopatikana haikidhi uhalisia wa mahitaji.
- Kuhusu usafiri katika dakhalia za Pemba unazo ila huwa zinahitaji kufanyiwa matengenezo mara kwa mara zinapoharibika.
- Idara imehakikisha kuwapatia wahudumu wakiwemo wapishi matron/patron

na basa ili kuhakikisha mazingira na usimamizi bora kwa wanafunzi yanafikiwa.

Kwa upande wa skuli za ufundi, Wizara ya Elimu ina skuli mbili za ufundi ambazo ni Mikunguni kwa Unguja na Kengeja kwa Pemba ambapo:-

- Katika kuimarisha mazingira ya skuli hizo, Wizara inatoa fedha za uendeshaji kwa skuli hizo pamoja vifaa vya kuendesha mafunzo kwa vitendo ili kutimiza lengo la uanzishwaji wa skuli hizo.
- Vile vile, wanafunzi wanafanya mazoezi ya vitendo katika Taasisi na Mashirika mbali mbali kama vile ZECO, ZAWA, ZBC, POSTA na Matrekta.
- Pia, Kupitia Balozi wa China wamepatiwa msaada wa kila skuli kompyuta 15, fotokopi 1, printa 1.
- Wizara inasaidia kumalizia ujenzi wa Chumba cha Kompyuta kwa Mikunguni.
- Aidha kuhusu matumizi ya umeme mkali, shauri hilo limechukuliwa, na Idara husika imelipokea na inalifanyia kazi kwa kuzungumza na mwalimu anayefundisha Umeme ili kutoa ushauri zaidi wa kitaalamu.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC katika ufuatiliaji wa hoja hii, pamoja na mambo mengine iligundua mambo yafuatayo;-

- Kuna kutofautiana kwa majibu yaliyokuwa yakitolewa na Watendaji jambo ambalo limeipatia wasiwasi Kamati juu ya usahihi wa maelezo waliyokuwa wakiyatoa. Baadhi ya watendaji walieleza kwamba Unguja wanatumia basi la Dakhalia kuwasaidia wanafunzi huduma za usafiri wakati wengine walieleza kwamba hakukuwa na gari ya dakhalia isipokuwa walikuwa wakitumia gari ya Mumewe Matron wao.

  Kufuatia utata huo, Kamati imebaini ukweli kwamba lipo 'bus' lenye namba SMZ 1057A aina ya Toyota Coaster la 2019 lenye usajili nambari Z-048865245 linalomilikiwa na Wizara ya Elimu na sio Dakhalia. Kadhalika, 'bus' hilo linalala Wizarani badala ya Dakhalia ya Kibuteni sehemu ambayo wanafunzi wanakuwepo ili kuwasaidia wanafunzi iwapo kutatokezea dharura. Hivyo, gari iliyopo haikuwa gari ya Dakhalia badala yake ilikuwa gari ya Wizara kwa shughuli za Wizara. Lakushangaza, Kamati ilipouliza kuwa wamepanga kwenye bajeti kununua gari ndogo (pickup) kwa ajili ya Dakhalia hiyo nakuelezwa kwamba kwa mwaka huu hakuna bajeti hiyo.

- Kuhusu kutokuwepo kwa kituo cha huduma ya Afya kwa ajili ya huduma ndogo ndogo za afya. Kamati imebaini kwamba hakuna kituo cha Afya katika Dakhalia hizo isipokuwa katika baadhi ya Dakhalia wanatumia Mtaalamu wa Afya kutoka katika vituo vya Afya vilivyopo karibu nazo kwa mfano katika Dakhalia ya Micheweni wanatumia Mtaalamu wa Afya kutoka katika hospitali ya Wete.

- Kuhusu viwanja vya Michezo, Kamati imebaini kuwa kwasasa hawana viwanja rasmi vya michezo kwa ajili ya Watoto isipokuwa Dakhalia zote zinatumia viwanja vya michezo vilvyopo karibu nazo. Katika Dakhalia ya Kibuteni pekee ndio iliyokuwa haina kiwanja cha michezo. Kamati imeridhika na majibu ya Wizara kuhusiana na hoja ya viwanja vya michezo.
- Kamati imegendua kwamba kuna uchache wa Dakhalia kwani Dakhalia ya Chasasa ina wanafunzi hadi 300 jambo ambalo linahitaji uangalifu wa karibu zaidi. Aidha, kuhusiana na uchache wa upatikanaji wa fedha za chakula kwa mujibu wa bajeti za maskuli ambazo zinazoenda sambamba na wingi wa wanafunzi waliopo na wanaolala katika dakhalia, Kamati imebani ni kweli kuna ufinyu wa fedha ambapo kila mwezi wanapatiwa milioni 105 wakati wanahitaji zaidi ya hizo.
- Kuhusu kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya kufundishia masomo ya vitendo na nadharia ikiwemo "electronic drawing cards, computer drawing rooms, grinding machines". Kamati imebaini kwamba vifaa viliopo ni vichache ambavyo havikidhi mahitaji ya kufundishia. Kutokana na hilo, Skuli ya Mikunguni hivi sasa inashindwa kuzalisha bidhaa bora za uchongaji kama ilivyokuwa awali.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inaongeza bajeti ya wanafunzi na wanaolala katika skuli za Dakhalia.
2. Wizara itakapoandaa mpango wa bajeti ia mwakani izingatie kuweka bajeti ya ununuzi wa gari ndogo kwa ajili ya Dakhalia ya kibuteni.
3. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya iwe na utaratibu wa kumpeleka Mtaalamu wa Afya katika kila Dakhalia za wanafunzi.
4. Wizara ifanye utaratibu wa kuwepo kiwanja cha michezo kwa wanafunzi wa skuli ya Kibuteni.
5. Wizara iongeze bajeti ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia masomo ya ufundi stadi kwa wanafunzi wa Mikunguni.

**Hoja nambari 6.10.1.3: Dosari katika ununuzi wa Madawati shilingi 2,882,981,080**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeingia mkataba wa nyongeza (Addendum) uliosainiwa tarehe 15 Novemba, 2019 wenye thamani ya dola za kimarekani USD 1,254,529.20 kwa ajili ya ununuzi wa Madawati 35,610 na kupelekea uwepo wa mkataba halisi uliosainiwa tarehe 21 Septemba 2020 kufikia thamani ya dola za kimarekani USD 2,641,528.70.

Aidha, ukaguzi umebaini kujitokeza kwa dosari za kuitendaji katika utekelezaji wa mkataba wa nyongeza ambapo imebainika uwepo wa ziada ya matumizi ya dola za kimarekani 1,386,999.5 sawa na asilimia 111 ya ongezeko la gharama za awali.

Kutokana na kuwepo kwa ongezeko hilo kumejitokeza ukiukwaji wa sheria ya Ununuzi ambapo Kanuni ya 49(4-5) ya kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya

mwaka 2021 kinaeleza kwamba " iwapo malipo yatazidi bei ya mkataba zaidi ya asilimia 15 yawasilishwe kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata uthibitisho au Baraza la Wawakilishi (Approval)." Jambo ambalo ukaguzi haukupatiwa uthibitisho huo.

Kukosekana kwa muhtasari wa maamuzi ya kikao cha Bodi ya Zabuni kilichoamua kumpitisha mzabuni huyo na kuendelea na harakati za zabuni yake kwa mujibu wa kifungu cha 6(1)(c) cha Sheria Nambari 11 ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali ya mwaka 2016, pindipo inapotokezea nyongeza ya mkataba wa awali kupewa mzabuni wa mwanzo kuendela na kazi hiyo haitatakiwa kuongezeka kwa asilimia 25 ya thamani ya zabuni ya awali jambo ambalo halikuzingatiwa katika utowaji wa zabuni hiyo. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kwa mujibu wa dosari zilizobainika hapo juu Wizara ilipaswa kutangaza zabuni mpya ili kuweza kujitokeza wazabuni ambao watakuwa na ushindani wa bei kwa lengo la kuleta tija iliyokusudiwa vyenginevyo ni kuitia hasara Serikali na kupelekea upotevu wa fedha za Umma.

Vile vile kwa mujibu wa sheria kama Wizara ilikuwa haina budi kuendelea na mzabuni huyo ilipaswa kufanya malipo ya asilimia 25 na sio malipo yalofanyika ya aslimia 110 jambo ambalo limepelekea kuisababishia hasara Serikali kwa malipo ya asilimia 85 ya ziada ya malipo ya awali. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 180 : Fedha zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa madawati**

| **Hati namba** | **Kiasi cha Fedha (Tshs)** | **Aliyelipwa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| 1/10/2020 | Tshs. 960,818,930 (USD 416,102.85) | JIANGMEN KEYI METAL MANUFACTURE CO. LTD | Malipo ya fedha kwa Kampuni ya JIANGMEN KMM COY. LTD kwa ajili ya ununuzi wa Madawati. |
| 1/1/2021 | Tshs. 961,081,075 (USD 416,102.85) | | |
| 2/6/2021 | Tshs. 961,081,075 (USD 416,102.85) | | |
| **Jumla** | **2,882,981,080** | | |

**Majibu ya Wizara**

Wizara inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kuwa kunaongezeko katika ununuzi wa Madawati. Hii ni kutokana na umuhimu wa madawati hayo na kuwepo kwa changamoto ya vikalio kwa wanafunzi katika skuli zetu. Pia kwa upande wa Kamati ya Madawati waliweza kuona upo uharaka wa kupata vikalio kwa kupunguza gharama na muda katika mchakato wa manunuzi, hivyo kutokana na msambazaji wa Awali aliweza kuwasilisha vikalio kwa aslilimia 100% ndipo kamati iliyooundwa na Serikali Kuu ikatoa maamuzi kuwa Wizara iweze kuendelea na msambazaji huyo wa awali kwa gharama za

awali.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imegundua kwamba ununuzi wa awamu ya pili ambao ulipitiliza asilimia ya kiwango kinachotakiwa kununuliwa kwa Mkataba wa nyongeza ulifanywa kutokana na agizo kutoka Baraza la Mapinduzi. Hata hivyo, Kamati inagundua kwamba kuwepo kwa agizo sio kama ndio sababu ya kukiuka taratibu za kisheria, bado Kamati Maalum wa Madawati ilipaswa kuhakikisha wanafuata nini sheria inakitaka. Kadhalika, kupitia agizo hilo, Wizara haikuwa na ithibati yoyote ya kumuonesha Mkaguzi kwamba kulikuwa na agizo na ripoti yake yenye maamuzi husika haikuwepo wala hakukuwa na ripoti yoyote kutoka Bodi ya Zabuni. Kwa mantiki hiyo, matuizi ya shilingi 2,882,981,080 yalikosa kufuata utaratibu kitu ambacho kinaondoa uhalali wa kazi zote zilizotekelezwa.

Sambamba na hilo, Kamati imebaini kuwa Madawati mengi yaliyonunuliwa na kusambazwa skuli yalikuwa mabovu na mengine tayari yaliharibika kwa muda mfupi mno.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wizara inapopatiwa agizo linalohitaji utekelezaji, ihakikishe inalitekeleza kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Sheria au Kanuni.
2. Wizara ihakikishe utekelezaji wa agizo unafanywa kwa ithibati itakayokuwa ni kielelezo kwa Mkaguzi.
3. Wizara isiishie katika ununuzi wa Madawati bali ifuatilie hata katika matumizi na utunzwaji wake ili yaweze kutumiwa na wanafunzi kwa muda mrefu.

## 6.10.2: BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

### Taarifa ya Mapato

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,515,475,000. Hadi kufi kia tarehe 30, Juni 2021 Bodi ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 10,352,345,318 sawa na asilimia 294 ya makadirio.

### Taarifa ya Matumizi

Bodi ya mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 16,651,350,000. Kati ya fedha hizo shilingi 389,400,000 kwa ajili ya mshahara na shilingi 16,261,950,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shillingi 15,147,623,168 zilitumika ambazo ni sawa na asilimia 91 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 386,148,100 zilitumika kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 99 ya makadirio na shilingi 14,761,475,068 kwa ajili matumizi mengineyo sawa na asilimia 97 ya makadirio.

**Hoja nambari 6.10.2.1: Madeni ya wanafunzi shilingi 1,921,043,698.69**

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa deni kubwa la wanufaika wa mikopo ya Elimu wa fani mbalimbali kwa vipindi tofauti kuanzia mwaka 2006 hadi 2011, lakini hadi sasa mikopo hiyo bado haijarejeshwa pamoja na kufi kia muda wa kuanza kufanya marejesho. Wanufaika 206 ambao wamepata mkopo wa jumla ya shilingi 1,921,043,698.69 wanaonekana kuwa ni wadaiwa sugu wa Bodi ya Mikopo.

Kutofanya marejesho ya mkopo kwa wakati kunapelekea kuzirejesha nyuma juhudi za Serikali za kuwapatia fursa wananchi na kuweza kujiendeleza katika elimu ya juu jambo ambalo litakwaza utekelezaji wa shughuli za bodi ya mikopo walivyojipangia ikiwa mikopo hiyo haitarejeshwa kwa wakati, Kiambatisho Nambari 9 Kinahusika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Bodi ya Elimu ya Juu kuhakikisha juhudi za makusudi zinachukuliwa kuwatafuta wadaiwa wote popote walipo na taratibu za kuwakata madeni ya mikopo yao kutokana na mishahara wanayoipata katika taasisi wanazozifanyia kazi.

Aidha, uongozi uchukue juhudi za kusambaza majina ya wadaiwa kwa taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Muungano ili kuwataka Wakuu wa taasisi watoe ushirikiano wa taarifa za mtumishi yoyote ambae jina lake litakuwa limebainika katika taarifa za deni zilizosambazwa ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa juu yake ikiwemo urejeshwaji wa mikopo hiyo.

**Majibu ya Wizara**

Hatua mbali mbali za kuwatafuta wadaiwa 199 wa muda mrefu waliohitimu masomo kwa vipindi tofauti kuanzia 2006 hadi 2011 ambao wameorodheshwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wenye deni la jumla ya Tzs. 1,921,043,698.69 zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na :

1. Kutoa taarifa ya wito kwa kuyatangaza majina katika tovuti ya Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu.(www.zhelb.go.tz).
2. Kupeleka barua za kuomba majina ya wahitimu wa Elimu ya Juu katika taasisi mbali mbali za SMZ na taasisi binafsi.
3. Kuendelea na ziara za uhakiki kwa kuwatafuta wafanyakazi waliokopa katika taasisi mbali mbali kwa mashirikiano na waajiri.
4. Kuwatumia wadhamini wa wadaiwa katika kuwataka waliowadhamini waanze kurejesha mikopo yao.

Matokeo ya hatua hizo ni kama ifuatavyo:

Wadaiwa 78 wenye deni la masomo la jumla ya Tzs. 1,035,707,973/- sawa na 54% ya deni wameshapatikana na wameanza kurejesha mikopo yao (Kiambatisho nambari A1 kinahusika).

Wadaiwa 121 waliosalia wenye deni la jumla ya Tzs. 885,335.725.69 sawa na 46% ya deni wanaendelea kutafutwa (Kiambatisho nambari A2 kinahusika). Juhudi za kuendelea kuwatafuta wadaiwa hao zinachukuliwa kwa kupitia wadhamini wao na Waajiri nk.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imegundua kwamba madeni mengi yaliyoorodheshwa yalikuwepo kabla ya kuanzishwa kwa Bodi hii yaliyotokana na kukosa ufuatiliaji wa karibu katika Taasisi na Wanufaika wenyewe. Hali hiyo ilisababisha deni hilo kurudikana hadi kufikia kuonekana kubwa na kutoonekana juhudi za Bodi katika ufumbuzi wa changamoto hiyo. Hata hivyo Kamati imeridhika na juhudi zinazochukuliwa na Bodi za kuwapata wanafunzi waliorudisha deni la kwa asilimia 52. Hatua hiyo ni nzuri na inafaa kutekelezwa na Taasisi nyengine zinazodai madeni.

Sambamba na hilo, Kamati yetu ilitaka kujua sheria ya mikopo Zanzibar haina changamoto katika usimaimzi wa mikopo kwa wanafunzi walionufaka na kujibiwa kwamba Bodi tayari imeliona hilo na kwasasa inaendelea na hatua ya kuifanyia marekebisho sheria hiyo ikiwemo kuingiza kifungu kitakachowapa nguvu ya kuweza kupata taarifa ya wanaufaika popote pale watakapohitaji.

Vile vile, Kamati imebaini kwamba Bodi tayari wameshazungumza na Hazina ya Tanzania Bara ili iweze kuwakata fedha za marejesho watumishi walionufaika na Mkopo wa Elimu ya juu wa Jamhuri ya Muungano na wao kuchukua asilimia 2.5 ya marejesho hayo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Bodi ya Mikopo ya ELimu ya Juu ifuatilie wanufaika wake katika Taasisi za kodi na usajili wa kibiashara na mali zikiwemo ZRB, TRA na BPRA kwani kuna wanufaika wengi wa mikopo hawajaariwa katika Serikali lakini wanazo fedha nyingi wanazozipata kupitia biashara.
2. Bodi iharakishe mchakato wa kuifanyia marekebisho sheria yake ili kasoro zilizopo ziweze kupatiwa tiba.

**Hoja nambari 6.10.2.2: Kukosekana kwa mfumo wa uhakiki wa wanafunzi waliopo vyuoni**

Ukaguzi umebaini kwamba hakuna mfumo maalum uliotayarishwa kwa mashirikiano baina ya Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu Zanzibar na vyuo husika ili kuthibitisha uwepo wa wanafunzi wanaoendelea na masomo yao katika vyuo husika kuanzia muhula wa pili na kuendelea kwa mnasaba wa kuendelea kupatiwa mkopo. Mfumo huo ambao

ungekuwa ni uthibitisho wa wanafunzi wanaoendelea na masomo na wangepaswa kuendelea kupatiwa mkopo ili kuondoa utata wa kuwalipia wanafunzi ambao hawapo vyuoni kuendelea na masomo kutokana na sababu zozote zile zilizowakabili, ama kujitokeza kwa wanafunzi waliokosa sifa za kupata mkopo kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar.

Kukosekana kwa mfumo wa uhakiki wa wanafunzi kumepelekea Serikali kupoteza fedha nyingi kuendelea kuwalipa wanafunzi ambao kwa njia moja ama nyengine wamepoteza sifa ya kuwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka katika vyuo mbalimbali ima kwa sababu ya utoro au kushindwa kuendelea na masomo kutokana na sababu mbalimbali jambo litapelelekea ugumu wa kuwatambua walipo na hatimae kutokupatikana kwa marejesho ya fedha iliyokusudiwa kutumika kuwasomeshea wanafunzi wengine.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu kuhakikisha unafanya kazi karibu na Bodi ya mikopo ya elimu ya juu Tanzania Bara kwa lengo la kusaidiana utelekezaji wa majukumu yaoambapo utaibua kuwabaini wanafunzi wanaochukua mikopo na kushindwa kuirejesha kwa wakati.

**Majibu ya Wizara**

1. BMEJZ imeweka utaratibu kwa watendaji wake kufika vyuoni kwa ajili ya uhakiki wa wanufaika wa mikopo kabla ya kuanza kufanya malipo ya ada na posho za wanafunzi. Kupitia utaratibu huu, kila mnufaika anapaswa kuweka saini kwenye Fomu nambari 3 kwa ajili ya malipo ya ada na posho. Mnufaika atakayeshindwa kuweka saini kwenye fomu hizo zinapopelekwa vyuoni huhesabika hayupo Chuoni na BMEJZ haitomfanyia malipo yoyote.
2. Kuanzia mwaka 2022/23, Bodi imewasajili maafisa mikopo wa vyuo katika mfumo wa maombi ya mikopo ZOLAS, ambapo maafisa hao wanapokea majina ya wakopaji wapya na kutoa mrejesho kwa wanafunzi waliowasajili vyuoni kwa kila mwaka. Maafisa mikopo wa vyuo pia watatuma matokeo ya mitihani kupitia mfumo wa ZOLAS kwa kila mwaka.
3. Wakopaji/wanafunzi nao wanatakiwa kujaza mikataba yao kupitia mfumo ZOLAS na kuambatinisha na matokeo yao ya mitihani. Utaratibu huu unawahusu wanafunzi wote waliotuma maombi ya mikopo kupitia mfumo, na wale wachache walio nje ya mfumo ambao waliomba mikopo kabla ya kuanza kutumika kwa mfumo wa ZOLAS 2020/21 wataendelea kuhakikiwa kupitia Fomu Nambari 3 hadi wamalize masomo yao.
4. Katika bajeti ya 2022/23 BMEJZ imepanga pia kufanya usajili kwa kutumia mfumo wa usajili wa kidigitali (Biometric registration). Mfumo huo utaunganishwa na mfumo wa maombi ya mikopo wa ZOLAS unaotumiwa na BMEJZ.
5. Juhudi za kufanya kazi kwa ukaribu kati ya BMEJZ na Bodi ya Mikopo ya SMT zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kusaini MOU ya mashirikiano, kufanya zoezi la kuwatafuta wadaiwa wa Zanzibar kwa pamoja, kubadilishana utaalamu kwa wafanyakazi, kubadilishana majina ya wakopaji ili kuondoa wanafunzi

wenye mikopo miwili. Matumizi ya mifumo ya uhakiki kwa biometric kwa pamoja yameshindikana kwa sababu taasisi hizi zinatumia mifumo miwili tofauti ya mikopo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba mifumo ya taarifa za wanufaika wa mikopo wa Taaisisi hizi mbili za mikopo (Zanzibar na Tanzania Bara) haiwiani, jambo linalopekea kukosekana kwa taarifa za wanufaika walioajiriwa upande mwengine wa ajira. Hili limebainika kwa vile Bodi ya Mikopo ya Zanzibar inatumia mfumo unaopata taarifa kwa njia za kawaida (kukusanya 'manual') wakati mfumo wa Bodi ya Tanzania Bara unachukua taarifa zake kwa mfumo wa 'biometrix' ambao unatumia alama za vidole za wanufaika. Hivyo inakuwa rahisi kutambua wapi mnufaika huyo ameajiriwa kwa vile tayari umeshaunganishwa na Mamlaka nyengine nchini.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Umefika wakati kwa Bodi hizi mbili za mikopo (Zanzibar na Tanzania Bara) kuzidi kufanya kazi kwa pamoja ili kuondoa mwanya kwa wanufaika kutokujulikana taarifa zao kunakopelekea kukosekana kwa marejesho yanayowasaidia wanafunzi wengine kupata fursa ya kusoma.
2. Kwa vile Bodi ipo katika hatua za kuanzisha mfumo mpya, ni vyema ikawapatia mafunzo watendaji wote watakaohusika na usimamizi na uendeshaji wa mfumo huo.

BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU- PEMBA

**Hoja nambari 6.10.2.3: Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 3,187,830**/-

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 181: Malipo kwa Watoa huduma ambao Hawakusajiliwa na mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 3/7 24/7/2020 | 000061 | 300,000 | Pandu Bookshop | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya ofisi. |
| 1/8 3/8/2020 | 000063 | 400,000 | Ali Miraj Abdallah | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho na huduma nyengine . |
| 5/9 9/9/2020 | 000068 | 100,000 | Pandu Bookshop | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya ofisi. |
| 6/9 1/9/2020 | 000066 | 120,000 | | |
| 3/10 26/10/2020 | 000071 | 300,000 | Pandu Bookshop, Khamis Omar Moh'd na Masoud Khamis Moh'd | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya ofisi. |
| 6/11 10/11/2020 | 000077 | 300,000 | Pandu Bookshop na Abuu Ahmed Omar. | |
| 2/1 6/1/2021 | 000080 | 300,000 | Michenzani Store na Ali Suleiman Ali. | |
| 6/1 15/1/2021 | 000083 | 300,000 | Pandu Book Shop na African Café | |
| 12/1 20/1/2021 | 000097 | 85,000 | Juma Abdalla Kheir | Malipo ya fedha kwa ajili ya utengezaji wa Printer ya ofisi. |
| ½ 1/2/2021 | 000090 | 300,000 | Nassor Kassim Issa na Sharif Restaurant. | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya ofisi. |
| 1/3 9/3/2021 | 000096 | 300,000 | Nassor Kassim Issa na Ali Kheri Rashid. | |
| 5/6 2/6/2021 | TT | 285,180 | Ali Kheri Rashid | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7/6<br><br>2/6/2021 | 000101 | 300,000 | African Café | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya ofisi |
| 8/6<br><br>2/6/2021 | 000101 | 520,000 | Sharif Restaurant. | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula |
| 10/6<br><br>11/6/2021 | TT | 237,650 | Ali Kheir Rashid | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa |
| **Jumla** | | **3,187,830** | | |

**Majibu ya Bodi**

Watoa huduma husika walikuwa ni walipa kodi wa kawaida ingawa kwa mwaka wa fedha 2021/22 walichelewa kufanya malipo ya usajili kupitia Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Hata hivyo Kaimu Afisa Manunuzi wa Ofisi hakuwa na taaluma ya kutosha kuhusiana na taratibu za ununuzi.

Ofisi ya Uratibu Pemba inaendelea na jitihada za kumpata Afisa mwingine wa ununuzi mwenye taaluma ya kutosha kuhusiana na taratibu za ununuzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Watendaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu walikubali kuwepo kwa kasoro za kuwatumia Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka husika, hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kuwa kasoro hiyo ilichangiwa na upungufu wa wafanyakazi wa Bodi hiyo (wanao watumishi watano) na kupelekea Afisi kumtumia Afisa Uwezeshaji Mikopo kufanya kazi za Manunuzi pasi na kuwa na utaalamu na ujuzi wa kufahamu taratibu za utekelezaji kazi hiyo.

Aidha, Kamati imebaini kuwa wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake, Watoa huduma walikuwa hawajasajiliwa. Hata hivyo, hivi sasa wanatumia watoa huduma ambao tayari wameshasajiliwa na Mamlaka husika.

**Mapendekezo ya kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri Bodi ya Elimu ya Juu kuongeza watumishi wa kutosha kulinga na utaalumu wa fani husiki ili kuepusha kutokufuatwa kwa taratibu zinazoelekezwa na Sheria za Manunuzi.

**Hoja nambari 6.10.2.4: Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 3,425,180/=**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 3,425,180 zimetumika kwa

ajili ya ununuzi wa bidhaa mbali mbali kwa matumizi ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Pemba lakini bidhaa hizo hazikurikodiwa katika madaftari ya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa bidhaa hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### 6.10.5: BARAZA LA MITIHANI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Mitihani Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Baraza la Mitihani Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 183,095,000. Hadi kufi kia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 288,124,016 zilikusanywa sawa na asilimia 157 ya makadirio.

**Majibu ya Baraza**

**Jadweli Namba 1: Fedha zilizokusanywa**

| Chanzo cha mapato makadirio | Makadirio Tzs | MakusanyoTzs | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Usajili wa vituo vya mitihani vya Skuli binafsi | 42,550,000 | 62,700,000 | 147 |
| Usajili wa watahiniwa wa skuli Binafsi | 124,145,000 | 196,650,000 | 158 |
| Malipo ya watahiniwa wa vyuo vya Ualimu | 16,400,000 | 16,120,000 | 98 |
| Faini kwa skuli zilicheleweshа Kusajili watahiniwa | | 4,890,000 | |
| Faini kwa wahitimu waliopoteza Vyeti vya kumalizia masmo | | 7,764,016 | |
| **Jumla** | **183,095,000** | **288,124,016** | **157** |

Baraza la Mitihani limekukusanya kiwango hicho cha fedha kama ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Makusanyo hayo yamepanda kutokana na sababu zifuatazo;:

a) Kuongezeka kwa kiasi kikubwa kwa Watahiniwa wa Skuli binafsi.
b) Kujitokeza kwa vyanzo vyengine vya mapato vinavyotokana na faini za Skuli

ambazo zilicherewesha kufanya usajili wa Watahiniwa pamoja na faini za Wanafunzi waliopoteza vyeti vya kumalizia masomo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba vyanzo vya usajili wa watahiniwa binafsi na usajili wa vituo binafsi ndio vyanzo vikuu vya Baraza la Mitihani. Sambamba na hilo, Kamati imesisitiza kwamba kuna utitiri mwingi wa vituo vya kufanyia mitihani. Hivya Baraza lichukue hatua stahiki ili liweze kuvisimamia ipasavyo.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Mitihani Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilipanga kutumia jumla ya shilingi 5,672,231,000. Kati ya fedha hizo shilingi 419,400,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 5,252,831,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 4,093,485,826 zilitumika ambazo ni sawa na asilimia 72 ya makadirio. Kati fedha hizo shilingi 456,585,940 zilitumika kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 108 ya makadirio na shilingi 3,636,899,886 zilitumika kwa ajili matumizi mengineyo sawa na asilimia 89 ya makadirio.

**Majibu ya Baraza**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Mitihani Zanzibar lilikadiriwa kukusanya kiasi cha Shilingi 5,672,231,000/-. Hadi kufikia tarehe 30 June, 2021 Baraza lilikusanya kiasi cha Shilingi 4,171,387,826/-, kati ya hizo ni TZS 456,585,940/- sawa na ailimia 109 zilikua ni Mishahara ya Wafanyakazi, TZS 3,426,677,886/- sawa na asilimia 68 kwa ajili ya uendeshaji wa Mithiani ya Taifa pamoja na matumizi mengineyo, na TZS 288,124,000/- sawa na asilimia 157 kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato ya ndani. Jaduweli namba 2 linaonesha uafafanuzi wa fedha hizo.

**Jadweli Namba 2: Matumizi**

| **Maelezo** | **Makadirio**<br><br>**Tzs** | **Makusanyo**<br><br>**Tzs** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Mshahara | 419,400,000 | 456,585,940 | 109 |
| Matumizi mengineyo (oc) | 5,069,736,000 | 3,426,677,886 | 68 |
| Mapato kutoka vyanzo Vyengine | 83,095,000 | 288,124,000 | 157 |
| **Jumla** | **183,095,000** | **288,124,016** | **74** |

Baraza la Mitihani la Zanzibar, Imepatiwa kiwango cha fedha kwa ajili ya Mitihani ya Taifa Pamoja na matumizi ya kazi za kawaida za kiofisi. Kiwango hicho cha fedha kimeonekana ni kizuri kwa kiasi fulani ikilinganishwa na miaka ya iliyopita.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba mishahara ya wafanyakazi imeongezekwa kutokana na kuongezwa walimu waliohamishiwa katik Baraza. Kamati imeridhika na majibu kufuatia kupatiwa barua ya tarehe 18/5/2022 yenye kumbukumbu nambari WEMA/W/OR/FM/004/VOL.XVI/222.

**Hoja nambari 6.10.5.1: Mapungufu yaliyojitokeza katika ufungaji wa hesabu**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Baraza la Mitihani halikuweza kuzingatia matakwa ya ufungaji wa hesabu kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa na kupelekea hesabu za Baraza la Mitihani utokuonesha sura sahihi na halisi kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa.

Aidha, ukaguzi ulifanya mawasiliano ya mara kwa mara ikiwemo kuwataka wahusika wafanye marekebisho juu ya dosari zilizobainika ili kuepuka kujitokeza kwa wingi wa hoja za ukaguzi ambazo zitapelekea utolewaji wa hati isiyoridhisha jambo ambalo hawakuweza kutekeleza hadi ukaguzi unakamilika taarifa za hesabu za Baraza la Mitihani zilikuwa na dosari zifuatazo:-

a) **Taarifa ambazo hazikuambatanishwa na hesabu za mwisho wa mwaka**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika taarifa za mali za kudumu hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na kupelekea kubainika kwa kasoro mbalimbali zinazotokana na kutokujulikana sehemu mali zilipo, thamani halisi ya mali hiyo pamoja na kukosekana kwa hati miliki inayothibitisha umiliki halali wa mali hizo pamoja na kutokujulikana thamani na sera za uchakavu wa mali hizo ili kuweza kuishauri Serikali juu ya namna bora ya kuzitambua mali zake pamoja na kuziwekea kumbukumbu maalum ya utambulisho wa mali hizo ili zisiweze kuvamiwa, kuuzwa, pamoja na kukutumika vibaya kinyume na utaratibu uliowekwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Aidha, kutokuziainisha mali za Serikali na kuziingiza katika daftari maalum kunaweza kukapelekea mali hizo kutokujulikana na hatimae kuibiwa au kupotea na kuipelekea hasara Serikali. Ukaguzi unaushauri uongozi kuhakikisha mali zote zinaainishwa katika buku maalum la kuwekea kumbukumbu pamoja na kuziwekea hesabu yake mwisho wa mwaka ili kuweza kuonesha mtaji wa mali unaomilikiwa na taasisi za Serikali.

**Jadweli Nambari 184: Taarifa ambazo hazikuambatanishwa na hesabu za mwisho wa mwaka**

| Nam. | Aina ya Mali |
|---|---|

| | |
|---|---|
| 1. | Kiwanja kinachomilikiwa na Baraza la Mitihani kilichopo Pemba |
| 2. | Kiwanja kinachomilikiwa na Baraza la Mitihani kilichopo Tunguu |

**Majibu ya Wizara**

- Baraza limefanyia kazi mapungufu yaliyobainika wakati wa ukaguzi na Hesabu zimefungwa kwa kuzingatia sheria ya fedha 'Public Finance Act 2016' na kuwasilishwa kwa wakati Ofisi ya Mkaguzi wa Nje na nakala moja (OR), Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha husika.

- Baraza lilihitajika kuambatanisha thamani ya viwanja inavyomiliki kwa upande wa Unguja na Pemba lakini ilishindikana kutokana na swala hilo linahitaji kufanyiwa tathmini (Valuation) ya kina ili kuweza kujua thamani yake halisi.
- Kwa sasa Baraza tayari limepata hati za viwanja hivyo na taratibu za kuvifanyia tathmini zinaendelea kwa kushirikiana na Taasisi husika kuhusu uthaminishaji wa viwanja hivyo.

Kuhusu uwepo wa daftari la kumbukumbu (Assets Register book) hatua zimechukuliwa na Baraza linaendelea kuziingiza mali za Serikali katika daftari hilo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji kukubali hoja ya Mkaguzi, Kamati ilibaini kwamba hoja hiyo ilijitokeza kwa vile Watendaji walikuwa hawana uelewa kwamba tathmini ya mali ilikuwa ikihitajika na dhamani yake ilitakiwa iingizwe katika hesabu za Baraza ili kuonesha sura halisi ya mali (viwanja) inazozimiliki. Sambamba na hilo, Kamati yetu imegundua kuwa tayari Baraza limeshaomba katika Wizara husika kupitia barua nambari BMZ/97/5/130 ili wataalamu waweze kuja kuwafanyia tathmini hiyo. Hata hivyo, Kamati yetu imeridhika na majibu ya Baraza kwa vile Kamati imeona kuna juhudi za kurekebisha kasoro hiyo.

**Hoja nambari 6.10.5.2: Matumizi mabaya ya fedha za Umma shilingi 3,003,808,085**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kupitia hesabu za mwisho wa mwaka Baraza la Mitihani Zanzibar liliwasilisha matumizi yanayohusiana na usimamizi na usahihishaji mitihani ya taifa ya elimu ya Msingi na Sekondari ya awali yenye thamani ya shilingi 3,003,808,085 kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa matumizi ya shilingi 3,003,808,085 zilizotumika kwa ajili ya usimamizi na usahihishaji wa mitihani.
- Kukosekana kwa mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo jambo ambalo

limepelekea kushindwa kushibitisha kilichonunuliwa pamoja na thamani halisi ya kilicholipwa.

- Kukosekana kwa taarifa za kumbukumbu za matumizi hayo.
- Kukosekana kwa muongozo wa ulipwaji wa wasimamizi wa mitihani, watungaji wa mitihani, wasafirishaji, wasahihishaji na washughulikiaji wa mitihani jambo ambalo linapelekea Baraza kulipa thamani ndogo ya fedha ambayo haiendani na ugumu wa kazi yenyewe.
- Walimu kutokuwa na hamasa ya kushughulikia zoezi zima la mitihani kuanzia kutunga kusimamia kusainisha na hata kutoa matokeo kutokana na malipo dhaifu wanayolipwa na Baraza la Mitihani kutokana na kukosekana kwa muongozo wa malipo.

Kutokana na dosari zilizoainishwa hapo juu ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Elimu kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha wanatoa kipaumbele kwa walimu na washughulikiaji wa mitihani kuwapatia malipo stahiki kutokana na ugumu wa kazi wanayoifanya vyenginevyo inaweza ikajitokeza thamani ya elimu kushuka kutokana na walimu kupoteza ari ya kazi yao.

**Majibu ya Wizara**

- Kuhusu vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa matumizi hayo kwa ajili ya usimamizi na usahihishaji wa mitihani vipo na vimekamilika.
- Kuhusu mchanganuo wa kilichonunuliwa na thamani halisi ya kilicholipwa vipo na vimeambatanishwa katika vocha husika.
- Muongozo wa ulipaji wasimamizi wa mitihani, watungaji, wasafirishaji na washughulikiaji umeshaandaliwa na umeanza kutumika kwa kuwapa vipaumbele walimu.
- Kuhusu malipo ya walimu wasimamizi yameimarishwa katika muongozo huo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na majibu yaliyotolewa na Watendaji wa Baraza la Mitihani Zaznibar, hata hivyo, Kamati ya PAC haikuridhishwa na majibu Hayo kwa imeweza kubaini shilingi bilioni 3 zimepotea kutokana na uzembe wa baadhi ya Watendaji. Aidha, vielelezo vilivyowasilishwa mbele ya Kamati na Watendaji wa Baraza vilikosa usahihi na uhalali wa kuwa ni vielelezo thabiti kwani vingi vyao vilikuwa sio vya mwaka husika na hivyo vya mwaka husika vilikosa kuwekwa alama ya Mkaguzi. Kutokana na udhaifu uliobainika, Kamati ya PAC haikuweza kuvikubali vielelezo hivyo na kukubaliana na Mkaguzi kwamba watendaji wa Baraza wanayo hoja ya kujibu. Hivyo hoja hiyo imebakia pasi na kupata majibu yaliyosahihi.

Kufuatia kadhia hiyo, Kamati imepokea nakala za dokezo kutoka kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mheshimiwa Lela Mohamed Mussa inayoelezea hatua stahiki ambazo ameanza kuzichukua za kumuelekeza Mkaguzi Mkuu wa Ndani kuunda Kamati Maalum ya kufanya Ukaguzi Maalum kuchunguza matumizi ya shilingi Bilioni 3

zilizotumika katika mwaka 2020/2021. Hatua hiyo ni ya busara itakayoweza kutupatia majibu na hatua stahiki za kutekelezwa dhidi ya wafanyakazi wote watakaogundulika wamehusika na ubadhirifu wa matumizi ya fedha za Serikali

Kuhusiana na hoja ya kutokuwepo kwa muongozo wa Baraza la Mitihani Zanzibar, Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mkaguzi inafanya kazi zake za ukaguzi katika Baraza hilo, muongozo wa malipo na posho maalum za Baraza la Mitihani Zanzibar ulikuwa haupo, hati hivyo, kwasasa muongozo huo upo ambao uliandaliwa na kusainiwa mwaka 2022 muda ambao Mkaguzi alikuwa ameshakamilisha kazi zake za Ukaguzi katika Baraza hilo na kuwasilisha hoja alizozigundua.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Serikali kupitia Wizara husika ihakikishe inalichunguza kwa undani suala la upotevu wa shilingi bilioni 3 zilizotumika kuidanganyifu katika usimamizi na usahihishaji wa mitihani ili iweze kubaini wahusika wote waliohusika kufanya uzembe na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.
2. Muongozo uliondaliwa unaosimamia maslahi ya walimu wetu utumike iposavyo ili lengo la kuwapatia stahiki zao ziweze kupatikana bila ya usumbufu wowote.

OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU

**Taarifa ya Mapato**

Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 1,109,500,000. Kati ya fedha hizo shilingi 756,900,000 kwa ajili ya mshahara na shilingi 352,600,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,015,144,043 ziliingizwa na kutumika ambazo ni sawa na asilimia 91 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 892,270,193 zilitumika kwa ajili ya mshahara sawa na asilimia 118 ya makadirio na shilingi 122,873,850 zilitumika kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 35 ya makadirio.

**Majibu ya Wizara**

Mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ilikadiria kutumia fedha kama ifuatavyo:

| **Aina ya Matumizi** | **Makadirio ya Fedha** | **Fedha Zilizopatikana** | **%** |
|---|---|---|---|
| Mishahara | Tsh. 736,800,000/ | Tsh. 892,270,193/ | 121 |
| Matumizi ya Kawaida | Tsh.366,680,000/ | Tsh.122,673,850/ | 33 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jumla** | **Tsh.1,103,480,000/** | **Tsh.1,014,944,043/** | **92** |

**Mishahara**

Kiasi cha fedha kilichokadiriwa kwa malipo ya mshahara na stahiki za wafanyakazi kwa mwaka ilikua ni Sh. 736,800,000/ na kilichopatikana ni Tsh. 892,270,293 sawa na asilimia 121%,Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa watendaji 27ambaomni walimu waliohamishiwa kutoka skuli wanazofundisha na kuwa wakaguzi.

**Matumizi ya kawaida**

Ofisi ilikadiria kutumia Tsh. 366,680,000/ kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021 Ofisi ilifanikiwa kupata fedha Tsh. 122,673.850/sawa na asilimia 33% .miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa skuli ambapo Jumla ya skuli 760 kati ya 900 zilikaguliwa sawa na 84% ukaguzimkuu 250, ukaguzi wa somo200,ufuatiliaji 220, kushtukiza 50 na ukaguzi wa usajili 40. Aidha, Ofisi imeendesha vikao vya Bodi ya Vikao 4 vya bodi na 8 vya kamati vilifanyika sawa na asilimia 100.

Wadaiwa wa muda mrefu walioanza kulipa madeni yao ya Mikopo jumla yao ni 78 ambao wanadaiwa shilingi 1,035,707,973 na tayari wameshalipa shilingi 67,428,245. Wanufaika wa mikopo wa muda mrefu wanaoendelea kutafutwa jumla yao ni 121 na gharama wanazodaiwa ni **885,335,725.69.**

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba matumizi ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Zanzibar hususan kwenye malipo ya mishahara imezidi kwa vile kulikuwa na ongezeko la jumla ya Wakaguzi 26 waliohamishiwa Ofisi hiyo kwa barua E/M3/C7/VOL.V/ iliyowajumuisha walimu Kamaria Nasser Ahmed, Asha Bushir Khatib, na Ali Mussa Faki. Kamati imeridhika na majibu hayo.

**6.10.4: AFISI YA MRAJIS WA BARAZA LA ELIMU ZANZIBAR**

**Taarifa ya Mapato**

Ofisi ya Mrajis wa Baraza la Elimu Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 215,700,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Ofisi ya Mrajis wa Elimu Zanzibar ilikusanya jumla ya shilingi 141,018,343 sawa na asilimia 65.37 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba mapato ya Afisi hii ndio yale yale ya Wizara. Hali imetokana na Afisi hii kuwa tofauti na Ofisi nyengine maana inafunga hesabu zake za

kila mwisho wa mwaka kwa vile inapokea ruzuku. Aidha, mapato ya Afifi hii yameonekana kupungua kutokana na uwepo wa athari ya uviko 19. Kamati imeridhika na majibu hayo.

**Taarifa ya Matumizi**

Ofisi ya Mrajis wa Baraza la Elimu Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 264,200,000. Kati ya fedha hizo shilingi 154,000,000 kwa ajili ya mishahara, na shilingi 110,200,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 197,526,722 ziliingizwa na kutumika ambazo ni sawa na asilimia 75 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 145,176,831 zilitumika kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 94 ya makadirio, na shilingi 52,349,891 zilitumika kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 47 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Baada ya kupokea majibu ya Afisi hii, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.10.4.1: Kutofikia lengo la ukusanyaji wa mapato shilingi 74,681,657**

Ofisi ya Mrajis wa Baraza la Elimu ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 215,700,000 kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 ilikusanya jumla ya shilingi 141,018,343 ambazo ni sawa na asilimia 65 ya makadirio na kuwa na upungufu wa shilingi 74,681,657 sawa na asilimia 35 ya upungufu. Aidha, ukaguzi umebaini kutokufi kiwa kwa malengo yaliokusudiwa kunatokana na uwepo wa dosari zifuatazo:-

- Kukosekana kwa ufuatiliaji wa madeni ya wanafunzi.
- Kutokusimamia vyema ukusanyaji kwa mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato vinavyozalisha au kukodishwa kwa ajili ya kutoa huduma nyenginezo za Mrajis wa Baraza la Elimu.

Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato kunaweza kupelekea kushindwa kutekelezeka kwa baadhi ya malengo waliojipangia kwa wakati na muda husika. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Mrajis wa Baraza la Elimu kuhakikisha unaweka mfumo imara ambao utapelekea kuongezeka kwa makusanyo ya mapato yaliyokusudiwa iwapo watasimamia vyema vyanzo vya mapato. Mchanganuo wa makadirio na makusanyo halisi ya vyanzo vya mapato ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 183: Mapato yaliyokusanywa ambayo hayakufi kia lengo**

| Chanzo cha makusanyo | Makisio | Kilichokusanywa | Tofauti (%) |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| Usajili wa leseni za skuli binafsi | 115,700,000 | 91,608,840 | 79 |
| Leseni za walimu | 100,000,000 | 49,409,503 | 49 |
| Jumla | **215,700,000** | **141,018,343** | 65 |

**Majibu ya Wizara**

Leseni ya ualimu, usajili wa skuli na vyuo vya ualimu ni vyanzo vikuu vya mapato katika Afisi ya Mrajis wa Elimu. Leseni za walimu hulipwa kwa kipindi cha miaka mitano kwa walimu waliosomea fani ya ualimu au mwaka mmoja kwa ambao hawakusomea fani ya ualimu. Hivyo malipo hutegemea maombi katika mwaka husika. Kutokana na halihiyo kuna uwezekano mkubwa wa kutofikiwa kwa makadirio kutokana na upokeaji wa maombi ya leseni kwa kuzingatia kumalizika kwa muda wa matumizi ya leseni husika.

Pia, bei ndogo ya leseni ya ualimu ambayo haiendani na wakati wa sasa. Kwa mfano; leseni ya Astashhada ya Ualimu ni shilingi 5000, leseni ya stashahada shilingi 6000, leseni ya shahada ya kwanza shilingi 7000 na shahada ya pili na kuendelea ni shilingi 10,000.

Afisi ilitegemea kuwepo kwa ajira za walimu wapya ili kuweza kufikia kiwango cha makadirio ya fedha yatokanayo na leseni za walimu wapya lakini kwa kipindi hicho hakukuwa na ajira.

Kwa sasa Afisi inaendelea na utaratibu wa ubadilishaji wa leseni za walimu kutoka makaratasi na kwenda elektroniki. Hivyo Afisi ilikadiriya kupata jumla ya fedha 21,714,000/- kulingana na idadi ya walimu na elimu zao kwa bahati mbaya fedha hizo hazikupatikana kutokana na kuchelewa kwa utaratibu mzima wa mkato kufuatia kuwepo kwa maamuzi katika ngazi tofauti za Wizara ya Elimu na Wizara ya Fedha. kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Chanzo chengine cha mapato ni malipo ya usajili wa skuli na vyuovya ualimu ambavyo hulipwa kwa kila mwaka baada ya Skuli au Chuo kusajiliwa. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya skuli 68 za binafsi zimesajiliwa.

Kuhusiana na kukosekana kwa ufuatiliaji wa madeni ya wanafunzi, Ufuatiliaji unafanyika kwa kila robo ya mwaka. Afisi ilichukua hatua za kufuatilia malipo ya usajili wa skuli kulingana na idadi sahihi ya wanafunzi ambapo afisi ilipanga kuzifuatilia jumla ya skuli 1,050 kwa skuli za serikali na binafsi (470 za Serikali na 580 za Binafsi) kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Jumla ya skuli 921 zilifikiwa sawa na asilimia 87.7 kwa mwaka huo wa fedha, ambapo Mkoa wa Mjini Magharibi skuli 478, Mkoa Kaskazini Unguja skuli 106, Mkoa kusini Unguja skuli 154, Mkoa Kaskazini Pemba skuli 89 na Mkoa Kusini Pemba skuli 94.

Kutopatikana kwa takwimu sahihi za wanafunzi hasa kwa zile skuli ambazo zina idadi

kubwa ya wanafunzi kutokana na uhamaji wa mara kwa mara kwa wanafunzi kutoka skuli moja kwenda nyengine. Pia, uwepo wa nyakati tafauti za uandikishaji wa wanafunzi wapya kunapelekea kukosekana kwa taarifa zinazochangia kupatikana kwa takwimu sahihi malipo haraka iwezekanavyo. Hivyo tunashukuru kwamba walimu na wamiliki wa skuli waliitikia vyema agizo hilo.

Kutokusimamia vyema ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo mbali mbali vinavyozalisha au kukodishwa kwa ajili ya kutoa huduma nyenginezo za Mrajis wa Baraza la Elimu. Afisi ya Mrajis wa Elimu hukusanya mapato ya Serikali yanayotokana na vyanzo vikuu vya leseni ya ualimu, usajili wa skuli Binafsi na Vyuo Binafsi vya ualimu. Kwa muktadha huu Afisi inaendelea kusimamia vyema ukusanyaji wa mapato yanayotokana na vyanzo vyake isipokuwa makadirio yaliyopangiwa na Serikali ni makubwa ukilinganisha na vyanzo vilivyopo, Uhalisia ni kwamba skuli zilizosajiliwa za binafsi 703 walimu waliopatiwa leseni 17,147 ukizingaia ada zinazotozwa ni ndogo. Aidha, Afisi imejipanga kufanya matipio ya ada hizo ili mapato yaweze kuongezeka. Aidha, Afisi ya Mrajis wa Elimu haina chanzo cha kukodisha ambacho kitakachopelekea kupatikana kwa mapato ya Serikali.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Baada ya Kamati ya PAC kuyapitia na kujadiliana, imeridhika na majibu na haikuwa na hoja zaidi.

### 6.11.1: FUNGU L01 - WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

### Taarifa ya Mapato

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 113,035,689,777. Kati ya fedha hizo shilingi 42,707,249,777 kutoka Serikali Kuu, shilingi 59,860,176,000 kutoka kwa Washirika wa Mendeleo na shilingi 10,468,264,000 zikiwa ni Makusanyo kutoka Vyanzo vya Ndani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ilipokea shilingi 37,476,202,629 kutoka Serikali kuu ambapo ni sawa na asilimia 88 ya makadirio, na ilipokea shilingi 20,945,742,820 kutoka kwa Washirika wa Mendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 34 ya makadirio ya fedha zilizotarajiwa kupokelewa kutoka kwa Washirika wa Mendeleo. Aidha, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi 5,080,418,228 kutoka vyanzo vyake vya ndani sawa na asilimia 49 ya makadirio.

### Majibu ya Wizara

Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo haikuweza kufikia lengo kamili la makusanyo kutokana na chanagamoto mbali mbali zikiwemo:

a) Kuweo kwa mzao mdogo wa Karafuukwa mwaka huu wa fedha ambapo

mashamba yalioyokodishwa ni mashamba ya eka tatu kwa Pemba na shamba la Giningi lililopo Kizimbani Unguja.

b) Kuwepokwa janga la Maradhi ya Korona kulipelekea kupungua kwa mapato yatokanayo na uingiaji wa wageni.

c) Kukosekana kwa mapato ya bahari kuu kulikosababishwa na kutokuwepo na meli za kigeni ambazo ziliondoka baada ya kubadilishwa masharti ya leseni za uvuvi wa bahari kuu tokea 2019.

| Kifungu | Chanzo cha mapato | Bajeti | Makusanyo halisi | % |
|---|---|---|---|---|
| 1422022 | Ada ya mazao ya misitu | 150,000,000 | 330,857,800 | 221 |
| 1422023 | Ada ya uuzaji wa mawe, mchanga na kokoto | 6,700,764,000 | 2,570,375,810 | 38 |
| 1421001 | Mauzo ya uzalishaji wa miche | 7,000,000 | 2,265,800 | 32 |
| 1422060 | Mapato ya mashamba | 360,000,000 | 7,175,000 | 2 |
| 1422048 | Ada ukaguzi wa mazao | 98,000,000 | 323,127,750 | 330 |
| 1422026 | Leseni za uvuvi | 180,000,000 | 37,848,500 | 21 |
| 1422027 | Ada ya mazao ya baharini | 340,000,000 | 236,835,760 | 70 |
| 1421011 | Utibabu wa wanyama | 90,000,000 | 1,541,283,908 | 1713 |
| 1422068 | Mapato ya mifugo | 2,500,000 | 12,709,400 | 508 |
| 1422066 | Ada ya uingizaji wageni | 20,000,000 | 3,432,000 | 17 |
| 1423002 | mauzaji ya mazao na miche | 20,000,000 | 14,506,500 | 73 |
| 1422067 | mapato ya uvuvi wa bahari kuu | 2,500,000,000 | | 0 |
| **Jumla** | | **10,468,264,000** | **5,080,418,228** | **49** |

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC ilitaka kujua kwanini mapato ya leseni za uvuvi na mapato ya ada ya mazao ya Baharirini yalihamishwa mwezi wa Febuari kupelekwa Wizara ya Uchumi wa buluu lakini kuna mapato yalikusanywa na kuingizwa Wizara ya Kilimo na kuelezwa kwamba kulikuwa na baadhi ya walipaji walikuwa hawajui kama mapato hayo yamehamishwa.

Kwa upande wa mapato ya mashamba ya mikarafuu, Kamati yetu imepata wasiwasi

kwamba kwa mwaka mzima wa 2020/2021, kulikusanywa jumla ya shilingi 7,175,000 kwa makadirio ya shilingi 360,000,000 sawa asilimia 2. Hali hiyo inaonesha wazi kwamba kiuhalisia hayo ni mapato ya Shamba moja tu la Makue ukiachia mbali mashamba mengine yaliyopo Unguja na Pemba.

Kamati haikuridhishwa na majibu hayo na imegundua kwamba kuna upotevu mkubwa wa fedha za Serikali unafanyika au watendaji huwa hawawasilishi taarifa zilizokuwa sahihi Serikalini. Kwa mantiki hiyo, Kamati iliomba kupatiwa mchanganuo wa makusanyo ya Mikarafuu katika mashamba yote ya Unguja na Pemba kwa mwaka huo wa fedha ambapo hadi Kamati inakamilisha ukaguzi wake hakuna mchanganuo uliowasilishwa.

Kamati pia ilichunguza kwa undani zaidi na kugundua kwamba hakukuwa na mchangauo wa makusanyo hayo katika taarifa ya mwisho wa mwaka (Financial Statement) pamoja na kuwepo kwa utofauti wa asilimia ya makusanyo baina ya Mkaguzi na Wizara. Hali hiyo ilitoa taswira ya wasiwasi wa taarifa za hesabu ya mwisho za Wizara ya Kilimo.

Mapendekezo ya kamati ya PAC

1. Wizara ihakikishe inaandaa hesabu zake za mwisho wa mwaka zenye sura halisi na sahihi ya taarifa zinazohitajika.
2. Wizara ifuatilie na kusimamia kwa karibu makusanyo ya mapato yake hususan yanayotokana na mashamba ya mikarafuu na kuyawasilisha Serikalini.

Taarifa ya Matumizi

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi 21,707,249,777 kwa kazi za kawaida na jumla ya shilingi 80,860,176,000 kwa kazi za maendeleo; (shilingi 21,000,000,000 kutoka SMZ na shilingi 59,860,176,000 kutoka kwa wahisani).

Hadi kufikia 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 16,530,459,809 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 76 na jumla ya shilingi 498,000,000 zimeingizwa kutoka Serikalini kwa kazi za miradi ya maendeleo sawa na asilimia 2 ya makadirio. Aidha, jumla ya Shilingi 20,447,742,820 zilipatikana kutoka kwa Wahisani wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 34 ya makadirio.

Majibu ya Wizara

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi 21,707,249,777 kwa kazi za kawaida na jumla ya shilingi 80,860,176,000 kwa kazi za maendeleo; (shilingi 21,000,000,000 kutoka SMZ na shilingi 59,860,176,000 kutoka kwa Wahisani).

Hadi kufikia Juni 30, 2021, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo iliingiziwa

jumla ya shilingi 16,530,459,809 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 76 ya makadirio ya fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 10,236,935,592 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 1,595,238,583 kwa matumizi mengineyo na shilingi 4,698,285,634 ni ruzuku kwa Taasisi (Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Taasisi ya Utafiti wa mifugo na Wakala wa Serikali wa Zana za Kilimo na Huduma za Matrekta.

Kutokana na asilimia ya upatikanaji wa fedha Wizara imeweza kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa kiasi kikubwa kama yalivyoainishwa kwenye ripoti hii.

Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Juni 30, 2021, jumla ya shilingi 20,945,742,820 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 26 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 498,000,000 ni mchango Serikali kwa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 2 ya makadirio. Shilingi 20,447,742,820 sawa na asilimia 34 ya makadirio kutoka kwa Wahisani.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 102,567,425,777. Kati ya fedha hizo shilingi 10,365,921,974 kwa ajili ya mishahara, shilingi 4,900,048,531 kwa matumizi mengineyo, shilingi 21,000,000,000 na shilingi 59,860,176,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo na shilingi 6,441,279,272 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 37,476,202,629 ziliingizwa na kutumika sawa na asilimia 37 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 10,236,935,592 zimeingizwa na kutumika kwa mishahara sawa na asilimia 99 ya makadirio, shilingi 1,595,238,583 zimeingizwa kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na silimia 33 ya makadirio, shillingi 4,698,285,634 zimeingizwa ikiwa ni ruzuku kwa Kutoka Serikalini kwa taasisi zinazopewa ruzuku zilizopo chini ya Wizara sawa na asilimia 73 ya makadirio.

Aidha; Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilipokea shilingi 498,000,000 ikiwa ni mchango wa Serikali katika matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 2 ya makadirio na shilingi 20,447,742,820 ikiwa ni mchango wa Washirika wa Maendeleo katika matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 34 ya makadirio.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imegundua kwamba kuna utofauti wa fedha za matumizi zilizoainishwa na Mkaguzi na zilizoainishwa na Wizara na kuelezwa kwamba tofauti hiyo ilitokana na kugawanywa kwa Wizara ya Kilimo na Uchumi wa Buluu katika mwezi wa Febuari.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ihakikishe inaweka vizuri taarifa zake ambapo hata kama kutatokea kugawanywa kwa Wizara taarifa sahihi zinakuwepo na zikihitajika zinapatikana.

**Hoja nambari 6.11.1.1: Dosari zilizobainika katika Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2020/2021.**

Kwa mujibu wa muongozo wa uandaaji wa Taarifa za Hesabu uliotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kitengo cha Mhasibu Mkuu uliwataka Wahasibu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuainisha taarifa kuhusu mambo mbali mbali pamoja na yale yaliyozoeleka katika kipengele cha Maelezo ya Taarifa za Hesabu (Notes of Financial Statement) kama yalivyotajwa hapo chini.

a) Maelezo kuhusu Madeni (Debtors and Creditors);
b) Maelezo kuhusu Bakaa za Mali (Stock);
c) Maelezo kuhusu Mali Zisizohamishika (Asset List);
d) Maelezo kuhusu Ruzuku zinazoingizwa Wizarani kwa ajili ya Taasisi Tanzu za Wizara; na
e) Muhtasari wa Matumizi yake (Subvension Allocation with Expenses).

Ukaguzi umepitia hesabu za Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo za mwaka ulimalizika tarehe 30 Juni, 2021 na kubaini kutokuepo kwa maelezo ya hayo katika kipengele cha Maeelezo ya Taarifa za Hesabu (Notes of Financial Statement).

Kukosekana kwa maelezo hayo katika kipengele cha Maelezo ya Taarifa za Hesabu (Notes of Financial Statement) hizo ni kuenda kinyume toleo la Mhasibu Mkuu kuhusu uandaaji wa Taarifa za Hesabu kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha kufanya hivyo ni kuenda kinyume na viwango vya kiuhasibu vya kimataifa (IPSAS).

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imepokea ushauri uliotolewa na mkaguzi na inaendelea kufuata muongozo wa uandaaji wa Taarifa za Hesabu uliotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kitengo cha Mhasibu Mkuu, muongozo ambao unawataka waandaaji wa taarifa za hesabu za Wizara/Taasisi kuainisha taarifa kuhusu mambo mbali mbali pamoja na yale yaliyozoeleka katika kipengele cha Maelezo ya Taarifa za Hesabu (Notes of Financial Statement). Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara imeandaa hesabu zake kwa kuzingatia muongozo huo ili taarifa hizo ziende sambamba na viwango vya uhasibu vya kimataifa (IPSAS).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC baada ya kufuatilia kwa undani hoja hiyo, imegundua kwamba ni kweli taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka 2020/2021 ilikuwa na makosa mengi kama ilivyoelezwa na Mdhibiti ikiwemo kutokuainishwa kwa taarifa za mali ikijumuisha kutooneshwa taarifa za madeni wanayodai na wanayodaiwa ya Wizara ya Kilimo. Kamati ilitaka kujua sababu ya kutofuata muongozo wa uandaaji hesabu za mwisho wa

mwaka na kuelezwa kwamba hali hiyo ilitokana na makosa ya kibinadamu. Hata hivyo, Kamati yetu imebaini kwamba Watendaji wa Wizara walikuwa wazembe kwani muongozo ulikuwa unaelekeza mambo yote ya msingi wanayotakiwa kuyazingatia wanapoandaa hesabu zao.

Aidha, watendaji wa Wizara hawakuwa na mashirikiano wao wenyewe pamoja na Wizara ya Fedha ili kuweza kubaini mapema changamoto ya mambo ambayo hawakuyatekeleza.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wizara ya Kilimo waache kufanya kazi kwa mazoea na wawe tayari kufuata miongozo ya uandaaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ili waweze kwenda sambamba na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Hoja nambari 6.11.1.2: Kuchelewa kuwasilishwa kwa Taarifa za Hesabu za Mwaka 2020/2021.**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 119 (1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, Taasisi za Umma zinatakiwa kuwasilisha Taarifa za Hesabu za Mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha.

Ukaguzi umebani kwamba Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo iliwasilisha taarifa zake hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar mnamo tarehe 12/10/2021, hivyo Wizara ilichelewa kuwasilisha taarifa hizo kwa muda wa siku kumi na mbili.

Kuchelewa kuwasilisha Taarifa za Hesabu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar ni kuenda kinyume na kinyume na vifungu namabri 119 (1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Wizara**

Uongozi wa Wizara unakubaliana na hoja ya mkaguzi na kuahidi kuwa tatizo hili halitajirejea tena kwani lilisababishwa wakati wa Maandalizi ya Taarifa za Fedha (Financial Statement for (2020/2021) Muhasibu Mkuu wa Wizara alikuwa kwenye hali ya Ugonjwa na hatimae alifariki dunia. Ingawa Wizara ilichukua hatua za haraka kufanya maandalizi hayo baada ya kuonekana hali yake kiafya ilivyokuwa inaendelea. Aidha, kazi za uandaaji wa taarifa hizi za fedha zinahitaji uzoefu mkubwa. Kwa sasa Wizara

imeshapatiwa Mhasibu Mkuu mwengine na imewasilisha kwa wakati taarifa za fedha za mwaka 2021/2022.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Wizara imekubaliana na hoja ya Mdhibiti bila ya kuonesha chembe ya kukanusha, Kamati ya PAC haikuwa na maelezo ya ziada hasa ukizingatia hivi sasa changamoto hiyo imesharekebishwa. Hata hivyo, Kamati yetu imekemea tabia ya kazi za Taasisi kufanywa na Mtendaji mmoja pasi na kuwashirikisha watendaji wengine kwani hali hiyo huwa haioneshi taswira nzuri kiuwajibikaji hasa ukizingatia Taasisi inawajibika kwa pamoja.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Katika utekelezaji wa majukumu yao, Watendaji wa Wizara wawe na utaratibu wa kufanya kazi kwa pamoja ili ikitokezea mmoja hayupo mwengine anakuwa anaelewa kinachofanyika katika Ofisi yao.

**Hoja nambari 6.11.1.3: Kutokuanisha kwa Makusanyo ya Mapato yaliyopokelewa kwenye Nambari za Benki za Idara ya Misitu yenye Thamani ya Shilingi 1,483,400,503.47**

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Misitu inamiliki nambari za Benki mbali mbali ambazo inakusanyia mapato kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani. Mapato hayo hukusanywa kutoka katika hifadhi za Misitu, mauzo ya mazao ya misitu, fedha kutoka kwa wahisani na adhabu zinatozwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za usimamizi wa rasilimali za Misitu.

Aidha, Ukaguzi umepitia Taarifa za Hesabu za Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na kubaini kwamba jumla shilingi 1,483,400,503.47 ambazo zimekusanywa na Idara ya Misitu kutoka vyazo vyake vya ndani hazikuainishwa katika taarifa hiyo. Taarifa za mapato hayo ni kama zinavyonekana katika jadweli nambari 3 hapo chini:-

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa vya IPSAS na pia ni kwenda kinyume na vifungu nambari 27, 30 (2) na 34 vya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Jadweli Nambari 186: Makusanyo ya Mapato ambayo hayakuainishwa katika Taarifa za Hesabu za mwaka 2020 - 2021**

| Nambari ya Benki | Jina la nambari ya Benki | Jina la Benkina Tawi | Mapato yaliokusanywa kwa 2020-2021 (Tshs) | Jumla (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 404206000 | Mfuko wa Maendeleo ya Misitu | PBZ – Forodhani Branch TZS | 215,206,846.13 | 215,206,846.13 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 406009000 | Kiwengwa - Pongwe Forest Reserve | PBZ – Forodhani Branch TZS | 4,464,500.00 | 4,464,500.00 |
| 730065001 | Jozani Chwaka Bay Conservation | PBZ – Forodhani Branch TZS | 876,796,159.36 | 876,796,159.36 |
| 0404288000 | Maendeleo na Huduma za Kilimo | PBZ – Forodhani Branch TZS | 384,552,997.98 | 384,552,997.98 |
| 0404288000 | Maendeleo ya Huduma ya Kilimo | PBZ – Forodhani Branch TZS | 2,380,000.00 | 2,380,000.00 |
| **Jumla** | | | | **1,483,400,503.47** |

**Majibu ya Wizara**

Wizara kweli ilikusanya fedha TZS.1,483,400,503.47 kupitia Idara zake na kuweka kumbukumbu zote stahiki pamoja na vielelezo vya makusanyo hayo ila jambo ambalo kitengo cha uhasibu kilishindwa kukamilisha kwa mujibu wa standards ni kutokuainisha kwenye taarifa za hesabu za mwaka 2020/2021, hii ilitokana na uelewa wa kuingizwa taarifa za fedha ambazo hazipo kwenye System. Hata hivyo Wizara imezingatia ushauri huo uliotolewa na mkaguzi na kwa mwaka wa fedha 2021/2022 taarifa hizo zimeainishwa.

**Hoja nambari 6.11.1.4: Kutokuanisha kwa bakaa lenye thamani ya Shilingi 981,065,601.36 katika Taarifa za Hesabu za Mwaka 2020/ 2021.**

Ukaguzi ulipitia taarifa za nambari za Benki za Idara ya Misitu pamoja na Taarifa ya Hesabu ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na kubaini kwamba jumla ya shilingi 981,065,601.36 ambazo zilibakia katika nambari za Benki hizo hazikuanishwa katika Taarifa ya Hesabu ya Wizara ya mwaka 2020 /2021.

Jadweli nambari hapo chini linaonesha taarifa za bakaa la fedha katika nambari za Benki za Idara yaMisitu hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021.

**Jadweli Nambari 187: Makusanyo ya Mapato ambayo hayakuainishwa katika Taarifa za Hesabu za mwaka 2020 -2021**

| Nambari ya Benki | Jina la Nambari ya Benki | Jina la Benki na Tawi | Mapato yaliyokusanywa kwa 2020 -2021 (Tshs) | Jumla (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 404206000 | Mfuko wa Maendeleo ya Misitu | PBZ – Forodhani Branch TZS | 69,901,172.82 | 69,901,172.82 |
| 406009000 | Kiwengwa - | PBZ – | 15,998,066.45 | 15,998,066.45 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Pongwe Forest Reserve | Forodhani Branch TZS | | |
| 730065001 | Jozani Chwaka Bay Conservation | PBZ - Forodhani Branch TZS | 792,251,439.08 | 792,251,439.08 |
| 775026001 | Jozani Chwaja Bay Conservation | PBZ – Forodhani Branch USD | USD 6,362.00 | 14,632,600.00 |
| 0404288000 | Maendeleo ya Huduma ya Kilimo | PBZ – Forodhani Branch TZS | 88,282,323.01 | 88,282,323.01 |
| **Jumla** | | | | **981,065,601.36** |

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na viwango vya Uhasibu vya kimataifa vya IPSAS (Cash Basis) vile vile ni kwenda kinyume na vifungu nambari 56 na 122(2) vya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Wizara**

Kwa mujibu wa kifungu 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, Wizara inasimamia, inatunza na kurikodi miamala yote inayofanyika katika hesabu hizo. Vile vile, kwa kuwa bakaa hizo zinatokana na makusanyo ambayo hayapitii Serekalini bali yanagawiwa kwa Wadau husika kwa mujibu wa sheria na kanuni husika zilizowekwa; Wizara haikuzianisha bakaa hizo katika hesabu za mwisho.

Hivyo, Wizara inaomba kwa mujibu wa kifungu nambari 122(2)(f) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, kuziingiza taarifa zote za bakaa hizo katika hesabu zake za mwaka wa fedha 2021/2022 kwenye sehemu ya taarifa za hesabu (Disclosure note), ili Hesabu iendane na viwango vya uhasibu vya kimataifa (IPSAS).

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haikufurahishwa na majibu ya Watendaji wa Wizara kwani Sheria pamoja na viwango vya kimataifa vinaelekeza kwamba makusanyo yote yanatakiwa yawasilishwe hazina na baadae ndio yaweze kutumika. Lakushangaza, Wizara imekiri kwamba kweli walikuwa hawayaingizi katika Hazina mapato wanayoyakusanya badala yake huwapatia mgao (wanajamii) vikundi vinavyozunguka msitu wa Jozani waweze kutumia na kuwasilisha marejesho ya matumizi hayo. Kwa msingi huo, Watendaji wa Wizara hawakuwa wakiyaingiza mapato ya namna hiyo katika hesabu za mwisho na kupelekea hesabu hizo kutoonesha sura halisi na sahihi. Hivyo, Kamati inaungana na hoja iliyoelezwa na Mdhibiti kati Ripoti yake.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wizara wahakikishe fedha zote za mapato zinaingizwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka kwani kufanya hivyo kutaongeza udhibiti wake.

**Hoja nambari 6.11.1.5: Kutokuwepo kwa Taarifa ya Usuluhishi (Bank Reconciliation) wa Nambari ya Benki 0404360000 ya Kukusanyia Mapato.**

Ukaguzi umepitia taarifa za mapato za Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo zilizoanishwa katika taarifa za hesabu za mwaka wa fedha 2020-2021 na baadae kulinganisha taarifa zilizopo kwenye Idara zinazohusika na ukusanyaji wa mapato hayo na kubaini kuwepo kwa tofauti baina yake.

Kutokuwepo kwa taarifa za usuluhishi wa ukusanyaji mapato unaweza kupelekea kutopata taarifa sahihi za makusanyo ya fedha hizo ni kwenda kinyume na kifungu namabri 27 (1), (2)(a) na kifungu nambari 30 (1) na ( 2) vya Sheria namba 12 ya usimamizi wa fedha za umma mwaka 2016. Ufafanuzi zaidi unapatikana katika Jadweli nambari 188 (ukurasa 249) la Ripoti ya Mdhibiti inayohusiana na Taarifa za Serikali Kuu.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inakusanya mapato kupitia vyanzo vyake ambavyo vipo katika Idara na Taasisi tofauti. Mapato yote ya Wizara hukusanywa kupitia hesabu moja tu nambari ya benki 0404360000 inayojulikana kwa jina la Wizara ya Kilimo Unguja ambayo inasimamiwa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 30(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, mapato yote hayo huwasilishwa hazina kila inapofika mwisho wa mwezi. Aidha Wizara kupitia Idara zake zote zinazokusanya Mapato zinaendelea na utaratibu wa kufanya Usuluhisho kwa kila mwezi kama ilivyo ada.

Uwepo wa hoja hii ulitokana na mabadiliko ya kitengo Idara ya Misitu chenye kujishughulisha na masuala ya Mchanga kuhamishiwa Wizara ya nyengine, iliibuwa mambo mengi ikiwemo kukabidhiana majukumu na kumbukumbu muhimu. Hali iliyosababisha kucherewa kuziwasilisha nyaraka za taarifa za msingi ikiwemo za usuluhisho na benki.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Wizara ilikubaliana na hoja ya Mdhibiti kwamba kweli hakukuwa na usuluhishi wa kibenki uliokuwa ukifanyika na hivi sasa tayari wamejirekebisha, Kamati hiakuwa na maelezo zaidi isipokuwa imewasisitiza kwamba Wizara iendelee kufanya usuluhishi wa kibenki kwani huwa unasaidia kutambua kwa haraka iwapo kutatokea kufanyika kwa makosa ya kibenki na kuyapatia ufumbuzi wa haraka.

**Hoja nambari 6.11.1.6: Kuwepo kwa watumishi ambao hawajalipwa stahiki zao za likizo.**

Kwa mujibu wa kifungu cha 58(1)(a) cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 Mtumishi wa Umma anastahiki posho la likizo kila baada ya miaka mitatu. Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo haikuwa na utaratibu mzuri wa kulipa stahiki za watumishi ndani ya muda sahihi.

Orodha ya watumishi hao kutoka maeneo wanayofanya kazi zilipatikana kwa ajili ya ukaguzi na kubainika kwamba jumla ya shilingi 86,000,000 za stahiki za likizo zilikuwa bado hazijalipwa hadi kumalizika kwa ukaguzi huu. Jadweli hapo chini linaonesha jumla ya watumishi hao na fedha wanazodai.

**Jadweli Nambari 189: Taarifa za Watumishi Wanaodai Stahiki za Likizo**

| Idara | Jumla ya Watumishi Wanaodai | Kima cha Poshola Likizo (Tshs) | Jumla (Tshs) |
|---|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 17 | 100,000 | 1,700,000 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 2 | 100,000 | 200,000 |
| Idara ya Maendeleo ya Mifugo | 131 | 100,000 | 13,100,000 |
| Idara ya Mistu na Maliasili Zisizirejesheka | 333 | 100,000 | 33,300,000 |
| Idara ya Umwagiliaji Maji | 63 | 100,000 | 6,300,000 |
| Idara ya Kilimo | 126 | 100,000 | 12,600,000 |
| Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe | 17 | 100,000 | 1,700,000 |
| Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar | 171 | 100,000 | 17,100,000 |
| **Jumla** | | | **86,000,000** |

Kufanya hivyo ni kuenda kinyume kifungu cha 58(1)(a) cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014. Vile vile kutokuwalipa stahiki zao watumishi hao ndani ya muda kunaweza kukapelekea kushuka kwa ufanisi katika utendaji kazi.

**Majibu ya Wizara**

Wizara inakubaliana na hoja ya Mkaguzi ya kuwepo kwa taarifa za madeni ya watumishi. Wizara imefanya juhudi ya kuwalipa watumishi hao stahiki zao kwa kila inapopata fedha ili kuweza kupunguza idadi kubwa ya watendaji ambao hawajalipwa stahiki zao. Kuanzia Julai 2021 hadi kufikia Oktoba 2022 takriban watumishi 338 wameshalipwa stahiki zao. Hata hivyo Wizara inaendelea kulipa stahiki hizo kupitia Idara husika badala ya kulipwa moja kwa moja kutoka Ofisi kuu ya Wizara. Hali hii imepunguza kutokuwepo na mrundikano mkubwa wa madeni haya kama ilivyokuwa hapo awali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na majibu ya kutia moyo yaliyotolewa na Wizara, Kamati yetu ilitaka kujua kwamba ni kiasi gani cha deni ambalo Wizara imeshalipa na kuelezwa jumla ya shilingi 30,000,000 zimelipwa kwa Watumishi na kubakia milioni 56. Kamati imefanikiwa kuona

orodha ya Watumishi waliopatiwa malipo husika. Kwa vile Wizara imeanza kulipa deni hilo na Kamati yetu kuthibitisha hilo pamoja na kuahidi kuendelea kulipa madeni hayo, hivyo, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ya Kilimo inaandaa Mpango Maalum utakaohakikisha deni la malipo ya fedha za likizo linaondoka.

**Hoja nambari 6.11.1.7: Kuwepo kwa Watumishi 165 Ambao Washamaliza Muda wa Majaribio ila Bado Hawajathibitishwa.**

Kifungu cha 9(2) cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 zimeweka ukomo wa muda wa majaribio usiozidi mwaka mmoja na nusu na baada ya hapo mtumishi wa umma anahitajika kuthibitishwa, na endapo bado mtumishi huyo hajatimiza masharti ya kuthibishwa Taasisi ya Umma inatakiwa kuchukua hatua za kumuachisha kazi.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa jumla watumishi 165 katika Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ambao wameshapindukia muda wa majaribio na bado hawajathibitishwa. Jadweli nambari lifuatalo linaonesha idadi ya watumishi hao.

**Jadweli Nambari 190: Orodha ya baadhi ya Watumishi ambao hawajathibitishwa**

| Nambari | Jina Kamili | Tarehe yaAjira | Tarehe ya Ukaguzi | Siku alizochelewa kuthibitishwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Asma Kombo Haji | 11/05/2019 | 30/06/2021 | 234 |
| 2 | Abdulrahim Bakar Mataka | 11/05/2019 | 30/06/2021 | 234 |
| 3 | Husna Saleh Juma | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 4 | Raudha Abdalla Mohammed | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 5 | Riziki Abdalla Sheria | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 6 | Rukia Mashaka Issa | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 7 | Marya Afani Othman | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 8 | Abubakar Masoud Ibrahim | 06/05/2019 | 30/06/2021 | 239 |
| 9 | Sadik Maulid Khamis | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 10 | Hassan Shaaban Idd | 06/11/2019 | 30/06/2021 | 55 |
| 11 | Yussuf Bakar Salum | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 12 | Masoud Juma Ali | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 13 | Khamis Juma Makame | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 14 | Gora Haji Gora | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 15 | Abdul-Wahid Yusuf Mohd | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 16 | Ashura Abdalla Haji | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 17 | Khamis Haji Khamis | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 18 | Moh'd Ali Mohd | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 19 | Yassir Hamad Ali | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 20 | Talib Juma Khamis | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 21 | Abdul-Latif Ramadhan Abdalla | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 22 | Wanu Makame Makbul | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 23 | Wahid Juma Khamis | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 24 | Zuhura Makame Ali | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 25 | Wanu Khamis Nyange | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 26 | Salim Athumani Guzo | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 27 | Mahamudu Faki Mohammed | 06/05/2019 | 30/06/2021 | 239 |
| 28 | Maryam Hussen Ame | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 29 | Mkasi Maulid Simai | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 30 | Mohammed Mwinyiwesa Muhija | 06/05/2019 | 30/06/2021 | 239 |
| 31 | Khadija Abdalla Habib | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 32 | Lila Makata Mwintum | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 33 | Fathia Abdalla Juma | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 34 | Haitham Bakar Khatib | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 35 | Fatma Mmaka Hamad | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 36 | Fatma Khamis Hamad | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 37 | Habiba Mkombe Pandu | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 38 | Juma Moh'd Haji | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 39 | Hamad Yussuf Ameir | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 40 | Hassan Mussa Ali | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 9(2) cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014. Vile vile kutokuwathibitisha watumishi hao kunaweza kuwakosesha stahiki na haki zao za kazi.

## Majibu ya Wizara

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ina watumishi wapatao mia moja na arubaini na tatu (143) ambao waliajiriwa kipindi cha mwaka 2019 na walitarajiwa kuthibitishwa kazi mwezi Juni 2021. Wengi wa watumishi hawa bado hawajapatiwa mafunzo ya kuthibitishwa kazini kutokana na uhaba wa upatikanaji wa fedha kwa kipindi hicho, kwa kuwa muda wa kuthibitishwa ulikuwa ni mwisho wa mwaka wa fedha wa 2020/2021, Wizara ilijipanga kuwahudhurisha wafanya kazi hao katika mafunzo ya kuthibitishwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida. Aidha katika orodha iliyotajwa hapo, jumla ya wafanyakazi 83 wameshapata mafunzo na kukabidhiwa vyeti vya mafunzo; kati yao 52 wameshathibitishwa na 31 maombi yao yapo Tume ya Utumishi Serikalini kwa ajili ya kupatiiwa kibali cha uthibitisho.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba Watendaji wa Wizara hawakuwajibika ipasavyo kwani wafanyakazi hao walikuwa wengi mno na hakukuwa na juhudi za makusudi za kuhakikisha wanafuatilia na kuwapunguza kidogo kidogo. Hivyo, Kamati yetu imesisitiza kwamba watumishi hao wafanyiwe utaratibu wa kuthibitishwa haraka iwezekanavyo ili hoja kama hii isije ikajirudia tena mwaka ujao wa ukaguzi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaitaka Wizara ichukue juhudi za makusudi kuhakikisha Watumishi hao wanathibitishwa ili kuepusha kuwakosesha baadhi ya haki hususan wanapofikia muda wa kustaafu.

**Hoja nambari 6.11.1.8: Mapungufu katika Ujazaji wa Kalamazoo za Watumishi**

Ukaguzi umebaini kitengo cha utumishi chenye dhamana ya kutunza kumbukumbu za watumishi ikiwa pamoja na kujaza Kalamazoo hawajazi Kalamazoo hizo kwa ukamilifu wa taarifa zote za mtumishi. Hadi kufikia mwezi husika, Kalamazoo nyingi zilizojazwa taarifa zake zimeishia mwaka 2020.

Kutokujaza kwa ukamilifu kalamazoo kunaweza kupelekea usumbufu katika kutambua kwa uhakika taarifa za mtumishi, aidha inaweza kupelekea kukosekana taarifa kamili pale wanapojiandaa kumtengenezea haki za kiinua mgongo na pensheni pindi mfanyakazi anapostaafu. Kusita kujaza taarifa za mtumishi kunaweza kupelekea kuharibu mtiririko mzuri wa taarifa za stahiki na mikato ya mtumishi.

**Majibu ya Wizara**

Wizara inakubaliana na hoja ya kuwa na tatizo la upatikanaji wa “Folio Register sheet” katika kitengo cha Kalamazoo. Tatizo hili limesababisha kumbukumbu hizo kutohifadhiwa katika fomu hizo. Aidha, Wizara imeshalirekebisha tatizo hili na Folio tayari zimepatikana na zipo tayari kwa ukaguzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na kwamba Watendaji wa Wizara wamekiri kuwepo kwa hoja ya Mkaguzi ambayo wao hawakuifanyia kazi kikamilifu. Hata hivyo, Kamati yetu imebaini kwamba kutokujazwa kwa folio hizo kulichangiwa na kutokuwepo kwa folio husika kulikosababishwa na Wakala wa Uchapaji ambae ndio muhusika mkuu wa upatikanaji wa nyaraka hizo hakuwa nazo.

Hali hiyo ilipelekea Wizara kushindwa kupata nyaraka za kujaza taarifa za watumishi wao wakati walitakiwa waiandike barua Wakala huo ili uwapatie idhini ya kutafuta

sehemu nyengine zitakazowezesha upatikanaji wake.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inapendekeza kwamba Watendaji wa Ofisi ya Utumishi ya Wizara kuwa makini katika ujazaji wa kalamazoo wa Watumishi wao ili kuepusha haki za Watumishi wa Wizara kupotea.

**Hoja nambari 6.11.1.9: Kutokununua Vifaa vya kuandika kutoka kwa Wakala wa Mchapaji wa Serikali na Bohari Kuu.**

Kifungu nambari 35 cha Sheria ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar ya mwaka 2018 kimezitaka Taasisi zote za Serikali kupeleka kazi zake zote za uchapaji na mahitaji ya vifaa vya ofisi na vya kuandikia kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar.

Ukaguzi umebaini Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo iliafanya manunuzi ya vifaa vya kuandikia kutoka kwa wasamabazaji wengine na jumla shilingi 58,274,141 zilitumika kwa ajili manunuzi ya vifaa hivyo kutoka kwa wasambazaji ambao hawakuruhusiwa kisheria, Jadweli namabri 10 linaainisha:-

**Jadweli Nambari 191: Manunuzi ya Uchapaji na vifaa vya kuandikia**

| Code | Maelezo | Kima |
|---|---|---|
| 6112208 | Manunuzi ya Kompyuta | 17,513,088 |
| 6112209 | Manunuzi ya Mashine ya Kuchapishia (Printer) | 1,700,500 |
| 2206001 | Manunuzi ya Vifaa vya Kuandikia | 34,447,749 |
| 2206002 | Gharama za Uchapaji | 14,610,443 |
| 2206005 | Vifaa vya Kompyuta | 2,689,833 |
| **Jumla** | | **70,961,613** |

Kutokufuata utaratibu ambao umewekwa na serikali katika ununuzi wa vifaa vya ofi si ni kwenda kinyume na sheria ya 35(1) ya kifungu cha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar cha mwaka 2018.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ilifanya manunuzi ya vifaa mbali mbali. Kwa upande wa vifaa vya kuandikia na vifaa vya computer Wizara inakiri kununua vitu hivyo katika maduka yasio ya Serikali kwa sababu vifaa hivyo havikupatikana kwa Wakala wa Uchapaji. Kwa sasa Wizara inaendelea na utaratibu wa kununua vifaa kupitia Wakala wa uchapaji na hununua vifaa nje ya taasisi hiyo baada ya kupata uthibitisho wa maandishi wa kukosekana kwa vifaa husika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba Watendaji wa Wizara ya Kilimo pamoja na kukiri kwamba hawakununua vifaa kutoka Wakala wa Uchapaji lakini walikuwa hawana uelewa wa nini

wafanye iwapo vifaa wanavyovitaka havitakuwepo kwa Wakala wa Uchapaji wakati sheria ya Wakala inaruhusu ununuzi wa vifaa vya kuandikia nje ya Wakala isipokuwa kupatikane idhini kutoka Wakala wa Uchapaji itakayoruhusu ununuzi huo.

Kamati imegundua kwamba kwasasa Wizara inafuata utaratibu huo ambapo tarehe 21/6/2022 walijibiwa barua ya maombi yao na Wakala huo kupitia barua yenye kumbukumbu nambari ZGP/MV.22/12/VOL.VI125.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara iendelee na utaratibu wa kuiandikia barua Wakala wa Uchapaji kuhusu uombaji wa ruhusa ya kwenda kununua folio katika sehemu nyengine ili kuepusha hoja za Mkaguzi kujitokeza.

**Hoja nambari 6.11.1.10: Kuwepo kwa Vyombo vya Moto vilivyolala kwa Muda Mrefu.**

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inamiliki vyombo vya aina tofauti vya usafiri, Ukaguzi umebaini baadhi ya vyombo hivyo vimelala kwa sababu ya ubovu kwa muda mrefu sasa. Kuwacha vyombo vya moto vikiwa vimelala kwa muda mrefu kunaweza kupelekea kuitia hasara kubwa Wizara kwa kuongezeka kwa gharama za matengenezo au kupelekea kutotengenezeka kabisa. Baadhi ya magari yaliyolala ni kama ifuatavyo katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 192: Orodha ya Magari yaliyolala kwa Muda Mrefu.**

| Namba | Namba za Gari | Idara Inayotoka |
|---|---|---|
| 1. | SMZ 316 A Nissan na SMZ 166 B Nissan | Idara ya umwagiliaji maji. |
| 2. | SMZ 522 Toyota | Idara ya misitu |
| 3. | SMZ 478 A | Idara ya mifugo |
| 4. | SMZ 203 A Nissan | Idara ya mipango. |
| 5. | SMZ 136 A na SMZ 174 A | Taasisi ya utafiti |
| 6. | SMZ 603 A | Idara ya kilimo. |
| 7 | SMZ 166 A | Taasisi ya utafiti wa Kilimo Kizimbani |

Kuviacha vyombo hivyo vikiwa vimelala kwa ajili ya ubovu kunaweza kupelekea kuharibika kabisa na kutoweza kutumika tena.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo inamiliki vyombo vya aina tofauti vya usafiri ambavyo vimekaa kwa muda bila ya matengenezo. Aidha, Wizara ilikuwa katika

mpango wa kuvifanyia matengenezo vyombo hivyo. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, hazikufanyiwa matengenezo kutokana na uhaba wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida (OC) uliosababishwa na wimbi la Uviko 19. Kwa sasa baadhi ya gari hizi zimeshafanyiwa matengenezo na nyengine zipo Karakana Kuu ya Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba katika gari ambazo Mkaguzi ameziainisha, gari moja imepelekwa ZAFICO ambayo tayari imeshafanyiwa matengenezo na inafanyakazi, gari moja SMZ ipo Wizarani lakini bado haijatengenezwa (imewekwa katika banda), gari mbili zipo karakana Kuu ya Serikali kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo na gari tano zenye namba SMZ 139A, SMZ 136A hundai, SMZ 174A, SMZ 478A (One ten) na SMZ 203A (Nissan) zipo Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ambapo moja (SMZ 139A) inafanya kazi na mbili zinaendelea na matengenezo wakati moja haitegemewi kufanyakazi.

Kamati yetu imeshangazwa na majibu iliyopatiwa baada ya kuomba kupatiwa udhibitisho wa makabidhiano ya gari hizo zilizopelekwa ZAFICO na Wakala wa Matrekta na kujibiwa kwamba zilipelekwa pasi na kuwepo kwa kielelezo chochote jambo ambalo ni kinyume na taratibu za kiutendaji katika Ofisi za Serikali. Kadhalika, Kamati yetu imebaini kwamba bado Wizara inazo gari nyingi ambazo ni mbovu na zinahitaji kufanyiwa matengenezo ili ziweze kutumika ipasavyo. Sambamba na hilo, Kamati yetu imegundua kuwa gari namba SMZ 166A Taasisi ya utafiti wa Kilimo Kizimbani imekosewa kuandikwa lakini usahihi wake ni SMZ 616A.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara inapokabidhisha mali zake kwa Taasisi nyengine, makabidhiano hayo yanatakiwa yafanyike rasmi (maandishi) pamoja na kujumuisha vielelezo vyote vinavyotakiwa.
2. Wizara iyafanyie matengenezo gari zake ili ziweze kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

**Hoja nambari 6.11.1.11: Kutokukata Bima kwa Ajili ya Vyombo vya Moto vya Wizara.**

Ukaguzi umebaini Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo haikuchukua hatua za tahadhari kwa kuvikatia bima vyombo vyake ili kuiepusha Wizara na hasara za matengenezo endapo kutatokea ajali. Orodha ya gari ambazo hazijakatiwa bima zinaonekana katika jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 193: Orodha ya Gari Zisizokuwa na Bima**

| Namba | Namba ya Gari | Tarehe iliyokatiwa Bima | Tarehe iliyokwisha Bima |
|---|---|---|---|
| 1. | SMZ 382 B | 05/04/2019 | 04/04/2020 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | SMZ 653 A | 05/04/2019 | 04/04/2020 |
| 3. | SMZ 785 A | 05/04/2019 | 04/04/2020 |
| 4. | SMZ 383 B | 05/04/2019 | 04/04/2020 |

Kutovikinga vyombo kwa kuvikatia bima inaonesha udhaifu wa Wizara katika kujilinda na majanga yanayoweza kuleta hasara kwa Mali zinazomilikiwa na Wizara.

### Majibu ya Wizara

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inakiri kuwa na vyombo vya aina tofauti vya usafiri ambavyo vilikuwa bado havijalipiwa bima, hii ilitokana na kumalizika kwa bima kwa vyombo hivyo na kuandika barua kwa shirika la Bima kwa ajili ya kupatiwa tathmini, kwa kuwa tathmini haijafanyika Wizara imeandika tena barua kwa mara ya pili kwa ajili ya kukumbushia. Wizara inaahidi kuvilipia bima vyombo hivyo kwa ajili ya usalama wa vyombo vyake kwa kadri hali ya kifedha itakavyopatikana.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Pamoja na kwamba Wizara ya Kilimo imekiri kutokatiwa Bima gari za Serikali wanazotumia. Hata hivyo, Kamati yetu imegundua kwamba Wizara hiyo haijalitilia maanani suala la ulipaji wa bima kwa vyombo vyake vya moto hii ni kwasababu Shirika la Bima lilikuwa tayari limeshaipatia Wizara tathmini ya bei ya awali lakini Wizara haikufanya malipo wala kuonesha kwamba japo gari moja imeilipia bima.

Kama hiyo haitoshi, tarehe 4/11/2022, Shirika la Bima liliwasilisha tena ‘tax invoice’ nambari 0152/2022 ambayo ilikuwa ina jumla ya gharama ya shilingi 11,310,250 ambayo nayo haijafanyiwa malipo. Kwa utaratibu huu unaotumiwa na Wizara wa kuliandikia Shirika la Bima kufanya tathmini ya gharama za Bima zinazotakiwa kulipwa pasi na kufanya juhudi yoyote ya malipo hayo, haitaisaidia Wizara kuondoa changamoto ambayo Mkaguzi ameibaini.

Hata hivyo, Kamati yetu iliichunguza kwa undani ‘tax invoice’ iliyowasilishwa na Wizara na kugundua kwamba ni gari moja tu ambayo ni SMZ 785A kati ya gari tano zilizoainishwa na Mkaguzi kwamba hazikukatiwa Bima ndio iliyokuwemo, zilizobakia hazikwemo isipokuwa mlikuwa na gari nyengine zilizokuwa hazijaainishwa na Mkaguzi.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wizara iandae mpango unaotekelezeka ambao utajumuisha gharama za malipo ya Bima kwa vyombo vyake vyote inavyotumia.
2. Wizara ihakikishe inautekeleza kivitendo mpango huo ili changamoto zinazohusiana na kutokulipiwa bima vyombo vya Serikali iondoke.

### IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO ZANZIBAR

**Hoja nambari 6.11.1.12: Dosari katika Ukusanyaji wa Tozo za Leseni ya Mbwa**

Ukaguzi ulizungumza na maofi sa wa Idara ya Maendeleo ya Mifungo pamoja kupitia Sheria namabari 11 ya Usimamaizi wa Rasilimali za Wanyama ya mwaka 1999 na taarifa za mapato za Idara ya Maendeleo ya Mifugo ili kujua vyanzo vya mapato vya Idara hiyo.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 58, 59 na 60 vya Sheria namabri 11 ya Usimamaizi wa Rasilimali za Wanyama ya mwaka 1999 vinaonesha chanzo cha mapato cha Leseni za Mbwa ambao wana umri wa zaidi ya miezi mitatu na utaratibu wa udhibiti wake.

Ukaguzi ulipitia Jadweli la Saba (Malipo ya Tozo na Ada kwa Huduma za Mifugo) la Sheria namabri 11 ya Usimamaizi wa Rasilimali za Wanyama ya mwaka 1999 pamoja na taarifa za mapato za Idara ya Maendeleo ya Mifugo na kubaini kwamba chanzo hicho cha mapato hakikutumika katika ukusanyaji wa mapato ya mwaka wa fedha 2020-2021.

Kutokutumika kwa chanzo hicho cha mapato kunaweza kusababisha upungufu wa ukusanyaji wa mapato ya Idara na kufanya hivyo ni kwenda kinyume ya vifungu nambari 58, 59 na 60 vya Sheria namabri 11 ya Usimamaizi wa Rasilimali za Wanyama ya mwaka 1999.

**Majibu ya Wizara**

Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Mifugo inakiri kutokifanyia kazi chanzo hichi tokea sheria ilipoanza kutumika. Pamoja na kuwepo kipengele hicho katika sheria iliyopita, hakukuwa na kanuni inayotoa ufafanuzi wa namna bora ya utekelezaji wa kipengele hicho cha Sheria. Aidha, Wizara inaifanyia marekebisha sheria ili kuondoa upungufu wa utekelezaji.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba pamoja na kutokuwepo kwa Kanuni lakini Sheria iliyopo kama ingefuatwa ipasavyo, Idara ingeweza kukusanya tozo hizo kwani Sheria husika tayari ilikuwa imeziainisha pamoja na kwamba zilikuwa ndogo. Kwa mantiki hiyo, Kamati imegundua kwamba Watendaji wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo hawakuwajibika ipasavyo kutokana na uzembe wa kiutendaji uliofanyika ambao umeikiosesha Serikali mapato.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Mifugo ichukue juhudi za haraka kuzifanyia marekebisho Kanuni za Sheria ya Mifugo kwani utaratibu wake ni mfupi zaidi

ukilinganisha na kuifanyia marekebisho ya Sheria.

2. Watendaji wa Idara waitekeleze ipasavyo Sheria iliyopo pamoja na kwamba inazo kasoro lakini itasaidia kukusanya baadhi ya mapato ambayo yataongeza makusanyo ya Serikali.

IDARA YA MISITU ZANZIBAR

**Hoja nambari 6.11.1.13: Kutokuandaa Taarifa za Hesabu za Mfuko wa Maendeleo ya Misitu za mwaka wa fedha 2020-2021**

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Misitu inamiliki Mfuko wa Maendeleo ya Misitu ambao unafanya shughuli za maendeleo ya misitu kwa kupokea mapato na kufanya matumizi kupitia hesabu ya Benki kama inavyoainishwa katika jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 194: Muhtasari wa Nambari ya Benki ya Mfuko wa Maendeleo ya Misitu kwa Mwaka wa Fedha 2020 - 2021**

| Maelezo | 2020 - 2021 |
|---|---|
| Nambari ya Benki | 404206000 |
| Jina la Nambari ya Benki | MFUKO WA MAENDELEO YA MISITU |
| Benki na Tawi | PBZ - Forodhani Branch |
| Bakaa ya Mwanzo wa Mwaka | 12,367,920.02 |
| Mapato 2020 – 2021 | 215,206,846.13 |
| Matumizi 2020 -2021 | 157,286,676.50 |
| Fedha Zilizorejeshwa | |
| Gharama za Benki | 386,916.83 |
| Bakaa ya Mwisho wa Mwaka | 69,901,172.82 |

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 82(3) cha Sheria nambari 10 ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu ya mwaka 1996, kinamtaka Msimamizi wa Misitu (Forest Administrartor) kuandaa Taarifa za Kifedha za kila mwaka ambazo zitakaguliwa na kujumuishwa katika Taarifa ya Mfuko wa Maendeleo na kuwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana.

Kufanya hivyo ni kuenda kinyume na kifungu nambari 82 (3) cha Sheria nambari 10 ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu ya mwaka 1996. Vile vile ni kuenda kinyume na kifungu nambari 120(1) na kifungu nambari 119(1) vya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha hesabu za mfuko wa maendeleo ya misitu zinafungwa kwa wakati na kuwasilishwa sehemu zote husika kama matakwa ya sheria ya Mfuko yalivyoamrisha.

**Majibu ya Wizara**

Ushauri uliotolewa na Mkaguzi tumeupokea na tumeufanyia kazi. Kwa sasa tayari Wizara imetayarisha taarifa za hesabu za Mfuko wa Maendeleo ya Misitu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Watendaji wa Idara ya Misitu wamekiri na tayari wamerekebisha kasoro alizozibaini Mkaguzi, Kamati haikuwa na maelezo ya ziada kuhusu hoja hii.

**Hoja nambari 6.11.1.14: Kukosekana kwa Taarifa za Kielektroniki za Mapato ya Mchanga yanayokusanywa kwa Makampuni**

Ukaguzi ulifanya mahojiano na watumishi wenye dhamana ya mapato ya Mchanga na kubaini kwamba Idara ya Misitu ilikuwa inatumia Mfumo wa Kielectroniki (Mail Merge) kwa ajili ya kutunzia kumbu kumbu za Vibali vya Mchanga. Taarifa hizo zilitayarishwa na kutunzwa katika makundi matatu amabayo ni:-

1. Taarifa za Vibali vya Mchanga kwa Makampuni na Miradi.
2. Taarifa za Vibali vya Mchanga kwa Viwanda vya Matofali.
3. Taarifa za Vibali vya Mchanga kwa Wananchi wa Kawaida.

Ukaguzi ulihitaji kupatiwa Taarifa hizo na kuzikosa Taarifa za Vibali vya Mchanga kwa Makampuni na Miradi. Aidha, Ukaguzi ulihitaji maelezo ya kukosekana kwa Taarifa na kupata maelezo ya kwamba Kompyuta iliyokuwa ikitumika kuhifadhia Taarifa hizo liharibika na Idara ya Misitu haikuwa na nakala yake. Hadi kumalizika kwa Ukaguzi wa mwaka wa fedha 2020/2021, Taarifa za Vibali vya Mchanga kwa Makampuni na Miradi hazikupatikana kwa ajili ya Ukaguzi.

Kufanya hivyo ni kuenda kinyume na vifungu namabri 27 (2)(a), 32 (2) na 34 (1) vya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Wizara**

Taarifa za ruhusa za michanga ya miradi kwa njia ya kielekronic hazikuweza kupatikana wakati wa ukaguzi kutokana na kuharibika komputa iliyokuwa ikitumika kuhifadhia taarifa hizo. Hata hivyo, komputa hiyo baada ya kufanyiwa matengenezo taarifa hizo zimeweza kupatikana na kupatiwa wakaguzi kupitia Flash Disk. Kwa bahati mbaya hoja hiyo imerudi tena na taarifa hizo zipo na zinapatikana kwa kukaguliwa. Kwa sasa Masuala ya ukusanyaji wa mapato ya mchanga yamehamishiwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imepata wasiwasi wa kupotea kwa fedha nyingi za Serikali kutokana na kutokuwepo kwa vielelezo vya malipo ya makusanyo ya rasilimali ya mchanga. Kamati imebaini kwamba kuna ubabaifu katika majibu ya watendaji jambo ambalo lilipelekea vielelezo kukosekana wakati Mkaguzi anawajibika lakushangaza Kamati ya PAC imepatiwa vielelezo hivyo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali namba ya mwaka 2003, kunakuwa na fursa ya hadi mwezi mmoja wa kupeleka vielelezo ambavyo Mkaguzi amevikosa katika ukaguzi wake. Vile vile, mbali na Mkaguzi kutaka vielelezo vya kielektroniki lakini Wizara inakuwa na kumbukumbu za risiti za kawaida (hardcopies) ambazo haikuoneshwa kwamba Mkaguzi alipatiwa. Kama hiyo haitoshi, Wizara baada ya kuifanyia matengenezo kompyuta husika, hakukutumia njia muafaka za kimaandishi za kuwasilisha taarifa hizo za 'soft copies' kwa Mkaguzi ili kuweza kuithibitishia Kamati kwamba Watendaji wa Wizara hawakuwa na uzembe au hawakuchangia katika ukosefu wa vielelezo unaoashiria upotevu wa fedha za Serikali.

Kutokana na majibu yaliyowasilishwa na Wizara, Kamati haikuridhishwa nayo na haikubaliani na vielelezo vya Wizara kwani imebainika kuwepo kwa harufu ya upotevu wa fedha za Serikali uliotokana na uwajibikaji na usimamizi usioridhisha uliofanywa na baadhi ya Watendaji wa Wizara.

**Mapendekezo ya kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe inakuwa na mfumo madhubuti wa uhifadhi wa kumbukumbu za rasilimali zake ikiwemo uwepo wa 'back up' itakayokuwa inasaidia uwekaji na upatikanaji wa kumbukumbu hizo wakati wowote iwapo kompyuta itaharibika.
2. Watendaji wa Wizara watumie utaratibu rasmi wa mawasiliano wakati watakapokuwa wanawasilisha vielelezo au ujumbe kwa Taasisi nyengine.

**Hoja nambari 6.11.1.15: Kutopatikana kwa baadhi ya vitabu vya mapato kwa Ukaguzi katika Idara ya Misitu**

Ukaguzi uliomba taarifa za mapato ya Idara pamoja na kumbukumbu za ukusanyaji wa mapato hayo kwa ajili ya kazi za ukaguzi wa mapato. Aidha, baadhi ya vitabu vya risiti vilivyotakiwa kuwasilishwa kwa ukaguzi havikupatikana hadi kumalizika kwa Ukaguzi na hali hiyo kupelekea ukaguzi kushindwa kujiridhisha usahihi wa taarifa za mapato ya Idara.

**Jadweli Nambari 195: Orodha ya vitabu vya stakabadhi ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi.**

| Namba | Tarehe | Nambari ya Mwanzo ya Stakabadhi | Nambari ya Mwisho ya Stakabadhi | Idadi ya Vitabu vya Stakabadhi Vilivyokosekana kwa Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 1.8.2020 | 604901 | 604950 | 1 |
| 2. | 3.8.2020 | 604951 | 605000 | 1 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3. | | 605051 | 605100 | 1 |
| 4. | 4.8.2020 | 605001 | 605050 | 1 |
| 5. | | 605101 | 605150 | 1 |
| 6. | 5.8.2020 | 605151 | 605300 | 3 |
| 7. | 6.8.2020 | 605301 | 605400 | 2 |
| 8. | 7.8.2020 | 605401 | 605450 | 1 |
| 9. | | 681601 | 681650 | 1 |
| 10. | 10.8.2020 | 681651 | 681800 | 3 |
| 11. | 11.8.2020 | 681801 | 681900 | 2 |
| 12. | 12.8.2020 | 681901 | 682000 | 2 |
| 13. | 13.8.2020 | 676501 | 676600 | 2 |
| | 14.8.2020 | 626001 | 626100 | 2 |
| 14. | 15.8.2020 | 622101 | 622200 | 2 |
| 15. | 17.9.2020 | 723751 | 723800 | 1 |
| 16. | 2.10.2020 | 670851 | 670900 | 1 |
| 17. | 9.1.2021 | 7001 | 7200 | 4 |
| 18. | 13.1.2021 | 7201 | 7300 | 2 |
| 19. | | 10751 | 10800 | 1 |
| 20. | 14.1.2021 | 10801 | 10950 | 3 |
| 21. | 15.1.2021 | 10951 | 11050 | 2 |
| 22. | 16.1.2021 | 11051 | 11150 | 2 |
| 23. | 18.1.2021 | 11151 | 11250 | 2 |
| 24. | 19.1.2021 | 32201 | 32250 | 1 |
| 25. | | 32101 | 32150 | 1 |
| 26. | 20.1.2021 | 32151 | 32200 | 1 |
| 27. | | 32251 | 32400 | 3 |
| 28. | 21.1.2021 | 32401 | 32550 | 3 |
| 29. | 23.1.2021 | 32651 | 32750 | 2 |
| 30. | 22.1.2021 | 32551 | 32600 | 1 |
| 31. | 25.1.2021 | 32601 | 32650 | 1 |
| 32. | | 67001 | 67100 | 2 |
| 33. | 26.1.2021 | 32751 | 32850 | 1 |
| 34. | | 67101 | 67150 | 2 |
| 35. | 27.1.2021 | 67151 | 67300 | 3 |
| 36. | 28.1.2021 | 67301 | 67400 | 2 |
| 37. | 29.1.2021 | 67401 | 67500 | 2 |
| 38. | 30.1.2021 | 66701 | 66800 | 2 |
| **Jumla** | | | | **70** |

Kufanya hivyo kunapelekea kutokukamilika kwa taarifa zinazohitajika kwa ajili ya ukaguzi hivyo kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kuhusu taarifa za fedha za Wizara.

**Majibu ya Wizara**

Wizara inakubaliana na hoja ya Mkaguzi, hali hii ilitokana na kuhamishwa kwa Maliasili Zisizorejesheka kutoka Wizara ya Kilimo na kwenda Wizara ya Maji, Nishati na Madini, hali ambayo ilipelekea kuondoka na baadhi ya vitendea kazi vikiwemo vitabu vya risiti. Wizara inaendelea kufanya ufuatiliaji vitabu hivyo katika Ofisi za Wizara ya Maji, Nishati na Madini ili viweze kupatikana kwa ukaguzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati yetu imebaini kwamba Watendaji wa Wizara ya Kilimo walifanya uzembe na hawakuwajibika ipasavyo kwani suala la kuhama kwa Taasisi ni jambo la kawaida na iwapo kutakuwa na uwekaji mzuri wa kumbukumbu, suala la kupotea au kutoonekana kwa nyaraka halitojitokeza. Kamati, katika ukaguzi wake iligundua, katika vitabu ambavyo Mkaguzi aliviorodhesha, vitabu 62 Wizara ilibahatika kuvionesha na kukaguliwa na Kamati lakini vitabu 8 havikupata kuonekana na kuifanya Kamati kuwa na wasiwasi kuhusiana na kumbukumbu zake na fedha zilizoainishwa ndani ya vitabu kuwa zimepotea. Kamati yetu ilibahatika kuvikagua vitabu 8 vyenye namba 605001, 605101, 605151,605301 na 605401na kuridhika navyo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara iandae utaratibu mzuri wa uhifadhi wa kumbukumbu zake ili kuepusha kutopatikana iwapo zitahitajika kwa ukaguzi.

Wizara ivitafute kwa makini vitabu vinane vilivyokuwa havijaonekana ili vihifadhiwe vizuri pamoja na vyenziwe hasa ukizingatia hizo ni fedha za umma.

**Hoja nambari 6.11.1.16: Malipo ya Posho yaliyolipwa Bila ya Toleo Maalum**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna maposho ambayo yamelipwa bila ya kuwepo kwa ruhusa maalum ambayo inaidhinisha kulipwa kwa maposho hayo. Aidha ukaguzi umeshindwa kupata orodha maalum ya wanaostahiki kulipwa maposho hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Malipo yenyewe ni kama yafuatayo:-

**Jadweli Nambari 196: Malipo ya Posho yaliyolipwa Bila ya Toleo Maalum**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 06/10 | 001264 | 4,420,000 | Mfuko wa maendeleo ya misitu | Ikiwa ni malipo ya posho maalum kwa mwezi wa Agosti 2020 kwa watendaji wa mchanga |

Kufanya malipo ya posho za watumishi bila ya kuwepo kwa toleo ni kuenda kinyume na sheria za utumishi wa umma.

### Majibu ya Wizara

Fedha zote za makusanyo ya mchanga zilikuwa zikiingizwa kwenye hesabu moja ya (OR), Fedha na mipango, ambao walikuwa wanarejesha kwa wadau ikiwemo Wizara ya Kilimo kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za Mchanga. Fungu la fedha ambazo zilirejeshewa Wizara ya Kilimo ilikuwa ni kwa ajili ya malipo ya fidia mbali mbali, urejeshaji wa maeneo yaliyochimbwa Mchanga pamoja na gharama za uendeshaji wa masuali ya mchanga. Maposho yaliyolipwa yalitokana na fedha hizi ambazo (OR), Fedha na Mipango waliwasilisha Wizara ya Kilimo kwa mujibu wa mpango kazi wa Fedha hizo ikiwemo malipo ya posho za wafanyakazi waliokuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu.

### Uchunguza wa Kamati ya PAC

Kamati ya PAC imebaini kwamba katika kipindi hicho, Baraza la Mapinduzi liliunda Kamati Maalum kushughulikia suala la usimamizi wa rasilimali ya mchanga ili iweze kuleta tija kwa Serikali. Kupitia Kamati hiyo, kulitolewa mapendekezo ya malipo ya posho kwa watendaji waliokuwa wakifanya kazi hizo.

Hata hivyo, Kamati imeshangazwa na utendaji wa Wizara kwa vile maelekezo ya Baraza la mapinduzi huwa ni sera ambayo inahitaji utekelezaji lakini Wizara ilishindwa kuandaa utaratibu wa kimaandishi utakaothibitisha kwa Mkaguzi kwamba kweli kulikuwa maelekezo hayo ikiwemo ripoti ya maandishi ya kikao husika na maamuzi yaliyofikiwa.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara inapopatiwa maelekezo juu ya utekelezaji wa jambo fulani, inatakiwa kuandaa uthibitisho wa maandishi ili wanapopita Wakaguzi uweze kutumika kama kielelezo au ithibati ya utendaji wao.

### Hoja nambari 6.11.1.17: Uhamishaji wa Vitabu 109 vya Stakabadhi bila ya kuwepo kwa maandishi kutoka Idara ya Misitu kwenda Wizara ya Ardhi

Awali, Taasisi za Umma huchukua Vitabu vya stakabadhi kutoka Ofi si ya Rais Fedha na Mipango, kwa jukumu la kuvitunza na kuvitumia kwa dhumuni la kukusanya mapato ili kupata uhalali wa mapato hayo.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Misitu ilitoa jumla ya vitabu vya stakabadhi 109 na kuvipeleka Wizara ya Ardhi bila ya kuwepo kwa barua ya makabidhiano hali ambayo

inaweza kupelekea kutokea kwa upotevu au udanganyifu. Orodha ya vitabu vya stakabadhi vilivyopelekwa Wizara ya Ardhi vinaonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 197: Orodha ya vitabu vilivyopelekwa Wizara ya Ardhi Bila ya Idhini ya Kimaandishi**

| Namba | Jina la Mtumishi Aliechukua Vitabu | Nambari ya Mwanzo ya Stakabadhi | Nambari ya Mwisho ya Stakabadhi | Idadi ya Vitabu vya Stakabadhi Vilivyochukuliwa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Juma Khamis Ame | 749501 | 749600 | 2 |
| | - | 001751 | 001850 | 2 |
| | - | 034401 | 035100 | 3 |
| | - | 001851 | 002000 | 3 |
| 2. | Time Shaame | 709651 | 709700 | 1 |
| | | 004851 | 005000 | 3 |
| 3. | Haji Ali Haji | 747001 | 747050 | 1 |
| | | 006251 | 006450 | 3 |
| 4. | Tausi Shaaban | 032101 | 032850 | 15 |
| | | 007001 | 007300 | 6 |
| 5. | Abdalla Abeid Yakut | 011251 | 011400 | 3 |
| 6. | Fatma Salum | 010751 | 011250 | 10 |
| 7. | Moh'd Tahir Moh'd | 004451 | 004550 | 2 |
| | | 003601 | 004450 | 16 |
| 8. | Rukia Mustafa | 000501 | 001000 | 10 |
| 9. | Fatma Amar | 007551 | 008000 | 9 |
| 10. | Haji Khamis | 032851 | 033350 | 10 |
| 11. | Haruna Abdallah | 033851 | 034350 | 10 |
| **Jumla** | | | | **109** |

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 27 cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma. Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara wanafuata taratibu za Makabidhiano kwa kuweka kumbukumbu za kimaandishi.

**Majibu ya Wizara**

Wizara imepokea ushauri kwa utekelezaji. Aidha, vitabu hivyo vimeshaorodheshwa kwa ajili ya kukabidhiwa Taasisi husika kwa maandishi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Wizara kukiri na kupokea ushauri uliotolewa na Mdhibiti. Hata hivyo, Kamati yetu imeshangazwa na majibu ya Wizara kwamba hadi Kamati inapokea majibu, bado vitabu hivyo havijakabidhiwa kwa maandishi katika Wizara husika jambo ambalo linaonesha wazi kwamba Watendaji wa Wizara hawapo makini katika utekelezaji wa majukumu yao.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizarai ihakikishe inatekeleza kivitendo ushauri na maelekezo yanayotolewa na Mdhibiti ili iweze kujiweka sawa pale inapoonekana kuna kasoro.

**Hoja nambari 6.11.1.18: Kukosekana kwa Daftari la Vifungu la Idara ya Misitu**

Barua rasmi ya Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ya tarehe 9 Juni 2021 yenye kumbu kumbu nambari AD.5/184/01/01/80 kwenda kwa Taasisi za Umma ilielekeza kwamba "Matumizi yote yaliyofanywa mwaka 2020/2021 yaingizwe katika "Vote Book" kwa mujibu wa Kasma husika. Aidha "Vote Book" zifungwe kwa ajili ya kukaguliwa". Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Misitu ilifanya matumizi ya shilingi 798,466,751.94 kupitia Nambari za Benki kama jadweli nambari 198 linavyoanisha hapo chini.

Aidha; Ukaguzi umebaini Idara ya Misitu haikuwa na Daftari la vifungu hali ambayo inasababisha ugumu katika kazi za Ukaguzi.

**Jadweli Nambari 198: Matumizi ya Idara ya Misitu kupitia Misitu kwa Mwaka wa Fedha 2020 - 2021**

| Nambari ya Benki | Jina la Nambariya Benki | Jina la Benki na Tawi | Matumizi kwa mwaka2020 - 2021 (Tshs) | Jumla (Tshs) |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 404206000 | Mfuko wa Maendeleo ya Misitu | PBZ - Forodhani Branch TZS | 157,286,676.50 | 157,286,676.50 |
| 730065001 | Jozani Chwaja Bay Conservation | PBZ - Forodhani Branch TZS | 641,180,075.44 | 641,180,075.44 |
| **Jumla** | | | | **798,466,751.94** |

Kutotumia Daftari la vifungu kunasababisha mambo yafuatayo:-

- Kumsababishia mkaguzi mzunguko mrefu wa kujua uwiano wa hesabu katika kila kasma (Component) na uhalisia wa matumizi.
- Kufanya uhaulishaji wa vifungu bila kuzingatia sheria na kujifi cha kwa taarifa endapo mkaguzi hatokuwa na upeo mkubwa katika kazi zake.
- Kusababisha kutoelewana kwa mkaguzi na mkaguliwa na kuleta uhusiano mbaya endapo mkaguzi atakapotaka kuchambuliwa taarifa hizo ili kujiridhisha kama ilivyo katika lengo mojawapo la ukaguzi n.k.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuanzisha matumizi ya Daftari la Vifungu kwa ajili ya utunzaji mzuri wa hesabu.

**Majibu ya Wizara**

Hoja tumeipokea na ushauri uliotolewa na mkaguzi. Kwa sasa Idara tayari imeshalifanyia kazi na imeshaandaa na kuanza kutumia Daftari la vifungu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Wizara kukiri na kupokea ushauri lakini Kamati yetu imebaini Watendaji wa Wizara walikuwa hawana uelewa wa uandaaji wa daftari la vifungu vya Idara ambavyo vitaweza kurahisisha kutambulika kwa matumizi ya Idara kwa urahisi zaidi kama ilivyoelekezwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wizara hususan Wahasibu wawe karibu na Wizara ya Fedha na Mipango ili kujua maelekezo yanayotolewa na jinsi ya utekelezaji wake.

**Hoja nambari 6.11.1.19: Kufanya Matumizi ya shilingi 798,466,751.94 Bila ya Mpango wa Manunuzi wa Idara ya Misitu**

Kifungu nambari 29 (e) na kifungu nambari 42 (2) vya Sheria namabri 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 vinaitaka Taasisi ya Umma kuandaa na

kutangaza mpango wa manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma. Vile vile kifungu nambari 42 (7) kimeeleza kwamba ununuzi hautofanyika kinyume na mpango wa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma isipokuwa kwa hali ya haraka na dharura.

Ukaguzi umebaini Idara ya Misitu ilifanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 798,466,751.94 kupitia Hesabu za Benki namabri 404206000 na 730065001 kama inavyoanishwa katika jadweli nambari 18 hapo juu. Aidha, Ukaguzi umebaini manunuzi hayo yalifanywa katika hali ya kawaida bila ya kuwepo kwa mpango huo wa manunuzi. Kufanya hivyo ni kuenda kifungu nambari 42 (7) cha Sheria namabri 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha wanandaa mpango wa manunuzi wa mwaka (Annual Procurement Plan) ili kuepukana na manunuzi holela.

**Majibu ya Wizara**

Wizara imekuwa ikitayarisha Mpango wa Manaunuzi kwa fedha za matumizi mengineyo (OC) tu. Kwa upande wa fedha za Mfuko wa maendeleo ya Msitu wa Jozani, Wizara imekuwa ikitayarisha mpango kazi tu wa matumizi. Hata hivyo, Wizara inakubaliana na ushauri wa Mkaguzi na imeshaandaa Mpango wa Manunuzi mwaka 2021/2022.

**Uchunguzi wa kamati ya PAC**

Kwa vile Watendaji wa Wizara wamekubaliana na hoja iliyoelezwa na Mkaguzi, Kamati haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.11.1.20: Kutopatikana kwa ripoti ya tathmini ya malipo ya Fidia Shilingi 32,248,400**

Idara ya misitu na mali zisizorejesheka imefanya malipo kwa ajili ya fidia kwa wakulima wa Kiombamvua waliothirika na shughuli za uchimbaji wa mchanga, hadi tunamaliza ukaguzi Ripoti ya Tathmini haikupatikana kwa ajili ya ukaguzi ili kuthibitisha uhalali wa viwango walivyolipwa kwa Waathirika. Malipo hayo yamefanyika kupitia hati namba 04/07 kupiti hesabu ya Mfuko wa Maendeleo ya Misitu.

Kufanya malipo bila ya kuambatanisha nyaraka kwa ukamilifu nikuenda kinyume na kanuni 95(4) ya kanuni za sheria ya fedha za umma. Ukaguzi unawashauri viongozi wa idara kuwasilisha ripoti ya tathmini kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi.

**Majibu ya Wizara**

Wizara inakubali kuwa ripoti hiyo ya tathmini haikupatikana wakati wa ukaguzi. Aidha, uongozi wa Wizara unaendelea kuitafuta ripoti hiyo ili kuiwasilisha kwa ukaguzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati haikuridhishwa na majibu mepesi ya Wizara kwa hoja nzito ya upoteaji wa mamilioni ya fedha za Serikali. Kulipwa kwa malipo ya Fidia Shilingi 32,248,400 bila ya kuwepo Ripoti ya Tathmini inathibitisha wazi kwamba fedha hizo hazikuwafikia walengwa au kuna baadhi ya fedha imeenda kwenye matumbo ya wasiohusika.

Kamati ilitegemea muda ambao ipo kikaoni Ripoti hiyo iwe ishapatikana maana Mkaguzi amepita muda mrefu hakubahatika kupatiwa na Kamati nayo pia haikupatiwa. Kitendo hicho kinaonesha RIpoti hiyo haipo na kutokuwepo kwake hakuoneshi taswira nzuri na nidhamu katika matumizi ya fedha za umma kwa maslahi ya umma.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe inafuatilia kwa karibu utendaji wa Maofisa wake ili kuepusha wasi wasi unaojitokeza katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.
2. Vyombo vinavyohusika na usimamizi au uchunguzi wa fedha za umma ikiwemo ZAECA wafuatilie kwa undani kadhia hii ya upotevu wa shilingi milioni 32,248,400 ili kubaini kama kuna uzembe uliofanyika uchukuliwe hatua, kama kuna waliokosa haki zao wapatiwe na ikigundulika uzembe umetendeka wahusika wachukuliwe hatua za kisheria ikibidi kurudishwa kiasi cha fedha kilichogundulika kupotea kwa maslahi ya umma.

**Hoja nambari 6.11.1.21: Dosari katika Hifadhi ya Taifa ya Jozani**

Ukaguzi ulifanya mazungumzo na watumishi wa Hifadhi ya Taifa Jozani kwa lengo la kujua hali halisi ya uendeshaji wa hifadhi hiyo. Ukaguzi ulibani mbali mbali katika hifadhi hiyo kama zinavyoanishwa hapo chini:-

**a) Kukosekana kwa Mihutasari ya Vikao vya Kamati ya Kiintelijensia ya Hifadhi ya Taifa ya Jozani**

Vifungu vya 10 na 11 vya Kanuni ya Hifadhi ya Ukanda Jozani Chakwa ya mwaka 2018 iliyotolewa katika Gazeti Rasmi la Serikali nambari 62 vimetambulisha na kutaja kazi za Kamati ya Kiintekigenisia.

Ukaguzi ulitaka kuona mihutasari ya vikao vya kamati hiyo ili kujiridhisha utekelezaji wa majukumu yake ya kiusalama na uimarishaji wa mahusiano mazuri na wadau wanaoizunguka Hifadhi ya Taifa ya Jizani. Hadi kumalizika kwa Ukaguzi mihutasari ya vikao vya kamati hiyo haikupatikana kwa ajili ya Ukaguzi.

**Majibu ya Wizara**

Wizara iliwasilisha ripoti za vikao vya uongozi (intelijensia) wa Jozani pamoja na wadau wa uhifadhi kwa imani kuwa vikao hivyo vimeongeza wigo na vinasaidia zaidi kutatua changamoto za Hifadhi ya Jozani. Hata hivyo tulipowasilisha ripoti hizo wakaguzi

walitaka tuwasilishe ripoti ya uongozi tu. Mara baada ya ushauri huo Wizara imekuwa ikitayarisha ripoti za vikao vya uongozi wa Jozani na ripoti za vikao vya pamoja vya uongozi na wadau wa uhifadhi. Ripoti hizo zipotayari kwa ukaguzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imegundua kwamba Watendaji wa Hifadhi ya Taifa ya Wizara ilikuwa ikifanya vikao vya pamoja na wadau wa Hifadhi isipokuwa watendaji walikuwa hawaandai Ripoti za Vikao hivyo, kwasasa Kamati imejiridhisha kwamba hoja hii haitegemewi kutokea tena kwa vile watendaji wanaandaa Ripoti hizo. Kwa mantiki hiyo, Kamati ya PAC haikuwa na maelezo mengine.

**b) Kutokuwepo kwa Bodi ya Ushauri ya Hifadhi ya Taifa ya Jozani**

Kwa mujibu wa kifungu 12 cha Kanuni ya Hifadhi ya Ukanda Jozani Chwaka ya mwaka 2018 kinaitaka Hifadhi ya Taifa ya Jozani kuwa na Bodi ya Ushauri ambayo utendaji wake umetajwa katika kifungu nambari 13 hadi 16 vya Kanununi hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba Hifadhi ya Taifa ya Jozani haikuwa na Bodi ya Ushauri kwa mwaka wa fedha uliomalizika tarehe 30 Juni, 2021.

**Majibu ya Wizara**

Bodi ya ushauri ya Hifadhi ya Taifa ya Jozani ilianzishwa na kuwahi kufanya kazi hadi mwaka 2017. Hivyo Bodi ilisita kufanyakazi kutokana na kumaliza kipindi cha utumishi kwa mujibu wa kanuni. Hata hivyo, Wizara imeshachukua hatua za kuteuwa Bodi mpya.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba licha ya Bodi ya Hifadhi kumaliza muda wake. Kamati imegundua kwamba Watendaji wa Idara ya Misitu hawakuchukua juhudi yoyote ya kukumbusha katika ngazi yenye mamlaka na uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi hiyo kwani Kamati iliomba kupatiwa kielelezo chochote kinachothibitisha hatua iliyochukuliwa na Idara ya Misitu kuomba kuteuliwa kwa Mwenyekiti wa Bodi ambae kwa mujibu wa Kanuni anateuliwa na Waziri wa Wizara hiyo hiyo lakini kwa bahati mbaya hakukuwa na kielelezo chochote. Kwa mnasaba huo, Kamati inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kwamba Hifadhi ya Taifa ya Jozani haikuwa na Bodi wakati Mkaguzi anakagua isipokuwa hivi sasa ipo na inafanya kazi zake.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Idara ya Misitu wawe na utaratibu wa kuikumbusha ngazi ya Uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ili uteuzi wake ufanyike kwa wakati na majukumu ya Hifadhi yaweze kutekelezeka kwa mujibu wa Kanuni.

**c) Mapato ya Mgahawa kutumika kwa kulipa Posho la muda wa ziada kwa**

**Wafanyakazi wa Hifadhi ya Taifa Jozani bila ya Idhini ya Kiimandishi.**

Ukaguzi ulifanya mazungumzo na uongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Jozani na kubaini kuwepo kwa Mgahawa katika hifadhi hiyo ambao mapato yanayopatikana katika mgahawa huwo hutumika kwa kulipa posho la muda wa ziada kwa wafanyakazi wa hifadhi hiyo.

Ukaguzi ulihoji na kuomba kupatiwa ruhusa ya kiimandishi iliyodhinisha kufanyika hivyo.

Hadi kumalizika kwa ukaguzi ruhusa ya kufanya hivyo haikupatikana kwa ajili ya Ukaguzi.

**Majibu ya Wizara**

Hoja tumeipokea na ushauri uliotolewa na Mkaguzi. Uhalisia ni kwamba Mkahawa si sehemu kwa sasa ya mapato ya Serikali bali ni Mradi uliobuniwa tokea kipindi cha Mradi wa Care katikati ya miaka ya 90 baada ya wafanyakazi kulalamika kwamba hawapati malipo ya muda wa ziada. Hivyo, Mradi wa Care uliwakopesha fedha za kuanzisha Mradi huo kwa ajili ya kusaidia kipato cha ziada kwa wafanyakazi wa Jozani. Hata hivyo, kwa sasa kufuatia kutayarishwa kwa muongozo wa uwekezaji katika misitu ya hifadhi ya Jozani, Ngezi, Masingini na Kiwengwa ni sehemu ya miradi iliyoainishwa katika muongozo huo na itakuwa ni moja kati ya vyanzo vya mapato ya Serikali mara watakapopatikana Wawekezaji.

Sambamba na hayo, Wizara imeshachukua hatua ya kuutangaza Mkahawa huo katika gazeti la Zanzibar Leo la Tarehe 30 Aprili, 2022 na Website ya Wizara.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kwa vile Watendaji wa Wizara wamekiri kuwepo kwa changamoto hiyo na tayari wameshajirekebisha, Kamati yetu haikuwa na hoja zaidi.

**d) Kukosekana kwa Mikataba ya Makampuni yanayotembeza Wageni kwa Mkopo katika Hifadhi ya Msitu wa Jozani**

Ukaguzi umebaini Hifadhi ya Msitu wa Jozani hupokea wageni kutoka Makampuni yanayotembeza Wageni hao kwa njia ya mkopo. Makampuni hayo huandaliwa Ankara za thamani ya fedha ya ada za Wageni waliokwenda katika Hifadhi hiyo kwa muda wa mwezi kutoka Idara ya Misitu na baadae hulipa kupitia hesabu ya Benki ya Hifadhi ya Taifa ya Jozani.

Ukaguzi ulihitaji kupatiwa nakala za mikatba inayotoa ruhusa kwa makampuni hayo kutolipa fedha taslim wakati wakitembeza wageni katika hifadhi, hadi kumalizika kwa Ukaguzi mikataba hiyo haikupatikana. Orodha ya Makampuni hayo yanatembeza wageni ni kama inavyonekana hapo chini:-

- Zan Tours

- Gallery
- Africa Spirit
- Madeira

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 42 (7) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuongezeka kwa changamoto za kiutendaji na kudhoofi sha uendelezaji wa Hifadhi ya Taifa ya Jozani.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha wanafuta taratibu na sheria kwa ajili ya uendeshaji mzuri wa Hifadhi ya Taifa ya Jozani.

**Majibu ya Wizara**

Ushauri umepokelewa na mikataba imeshatayarishwa na kusainiwa na Wahusika (Wizara na Kampuni) kwa ajili ya kutumika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na kwamba Watendaji wa Wizara kukubali kutokuwepo mikataba ya watembeza Wageni kueleza kuwa tayari wameshachukua juhudi ya kurekebisha kasoro hizo. Hata hivyo, Kamati iliomba kupatiwa mikataba husika, kuipitia na kuridhika kwamba mikataba ipo na imetiwa saini tarehe 26/10/2022. Baada ya kujiridhisha, Kamati yetu haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.11.1.22: Dosari katika Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Masingini**

Ukaguzi ulifanya mazungumzo na watumishi wa Msitu wa Asili wa Masingini kwa lengo la kujua hali halisi ya uendeshaji wa hifadhi hiyo. Ukaguzi ulibani mbali mbali katika hifadhi hiyo kama zinavyoanishwa hapo chini:-

**a) Kutokuwepo kwa Bodi ya Ushauri ya Hifadhi ya Msitu ya Asili wa Masingini**

Kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Kanuni ya Hifadhi ya Misitu ya Asili ya mwaka 2018 kinaitaka Hifadhi ya Msitu ya Asili wa Masingini kuwa na Bodi ya Ushauri ambayo utendaji wake umetajwa katika kifungu cha 11 cha Kanununi hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba Hifadhi ya Msitu ya Asili wa Masingini haikuwa na Bodi ya Ushari kwa mwaka wa fedha uliomalizika tarehe 30 Juni, 2021.

**Majibu ya Wizara**

Ushauri wa kuanzisha Bodi umepokelewa na Bodi ya Ushauri ya Hifadhi ya kimaumbile ya Masingini itaanzishwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati haikuridhishwa na majibu ya Wizara kwani suala la kuanzisha Bodi limo ndani ya mamlaka ya Wizara kupitia Waziri husika na ukizingatia ni muda mrefu tangu Mkaguzi amepita na kutoa ripoti yake. Iwapo Wizara ingekuwa ipo makini na urekebishaji wa kasoro zilizojitokeza katika Ripoti ya Mkaguzi basi kwasasa Bodi ingekuwa ishaundwa na inaendelea kufanya kazi zake.

Kutokana na kutokuwepo kwa Bodi hiyo, Kamati yaPAC imegendua kuna majukumu kadhaa ambayo Hifadhi inashindwa kuyatekeleza na kurudisha nyuma maendeleo ya Msitu huo. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na kupima na kulitambua eneo lote la hifadhi ya Msitu, kuwatambua watu wote walioanzisha makaazi ndani ya msitu kabla ya kutangazwa msitu kuwa hifadhi ya Taifa na kuwaeleimisha wanajamii kuhusu mpango wa Idara ya Misitu kuhusu uendelezwaji wa Msitu huo na mapato yanayotokana na Msitu.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati inaiomba Wizara ndani ya miezi sita baada ya kuwasilishwa Ripoti hii ifanye haraka kuiunda Bodi ya Ushauri ya Hifadhi ya Kimaumbile ya Msitu wa Masingini kama inavyoelekeza kifungu cha 10 cha Kanuni ya Hifadhi ya Misitu ya Asili ya mwaka 2018.
2. Idara ya Misitu ilipime eneo lote la Msitu ili kulitambua na kuliwekea alama za kudumu.
3. Idara ya Misitu ikae na wanajamii kuwaelemisha kuhusu uendelezwaji wa Msitu na rasilimali zilizomo ndani yake.
4. Idara ya Misitu ifanye utafiti kuwatambua wale wote walioanzisha makaazi ndani ya eneo la Msitu kabla ya kutambuliwa hifadhi hiyo na wote waliokuwa wavamizi.

**b) Uchakavu wa Miundombinu na Kukosekana kwa baadhi ya Huduma katika Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Masingini**

Ukaguzi ulitembelea Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Masingini tarehe 17.12.2021 kwa madhumuni ya kuona hali halisi ya hifadhi na uendeshaji wake, ukaguzi ulibaini dosari mbalimbali katika miundombinu ya hifadhi hiyo kama zifuatazo:-

- Njia ya kuingilia kwenye hifadhi ilikuwa na mabonde na hivyo hupelekea kutokufika kwa wepesi na haraka katika hifadhi ya Masingini.
- Mnara unaotumika kuangalia Mji wa Zanzibar uliojengwa kwa kutumia magogo ya miti na boriti ulionekana na athari za kuoza na paa la makuti likiwa lishaharibika, pamoja na kuwa mnara huo ni chanzo kizuri cha kuingiza mapato lakini hakuna kilichoingia kwa muda mrefu.

- Vibaraza vya maeneo ya kumpumzikia wageni na Vyoo havijaendelezwa toka mwaka 2018 vilipojengwa.
- Paa la banda la mkahawa lilijengwa kwa makuti lilioneka kuwa lishaharibika hivyo.
- kuhatarisha kuoza kwa miti na magogo yaliyojengewa mkahawa huo.

**Majibu ya Wizara**

Wizara imewasilisha Muongozo wa Uwekezaji katika Misitu ya hifadhi na kuitangaza katika tovuti ya Wizara ya Utalii na Magazeti ya Zanzibar. Tayari yupo Muwekezaji ambae ameomba kuwekeza kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ikiwemo mkahawa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imegundua kwamba Msitu wa masingini hauwezi kujiendesha kupitia mapato yake ya ndani badala yake Idara ya Misitu imechukua asilimia 25 ya mapato ya Jozani kuchimba kisima katika msitu wa Masingini ili kuimarisha upatikanaji maji ndani ya msitu huo. Sambamba na hilo Kamati ilitaka kujua mpango uliopo wa ujenzi wa barabara iliyotoka Masingini barabara kuu hadi eneo la msitu na kuelezwa kwamba ujenzi wake umeingizwa katika mpango mkuu wa Serikali wa ujenzi wa barabara za ndani. Hivyo, Idara inasubiri utekelezaji wa mpango huo.

Kutokana na hatua iliyochukuliwa na Idara, bado Kamati haikuridhishwa na juhudi hizo kwani changamoto nyingi ambazo Mkaguzi zmeziainisha zikiwemo Mnara unaotumika kuangalia Mji wa Zanzibar na vyoo vimebakia kuwa changamoto ya msitu huo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Idara ya Misitu ichukue juhudi zaidi kutafuta wawekezaji wengine ili wauimarishe msitu wa Masingini na kuwa chanzo kizuri cha mapato.
2. Idara iandike barua kukumbushia ujenzi wa barabara inayotoka barabara ya mwera kuelekea katika msitu huo.

### c) Kutokuendelezwa kwa mradi wa kujenga vyoo kwa muda mrefu

Hifadhi ya masingini ilianzisha mradi wa kujenga vyoo ndani ya hifadhi hiyo ili kuepusha usumbufu kwa wageni wanaotembelea hifadhi kadhalika wafanyakazi, ukaguzi umebaini ujenzi huo haukuendelezwa tangu uliposimama 2018 hivyo kushindwa kutatua changamoto hiyo na kupelekea kupotea kwa rasilimali fedha zilizowekezwa kwenye mradi huo na kushusha mapato ya hifadhi hiyo kwa kuondosha mvuto kunakosababishwa na kukosekana na huduma muhimu za vyoo.

**Majibu ya Wizara**

Wizara imetayarisha Kanuni ambayo inaelekeza mgao wa mapato kwamba asilimia 50 ya mapato yataingia Wizara ya Fedha, asilimia 30 inakwenda kwa jamii zinazozunguka hifadhi na asilimia 20 inabakia katika hifadhi kwa kuendeleza shughuli za uhifadhi. Fedha hiyo itatumika kwa ukamilishaji wa ujenzi wa vyoo na miundombinu mengine.

**Uchunguzi na pendekezo la Kamati ya PAC**

Kamati yetu imegundua kwamba vyoo viliopo hivi sasa vinakidhi mahitaji ya wageni wanaotembelea msitu huo pamoja na kuwepo kwa ongezeko la wageni. Kadhalika, Kamati imebaini kwamba vyoo havijaendelezwa licha ya kuwepo kwa mpango wa mgawanyo wa mapato utakaolenga ujenzi wa vyoo husika. Hivyo, Kamati inasisitiza utekelezaji wa Kanuni zilizotayarishwa ufanyike kwa haraka ili ujenzi wa vyoo hivyo ufanyike.

**d) Idadi Isiyokidhi ya Wafanyakazi Ndani ya Hifadhi ya Masingini**

Ukaguzi umebaini Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo haijaandaa mpango mzuri wa wafanyakazi kwa ajili ya kutunza hifadhi, kulinda, kutembeza wageni na kuendeleza eneo la uhifadhi, kumekuwa hakuna mbadala wa wafanyakazi wanaofariki, wanaostaafu kwa mujibu wa sheria na wanaohamishwa kikawaida hali iliyopelekea kuwepo na idadi ya chini ya wafanyakazi wanaoelekea kushindwa kutoa huduma kamilifu ndani ya hifadhi.

**Majibu ya Wizara**

Wizara inakiri kuwa na wataalamu kidogo katika maeneo yote ya hifadhi. Hata hivyo, inaendelea na mpango maalum wa kuwasambaza wataalamu hao wachache wakati tukisubiri Serikali kutafuta na kutupatia wataalamu wengine. Aidha, Wizara inashirikiana na Kamati za Uhifadhi wa Jamii katika kusimamia hifadhi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na majibu yaliyotolewa na watendaji wa Idara ya Misitu, Kamati yetu imegundua suala la uchache wa Wafanyakazi ni la Wizara nzima ya Kilimo, Umwagiliaji, maliasili na Mifugo linalotokana na kustaafu kwa wafanyakazi waliopo na hakuna ajira kuziba pengo

liliopo. Aidha, Kamati yetu imebaini kwamba mara nyingi wafanyakazi wanaoajiriwa katika hifadhi ya Misitu huajiriwa kwa vigezo vinavyopangwa na Wizara inayoshughulikia utumishi na kupekelea kutoajiri wafanyakazi wanaotoka karibu na msitu husika. Suala hilo hupelekea ugumu katika uendelezwaji na uhifadhi wa Misitu yetu.

Hata hivyo, Idara inazo kamati zipatazo 23 pamoja na Polisi Jamii wanaotumika katika ulinzi na ushughulikiaji wa Misitu yake.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ifuatilie kwa karibu suala la uajiri wa wafanyakazi watakaotumika katika hifadhi za misitu yetu ikiwemo Msitu wa Asili wa Masingini

e) **Upungufu wa ziara za Viongozi wa Wizara na Idara Kukagua Changamoto za Hifadhi ya Masingini**

Ziara za mara kwa mara za viongozi husaidia uongozi kutambua kwa kina mafanikio na changamoto zinazoikabili sehemu husika, ukaguzi umebaini viongozi wa Wizara na idara hawana utaratibu wa kufanya ziara ndani ya hifadhi ilikutambua vikwazo wanavyokabiliana navyo watendaji. Kufanya hivyo kunadumaza jitihada za watendaji na kuongezeka kwa changamoto zitazopelekea kudumaa na huenda kutoweka kwa hifadhi hiyo.

Kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kupelekea kuongezeka kwa changamoto za kiutendaji na kudhofi sha uendelezaji wa Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Masingini. Uongozi wa Wizara unapaswa kuhakikisha miradi yote iliyoanzishwa inatekelezwa na kukamilika ili kuepusha kupotea kwa rasilimali fedha iliyowekezwa ikiwa ni pamoja na kutilia mkazo kukakamilika kwa ujenzi wa vyoo ili kurejesha haiba njema ya hifadhi ya masingini.

Aidha, uongozi wa Wizara inaweza kuimarisha hifadhi kwa kuweka utaratibu na idadi yakutosha ya watumishi katika Hifadhi pamoja  na kuandaa utaratibu wa usafi ri kwa wafanyakazi ili waweze kutimiza majukumu yao kwa ufanisi, vile vile kuwaandalia malipo ya utumishi baada ya saa za kazi kwa watendaji wa hifadhi.

**Majibu ya Wizara**

Wizara inaahidi kupanga utaratibu maalum wa kufanya ziara katika miradi yote iliyoanzishwa ili kuweza kutambua changamoto zinazowakabili watendaji.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba kuna upungufu wa ziara za viongozi kutembelea mara kwa mara msitu huo. Hata hivyo, kuna wageni wengi huwa wanatembelea Msitu huo isipokuwa huwa hawajiorodheshi rasmi katika daftari la kumbukumbu za wageni wanaotembelea msitu huo na wengine hupitia njia zisikuwa rasmi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inapendekeza kwamba Idara ya Misitu ianzishe mlango (gate) la kuingia wageni upande wa barabara ya Mwera ili iwe rahisi kwa wageni wanaotoka mjini kufika kwa urahisi katika msitu huo.

**IDARA YA KILIMO**

**Hoja nambari 6.11.1.23: Malipo yasiyokuwa na stakabadhi shilingi 56,840,000**

Ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo yamefanyika lakini stakabadhi za malipo husika hazikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanisha stakabadhi za malipo ni kwenda kinyume na sheria za fedha za Zanzibar za mwaka 2016. Malipo hayo yanaonekana katika mchanganuo wa jadweli nambari 21 hapo chini:-

**Jadweli Nambari 199: Orodha ya Malipo yasiyokuwa na Stakabadhi**

| Namba | Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (shs) | Alielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | M4/06 | | 56,840,000 | Mafada kilimo limited | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuziwa pembejeo |

Kutoambatanishwa kwa stakabadhi za malipo hayo kutapelekea kukosekana kwa uhalali wa malipo hayo.

Ukaguzi unapendekeza kwamba ni vyema kwa Wizara ikahakikisha kwamba stakabadhi zote zinaambatanishwa na hati za malipo husika.

**Hesabu ya Maendeleo na Huduma za Kilimo - Nambari 0404288000**

**Majibu ya Idara**

Wakati wa ukaguzi stakabadhi husika haikuonekana, lakini kwa sasa ipo tayari kwa ukaguzi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Watendaji wa Wizara kukiri kwamba Kamati ya PAC imebaini wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake katika Idara ya Kilimo stakabadhi zilikosekana. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua sababu ya Mkaguzi kukosa stakabadhi hizo na kuelezwa kuwa 'Supplier' alikuwa Tanzania Bara.

Kamati ilitaka kufahamu juhudi gani ambazo Wizara ilichukua kuhakikisha stakabadhi husika zinapatikana ndani ya wakati na kuelezwa kwamba kielelezo kililetwa na kuwasilishiwa Mkaguzi jambo ambalo halikuwa na ukweli wowote kwani Kamati ilishindwa kukikubali kielelezo hicho kwa vile hakikuwa na alama yoyote ya Mkaguzi inayothibitisha uhalali wake.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC haikuridhika na majibu yaliyowasilishwa kwani kuna kipindi cha takriban mwezi mmoja wa kusawazisha kasoro zilizojitokeza wakati wa ukaguzi lakini Wizara ilishindwa kufanya hivyo jambo ambalo linaonesha wazi kwamba Watendaji wa Wizara walihusika na upotevu wa shilingi 56,840,000 kutokana na uzembe wa kushindwa kufuatilia vielelezo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Watendaji wa Wizara wawe na utamaduni wa kufuatilia stakabadhi za malipo mara wanapomaliza matumizi ili kuondosha wasiwasi na mwanya wa upotevu wa fedha za umma.
2. Wizara ifuate utaratibu wa kuhifadhi vizuri kumbukumbu za malipo baada ya kulipa huduma au kifaa.
3. Wizara iwe karibu sana na Ofisi ya Mkaguzi ili waweze kueleweshwa ipasavyo kuhusiana na utaratibu wa malipo ya fedha za umma.

**Hoja nambari 6.11.1.24: Kukosekana kwa Toleo Maalum linaloruhusu utumiaji wa fedha za mapato**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba akaunti hii ya Maendeleo na huduma za Kilimo ni Akaunti inayokusanya mapato kupitia vyanzo vifuatavyo:-

- Mabanda ya maonyesho
- Matangazo ya Tenda mbalimbali
- Pesa za Pembejeo
- Bajeti kutoka Hazina.

Kwa mujibu wa Kanuni za fedha za mwaka 2021, namba 29 (1-4) ambayo inaitaka Taasisi kuwasilisha mapato yote katika mfuko mkuu wa Hazina au kuwe na toleo

maalum linaloidhinisha kutumika kwa mapato hayo.

Hadi tunamaliza ukaguzi tulishindwa kupata toleo hilo ambalo linaidhinisha kufanyika kwa matumizi kwa fedha hizo. Kufanya matumizi bila kupata idhini ya kutumiwa kunaweza kupelekea kutumika vibaya kwa rasilimali za Serikali. Ukaguzi unaushauri uongozi wa wizara kuhakikisha wanafata taratibu za matumizi ya fedha za umma.

### Majibu ya Idara

Wizara ilifungua hesabu ya MAENDELEO NA HUDUMA ZA KILIMO yenye nambari 0404288000 katika Benki ya Watu wa Zanzibar kwa lengo la kuweka fedha kwa kazi maalumu kama vile fedha za miradi midogo midogo ambayo hutekelezwa chini ya mwaka au miezi sita pamoja na ruzuku inayopatikana kwa ajili ya uuzaji wa pembejeo za wakulima na sio hesabu ya mapato. Kwa kuwa fedha iliyokusanywa katika hesabu hii haikuwa mapato bali ni fedha ya ruzuku ya mbolea ambayo hutumika kwa kununulia mbolea na ile ya miradi hutumika kwa miradi husika. Vyanzo ambavyo ameainisha mkaguzi vilikuwa na malengo kama ifuatavyo;

- Mabanda ya maonesho: Huu ni mchango wa washiriki wa maonesho ambao unatumika katika maandalizi ya maonesho.
- Matangazo ya tenda mbalimbali: Fedha hizi zinaingizwa kwenye hesabu hii kwa ajili ya kuchangia gharama za utayarishaji wa makabrasha ya tenda za ununuzi wa pembejeo.
- Pesa za pembejeo: fedha hizi zinatokana na uuzaji wa pembejeo kwa njia ya ruzuku na badae zinatumika kwa ununuzi wa pembejeo kwa msimu unaofata. Aidha, kwa sasa fedha hizi zinawasilishwa kwenye mfuko mkuu wa mapato kwa kutokana na kutokuwepo kwa ununuzi wa pembejeo na kwa kufuata kanuni za fedha mwaka 2021.
- Bajeti kutoka hazina: Fedha hizi ziliingizwa kwenye hesabu hii ikiwa ni marejesho ya fedha za OC ambazo zilitumika kwa maandalizi ya maonesho. Wakati ambao maandalizi yanaanza inakuwa bado OC ya mwaka husika haijaanza kutolewa kwa hiyo Wizara ilikuwa ikitumia fedha za hesabu hii kwa dharura na hatimae fedha za maonesho zinapoingizwa ndio hurejeshwa katika hesabu hii kwa matumizi husika.
- Aidha, Wizara imeupokea ushauri wa mkaguzi kwa lengo la kuhakikisha taratibu za matumizi ya fedha za umma zinafatwa.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kwa vile Watendaji wa Wizara wamekubaliana na Mkaguzi kuhusiana na matumizi ya fedha hizo kutokana na kuchelewa kwa fedha zao za Matumizi Mengineyo (OC), hata hivyo, watendaji walieleza kwamba utaratibu huo hautumiki tena baada ya Serikali kuelekeza kutafuta Wahisani ili waweze kuchangia kufanyika maonyesho ya Kilimo.

Pamoja na ushauri mzuri wa Serikali uliotolewa lakini Kamati ya PAC inaielekeza Wizara

kuendelea kupanga bajeti ya maonyesho hasa ukizingatia fedha za Wahisani hazina uhakikia katika upatikanaji wake.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara iendelee kupanga bajeti yake lakini wabadilishe muda wa matumizi ya fedha hizo ili ziweze kuingizwa na Serikali mapema na kuweza kuzitumia.

**Hoja nambari 6.11.1.25: Kutokugongwa muhuri wa paid katika hati na nyaraka za malipo**

Ukaguzi umebaini Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo hukugonga muhuri wa "PAID" kwenye hati na nyaraka za malipo, kufanya hivyo ni kuenda na kinyume na kifungu cha 95(1) cha kanuni za sheria za fedha za umma.

Kutokukugonga muhuri wa paid kwenye hati na nyaraka za malipo kunaweza kupelekea kufanya malipo mara mbili kwa nyaraka zilizokuwa tayari zimelipwa. Uongozi wa wizara unawajibu kuhakikisha hati na nyaraka za malipo zinagongwa muhuri wa paid mara tu baada ya kukamilika malipo.

**Majibu ya Idara**

Ni kweli wakati alipopita mkaguzi kuna baadhi ya vocha hazijagongwa muhuri wa "PAID" kwa sasa tayari vocha zote zimeshagongwa muhuri huo na Wizara inaendelea kufanya hivyo mara tu inapokamilisha taratibu za malipo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Watendaji wa Wizara kukubaliana na hoja ya Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kuwa Watendaji walikuwa wazembe na hawakuwajibika ipasavyo na kupelekea kasoro hii kujitokeza na kuitia doa la kiutendaji Serikali yetu.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wizara wahakikishe wanazigonga muhuri nyaraka zikazotumika kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 94(1) ya Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

**Hoja nambari 6.11.1.26: Kutofuatwa kwa Sheria nambari 11 ya mwaka 2016, Sheria ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 29 (a) cha Sheria Nambari 11 ya mwaka 2016 ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinazitaka taasisi zote za umma kufanya manunuzi yote kwa kufuata sheria hiyo ambayo imezilazimisha taasisi zote zitakazofanya manunuzi ni lazima yapitie kitengo cha manunuzi cha wizara (PMU).

Ukaguzi umebaini manunuzi yote yaliyofanyika kupitia hesabu za maendeleo ya huduma za kilimo hayakuanzia katika kitengo cha manunuzi. ya umma kufanya hivyo nikuenda kinyume kifungu namba 29 (a).

Kufanya manunuzi ya umma bila kupitia kitengo cha manunuzi nikuenda kinyume na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za umma. Ukaguzi unashauri uongozi wa wizara kuhakikisha unatumia kitengo cha manunuzi ya umma kufanya manunuzi yote ya wizara.

**Majibu ya Idara**

Wizara imeupokea ushauri na inakubaliana na hoja ya mkaguzi ya kuwepo kasoro hiyo iliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria nambari 11 ya mwaka 2016, ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Hii ilijitokeza kwa sababu ya uharaka wa mahitaji. Aidha, kwa sasa Wizara imefanya marekebisho makubwa katika kitengo cha manunuzi. Wizara imepokea na sasa viambatanisho na nyaraka muhimu zote zipo tayari kwa ajili ya kukaguliwa ili kutoa uhalali wa matumizi husika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Wizara kukiri kujitokeza kwa hoja hii wakati Mkaguzi anatekeleza majukumu yake. Hata hivyo, Kamati ya PAC iligundua kwamba Sheria hiyo haikufuatwa kutokana na uzembe wa Watendaji wa Idara ya Kilimo kwani walikuwa hawawatumii wataalamu waliopo wa Manunuzi wenye shahada na uzoefu wa kazi. Kwa mantiki hiyo, Kamati yetu haikuridhika na maamuzi ya Wizara.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inawashauri Watendaji wa Wizara kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa kufuata Sheria za Manunuzi kwa kuwatumia ipasavyo Maafisa Manunuzi ambao ndio weledi wa kutambua utaratibu wa ununuzi bidhaa au huduma.

**Hoja nambari 6.11.1.27: Malipo yasiyokamilisha vielelezo shilingi 103,257,694**

Ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo yamefanyika lakini viambatinisho muhimu havikuweza kuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanisha nyaraka za malipo ni kwenda kinyume na sheria ya fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016. Malipo yenyewe ni kama yanavyoanishwa katika jadwweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 200: Orodha ya Malipo Yasiyokuwa na Viambatanisho Kamili**

| Namba | Hati Namba | Aliyelipwa | Maelezo | Thamani (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 02/07 | Katibu Mkuu | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matayarisho | 3,000,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2. | 03/07 | Wkmm U | yamaonyesho nane nane | 3,000,000 |
| 3 | 05/07 | Thiney Ali Juma | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ukodishwaji wamashamiana. | 16,970,873 |
| 3 | 06/07 | | | 21,628,641 |
| 4 | 04/07 | Katibu Mkuu WKMMU | Ikiwa ni sehemu ya malipo kwa ajili ya ufungajiwa gazebo kwa ndg. Beatus Haule | 2,662,500 |
| 5 | 10/07 | Katibu Mkuu WKMMU | Malipo kwa ajili ya maandalizi ya kamati ya uenezi katika maonyesho ya kilimo nane nane 2020. | 3.480,000 |
| 6 | 13/07 | Katibu Mkuu WKMMU | Ikiwa ni malipo ya safari ya kikazi Pemba | 530,000 |
| 7 | 05/08 | Katibu Mkuu WKMMU | Ikiwa ni sehemu ya malipo kwa ajili ya ufungajiwa gazebo pemba | 4,050,000 |
| 8 | 15/08 | Thney Ali Juma | Ikiwa ni bakaa ya malipo kwa ajili ya kukodishamashamiana yaliyotumika | 21,628,641 |
| 9 | 16/08 | Thney Ali Juma | Ikiwa ni malipo ya asilimia 50 kwa ajili ya kukodishia mashamiana. | 16,924,757 |
| 10 | 01/10 | Thney Ali Juma | Ikiwa nai malipo kwa ajili kukodishwamashamiana ya ziada | 10,007,282 |
| 11 | 09/11 | Katibu Mkuu WKMMU | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ufuatiliaji wa mrejeshowa mkutano mkuu wa upovu | 1,280,000 |
| 12 | 09/12 | Katibu Mkuu WKMMU | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kuhudumia kikao chamadeni ya jamuhuri ya muungano wa tanzania | 1,575,000 |
| **Jumla** | | | | **103,257,694** |

Kukosekana kwa viambatisho vya malipo kutapelekea kukosekana kwa uhalali wa malipo hayo. Ukaguzi unapendekeza kwamba ni vyema kwa Wizara ikahakikisha kwamba viambatisho vyote vinambatanishwa.

**Majibu ya Idara**

Wizara imepokea na sasa viambatanisho na nyaraka muhimu zote zipo tayari kwa ajili ya kukaguliwa ili kutoa uhalali wa matumizi husika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba fedha hizi ni nyingi ambazo zimetumiwa bila kuwepo vielelezo vyovyote, hali hiyo inaonesha wazi kwamba fedha za umma zimepotea. Hili limethibitishwa na Watendaji kwa kukiri kwamba matumizi hayo yamefanyika pasi na kuwepo vielelezo. Kamati yetu haikuridhika na majibu ya Watendaji wa Wizara na kusisitiza fedha zote zitumike kama zinavyoelekeza Sheria za fedha.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kwa vile fedha iliyotumika ni nyingi, Kamati yetu inavishauri vyombo vya uchunguzi ikiwemo ZAECA kufuatilia kwa undani suala hili na kama itabainika Mtendaji yeyote kuhusika na upotevu huo, achukuliwe hatua za kisheria ikiwemo kurudisha fedha husika zilizosababishwa kupotea kwa uzembe wake.
2. Wizara iwe na utaratibu mzuri wa kuhifadhi vielelezo vya malipo wanapomaliza kutumia fedha za umma.

## TAASISI YA UTAFITI WA MIFUGO ZANZIBAR (ZALIRI)

### Taarifa ya Matumizi

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZALIRI) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,310,971,925 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 850,343,925 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 65 ya makadirio.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Katika kufuatilia mwenendo wa malipo ya mishahara ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo iligundua kwamba kuna baadhi ya miezi mishahara wa wafanyakazi ilikuwa ikizidi na kuelezwa kwamba kwa wakati huo Taasisi hii ilikuwa changa, hivyo ilikuwa ikipokea wafanyakazi tofauti kwa njia ya kuhamishwa (transfer) ili kuziba mapengo ya wafanyakazi na kupelekea mabadiliko ya mshahara hiyo.

Sambamba na hilo, Kamati yetu ilitaka kufahamu malipo ya Mshauri Elekezi yanatokana na kitu gani kwani ZALIRI imeonekana kutumika fedha kumlipa Mshauri huyo na kuelezwa kwamba Taasisi ilipoanzishwa ilikuwa haina majengo yenye mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Hivyo, kwa mujibu wa sheria, walilazimika kumtafuta Mshauri Elekezi kutoka Serikalini ili aweze kufanya tathmini ya majengo na kuwapatia malipo yao.

Kamati baada ya kupatia ufafabuzi huo iliridhika na mjibu hayo na haikuwa na hoja zaidi.

### Hoja nambari 6.11.2.1: Kukosekana kwa Sera za Utafiti wa Mifugo

Kwa mujibu wa kifungu nambari 8 (1) (c) cha Sheria Nambari 7 ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar ya mwaka 2020 kimeanisha kwamba Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi hiyo ina jukumu la kutoa miongozo kuhusu utayarishaji na utekelezaji wa sera za utafiti wa mifugo.

Ukaguzi uliomba kupatiwa sera za utafiti wa mifugo kwa dhumuni la kuzipitia na kujiridhisha utekelezaji wake. Hadi kumalizika kwa ukaguzi sera za utafiti wa mifugo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kukosekana kwa sera hizo katika ukaguzi kumepelekea kujitokeza kukwamisha jitihada za wakaguzi za kuweza kushauri namna bora ya utayarishaji na utekelezaji wa sera za utafiti wa mifumo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar kuhakikisha unaandaa sera madhubuti na kuziwasilisha wa wakaguzi kwa lengo la kuzipitia na kutoa ushauri wao juu ya maboresho ya sera hizo kwa lengo la kuisaidia Serikali kufikia malengo ya kuanzishwa kwa Taasisi hiyo.

**Majibu ya ZALIRI**

Kwa wakati huu Taasisi inatumia agenda ya Utafiti ya Serikali (Zanzibar Research Agenda) katika kutekeleza majumu yake ya utafiti wa Mifugo.

Vile vile, Taasisi imeshakamilisha uandaaji wa miongozo ya utafiti (Standard Operating Procedures SOP's) ambazo zitafanikisha upatikanaji wa sera ya Utafiti wa Mifugo kwa ajili ya Taasisi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba ni kweli wakati Mkaguzi inamaliza majukumu yake ya ukaguzi katika Taasisi hii, hawakuwa na Sera za Utafiti wa Mifugo isipokuwa walikuwa wakitumia sera ya mifugo iliyomo ndani ya sera ya utafiti wa kilimo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inaitaka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kuharakisha mchakato wa kuandaa sera ya mifugo ili kuepusha kasoro kama hii kujirudia tena katika ukaguzi unaofuata.

**Hoja nambari 6.11.2.2: Kukosekana kwa Daftari la Usajili wa Utafiti na Maendeleo ya Mifugo**

Kwa mujibu wa kifungu 5(2)(j) cha Sheria nambari 7 ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar kimeanisha kwamba ZALIRI itakuwa na jukumu la kusajili watoa huduma muhimu wa tafiti za mifugo katika sekta ya umma na sekta binafsi, na itaendeleza daftari kuu la usajili wa utafiti na maendeleo ya mifugo.

Ukaguzi umebaini kwamba Taasisi ya Utafiti wa Mifugo haikuandaa daftari la usajili wa utafiti na maendeleo ya mifugo kama ilivyopaswa kisheria.

Kutokuanzishwa kwa daftari hilo kunapelekea kushindwa kuwatambua na kuwasajili watoa huduma muhimu wa tafiti za mifugo katika sekta ya umma na sekta binafsi jambo ambalo linaweza kupelekea kukwamisha jitihada za Serikali za kuwawezesha na kuwajengea uwezo watoa huduma hao.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZALIRI kuhakikisha unatekeleza matakwa ya kifungu 5(2)(j) cha Sheria nambari 7 ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar ili kuweza kufikia malengo ya Serikali ya kuwafikia na kuwawezesha watoa huduma wadogo wadogo ili waweze kufikia malengo waliyojipangia.

**Majibu ya ZALIRI**

Kwa mujibu wa kifungu namba 5(2)(j) ya sheria no. 7 ya mwaka 2020 ya Taasisiya Utafiti wa Mifugo, "Taasisi itasajili watoa huduma muhimu wa tafiti za mifugo katika sekta ya Umma na sekta binafsi, na itaendeleza daftari kuu la usajili wa utafiti na mandeleo ya mifugo"

Katika kutekeleza takwa hili la kisheria, Taasisi ipo katika hatua za kuandaa kanuni zitakazo tumika katika usajili wa watoa huduma za utafiti pamoja na mambo mengine ya utafiti wa mifugo kama yalivyojawa katika sheria hii.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Watendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo wamekiri kuwepo kwa kasoro hiyo na wanaandaa Kanuni za utekelezaji wake, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa Taasisi hii inatekeleza majukumu yake katika mazingira magumu kwa vile fedha zinazotokana na makusanyo ya vyanzo vyake yanawasilishwa yote katika Mfuko Mkuu wa Serikali (Hazina) na kupelekea kutobakia na fedha za gharama za uendeshaji wa Miradi wanayoitekeleza ikiwemo ufugaji ya kuku. Baada ya kugundua mambo hayo, Kamati yetu haikuwa na maoni zaidi.

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO ZANZIBAR (ZARI)

**Taarifa ya Mapato**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 95,000,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar iliweza kukusanya jumla ya shilingi 19,078,500 sawa na asilimia 20 ya makadirio.

**Majibu ya Taasisi**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar ilipata jumla Shillingi Bilioni Mbili Milioni Mia Nne Hamsini na Mbili Laki Saba Ishirini na Nne Alfu Mia Nne na Ishirini (2,452,724,420.00) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 sawa na asilimia 80 ya fedha zote. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Mbili Milioni Mia Tatu na Sita Laki Nane na Sabiini na Nne Alfu na Mia Tano (2,306,874,500.00) sawa na asilimia 96 ni kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi na Shilingi Milioni Mia Moja na Arobaini na Tano Laki Nane Arubaini na Tisa Alfu Mia Tisa na Ishirini (145,849,920.00) sawa na asilimia 22 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kama inavyoonekana kwenye Jadueli Namba 1 hapa chini.

| Maelezo | Makadirio | Kiasi halisi | Asilimia |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 2,392,200,000.00 | 2,306,874,500.00 | 96% |
| Matumizi mengineyo | 660,000,000.00 | 145,849,920.00 | 22% |
| **Jumla** | **3,052,200,000.00** | **2,452,724,420.00** | **80%** |

## Mapato halisi

Katika vyanzo hivyo Taasisi ilikusanya jumla Shilingi Milioni Kumi na Tisa Sabiini na Nane Elfu na Mia Tano (19,078,500.00) sawa na asilimia 20 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kati ya fedha hizo, Shilingi Milioni Tatu Laki Nne na Thalathini na Mbili Alfu (3,432,000.00) sawa na asilimia 17 zilikusanywa kupitia ada za uingizaji wageni, Shilingi Milioni Kumi na Nne Laki Tano na Tisiini na Sita Alfu na Mia Tano (14,596,500.00) sawa na asilimia 97 zilikusanywa kwa mauzo ya mazao na miche na Shilingi Milioni Moja na Alfu Hamsini (1,050,000.00) sawa na asilimia 2 kutoka mashamba ya ukodishwaji karafuu kama jedueli namba 2 linavyoonesha.

**Jadueli Namba 2: makadirio ya mapato ya ndani**

| Nam. | Chanzo cha mapato | Makadirio | Kiasi halisi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | UingizajiWageni | 20,000,000.00 | 3,432,000.00 | 17% |
| 2 | MauzoyaMazao/miche | 15,000,000.00 | 14,596,500.00 | 97% |
| 3 | MashambayaKarafuu | 60,000,000.00 | 1,050,000.00 | 2% |
| **Jumla** | | **95,000,000.00** | **19,078,500.00** | **20%** |

## Fedha za Washirika wa Maendeleo

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar ilikuwa na Washirika wa Maendeleo watano kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Katika kipindi hicho, ZARI ilipata jumla ya Shilingi Milioni Tisiini Laki Mbili na Alfu Hamsini na Saba Mia Sita na Sabiini na Mbili na Senti Nne (90,257,672.40) kama jedueli namba 3 linavyosomeka.

**Jadueli Namba 3: Fedha za Washirika wa Maendeleo.**

| Nam. | Jina | Kiasi (tzs) |
|---|---|---|
| 1 | Irri | 10,932,169.12 |
| 2 | Nafaka (acdi/voca) | 30,157,367.00 |
| 3 | Iita | 40,355,128.88 |
| 4 | Tari | 4,200,000.00 |
| 5 | Icipe | 4,613,007.40 |
| **Jumla** | | **90,257,672.40** |

## Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imegundua kwamba mapato yaliyokusanywa na Taasisi hii yalikuwa kidogo sana ukilinganisha na makadirio yake kwani Taasisi ilikusanya kwa asilimia 20 (makusanyo ya vyanzo vya ndani). Kamati ya PAC ilitaka kujua ni sababu ipi iliyopelekea kutokea makusanyo kidogo na kuelezwa mambo yafuatayo:-

a) kwamba mwaka 2020/2021 ulikuwa ni msimu mdogo wa uchumaji zao la Karafuu ambapo Wizara ya Fedha iliwapangia makadirio makubwa ukilinganisha na uhalisia, jambo lililopelekea kukusanya asilimia 2.
b) Kwa upande wa chanzo cha uigizaji wageni, Kamati imeelezwa kwamba chanzo hicho kiliathiriwa na kuwepo kwa maradhi ya Covid 19 kwani kinategemea zaidi watalii nchini.

Kutokana na maelezo hayo, Kamati yetu imebaini mapato ya mikarafuu yanabadilika kutegemeana na msimu husika lakini Taasisi haijaandaa taarifa ya kitaalamu watakayoiwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango ili iwawezeshe kuipangia Taasisi kiwango stahiki cha makadirio kwa mujibu wa mavuno yanayotarajiwa na kuitoa Taasisi na changamoto ya kila siku ya kutofikia lengo la makusanyo.

Kamati ya PAC pia ilitaka kujua Taasisi inayo mazao mengine katika mashamba yao zaidi ya mikarafuu na kuelezwa kwamba katika mashamba hayo kuna na mazao mengine ambayo huwa wanakodisha. Aidha, Kamati imefanikiwa kuelezwa mipango mipya ya Taasisi ya kuzalisha mafuta ya njugu na alizeti, kufanya utafiti wa mapapai ili kubaini kwanini ladha yake inabadilika pamoja na utafiti wa mboga za asili.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati inaitaka Wizara husika kukifuatilia chanzo cha mashamba ya mikarafuu kwani kuna uwezekano kikawa kina uwezo mkubwa wa kuzalisha zaidi hasa ukizingatia ndani ya mashamba hayo kuna miti mingine ambayo Taasisi huwa inaikodisha.
2. Taasisi ifanye utafiti na kutoa ripoti na kuiwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango ili kubaini kipindi gani Mashamba ya Mikarafuu huwa yanazalisha zaidi na kipindi gani huzalisha kidogo ili kuiepusha Wizara kuwekewa makadirio makubwa wakati mapato ya mashamba hayo kwa kipindi husika ni madogo.

**Taarifa ya Matumizi**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 3,052,200,000 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 2,542,982,092 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 83 ya makadirio.

**Majibu ya Taasisi**

Kwa upande wa matumizi ya kazi za maendeleo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 haikupanga kufanya matumizi kwa ajili ya kazi za

maendeleo. Hata hivyo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Taasisi ilipokea msaada wa shilingi 90,257,672 kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya kazi za maendeleo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilitaka kujua fedha za Taasisi zilitumika hasa katika maeneo gani na kuelezwa kwamba kulifanyika tafiti mbili mpunga, mbili za muhogo na nyengine ilihusu utafiti wa wadudu waharibifu wa mboga mboga.

Kamati yetu imebaini kwamba Taasisi ina maeneo yenye hekta kidogo kwa ajili ya kufanyia majaribio ya kile walichokigundua kupitia utafiti walioufanya. Maeneo yaliopo Dodeani Pemba, Mwera pamoja na Kibonde mzungu hayatoshelezi kufanyia majaribio yatakayowasaidia wao kuwaonesha wakulima matokeo ya kivitendo ya kile walichokitafiti.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo itafute mashamba mengine yatakayotumika kufanyia majaribio ya matokeo ya tafiti zao.

**WAKALA WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO - UNGUJA**

**Taarifa ya Mapato**

Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 2,211,833,672 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Kati ya fedha hizo shilingi 1,374,900,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 836,933,672 kwa ajili ya Mishahara.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ilipokea jumla ya shilingi 1,559,210,786 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 70.49 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 613,246,711 kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 44.6 ya makadirio na shilingi 830,929,504 kwa ajili ya mshahara sawa na asilimia 99.28 ya makadirio.

Aidha Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ilikusanya jumla ya shilingi 115,034,571.00 kutoka vyanzo vyake vya ndani kwa mwaka huo ambapo Wakala haikuwa na makadiro ya makusanyo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haikupokea majibu ya taarifa ya Mapato na Matumizi siku mbili kabla ya kikao husika kama ilivyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2020). Hata hivyo, Kamati yetu ilitaka kujua kwanini kwa mwaka huo Wakala haukuwa na makadirio ya Mapato kupitia vyanzo vyake vya ndani na kuelezwa kwamba kwa wakati huo Wakala ulikuwa mchanga (ulianzishwa 2019). Hivyo walikuwa

wanategemea ruzuku kama Idara ya Serikali. Kufuatia maelezo hayo, Kamati yetu ilibaini kuwa Wakala huo ulikuwa na vyanzo vyake vya mapato yatokanayo na huduma za ukulima wa matrekta tangu upo Idara ya Serikali. Kamati haikuridhika na majibu ya Wakala pamoja na kwamba kasoro hiyo kwasasa imesharekebishwa.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala uhakikishe unaainisha makadirio ya mapatov yake katika Mpango wake ili iweze kujipima kwa kiasi gani ameweza kutekeleza malengo yake.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,211,833,672. Kati ya fedha hizo shilingi 836,933,672 kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,374,900,000 kwa ajili ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 1,444176,215 sawa na asilimia ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 830,929,504 kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia ya makadirio na shilingi 613,246,711 kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC haikupokea majibu ya taarifa ya Mapato na Matumizi siku mbili kabla ya kikao husika kama ilivyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2020). Hata hivyo, baada ya kupata maelezo ya majibu hayo iliridhika na majibu na haikuwa na hoja zaidi.

**Hoja nambari 6.11.4.1: Kutokuwepo kwa hesabu (account) ya Mapato Unguja na Pemba**

Wakala wa serikali wa huduma za Matrekta na zana za kilimo kwa upande wa Unguja na Pemba hakuna hesabu ya mapato ambayo itahusika na uingizwaji wa fedha zinazohusiana na mapato pekeyake. Hali iliyopelekea mapato yote yanayokusanywa huchanganywa na fedha za matuimizi ya kawaida (OC) na kufanya uwepo wa hesabu za matumizi pasi na kuwepo hesabu ya mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 28(5) cha sheria namba 2 ya ya uanzishwaji wa Wakala wa Serikali wa huduma za Matrekta na zana za kilimo ya mwaka 2019

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekata na Zana za Kilimo kufungua hesabu kwa ajili ya uwekaji taarifa za mapato yanayokusanywa kutoka katika vyanzo vyake vya ndani.

**Majibu ya Wakala**

Katika jitihada za kuitatua changamoto hii kwa kufuata misingi ya Sheria Ofisi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo- imechukuwa hatua ya kufanya mazungumzo na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ajili ya kuangalia namna gani ya kufanikisha suala hili bila ya kuathiri shughuli za ukulima. Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imetuandikia barua rasmi yenye kumbu kumbu Namb. EA. 184/372/01/02/37 ya tarehe 23/05/2022 ambayo pamoja na mambo mengine inaeleza kuwa fedha za ukulima hazipaswi kuhesabiwa kama mapato bali ni fedha kwa ajili ya kazi maalum hadi pale gharama za ukulima zitakapotolewa. (kiambatanisho namba 1). Aidha, kwa sasa tumeshafungua Account ya mapato (kwa muongozo wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango) na tumeanza kutumia Mfumo wa ZANMALIPO na kutoa risiti za Electroniki bila ya kuathiri shughuli za ukulima

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba ni kweli Wakala ulikuwa hauna hesabu ya mapato. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba fedha za Wakala ni fedha zinazotokana na huduma kutoka kwa Wakulima zinazohitaji kuongezewa ili huduma ya kulimiwa iweze kufanyika, kwa msingi huo, Wakala haukuwa na fedha iliyobakia pasi na kufanyiwa matumizi.

Kamati pia imebaini kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 28 cha sheria ya kuanzishwa Wakala wa Huduma za Matrekta Zanzibar imeweka wazi kwamba fedha hizo sio chanzo cha mapato iwapo Waziri wa Kilimo kwa kushauriana na Waziri wa Fedha watakubaliana kutoa toleo litakaloeleza wazi kwamba fedha kutoka kwa Wakulima hazitotambuliwa kama mapato isipokuwa fedha zitakazobakia baada ya kutolewa huduma ya kilimo ndio zitawasilishwa hazina.

Kupitia barua ya tarehe 23/5//2022 yenye kumbukumbu nambari EA.184.372.01.02.37 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango imekamilisha utaratibu ulioelezwa na SHeria ya Wakala. Kutokana na maelezo hayo pamoja na kwamba barua hiyo imewasilishwa wakati Mkaguzi ameshaondoka lakini Kamati imeridhika na majibu yaliyoelezwa.

**Hoja nambari 6.11.4.2: Kutokuoneshwa kwa Makadirio ya Mapato shilingi 115,034,571**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa serikali wa huduma za Matrekta na zana za kilimo Zanzibar imekusanya jumla ya Tsh 115,034,571 ikiwa ni mapato ya ndani yanatokana na vyanzo mabali mbali vya mapato ya wakala, lakini makadirio ya mapato hayo hayakuweza kubainishwa ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamaizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 .

Ukaguzi unashauri kuwepo makadirio ya mapato ili kuweza kupima ufanisi utokanao na makusanyo kutoka katika vyanzio mbali mbali vya mapato sambamaba na upatikanajai

wa ufanisi wa shughuli za Wakala.

**Majibu ya Wakala**

Uongozi wa WAKALA unakubaliana kwamba kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hakukua na makadirio ya mapato. Hata hivyo suala hili tayari limeshafanyiwa kazi ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 WAKALA imeweka makadirio ya mapato na matumizi kama ilivyoshauriwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Amati imebaini kwamba wakati Mkaguzi anatekeleza wajibu wake wa Kikatiba, ni kweli Wakala haukuonesha makadirio yake ya mapato kama yalivyooneshwa kati Ripoti ya Mkaguzi. Hata hivyo, hivi sasa Wakala umeshapata muongozo kutoka Wizara ya Fedha na Mipango na Kamati yetu imesisitiza kuwa iendelee kuutekeleza muongozo huo ipasavyo.

**Hoja nambari 6.11.4.3: Kutokuidhinishwa kwa chanzo kipya cha kodi**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 1,650,000 zimepokelewa na Wakala wa seikali wa wa huduma za Matrekta na zana za kilimo kupitia mkataba wa 1/4/ 2021 wa makubaliano ya ukodishwaji wa Trecta kwa Sinohdro Coparation Ltd kwa ajili ya utayarishaji wa mashamba kupitia makubaliano hayo imebainika kuwa mkodishwaji atapaswa kufanya malipo ya muda wa saa moja la ufanyaji kazi wa trekta na fedhaa hizo ziingizwe kwenye muamala wa Wakala baada ya kutoa Ankara (invoce) ya kudai malipo kwa mpokea huduma.

Ukaguzi umebaini kuwa mapato yanayotokana na chanzo hicho hayakuidhinishwa na na Bodi ambao ndio wasimamizi wakuu wa wakala wa serikali wa huduma za Matrekta na zana za kilimo kinachohusika na mipango ya kibiashara.

Ukaguzi unashauri kuwa katika kila hatua ya utekelezaji wa Shughuli za Wakala ni vyemakufanya ushirikishwaji wa bodi katika masuala yote ya maamuzi ili kuepusha ataharai ya kufanyika kwa shughuli ambazo hazijaridhiwa na bodi.

**Majibu ya Wakala**

- Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo inakataa hoja ya Mkaguzi kuwa kulikuwa na chanzo kipya ambacho hakikusajiliwa, kiuhalisia ni kwamba kutoa huduma za matrekta na zana za kilimo kwa wakulima, taasisi za Serikali na binafsi ni jukumu la msingi la Wakala kwa mujibu wa Sheria Nam. 2 ya

2019.

- Kwa upande wa kufanyakazi na kampuni ya SINOHDRO COPARATION LTD haikuwa na chanzo kipya cha kukusanya mapato kwani Wakala ililazimika kuingia mkataba na kampuni hio kutokana na namna ya malipo yalivyokuwa yakifanyika. Kwa maana ya kwamba kampuni hii ilikuwa ikilipa baada ya kazi kufanyika tofauti na wakulima na wateja wengine ambao kwa kawaida hulipa kabla ya kazi kuanza. Aidha, kwa sasa Wakala haina kazi inayoendelea na kampuni hii.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya PAC imegundua kwamba mapato ndio yaliyokuwa hayakuidhinishwa na Bodi na sio kodi kama ilivyoelezwa na Mkaguzi kwani Wakala huwa unatoa huduma ya kuwalimia shamba zao wakulima na kuchangia ujira mdogo unaotambulika kuwa mapato ya Wakala na sio Kodi.

Kadhalika, Kamati yetu imeisisitiza Wakala kuwa na viwango tofauti vya utozaji wa gharama za malipo kwa wakulima wanyonge ukilinganisha na Makampuni. Hata hivyo, Kamati imebahatika kupatiwa baadhi ya viwango tofauti vya huduma zinayotolewa na Wakala.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wakala uhakikishe unaendelea kuandaa viwango vinavyoendana na hali halisi ya wanaopewa huduma kwani haitokuwa sahihi kwa malipo ya Mkulima wa kawaida yawe sawa na malipo ya Makampuni.

**Hoja nambari 6.11.4.4: Kuwepo kwa fedha zisizostahiki katika hesabu (account) ya Wakala shilingi 5,795,072.98**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa katika hesabu ya wakala kuna ongezeko la fedha kiasi cha shilingi 5,795,072.98 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 bila ya kupatikana kwa maelezo yanayohusiana na fedha hiyo hali mabyo inaweza kupelekea kutokupatikana kwa usahihi wa hesabu za wakala ambapo ni kwenda kinyume na viwano vya ufungaji wa Hesabu za mwishoo wa mwaka vya Kitaifa na Kimataifa

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuwa makini katika kuandaa Taarifa za Hesabu kwa usahihi na kwa mujibu wa sheria na viwango vilivyoekwa ili kuepuka kuingiza kiasi cha fedha zisizostahiki katika hesabu za wakala.

**Majibu ya Wakala**

Uongozi wa WAKALA umeupokea ushauri na tayari umeufanyia kazi kwa kuwasiliana na Benki husika kwa barua yenye kumbu kumbu nambaWSHM/2017/BNK/005 ya tarehe 14/04/2022 ili kupata ufafanuzi wa miamala hiyo na kurekebisha kasoro zilizokuwepo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuchunguza hoja hii, Kamati ya PAC imebaini kuwa Wakala ulifanya malipo kwa Mtoa Huduma (El-Nabhany Auto Mobile) na kumlipa fedha zake. Hata hivyo, kulijitokeza tatizo benki ambapo imebainika watendaji wa benki hawatoa fedha katika hesabu ya Wakala na kuonekana uwepo wa bakaa hiyo wakati wa ufungaji wa hesabu.

Kwa bahati nzuri, Kamati yetu ilibahatika kuziona risiti zinazothibitisha Mtoa Huduma kupokea fedha hizo kupitia risiti ya tarehe 3/7/2020 yenye nambari 15520 (560,094,91), tarehe 10/4/2020 yenye kumbukumbu nambari 1778 (829,345,80) tarehe 18/3/2018 yenye nambari 0250 (1,212,542 na risiti ya tarehe 23/6/2020 yenye nambari 15507 (1,407,545,77). Kutokana na maelezo hayo, Kamati iliridhika nayo na haikuwa na maelezo zaidi.

**WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO - PEMBA**

**Hoja nambari 6.11.4.5: Kutokuwepo kwa Kitengo cha uhasibu.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa kitengo cha uhasibu katika ofisi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na zana za Kilimo Pemba ili kuweza kudhibiti mfumo wa fedha wa mapato na matumizi pamoja na usimamia wa rasilimali za Umma

Hali hii imepelekea kutokuwepo kwa udhibiti wa mapato na matumizi yanayohusu ofisi hiyo kwa upande wa Pemba ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na zana za Kilimo Pemba kuhakikisha kwamba kitengo cha uhasibu kinakuwepo na kinafanya kazi ya utowaji wa huduma zinazokusudiwa kwa kufanya mawasiliano ya karibu na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba ili kuharakisha upatikanaji wa watendaji kwa ajili ya kuhudumia kitengo hicho.

**Majibu ya Wakala**

Ni kweli Ofisi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo - Pemba haikuwa na Kitengo cha uhasibu wakati wa ukaguzi na imeendelea kuwa hivyo hadi mwezi Agost 2022 na hivyo kulazimika kutumia Kitengo cha uhasibu cha Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo Ofisi kuu Pemba kwa ajili ya kusimamia masuala yote ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma.

Katika jitihada za kuitatua changamoto hii kwa kufuata misingi ya Sheria, Ofisi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo- Pemba imechukuwa hatua ya kuomba kupatiwa muhasibu kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango – Pemba (barua namba WSHM/MMM/2022 ya tarehe 3/03/2022 inahusika) na kwa sasa ujenzi wa Kitengo cha uhasibu umeanza na kimeanza kufanyakazi zake baada ya kupatikana

kwa muhasibu mnamo mwezi Julai 2022 kama inavyosomeka katika barua AG.03/0406/01/37 ya tarehe 20/7/2022.

Hatua hii imezingatia matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya 2016 kifungu nambari 17 (1) (d) kimempa uwezo Muhasibu Mkuu wa Serikali kuajiri, kupandisha daraja kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, kutoa mafunzo na kuhamisha maafisa wahasibu wanaohusika na masuala ya uhasibu katika Taasisi za Umma.

Aidha, Ofisi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo - Pemba tayari imechukuwa hatua ya kuiomba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango - Pemba kuipatia watendaji wengine kwa ajili ya kukamilisha uundji wa kitengo hichi barua AB.143/2/02 ya tarehe 19/10/22 inahusika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati baada ya Kamati kupata majibu ya wizara imeelezwa kwa vile wakala wa matreta ndo kwanza inameanzishwa walikuwa hawana kitengo cha uhasibu , hata hivyo,2019 taasisi imeanzishwa na muundo umedhibitishwa 2021 hadi kamati inaondoka tayari wakala imechukua hatua ya kupatiwa watendaji.

**Hoja nambari 6.11.4.6: Dosari zilizobainika katika mapokezi ya Vitabu vya Mapato.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari za mapokezi ya vitabu vya mapato kwa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba ambapo dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kutokujulikana idadi kamili ya vitabu vilivyopokelewa.
- Kukosekana kwa uthibitisho wa mapokezi (Delivery Order).

Kukosekana kwa taarifa kamili ya vitabu vilivyowasilishwa kutoka makao makuu ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Zanzibar na kujulikana idadi halisi ya vitabu vilivyopokelewa kunatia shaka juu ya ukusanyaji wa mapato kuwa umeendana na vitabu halisi vilivyopokewa jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa mapato kwa kutumia vitabu ambavyo havikupokelewa na kuorodheshwa katika daftari maalum la kuwekea kumbukumbu za vitabu vya ukusanyaji wa mapato (counter foil register).

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba kuhakikisha kwamba mapokezi yote yanayofanyika yanatakiwa kufuata utaratibu ikiwemo kuweka rikodi katika vitabu vya uthibitisho wa mapokezi na kuwasilisha hati ya mapokezi (delivery Order).

**Majibu wa Wizara**

Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo - Pemba ilipokea vitabu vya risiti 10 kutoka Ofisi kuu Unguja tarehe 27/08/2018 vitabu hivi vimeanzia nambari 000501 mpaka 01000. Kumbukumbu za vitabu vilivyopokelewa zimerikodiwa katika daftari la kumbukumbu katika Ofisi za Wakala Unguja na kusainiwa na Ofisa aliyepokea wakati wa mapokezi.

Aidha, Ushauri wa Mkaguzi tumeupokea na tumeufanyia kazi. Vitabu vyote vya kupokelea mapato vilivyopokewa kutoka makao makuu ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo – Zanzibar vimeingizwa katika daftari la mapokezi Ofisi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo - Pemba kama ilivyoelekezwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Wakala umekiri kutokea dosari hiyo na waliieleza Kamati kwamba tayari wameshachukua hatua kama majibu yanavyojieleza.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inaishauri Wakala kufuata taratibu za manunuzi kama zilivyoelekezwa na Sheria husika.

**Hoja nambari 6.11.4.7: Kutokuonekana kwa Mapato katika Taarifa za Benki Shilingi 3,257,500**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 3,257,500 ni mapato ya Wakala kutokana na utoaji wa huduma mbali mbali lakini mapato hayo hayakuonekana katika taarifa za benki hali ambayo inatia shaka katika ufuatiliaji wa taarifa za mapato yatokanayo na huduma mbali mbali zinazotolewa, hivyo kushindwa kujiridhisha juu ya ufanisi wa mapokezi na matumizi halisi ya mapato hayo.

Kufanya hivyo nikwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mapato yaliokosekana ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 201: Mapato yaliyokosekana katika taarifa za benki**

| Nambari ya stakatabadhi | Nambari ya slip ya benki | Tarehe iliyolipwa | Aliyelipa | Kiasi cha fedha kilichopokelewa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 00604 | Haina | 30/4/2021 | Wakala wa Matrekta na zana za Kilimo | 110,000 | Fedha Kwa ajili ya uchongaji na Ukodishaji matrekta |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 00512 | 0665813 | 21/9/2020 | Khamis Mgau Kombo | 20,000 | Fedha kwa ajili ya kuchoma na kuchonga |
| 00590 | 0358035, 0637900, 0358273, 0665812 | 30/9/2020 | Wakala wa Matrekta na zana za Kilimo | 3,127,500 | Fedha kwa ajili ya huduma ya kulimia. |
| **Jumla** | | | | **3,257,500** | |

**Majibu ya Wizara**

Mapato yenye Jumla ya Shilingi 3,257,500/- yaliyolipwa katika hesabu za WAKALA yanaonekana katika taarifa za Benki za mwezi wa Septemba 2020 na April 2021 pamoja na slip zake za malipo kama zinavyofafanuliwa katika jadweli nambari 1 lililopo chini:- Aidha, nyaraka zote husika na vielelezo vimeambatanishwa na viko tayari kwa ukaguzi.

**Jadweli nambari 1: Ufafanuzi wa Mapato yaliyokosekana kuonekana wakati wa ukaguzi**

| **Nambari ya stakabadhi** | **Nambari ya slip ya benki** | **Tarehe ya uandishi wa stakbadhi** | **Aliyelipa** | **Kiasi cha fedha kilichopokelewa Tsh** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|
| 00604 | 0640135<br><br>0640136 | 30/4/2021 | Wakala wa Matrekta na zana za kilimo | 100,000<br><br>10,000 | Fedha hizi ziliingizwa benki tarehe 23/04/2021 taarifa ya benki ya mwezi wa Septemba 2021 inafafanua. |
| 00512 | 0665813 | 21/9/2020 | Khamis Mgau Kombo | 20,000 | Fedha hizi zilingizwa benki<br><br>21/09/2020 |
| 00590 | 0358035,<br><br>0637900,<br><br>0358273,<br><br>0665812 | 30/9/2020 | Wakala wa matrekta na zana za kilimo | 600,000<br><br>405,000<br><br>600,000<br><br>1,522,500 | Fedha hizi ziliingizwa benki<br><br>29/9/2020<br><br>28/9/2020<br><br>25/9/2020<br><br>21/9/2020 |
| **Jumla** | | | | **3,257,500** | |

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Wakati kamati ilipokuwa katika uchunguzi wake imebaini kuwa mkaguzi kutoka Ofisi ya Mkaguzi wa Serikali wakati wa ukaguzi hakupatiwa vielelezo ila jambo la kusikitisha kamati ilipatiwa vielelezo hivo na kuelezwa kwamba hali hii imetoka na kuchanganyika kwa majalada kamati haikufurahishwa hoja hii.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Kamati ya PAC inashauri wakala waweke kukumbuku vizuri ili kuepusha mgongano wakati mkaguzi anapokuja kwa ajli ya ukaguzi na kupatiwa ushirikiano wakati wa ukaguzi.

### RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM KUHUSU MALIPO YA WAZEE YA PENCHENI JAMII KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2020

### 2.5: UHAKIKI WA PENCHENI JAMII

Kutokana na tathmini iliyofanywa katika uhakiki wa mfumo wa ndani wa usimamizi wa malipo wa pencheni jamii ambapo katika uhakiki huo zimebainika dosari zifuatazo:-

### Hoja namba 2.5.1: Fedha ambazo hazikuwasilishwa Benki baada ya zoezi la Pencheni Tzs. 2,720,000.

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 2,720,000 ni bakaa ya malipo ya Pensheni ya mwezi wa Julai na Agosti, 2020 ambazo hazikurejeshwa benki badala yake zimetumika kwa ajili ya shughuli za uendeshaji. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma namba 12 ya 2016.

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 2,720,000 ni bakaa ya malipo ya pencheni ya mwezi wa Julai na Agosti, 2020 ambazo hazikurejeshwa benki badala yake zilitumika kwa ajili ya shughuli za uendeshaji. Bakaa ya fedha hizo zinajionesha katika Jadweli lifuatalo:-

| Mwezi | Wilaya Magh. (A na B) | Wilaya Kask. A | Wilaya Mjini | Wilaya Kati | Wilaya Kask. B | Fedha zilizobaki |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Julai | 580,000 | 40,000 | 700,000 | 100,000 | - | 1,420,000 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2020 | | | | | | |
| Agosti 2020 | 560,000 | 40,000 | 580,000 | 80,000 | 40,000 | 1,300,000 |
| **Jumla** | | | | | | **2,720,000** |

Ukaguzi unashauri kupitia uongozi wa Wizara kuhahakikisha unafuata utaratibu na miongozo iliyoaiishwa katika utekelezajiwa malipo ya pencheni.

**Majibu ya Wizara**

Kuchelewa kurudishwa fedha shilingi 2,720,000 za mwezi wa Julai na Agosti kumetokana na kuwepo kwa uhakiki ambao umesababisha uchelewaji wa uhakiki wa fedha halisi zinazopaswa kurudishwa benki kwa miezi hiyo husika. Pia, Mshika Fedha anatakiwa kabla ya kuzirudisha ajiridhishe kwa kupitia vocha moja baada ya moja ambapo zoezi hili lilipelekea kuchukua muda mrefu. Vile vile, alijiridhisha kwa kufanya uhakiki baina ya orodha za malipo na marejesho ya walipaji vituoni. Hata hivyo, baada ya kukamilika na kujiridhisha fedha hizo zilirejeshwa Benki kwa stakabadhi ya tarehe 10/11/2020.

Aidha, hakukuwa na matumizi yoyote ya shilingi 2,720,000 yaliyofanyika kwa ajili ya Kitengo cha Pensheni kwa shughuli za Uendeshaji isipokuwa fedha zilichelewa kurudishwa benki kama ufafanuzi wa hapo juu unavyojionesha. Hata hivyo, Wizara inauchukua ushauri na kuhakikisha unafuata utaratibu na miongozo iliyoainishwa katika muongozo wa utekelezaji wa Pensheni Jamii.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Wizara kukiri kuhusu kuwepo kwa hoja ya Mdhibiti, Kamati imebaini kuwa Wizara ilikiuka utaratibu ulioainishwa katika Muongozo wa Pencheni Jamii kwamba fedha ikipitwa na miezi mitatu inatakiwa irudishwe Hazina badala yake Wizara ilikuwa inakaa na fedha kwenye akaunti yao ya Wizara jambo ambalo sio sahihi. Hata hivyo, Kamati iliridhika na maelezo na vielelezo vilivyotolewa na kubaini kwamba hakukuwa na matumizi mabaya ya bakaa ya fedha ya shilingi 2,720,000 badala yake fedha zilirudishwa benki kupitia dokezo la tarehe 10/11/2020 kwa bakaa ya shilingi 1,420,000 ya mwezi wa Julai, 2020 na shilingi 1,300,000 kwa mwezi wa Agosti, 2020.

Kadhalika, Kamati imebaini fedha ya Pencheni Jamii na fedha ya uendeshaji zinatumia akaunti moja kinyume na utaratibu unavyoelekezwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, nambari 12 ya mwaka 2016 pamoja na muongozo wa Pencheni Jamii. Kutokana na hali hiyo, Kamati imegundua kwamba Wizara inashindwa kuzitambua ipasavyo kiasi gani cha fedha kilicholipwa Wazee na zipi zimebakia kulingana na bakaa

ya mwezi husika ambapo Wizara ilieleza itawasilisha orodha ya fedha zilizotumika na fedha zilizowasilishwa benki lakini hadi kamati inawasilisha hotuba hii hakuna orodha iliyopokelewa na Kamati.

Kutokana na kuchanganywa kwa fedha zenye vyanzo viwili tofauti katika hesabu moja, ndio hoja ya Mdhibiti kueleza kwamba fedha hizo zilikuwa zikitumika kwa shughuli za uendeshaji kitu ambacho kwa kiasi kikubwa Kamati inakubaliana nacho.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inapendekeza kwamba hesabu (account) ya Pencheni Jamii isichanganywe na hesabu ya uendeshaji ili kuepusha kuwepo kwa dhana ya kuchanganywa kwa matumizi ya hesabu hizo mbili.
2. Kamati inapendekeza kuwa Wizara ifuate muongozo ulipo unaoelekeza utaratibu wa malipo ya Pencheni Jamii kwamba fedha za miezi mitatu zinazobakia ziwasilishwe benki kwa wakati.

**Hoja namba 2.5.2: Bakaa ya fedha nyingi ambazo zinahifadhiwa kwenye matajuri baada ya malipo ya shilingi 106,720,000/-**

Ukaguzi umebaini uwepo wa fedha jumla ya shilingi 106,720,000 ambazo zinahifadhiwa kwenye matajuri ikiwa ni bakaa ya fedha baada ya kukamilika kazi ya ulipaji wa Pensheni kwa Wazee, hali hii huweza kupelekea upotevu wa fedha au kuweza kufanyika kwa matumizi kinyume na utaratibu. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

**Jadweli lifuatalo linaonesha muhtasari wa bakaa ya jumla ya shilingi 106,720,000**

| Mwezi | Bakaa ya Fedha baada ya malipo (Tshs) | Fedha ilopitiwa na muda na kupelekwa benk (Tshs) | Fedha iliyohifadhiwa katika Tajuri (Tshs) |
|---|---|---|---|
| Agosti | 28,200,000 | 2,140,000 | 26,060,000 |
| September | 25,400,000 | 1,420,000 | 23,980,000 |
| Oktoba | 23,440,000 | 1,300,000 | 22,140,000 |
| November | 34,540,000 | - | 34,540,000 |
| **Jumla** | **111,580,000** | **4,860,000** | **106,760,000** |

Ukaguzi unashauri kupitia uongozi wa Wizara kuhakikisha unafuata taratibu na muongozo wa utekelezaji wa Pencheni Jamii ikiwemo fedha zinazobakia kupelekwa benki kwa wakati kwa mujibuwa taratibu.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ilikuwa inafuata utaratibu wa kurejesha benki bakaa la fedha zote zilizomaliza mzunguko wa malipo kwa muda wa miezi mitatu na kubakisha fedha za miezi miwili kwa ajili ya malipo yanayoendelea.

Wizara tayari imeanza utaratibu wa kuzipeleka fedha zote zinazobaki katika ulipaji wa Pensheni bila ya kuangalia zile zinazobaki katika mzunguko wa miezi mitatu.

**Uchunguzi ya Kamati ya PAC**

Kamati imebaini fedha zilizokuwepo kwenye matajuri ni fedha ambazo zilikuwa katika mzunguko kwani Wizara ilikuwa inachukua zaidi ya fedha za mwezi mmoja kwa ajili ya kuzipeleka kwenye vituo mbali mbali vya ugawaji pencheni Unguja na hatimae kubakia na kuzihifadhi. Hata hivyo, Kamati ilihoji ni utaratibu gani unaotumika katika uchukuaji wa fedha hizo benki na kuelezwa kuwa fedha huchukuliwa benki kabla ya siku ya kuzigawa. Baada ya mjadala mkubwa, Kamati ilibaini kwamba hoja ya Mdhibiti ilikuwa sahihi kwamba fedha zilikuwa zinabakia kwenye matajuri isipokuwa wamejirekebisha na kasoro hiyo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati inapendekeza kwamba wakati fedha inapotaka kugaiwa kwenye vituo husika ni lazima wafanye utaratibu wa kuzichukua Benki siku husika ili kuepusha ulimbikizaji wa fedha nyingi kwenye matajuri.

**Hoja namba 2.5.3: Kutokuandaliwa kwa taarifa ya usuluhishi wa benki (bank reconcilation).**

Ukaguzi umebaini ya kwamba Kitengo cha Pensheni Jamii hakiandai taarifa za usuluhishi wa kibenki (Bank reconcialition) kupelekea kushindwa kudhibitisha usahihi wa bakaa za fedha zinazoonekana katika daftari la kuhifadhia fedha za pencheni. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, nambari 12 ya mwaka 2016 .

**Majibu ya Wizara**

Wizara imeupokea na kuanza kuufanyia kazi ushauri wa kufuata taratibu za kifedha za kutayarisha taarifa ya usuluhishi wa kibenki (bank reconciliation) ili kuweza kujua mtiririko wa fedha baina ya daftari la fedha (cash book) na miamala ya kibenki. Na kwa hivi sasa tayari utaratibu unafanyika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Wizara kukubaliana na hoja ya Mdhibiti, Kamati ilitaka kujua ni mwezi gani ambao Wizara imeanza kufanya usuluhishi wa kibenki na kuelezwa kwamba

zoezi hilo limeanza mwezi wa Julai, 2021. Baada ya ufafanuzi huo, Kamati iliridhika na majibu na haikuwa na maelezo zaidi.

**Hoja namba 2.5.4: Malipo yaliyolipwa kinyume na taratibu Tzs. 1,560,000.**

Katika uhakiki imebainika kwamba jumla ya shilingi 1,560,000 zilipangwa kwa ajili ya malipo ya wazee 78 kutoka shehia mbali mbali za Unguja ambao hawakutimiza kigezo cha ukamilifu wa umri kwa mujibu wa muongozo wa utekelezaji wa Pensheni Jamii.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuweka utaratibu mzuri wa Usajili wa Wazee ambao wanastahiki kupokea Pencheni Jamii pamoja na kufanya uhakiki mara kwa mara.

**Majibu ya Wizara**

Programu ya Pensheni Jamii inaongozwa kwa kupitia Sheria ya Wazee namba 2 ya mwaka 2020 pamoja na Mwongozo wa Utekelezaji wa mwaka, 2016 ambao unatoa maelekezo kwa watu wote watakaohusika na utekelezaji wa Mpango wa Pensheni Jamii kwa Wazee Zanzibar (MPJWZ).

Mwongozo, pamoja na mambo mengine, unaainisha wajibu na majukumu ya wadau wote, sifa za waombaji pamoja na watakaohusika na utekelezaji wa programu hiyo, kama zinavyoelekezwa katika sehemu ya 3.3 ya Utaratibu wa Maombi katika mwongozo wa utekelezaji wa Pensheni Jamii.

Vile vile, katika kipengele cha 3.4 Utaratibu wa Uhakiki kinaeleza Uhakiki unachukua nafasi muhimu katika kufanya maamuzi juu ya fomu ya maombi au lalamiko. Taarifa zote zilizojazwa katika Fomu ya Maombi zitahitajika kuhakikiwa ili kuhakikisha kuwa waombaji wametimiza vigezo. Uhakiki utafanyika kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kwa ajili ya Mpango huu.

Hata hivyo, mbali ya Kitambulisho cha Mzanzibari kuna vitambulisho vyengine ambavyo Programuu huvitumia ili kutambua umri wa mzee, vitambulisho hivyo ni pamoja na kitambulisho cha Saidi Washoto, Tarjisi ya kuzaliwa, Kitambulisho cha zamani cha wapiga kura na Kitambulisho cha Mtanzania.

Hivyo ni wazi kuwa wazee hao 77 licha ya kuwa vitambulisho vyao vya Mzanzibari havikuendana na umri unaotakiwa kwa ajili ya usajili ndani ya Programmu lakini pia waliwasilisha vielelezo vyengine au walipitia kipengele cha uhakiki ambacho ni muhimu katika kuthibitisha maamuzi yanayofanywa kabla ya mzee kusajiliwa.

Pia, ifahamike kwamba wazee hawa wengi wao walikuwa tayari wamo kwenye programu hii tokea mwaka 2016 ambapo programu hii ilianza rasmi. Tunaamini lengo la Serikali la kuwafikia walengwa limefikiwa na linaendelea kusimamiwa uzuri sana.

Hata hivyo, inajulikana kuwa vitambulisho hivi vingi vyao haviendani na umri halisi wa wazee, na ndio maana vingi vyao havina tarehe wala mwezi bali huwekwa xx na kwa

sasa inatumika tarehe 1/1, hii ni kutokana na asilimia kubwa ya wazee kutokuwa na tarjisi ya kuzaliwa ya uthibitisho wa umri halali wa mzee. Baada ya kuonekana athari hii na wazee wengi kulalamika kuwa wakubwa kiumri ila vitambulisho vyao vinawakana ndipo kilipoekwa kipengele cha uhakiki ili kutatua changamoto hiyo. Hivyo kwa wazee hao 77 hadi kuingizwa katika Mpango wa Pensheni Jamii tayari wameshapitia hatua hiyo ya uhakiki na ikathibitika kuwa wamekidhi vigezo, na ndio maana wapo kama walengwa.

Ili kujiridhisha umri wa mzee Afisa husika hufanya uhakiki huo kwa kutumia njia ya mahojiano ambayo hujumuisha mzee mwenyewe, familia, watoto, majirani au mtu wake wa karibu ili kuweza kufanya tathmini ya umri wa mzee. Vile vile, huwa tunatumia matukio ya kihistoria katika uhakiki ili tuweze kupata umri halisi wa mzee.

Pamoja na majibu hayo tunaambatanisha na nakala za fomu za maombi za wazee hao ambapo zimepitia hatua ya uhakiki na kuthibitisha umri wao umekidhi vigezo.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati ilibaini kwamba Wazee waliodaiwa kulipwa bila ya kukamilisha kigezo cha kutimiza umri wa miaka 70 walikuwa ni 77 badala ya 78 kama walivyoainishwa katika kitabu cha Mdhibiti. Hilo limetokana na kutoandikwa kwa nambari 43 ambapo baada ya 42 imeruka hadi 44. Hata hivyo, Wizara imeweza kuwasilisha vielelezo vya umri vya Wazee 72 na ilishindwa kuwasilisha vielelezo vya Wazee 5 kwa Wizara kudai kwamba inawezekana vielelezo vyao vilipotea kutokana na kuhamisha nyaraka wakati walipohamia katika jengo jengine.

### Mapendekezo ya Kamati

1. Wizara iwe na utaratibu mzuri wa kuhifadhi nyaraka za Wazee wanaowahudumia ili ziweze zinapatikana wakati wowote zinapohitajika.
2. Wizara ihakikishe inawasajili wazee waliotimiza kigezo cha miaka 70 pasi na kuwa na shaka yoyote. Kufanya hivyo, kutaondoa malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba kuna upendeleo unafanyika katika uteuzi wa wazee wanaoingizwa katika mpango huo.

### UKAGUZI WA MFUMO WA USIMAMIZI WA PENCHENI JAMII (ZANZIBAR UNIVERSAL PENSION SYSTEM - ZUPS)

Kitengo cha Pencheni Jamii kinatekeleza shughuli zake kwa kutumia Mfumo wa Usimamizi wa Pencheni Jamii ambao unatumika kwa ajili ya kusajili taarifa za walengwa, kupanga bajeti ya malipo ya walengwa pamoja na kutunza kumbukumbu za malipo wanayofanyiwa walengwa hao. Aidha, mfumo huo umeunganishwa na vifaa vya

kufanyia miamala (ving'amuzi) vinavyotumika katika vituo vya malipo.

Vile vile vifaa hivyo vinatumika kufanya uhakiki wa walengwa kwa kutumia alama za vidole kabla ya malipo. Baada yakukagua mfumo huo, ukaguzi umebaini dosari mbali mbali zifuatazo:-

**Hoja namba 2.6.1: Kutokuwa na udhibiti kwa Watumiaji wa Mfumo (System User Controls).**

Ukaguzi umebaini kwamba kuna watumiaji wa mfumo bado wanaonekana kuwa na uwezo wa kutumia mfumo (active status) licha ya kutohusika na shunguli za matumizi ya mfumo huo. Kuendelea kuwepo kwa watumiaji hao kunaweza kupelekea kufanyika kwa matumizi yasiostahiki ya mfumo ikiwemo kufanya miamala iliyo kinyume na utaratibu uliowekwa kupitia watumiaji hao.

Ukaguzi unapendekeza kwamba kuwe na utaratibu kwa kupitia watumiaji wa mfumo (user Access Review ) ili kuhakikisha kila mtumiaje asiyesajiliwa kwenye mfumo anastahiki kwa mujibu wa matumizi yake, vile vile kuwepo kwa sera na miongozo itakayodhibiti matumizi ya mfumo wa Pencheni Jamii.

**Majibu ya Wizara**

Orodha ya watumiaji wa mfumo wa ZUPS, ambao wameorodheshwa kutumia mfumo, wote wanasababu za uwepo wao 'active' kwa kipindi ambacho wakaguzi walifanya ukaguzi huo kwenye Programu ya Pencheni Jamii. Ila kwa sasa wengi wao wamekuwa hawajiwezi kutokana na kutokuwa na kusita kushiriki au kutumika katika mfumo huu. Orodha ya watumiaji hao ni kama ifuatayo:

1. **Msimamizi 'Admin' Unguja:** Ndugu Rukaiyya Khamis Othman, alikuwa ni Msimamizi Mkuu wa Mfumo wa ZUPS ambapo alipaswa kuwepo 'active' kutokana na kutokabidhisha rasmi mfumo wa Pensheni Jamii.
2. **Kalinda, Omar.Web na Maina Unguja**: Hawa ndio watengenezaji wa mfumo wa Pensheni Jamii (ZUPS-MIS) kutokana na Mfumo kutokuwa sawa katika kipindi hicho kimatumizi tulilazimika kuwaweka 'active' kwa lengo la kutupatia 'support' ili kufanikisha zoezi la malipo. Ila kwa sasa Kalinda na Maina wao wamekuwa (disabled) kutokana na kumaliza 'support' kwa upande wa Unguja, ila kwa upande wa Pemba Omar.web bado anaendelea kutoa support kwa upande wa Pemba kwa hiyo huyo active mpaka sasa.
3. **Khatibu.Bushiri, Zahor.salum, Yussuf.Husen, Fatma.Hassan na Zakaria Fabian:** Hawa ni maafisa ambao huwa wanashiriki katika zoezi la Pensheni Jamii katika nafasi tofauti kama maafisa ustawi, walipa fedha au wakaguzi. Hivyo uwepo wao kwenye mfumo ni kutokana na kuwa wanatumika katika zoezi la malipo ya Pensheni Jamii.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba kuna Mfanyakazi (Omari.web kutoka Wizara ya Mawasiliano) ambae anafanya kazi za mfumo lakini sio Mfanyakazi wa Wizara. Kamati imeelezwa kwamba wakati mfumo unawekwa, mfanyakazi huyo alikuwa miongoni mwa waanzilishi walioshirika kuufunga na kwa kipindi hicho Wizara ilikuwa haina mtu wa kuongoza 'IT' ambae anaufahamu kwa undani mfumo huo.

Sambamba na hilo, Kamati imebaini kuwa mfumo wa Pencheni Jamii mpaka sasa hauna 'security' jambo ambalo linaweza kupelekea hatari kubwa kwa Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla. Kamati imeelezwa kwamba kutokana na changamoto ya uhaba wa wafanyakazi wa 'IT' Wizara inaendelea na hatua za kuajiri wafanyazi wapya wa 'IT'.

Kamati imepata mashaka makubwa kwa vile mtu ambae anauendesha mfumo huo anatoka nje ya Wizara hiyo ambae anaweza kufanya jambo lolote la kuhujumu (kuharibu) mfumo huo. Kubwa zaidi ni kwamba mfanyakazi huyo hana hata mkataba unaoonesha kwamba ana makubaliano ya kuuongoza mfumo au anapatiwa ujira kutokana na kazi anayoifanya.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC inaishauri Wizara kuharakisha uajiri wa Wafanyakazi wapya watakaokuwa na utaalamu wa kuusimamia Mfumo huo ili iweze kuondokana na changamoto ya kumtumia Mfanyakazi kutoka nje ya Wizara.
2. Wizara ihakikishe kila Mtumiaji wa Mfumo anasajiliwa kwa kupatiwa utambulisho maalum utakaomruhusu kuingia ndani ya Mfumo huo.
3. Mfumo uwekewe ulinzi (security) wa kutosha ili uweze kuhifadhi taarifa ipasavyo na ziweze kutumika zinapohitajika.

**Hoja namba 2.6.2: Kutokuwiana kwa taarifa za Mfumo**

Ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa uwiano wa taarifa za mfumo wa malipo ya pencheni baina ya taarifa za Ving'amuzi (POS) na taarifa zilizomo kwenye orodha ya hati za malipo kwa wanufaika wanaotarajiwa kulipwa. Kutokuwiana kwa taarifa za Mfumo wa Malipo kunaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa fedha na uwezekano wa kufanyika malipo yasiostahiki.

**Majibu ya Wizara**

Mpango wa Pensheni Jamii (ZUPS) kwa sasa unatumia mifumo miwili ya kuhifadhia taarifa za wazee, mfumo wa zamani (MS Access) na mfumo mpya (ZUPS MIS). Mfumo mpya umeanza kutumika rasmi mwanzoni mwa mwezi wa Februari, 2020. Tokea kipindi hicho mfumo huo mpya ulikuwa katika zoezi la maboresho ya uwekaji sawa wa taarifa na hadi unafika muda wa ukaguzi kulikuwa bado haujakaa sawa jambo ambalo lilipelekea kutokuwa na usahihi wa taarifa hizo.

Hivyo, kutokana na tatizo hilo, ilitulazimu kwenda katika vituo vya malipo na orodha za majina ya wazee kutoka katika mfumo wa zamani (eligible lists) ili kuhakikisha kuwa taarifa za wazee zinazotolewa katika ving'amuzi (POS) ziko sawa na za uhakika katika malipo. Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa msimamizi mkuu wa mfumo na kumalizika muda wa mkataba wa "support" kutoka kwa Mtaalamu Muelekezi, Aidha suala hili Uongozi wa sasa umeliona na uko mbioni kulitafutia ufumbuzi.

Kwa hatua za awali, Uongozi ulijaribu kuomba majalada na nyaraka zote muhimu za mfumo huu ili taratibu za utatuzi wa changamoto za mfumo huo zianze kutoka kwa Wizara husika (ambayo ilitambulika kwa jina la Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto) ambapo Kitengo cha Pensheni Jamii kilikuwa ndani yake. Nyaraka zilipatikana katika hali ya kuchelewa na wakati huo huo zilihitajiwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa ajili ya zoezi maalum la ukaguzi uliofanyika ndani ya Kitengo hicho kwa kipindi cha muda wa miezi miwili (Disemba, 2021 - Febuari, 2022). Ili kufanikisha zoezi la ukaguzi huo likamilike Kitengo kililazimika kusitisha utaratibu huo wa utatuzi wa changamoto hizo hadi ukaguzi maalum umalizike.

Kwa hatua ya pili, baada ya ukaguzi kukamilika watendaji wa Kitengo walilijadili suala hili pamoja na Mkurugenzi husika na kuja na rai ya kwamba Wizara ipeleke ombi kwa Wakala wa Serikali Mtandao (e-GOZ) Zanzibar, la kupatiwa wataalamu kwa ajili ya kuja kuufanyia tathmini mfumo huo (ZUPS-MIS) na kuishauri Wizara juu ya maamuzi ya kuendelea kuutumia Mfumo huo na kufanyiwa maboresho ya changamoto hizo au kuundwa kwa mfumo mwengine mpya wa malipo ya Wazee ambao utakidhi haja ikibidi kufanya hivyo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba Mfumo unatumia mifumo miwili kuweza kutekeleza majukumu husika. Hili limesababishwa na uhamishaji wa taarifa kuzipeleka katika Mfumo Mkuu wa Serikali (e-government). Hali hiyo imepelekea wasiwasi juu ya usahihi wa taarifa zilizomo katika Mfumo wa Malipo.

Aidha, Kamati imebaini kwamba watendaji wa Wizara wanafanya kazi kwa kasi ndogo sana isiyokidhi utatuzi wa changamoto zilizojitokeza kwani ni kipinfi kirefu kimepita tangu wakaguzi walipokamilisha kazi zao na muda ambao Kamati imefuatilia hoja za Mdhibiti. Kamati ilitegemea kuelezwa kwamba tathmini ya mfumo huo iwe tayari

imeshafanyika ili iweze kujua kama unakidhi haja ya kufanya kazi za pencheni jamii au hauwezi badala yake Kamati imeshuhudia changamoto ya kutokuwepo majibu ya tathmini ya mfumo.

**Mapendekezo ya Kamati**

1. Wizara kuhakikisha Mfumo utakaotumika kwa malipo ya Pencheni Jamii unakuwa na taarifa zilizokamilika na zilizo sahihi.
2. Watendaji wa Wizara waharakishe kuufanyia tathmini mfumo ya pencheni jamii ili uweze kujulikana uwezo na ufanusi wake.

**RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM KUHUSU UFANISI WA UTEKELEZAJI WA MRADI WA KILIMO CHA PILIPILI HOHO KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2020.**

Katika ufuatiliaji wa Ripoti Maalum ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na Miradi ya kilimo cha Pilipili Hoho ambayo ilibuniwa na Wizara inayoshughulikia vijana ili uweze kuwanyanyua kiuchumi. Jumla ya shilingi milioni 560,000,000 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi hiyo. Miongoni mwa miradi iliyoibuliwa ulikuwa Mradi wa kilimo cha Pilipili Hoho ambao kupitia utafiti uliofanywa na kampuni ya Vegrab ilibaini maeneo ya Bambi Okoteni, Kijini Matemwe, Jendele na Mihulani ndio maeneo ambayo kilimo hicho kinaweza kustawi (kwa upande wa Unguja) na maeneo ya Dodo Pujini na Finya kwa upande wa Pemba chini ya usimamizi wa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC). Kiuhalisia, Miradi hiyo ilianza kutekelezwa katika maeneo mawili ya Bambi na Pangatupu bila ya mafanikio na haukuweza kutekelezwa kwa upande wa Pemba kutokana na changamoto zilizoanza kutokea wakati wa utekelezaji wake Unguja.

Miongoni mwa hoja zilizobainika ni:

**Hoja nambari 3.5.1 Mapungufu katika Mkataba wa miundombinu ya visima**

Katika kupitia mkataba wa makubaliano baina ya Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) na Kampuni ya Kasara Construction kwa ajili ya uchimbaji wa visima viwili, ujenzi wa minara miwili na uwekaji wa matangi mawili ya kuhifadhia maji yenye ujazo wa lita 5,000 katika eneo la Pangatupu Wilaya ya Kaskaizini ‘B’ na Bambi Wilaya ya Kati .

Ukaguzi umebaini mapungufu yafuatayo:

- Kutokuainishwa kwa tarehe ya ufungwaji wa mkataba pamoja na muda wa kuanza na kumalizika kwa kazi ya uchimbaji wa visima.
- Kutokuainishwa kwa Mshauri Elekezi (Consultant) kwa kazi ya uchimbaji wa visima.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 63 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na taratibu za ufungwaji wa mikataba.

**Majibu ya Wizara**

Mkataba wa uchimbaji wa Visima baina ya ZSTC na Kampuni ya Kasara Construction ulianisha tarehe ya ufugwaji ambayo ni tarehe 11/6/2019 na kumalizika ni tarehe 11/7/2019. Kazi hii ilikuwa ni ya mwezi mmoja kutoka siku ya kuanza kazi.

Mshauri Elekezi hakuainishwa katika mkataba huo kutokana na Kampuni ya Kasara kuwa na uwezo wa kuchimba visima. Aidha, uwepo wa Kampuni ya Vegrab uliweza kutoa ushauri kwani wao ndio waliofunga miundombinu ya umwagiliaji maji katika mashamba ya pilipili.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imehoji kwa nini Mkaguzi kutoka kwa Ofisi ya Mthibiti hakupatiwa Mkataba huo na kuelezwa kwamba kulikuwa na kutokufahamiana baina ya Watendaji wa ZSTC na Mkaguzi. Hata hivyo, Kamati imefanikiwa kukagua mkataba huo na kujiridhisha kwamba kweli uliofungwa tarehe 11 Julai, 2019 baina ya ZSTC na Kasara Consruction and Elecrical Services Limeted

Kamati haikufanikiwa kuthibitisha uainishwaji wa Mshauri Elekezi katika Mkataba huo kwani hakukuwa na makubaliano ya wazi kati ya Wizara na Mshauri Elekezi huyo, pamoja na kwamba Wizara ilimtumia 'Vegrab Oganic Farming Company Limited' kama Mshauri Elekezi kwa vile alikuwa msimamizi wa mashamba na mtekelezaji wa mradi wote kwani alikuwa na utaalamu wa umwagiliaji maji na masuala miundombinu ya mashamba hayo

Kamati imebaini kuwa kulikuwa na mikataba miwili katika utekelezaji wa mradi wa Pilipili hoho, ambapo wa kwanza ulihusisha ZSTC na 'Vegrab Oganic Farming Company Limited' ulifungwa tarehe 31 May, 2019 ambao ulikuwa unaeleza 'Vegrab' atashughulikia utekelezaji wa shamba ikiwemo kuwapatia soko la pilipili, kusambaza mbengu pamoja na kufunga miundombinu yote ya shamba wakati mkataba wa pili ulikuwa baina ya ZSTC na 'Kasara Consruction and Electrical Services Limited' ambao unahusiana na uchimbaji wa visima viwili pamoja na kujenga mnara ambao umefungwa tarehe 11 Julai, 2019 baina ya Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) na Kampuni ya 'Kasara'.

Kamati ya PAC, baada ya kupata ufafanuzi wa hoja hiyo iliridhika na majibu hao isipokuwa ilitoa mapendekezo yafuatayo:

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara inapotekeleza Miradi ambayo inatumia fedha nyingi za Serikali ihakikishe wana muajiri Mshuri Elekezi ili aweze kusaidia katika uwekaji sawa wa baadhi ya changamoto zinazojitokaeza kabla, wakati na baada ya kilimo.
2. Wizara iwe na utaratibu mzuri wa uwekaji wa kumbukumbu zake na iwapo zitahitaji wakati CAG anakagua lazima apatiwe.

**Hoja nambari 3.5.2: Mapungufu katika miundombinu ya usambazaji wa maji Pangatupu.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo jumla ya shilingi 41,167,500 ambazo zilitengwa na kutumika kwa ajili ya uwekaji wa miundombinu ya usambazaji wa mtandao wa maji katika eneo la ekari 15 lililopo Pangatupu.

Ukaguzi umebaini upungufu wa kutokuwepo kwa uthibitisho wa utekelezaji wa mradi kulingana na gharama halisi zilitumika katika uwekaji wa miundombinu ya usambazaji wa maji katika eneo husika. Aidha, miundombinu ya usambazaji wa maji katika eneo lilikosudiwa iliondoshwa kutokana na eneo husika kuanzishwa kilimo kingine cha viazi.

Kutokuwepo kwa uthibitisho wa gharama zilizotumika katika uwekaji wa miundombinu ya maji ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, nambari 12 ya mwaka 2016.

Majibu ya Wizara

Makubaliano ya utekelezaji wa kilimo cha Pilipili Hoho ni kuwa kila ekari moja ina gharimu kiasi cha TZS 5,664,500. Fedha hizi zinahusisha uandaaji wa shamba na upigaji wa matuta, ufungaji wa miundombinu ya umwagiliaji maji, upandaji wa mipilipili, madawa pamoja usimamizi wa shamba hadi uvunaji wa pilipili.

Utekelezaji wa mradi kwa shamba la Panga Tupu ulianza na kuzinduliwa na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B kwa wakati huo (Ndg. Rajab A. Rajab) mnamo tarehe 25/09/2019. Aidha, mradi huu uliingizwa katika ratiba ya miradi iliyotarajiwa kuzinduliwa katika sherehe za Maadhimisho ya Mapinduzi ya Zanzibar Januri, 2020. Hata hivyo, mradi huu ulikuja kuondoshwa kutokana na changamoto ya mvua iliyopelekea kutofikika vizuri katika eneo la shamba pamoja na shamba kujaa maji.

Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imebaini kuwa bakaa ya fedha ya shilingi 4,167,500 zilitumika katika shamba kwa kusambazia miundombinu ya maji lakini katika kipindi cha ukaguzi, Mdhibiti hakuona miundombinu hiyo kwa sababu iliondoshwa kwa ajili ya kilimo cha viazi baada ya kumefanyika uharibufu wa miundombinu na kuibiwa na kuna kesi ipo Polisi.

Kwa bahati mbaya, Kamati haikufanikiwa kuthibitisha uwepo wa kesi hiyo isipokuwa walifanikiwa kutembelea maeneo yaliyokuwa yamefungwa miundombinu hiyo.

Kamati imebaini kuwa katika utafiti mdogo (study) iliyofanywa na kampuni ya Vegrab na kutoa ripoti yake juu ya maeneo ambayo yangeweza kupandwa Pilipili Hoho, halikuwemo eneo la Pangatupu. Kamati ilipotaka majibu kuhusiana na hoja hiyo ilijibiwa kwamba eneo hilo liliingizwa kisiasa na sio kutokana na 'study' ilifanyika. Aidha, Kamati ilipotembelea eneo la Pangatupu ilibaini kwamba eneo hilo ni lenye ardhi aina ya kichanga ambalo lipo bondeni, sehemu ambayo inakaa (inatuwama) maji ya mvua.

Sambamba na hilo, Kamati imegundua hakukuwa na uhifadhi mzuri wa miundombinu iliyowekwa katika eneo hilo kwani miundombinu yote imeondolea (haikuwepo) na wala haikuhifadhiwa ili iweze kutumika maeneo mengine hasa ukizingatia miundombinu hiyo ilitumia fedha nyingi za umma. Pia, hakukuwa na ushirikishwaji mzuri wa vijana katika maamuzi yaliyofanyika ya kulima viazi badala ya Pilipili Hoho kama ilivyokusudiwa.

Kiujumla, Kamati ya PAC imebaini kuwa zoezi zima la usamabazaji wa miundombinu ya maji katika shamba la Pangatupu lilikabiliwa na uzembe mkubwa uliofanywa na watendaji wa ZSTC na hatimae kupelekea matokeo yasiyokuwa na tija yoyote kwa vijana na wananchi kwa ujumla.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wizara inapotaka kutekeleza mipango yake ifuate tafiti (study) zinazofanywa ili kutekeleza miradi yake ipasavyo na kuleta tija kwa wananchi.
2. Wizara inatakiwa ishirikishe wadau wa sekta husika wanapoamua kufanya maamuzi ya jambo linalowahusu vijana ili kupunguza malalamiko yao.

### Hoja nambari 3.5.3: Mapungufu katika miundombinu ya usambazaji maji Bambi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo jumla ya shilingi 27,445,000 ambazo zilitengwa kwa ajili ya uwekaji wa miundombinu ya usamabazaji wa maji katika shamba la Pilipili hoho lenye ekari kumi (10) liliopo Bambi. Hadi ukaguzi unakamilika jumla ya shilingi 19,211,500 zilibainika kutumika kwa ajili ya uwekaji wa miundombuni katika eneo la ekari saba (7)

Ukaguzi umebaini mapungufu yafuatayo-:

- Kutokuwepo kwa udhibitisho wa utekelezaji wa mradi kulingana na gharama halisi zilizotumika kwa ajili ya uwekaji wa miundombinu ya usamabazaji maji katika ekari husika. Aidha, baadhi ya miundombinu katika eneo la utekelezaji wa mradi umeonekana kuwa chakavu hivyo kushindwa kusambaza maji katika eneo husika.
- Kuwepo kwa bakaa ya fedha ya shilingi 8,238,500 ambazo hazikutumika kwa ajili ya usambazaji wa maji hivyo kupelekea kushindwa kufika malengo yaliyokusudiwa.

Kutokuwepo kwa uthibitisho wa gharama zilizotumika katika uwekaji wa miundombinu ya maji ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar

nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu ya Wizara**

Mradi wa Pilipili Hoho kwa Wilaya ya Kati shamba la Bambi ni kwa ekari 10, katika shamba hili kulikuwa na changamoto za upatikanaji wa eneo la shamba ambapo kulikuwa na wakulima wanaolima viazi. Hali hii ilipelekea kufungwa miundombinu yote ya umwagiliaji maji kwa ekari 7. Hata hivyo, baada ya kumalizika kwa mavuno ya viazi shamba lote liliandaliwa matuta na kufungwa miundombinu ya umwagiliaji na kufikia ekari 10.

Bakaa hiyo ya fedha ilikuwa kwa ajili ya madawa na pembejeo nyengine ambazo zilitarajiwa kutumika wakati wa utekelezaji wa mradi kwa kupambana na wadudu waharibifu na wakati wa uendelezaji wa shamba pembejeo hizo zilitumika.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imegundua kwamba kulikuwa na bakaa hiyo ya fedha  zilitumika kwa ajili ya kufungwa miunfombinu kilimo cha Pilipili hoho. Hata hivyo, mradi wa Pilipili Hoho katika eneo la Bambi ulishindwa kutekelezeka na kuleta tija iliyokusudiwa kutokana na sababu tofauti zikiwemo za kutopatiwa mafunzo ya kujengewa uwezo (Capacity building) vijana waliokuwa wakishughulikia Mradi huo pamoja na kutokuwepo mashirikiano kati ya vijana na wanachama wa Jumuiya ya Wazazi wa CCM waliokuwa wanamiliki eneo hilo.

Hili limethibitishwa na Kamati baada ya kulitembelea eneo hilo na kugundua hakukuwa na miundombinu wala Pilipili Hoho isipokuwa kulikuwa na mnara pamoja na tangi moja la maji la lita 5,000, banda moja na choo chake linalotumiwa na watu waliowekwa na katibu wa Jumuiya ya Wazazi. Kamati ilipohoji kuhusu miundombinu ya maji, ZSTC walieleza tayari wameshaikabidhi Wizara inayoshughulikia Vijana pamoja na fedha zilizobakia (milioni 300) lakini kamati ilibaini kuwa baadhi ya miundombinu ya maji michache sana iliyokuwepo katika shamba hilo na mingine ilikuwa imehifadhiwa nje ya shamba kwenye nyumba ya Sheha.

Aidha, Kamati ilibaini kuwepo kwa mgogoro wa eneo hilo la ardhi kwani vijana waliazimwa kulitumia kwa miaka mitatu lakini hakuna kilichotekelezwa na Jumuiya ya Wazazi kulichukua na kuanza kuliendeleza kwa kulima mazao mengine.

Kamati pia imegundua makabidhiano ya shamba hilo kwa vijana kulima hayakufanyika kimaandishi kwani walipewa kwa maelezo ya mdomo kutoka Serikali ya Wilaya. Hali hiyo imechangia kukuza mgogoro uliojitokeza.

Kamati baada ya kupatiwa maelezo hayo iliridhika na majibu yaliyowasilishwa na kutoa mapendekezo yafuatayo:

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati imesikitishwa na utekelezaji wa mradi kwa vile fedha za Serikali zimepotea bila ya kuwafaidisha walengwa wa mradi huo. Kadhalika, Kamati imebaini eneo lililofanyika mradi huo linaweza kuleta tija kubwa kwani linaruhusu ukuaji na uendelezwaji wa kilimo hicho iwapo mradi utatekelezwa na kusimamiwa ipasavyo.

1. Wizara inapotekeleza miradi ya maendeleo ihakikishe inaisimamia ipasavyo ili iweze kutekelezeka na kufikia malengo yaliyokusudiwa.
2. Wizara kwa kushirikiana na ZSTC na Wizara ya Vijana wahakikishe mgogoro wa ardhi uliopo unapatiwa ufumbuzi.
3. Wizara ihakikishe kunakuwepo makubaliano ya maandishi iwapo pande mbili zitajitokeza kuazimia kutekeleza mradi.

**Hoja nambari 3.5.4: Utunzaji usioridhisha wa vifaa vya usambazaji wa maji**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa utunzaji na usimamamizi usioridhisha kwa vifaa vya usambazaji maji katika maeneo ya utekelezaji wa mradi wa kilimo cha pilipili katika eneo la Pangatupu na eneo la Bambi.

Baadhi ya mapungufu yaliyojitokeza kwa mipira uliyokusudiwa kusambaza maji kutoka kwenye visima hadi kwenye shamba za pilipili hoho za Pangatupu na Bambi wenye thamani ya shilingi 14,167,5000.

Kutokuwepo kwa utunzaji na usimamizi usioridhisha wa vifaa vya usambazaji maji ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(1)(a) cha Sheria ya Usiamamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu ya Wizara**

Miundombinu ya umwagiliaji maji katika mashamba ya Pilipili Hoho yalifungwa katika matuta kulingana na mahitaji ya umwagiliaji maji. Kutokana na chagamoto ya mvua katika shamba la Pangatupu, kumeipelekea Serikali kutoa maamuzi ya kusitisha ulimaji wa pilipili katika shamba hilo na miundombinu ihamishiwe sehemu nyengine itakayoonekana inafaa. Hata hivyo, Serikali ya Wilaya ya Kaskazini B ilihifadhi miundombinu hiyo na kupisha kilimo cha viazi katika shamba hilo.

Aidha, kwa upande wa shamba la Bambi kulikuwa na wizi wa mpira mkubwa wa usambazaji maji kutoka kwenye Tenki na kupeleka shambani ambapo jambo hili liliripotiwa Polisi Dunga na kuchukuliwa hatua. Miongoni mwa hatua hizo ni kufikishwa Mahakamani kwa mtuhumiwa aliyekamatwa na mpira huo wa maji. Vile vile, wamiliki wa shamba la Bambi ambao ni Jumuiya ya Wazazi CCM walikabidhi shamba hilo kwa mtu mwengine kwa ajili ya kilimo cha matikiti. Mtu huyo aliondoa miundombinu hiyo na baadhi yake kuihifadhi kwenye banda liliopo kwenye shamba hilo na kuingiza trekta kwa ajili ya kulima, jambo ambalo lilileta sintofahamu baina ya Sheha wa Shehia ya Bambi pamoja na mkulima huyo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imegundua kwamba ni kweli kulikuwa na uhifadhi wa miundombinu ya shamba usioridhisha kwani Kamati ilikuta mpira mmoja wa maji wenye urefu wa mita 60 (kwa kukisia) na kuambiwa mwengine umewekwa nje ya Afisi ya Sheha lakini mwengine mwingi umeibwa. Hata hivyo, Kamati haikuweza kuthibitisha kuibwa kwa mpira huo kwani hakukuwa na kielelezo chochote kinachothibitisha hayo. Aidha, Kamati imebaini kuwepo kwa mnara pamoja na tangi lake la maji la lita 5,000, kisima lakini pampu ya maji yake iliyokuwa ikitumika iliibwa.

Sambamba na hilo, Kamati imeona banda na choo kiliopo nje ya banda hilo ambalo linakaliwa na vijana waliowekwa na Katibu wa Wazazi wa eneo hilo baada ya kuona Mradi umeshindwa kutekelezeka.

Kamati imebaini kuwa ardhi ya eneo hilo inakubali kilimo cha Pilipili kwani imekuta mipilipili michache iliyobaki ikiwa imezaa vizuri. Vile vile, kulikuwa na kisima na pampu nyengine iliyosemekana haikuwekwa na Mradi.

Kamati haikuridhika na majibu ya Watendaji wa Wizara kuhusu uwekaji mbaya wa kumbukumbu na kuungana na hoja ya Mdhibiti kwa kupendekeza yafuatayo:

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara husika ifuatilie mipira iliyopo kwa Sheha na kuihifadhi vizuri kwa matumizi endelevu ya umma.
2. Wizara husika ifanye maamuzi ya tangi ya matumizi ya tangi liliopo katika shamba hilo ili liweze kutumika kwa maslahi ya umma kwani kuliwacha pale bila ya kuwepo ulinzi wowote linaweza kuibwa.
3. Wizara husika iwakabidhi Umoja wa Wazazi eneo lao kwa vile wao hawana mpango wa kulitumia eneo hilo.

**Hoja nambari 3.5.5: Kutokufikiwa kwa lengo la Utekelezaji wa Mradi**

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba WBV/W.10/1V0L.1/161 ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Mradi wa Kilimo cha Pilipili Hoho ulipaswa kutekelezwa kwa ujumla eneo la ekari sitini (60) ambapo Unguja ni eneo la ekari thalathini (30) na Pemba ni ekari thelathini (30).

Katika ufuatiliaji wa maeneo yaliyokusudiwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, ukaguzi ulibaini upungufu wa kutokufikiwa kwa lengo la kulima eneo la ekari kumi na tano (15) katika eneo la Bambi Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja ambapo hadi ukaguzi unakamilika imebainika ni eneo la ekari saba (7) zilizolimwa. Aidha kwa upande wa utekelezaji mradi katika kisiwa cha Pemba jumla ya ekari thalathini (30) zilizotengwa hazikulimwa.

Kutokufikia kwa lengo la utekelezaji wa mradi ni kwenda kinyume na Sheria ya

Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Aidha ni kwenda kinyume na agizo la barua kutoka Wizara husika pamoja na Mikataba.

**Majibu ya Wizara**

Kwa upande wa shamba la Bambi, Serikali ya Wilaya ya Kati ilishindwa kupata eneo la ekari 15, hivyo mradi ulitekelezwa kwa ekari 10 na makubaliano yote yalifikiwa baina ya Serikali ya Wilaya ya Kati, Baraza la Vijana na ZSTC juu ya ulimaji wa ekari 10 kwa kilimo cha Pilipili Hoho kwa shamba la Bambi. Aidha, kwa upande wa Pemba mradi huu haukutekelezwa kutokana na changamoto zilizojitokeza kwa mashamba ya Unguja. Hivyo, ilionekana ni vyema kutatua changamoto zilizojitokeza kwa upande wa Unguja ndipo mradi uendelee kwa Pemba.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Katika kuifuatilia hoja hii, Kamati imegundua kwamba majibu yaliyotolewa na ZSTC pamoja na Wizara ya Kilimo yanagongana na kugusa Wizara nyengine za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, Kamati imebaini kuwa miongoni mwa sababu zilizozorotesha utekelezaji wa Mradi huu ni kutozishirikisha baadhi ya Taasisi muhimu ikiwemo ZAWA.

Kadhalika, Kamati imebaini kuwa hakukuwa na makubaliano yoyote ya maandishi yaliyothibitisha kwamba utekelezaji wa kilimo cha pilipili hoho ufanyike katika ekari kumi (10) kama inavyoelekezwa na Mkataba kwa upande wa eneo la Bambi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Miradi ya Serikali inapoanzishwa iwashirikishe wataalamu wote wanaohusika na utekelezaji wa Mradi husika.
2. Wizara inapofanya utekelezaji wa Mradi, kunatakiwa kuwepo kwa maandishi yatakayothibitisha mabadiliko yoyote yaliyojitokeza katika utekelezaji halisi.

**Hoja nambari 3.5.6: Mapungufu Katika hatua za utekelezaji wa Mradi**

Katika ukagazi uliofanyika imebainika kwamba kuna maeneo mbali mbali yaliyofanyiwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya utekelezaaji wa mradi wa kilimo cha Pilipili Hoho ambapo maeneo yaliyopendekezwa ni Bambi Oketoni, Kijini Matemwe, Jendele, Mihulani, Dodo, Pujini na Finya.

Ukaguzi umebaini mambo yafuatayo:-

- Kutekelezwa mradi wa Pilipili hoho katika eneo la Pangatupu ambalo halikuainishwa na kupendekezwa katika maeneo ya utekelezaji wa maeneo ya mradi huu.
- Kutokushirikishwa kwa wataaalamu wa kilimo ambao wangeweza kutoa ushauri kitaalum unaohusiana na maeneo yanayofaa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi

huu.

Kutokufuatwa kwa hatua za utekelezaji wa mradi ni kwenda kinyume na matakwa ya ripoti ya upembuzi yakinifu inayohusiana na mradi huu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kufuatia hoja na majibu yaliyotolewa, Kamati ya PAC imebaini kuwa baadhi ya maeneo ikiwemo Pangatupu liliamuliwa kulimwa kilimo cha Pilipili hoho wakati eneo hilo lilikuwa halifai kwa mujibu wa tafiti ndogo iliyofanywa. Hata hivyo. Kamati ilifanya kikao cha pamoja na Wizara nne ikiwemo Wizara Kilimo, Wizara ya Biashara, Wizara ya Fedha na Wizara ya Vijana ili kujua ushikishwaji wa kila Taasisi katika mradi huu. Baada ya majadiliano hayo. Kiujumla, Kamati ya PAC imebaini kuwa katika utekelezaji mradi huo hakukuwa na ushirikishwaji uliotekelezwa na Wizara zilizohusika. Hili lilibainika baada ya Wizara hizo kutofautiana katika baadhi ya majibu waliyokuwa wakiyawasilisha.

Hata hivyo, Kamati yetu imepata uthibati kwa kuona ushahidi wa makabidhiana ya shilingi 377,000,000 zilizokuwa hazijatumika baina ya ZSTC na Wizara ya Vijana, kuhusiana na uhaulishwaji wa fedha kutoka ZSTC A/C NO: 0404078000 na kwenda katika A/C NO: WIZARA YA VIJANA

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Serikali inapofanya Miradi yake ya Maendeleo kama hii ifanye katika maeneo yanayomilikiwa na Serikali.
2. Kamati inashauri Serikali inapotekeleza Miradi ya Serikali ifuate Ripoti za Kitaalamu.

**UTEKELEZAJI WA MRADI WA PILIPILI HOHO KATIKA ENEO LA BAMBI**

Katika eneo la Bambi, Mradi ulitekelezwa katika ekari 10 kwa kuchimba kisima kimoja, ujenzi wa banda la kuhifadhia vifaa, choo pamoja uvutaji wa umeme kwa kuweka nguzo tano, kusambaza miundombinu ya maji, ununuzi wa mbolea pamoja na kilima Pilipili hoho.

Kupitia Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kusini (Afisa Tawala) ambae ilikubaliana na wamiliki wa eneo hilo (Jumuiya ya Wazazi) kuwaazima vijana (bila ya malipo yoyote) ili waweze kuanzisha Mradi wa kulimo cha Pilipili hoho kwa muda wa miaka mitatu na baadae waweze kukubaliana tena kama waendelee au wasiendelee kulitumia eneo hilo kwa shughuli za kilimo hicho. Lakushangaza, makubaliano hayo yalifanywa pasi na kuwepo maandiko yoyote.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

1. Kamati iligundua kuwa Mradi umefeli na haukuwa na tija yoyote iliyopatikana kulikotokana na sababu tofauti ikiwemo kutowashirikisha ipasavyo vijana ambao

ndio wadau wakuu wa Mradi.
2. Upatikanaji wa eneo la kilimo hicho haukufuata taratibu zinazotakiwa kwani hakukuwa na mkataba au maandishi yoyote yanayothibitisha makubaliano ya kulitumia eneo hilo kwa shughuli za kilimo.
3. Kamati imebaini hakuna kilimo cha Pilipili hoho kinachoendelea kufanyika katika shamba hilo badala yake Kamati imeshuhudia watu binafsi wanaendeleza kilimo cha yanya chungu.
4. Banda lililijengwa katika shamba hilo linatumiwa na vijana (kimakaazi) waliowekwa na Katibu wa Wazazi.
5. Hakuna miundombinu ya maji katika eneo hilo isipokuwa kuna baadhi ya mipira ya maji ipo katika Afisi ya Sheha na mingine imeibwa.
6. Mradi haukuwashirikisha wataalamu wa kilimo badala yake walikabidhiwa ZSTC kushughulikia na kutafuta soko hali ya kwamba hawana utaalamu wa kilimo hicho.
7. Kuna mgogoro wa matumizi ya eneo hilo unaendelea kati ya Jumuiya ya Wazee na baadhi ya vijana waliokuwa wakinufaika na Mradi huo.
8. Kuna upotevu wa rasilimali fedha iliyotumika kununulia miundombinu ya maji pamoja na fedha za uanzishwaji na uendelezwaji wa kilimo cha Pilipili hoho.

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Miradi ya Serikali inapotekelezwa inatakiwa ishirikishe wataalamu wa kila Idara inayohusika na uanzishwaji na uendelezwaji wa mradi husika.
2. Miundombinu ya miradi ihifadhiwe vizuri ili iweze kutoa tija iliyokusudiwa kwa vile huwa inatumia fedha nyingi.
3. Serikali ihakikishe inafuata taratibu zote za upatikanaji wa eneo kwa ajili ya utekelezaji Mradi kabla ya utekelezaji kuanza.
4. Wizara ihakikishe inafuatilia miundombinu ya maji iliyokuwa imewekwa katika shamba hilo na kupelekwa katika Afisi ya Sheha na mingine kuchukuliwa na watu wasiojulikana (kupotea).

## MRADI WA PILIPILI HOHO PANGATUPU

1. Katika kusimamia matumizi ya fedha za Mradi huu, Kamati ililazimika kufika katika eneo jengine la Pangatupu ambalo Mradi huu wa Pilipili Hoho ulitekelezwa. Jumla ya Milioni 9.5 zilitumika katika eneo la Pangatupu kwa uchimbaji wa kisima, ujenzi wa mnara na uwekaji tenki a lita 5,000. Aidha, Mradi huo ulifanikiwa kupeleka umeme kutoka Skuli kwa kununua nguzo tatu.
2. Eneo la Pangatupu halikuainishwa katika Ripoti ya Kitalaamu lakini Wizara ilielekeza Mradi huo utekelezwe katika eneo hilo kinyume na ushauri ilivyokuwa. Katika Ripoti ya Kitaalamu maeneo ya Bambi Okoteni, Kijini Matemwe, Jendele na Mihulani yaliyoainishwa kuwa yanaweza kutumika kwa kuzalisha Pilipili Hoho. Kadhalika, Kamati ya PAC imegundua kwamba fedha za Serikali zimepotea kwani hakukupatikana tija yoyote iliyotokana na Mradi wa Pipili hoho kwani eneo hilo

lipo chini na kusababisha maji ya mvua kufurika na kuozesha pilipili hoho zote zilizokuwa zimeoteshwa. Sambamba na hilo, Kamati imebaini Mradi haukutumia fedha zote ambapo jumla ya shilingi milioni 377 zilibakia ZSTC na kukabidhiwa Wizara inayohusiana na Vijana.

3. Kamati ilipotaka kujua ukweli wa hilo, ZSTC walieleza kwamba kufeli kwa Mradi huo kulizihususha Taasisi nyingi za Serikali ambazo ni: Wizara ya kilimo, Tawala za Mikoa, biashara na Vijana. Kamati iliaona kuna haja hoja hii kuendelea kuifuatilia kwa kufanya kikao kitakachowakutanisha watendaji wakuu wa Wizara hizo.

## Mapendekezo ya Kamati ya PAC

Wizara inapoanzisha Miradi kama hii, ifuate Ripoti za kitaalamu zinazotolewa ambazo katika uandaaji wake zimetumia fedha nyingi za Serikali lakini huwa haileti tija iwapo hatukuzitumia ipasavyo.

## UTEKELEZAJI WA MRADI WA PILIPILI HOHO KATIKA MAENEO YA PUJINI NA FINYA KISIWANI PEMBA

Kwa upende wa kisiwa cha Pemba, Mradi ulikusudiwa kutekelezwa katika mashamba mawili; shamba liliopo Pujini na shamba la Finya. Kiujumla, katika mashamba/maeneo yote hayo Mradi haukuweza kutekelezeka baada kuona changamoto za maeneo ya kilimo hususan kwa kusafisha maeneo hayo ya kulima kukosa tija kwa miradi iliyofanyika Unguja isipokuwa kulikuwa na fedha kidogo ambazo zilitumika kwa shughuli za uendeshaji ikiwemo uandaaji wa.

Kamati ilibahatika kutembelea shamba la Finya na kushuhudia vichaka na bonde lililokuwa halitumiki tangu shughuli za Mradi zilipokuwa zimesimamishwa.

## KIKAO MAALUM CHA WIZARA ZILIZOHUSIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI WA PILIPILI HOHO

Katika kufuatilia hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na Mradi wa Pilipili Hoho uliopangwa kutekelezwa na iliyokuwa Wizara ya Biashara na Viwanda kupitia Shirika lake la ZSTC, Kamati ilipata wasiwasi kuhusiana na majibu yaliyotolewa na Watendaji wa Wizara hiyo juu ya sababu zilizopelekea kushindwa kutekelezeka kwa Mradi huo hasa ukizingatia utekelezaji wa Mradi huo ulihusisha Wizara tofauti.

Ili kupata ufafanuzi wa kutosha na Kamati kuweza kushauri ipasavyo, tarehe 14 Aprili, 2022 Kamati ya PAC ilikutana na Watendaji wa Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo pamoja na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa lengo la kufahamu ushiriki wa kila Wizara katika utekelezaji wa Mradi wa Pilipili Hoho hadi kupelekea Mradi huo ukashindwa kutekelezeka na kuleta tija iliyokusudiwa. Kupitia majadiliano yaliyofanyika, Kamati

imegundua mambo yafuatayo:

1. Mradi ulipangiwa kutumia jumla ya shilingi milioni 560 ambazo awali ziliingizwa Wizara ya Vijana kupitia Idara ya Maendeleo ya Vijana ambayo iliibua Programu ya ajira kwa Vijana na baadae fedha hizo zikahamishiwa Wizara ya Biashara na Viwanda.
2. Jumla ya shilingi milioni 183 zilitumika na shilingi milioni 377 zilibakia na kurudishwa Wizara ya Vijana ambapo kati ya hizo shilingi milioni 112 zimeshanunuliwa banda liliopo Bweleo ili litumike kwa shughuli za ujasiriamali wa ushoni. Aidha, fedha nyengine zilizobakia zimepangwa kutumika katika utengenezaji wa banda lililonunuliwa.
3. Kwasasa Wizara ya Vijana hawana mpango wa kuendelea na ukulima wa Pilipili Hoho pamoja na kwamba zinazo soko kubwa nje ya nchi na pia kuna maeneo zinaweza kulimwa, kumea na kuleta tija ipasavyo.
4. Kutokushirikishwa kwa watendaji wa Wizara ya Kilimo (tangu hatua za awali) ambao ndio wenye utaalamu wa kilimo cha pilipili nchini kinyume na ilivyodaiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwamba waliwashirikisha ipasavyo.
5. Wizara ya Vijana wameshakabidhiwa maeneo yaliyokuwa yamepangwa kulimwa Pilipili hoho lakini hakuna miundombinu yoyote waliokabidhiwa kwani asilimia kubwa ya miundombinu hiyo ilikuwa imeshaharibiwa.
6. Wizara inayoshughulikia Tawala za Mikoa ilishirikishwa baada ya ZSTC kutafuta maeneo wao walikuja kutoa baraka zao kwa vile maeneo hayo yanapatikana ndani ya mamlaka zao.
7. Wizara inayoshughulikia Tawala za Mikoa haikuhusishwa katika mikataba ya maeneo yaliyotumika kulima Pilipili hoho badala yake walihusika katika utoaji uelewa ili wananchi wakubali kutumiwa kwa maeneo husika.
8. Suala la maamuzi ya kulima katika eneo ambalo halikupendekezwa na Wataalamu lilianza kwa utashi wa kisiasa wa kujivutia maeneo ili kuonekane kuna jambo limetekelezwa. Hata hivyo, Wizara ya Biashara na Viwanda walikubali kutekeleza maelekezo hayo yalikuwa kinyume na mapendekezo ya Ripoti.
9. Mradi wa Vijana wa Pilipili hoho hatimae ulishindwa kuendelea na kuwasaidia Vijana waliolengwa kujikwamua na hali duni ya maisha.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ilisisitiza fedha zilizokuwa hazijatumika zikatumike vizuri kwa mujibu wa mpango wake ili ziwapatie tija vijana. Aidha, mapendekezo mengine ni kama yanavyoonekana katika hoja zzilizoelezwa awali katika ya ripoti hii.

**RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM KUHUSU UNUNUZI WA MCHELE NA MBOLEA KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2020.**

**5.2: IDARA YA UHAKIKI WA CHAKULA NA LISHE**

**Hoja nambari 5.2.1 Bakaa ya fedha katika ununuzi wa mchele wa Idara ya Uhakiki wa**

**Chakula na Lishe shilingi 29,887,380.60**

Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe ilipangiwa kutumia TZS 420,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa mchele wa hifadhi ya chakula.

Aidha Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe iliandika barua kwenda Wizara ya Kilimo yenye kumbukumbu nambari WKM/IUCL/29//VOL1 ya tarehe 6/09/2018 kwa ajili ya kupatiwa shilingi milioni 420,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa mchele. Taratibu za manunuzi ya Mchele kwa mujibu wa maagizo ya barua yenye kumbukumbu nambari BLM/30/M/C.28/vol. II/34 ya tarehe 17 Febuari 2020 zilitakiwa zifanywe na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC).

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kuna bakaa ya fedha yenye jumla ya shilingi 29,887,380.60 kutokana na ununuzi wa mchele ambapo fedha halisi zilizoingizwa zilikuwa ni shilingi 420,000,000 ambapo matumizi halisi ya ununuzi wa mchele ni shilingi 390,112,619.40 sawa na tani 338.

**Majibu ya Wizara**

Wizara inakiri kuwa ilitumia fedha hizo kwenda Shirika la Biashara (ZSTC) kwa ununuzi wa mchele ambapo jumla ya Shilingi 390,112,619.40 zilitumika. Kwa kuwa fedha zilizotumwa zilikuwa shilingi milioni 420,000,000 hivyo kulikuwa na bakaa ya shilingi milioni 29,887,380.60 huko ZSTC. Lengo kuu la hifadhi ya chakula ni kuweka chakula ili kukabiliana na dharura ya majanga ya maumbile yalopelekea kuwepo kwa upungufu wa chakula. Hivyo, chakula kilikusudiwa kutolewa bure kwa waathirika. Lakini baada ya kutokuwepo kwa janga lolote ZSTC walitakiwa kuuuza mchele huo na pesa zilizopatikana ziliendelea kuwepo ZSTC, ili kuweza kuendelea na ununuzi mwengine pale inapobidi.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kwamba kulikuwa na uzembe uliofanywa na Watendaji wa Wizara ya Kilimo kwa kutuma fedha nyingi kinyume na uhalisia wa mchele ulionunuliwa. Kufanya hivyo, kunaitia shaka Kamati yetu kwamba kuna uwezekano wa fedha zilizobakia kutumika kwa maslahi binafsi kinyume na matarajio ya Serikali ya kuwasaidia wananchi wake pindipo jana likitokea.

Kamati ya PAC pia imebaini Wizara ya Kilimo ina utunzaji mbaya wa kumbukumbu, hili limejitokeza wakati watendaji waliposhindwa kuipatia Kamati barua yenye kumbukumbu nambari BLM/30/M/C.28/VOL iliyotoa agizo la uuzwaji wa bidhaa hiyo badala ya kuhifadhiwa kwa matumizi ya baadae. Kadhalika, Kamati ilipata mashaka kuhusiana na nyaraka iliyotumika kuhaulisha fedha hizo ya tarehe 19/9/2018 kutoka Wizara ya Kilimo kwenda Wizara ya Biashara (ZSTC) kama ilivyoelekezwa na Baraza la Mapinduzi kwani kulikosekana saini ya “payment voucher”, saini ya “witness to payment” pamoja na saini ya “payee/receiver”.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara ihakikishe inafuata taratibu zote za ununuzi wa bidhaa kama zilivyoainishwa katika Sheria za Usimamizi wa Fedha za Umma.

**Hoja nambari 5.2.2 Uchakavu wa maghala ya kuhifadhia mchele**

Ukaguzi umebaini kwamba mchele ulionunuliwa ulihifadhiwa kwenye maghala ambayo yalikuwa na dosari ya kuvuja na kupelekea uharibifu wa baadhi ya mchele uliohifadhiwa jambo lililopelekea kushindwa kufikia kwa malengo yaliyokusudiwa na kusababisha Serikali kupata hasara.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuzidisha umakini katika kuhakikisha kuwa inatenga sehemu salama kwa ajili ya kuhifadhia chakula cha akiba kwa matumizi ya binadamu.

**Majibu ya Wizara**

Ni kweli kulikuwa na changamoto katika uhifadhi wa mchele ghalani kufuatia kiwango kikubwa cha mvua iliyonyesha kupita wastani, hali iliyopelekea kuingia maji ghalani kupitia chini ya milango baada ya maji mengi kutuwama kutokana na njia ya kutokea maji kuwa ndogo kulingana na kiwango hicho cha maji.

Hali hiyo ilipelekea Wizara na Serikali kwa ujumla kushirikiana na Katibu Mkuu Kiongozi aliemaliza muda wake, kuchukua hatua za dharura za kuhamisha maji hayo kwa kuagiza Kikosi cha Zimamoto kuja kuyatoa maji katika eneo la ghala na kupunguza kiwango cha uharibifu.

Aidha, Serikali iliamua kujenga uzio wa vyuma mbele ya mlango ili kuzuia maji kupenya chini ya mlango. Pia kulijengwa mtaro ili kurahisisha utoaji wa maji kwa muda mfupi ili kuondoa uwezekano wakuendelea uharibifu huo. Hata hivyo, athari ya mvua hiyo kubwa ilipelekea vipolo 6 vya mchele kuharibika lakini hivi sasa hali hiyo imedhibitiwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba majibu ya Wizara yapo tofauti na hoja ya Mkaguzi ambae ameeleza kuwa ghala lilikuwa chakavu lakini majibu ya Wizara yanasema kupita kwa maji chini ya milango ya ghala ndio sababu ya kuharibika kwa mchele kama inavyoonekana kwenye majibu.

Hata hivyo, Kamati baada ya uchunguzi imebaini kwamba awali ghala lilikuwa lipo vizuri lakini baada ya mvua kunyesha, ghala lilipitisha maji chini ya milango na kusababisha unyevu uliopelekea baadhi ya polo za mchele kupata unyevu na kuharibika. Hali hii ilipelekea Mkaguzi kuona ghala lilikuwa chakavu. Kamati ilipata fursa ya kuliona ghala hilo na kubaini tayari limeshafanyiwa matengenezo na

kwasasa halipenyezi tena maji.

Kamati pia imegundua kwamba mchele ulioharibika na kupelekea kuuzwa chini ya bei stahiki ulikuwa zaidi ya polo 6. Kwa mazingira yaliopo, unyevu hauwezi kuingia na kuathiri polo hizo tu kwa vile kulikuwa na polo nyingi zilizokuwa zimebandishiwa polo nyengine.

Kamati haikuridhirishwa na majibu ya Watendaji wa Wizara ya Kilimo kwa sababu majibu yao yalikuwa yakitofautiana kuhusiana na uchakavu wa ghala na polo zilizoharibika na kupelekea wasiwasi katika usahihi wa majibu waliyokuwa wakiyatoa. Hali hiyo imechangiwa zaidi na kutokuwepo kwa Afisa Masuul wa Wizara wakati Kamati inapokea majibu hayo kwani masuala mengi yeye ndio aliyekuwa akitambua undani na usahihi wake.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wizara ihakikishe inaandaa miundombinu mizuri itakayowezesha maji ya mvua kupita bila ya kusababisha athari kwa mali iliyohifadhiwa ndani ya ghala hilo.
2. Wizara ihakikishe inazishughulikia ipasavyo hoja zinazowasilishwa na 'CAG' katika 'management letter' yake ili kuondosha kasoro kuandikwa katika kitabu chake.
3. Vyombo vya uchunguzi vihakikishe vinalifuatilia suala kwa kumtafuta na kumuhoji Afisa Masuul aliyehusika na kadhia hii ili kuweze kupatikana uhalisia wa kilichotokea Kamati imeona ilibainishe hili kwa vile, mara nyingi Kamati ikikutana Afisa Masuul huyo huwa hashiriki vikao wakati yeye ndio mwenye majibu kamili ya kilichotokea.

## 5.3: UNUNUZI WA TANI 740 ZA MBOLEA (UREA) U$D 279,720

### Hoja nambari 5.3.1: Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi katika ununuzi wa mbolea

Kifungu nambari 38 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 kinazitaka Taasisi za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kutumia ushindani wa wazi wa zabuni kama njia inayopendelewa katika ununuzi na uondoshaji wa mali za umma. Ukaguzi umebaini kwamba Wizara imekiuka taratibu za manunuzi kama ifuatavyo:

- Kukosekana kwa ushindi wa zabuni katika kumtafuta muuzaji wa mbolea.
- Kutokutangazwa kwa zabuni katika magazeti.
- Kukosekana ushindani wa bei.
- Kukosekana Nyaraka za Zabuni.

- Kukosekana Ripoti ya Tathmini ya Ununuzi.
- Kukosekana idhini ya Bodi ya Ununuzi.

**Majibu ya Wizara**

Ni kweli Wizara ilikiuka utaratibu wa ununuzi wa Urea Tani 740, Kwa kuwa Wizara tayari ilikuwa imeshachelewa katika mchakato wake wa kupata mbolea hiyo kwa ajili ya pembejeo za wakulima, Wizara ilionelea kuchukua hatua za haraka kwa ajili ya kuokoa muda na kuwasaidia wakulima kupata pembejeo hizo kwa wakati.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

1. Kamati imekubaliana na hoja iliyoelezwa na Mdhibiti kwamba Watendaji wa Wizara hawakuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya kuwepo kwa ushindani wa wazi wa zabuni zinazofanywa na Taasisi za umma.
2. Kamati imebaini Kampuni ilipatiwa zabuni ya ununuzi wa mbolea pasi na kuwepo vielelezo vinavyoonesha uwazi katika utangazwaji wa zabuni, usawa katika ushindani wa bei, kukosekana ripoti ya tathmini pamoja na kukosekana idhini ya Bodi ya Manunuzi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kwa vile Mkaguzi amefanya kazi yake na Kamati ya PAC imelichunguza suala hili na kutokuridhika na utekelezwaji wake, Kamati inaishauri Serikali kupitia vyombo vya uchunguzi kuwafuatilia wote waliohusika na uzembe uliofanyika wa kukiuka Sheria husika na kuipelekea Serikali kupata hasara.

**Hoja nambari 5.3.2: Ukiukwaji wa taratibu za malipo ya U$D 279,720**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba mtoa huduma amelipwa fedha yote kwa asilimia 100 ya bei ya makubaliano ya mkataba jambo ambalo ni kinyume na taratibu na sheria ya fedha kuhusiana na ununuzi wa bidhaa.

**Majibu ya Wizara**

Ni kweli malipo ya U$D 279,720 yamelipwa pasi na kufuata utaratibu. Aidha, malipo haya kwa bahati mbaya hayakufanywa na Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo bali yalifanywa moja kwa moja na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na kwa upande wa Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo iliingiziwa DUMMY ya TZS 642,905,651 ambapo Wizara iliifanyiakazi kwa ajili ya kuweka sawa hesabu zake na ilifanya jitihada ya kupata kielelezo cha malipo hayo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

1. Wizara imekiri juu ya ukiukwaji wa taratibu za manunuzi wakati wanazifahamu. Kamati haikuridhishwa na majibu ya Watendaji kwani inaonekana wamefanya kwa makusudi.
2. Serikali kupitia vyombo vyake vya uchunguzi ifuatilie kadhia hii na kuwawajibisha wote wanaohusika.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Mapendekezo ya Kamati ya PAC yanalingana na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika hoja nambari 5.3.1

**Hoja nambari 5.3.3: Mapungufu yaliyojitokeza katika Mkataba**

Kukosekana kwa kipengele kinachoonesha adhabu yoyote ya mtoa huduma (Supplier) endapo atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mkataba husika.

**Majibu ya Wizara**

Mnamo tarehe 03/01/2020, Wizara ya Kilimo ilifungiana mkataba na Kampuni ya Pansel Trading Company Limited ya Hong Kong nchini China kwa ajili ya unnuzi na usafirishaji wa wa Tani 740 za mbolea (UREA) zenye thamani ya USD 279,720 za kimarekani. Katika mkataba huo kulikuwepo na kipengele cha adhabu kwa Mtoa huduma endapo atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mkataba na sio kama inavyosomeka katika hoja kuwa hakukuwa na kipengele cha adhabu yoyote kwa Mtoa huduma endapo atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mkataba. Hivyo, kipengele cha 'liquidated demage' kipo katika GCC 25.1 /SCC 22 na 'Performance Security' GCC 9/SCC7 ni vipengele vinavyoonesha adhabu kwa Mtoa huduma ikiwa atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mkataba.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kutokana na kutofautiana kwa maelezo ya Mkaguzi na Wizara na baada ya Kamati kuupitia Mkataba husika, Kamati ya PAC ilibaini kwamba ni kweli kifungu cha adhabu (liquidated demage) kilikuwepo kama ilivyoelezwa na Watendaji wa Wizara. Hata hivyo, Kamati ilitaka kujua kama Mkataba huo ulifuata taratibu za kupelekwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu lakini Kamati ilishindwa kulithibitisha hilo kwani haikupatiwa kielelezo husika. Hivyo, Kamati haiweza kuthibitisha juu ya kukamilika kikamilifu kwa masharti yaliyomo ndani ya Mkataba Mkataba huo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ya Kilimo iwe na utaratibu mzuri wa kuhifadhi kumbukumbu zake ili ziweze kuwasaidia zinapohitajika.
2. Wizara iwe makini inapoandaa mikataba yake ikiwa ni pamoja na kuiwasilisha

rasmi Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Hoja nambari 5.3.4: Kutokupokelewa kwa Tani 740 za mbolea (UREA) kutoka kwa Kampuni ya Pensel Trading Limited**

Kutokana na mapungufu ya Mkataba yaliobainishwa hapo juu, ukaguzi ulibaini moja ya vipengele vya mkataba vya mkataba ni kumtaka "Supplier" kuwasilisha tani 740 ndani ya kipindi cha siku 90 mara baada ya kufunga mkataba huo, dosari iliyobainika hadi tunakamilisha ukaguzi wetu hakuna kielelezo chochote kinachoonesha kuwa mbolea hiyo imepokelewa jambo ambalo tumeshindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa malipo ya fedha yalivyotumika.

**Majibu ya Wizara**

Wizara inakiri kuwa haikupokea tani 740 za mbolea (UREA) kutoka kwa Kampuni ya Pansel Trading Company Limited. Hata hivyo, Wizara ilipokea nakla ya barua yenye kumbukumbu nambari CBC.182/193/01/28 yenye kichwa cha habari kinachohusu Makubaliano ya Kurejesha Fedha za Mbolea TZS 642,671,431 Kutoka Wizara ya Kilimo na fedha hizo zitaingizwa katika hesabu ya Mfuko Mkuu wa Hazina wenye nambari 0404381000.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Pamoja na Watendaji wa Wizara kukiri kwamba ni kweli hawakupokea tani 740 za mbolea (UREA) na kueleza kwamba kwasasa Wizara ya Fedha na Mipango imeingia makubaliano na Kampuni hiyo kuzilipa fedha hizo kidogo kidogo kuanzia mwezi wa Januari, 2022 kupitia barua nambari CBC.182/193/01/28 lakini hadi Kamati inamaliza kazi zake Wizara ya Kilimo imekiri kwa kusema kwamba haijapokea malipo yoyote.

Kulitafutia ufumbuzi suala hili, Kamati yetu iliitisha kikao siku ya tarehe 14/4/2021 kilichowakutanisha Watendaji wa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha na Mipango ili kubaini uhalisia kama kulikuwa na makubaliano ya kurudishwa fedha hizo na kiasi gani tayari kimesharudishwa. Kamati ilibaini kuwa kweli Wizara ya Fedha na Mipango inalifahamu suala hilo na walisema wamekubaliana kurudishwa fedha hizo kwa kulipa kila mwezi 50,000,000 ambapo hadi Kamati inawasilisha taarifa yake, imeelezwa shilingi 100,000,000 zimerudishwa.

Sambamba na hilo, Kamati ya PAC imegundua kwamba kuna uzembe umefanyika uliosababishwa na Watendaji wa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha iliamua kuilipa 'PANSEL TRADING COMPANY' fedha zote hata kabla ya mbolea kufika nchini kinyume na makubaliano ya Mkataba unavyoeleza kwamba atalipwa baada ya mbolea kufika. Kama hayo hayatoshi, malipo hayo yalifanyika bila ya kuwepo maombi kutoka kwa Kampuni au Afisa Masuul (Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo) juu ya upokelewaji wa mbolea husika, wakati Wizara ya Kilimo haikuchukua hatua yoyote baada ya kupata taarifa ya malipo yaliyofanywa kupitia mfumo wa 'swift'. Kwa mantiki hiyo, Kamati imebaini kwamba Watendaji wa Wizara hizi mbili walikuwa na mpango

mmoja katika upoteaji wa fedha hizo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe fedha zote zilizopangwa kurudishwa na Kampuni zinarudishwa na zinaingia katika hesabu ya Mfuko Mkuu wa Serikali.
2. Watendaji wote waliohusika na kadhia, Serikali ihakikishe inawafuatilia, kuwahoji na wakikutikana na hatia, hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

**Hoja nambari 5.3.5: Kukosekana kwa vielelezo vya manunuzi ya mbolea, U$D 279,720**

Jumla ya USD 279,720 zimelipwa kwa Kampuni ya Pansel Trading Company Limited kwa ajili ya ununuzi wa mbolea ya UREA lakini vielelelzo vya manunuzi hayo havikupatikana wakati wa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika. Baadhi ya vielelezo vilivyokosekana ni pamoja na Ankara (Invoice), GRN pamoja na Stakabadhi.

**Majibu ya Wizara**

Ni kweli kwamba baadhi ya vielelezo vya manunuzi ya mbolea havikuwepo Wizarani kwasababu vielelezo vyote vinakaa sehemu iliyofanyiwa malipo. Kwa kuwa ulipita muda mrefu bila ya mbolea hiyo kupatikana, Wizara ilipitisha jitihada ya kufatilia suala hili na kufanikiwa kupata barua yenye kumbukumbu nambari **CBC.182/193/01/28** yenye kichwa cha habari kinachohusu Makubaliano ya Kurejesha Fedha za Mbolea TZS 642,671,431 Kutoka Wizara ya Kilimo. Kwa muhtadhaa huo, mbolea hiyo haikufika na ametakiwa msambazaji huyo arejeshe fedha hizo Serekalini.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Licha ya Wizara kukubaliana na hoja ya Mkaguzi ya kutokuwepo kwa vielelezo vya manunuzi ya mbolea. Hata hivyo, Kamati ya PAC nayo haikupatiwa vielelezo hivyo badala yake walipatiwa barua ya marejesho ya fedha husika. Hata hivyo, pamoja na Wizara kueleza kwamba vielelezo vilitakiwa kuwepo sehemu malipo yalipofanyika, Kamati yetu ilisisitiza ni jukumu la mtekelezaji nae kuwa na nakala husika. Kamati yetu haikuridhishwa na majibu yaliyowasilishwa na inaungana na Mkaguzi kwamba vielelezo havipo hasa ukizingatia ni muda mrefu tangu Mkaguzi kupita na Kamati kufanya uchunguzi wake.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wizara ya Kilimo wahakikishe wanakuwa na vielelezo vyote vinavyohitajika mara baada ya kufanyika malipo ili vitakapohitajika viweze kuoneshwa kama uthibitisho wa jambo walilolitekeleza.

**Hoja nambari 5.3.6: Kukosekana kwa ufafanuzi juu ya ununuzi wa mbolea ya urea tani 454 shilingi 241,136,030**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Kilimo ilifanya Manunuzi yenye jumla ya Shiling 241,136,030 kwa ajili ya ununuzi wa mbolea aina ya Urea tani 454 lakini ufafanuzi wa ununuzi haukupatikana.

Kutokupatikana uthibitisho juu ya ununuzi, upokeaji na utumiaji wa mbolea hiyo kunaweza kupelekea upotevu wa fedha na matumizi mabaya ya fedha za Serekali.

**Majibu ya Wizara**

Wizara inakiri kufanya manunuzi wa Mbolea yenye jumla ya TZS 241,136,030 tani 454. Mbolea hiyo ilinunuliwa kupitia mkataba baina ya Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo na Kampuni ya Biziredi ya Zanzibar ambayo ndio iliyoshinda zabuni. Mbolea ya Urea tani 454 ilipokelewa katika maghala makuu Unguja na Pemba kwa stakbadhi za kupokea (Delivery notes). Vielelezo vya malipo na upokeaji wa mbolea hiyo vipo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kwamba wakati Mdhibiti amefika Wizara ya Kilimo kutekeleza kazi zake, watendaji wa Wizara ya Kilimo hawakumpatia mashirikiano na kupelekea kukosekana kwa ufafanuzi wa ununuzi wa mbolea. Hata hivyo, Kamati ilipofika na kukutana na watendaji wa Wizara hiyo, ilifanikiwa kupatiwa vielelezo hivyo, ilivikagua na kugundua kwamba kuna mikataba miwili ya ununuzi wa mbolea.

Mkataba wa mwanzo ulihusu ununuzi wa mbolea wenye thamani ya shilingi milioni 274 na Mkataba wa pili ulikuwa wa shilingi milioni 180 wa tarehe 30/3/2020 wakati Mdhibiti alifika tarehe 17/3/2020. Kwa mantiki hiyo, Kamati ilishindwa kuthibitisha usahihi na ukweli wa mikataba hiyo. Sambamba na hilo, Mkaguzi wa ndani wa Wizara hiyo hafahamu yote yaliyofanyika katika kipindi hicho. Kwa mnasaba huo, Kamati haikuridhika na majibu kwani Wizara haikuwa makini katika uwekaji wa kumbukumbu zake.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Watendaji wa Wizara ya Kilimo wahakikishe wanawapatia ushirikiano watendaji wa Mdhibiti wanapofika katika maeneo yao kutekeleza majukumu yao ya kikatiba.
2. Wizara ifanyekazi kwa pamoja na Mkaguzi wa Ndani ili makosa yaweze kubainika mapema na kutafutiwa ufumbuzi kabla ya Mkaguzi wa nje kufika.
3. Watendaji wa Wizara wahakikishe wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria za Usimamizi wa Fedha za Umma na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ikiwemo kuwasilisha Rasimu za Mikataba yao Afisi ya Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa.

## RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM KUHUSU UKODISHWAJI WA MASHAMBA YA MIKARAFUU.

### Hoja nambari 6.3.1: Kutokuwepo kwa mchanganuo mzuri wa ukusanyaji wa mapato

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo - Pemba ina vyanzo mbali mbali vya mapato yanayokusanywa kupitia Idara zake za Kilimo, Misitu, Umwagiliaji na Mifugo na kuingizwa katika hesabu nambari 041101000013 yenye jina la Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo - Pemba.

Ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa mchanganuo mzuri wa makusanyo ya mapato, ambapo kumbukumbu za kuingizia mapato hayo benki (pay in slip) hazikuweza kuwekwa kwa utaratibu kulingana na chanzo halisi cha makusanyo jambo ambalo limepelekea kushindwa kujua kima halisi cha fedha zilizokusanywa kutoka katika kila chanzo.

Kutokuwekwa kwa kumbukumbu za ukusanyaji wa mapato vizuri ni kwenda kinyume na kifungu nambari 30(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

### Majibu ya Wizara

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inakubaliana na hoja ya kutokuwepo kwa mchanganuo mzuri wa ukusanyaji wa mapato ya mikarafuu peke yake. Hali hii ilitokana na muongozo wa Serikali ambapo Wizara ilitakiwa kuwa na hesabu (Account) moja tu ambayo ilikuwa inasomeka WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI PEMBA hesabu namba 041101000013, kwa ajili ya kukusanyia mapato yake ambayo ilikuwa inakusanya fedha za mapato kutoka katika vyanzo vyake vyote vya mapato ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo kwa wakati huo.

Hata hivyo, katika ukaguzi wa kawaida uliofanyika wa kila mwaka kutoka 2017 hadi 2019, hoja hii ilijitokeza na ilifanyiwa kazi na Wizara baada ya kushauriana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo juu ya kuwepo kwa hesabu maalum itakayohusika na mapato ya mikarafuu tu.

Hoja hii imeshafanyiwa kazi mwaka 2019/2020 ambapo baada ya mawasiliano na Wizara ya Fedha, hesabu (Account) maalum ya kukusanyia mapato ya mashamba ya mikarafuu ilifunguliwa na ikawa inasomeka hesabu namba 0735684001 MAPATO YA MIKARAFUU baada ya kupata idhini ya Serikali ya kufungua hesabu hiyo kwa malengo yaliyotajwa hapo juu.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Pamoja na watendaji wa Wizara kukiri kutokea kwa kasoro ya kutokuwepo mchanganuo mzuri waukusanyaji wa mapato, hata hivyo, Kamati ya PAC ilitaka kujua utaratibu uliotumika katika ukodishwaji wa mashamba ya Mikarafuu na kuelezwa kwamba

kulifanyika tathmini ya kuyatambua mashamba na Eka za Mikarafuu iliyofanywa na Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na baadaye kukaundwa timu ya ukodishwaji iliyojumuisha watendaji kutoka Taasisi tofauti za Serikali zikiwemo; Wizara ya Kilimo, ZAECA na watendaji Mikoa.

Kamati hiyo ilikuwa ikisimamiwa na Afisi za Mkuu wa Mkoa kupitia Wilaya zake. Kamati hizo zilipanga ratiba na kuanza ukodishaji wa mashamba ambapo Mkodishaji hutakiwa kulipa asilimia 25 ya kodi la shamba au eka husika ambayo hutakiwa alipe ndani ya siku mbili na fedha nyengine akamalishe ndani ya wiki mbili. Malipo hayo yalikuwa yakifanyika benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na kujazishwa Mkataba wake.

Kutokana na majibu ya Wizara, Kamati iligundua kuna uzembe mkumbwa uliofanyika uliosababishwa na kutowajibika ipasavyo Watendaji wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na kupelekea kutokezea yafuatayo:

1. Kuwepo na hesabu (account) moja ya kuingiza mapato yote yanayotokana na Kilimo, Maliasili, na Mifugo. Hili ni kinyume na utaratibu unaoelezwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha, nambari 12 ya mwaka 2016 inayoekeleza kila chanzo kinachojitegemea basi kiwe na utaratibu wake wa makuanyo na uhifadhi wake. Kufanyika hivyo, kumepelekea Wizara kushindwa kuzitambua fedha halisi zinazotokana na ukodishwaji mikarafuu na fedha za mazao mengine.
2. Baadhi ya wakodishwaji walikuwa hawapatiwi mikataba yao baada ya kufanya malipo.
3. Kuna baadhi ya mashamba yameonekana kukodishwa kwa wakulima zaidi ya mmoja na kusababisha utata juu ya uhalali wa ukodishwaji wake.
4. Kuna baadhi ya mashamba yamekodishwa kwa bei ndogo isiyostahiki kukodishwa kwake na kupelekea mapato kidogo ya fedha zilizopatikana.
5. Baadhi ya Watendaji wa Wizara waliingilia utaratibu wa ukodishwaji na kujikodisha mashamba hayo kwa kujinufaisha kibinafsi.
6. Kukosekana kwa mashirikiano ya karibu kwa Wizara ya kilimo na Wizara ya Fedha kwani Kamati imegundua kuna wakodishwaji walikuwa wakilipa na kupatiwa risiti na Wizara ya Fedha lakini hakukuwa na orodha ya waliolipa katika Wizara ya Kilimo. Suala hilo limeisikitisha Kamati na kujiaminisha kwamba fedha hizo zilikuwa zikiishia katika matumbo ya watendaji.
7. Kukosekana kwa muongozo kutoka Baraza la Mapinduzi kama ilivyodaiwa katika majibu ya Watendaji wa Wizara kwamba muongozo huo uliwaelekeza kutumia hesabu moja ya mapato hayo. Kamati ilipofuatilia kwa undani kwa kutaka barua au kielelezo kutoka Baraza la Mapinduzi, Wizara ilishindwa kuwasilisha kielelezo hicho na kuipa wasiwasi Kamati kwamba maelezo yaliyotolewa hayakuwa yakileta sura sahihi na yenye ukweli.
8. Kamati imegundua kwamba Mhasibu aliyekuwepo kipindi hicho hakuwajibika ipasavyo kwa kuruhusu mapato kutoka vyanzo tofauti kuingizwa katika hesabu moja na kupelekea kutotambulika na kupotea kwa mapato ya ukodishwaji.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Watendaji wa Wizara wahakikishe wanaweka hesabu (account) maalum ya fedha za malipo ya ukodishwaji mashamba na eka za mikarafuu.
2. Watendaji wa Wizara wahakikishe wanawapatia mikataba wakodishwaji wote wa Mashamba na eka za Mikarafuu.
3. Viongozi wa Wizara wawasimamie na wawajibishe watendaji wote waliohusika na ukiukwaji wa uwekaji au utumiaji mbovu wa mapato ya Serikali.
4. Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha zihakikishe zinafanya kazi kwa pamoja ili taarifa za fedha za wakodishwaji ziwe zinapatikana katika usahihi unaotakiwa.

**Hoja nambari 6.3.2: Mapungufu yaliyobainika katika mikataba ya ukodishwaji Mashamba ya Mikarafuu**

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo ilkodisha mashamba ya mikarafuu yaliyopo kwenye maeneo mbali mbali kisiwani Pemba kwa misimu tofauti ya mavuno kuanzia mwaka 2017 hadi 2019 ambapo katika ukodishaji huo ukaguzi umebaini mapungufu mbali mbali ya mikataba ya ukodishwaji wa mashamba hayo.

Aidha miongoni mwa mapungufu yaliyobainika ni kutokuwepo kwa kifungu muhimu cha hatua za kuchukuliwa pindipo Mkodishwaji akishindwa kulipa deni lake kwa wakati ulioelezwa kwenye mkataba huo. Kukosekana kwa kifungu hicho kunaifanya Wizara kutokuwa na nguvu kwa mujibu wa Mkataba kumchukulia hatua Mkodishwaji pale atakapobainika ameshindwa kulipa gharama za ukodishwaji.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo inakiri uwepo wa mapungufu katika mikataba hiyo ya ukodishwaji wa mashamba ya mikarafuu kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali kama ilivyoonekana na Mkaguzi.

Wizara ilitekeleza mkataba huo uliotumiwa ambao uliandaliwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwamba sisi kama Wizara ya kilimo hawakuwa na uwezo wa kubadilisha kipengele chochote cha muundo wa mkataba huo na kuendelea kuutumia kama walivyoelekezwa.

Hata hivyo, katika kaguzi nyengine zilizopita za kawaida zilizofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hawakuwahi kuhoji kipengele hiki na kwa upande wao kama Wizara kwa vile ukaguzi ulifanyika na hawakupata hoja hii walijiridhisha kwamba mikataba ile iko sahihi cha kushangaza ni kwamba hoja hii imejitokeza katika ukaguzi maalum (Special Audits) zilizofanyika kati ya mwaka 2017 hadi 2019.

Hata hivyo, endapo hoja hii ingejitokeza katika kaguzi za kawaida za mwaka 2017 hadi 2019, Wizara ingeliona hili na ingewasiliana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya marekebisho yanayohusu kipengele hicho ambacho ukaguzi ulikiiona kwa wakati huo.

Kutokana na mapungufu yaliyobainika, Wizara itawasiliana na Ofisi ya Mwanasheria

Mkuu ili kurekebisha kasoro hiyo isiendelee kuwepo kwenye mikataba yao ya ukodishaji wa mikarafuu na mali nyenginezo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imegundua kwamba mkataba uliokuwa unatumika katika shughuli za ukodishwaji ulipelekwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kupitia barua nambari LD.6IIVOL.XXIV/ ya tarehe 5/7/2017 ambao ulikosa kifungu muhimu cha kuchukuliwa hatua Mkodishwaji aliyeshindwa kulipa fedha za ukodishwaji wake. Aidha, Kamati ilibaini baadhi ya mikataba hiyo ilikuwa haina saini za Wakodishwaji na kusababisha utata, migogoro na ukosefu wa mapato ya Serikali. Hili limebainika baada ya baadhi ya wakodishwaji kudai kutokuwa na mkataba wa ukodishwaji mashamba hayo kutoka Wizara ya Kilimo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe mambo yote yanayostahiki kuwemo katika Mkataba wa ukodishwaji mali yanaingizwa wakati wa kuandaa mkataba ya aina hiyo ikiwemo hatua za kuchukuliwa iwapo Mkodishwaji atashindwa kulipa deni analodaiwa.
2. Wizara ihakikishe inaingia mikataba na wakodishwaji wa mashamba au eka za mikafuu kabla ya kuanza shughuli za uchumaji wa karafuu.
3. Wizara iwapatie Wakodishwaji Mashamba nakala ya Mikataba yao.

**Hoja nambari 6.3.3; Kukosekana kwa vielelezo vya ukodishwaji wa Mashamba ya Mikarafuu shilingi 365,010,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa wastani wa Wakodishwaji 247 waliokodishwa wastani wa mashamba 291 yenye thamani ya shilingi milioni 365,010,000 yaliyopo katika maeneo mbali mbali Kisiwani - Pemba lakini uthibitisha wa vieleleza vya malipo yao havikupatikana kwa ukaguzi.

Kutokupatikana kwa vielelezo vya ukaguzi ni kwenda kinyume ya Usimamizi wa Fedha za Umma kifungu cha 34(1) namba 12 ya mwka 2016 ukiukwaji wa utekelezaji wa kifungu hicho cha sheria inarekea kuikosesha Serikali mapato.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo imeona hitilafu hii ya kukosekana kwa vielelezo vya ukodishawaji wa mashamba ya mikarafuu (vielelezo vya malipo) shilingi 365,010,000/- wakati wa ukaguzi.

Hali hii ilisababishwa na Wakodishwaji wa Mashamba ya Mikarafuu wao wenyewe

kutakiwa kwenda kulipia benki na baadae wawasilishe Wizarani hati ya malipo ya benki (Pay in Slip) na Wizara iandike stakabadhi zao (receipt) kwa ajili ya utambuzi wa malipo hayo. Hitilafu ilijitokeza zaidi kwani mpaka wakati huo hesabu ilikuwa moja tu inayopokea malipo yote ya mapato ya Wizara.

Sambamba na hilo, Wizara imeshindwa kupata ripoti ya kamati maalum ya Baraza la Mapinduzi iliyosikiliza malalamiko ya waliokodishwa mashamba ambapo baadhi ya wananchi walisamehewa na wengine walipunguziwa madeni yao na kamati hiyo.

Vile vile malipo ya watu wa mabao wametajatwa katika kiambatanisho 6a na wakaonekana hawakulipa madeni yao wapo ambao waliokatwa katika vifuta jasho vyao ambavyo walilipwa na Wizara ya Fedha.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imegundua kwamba majibu ya Wizara hayakuwa na ukweli wowote hususan katika suala la baadhi ya Wakodishwaji kusamehewa madeni yao kupitia Ripoti ya Kamati Maalum ya Baraza la Mapinduzi iliyoundwa kusikiliza malalamiko ya wakodishwaji. Kamati ilifuatilia kwa undani majibu hayo kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo (Mheshimiwa Haji Omar Kheir) na kueleza kwamba Kamati haikusamehe deni lolote isipokuwa ilisisitiza wale wote wanaodaiwa, Wizara ihakikishe wanalipa madeni yao.

Aidha, Kamati imesikitishwa na majibu kwamba Wizara ilishindwa kuwakata wakodishwaji fedha wanazodaiwa kupitia vifutajasho vyao. Hili limelibaini baada ya Kamati kutaka ipatiwe orodha ya waliolipa madeni yao kwa kukatwa katika vifutajasho vyao ambapo Wizara ilipata kigugumizi na kugundua kuwa majibu ya Wizara hayakuwa ni yenye kutoa taswira halisi.

Vile vile, Kamati imebaini watendaji wa Wizara ya Kilimo hawafuatilii kwa karibu hoja zinazoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa vile wameeleza kitabu chenye hoja zao wamekiona baada ya kupelekewa barua ya Kamati.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ifuatilie Ripoti ya Kamati Maalum ya Baraza la Mapinduzi na kuyafanyia kazi yote yaliyomo ndani yake.
2. Watendaji wa Wizara wafuatilie kwa karibu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili waweze kujibu kutambua na kujiandaa ipasavyo na majibu na sio kutoa majibu yasiyokuwa sahihi.

**Hoja nambari 6.3.4; Kukosekana kwa mikataba ya ukodishwaji Mashamba ya Mikarafuu shilingi 125,720,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa Wakodishwaji 66 ambao wamekodishwa mashamba 72 yenye thamani ya shilingi 125,720,000 yaliopo maeneo

mbali mbali lakini mikataba ya ukodishwaji wa mashamba hayo hayakuweza kupatikana kwa ukaguzi.

Kutopatikana kwa mikataba hiyo kunaweza kupelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa ukosdiahswaji wa mashamba hayo.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo inasikitika kukosekana kwa mikataba ya ukodishwaji wa mashamba ya mikarafuu yenye thamani ya shilingi 125,720,000/- wakati wa ukaguzi.

Hali hii ilisababishwa na wingi wa mikataba ya ukodishwaji ambayo ilikuwa vigumu kuweza kuiona yote kwa muda mchache wa ukaguzi kama inavyoeleweka ukaguzi maalum huwa una muda maalum na kwa hivyo basi hali hii hupelekea wakagusi kutojiridhisha ipasavyo juu vielelezo vingi kama hivi kwa kuwa iliwekwa katika sehemu tofauti tifauti na kukaliana. Hivyo muda wa kutosha ulihitajika ili iweze kutafutwa hadi kupatikana kwa pamoja.

Kwa sasa Wizara inaendelea na utaratibu wa mikataba hiyo kuiweka kwa pamoja ili kurahisisha katika ukaguzi na ufuatliaji wa mikataba hiyo. Mingine ipo tayari kwa ukaguzi na kujiridhisha uwepo wake.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati haikuridhishwa na majibu ya Wizara kwani baada ya kupitia mikataba husika iligundua kuna uzembe mkubwa ulifanyika wakati wa uandaaji na utekelezaji wa mikataba hiyo na kusababisha upotevu wa fedha za Serikali zinazotokana na ukodishwaji wa mashamba au eka za mikarafuu. Aidha, Kamati iligundua kuna baadhi ya wakulima walikuwa wakikodishwa mashamba mara 3,4, 22 hadi 39 bila ya kupatiwa mkataba au kuwa na mikataba michache ukilinganisha na eka alizokodishwa.

Kadhalika, katika uandaaji wa majibu ya hoja za Mdhibiti (CAG), watendaji wa Kitengo cha Mipango hawakushirikishwa ipasavyo wakati ndio Ofisi pekee ya kuratibu taarifa za Wizara. Sambamba na hilo, Kamati imebaini kuwa masuala ya ukodishwaji mashamba hiyo ni biashara ambapo mwenye fedha ndio anayepatiwa mashamba mengi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara hususan Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba ihakikishe inawashirikisha watendaji wa Mipango katika uandaaji wa taarifa zao hususan majibu ya hoja za Mdhibiti.
2. Wizara iachane na utaratibu uliokuwa unatumia wa kuwakodishwa mashamba mengi wakulima pasi na kuwa na mikataba.

**Hoja nambari 6.3.5; Kukosekana kwa taarifa za Wakodishwaji Mashamba ya Mikarafuu katika taarifa za Wizara**

Katika kupitia taarifa za Wizara juu ya ukoshwaji wa mashamba ya mikarafuu kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2018. Ukaguzi umebaini jumla ya wastani wa watu 270 waliotambuliwa kumilikishwa mashamba kumilikishwa mashamba 454 yenye thamani ya shilingi 566,685,000 ambao wamepatiwa mikataba ya ukodishwaji lakini imebaikina uwepo wa deni la shilingi 252,772,500 ambalo limeshindwa kuhakikiwa na kuthibitishwa taarifa za malipo ya deni hilo katika taarifa ya Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo kimsingi imepatwa na hofu juu ya hoja hii kwani kiambatanisho 6(c) kimetoa ripoti ya Wizara kwa hoja hii ni uwepo wa ripoti ya Wizara ya mashamba ya Wizara ndio wenzetu walipata uwezo wa kuhoji kiambatanisho hicho.

Ripoti ya mwaka ya Wizara (Final Account) inaandaliwa na Wizara Ofisi Kuu Zanzibar kwani wao ndio wanaoandaa 'balance sheet' ya Wizara kwa mwaka. Kikawaida Wizara makao Makuu Zanzibar huwa inaanda huo uwiano wa hesabu (Balance Sheet) ambalo huonesha 'Fixed Asset' na 'Current Asset' za Wizara. Deni ambalo wanaandaa ni mali tunayoitarajia.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Wizara kupitia majibu ya watendaji wake walikiri kuwepo kwa changamoto hiyo kama ilivyoelezwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hata hivyo, kamati ya PAC haikuridhika na majibu yaliyotolewa na kuagiza deni la shilingi 252,772,500 ambalo limeshindwa kuhakikiwa na kuthibitishwa taarifa zake lifuatiliwe hasa ukizingatia wadaiwa bado wapo na wameainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Wizara ihakikishe inalifuatilia deni la shilingi 252,772,500 ambalo limeshindwa kuhakikiwa na kuthibitishwa taarifa zake kwa kuwafuatilia mmoja baada ya mwengine katika orodha iliyobainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.
2. Wakulima waliokuwa na madeni wasipatiwe fursa nyengine ya kukodishwa mashamba ya Serikali.

**Hoja nambari 6.3.6: Malimbikizo ya madeni ya ukodishwaji wa Mashamba ya Mikarafuu shilingi 830,476,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa malimbikizo ya madeni yenye jumla ya shilingi 830,476,000 mabayo hayajalipwa kutoka kwa baadhi ya wakodishwaji wa mashamba ya mikarafuu mwaka 2017 hadi 2020 walipokamilisha ukaguzi wao. Baada

ya kupitia baadhi ya mikataba ya ukodishaji, ukaguzi umebaini kwamba wakoshishwa wote walipaswa ulipa asilimia 25 kabla au si zaidi ya siku mbili tokea siku ya kutia saini mkataba wa ukodishwaji na kiasi kilichobakia kilipwe katika kipindi kisichozidi wiki mbili (2) tokae tarehe ya kutia saini mkataba huo.

Aidha, ukaguzi umebaini mapungufu katika usimamizi na udhibiti wa ndani kwani kumejitokeza ukiukwaji mkubwa wa usimamizi wa mikataba na hakuna hatua yoyote iliyobainika kuchukuliwa kwa walioshindwa utekeleza masharti ya mikataba hiyo na kupelekea Serikali kukosa mapato ambayo yangeliweza kutumika kwa shughuli mbali mbali za kimaendeleo. Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 736,230,000 ni deni linalodaiwa kwa Mkoa wa Kaskazini - Pemba kwa mwaka 2017 na shilingi 74,236,000 ni kwa Mkoa wa Kusini – Pemba kwa mwaka 2019 na shilingi 20,000,000 zilikuwa ni deni la msimu mdogo wa mwaka 2019.

Kufanya hivyyo, ni kwenda kinyume na kifungu cha 3(b) cha mkataba wa ukodishaji wa shamba la karafuu.

Ukaguzi umebaini kwamba idadi ya mikataba 702 ilifungwa baina ya Wizara ya kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo na Wakodishwaji wa Mashamba hayo yenye thamani ya shilingi 1,186,966,000 ambapo kati ya hizo jumla ya shilingi 357,490,000 zimelipwa na kupelekea uwepo wa deni la shilingi 830,476,000.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inakiri uwepo wa malimbikizo ya madeni ya ukodishwaji wa mashamba ya mikarafuu.

Aidha, Wizara inakiri kwamba mkataba wa ukodishwaji unataka malipo ya asilimia 25 ya kodi yafanywe kabla au si zaidi ya siku mbili tokea siku ya kutia saini mkataba wa ukodishaji na kiasi kilichobakia kilipwe katika kipindi kisichozidi wiki mbili (2) tokea tarehe ya kutiwa saini mkataba huo.

Pamoja na kuwepo mapungufu ya mkataba wa ukodishwaji, Wizara na Serikali kwa jumla zimechukua hatua kadhaa ili kuhakikisha madeni hayo yanalipwa na wahusika. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na:

1. kutoa matangazo ya kuwataka wadaiwa kulipa madeni yao;
2. Kuwakabidhi wadaiwa kwa kamati za ulinzi na usalama za Wilaya kwa maelekezo ya Baraza la Mapinduzi ili kila Wilaya iweze kuwafuatilia na waweze kulipa;
3. Kuwataka wadaiwa madeni yao wakati wa kuwalipa fedha za kifujasho; na
4. Kutoa barua za indhari za kuwataka kuwashitaki wadaiwa.

Kwasasa Wizara inaamini kuwa kiasi kikubwa cha deni hilo tayari kimeshalipwa. Hata hivyo, kutopatikana kwa baadhi ya taarifa muhimu (vielelezo vya malipo) kumesababisha wakodishwaji waliolipa kutoondolewa katika orodha ya wenye madeni.

Miongoni mwa taarifa zilizokosekana ni:

Wakodishwaji kutowasilisha stakabadhi walizofanyia malipo benki ili kuandikiwa stakabadhi ya Wizara;

Kukosekana kwa taarifa za waliolipwa madeni kupitia makato ya vifuta jasho kutoka Wizara ya Fedha licha ya kuomba taarifa hizo; na

Kukosekana kwa ripoti ya kamati maaluo ya Baraza la Mapinduzi iliyoundwa kusikiliza malalamiko ya wakodishwaji ambapo baadhi yao walisamewa na wengine walipunguziwa madeni yao.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati haikuridhishwa na majibu yaliyotolewa na watendaji wa Wizara na ilisikitishwa sana kwani Wizara ilishindwa kuwa na taarifa zilizokuwa sahihi kwa madai kwamba kuna Wakulima walikuwa wanaenda kulipa madeni yao benki lakini hawarudishi risiti ili kupunguza deni wanalodaiwa. Kamati imegundua kwamba watendaji wa Wizara hususan Pemba walikuwa hawatekelezi majukumu yao ipasavyo kwa vile walikuwa wakitekeleza majukumu yao kwa kuweka maslahi binafsi mbele kuliko maslahi ya Taifa. Hali hiyo imepelekea fedha nyingi kupotea katika mikono ya wachache. Kwa mantiki hiyo, hoja hii imebakia.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Serikali kupitia vyombo vyake vya uchunguzi ilifuatiliw kwa karibu kadhia hii iliyokuwa ya siku nyingi na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaobainika kuhusika ikiwemo kulipia madeni wanayodaiwa hadi ifikie shilingi 830,476,000 linalotokana na ukodishwaji wa mashamba hayo.
2. Wizara ihakikishe wale wote wanaodaiwa wasikopeshwe tena mashamba hayo kwa vile wamekosa kujiaminisha kwa Serikali.

**Hoja nambari 6.3.7 Kutokutayarishwa kwa usuluhisho wa kibenki (bank reconciliation) wa hesabu ya mapato ya mikarafuu**

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo inatakiwa kukusanya mapato kutoka katika vianzio vyake mbali mbali vya mapato kwa mujibu wa sheria na kanuni za fedha za Zanzibar.

Katika kupitia kumbukumbu za madaftari ya utunzaji wa fedha, ukaguzi umeshindwa kujiridhisha juu ya kiwago sahihi cha fedha kilichooneshwa katika daftari la kutunzia kumbukumbu za fedha “cash book” na fedha halisi iliyohifadhiwa benki kupitia hesabu namba 0735684001 inayotambulika kwa jina la “hesabu ya mapato ya Karafuu”.

Kutukuandaa taarifa za usuluhisho wa benki kunapelekea utojua mtiririko wa fedha baina ya daftari la fedha na taarifa ya mialaka ya fedha za benki jambo ambalo

hupelekea kuksekana kwa usahihiwa taarifa za fedha zinazoandaliwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma ya Zanzibar nabari 12 ya mwaka ya 2016.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inakubaliana na hoja ya kutokutayarishwa kwa usuluhisho wa kibenki (Bank Reconsiliation) kwa hesabu ya mapato ya mikarafuu. Hali hii ilitokana na ugumu uliokuwepo kwa kuwa Wizara ilikuwa na hesabu (account) moja tu ya kukusanyia mapato yakr.

Hata hivyo, kwa kuwa hivi sasa Wizara inatumia hesabu maalum ya kukusanyia mapato ya mashamba ya karafuu yenye namba 0735684001 baada ya kupata idhini ya Serikali ya kufungua hesabu hiyo, suala la utayarishaji wa usuluhishi wa kibenki wa hesabu ya mapato ya mikarafuu sio tatizo tena.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Watendaji wa Wizara wamekiri kwamba hawakuwa wakifanya usuluhisho wa kibenki jambo ambalo limepelekea kushindwa kutambua mapema changamoto ya malipo yanayofanywa na wakulima na kupelekea hadi Kamati inaondoka ilikosa kupata malipo sahihi yaliyofanywa licha ya Wizara kudai kwamba baadhi ya Wakulima walikuwa wakilipa.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Wizara iandae utaratibu wa muda baada ya muda kufanya usuluhisho wa kibenki ili kutambua mapema kasoro zinazojitokeza.

**Hoja nambari 6.3.8: Deni la fedha za kifutajasho zinazodaiwa na wakulima wa mikarafuu shilingi 80,065,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 80,064,000 zinadaiwa na Wakulima 171 wa mashamba ya eka (eka tatu) za mikarafuu ambao ameahidiwa kuptiwa kifuta jasho kutokana na kushughulikia mashamba ya mikarafuu hiyo. Kifuta jasho hicho hutolewa kwa kiwango cha asilimia tofauti kati ya asilimia 40, 30, 20 na 10 kulingana na ushughulikiaji wa shamba husika kwa lengo la kuwatia moyo.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inatambua uwepo wa deni a fedha za kifutajasho zinazodaiwa na wakulima 171 wa mashamba ya Serikali ya eka tatu ya mikarafuu. Deni sahihi ni shilingi milioni 83,664,000 na sio shilingi 80,064,000 kama ilivyoainishwa katika ripoti ya ukaguzi.

Wizara tayari imashawasilisha Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango orodha kamili ya majina ya wakulima wanaodai vifutajasho kwa ajili ya kufanyiwa malipo hayo.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Watendaji wa Wizara wamekiri kuwepo kwa deni linalotokana na vifutajasho vya wakulima walioyaendeleza mashamba ya mikarafuu ambao hawakuwa na uwezo wa kuyakodi. Kamati imegundua kwamba juhudi za kufuatilia kwa karibu malipo ya fedha hizo bado haziridhishi na zinahitaji kuongezwa.

### Mapendekezo ya Kamati ya PAC

1. Wizara ihakikishe fedha za kifutajasho zinalipwa na zinawafikia walengwa.
2. Wizara iweke vizuri kumbukumbu za malipo ya wakulima hao.

### MAMBO YALIYOBAINIKA WAKATI KAMATI ILIPOKUTANA NA BAADHI YA WAKODISHWAJI WA MASHAMBA YA MIKARAFUU

Kutokana na kuwepo changamoto nyingi zinazoashiria udanganyigu na upotevu wa fedha za Serikali uliotokana na ukodishwaji wa Mashamba ya Mikarafuu Kisiwani Pemba, Kamati kwa nia njema iliamua kuwakutanisha Watendaji wa Wizara ya Kilimo na baadhi ya Wakodishwaji Mashamba hayo ili kuwasikiliza kwa jinsi gani waliweza kutekeleza shughuli za ukodishwaji. Aidha, walikuwemo pia wakulima ambao wanadaiwa fedha za mashamba hayo na wengine walioorodheshwa katika Ripoti ya Mdhibiti ya ukodishwaji wa mashaba hayo.

Miongoni mwa wakulima iliyokutana nao ni:

1. Bwana Mwinyi Faki Hassan;
2. Bwana Mohamed Kai Hassan;
3. Bwana Salum Jadi Kadika;
4. Bwana Ohman Yahya Othman;
5. Bwana Jecha Mohammed Faki;
6. Bwana Omar Abdalla Kilindi;
7. Bwana Mussa Zaid Mbarouk;
8. Bibi Salama Haji Khamis; na
9. Bwana Ali Abdalla Saleh.

Sambamba na kukutana na wakulima hao, Kamati pia ilifanikiwa kutembelea Mashamba kadhaa yaliyokodishwa pamoja na kuangalia kumbukumbu za mikataba iliyofungwa na wakulima hao. Kwa ujumla wake, Kamati iliweza kugundua mambo yauatayo:-

1. Zoezi la ukodishwaji mashamba ya mikarafuu lilikabiliwa na utumiaji mbaya wa madaraka kwa baadhi ya watendaji wa Serikali kujilimbikizia mali za umma;
2. Baadhi ya mikataba ilionekana kuwa ya kughushi kwa vile Msimamizi wa

ukodishwaji (Ndugu Haji Mussa) alikuwa ameshasimamishwa kazi lakini ilionekana imesainiwa wakati yeye haupo au kusainiwa na Msimamizi Msaidizi (Ndugu Ali Othman Ibrahim) kwa tarehe za nyuma ambayo yeye alikuwa hayupo Ofisini wala hajakabidhiwa rasmi kazi hiyo na kupelekea jumla ya shilingi 830,476,000/- kupotea;

3. Kulikuwa na uwajibikaji mbovu na usioridhisha uliofanywa na watendaji wa Wizara ya Kilimo hususan waliokuwepo katika nafasi ya usimamizi wa minada ya ukodishwaji huo kwani walijishirikisha katika biashara ya minada na kuacha majukumu yao ya usimamizi;
4. Kulikuwa na uwekaji mbaya wa kumbukumbu za mikataba kwani hata baadhi ya mikataba ilipohitajika haikupatikana au ilichukua muda mrefu kupatikana. Kwa mfano, Kamati imejionea mikataba imetiwa kwenye bahasha za A4;
5. Wakulima waliyoyaendeleza mashamba hayo baadhi yao walipatiwa fedha kidogo. Kwa mfano, Bwana Mwinyi Faki Hassan alipatiwa shilingi elfu kumi kama kifuta jasho kisicholingana na uhalisia wa shamba lenyewe lilivyokuwa na hatimae kukodishwa watu wengine;
6. Kuna baadhi ya mikataba haikutiwa saini na wakodishwaji na kupelekea wasiwasi kuhusu uhalali wa ushahidi huo;
7. Kuna baadhi ya wakulima walikodishwa mashamba lakini hawajawahi kusaini hata mkataba mmoja;
8. Ukodishwaji wa baadhi ya mashamba ulifanywa kwa kujuwana kwa kutumia msemo 'lianatundikwa' kwa maana kwamba shamba hilo halijafikia bei katika mnada na baadae watu wanazunguka nyuma na kuuziwa kwa bei ya chini kabisa;
9. Kuna baadhi ya Wakodishwaji wanadaiwa fedha nyingi ambazo hawajalipa kutokana kutosimamiwa ipasavyo. Kwa mfano Bwana Salum Jadi Kadika anadaiwa shilingi 15,560,000 ambae anapatikana katika ukurasa wa 126;
10. Kuna baadhi ya wakodishwaji wameonakana wanadaiwa madeni kidogo katika kitabu wakati uhalisia wanadaiwa madeni makubwa. Mfano, Bwana Haji Abdalla Abdalla anaonekana kudaiwa shilingi milioni 1,770,000/- wakati anadaiwa zaidi ya shilingi milioni 30,000,000/-;
11. Kuna baadhi ya Wakodishwaji wameonekana hawadaiwi kwa madai kwamba walilipa madeni yao lakini walikuwemo katika orodha ya watu wanaodaiwa;
12. Kuwepo kwa mfumo mbaya wa ulipaji madeni. Wakulima waliokuwa wanadaiwa kifuta jasho ambao hawakulipa walikuwa wanakatwa katika malipo yao ya ukodishwaji na kutakiwa kupatiwa risiti kutoka Wizara ya Fedha na kuiwasilisha Wizara ya Kilimo kwa kufutwa deni analodaiwa. Changamoto iliyopo ni kwamba baada ya kupatiwa risiti huwa hawaendi Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kupatiwa risiti ya kupunguza deni au kufutwa katika orodha ya wanaodaiwa iwapo amemaliza deni;
13. Kuna baadhi ya wakulima wameorodheshwa katika watu wanaodai kifutajasho lakini hawastahiki kupatiwa kwa vile Mkulima aliyekuwa analishughulikia shamba hilo alikuwepo lakini alikuwa mgonjwa isipokuwa aliandika jina lake kwamba anadai kwa vile aliidhinishwa kwa maneno kulisimamia. Mfano Bwana Mohammed Kai Bakar hakustahiki kuwemo kwenye orodha ya wanaodai kifutajasho lakini anaonekana anadai shilingi 800,000/- (ukurasa 149);
14. Wakulima wengi wamejazishwa mikataba pasi na kupatiwa uelewa kabla

kuhusiana na athari ya mikataba hiyo;
15. Wakulima wengi waliojazishwa mikataba hawakupatiwa nakala yao ya mkataba husika. Mfano hai ni Bwana Salum Jadi Kadika;
16. Shamba moja lilikuwa likikodishwa zaidi ya mara moja na kusababisha utata juu ya umiliki wa shamba husika;
17. Baadhi ya wakodishwaji walikodishwa zaidi ya shamba moja pasi na kulipa mashamba ya awali. Kwa mfano, Bwana Haji Abdalla Abdalla na Bwana Mhene Ali Suleiman (ukurasa wa 43 na 107);
18. Kuna baadhi ya wakulima walikodishwa shamba kwa mnada na kusaini lakini baadae alinyang'anywa na kupewa mtu mwengine;

**Mapendekezo ya Kamati**

1. Kwa vile kuna udanyanyifu na ubadhirifu mkubwa uliojitokeza katika zoezi zima la ukodishwaji wa Mashamba ya Mikarafuu ambao ulipelekea upotevu wa fedha za Serikali za jumla ya shilingi milioni 830,476,000/-. Hivyo, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi iwatafute na kuwahoji wale wote waliohusika na hujuma hizo na wakithibitika wapelekwe mahakamani kwa hatua zaidi.
2. Wizara ya Kilimo ikitathmini na kuundwa upya kitengo cha ukodishwaji mashamba kwani kimeonekana kina kasoro nyingi zilizopelekea kushindwa kusimamia ipasavyo majukumu yao.
3. Wakodishwaji wote wanaodaiwa walipe malimbikizo ya madeni yao.
4. Kuundwe kwa Kamati ndogo ifuatilie wadaiwa wote wa madeni ili kubaini madeni halisi wanayodaiwa na kuwalazimisha kulipa ndani ya muda maalum kinyume na hivyo wawachukulie hatua za kisheria.
5. Wizara ihakikishe inawweka vizuri kumbukumbu za wakodishwaji mashamba kwa utaratibu wa kidigitali na sio kuzihifadhi katika bahasha.
6. Wananchi waliyoyaendeleza Mashamba ya Mikarafuu watathminiwe na ikithibitika walipwe kifuta jasho wanachostahiki.

## UCHUNGUZI WA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KUHUSU RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO (CDF) KUANZIA MWAKA 2019 HADI 2020

### MAELEZO YA JUMLA YA KAMATI YA PAC

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ilitarajiwa kufuatilia na kuchunguza Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na Ukaguzi wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa kipindi cha miaka miwili (2018 hadi 2019 na 2019 hadi 2020).

Hata hivyo, Kamati ya PAC haikufanikiwa kutekeleza ipasavyo jukumu lake hilo, kutokana na maelekezo ya Kamati ya Uongozi ya Baraza la Wawakilishi kuamua kwamba Ripoti ya Ukaguzi wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa

mwaka 2018 hadi 2019 isifanyiwe kazi kwa vile kuna kazi kubwa ambayo Kamati ya PAC inatakiwa izitekeleze kufuatia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuwasilisha Ripoti nyengine za Ukaguzi Maalum. Sababu nyengine ni kupitwa sana kwa muda kwa ukaguzi huo. Kwa maelekezo hayo mafupi, Kamati ya PAC ilikagua Miradi ya mwaka 2019 hadi 2020 pekee.

Sambamba na hilo, kutokana na muda wa kazi ya Kamati ya PAC kuwa mdogo, hasa ukizingatia Mkaguzi amewasilisha vitabu vyengine tukuki katika mwaka 2020 hadi 2021 vinavyohusu Ukaguzi tofauti. Hivyo, Kamati ya PAC, kwa upande wa uchunguzi wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo za mwaka 2019 hadi 2020, ulifanikiwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika Majimbo yanayoelezwa hapa chini.

### UTEKELEZAJI WA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KATIKA WILAYA YA WETE - PEMBA KWA MWAKA 2019 HADI 2020

### JIMBO LA MTAMBWE

| Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ujenzi wa mnara wa maji na kuweka tangi la maji. | Piki | 5,000,000 | Mradi umekamilika |
| | Matengenezo ya barabara kwa kiwango cha fusi MakongeniKinazini. | Mtambwe Kusini | 6,900,000 | Mradi umekamilika |
| | Ununuzi wa kompyuta moja na printa moja kwa skuli ya Maziwani. | Maziwani | 4,000,000 | Mradi umekamilika |
| | Ununuzi wa mafuta ya kuchimba na kutawanya fusi Uondwe-Kele. | Mtambwe kaskazini | 3,000,000 | Mradi umekamilika |

### Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mtambwe

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mtambwe imekiri kuingiziwa jumla ya Shilingi 20,000,000 kutoka Serikalini na kutekeleza miradi mbali mbali katika Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imekagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji wa miradi zikiwemo barua ya maombi ya Mnara wa maji kutoka Skuli ya Piki Msingi, barua ya maombi ya kupatiwa 'computer' kutoka Skuli ya Msingi na Maandalizi ya Maziwani, fomu za maombi ya fedha pamoja na utekelezaji. Vile vile Kamati iligundua kuna kazi mbali mbali zilizotekelezwa kupitia Miradi hiyo, ikiwemo:-

1. Mradi wa ujenzi wa kituo cha Afya cha Maziwani ambapo fedha za Mfuko zilitumika kuweka sakafu pamoja na 'fitting' ya umeme na maji. Aidha, Kamati ilitembelea Mradi wa ununuzi wa 'computer' na 'printer' vilivyopo katika skuli ya Msingi ya Maziwani.

2. Mradi wa Mnara wa tenki la maji safi la lita 5,000 liliopo katika Skuli ya Msingi, Maandalizi na Sekondari ya Piki. Fedha za Mfuko zilijenga Mnara, kununua tenki na miundombinu ya maji. Aidha, Kamati imegundua kwamba 'Pump' ya maji haikuwemo ndani ya kisima na huduma ya maji ilikuwa haipatikani). Kamati ilipohoji kaddhia hiyo ilielezwa 'pump' iliharibika na kusemekana imepelekwa kwa fundi lakini haikurudishwa ambapo Mwenyekiti wa Kamati hakuelezwa lolote na Wsjumbe wa Kamati yake kuhusiana na suala hilo.

**Mapendekezo ya Kamati**

1. Kamati iwe makini inapojaza fomu za maombi ya fedha ili kuondosha kasoro zinazojitokeza.

2. Kamati ihakikishe inatafuta na kuvihifadhi vizuri vielelezo vya matumizi ya fedha za Mfuko.

3. Kamati ishirikiane na Mwenyekiti wake kuhakikisha inafuatilia matengenezo ya 'pump' iliyopelekwa katika matengenezo ili huduma ya maji iweze kupatikana.

**UTEKELEZAJI WA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KATIKA WILAYA YA CHAKE CHAKE - PEMBA KWA MWAKA 2019 HADI 2020**

**JIMBO LA CHAKECHAKE**

| Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ununuzi wa mafuta ya diesel lita 431 kwa ajili ya ujenzi wa njia ya Ngomahazingwa. | Tibirinzi | 800,000 | Mradi umekamilika |
| | Uwezekaji wa mabanda matatu skuli ya msingi Shungi. | Shungi | 9,000,000 | Mradi umekamilika |
| | Uwezekaji wa mabanda mawili skuli ya msingi ya Chanjaani. | Chan-jaani | 6,000,000 | Mradi umekamilika |
| | Ununuzi wa vifaa vya maji na uungaji wa maji Madungu Kosovo. | Madungu | 3,900,000 | Mradi umekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chakechake**

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Chakechake imekiri kuingiziwa jumla ya Shilingi 20,000,000 kutoka Serikalini na kutekeleza miradi mbali mbali katika Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati imekagua nyaraka mbali mbali za maombi na utekelezaji wa miradi zikiwemo kumbukumbu za kikao cha tarehe 3/4/2018 kilichoidhinisha miradi iliyotekelezwa, fomu za maombi ya fedha pamoja na fomu ya utekelezaji.

Kamati imebaini jumla ya shilingi milioni 1.1 zilitumika kama ni posho kwa Wajumbe wa Kamati ya Mfuko wa maendeleo ya Jimbo lakini hazikuoneshwa katika fomu ya utekelezaji. Aidha, malipo hayo yalifanyika kinyume na maelekezo yaliyotolewa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambapo inazitaka Kamati za Mfuko zitumie jumla ya shilingi milioni 1 kama ni gharama za uendeshaji badala yake zimetumika jumla ya shilingi milioni moja na laki moja.

Baada ya kupitia vielelezo, Kamati ilifuatilia kwa undani utekelezaji huo kwa kutembelea ujenzi wa banda la skuli ya msingi Shungi hadi kiwango cha kuezeka

lakini hayajatiwa sakafu ambapo jumla ya shilingi milioni 13 kwa mwaka 2018/2019 zimetumika kwa ujenzi wa matofali, plasta na madirisha. Kwa mwaka 2019/2020, zilitumika jumla ya shilingi milioni 9 kwa kuezekea skuli hiyo. Kijumla, Kamati haikuridhika na matumizi ya fedha hizo kwani hayaendi sambamba na thamani hali ya fedha iliyotumika.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo zitumike kwa mujibu wa Sheria namba 4 ya mwaka 2007 pamoja na maelekezo yanayotolewa na Msimamizi Mkuu wa Miradi hiyo (Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

## JIMBO LA CHONGA

| Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Upelekaji wa umeme Kijiji cha Matale nguzo sita. | Matale | 4,008,000 | Mradi umekamilika |
| | Ujenzi wa banda la skuli ya maandalizi Tundauwa. | Kilindi | 14,800,000 | Mradi umekamilka |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chonga**

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Chonga imekiri kuingiziwa jumla ya Shilingi 20,000,000 kutoka Serikalini na kutekeleza Miradi mbali mbali katika Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imekagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji wa Miradi zikiwemo kumbukumbu za kikao cha tarehe 12/5/2020 kilichoidhinisha miradi iliyotekelezwa, fomu za maombi ya fedha pamoja na fomu ya utekelezaji. Hata hivyo, Kamati ya PAC imebaini kuwa kuna tofauti ya jumla ya fedha iliyotumika ambapo Ripoti ya Mdhibiti imeainishwa jumla ya shilingi 18,808,000 wakati Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ni shilingi 20,108,000 sawa na tofauti ya shilingi 1,192,000 ukiacha fedha alizochangia Mwenyekiti (Mwakilishi).

Kamati ilipoangalia fomu ya utekelezaji iligundua kwamba Kamati ya Mfuko wa

Jimbo imetumia shilingi 1,300,000 kwa gharama za uendeshaji, jambo ambalo linaenda kinyume na utaratibu uliowekwa wa kutumia si zaidi ya shilingi 1,000,000.

Sambamba na ukaguzi huo, Kamati ya PAC imebaini kwamba kikao cha uibuaji miradi kilihudhuriwa na watu 15 ambapo Waalikwa walikuwa watatu na kupelekea fedha ya uendeshaji iliyolipwa kuongezeka. Aidha, kuna baadhi ya fomu nambari 1 na 2 Kamati haikupata kuziona na kuzipitia.

Vile vile Kamati iligundua kuna kazi mbali mbali zilizotekelezwa kupitia Miradi hiyo, ikiwemo Mradi wa ujenzi katika skuli ya Maandalizi Tundauwa ambapo kumejengwa vyumba viwili (madarasa) pamoja na Ofisi mbili za Walimu hadi kufikia katika kiwango cha 'gebo'.

### Mapendekezo ya Kamati

1. Wakurugenzi wa Serikali za Mitaa wahakikishe fedha ya uendeshaji inatumika kwa mujibu wa kiwango kilichokubalika.
2. Baraza la Mji Chake chake lihakikishe linatunza vizuri kumbukumbu za Mfuko ili zitakapohitajika ziweze kupatikana kwa wakati.

### JIMBO LA WAWI

| Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ujenzi wa skuli ya maandalizi Kibokoni<br><br>(Madarasa Mawili na Ofisi ya Walimu). | Kibokoni | 19,000,000 | Mradi umekamilika |

### Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Wawi

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Wawi imekiri kuingiziwa jumla ya Shilingi 20,000,000 kutoka Serikalini na kutekeleza miradi mbali mbali katika Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imekagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji wa miradi zikiwemo kumbukumbu za kikao cha tarehe 6/3/2020 kilichoidhinisha miradi iliyotekelezwa, fomu za maombi ya fedha pamoja na fomu ya utekelezaji.

Vile vile Kamati iligundua kuna kazi mbali mbali zilizotekelezwa kupitia Miradi hiyo, ikiwemo Mradi wa ujenzi wa banda la skuli ya Maandalizi (vyumba 4), Ofisi za Walimu Vitongoji - Kibokoni pamoja na kuweka kifusi kwenye vyumba vyote.

Baada ya Kamati ya PAC kupokea taarifa na kutembelea Mradi, Kamati iliridhika na haikuwa na mapendekezo yoyote.

### UTEKELEZAJI WA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KATIKA WILAYA YA KUSINI - PEMBA KWA MWAKA 2019 HADI 2020

### JIMBO LA CHAMBANI

| Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha iliyotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ujenzi wa darasamoja la Tutu na Ofisi Mapape. | Chambani | 9,300,000 | Mradi umekamilika |
| | Uanzishaji wa darasa la Nursery Shule ya Kwamkoba. | Mgagadu | 5,000,000 | Mradi umekamilika |
| | Kusaidia bati 35 skuli ya TUTU Chambani na mipira ya maji Ukutini. | Chambani na Ukutini | 1,700,000 | Mradi umekamilika |

### Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chambani

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Chambani imekiri kuingiziwa jumla ya Shilingi 20,000,000 kutoka Serikalini na kutekeleza Miradi mbali mbali katika Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

### Uchunguzi wa Kamati ya PAC

Kamati imekagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji wa Miradi zikiwemo

kumbukumbu za kikao cha tarehe 30/7/2019 kilichoidhinisha Miradi iliyotekelezwa, fomu za maombi ya fedha pamoja na fomu ya utekelezaji.

Katika ukaguzi wa mwaka 2019/2020, Kamati ilielezwa kuna shilingi 3,500,000 hazikutumika kwasababu zilikuwa zimabakia benki pasi na kuwepo kwa 'bank statement'. Kamati ilifuatilia kwa undani maelezo hayo na kugundua kwamba fedha hizo zilitumika kwa ujenzi wa darasa la wanafunzi wa chekecheka liliopo ndogoni - Wambaa. Hali hiyo ilijitokeza kwa vile Mradi huo haukutekelezwa kwa wakati. Vile vile Kamati iligundua kuna kazi mbali mbali zilizotekelezwa kupitia Miradi hiyo, ikiwemo:

Mradi wa ujenzi wa skuli ya wanafunzi (Tutu) uliopo Mapape – Chambani. Katika Mradi huu, fedha za Mfuko zilielekezwa katika ujenzi wa darasa moja na chumba cha Ofisi ya Walimu ambapo jumla ya shilingi milioni 9 zilitumika.

Kamati imebaini kwamba skuli hiyo haikujengwa katika mazingira rafiki ya wanafunzi kuweza kufika kwa urahisi na kufunzwa, vifaa vilivyotumika kwa ujenzi vilikuwa vichakavu (mbao), madarasa yalikuwa na nyufa, hayakuwa na sakafu, madirisha pamoja na ngazi za kuingilia ndani. Kadhalika, wakati Kamati inautembelea ujenzi huo, hakukuwa na watoto wanaosoma katika skuli hiyo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Fedha za Mfuko zitumike katika ujenzi wa Miradi itakayotumika na kuleta tija kwa wananchi.
2. Miradi itekelezwe katika maeneo rafiki yatakayowawezesha wananchi kufika na kutumia mradi.
3. Baraza la Mji la Mkoani pamoja na Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chambani wahakikishe wanauendeeza ujenzi wa Skuli ya Mapape hadi kukamilika kwake ili skuli hiyo iweze kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.
4. Baraza la Mji la Mkoani pamoja na Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chambani wahakikishe wanawahamasisha wanakijiji waweze kuwaleta wanafunzi kusoma katika skuli hiyo na kuacha kuwapeleka katika madrsa kujifunza.

## JIMBO LA MTAMBILE

| Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha iliyotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Kuweka kifusi barabara ya Kengeja Polisi/Mwakunguu/ Jomvu na njia ya Kimbini. | Kengeja | 9,450,000 | Mradi umekamilika |
| | Ukarabati barabara ya Mgongeni Jembele. | Kangani | 8,400,000 | Mradi umekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mtambile**

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mtambile imekiri kuingiziwa jumla ya Shilingi 20,000,000 kutoka Serikalini na kutekeleza miradi mbali mbali katika Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati imekagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji wa miradi zikiwemo kumbukumbu za miradi iliyotekelezwa, fomu za maombi ya fedha pamoja na fomu ya utekelezaji. Hata hivyo, Kamati imebaini kutumika jumla ya shilingi 17,850,000 zilitumika na fedha zilizobakia zilikuwa benki lakini Kamati ilishindwa kulithibitisha hilo kwa vile hakukuwa na kielelezo (bank Statememnt). Vile vile, Kamati iligundua kuna kazi mbali mbali zilizotekelezwa kupitia Miradi hiyo, ikiwemo:

Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Kangani. Katika Skuli hiyo, Mradi ulifanikiwa kujenga madarasa 4 kuanzia gebo hadi kuezeka kwa jumla ya shilingi milioni 12. Kamati imeridhika na matumizi ya fedha za Mfuko kwani umeleta tija kwa wanafunzi wetu ambao wanasoma katika madarasa hayo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya PAC inapendekeza kwamba fedha za Mfuko wa Maendeleo zitumike ipasavyo kama inavyoelekezwa na Sheria nambari 4 ya mwaka 2007.

### UTEKELEZAJI WA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KATIKA WILAYA YA MJINI KWA MWAKA 2019 HADI 2020

## JIMBO LA AMANI

| Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha Zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ukarabati wa barabara za ndani kwa hatua ya uwekaji wa kifusi | Jimbo zima | 20,000,000 | Mradi Umekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Amani**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Amani imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zilitumika katika utekelezaji wa mradi mmoja kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC ilibaini kuwa posho za vikao kwa Wajumbe wa Kamati ya Mfuko ilikuwa inalipwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Kamati imebaini kuwa kuwepo kwa utaratibu mbaya ya uendelezwaji wa Miradi iliyotekelezwa baada ya kumalizika kwa awamu ya Mwenyekiti aliyeitekeleza Miradi hiyo (Projects sustainability).
2. Kamati pia imebaini kuwa Katibu wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hatokani na Baraza la Manispaa Mjini kama inavyoelekeza Sheria ya Mfuko wa Jimbo Namba 4 ya mwaka 2012.
3. Vile vile Kamati imegundua kuwa kulikuwa na mashirikiano mazuri katika zoezi la utiaji wa kifusi kwani ulihusisha maeneo mbali mbali yakiwemo ya Amani Fresh, Makawa, Matopeni hadi Ziwatuwe.

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji Mradi pamoja na maeneo ya barabara zilizotiwa kifusi ambapo kwa ujumla Kamati imeridhika na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC inashauri kuwa kuwe na muendelezo mzuri wa utekelezaji Miradi iliyoibuliwa pindipo ikitokezea Mwenyekiti wa Mfuko kuwa mpya.

## JIMBO LA CHUMBUNI

| Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha Zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ununuzi wa vifaa vya michezo | Jimbo la Chumbuni | 3,426,000 | Mradi Umekamilika |
| | Uwekaji wa kifusi barabara za ndani | Banko | 1,200,000 | Mradi Umekamilika |
| | Uwekaji wa madirisha skuli ya secondari ya Chumbuni. | Banko | 2,600,000 | Mradi Umekamilika |
| | Uekezaji na uwekaji wa madisha katika skuli ya maandalizi Banko | Banko | 8,107,000 | Mradi Umekamilika |
| | Ujengaji wa mnara wa maji pamoja na ununuzi wa tangi la maji | Masumbani | 4,690,000 | Mradi Umekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chumbuni**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chumbuni imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 kutoka Serikalini ambazo zimetumika katika kutekeleza

Miradi mbali mbali iliomo katika Jimbo la Chumbuni.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imebaini kuwa Katibu wa Kamati ya Mfuko huo wa Maendeleo ya Jimbo hatokani na Baraza la Manispaa Mjini kama inavyoelekeza Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Namba 4 ya mwaka 2012.

Kamati ilikagua nyaraka mbali mbali za Mradi zikiwemo fomu za mradi pamoja na nyaraka za matumizi ya Mradi huo. Aidha, Kamati ilipata nafasi ya kukagua Miradi ya Shehia ya Mwembe Makumbi ikiwa ni moja ya Skuli iliyoezekwa na kuwekwa kwa madirisha katika skuli ya maandalizo Banko. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa Mradi, matumizi ya fedha zake pamoja na utunzaji mzuri wa kumbukumbu za utekelezaji Mradi huo.

## JIMBO LA JANG'OMBE

| **Fedha zilizoingizwa** | **Mradi** | **Shehia** | **Fedha Zilizotumika** | **Hatua ya utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ugaawaji wa chakula cha kambi (wanafunzi wa jimbo la Jang"ombe wa kidatu cha sita ) Ugawaji wa jezi za michezo | Jangombe | 725,000 | Lengo limefanikiwa |
| | Ugawaji wa jezi za michezo. | Jimbo zima | 2,340,000 | Lengo limekamilika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Ukarabati wa kituo cha ujasiri amali | kilimani | 15,058,912 | Hatua ya utekelezaji |
| | Ununuzi wa mipira ya maji na usambazaji | Kidongo chekundu,k walinatu,na jangombe urusi | 1,050,000 | Mradi umekamilika |
| | Ununizi wa betri za gari nza jimbo | Jimbo zima | 360,000 | Mradi umekamilika |
| | Malipo ya posho kwa wajumbe | Jimbo zima | 480,000 | Mradi umekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Jan'gombe**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Jang'ombe ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 kutoka Serikialini ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mbali mbali kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:-

1. Uwekaji usioridhisha wa kumbukumbu za Miradi ambapo ilibainika kukosekana kwa vielelezo halisi (Original documents) hususan za fomu za Miradi. Kamati ya Mfuko wa Jimbo ilieleza kuwa waliwasilisha vielelezo halisi Ofisi ya Uratibu wa Miradi iliyopo kwa Ofisi ya Makmo wa Pili wa Rais. Hata hivyo, Watendaji wa Ofisi ya Uratibu wa Miradi hiyo, walieleza kuwa hawakuwa nazo.

2. Kukosekana kwa nyaraka na vielelezo vya fedha shilingi 20,000,000 baada ya Mwenyekiti wa Mfuko wa Jimbo kuondoka na nyaraka zote wakati

ilipoingia awamu mpya. `

3. Kitengo cha ufuatiliaji wa miradi ya Jimbo katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kushindwa kufuatilia Majimbo kila baada ya miezi mitatu kama inavyotakiwa kutokana na uhaba wa fedha.

4. Katika ziara ya kutembelea miradi ya usambazaji wa maji katika Shehia za Jang'ombe na Urusi Kamati ya PAC imeridhika na hali ya upatikanaji wa maji katika Jimbo hilo kutokana na miradi hiyo pamoja na utaratibu uliowekwa na wananchi wa kuchangia shilingi 5,000,000 kwa mwezi. Aidha, ilielezwa kuwa miradi hiyo imefanikiwa kwa ushirikiano mkubwa pia na Mbunge wa Jimbo hilo kwa wakati huo.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

Serikali iangalie kwa uzito unaostahili suala la kukiimarisha na kukiwezesha kitengo kinachofuatilia miradi katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ili kiweze kufanya kazi zake kama inavyotakiwa hasa ikizingatiwa kuwa, miradi inayohitaji kusimamiwa na kufuatiliwa ni mingi na imegharimu fedha nyingi za Serikali.

## JIMBO LA KIKWAJUNI

| Fedha Zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha Zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ununuzi wa jenereta kwa ajili ya matumizi ya mskiti wa ijumaa miembeni | miembeni | 3,200,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Ununuzi wa gari aina ya Toyota Alhard kwa ajili utoaji wa huduma kwa wagonjwa na wananchi | miembeni | 16,000,000 | Mradi umekamilika |
| | Upatikanaji wa huduma za maji safi na salama | Kikwajuni mashariki | 1,000,000 | Mradi umekamilika |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya PAC kwa Fedha za Mfuko ya Jimbo la Kikwajuni**

Kamati ya PAC imeshindwa kukutana Kamati wa Mfuko wa Jimbo la Kikwajuni kutokana na kutopata mashirikiano mazuri KUTOKA KWA Mwenyekiti wa Kamati hiyo kwani kila Kamati ilipokuwa ikiwasiliana nae alikuwa akitoa dharura zisizo msingi kwamba yupo kwenye kazi za Kamati nyengine. Kwa hiyo, Kamati imeshindwa kufanya uchunguzi wake wa mipango na matumizi ya fedha za Miradi (shilingi 20,000,000) zilizotumika katika Jimbo hilo kw mwaka 2019/2020.

## JIMBO LA KWAHANI

| Fedha Zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha Zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ukarabati wa njia za ndani kwa hatua ya uwekaji vivusi | Jimbo zima | 12,000,000 | Mradi umekamilika |
| | Ununuzi wa mashine nne,za maji, mipira ya kusambazia maji,tangi la maji na vifaa vyengine vya kusambaza maji (plumbing | Kwalaamsha sebleni. | 8,000,000 | mradi |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kwahani**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kwahani ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbali mbali ya Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini yafuatayo:

1. Uwekaji mbaya wa kumbukumbu za nyaraka mbali mbali zinazohusu utekelezaji na matumizi ya fedha za Miradi ya Mfuko wa Jimbo. Hali hiyo imepelekea kukosekana kwa baadhi ya nyaraka wakati wa Kikao cha Kamati ya PAC zikiwemo stakabadhi halisi (original) za miradi ukiwemo mradi wa ununuzi wa mashine nne za maji na mpira wa kusambaza. Hadi Ripoti hii inaripotiwa, nyaraka hizo zilikuwa bado hazijawasilishwa katika Kamati ya PAC.

2. Kuchelewa kufuatilia stakabadhi (risiti) madukani ambapo baadhi ya stakabadhi zilibainika kuwa sio za mwaka husika yaan 2019/2020.

3. Kukoeskana kwa umakini katika uandaaji wa ripoti mbal imbali

kumepelekea kumbukumbu za vikao kutoainisha tarehe ya kufanyika vikao hivyo vya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

4. Kukosekana kwa ushirikiano baina ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo hilo na Baraza la Manispaa Mjini kwani hata Katibu wake hatoki Manispaa ya Mjini.

Kamati hikuridhishwa na uwekaji mbaya wa kumbukumbu za Miradi iliyotekelezwa katika Jimbo hilo kwa mwaka 2019/2020.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Kamati za Mfuko wa Jimbo zitekeleze miradi ya Jimbo kama Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo inavyoelekeza ikiwa ni pamoja na kutekeleza miradi inayokubalika kisheria na kushirikiana na Serikali za Mitaa ambako ndiko anapopatikana Katibu wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo kisheria.
2. Kamati za Mfuko wa Jimbo zihakikishe kuwa kumbukumbu za utekelezaji na matumizi ya Miradi ya Mfuko wa Jimbo zinapatikana kikamilifu wakati wote ambao Vyombo vya ukaguzi vinapofanya kazi zake.
3. Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo zitoe ushirikiano wa kutosha kwa Wakaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti kwa kutoa maelezo na vielelezo kikamilifu wakati wa ukaguzi.

## JIMBO LA MAGOMENI

| **Fedha Zilizoingizwa** | **Mradi** | **Shehia** | **Fedha Zilizotumika** | **Hatua ya utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ununuzi wa barakoa kwa ajili ya kujikinga maambukizi ya homa ya mapafu | Jimbo zima | 8,800,000 | Mradi umekamil;ika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kutoa mafunzo ya ushoni kwa vijana ishirini | Jimbo zima | 11,200,000 | Mradi umekamil;ika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Magomeni**

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Magomeni ilikiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambazo zimetumika katika kutekeleza miradi mbali mbali kama ilivYoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

1. Kutokuwepo kwa mashirikiano mazuri kutoka Manispaa ya Mjini kwa kuwa ilielezwa Kamati ya Mfuko wa Jimbo iliwajuilisha wahusika wa Manispaa ya Mjini lakini hawakuwa wakishiriki katika utekelezaji wa miradi ya Jimbo.

2. Kutokuwa na muendelezo wa miradi endapo Mwenyekiti wa Mfuko wa Jimbo hakuendelea. Hali hiyo inakwaza muendelezo wa miradi iliyoachwa na kupelekea kufa hali ya kuwa ina manufaa makubwa kwa wananchi.

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**

1. Pamoja na kwamba kuna baadhi ya Wenyeviti wa Mifuko hii ya Maendeleo ya Jimbo hawakupata nafasi ya kuchaguliwa kwa kipindi chengine lakini Miradi ambayo wameianzisha inatakiwa iendelezwe kwa kupata mashirikiano ya kutosha kutoka katika Kamati mpya za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

2. Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kupitia kitengo chake cha Miradi itoe muongozo ambao pamoja na mambo mengine utafafanua kwa uwazi zaidi miradi hasa inayopaswa kutekelezwa kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo.

**JIMBO LA MALINDI**

| Fedha | Mradi | Shehia | Fedha | Hatua ya |
|---|---|---|---|---|

| Zilizoingizwa | | | Zilizotumika | utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ujenzi wa darasa ,mskitinina choo katika skuli ya msingi makadara | makadara | 17,753,000 | Mradi unaendelea |
| | Ununuzi wa vifaa vya usafi kwa vikundi vya usafi miiulaya na vikokotoni | Makadara na vikokotoni | 1,750,000 | Mradi umekamil;ika |
| | Gharama za usafari na ufuatiliajiwa miradi | Jimbo zima | 497,000 | Mradi umekamil;ika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Malindi.**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Malindi imekiri kupokea shilingi milioni ishirini (20,000,000) kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbali mbali katika Jimbo hilo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imepitia vielelezo na nyaraka mbali mbali za Miradi ya Mfuko wa Jimbo la Malindi. Sambamba na hilo, imepitia fomu ya utekelezaji wa miradi pamoja na kuitembelea Miradi hiyo katika maeneo tofauti ilipotekelezwa na hatimae, Kamati yetu imeridhika na utekelezwaji wake.

**JIMBO LA MPENDAE**

| Fedha Zilizotumika | Mradi | Shehia | Fedha Zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Uchimbaji wa kisima, ujenzi wa mnara wan maji na ununuzi wa tangi na vifaa vya maji | Kwa binti hamrani | 8,000,000 | Mradi umekamil;ika |
| | Ukarabati wa njia za ndani mpendae - kwa bint hamrani | Mpendae kwa bint hamrani | 12,000,000 | Mradi umekamil;ika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Mpende**

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mpendae imekiri kupokea shilingi 20,000,000 amabazo zimetumika kutekeleza Miradi mbali mbali kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbali mbali zinazohusiana na matumizi pamoja na utekelezaji wa Miradi hiyo, Aidha, Kamati ya PAC ilipata nafasi ya kukagua kisima cha kwa Binti Amrani ambapo kwa ujumla, Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa Miradi katika Jimbo hilo.

**JIMBO LA SHAURIMOYO**

| **Fedha Zilizotumika** | **Mradi** | **Shehia** | **Fedha Zilizotumika** | **Hatua ya utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Uwekaji wa kifusi barabara za ndani | Shaurimoyo | 20,000,000 | Mradi umekamil;ika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Shaurimoyo**

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Shaurimoyo imekiri kupokea shilingi 20,000,000 na kutekeleza mradi wa Uwekaji wa kifusi barabara za ndani (Shaurimoyo) kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati imepitia na kuchunguza nyaraka mbali mbali zinazohusiana utekelezaji wa Miradi zikiwemo fomu za maombi ya miradi na fomu za utekelezaji wa miradi. Hivyo, Kamati ilibahatika kutembelea na kukagua barabara hiyo lakini kwa vile siku zilikuwa zimepita sana na Mradi wenyewe ulikuwa unahusu uwekaji wa kufusi kwa barabara ya Jimbo hilo. Kamati iligundua kifuzi chote kimeondolewa na mvua na kubakia baadhi ya alama. Kwa ujumla, Kamati ta PAC imeridhika na matumizi ya fedha za Mradi na utekelezaji wake.

MIRADI ILIYOTEKELEZWA NA MFUKO WA MAENDELEO YA JIMBO KATIKA MANISPAA YA MAGHARIBI - “A” KUANZIA MWAKA 2019/2020

JIMBO LA BUBUBU

| Fedha Zilizotumika | Mradi | Shehia | Fedha Zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Uwekaji wa kifusi barabara za ndani na kwenye daraja | Kijichi mbuzini | | |
| | katika shehiya ya chemchem na kizimbani<br>Ununuzi wa mshine mbili za maji kwa ajili ya shehiya ya | Kijichi zimbzni | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kizimbani | | | |
| | Ununuzi wa tangi mbili za maji kwa ajili ya shehiya chemchem na kizimbani | | | |
| | Ununuzi wa mipira ya maji 17 kwa ajili ya shehiya ya kizimbani ,mbuzini na dole | | | |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Bububu**

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Bububu imekiri kupokea fedha shilingi 20,000,000 kutoka Serikalini na kutekeleza Miradi mbali mbali kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti inagawa uongozi wa Jimbo hilo umetoa fedha za ziada kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilikagua nakala za nyaraka mbali mbali zinazohusu utekelezaji na matumizi ya fedha za Miradi hiyo, zikiwemo Fomu za Miradi na stakabadhi za malipo. Aidha, Kamati ya PAC ilipata nafasi ya kukagua baadhi ya miradi iliyotekelezwa ikiwemo ujenzi wa miradi ya maji katika shehia ya Chemchem na Kizimbani. Licha ya dosari za hapa na pale katika baadhi ya nyaraka za miradi, kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi ya Jimbo hilo kwa mwaka 2019/2020.

JIMBO LA MFENESINI

| Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Utoaji wa chakula kwa wananchi waliopata maafa ya mafuriko ya mvua. | Chuini, Kihinani na Mfenesini | 8,000,000 | Lengo limefi kiwa |
| | Ufukiaji wa mashimo kwa hatua ya kifusi. | Kikaangoni na Kihinani | 4,000,000 | Mradi Umekamilika |
| | Ununuzi wa matofali 1000 kwa ajili ya ujenzi wa skuli ya msingi Kama. | Kama | 1,200,000 | Mradi Umekamilika |
| | Ukarabati wa vyumba vinne vya skuli ya msingi ya Kama na Mwenge kwa hatua ya upigaji wa plasta. | Kama | 2,115,000 | Mradi Umekamilika |
| | Ununuzi wa tangi la maji lita 5000 kwa ajili ya ujenzi | Mwakaje | 895,000 | Mradi Umekamilika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | wa mnara wa maji. | | | |
| | Ununuzi wa mita ya umeme na uungaji wa umeme. | Chuini | 2,500,000 | Mradi Haujakamilika |
| | Posho kwa kamati | Jimbo zima | 350,000 | |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo waJimbo la Mfenesini**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Bububu imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya Jimbo hilo kwa mwaka 2019/2020 kama ilivyaoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbali mbali zinazohusu utekelezaji na matumizi ya fedha za Miradi hiyo zikiwemo stakabadhi za malipo na kumbukumbu za vikao mbali mbali vinavyohusiana na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa Miradi hiyo pamoja na matumizi ya fedha zilizotumika kwenye utekelezaji wake.

JIMBO LA MTONI

| Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Uendelezaji wa ujenzi wa banda la skuli ya msingi Mtoni. | Mtoni | 5,000,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Ununuzi wa mifuko ya saruji thelathini kwa ajili ya kutia zege barabara za ndani. | Kibweni (Mshe- lishelini) | 576,000 | Mradi umekamilika |
| | Ukarabati wa njia ya ndani kwa hatua ya uwekaji zege. | Mwanyanya kwa Goa njia ya Silver Stand. | | Mradi umekamilika |
| | Uwekaji wa kifusi barabara za ndani. | Kibweni kwa Botoro | 2,450,000 | Mradi umekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mtoni**
Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mtoni imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zimetumika katika utekelezaji wa Miradi mbali mbali ya Jimbo hilo kwa mwaka 2019/2020 kama ilivyaoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**
Kamati ya PAC imebaini kwamba kulikosekana mashirikiano baina ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo na Manispaa ya Magharibi "A" kwa vile watendaji wa Manispaa hiyo walikuwa hawashiriki vikao ingawa ilielezwa kuwa walikuwa wakipewa taarifa. Hata hivyo, Kamati imeridhika na utekelezaji wa miradi ya mfuko wa jimbo kwa mwaka 2019/20202

**Mapendekezo ya Kamati ya PAC**.
Wenyeviti wa Kamati za Kamati za Mfuko wa Jimbo wahakikishe kuwa Wajumbe waliomo katika Kamati hizo ni wale tu wanaokidhi vigezo na masharti ya kisheria.

JIMBO LA MTOPEPO

| **Fedha zilizoingizwa** | **Mradi** | **Shehia** | **Fedha zilizotumika** | **Hatua ya Utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|

| | |
|---|---|
| 20,000,000 | Taarifa za Miradi iliyotekelezwa hazikupatikana kwa ukaguzi. |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo lla Mtopepo**

Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Mtopepo imekiri kupokea jumla ya shilingi 20,000,000 ambazo zimetumika katika utekelezaji wa miradimbali ya Jimbo hilo kwa mwaka 2019/2020 kama ilivyaoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

1. Kamati ya PAC ilielezwa kuwa wakati Mkaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali alipokwenda kwa ajili ya ukaguzi vielelezo vya utekelezaji wa Miradi mbali mbali ya Maendeleo ya Jimbo hilo kwa mwaka 2029/2020 havikuwepo. Hali hiyo ilitokana na vielelezo vyote vilikuwa katika Manispaa ya Magharibi 'A' na kupelekea kutokupatikana. Hata hivyo, Kamati wakati inafanya kazi zake ilipata fusra ya kuviona na kuvikagua.
2. Kamati ya PAC ilivipitia baadhi ya vielelezo ikiwemo fomu ya za Miradi ya Jimbo. Kamati yetu iliitembelea Miradi ya Jimbo hilo ikiwemo Mradi wa kuimarisha barabara za ndani katika Jimbo zima ambao ilitumia jumla ya shilingi 20,000,000.
3. Kamati pia ilipitia ilipitia kumbukumbu ya kikao cha Kamati ya Mfuko kilichifanyika tarehe 20/02/2020 pamoja na hati za malipo na kuridhika na utekelezaji wa Miradi hiyo.

**Mapendekezo ya Kamati ya Kamati ya PAC**

Viongozi wa Kamati za Mfuko wa Jimbo wahakikishe kuwa Fomu za Miradi zinajazwa kikamilifu katika maeneo husika yaliyoainishwa katika Fomu hizo.

JIMBO LA WELEZO

| **Fedha zilizoingizwa** | **Mradi** | **Shehia** | **Fedha zilizotumika** | **Hatua ya utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|
| | Ujenzi wa kisima cha | Mtofaani | 10,000,000 | Mradi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | maji na Mnara wa maji safi | | | umekamilika |
| | Ujenzi wa kisima cha maji. | Hawaii | 12,500,000 | Mradi unaendelea. |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maenedeleo ya Jimbo la Welezo**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Welezo ilikiri kupokea shilingi 20,000,000/- kwa ajili ya kutekeleza Miradi iliyojipangia kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC imebaini kukosekana kwa mashirikiano kati ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo na iliyokuwa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo hilo. Hata hivyo, Kamati ya PAC baada ya kukagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na baadhi ya miradi iliyotekelezwa mwaka 2019/2020 ikiwemo kisima cha Welezo (Kwa Bi Mgeni), kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mependekezo ya Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilimshauri Mwenyakiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Welezo aunde Kamati mpya ya Mfuko wa Jimbo kwa mujibu wa Sheria na ashirikiane nayo kikamilifu katika uibuaji na utekelezaji wa Miradi ya kijamii katika Jimbo hilo katika kipindi cha mwaka 2020 - 2025.

**MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA MANISPAA YA MAGHARIBI – 'B' KWA MWAKA 2019-2020**

**JIMBO LA CHUKWANI**

| Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ukarabati wa njia za ndani kuanzia hospitali ya Mina, skuli ya Laurent, mitondooni, maisha plus, kwarara na tomondo changu, Langoni na shakani. | Jimbo zima. | 15,650,000 | Mradi umekamilika. |
| | Ujenzi wa darasa moja skuli ya Abdallah Sheria. | Tomondo | 3,500,000 | Mradi umekamilika. |
| | Ununuzi wa tangi la maji lita 5000 na mipira ya kusambaza maji. | Kisauni. | 1,500,000 | Mradi umekamilika. |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chukwani**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Chukwani ilikiri kupokea shilingi 20,000,000/- kwa ajili ya kutekeleza miradi mbali mbali katika Jimbo la Chukwani kama zilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbalimbali za utekelezaji na matumizi ya mradi huo na kuridhika na utekelezaji wa Miradi yake

JIMBO LA DIMANI

| **Fedha zilizoingizwa** | **Mradi** | **Shehia** | **Fedha zilizotumika** | **Hatua ya utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ununuzi wa tenki moja la maji na ujenzi wa mnara wa maji katika shehia ya Dimani Kae. | Dimani | 4,500,000 | Mradi umekamilika |
| | Ununuzi wa paipu za chuma kwa ajili ya kuhifadhia mipira ya kusambazia maji. | Bweleo | 1,500,000 | Mradi umekamilika |
| | Ukarabati wa bomba<br><br>la maji Nyamanzi | Nyamanzi | 450,000 | Mradi umekamilika |
| | Ununuzi wa madawati mapya skuli za msingi Maugani, Kombeni, Bwefum, Dimani | Jimbo zima | 1,200,000 | Mradi umekamilika |
| | Ununuzi wa charahani nne kwa vikundi vya wajasiria mali jimboni. | Nyamanzi,<br><br>Kombeni,<br><br>Maungani,<br>Kisauni. | 800,000 | Mradi umekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo la Dimani**

Kamati ya PAC haikupata kukagaua nyaraka na Miradi iliyotekelezwa katika Jimbo la Dimani kwa vile Mwenyekiti wa Mfuko wa Jimbo hilo alipata dharura na kwasasa ameshakuwa marehemu.

**JIMBO LA FUONI**

| Fedha zilizoingizwa | Mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ujenzi wa madarasa matatu ya skuli ya msingi chunga | Chunga | 20,000,000 | Mradi umekamilka |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Fuoni**
Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Fuoni ilikiri kupokea shilingi 20,000,000/- kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa Madarasa matatu ya Skuli ya Chunga kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**
Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbali mbali zikiwemo risiti za malipo pamoja na fomu za utekelezaji wa Miradi. Hata hivyo, Kamati ilipata fursa ya kukagua madarasa matatu ya Skuli ya Msingi Chunga na kiujumla, Kamati imeridhika na ujenzi wa Madarasa hayo kwa vile thamani halisi ya fedha iliyotumika imeonekana.

JIMBO LA KIEMBE SAMAKI

| **Fedha Zilizoingizwa** | **Mradi** | **Shehia** | **Fedha zilizotumika** | **Hatua ya utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Uchimbaji wa visima viwili. | Shehia ya mombasa na kwa mchina. | 6,000,000 | Mradi umekamilika |
| | Ununuzi wa mashine tatu za maji. | Jimbo zima | 2,250,000 | Mradi umekamilika |
| | Ujenzi wa minara miwili. | Kiembe Samaki | 6,000,000 | Mradi umekamilika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Gharama za ufundi wa minara | Jimbo zima | 2,000,000 | Lengo limefikiwa |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kiembe Samaki**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kiembe Samaki ilikiri kupokea shilingi 20,000,000/- kwa ajili ya kutekeleza miradi mbali mbali ukiwemo Mradi wa uchimbaji wa visima viwili kama ilivyoripotiwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**

Kamati ilikagua vielelezo vya miradi mbali mbali ikiwemo fomu ya utekelezaji Miradi na baadhi ya risiti za malipo yaliyofanyika na kukagua mradi wa uchimbaji wa visima viwili. Kiujumla, Kamati yetu iliridhika na utekelezaji wa miradi hiyo.

JIMBO LA KIJITOUPELE

| **Fedha Zilizoingizwa** | **Mradi** | **Shehia** | **Fedha zilizotumika** | **Hatua ya utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ununuzi wa vifaa vya usambazaji maji. | Taveta, Melinne, Uzi, Kijitoupele. | 14,280,000 | Mradi umekamilika |
| | Ukarabati wa njia za ndani. | Tomondo, Taveta, Uzi. | 4,708,000 | Mradi umekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Kijitoupele**

Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Kijitoupele ilikiri kupokea Shilingi Milioni Ishirini (20,000,000/-) ambazo zilitumika katika utekelezaji wa miradi miwili ya Maendeleo ya Jimbo hilo kama ilivyoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**
Kamati ya PAC ilikagua nyaraka mbali mbali za utekelezaji wa Miradi hiyo na vielelezo vya matumizi ya fedha za Miradi husika vikiwemo Fomu za Miradi, stakabadhi za malipo (risiti) pamoja na kumbukumbu za kikao cha Kamati ya Mfuko wa Jimbo.

Kamati ya PAC pia ilikagua njia za ndani zizofanyiwa matengenezo. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na matumizi ya fedha za Miradi pamoja na utekelezaji wa Miradi hiyo.

JIMBO LA MWANAKWEREKWE

| **Fedha Zilizoingizwa** | **mradi** | **Shehia** | **Fedha zilizotumika** | **Hatua ya utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Uendelezaji wa ujenzi wa jengo la Wajasiria mali. | Ijitimai | 20,000,000 | Mradi umekamilka |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Mwanakwerekwe**
Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Mwanakwerekwe ilikiri kupokea Shilingi Milioni Ishirini (20,000,000/-) kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbali mbali katika Jimbo hilo..

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**
Kamati ilikagua vielezo vya matumizi ya fedha za Mradi wa Uendeleaji wa Ujenzi wa Jengo la Wajasiriamali na kupata fursa ya kulikagua jengo linyewe liliopo Ijitimai na Kamati imeridhika na fedha iliyotumika kulinganisha thamani halisi ya jengo hilo. Aidha Kamati, imebaini kwamba jengi limemaliza na tayari huduma za ujasiriamali zinatekelezwa ndani yake ikiwemo mafunzo ya ushoni.

JIMBO LA PANGAWE

| Fedha Zilizoingizwa | mradi | Shehia | Fedha zilizotumika | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 20,000,000 | Ukarabati wa njia za ndani. | Mnarani | 5,440,000 | Mradi umekamilika |
| | Ununuzi wa tangi tatu za maji na ujenzi wa mnara wa maji. | Kinuni | 4,275,000 | Mradi umekamilika |
| | Ujenzi wa msingi kwa ajili ya uendelezaji wa mabanda ya skuli ya msingi Kinuni na ujenzi wa skuli kwa ajili ya elimu ya watu wazima. | Mnarani<br>Kinuni | 10,242,000 | Mradi umekamilika |

**Majibu ya Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Pangawe**
Kamati ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Pangawe ilikiri kupokea Shilingi Milioni Ishirini (20,000,000/-) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbali mbali katika Jimbo hilo.

**Uchunguzi wa Kamati ya PAC**
Kamati ilikagua vielelezo mbali mbali vya utekelezaji na vya matumizi ya miradi zikiwemo kumbukumbu za vikao mbali mbali, Fomu za Miradi na Stakabadhi za malipo. Vile vile, Kamati iliukagua mtaro uliopo katika Shehia ya Pangawe. Kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na matumizi pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo.

## SEHEMU YA TATU

## HITIMISHO

Kamati ya PAC kama zilivyo Kamati nyengine zinazosimamia masuala ya kifedha, hufanya kazi zake za ukaguzi kwa kupitia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuchunguza hoja mbali mbali zilizojitokeza katika Ripoti hizo pamoja na kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu Hesabu za Mawizara na Taasisi zisizojitegemea kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2020.

Katika kutekeleza hayo, Kamati ya PAC ilieleza mambo ambayo imeyabaini kupitia majibu ya Watendaji na kutoa Mapendekezo kwa Wahusika kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Taasisi za Umma. Kwa mnasaba huo, Kamati hii inaliomba Baraza la Wawakilishi, kuipitia, kuijadili na hatimaye kuiridhia Ripoti hii kwa lengo la kufanyiwa kazi na Serikali.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati ya PAC inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Mawizara na Taasisi zake kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati hii wakati inatekeleza majukumu yake ya kikatiba. Shukurani pia ziwafikie Watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mashirikiano yao kwa Kamati hii.

Kwa umuhimu wa pekee, tunatoa shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza pamoja na Watendaji wote wa Afisi ya Baraza hilo kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoyaonesha katika muda wote ambao Kamati hii ilipokuwa ikiwajibika.

****Mwisho****